

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

Juzuu ya Tisa

Al-Jaathiyah mpaka Al-Munafiqun

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

IBN HAZM MEDIA CENTER
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم
للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.

Chapa ya Kwanza 2021.

Msimamizi Mkuu wa Mradi:
Yassir Salim Awadh Masoud

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

Kimehaririwa na:
Wanazuoni wa Kiislamu

Usanifu Kurasa:
Ally Said Abdallah
Ibn Hazm Media Center
P.O. Box 22197,
Dar es Salaam
Tanzania.

Kimechapwa:
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

Haki Zote Zimehifadhiwa.

Yaliyomo:

Tafsiri ya <i>Suratu Al-Jaathiyah</i>.....	1
Mwongozo Kweye Kutafakari Ishara za Allah تعالی.....	2
Sifa za Mwongo, Mwingi wa Dhambi na Malipo Yake.....	4
Kutiishwa kwa Bahari na ni Miongoni mwa Ishara za Allah تعالی.....	8
Amri ya Kusubiri Maudhi ya Washirikina	9
Fadhila za Allah تعالی kwa Wana wa Israel na Kukhalifiana Kwao.....	11
Umma Huu Unatahadharishwa Kutofuata Njia ya Wana wa Israel.....	12
Maisha na Mauti ya Waumini Hayalingani na ya Makafiri.....	14
Itikadi ya Makafiri, na Majibu ya Hoja Zao.....	16
Baadhi ya Hali za Siku ya Kiyama na Vitisho Vyake.....	21
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Ahqaaf</i>.....	31
Qur'an ni Uteremsho kutoka kwa Allah تعالی.....	32
Kubainisha Uongo kwa Washirikina.....	33
Kubainisha Uongo wa Kauli za Washirikina Dhidi ya Qur'an	36
Qur'an ni Maneno ya Kweli ya Allah تعالی.....	42
Wasia wa Allah تعالی kwa Wazazi Wawili.....	48
Uthibitisho wa Hukumu ya Muda wa Ujauzito kuwa Miezi Sita.....	49
Kutaja Hatma ya Watoto Wakosefu kwa Wazazi wao na Hatima Yao.....	54
Kisa cha 'Ad.....	59
Kisa cha Majini Kusikiliza Qur'an.....	68
Dalili ya Kuwepo Maisha baada ya Mauti.....	74
Amri kwa Mtume ﷺ Awe na Subira.....	75
Tafsiri ya <i>Suratu Muhammad</i>.....	79
Malipo ya Makafiri na Waumini.....	80
Amri ya Kupigana na Maadui na Kuwashika Mateka.....	83
Fadhila za Mashahidi.....	86
Mnusuruni Allah تعالی, Atakunusuruni.....	88
Moto ni kwa Ajili ya Makafiri, na Pepo ni kwa Ajili ya Wachamungu.....	91
Hawalingani Wenye Kuabudu Haki na Wenye Kuabudu Matamanio.....	95
Sifa za Pepo na Mito Yake.....	96
Ubainifu wa Hali za Wanafiki na Agizo la Tauhidi.....	100
Hali ya Muumini wa kweli na Wanafiki.....	106
Amri ya Kuzingatia Qur'an.....	111

Lawama Dhidi ya Kuritadi.....	111
Kufichua Siri Zilizofichika za Wanafiki	114
Kufutwa Amali za Makafiri na Amri ya Kupigana Nao.....	117
Ubainifu wa udhalili wa Dunia na Uhamasishaji Katika Kutoa.....	120
Tafsiri ya Surat Al-Fat'h.....	123
Fadhila za Surat Al-Fat'h.....	123
Allah تعالی Aliteremsha na Kujaalia Utulivu katika Nyoyo za Waumini.....	129
Sifa za Mtume ﷺ.....	134
Uungaji Mkono (<i>Bai'ah</i>) na Arridhwaani.....	135
Kutaja Hadithi Zinazosimulia Suala la ' <i>Bai'ah</i> '.....	136
Kutaja Sababu za <i>Bai'ah</i> Uungaji mkono huu Mkubwa.....	137
Udhuru wa Uongo kwa Waliojitenga na Mkataba wa Hudaibiyah.....	145
Allah تعالی Anatoa Tangazo la Kuendelea na Jihad	150
Udhuru wa Kisharia wa Kuacha Jihadi pamoja na Agizo la Utii.....	151
Bishara ya Radhi na Ghanima kwa Ajili ya Watu wa <i>Bai'ah</i>	152
Bishara ya Ghanima Nyingi.....	154
Bishara ya Kupata Ushindi Waislamu Mpaka Siku ya Kiama.....	155
Kama Makafiri wa Makkah Wangelipigana Hudaybiyah.....	156
Hekima ya Allah تعالی Kuzuia Vita.....	157
Miongoni mwa Faida za Sulhu ya Hudaybiyah.....	160
Kubainisha Ukweli wa Ndoto ya Mtume ﷺ	176
Bishara ya Ushindi wa Waislamu Ulimwenguni	181
Sifa za Waumini.....	183
Tafsiri ya Surat Al-Hujuraat.....	189
Kukatazwa Kumtangulia Allah تعالی na Mjumbe Wake.....	190
Karipio kwa Wanaomuita Mtume ﷺ.....	195
Agizo la Kuifanyia Uchunguzi Habari ya Fasiki.....	197
Uamuzi wa Mtume ﷺ ni Bora Zaidi.....	198
Tofauti Baina ya Uislamu na Imani.....	199
Amri ya Kusuluhisha Waumini Wanaopigana.....	203
Kukatazwa Kejeli na Dharau.....	207
Kukatazwa Dhana	210
Kukubaliwa Toba ya Msengenyaji na Mfitinishi.....	216
Wanadamu Wote ni Wazao wa Adamu عليه السلام na Hawa.....	217
Utukufu Hupatikana kwa Uchamungu.....	218

Tofauti Baina ya Muumini na Muislamu.....	222
Tafsiri ya <i>Suratul Qaf</i>.....	229
Mwanzo wa Sehemu ya <i>Mufasswal</i> katika Qur'an.....	229
Fadhila za Surat Qaf.....	230
Makafiri Wanaustaajabia Ujumbe na Ufufuo	232
Ubainifu wa Uwezo wa Allah تعالی Juu ya Jambo Kubwa Kuliko Ufufuo.....	235
Makuraishi Kukumbushwa Juu ya Kuhilikishwa Umma Uliotangulia.....	239
Kurudia Uumbaji ni Rahisi Zaidi.....	240
Ujuzi wa Allah تعالی Huangazia Kila Jambo la Mwanaadamu.....	243
Kuwakumbusha Wanadamu Juu ya Uchungu wa Umauti.....	246
Ushahidi wa Malaika; na Allah تعالی Kuamuru Makafiri Watupwe Motoni.....	250
Kugombana Mwanaadamu na Shetani Mbele ya Allah تعالی.....	252
Hali za Jahanamu na Pepo Pamoja na Wakazi Wake.....	254
Makafiri Waonywa Kupewa Adhabu na Mtume	260
Kukumbushwa baadhi ya Yatakayotukia Siku ya Ufufuo.....	266
Kumfariji Mtume ﷺ.....	268
Tafsiri ya <i>Suratu Adh-Dhaariyaat</i>.....	271
Kuthibitisha Habari za Ufufuo na Hesabu.....	272
Kutofautiana Kauli za Washirikina.....	274
Sifa za Wachamungu na Malipo Yao.....	277
Ishara za Allah تعالی Duniani na Ndani ya Nafsi.....	282
Wageni wa Nabii Ibrahim عليه السلام.....	285
Malaika Walipelekwa Kuangamiza Kaumu ya Nabii Lut عليه السلام.....	289
Mafundisho na Mazingatio Kutokana na Kuangamizwa kwa Firauni.....	292
Ushahidi wa Upweke wa Allah تعالی Umo Katika Kuumbwa.....	297
Mitume Wote Walipingwa na Mataifa Yao.....	299
Allah تعالی Ndiye Aliyewaumba Wanaadamu na Majini ili Wamuabudu.....	300
Tafsiri ya <i>Suratu At-Tur</i>.....	303
Fadhila za <i>Suratu At-Tur</i>	303
Kiapo cha Allah تعالی Juu ya Kutokea Adhabu.....	305
Maelezo ya Siku ya Adhabu.....	308
Maelezo ya Makazi ya Watu Wema.....	310
Kizazi cha Muumini Kukutanishwa nae Katika Makazi (Peponi).....	314
Uadilifu wa Allah تعالی kwa Wenye Madhambi.....	317
Wasifu wa Pombe ya Peponi na Neema za Wakazi Wake.....	317

Mtume ﷺ ni Mtu Safi dhidi ya Tuhuma za Washirikina.....	321
Maswali Yanayothibitisha Tawhidi na Kutengua Hila za Washirikina.....	325
Ubainifu wa Ukaidi wa Washirikina na Kwamba Nao Pia Wataadhibiwa.....	329
Mtume ﷺ Kuamrisha Kuwa na Subira, na Kumtukuza Allah تعالی.....	331
Tafsiri ya Suratu An-Najm.....	335
Sura ya Kwanza ambamo Aya ya Sijida Iliteremshwa Ndani Yake.....	335
Allah تعالی Ameapa kuwa Mjumbe ni Kweli	336
Mtume Muhammad ﷺ ni Rehema kwa Viumbe Wote.....	337
Mwalimu wa Mtume Mwaminifu ﷺ ni Roho Mwaminifu عليه السلام.....	340
Maana ya Akawa “Baina ya Pinde Mbili.”.....	342
Je Mtume ﷺ alimuona Mola Wake Mlezi Usiku wa Isra?.....	344
Malaika, Nuru na Rangi Viliifunika <i>Sidrat Al-Muntaha</i>	349
Majibu Dhidi ya Washirikina na Kubainishwa kwa Al-Lat na Al-'Uzza.....	351
Kuwakanusha Washirikina.....	354
Mawazo ya Kutamani Hayamfanyi Mtu Kuwa Muadilifu.....	356
Hakuna Uombezi Isipokuwa kwa Idhini ya Allah تعالی.....	357
Kukanusha Madai ya Washirikina Kuwa Malaika ni Watoto wa Kike.....	359
Amri ya Kuwapuuzwa Watu wa Batili.....	360
Allah تعالی Anajua Kila Kitu, Kidogo na Kikubwa, na Anamjazi Kila Mmoja.....	361
Sifa za Waja Wema na Kusamehe Yale Makosa Madogomadogo.....	361
Kuhamasisha Toba na Kukatazwa Mtu Kujisifu.....	363
Ukosoaji Dhidi ya Watu Wanaomuasi Allah تعالی	366
Ubainifu wa Sahifa za Musa عليه السلام na Ibrahim عليه السلام.....	367
Hatabeba Yeyote Mzigo wa Mwingine Siku ya Kiyama.....	368
Baadhi ya Sifa za Mola Mlezi,.....	372
Onyo na Uzinduzi, Amri ya Kusujudu na Kuwa Wanyenyekevu.....	377
Tafsiri ya Surah Iqtarabat As-Sa'ah.....	381
Kiyama Kimekaribia na Mwezi Umepasuka.....	383
Hadithi Kuhusu Saa ya Mwisho.....	383
Hadithi Zinazoeleza Kupasuka kwa Mwezi.....	385
Ukaidi wa Washirikina na Msimamo wao Mbaya.....	387
Mwisho Mbaya wa Makafiiri Siku Ile ya Kiyama.....	390
Kisa cha Watu wa Nabii Nuhu عليه السلام na Mafunzo Yake.....	392
Habari ya 'Ad	398
Kisasi dhidi ya Thamud.....	400

Kisa cha Watu wa Nabii Lut عليه السلام	403
Kisa cha Firauni na Watu Wake.....	407
Nasaha za Makuraishi na Kupewa Onyo.....	407
Mwisho wa Watu Waovu.....	409
Kila kitu Kiliumbwa na Makadirio Yake.....	410
Onyo la Kujihadhari na Makamio ya Allah تعالى	414
Mwisho Mwema ni wa Wachamungu.....	416
Tafsiri ya Suratu Ar-Rahman.....	419
Utangulizi wa Suratu Ar-Rahman.....	419
Ar-Rahman Ameteremsha Qur'an na Kuifundisha.....	422
Miongoni mwa Dalili za Allah تعالى, Jua, Mwezi, Mbingu na Ardhi.....	422
Mwanaadamu Amezungukwa na Neema za Allah تعالى.....	426
Ubainisho wa Kuumbwa kwa Wanaadamu na Majini.....	428
Allah تعالى ni Mola Mlezi wa Mashariki Mbili na Magharibi Mbili.....	429
Allah تعالى Ameumba Aina Mbalimbali za Maji.....	430
Allah تعالى ni Mwenye Uhai wa Milele, Asiyehitaji Chohote.....	433
Onyo kwa Wanaadamu na Majini.....	436
Vitisho vya Kiyama.....	439
Hali za Wachamungu na Starehe Zao Peponi.....	445
Tafsiri ya Surat Al-Waqi'ah.....	459
Fadhila za Surat Al-Waqi'ah.....	459
Utajo wa Vitisho vya Siku ya Kiyama.....	461
Makundi ya Watu katika Siku ya Kiyama.....	464
Malipo ya wa Mbele katika Imani.....	467
Watu wa Kuliani na Malipo Yao.....	470
Hali za Watu wa Upande wa Kushoto na Malipo Yao.....	487
Ushahidi kwamba Kiyama Kitatokea na Hoja za Kuwepo Ufufuo.....	493
Utanabahishwaji wa Upweke wa Allah تعالى	496
Kuapa kwa Allah تعالى juu ya Utukufu wa Qur'an	503
Hakuna Awezaye Kuizuiya Roho Pindi Inapotolewa.....	508
Hali za Watu Wakati wa Kufa Kwao.....	510
Tafsir ya Suratu Al-Hadid.....	517
Fadhila za Surat Al-Hadid.....	517
Kila kitu kilichopo Kinamtukuza Allah تعالى.....	519
Ujuzi, wa Allah تعالى Uweza na Ufalme Wake, Havina Ukomo.....	522

Kuamrisha Imani na Kuhamasisha Kutoa.....	528
Fadhila za kutoa Mali na Kupigana Kabla ya Ukombozi wa Makkah.....	532
Kuhimizwa Kutoa katika Njia ya Allah <small>تعالى</small>	535
Siku ya Kiyama Waumini Watapewa Nuru, Kulingana na Amali.....	538
Hali za Wanafiki Siku ya Kufufuliwa.....	539
Kuhimizwa Unyenyekevu na Katazo la Kuwaiga Watu wa Kitabu.....	544
Malipo ya Watoa Sadaka, Waumini wa Kweli na waliokufa Shahidi.....	546
Maisha ya duniani ni Starehe Yenye Kupita.....	551
Kila Kinachomfika Mwanadamu Kimeshakadiriwa na Allah <small>تعالى</small>	557
Kuamrisha kuwa na Subra na Shukurani.....	558
Kukatazwa kwa Ubakhili.....	559
Mitume Walipewa Miujiza na Walitumwa na Ukweli na Haki.....	560
Faida za Chuma.....	562
Wengi katika Nyumati wa Mitume Walikuwa Waasi.....	564
Waumini Miongoni mwa Watu wa Kitabu Watapewa Malipo	568
Tafsiri ya Surat Al-Mujadilah.....	573
Sababu za Kushuka Surah hii.....	573
<i>Adh-Dhihar</i> na Kafara Yake.....	575
Ubainifu wa Adhabu ya Maadui wa Dini.....	583
Elimu ya Allah <small>تعالى</small> Inawaenea Viumbe.....	584
Uovu wa Wayahudi.....	586
Adabu za <i>Najwa</i> , (Mazungumzo ya Siri).....	590
Adabu za Vikao.....	593
Fadhila za Elimu na Watu wa Elimu.....	596
Amri ya Kutoa Sadaka kabla Mtu Hajazungumza Faragha na Mtume.....	598
Kuwarudi Wanafiki.....	601
Wapinzani wa Allah <small>تعالى</small> na Mtume Wake ni Washindwa.....	607
Waumini Hawafanyi Urafiki na Makafiri.....	608
Tafsir ya Surat Al-Hashr.....	613
Kila kitu Kinamtukuza Allah <small>تعالى</small> kwa Namna Yake.....	615
Mambo Yaliyowakuta <i>Bani An-Nadhir</i>	616
Sababu za Vita vya <i>Bani An-Nadhir</i>	618
Mitende ya Wayahudi Ilikatwa kwa Idhini ya Allah <small>تعالى</small>	623
Matumizi ya Mali Iliyopatikana bila ya Vita 'Fai'	627
Amri ya Kumtii Mtume <small>ﷺ</small> kwa Kila Alichokataza.....	631

Ubainifu wa Watu wanaostahiki Mali ya Fai'.....	533
Ansar Hawakuwafanyia Husuda Muhajirin	635
Ukarimu wa Ansari	635
Ahadi ya Uongo ya Wanafiki kwa <i>Bani An-Nadhir</i> (Wayahudi).....	641
Mfano wa Wanafiki na Wayahudi.....	644
Amri ya kuwa na Taqwa na Kujiandaa kwa ajili ya Siku ya Kiama.....	647
Watu wa Peponi na Watu wa Jahanamu Hawalingani.....	649
Kubainisha Ukubwa na Utukufu wa Qur'an.....	651
Kumtukuza Allah <small>تعالى</small> kwa Kutaja Majina na Sifa Zake.....	653
<i>Al-Asma' Al-Husna</i>	657
Kila Kitu Kinamsifu na Kumtukuza Allah <small>تعالى</small>	657
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Mumtahanah</i>.....	659
Sababu za kushuka <i>Surat Al-Mumtahanah</i>	660
Amri ya Kutowafanya Marafiki Maadui na Kuacha Kuwasaidia.....	663
Waislamu wana Kigezo Kizuri kwa Ibrahim <small>عليه السلام</small> na Wafuasi wake.....	667
Huenda Allah <small>تعالى</small> Ataweka Urafiki baina Yenu na Maadui Zenu.....	673
Ruhusa ya Kuwafanyia Ukarimu Makafiri Wasiopigana.....	675
Kukatazwa Kuwafanya Marafiki Makafiri na Washirikina.....	677
Baada ya Al-Hudaybiyyah, Muhajirina Wanawake Wasirejeshwe.....	680
Mwanamke Muumini Amekatazwa Kuolewa na Mshirikina.....	682
Mambo ambayo Wanawake Waliyawekea Ahadi ya Utii.....	686
Tafsiri ya <i>Suratu As-Saff</i>.....	695
Fadhila za <i>Surat As-Saff</i>	695
Karipio Kwa Wanaosema Wasiyoyatenda.....	697
Musa <small>عليه السلام</small> Anawasihi Watu wake Wasimuudhi.....	700
Bishara Alizotoa 'Isa <small>عليه السلام</small> Kuhusu Mtume Wetu	702
Kutajwa Kwa Watu Madhalimu Zaidi Kuliko Wote,.....	707
Biashara Inayomwoko Mtu na Adhabu lumizayo.....	708
Waislamu Mara zote ndio Wenye Kususuru Dini.....	711
Kundi Moja la wana wa Israel Lilimwamini 'Isa <small>عليه السلام</small>	712
Allah <small>تعالى</small> Huwapa Ushindi Kundi la Waumini.....	713
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Jumu'ah</i>	715
Fadhila za Surat Al-Jumu'ah.....	715
Kila Kitu Kinamsifu na Kinamtukuza Allah <small>تعالى</small>	717
Fadhila za Allah <small>تعالى</small> kwa Kumtuma Muhammad <small>ﷺ</small>	717

Muhammad ﷺ ni Mtume kwa Waarabu na Wasio-Waarabu.....	719
Kuwaonya Wayahudi na Kuwapa Changamoto ya Kutamani Mauti.....	723
Al-Jumu'ah, na Amri na Fadhila za Siku ya Ijumaa.....	726
Umuhimu wa Kumtaja Allah تعالی katika Siku ya Ijumaa.....	728
Fadhila za Jumu'ah.....	730
Maana ya Wito katika Ayah ni Adhana Inayotangulia Khutbah.....	732
Kukatazwa Kununua na Kuuza Baada ya Wito wa Ijumaa.....	733
Kukatazwa Kuondoka Masjid Wakati Imamu Anahutubu.....	735
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Munafiqun</i>.....	738
Hali ya Wanafiki na Tabia Zao.....	738
Wanafiki Hawapendi Mtume ﷺ Awaombe Msamaha kwa Allah تعالی.....	742
Msisitizo Kuacha Kuipa Dunia Kipaumbele.....	748

Tafsiri ya Suratul Jaathiyah

Sura ya 45

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْجَاثِيَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمَّ ﴿١﴾ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿٢﴾ إِنَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِّمُؤْمِنِينَ ﴿٣﴾ وَفِي خَلْقِكُمْ وَمَا يَبُتُّ مِنْ دَابَّةٍ آيَاتٌ لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾ وَأَخْتَلَفِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارَ وَمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ رِزْقٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَتَصْرِيفِ الرِّيحِ آيَاتٌ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٥﴾ تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ تَقْلُومًا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَ اللَّهِ وَءَايَاتِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ وَيَلُّ لِكُلِّ أَفَّاكٍ أَثِيمٍ ﴿٧﴾ يَسْمَعُ آيَاتِ اللَّهِ تُتْلَىٰ عَلَيْهِ ثُمَّ يُصِرُّ مُسْتَكْبِرًا كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا فَبَشِيرَةٌ لِّعَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٨﴾ وَإِذَا عَلِمَ مِنْ آيَاتِنَا شَيْئًا اتَّخَذَهَا هُزُوًا أُولَٰئِكَ هُمُ عَذَابُ مُهِينٍ ﴿٩﴾ مِّن وَرَائِهِم جَهَنَّمُ وَلَا يُغْنِي عَنْهُمْ مَا كَسَبُوا شَيْئًا وَلَا مَا اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ ۗ هُمْ وَعَدَابُ عَظِيمٌ ﴿١٠﴾ هَذَا هُدًى ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ هُمُ عَذَابُ مِّن رَّجَرٍ أَلِيمٌ ﴿١١﴾

حَمَّ ﴿١﴾ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿٢﴾ إِنَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِّمُؤْمِنِينَ ﴿٣﴾ وَفِي خَلْقِكُمْ وَمَا يَبُتُّ مِنْ دَابَّةٍ آيَاتٌ لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾ وَأَخْتَلَفِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارَ وَمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ رِزْقٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَتَصْرِيفِ الرِّيحِ آيَاتٌ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٥﴾

1. "H'a Mim."

2. "Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima."

3. "Hakika katika mbingu na ardhi ziko Ishara kwa Waumini."

4. "Na katika umbo lenu na katika Aliovyovitawanya

(katika dunia) katika viumbe vinavyotambaa zimo Ishara kwa watu wenye yakini."

5. "Na kupishana usiku na mchana, na riziki Anayoiteremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwayo Akaifufua ardhi baada ya kufa kwake, na mabadiliko ya upepo, ni Ishara kwa watu wenye akili."

Mwongozo kwenye Kutafakari Ishara za Allah تعالی:

Allah تعالی Anawaelekeza viumbe Wake watafakari kuhusu fadhila, neema na kudura Zake, ambazo kwazo Ameumba mbingu na ardhi na viumbe wa jinsi tofauti waliopo baina ya viwili hivyo. Na namna kadha za Malaika, majini, watu, wanyama, ndege, wanyama mwitu, wawindao na kula wanyama wengine, wadudu na namna mbali mbali za viumbe wa baharini. Kutofautiana usiku na mchana, daima hupishana na wala haukutani usiku ukitoa giza na mchana ukitoa mwanga, Allah تعالی Huteremsha kutoka Mawinguni mvua katika wakati wa haja. Allah تعالی Ameyaita mawingu yanayotengeneza mvua 'riziki', kwa sababu mvua ni sababu ya kupatikana chakula.

فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا

"...na kwayo Akaifufua ardhi baada ya kufa kwake..."

Maana: Baada ya ukame, kwa kutokuwa na mimea wala kitu chochote (kilicho hai). Kauli ya Allah تعالی:

وَتَصْرِيفِ الرِّيحِ

"...na mabadiliko ya upepo..."

Maana yake: Kutokea kusini na kaskazini, mashariki na magharibi, nchi kavu na baharini, usiku na mchana. Miongoni mwa upepo upo wa mvua, mwingine wa kuotesha mazao (kupandikiza), mwingine ni chakula cha roho, mwingine ni tasa hauna faida. Allah تعالی Amesema:

لَا يَسْتَلْمِؤْمِنِينَ

"...ziko Ishara kwa Waumini." Halafu,

لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ

"... kwa watu wenye yakini." Halafu,

يَعْقُلُونَ

“...wenye akili.”

Nako ni kupanda kutoka katika hali ya heshima mpaka hali ya utukufu zaidi. Aya hizi zinashabihiana na Aya iliyo katika Surat Al-Baqarah. Nayo ni Kauli ya Allah تعالى isemayo:

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنْفَعُ النَّاسَ وَمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ مَّاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيْحِ وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ

يَعْقُلُونَ ﴿٤٥﴾

“Hakika katika Kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na kupishana usiku na mchana, na marikebu ambazo hupita baharini kwa viwafaavyo watu, na maji Anayoyateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwa hayo Akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na Akaeneza humo kila aina ya wanyama; na katika mabadiliko ya pepo, na mawingu yanayoamrishwa kupita baina ya mbingu na ardhi, bila shaka zimo Ishara kwa watu wanao zingatia.” (2:164)

تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ تَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَ اللَّهِ وَءَايَاتِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿٤٦﴾ وَبَلِّغْ لِكُلِّ أَفَّاكٍ أَثِيمٍ ﴿٤٧﴾ يَسْمَعُ آيَاتِ اللَّهِ تُتْلَىٰ عَلَيْهِ ثُمَّ يُصِرُّ مُسْتَكْبِرًا كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا فَبَشِيرَةٌ لِّعَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٤٨﴾ وَإِذَا عَلِمَ مِنْ آيَاتِنَا شَيْئًا اتَّخَذَهَا هُزُوًا أُولَٰئِكَ هُمُ عَذَابُ مُهِينٍ ﴿٤٩﴾ مِّنْ وَرَائِهِمْ جَهَنَّمُ وَلَا يُغْنِي عَنْهُمْ مَا كَسَبُوا شَيْئًا وَلَا مَا اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ ﴿٥٠﴾ وَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٥١﴾ هٰذَا هُدًىٰ وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ هُمُ عَذَابُ مِّنْ رَّجَزٍ أَلِيمٌ ﴿٥٢﴾

6. “Hizi Aya za Mwenyezi Mungu Tunakusomea kwa haki; basi hadithi gani watakayoiamini baada ya Mwenyezi Mungu na Aya zake?”

7. “Kuangamia ni kwa kila muongo mwingi wa madhambi!”

8. ***“Anayesikia Aya za Mwenyezi Mungu akisomewa, kisha anashikilia yale yale aliyokatazwa, na anajivuna, kama kwamba hakuzisikia. Basi mpe habari ya adhabu chungu!”***

9. ***“Na anapokijua kitu kidogo katika Aya Zetu hukifanyia mzaha. Watu hao ndio watakaokuwa na adhabu ya kufedhehesha.”***

10. ***“Na nyuma yao ipo Jahannamu. Na walioyachuma hayatawafaa hata kidogo, wala walinzi waliowashika badala ya Mwenyezi Mungu. Na watapata adhabu kubwa.”***

11. ***“Huu ni uwongofu. Na wale wanayoipinga Qur’an maneno ya Mola wao Mlezi watapata adhabu kutokana na adhabu kubwa iumizayo.”***

Sifa za Mwongo, Mwingi wa Dhambi na Malipo Yake.

Allah تعالی Anasema:

تَلَّكَ ءَايَاتُ اللَّهِ

“Hizi Aya za Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Qur’an yenye hoja iliyobainifu,

تَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ

“...Tunakusomea kwa haki...”

Kwani ina ukweli kutoka kwa Aliye Mkweli (Yaani, Allah تعالی). Ikiwa hawaiamini wala kuifuata, basi ni mazungumzo gani mengine baada ya Allah تعالی na Aya Zake watakayoyaamini? Kisha Allah تعالی Akasema,

وَوَيْلٌ لِّكُلِّ أَفَّاكٍ أَثِيمٍ

“Ole wake kila mzushi mwenye dhambi!”

Mzushi, anayeongopa katika kauli yake, muapaji, aliye dhalili, mwenye dhambi katika matendo na moyo wake, hukanusha Aya za Allah تعالی. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

يَسْمَعُ ءَايَاتِ اللَّهِ تَتْلَىٰ عَلَيْهِ

‘Anayesikia Aya za Mwenyezi Mungu zikisomwa juu yake.’ Maana yake, akisomewa,

ثُمَّ يُصِرُّ

“...*kisha anashikilia...*” Ukafiri wake na ubishi wake, kwa kiburi na inadi,

كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا

“...*kama kwamba hakuzisikia.*” Kana kwamba hakuzisikia,

فَبَشِّرْهُ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ

“*Basi mbashirie adhabu chungu!*”

Basi mpe habari kuwa ana adhabu iumizayo, huko kwa Allah تعالى,

وَإِذَا عَلِمَ مِنْ آيَاتِنَا شَيْئًا أَخَذَهَا حُزُورًا

“*Na anapokijua kitu kidogo katika Aya Zetu hukifanyia mzaha.*”

Maana yake Akishahifadhi jambo katika Qur'an, hulipinga na kulifanyia dhihaka na kejeli.

أُولَئِكَ هُمُ عَذَابٌ مُّهِينٌ

“*Watu hao ndio watakao kuwa na adhabu ya kufedhehesha.*”

Kama malipo ya kuikejeli na kuifanyia kejeli Qur'an. Katika Sahih Muslim, kumenukuliwa Hadithi ya 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما kwamba Mtume ﷺ alikataza kusafiri pamoja na Qur'an kwenda katika ardhi ya adui kwa kuchelea kwamba inaweza kupatwa na adui.¹

Halafu akatafsiri adhabu atakayoipata katika Siku ya marejeo yake. Akasema:

مِّنْ وَرَائِهِمْ جَهَنَّمُ

“*Na nyuma yao ipo Jahannamu.*”

Maana yake: Wote walio na sifa hii wataishia Jahanamu Siku ya Kiyama.

وَلَا يُغْنِي عَنْهُمْ مَا كَسَبُوا

“*Na walioyachuma hayatawafaa hata kidogo.*”

Maana yake: Mali zao na watoto wao katu hawatawanufaisha wao.

¹ Muslim 3:1491.

وَلَا مَا اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ

"...wala walinzi waliowashika badala ya Mwenyezi Mungu."

Inamaanisha, wala miungu yao waliyoiabudu badala ya Allah تعالى, haitawasaidia chochote,

وَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ

"Na watapata adhabu kubwa."

Kisha, Allah تعالى Akasema:

هَذَا هُدًى

"Huu ni uwongofu."

Maana yake: Hii Qur'an,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِعَايَةِ رَبِّهِمْ هُمْ عَذَابٌ مِّن رَّجْزٍ أَلِيمٍ

"Na wale waliozikataa Ishara za Mola Wao Mlezi watapata adhabu inayotokana na ghadhabu iliyo chungu."

Ambayo ni yenye kuumiza na kutia uchungu. *Allahu Aalam.*

* * *

* اللَّهُ الَّذِي سَخَّرَ لَكُمْ الْبَحْرَ لِتَجْرِيَ الْفُلُكُ فِيهِ بِأَمْرِهِ
 وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلِعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢﴾ وَسَخَّرَ لَكُمْ مَاءً
 فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِّنْهُ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٣﴾ قُلِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا
 يَغْفِرُوا لِلَّذِينَ لَا يَرْجُونَ أَيَّامَ اللَّهِ لِيَجْزِيَ قَوْمًا بِمَا
 كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾ مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ
 أَسَاءَ فَعَلَيْهَا ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١٥﴾ وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا
 بَنِي إِسْرَائِيلَ الْكِتَابَ وَالْحَكْمَ وَالنُّبُوَّةَ وَوَزَقْنَاهُمْ مِّنَ
 الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٦﴾ وَءَاتَيْنَاهُمْ بَيْنَتَ
 مِّنَ الْأَمْرِ ۗ فَمَا اخْتَلَفُوا إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَعِيًا
 بَيْنَهُمْ ۗ إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ
 يَخْتَلِفُونَ ﴿١٧﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاكَ عَلَىٰ شَرِيعَةٍ مِّنَ الْأَمْرِ
 فَاتَّبِعْهَا وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٨﴾ إِنَّهُمْ لَن
 يُغْنُوا عَنْكَ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۗ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ
 بَعْضٍ ۗ وَاللَّهُ وَلىُّ الْمُتَّقِينَ ﴿١٩﴾ هَذَا بَصِيرَةٌ لِّلنَّاسِ
 وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٢٠﴾

* اللَّهُ الَّذِي سَخَّرَ لَكُمْ الْبَحْرَ
 لِتَجْرِيَ الْفُلُكُ فِيهِ بِأَمْرِهِ
 وَلِتَبْتَغُوا
 مِنْ فَضْلِهِ وَلِعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢﴾
 وَسَخَّرَ لَكُمْ مَاءً فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي
 الْأَرْضِ جَمِيعًا مِّنْهُ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٣﴾ قُلِ
 لِلَّذِينَ ءَامَنُوا يَغْفِرُوا لِلَّذِينَ لَا
 يَرْجُونَ أَيَّامَ اللَّهِ لِيَجْزِيَ قَوْمًا بِمَا
 كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾ مَنْ عَمِلَ
 صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا
 ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١٥﴾

12. "Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyeifanya bahari ikutumikieni, ili humo yapite majahazi kwa Amri Yake, na ili mtafute Fadhila Yake, na mpate kushukuru."

13. "Na Amefanya vikutu-mikieni vilivyomo mbinguni na ardhini, vyote vimetoka

Kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaofikiri kwa kina."

14. "Waambie walioamini wawasamehe wale wasiozitaraji siku za Mwenyezi Mungu, ili Awalipe kwa waliyokuwa wakiyachuma."

15. "Mwenye kutenda wema basi ni kwa ajili ya nafsi yake, na mwenye kutenda uovu ni juu yake mwenyewe. Kisha mtarudishwa kwa Mola Wenu Mlezi."

Kutiishwa kwa Bahari ni Miongoni mwa Ishara za Allah تعالى

Allah تعالى Anataja neema Zake kwa waja Wake, kama vile Kutiisha bahari kwa ajili yao,

لِتَجْرِيَ الْفُلُكُ فِيهِ بِأَمْرِهِ

“...ili humo yapite majahazi kwa Amri Yake...”

Hizo ni meli. Allah تعالى Ndiye Aliyeziamuru bahari zizichukue,

وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ

“...na ili mtafute Fadhila Yake...”

Katika masuala ya biashara na chumo,

وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“...na mpate kushukuru.”

Kwa kupata manufaa yanayoletwa kwenu kutoka katika majimbo na maeneo ya mbali. Kisha, Allah تعالى Alisema:

وَسَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

“Na Amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na ardhini...”

Miongoni mwa nyota, milima, bahari, mito, na yote ambayo nyinyi hujinufaisha kwayo. Yaani, Fadhila, Ihsani na Neema Zake zote. Kwa ajili hii, Amesema:

جَمِيعًا مِنْهُ

“...vyote vimetoka Kwake.”

Maana yake: Kutoka Kwake Yeye Peke Yake, Hana mshirika katika mambo Yake. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَمَا بِكُمْ مِنْ نِعْمَةٍ فَمِنَ اللَّهِ ثُمَّ إِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فَإِلَيْهِ تَجْرُونَ ﴿٥٣﴾

“Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kisha yakikuguseni madhara mnamlilia Yeye.” (16:53)

Ibn Jarir رضي الله عنهما Al 'Awfi kuwa Ibnu 'Abbas رحمة الله تعالى alisema katika Kauli ya Allah تعالى Aliyetukuka:

وَسَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِّنْهُ

“Na Amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na ardhini vyote vimetoka Kwake...”

Kila kitu kinatoka kwa Allah تعالى, na hilo jina ni miongoni mwa Majina Yake. na hivyo, vyote vinatoka Kwake, wala hana washindani wa kushindana Naye katika hilo. Nathibitisha kwamba Yeye Yupo hivyo.”¹

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

“Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaofikiri.”

Amri ya Kusubiri Maudhi ya Washirikina

Kauli ya Allah تعالى:

قُلِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا يَغْفِرُوا لِلَّذِينَ لَا يَرْجُونَ

“Waambie walioamini wawasamehe wale wasiozitaraji ...”

Maana yake: Waumini wawasamehe makafiri na wastahamili maudhi yao. Hukumu hii ilikuwa mwanzoni mwa Uislamu, waliamriwa kuwa na subira juu ya usumbufu wa washirikina na watu wa Kitabu ili kwamba huenda nyoyo zao zikaelekea katika Uislamu. Lakini baada ya kuendelea kwao na ukaidi, Allah تعالى Aliwapa Shariah waumini juu ya kujihami, kuwa imara na kupigana Jihadi. Haya yamesimuliwa na 'Abdullah bin 'Abbas na Qatadah.² Mujahid amesema kuwa,

لَا يَرْجُونَ أَيَّامَ اللَّهِ

“...wale wasiozitaraji siku za Mwenyezi Mungu...” Inamaanisha: “Hawatapata neema za Allah تعالى.”³ Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 22:65.

² At-Tabari 22:66, 87

³ At-Tabari 22:67

لِيَجْزِيَ قَوْمًا بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ

“...ili Awalipe kwa waliyokuwa wakiyachuma.” Maana yake: Ikiwa Waumini watawasamehe makafiri duniani, Allah تعالى Atawalipa kwa amali zao mbaya huko Akhera. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا ۖ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١٦﴾

“Mwenye kutenda wema basi ni kwa ajili ya nafsi yake, na mwenye kutenda uovu ni juu yake mwenyewe. Kisha mtarudishwa kwa Mola Wenu Mlezi.”

Maana yake: Mtarejea Kwake Siku ya Kiyama, ambapo nyinyi mtadhihirishiwa amali zenu. Naye Atawalipa kheri yake na shari yake. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

وَلَقَدْ آتَيْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَ وَالنُّبُوَّةَ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ الْعَالَمِينَ ﴿١٧﴾ وَآتَيْنَاهُمْ بَيِّنَاتٍ مِنَ الْأَمْرِ ۖ فَمَا اخْتَلَفُوا إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ ۗ إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١٨﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاكَ عَلَىٰ شَرِيعَةٍ مِنَ الْأَمْرِ فَاتَّبِعْهَا وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٩﴾ إِنَّهُمْ لَنْ يُغْنُوا عَنْكَ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۖ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۗ وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٢٠﴾ هَذَا بَصِّيرٌ لِلنَّاسِ ۖ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٢١﴾

16. “Na hakika Tuliwapa Wana wa Israeli Kitabu na kukifahamu hicho kitabu na Sheria zake, na Unabii, na Tukawaruzuku vitu vizuri vizuri, na Tukawafadhilisha kuliko walimwengu wote.”

17. “Na Tukawapa dalili zilizokuwa wazi za amri. Basi hawakukhitalifiana ila baada ya kuwajia hoja na ubainifu, kwa ajili ya hasadi iliyo kuwa baina yao. Hakika Mola Wako Mlezi Atawapambanua baina yao Siku ya Kiyama katika mambo waliyokuwa wakikhitalifiana.”

18. “Kisha Tukakufanya uwe juu ya sheria iliyo wazi kabisa, basi ifuate, wala usifuate matamano ya wasiojua kitu.”

19. “Kwa hakika hao hawatakufaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hakika wenye kudhulumu ni marafiki wao kwa wao. Na Mwenyezi Mungu ni Rafiki wa wamchao.”

20. "Hizi ni dalili zilizo wazi kwa watu wote, na ni uwongofu, na rehema kwa watu wanaoyakinisha."

Fadhila za Allah تعالیٰ kwa Wana wa Israel na Kukhalifiana Kwao Baada ya Hapo

Allah تعالیٰ Anataja Neema Zake kwa Wana wa Israel, kama vile Kuwateremshia Vitabu na Kuwatuma Mitume kwao, na Kuwajaalia ufalme katika wao.

Allah تعالیٰ Amesema:

وَلَقَدْ آتَيْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ

"Na hakika Tuliwapa Wana wa Israeli Kitabu na hukumu na Unabii, na Tukawaruzuku vitu vizuri vizuri..."

Kama vile, vyakula na vinywaji,

وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ

"...na Tukawafadhilisha kuliko walimwengu wote."

Yaani, Tukawaweka mbele katika zama zao,

وَأَتَيْنَاهُم بَيْنَاتٍ مِنَ الْأَمْرِ

"Na Tukawapa uthibitisho wa wazi wa amri."

Maana yake: Hoja na dalili zenye nguvu. Kwa hivyo, ukawepo ushahidi wenye nguvu juu yao. Hatimaye, wakakhitilafiana baada ya ushahidi kusimama. Hayo yalitokana na ufidhuli wa baadhi yao kwa wengine,

إِنَّ رَبَّكَ

"Hakika Mola Wako Mlezi..."

Ewe Muhammad!,

يَقْضَىٰ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ

"...Atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika mambo waliyokuwa wakikhitalifiana."

Maana yake: Atahukumu baina yao kwa uadilifu.

Umma Huu Unatahadharishwa Kutofuata Njia ya Wana wa Israel

Katika Aya hii kunatolewa tahadhari kwa umati huu kutopita katika njia yao na kutoyachukua mambo yao. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

نُرَّ جَعَلْنَاكَ عَلَىٰ شَرِيعَةٍ مِّنَ الْأَمْرِ فَاتَّبِعْهَا

“Kisha Tukakuweka wewe juu ya Njia ya haya mambo, basi ifuate...”

Maana yake,

اتَّبِعْ مَا أَوْحَىٰ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ ۚ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۚ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٦﴾

“Fuata uliyofunuliwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi, Hapana mungu ila Yeye. Na jitenge na washirikina.” (6:106).

Katika Aya hii, Allah تعالى Amesema:

وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٧﴾ إِنَّهُمْ لَن يُغْنُوا عَنْكَ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۚ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ

“...wala usifuate matamano ya wasiojua kitu. Kwa hakika hao hawatakufaa kitu mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hakika wenye kudhulumu ni marafiki wao kwa wao.”

Maana yake: Utawasaidia nini urafiki wa wao kwa wao, kwani hauwazidishii, isipokuwa hasara, maafa na hilaki,

وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُتَّقِينَ

“Na Mwenyezi Mungu ni Rafiki wa wamchao.”

Naye Allah تعالى Anawatoa kizani na Kuwapeleka kwenye nuru, ilhali wale makafiri, walinzi wao ni miungu ya uongo ambayo huwatoa katika nuru na kuwapeleka kizani. Kisha, Allah تعالى Amesema:

هٰذَا بَصَائِرُ لِلنَّاسِ

“Hizi ni dalili zilizo wazi kwa watu wote...” Maana yake: Hii Qur’an,

وَهٰذِي وِرْحَمَةٌ لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿١٠٨﴾

“...na ni uwongofu, na rehema kwa watu wanaoyakinisha.”

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ اجْتَرَحُوا السَّيِّئَاتِ أَنْ نَجْعَلَهُمْ كَالَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَوَاءً مَحْيَاهُمْ وَمَمَاتِهِمْ ۗ سَاءَ مَا
 يَحْكُمُونَ ﴿٢١﴾ وَخَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ
 وَلَتَجْزَىٰ كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٢﴾
 أَفَرَأَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوْنَهُ وَأَصْلَهُ اللَّهُ عَلَىٰ عِلْمٍ وَخَتَمَ
 عَلَىٰ سَمْعِهِ وَقَلْبِهِ وَجَعَلَ عَلَىٰ بَصَرِهِ غِشَاوَةً فَمَنْ يَهْدِيهِ
 مِنْ بَعْدِ اللَّهِ ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٢٣﴾ وَقَالُوا مَا هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا
 الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا يُبْلِكُنَا إِلَّا الدَّهْرُ وَمَا لَهُمْ بِذَلِكَ
 مِنْ عِلْمٍ ۗ إِنْ هُمْ إِلَّا يَظُنُّونَ ﴿٢٤﴾ وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا
 يَنبَسِثُ مَا كَانَ حُجَّتِهِمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا اتُّوْنَا بِبَابِنَا إِنْ كُنْتُمْ
 صَادِقِينَ ﴿٢٥﴾ قُلِ اللَّهُ يُحْيِيكُمْ ثُمَّ يُمَيِّتُكُمْ ثُمَّ يَجْمَعُكُمْ إِلَىٰ
 يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَبَّ فِيهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٦﴾
 وَإِلَهُ مُلْكِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ
 يَوْمَ يَدْعُ خَسِرَ الْمُتَبَطِّلُونَ ﴿٢٧﴾ وَتَرَىٰ كُلَّ أُمَّةٍ جَائِيَةً كُلَّ
 أُمَّةٍ تُدْعَىٰ إِلَىٰ كِتَابِهَا الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٨﴾
 هَذَا كِتَابُنَا يَنْطِقُ عَلَيْكُمْ بِالْحَقِّ ۗ إِنَّا كُنَّا نَسْتَنسِخُ مَا
 كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٩﴾

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ اجْتَرَحُوا السَّيِّئَاتِ أَنْ نَجْعَلَهُمْ كَالَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَوَاءً مَحْيَاهُمْ وَمَمَاتِهِمْ ۗ سَاءَ مَا
 يَحْكُمُونَ ﴿٢١﴾ وَخَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ
 وَلَتَجْزَىٰ كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٢﴾
 أَفَرَأَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوْنَهُ وَأَصْلَهُ اللَّهُ عَلَىٰ عِلْمٍ
 وَخَتَمَ عَلَىٰ سَمْعِهِ وَقَلْبِهِ وَجَعَلَ عَلَىٰ بَصَرِهِ غِشَاوَةً
 فَمَنْ يَهْدِيهِ مِنْ بَعْدِ اللَّهِ ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٢٣﴾

21. "Je! Wanadhani wanao tenda maovu kuwa Tuta-wafanya kama wale walio amini, na wakatenda wema, kwamba uhai wao na mauti yao yawe sawa? Ni hukumu mbaya wanayoihukumu!"

22. "Na Mwenyezi Mungu Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki, na ili kila nafsi ilipwe yale iliyoyachuma. Nao hawatadhulumiwa."

23. "Je! Umemuona aliyefanya matamaniao yake kuwa ndiye mungu wake, na Mwenyezi Mungu Akamuacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi, na Akapiga muhuri juu ya usikivu wake, na moyo wake, na Akamfanyia kizuizi juu ya macho yake? Basi nani atamuongoa huyo baada ya Mwenyezi Mungu? Hamkumbuki?"

Maisha na Mauti ya Waumini Hayalingani na ya Makafiri

Allah تعالى Anasema kuwa Waumini na makafiri hawawi sawa. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾

“Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.” (59:20)

Katika Aya hii, Allah تعالى Amesema:

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ اجْتَرَحُوا السَّيِّئَاتِ

“Je! Wanadhani wanaotenda maovu...”

Maana yake: Wameyatenda na wakayachuma,

أَنْ تَجْعَلَهُمْ كَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَوَاءٌ مَّحْيَاهُمْ وَمَمَاتُهُمْ

“...kuwa Tutawafanya kama walioamini, na wakatenda wema, sawasawa uhai wao na kufa kwao?”

Kwamba Tutawachukulia kuwa sawa, Duniani na Akhera?

سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ

“...Ni hukumu mbaya wanayoihukumu!”

Maana yake: Wametudhania vibaya, kwamba kwa uadilifu Wetu, Tutawaweka sawa watu wema na waovu, katika nyumba ya Akhera na katika nyumba hii ya dunia.

At-Tabarani alimnukuu Masruq kwamba, Tamim Addari, alisimama usiku mmoja kusali mpaka asubuhi, akiisoma aya hii kwa kuirudiarudia,

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ اجْتَرَحُوا السَّيِّئَاتِ أَنْ نَجْعَلَهُمْ كَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Je! Wanadhani wanaotenda maovu kuwa Tutawafanya kama walioamini, na wakatenda wema...”¹

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

¹ At-Tabari 2:50.

سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ

“Ni hukumu mbaya wanayo hukumu!” Kauli ya Allah تعالی:

وَخَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ

“Na Mwenyezi Mungu Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki...”

Maana yake: Kwa uadilifu,

وَلِتُجْزَىٰ كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

“...na ili kila nafsi ilipwe yale iliyoyachuma, nao hawatadhulumiwa.”

Kisha, Allah تعالی Akasema:

أَفَرَأَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوَاهُ

“Je! Umemwona aliyefanya matamanio yake kuwa ndiye mungu wake...”

Maana yake: Anayeshikamana na kuongozwa na matamanio yake, akiona zuri hulifanya, na akiona baya huliacha. Kauli ya Allah تعالی:

وَأَضَلَّهُ اللَّهُ عَلَىٰ عِلْمٍ

“...na Mwenyezi Mungu Akamuacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi...”

Inamaanisha, Allah تعالی Amemuacha apotee kutokana na Elimu Yake kuwa huyo Anastahiki hivyo, au Allah تعالی Amemuacha apotee baada ya elimu kumfikia mtu huyo na hoja kusimama juu yake. Maana hii ya pili, inajumuisha na ile ya awali, na si kinyume chake. Kauli ya Allah تعالی:

وَحَتَمَ عَلَىٰ سَمْعِهِ وَقَلْبِهِ وَجَعَلَ عَلَىٰ بَصَرِهِ غِشَاوَةً

“...na Akapiga muhuri juu ya usikivu wake, na moyo wake, na Akambandika kizuizi machoni mwake?”

Maana yake: Hasikii ya kumnufaisha wala hafahamu kitakachomuongoza, wala haoni ushahidi wa kuweza kumpa mwangaza. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema:

فَمَنْ يَهْدِيهِ مِنْ بَعْدِ اللَّهِ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ

“Basi nani atamuongoa huyo baada ya Mwenyezi Mungu? Hamkumbuki?”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

مَنْ يُضَلِّلِ اللَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَيَذَرُهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٦﴾

“Aliyemuacha Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumuongoa. Atawaacha hao wakitangatanga katika upotovu wao.” (7:186)

وَقَالُوا مَا هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا يُهْلِكُنَا إِلَّا الدَّهْرُ وَمَا لَهُم بِذَلِكَ مِنْ عِلْمٍ إِنْ هُمْ إِلَّا يَظُنُّونَ ﴿٧٦﴾ وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا يَتَّبِعُهَا مَا كَانَ حُجَّتَهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا اتُّنُوا بِغَابِئِنَا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧٧﴾ قُلِ اللَّهُ يُخَيِّبُكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُجْمَعُكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَبَّ فِيهِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٧٨﴾

24. “Na walisema: Hapana ila huu uhai wetu wa duniani - tunakufa na tunaishi, na hapana kinachotuhiliki isipokuwa nyakati. Lakini wao hawana ilimu ya hayo, ila wao wanadhani tu.”

25. “Na wakisomewa Aya Zetu zilizowazi hawana hoja ila kusema: Waleteni baba zetu, ikiwa nyinyi ni wasemao kweli.”

26. “Sema: Mwenyezi Mungu Anakuhuisheni, kisha Anakufisheni, kisha Anakukusanyeni Siku ya Kiyama isiyoyana shaka. Lakini watu wengi hawajui.”

Itikadi ya Makafiri, na Majibu ya Hoja Zao.

Allah تعالى Anaeleza kuhusu makafiri na wanaoafikiana nao katika washirikina wa Kiarabu katika kupinga siku ya Qiyama,

وَقَالُوا مَا هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا

“Na walisema: Hapana ila huu uhai wetu wa duniani - twafa na twaishi...”

Maana yake: Huko hakuna kingine, isipokuwa dunia hii tu, watu wanakufa, na

wengine kuishi, wala hakuna watu kufufuliwa wala Kiyama. Haya yanasemwa na washirikina wa Kiarabu wanaopinga siku ya Kiyama. Pia ni maneno ya wanafalsafa wanaopinga kuwepo kwa Allah, ambao wanakanusha chanzo cha uumbaji wa binadamu na pia wanakanusha kufufuliwa. Ni kauli ya wanafalsafa wa *Ad-Dahriyyah* (wanaopinga ufufuo) ambao wanamkadhibisha Muumbaji, na wanaitakidi kwamba, katika kila miaka elfu thelathini na sita, kila kitu kinarejea katika maisha yake tena. Tena wanadai kwamba, hili limeshakariri mara nyingi, bila ya ukomo. Kwa hivyo, wakatukuza rai za kiakili, wakapinga maandiko. Kwa ajili hii, wakasema:

وَمَا يُلَكُنَّا إِلَّا الدَّهْرُ

“...na hapana kinachotuhilikisha isipokuwa zama.”

Allah تعالى Amesema:

وَمَا هُمْ بِذَلِكَ مِنْ عِلْمٍ إِنْ هُمْ إِلَّا يَظُنُّونَ

“Lakini wao hawana ilimu ya hayo, ila wao wanadhani tu.”

Yaani, ni fikra dhaifu zisizo na ushahidi.

Ama Hadithi iliyonukuliwa na Bukhari na Muslim, Abu Dawud na An-Nasai, kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ تَعَالَى: يُؤْذِنِي ابْنُ آدَمَ، يَسُبُّ الدَّهْرَ وَأَنَا الدَّهْرُ، بِيَدِي الأَمْرُ، أَقْلَبُ لَيْلَهُ وَنَهَارَهُ»

“Allah Taala Anasema: ‘Mwanaadamu Ananiudhi, anatumkana zama (nyakati), ilhali Mimi ni Dahar. Mkononi Mwangu kuna mambo yote, Ninageuza usiku wake na mchana.’¹

Katika masimulizi mengine,

«لَا تَسُبُّوا الدَّهْرَ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الدَّهْرُ»

“Msitukane dahari, kwani, Allah Mtukufu Ndiye Dahari.”²

Ash-Shafi, Abu ‘Ubaydah na wengine katika maimamu wa tafsiri wamesema katika kuitafsiri kauli ya Mtume ﷺ:

¹ *Fath Al-Bari* 8:437, Muslim 4:1762, Abu Dawud 5:423, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:457.

² Muslim 4:1763.

«لَا تَسُبُّوا الدَّهْرَ فَإِنَّ اللَّهَ تَعَالَى هُوَ الدَّهْرُ»

“Msitukane dahari, kwani, Allah Ndiye Dahari.”

Kuwa, katika enzi za Ujahili waarabu walikuwa wakitukana nyakati, pindi walipopatwa na shida au balaa, au janga, kwa kusema, “Nyakati ziangamie.” Walikuwa wakiegemeza matendo hayo kwa nyakati na kuzitukana, wakati kwa hakika mwenye kuyafanya hayo ni Allah تعالی. Kwa hivyo ni kama wanamtukana Allah تعالی, kwa ajili hii Amekataza kutukana nyakati kwa mazingatio haya. Ni kwa sababu Allah تعالی Ndiye Nyakati wanayoikusudia na kumnasibishia matendo hayo, pindi wanapozitukana nyakati. Hii ni kauli nzuri zaidi iliyosemwa katika tafsiri yake, na ndiyo makusudio. Allah تعالی ni Mjuzi zaidi.

Bin Hazm رحمه الله تعالی na wenye mtazamo kama wake miongoni mwa wafuasi wa *Dhaahiriya* wamekosea kwa kuingiza *Ad-Dahr* katika Majina matukufu ya Allah تعالی kwa ushahidi wa Hadithi hii. Kauli ya Allah تعالی:

وَإِذَا تَتَلَّى عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا يَلْمِزُوكَ

“Na wakisomewa Aya Zetu zilizo wazi...”

Yaani, Anapowaletea dalili kuwabainishia haki. Kwa hakika, Allah تعالی ni Muweza wa Kuirejesha miili, baada ya kumalizika na kutoweka au kusagika.

مَا كَانَ حُجَّتِهِمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَأَتْنُوا بِآبَائِنَا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

“...hawana hoja ila kusema: Waleteni baba zetu, ikiwa nyinyi ni wasemao kweli.”

Maana yake: Wahuisheni, ikiwa mnayoyasema ni ya kweli. Allah تعالی Amesema:

قُلِ اللَّهُ يُحْيِيكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ

“Sema: Mwenyezi Mungu Anakuhuisheni, kisha Anakufisheni...”

Inamaanisha, kama mnavyoyashuhudia haya, Anakutoeni kutoka katika kutokuwepo mpaka katika kuwepo,

كَيْفَ تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَكُنْتُمْ أَمْوَانًا فَأَحْيَاكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ إِلَيْهِ

تَرْجِعُونَ

“Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu na hali mlikuwa wafu Akakufufueni! Kisha Atakufisheni, tena Atakufufueni, kisha Kwake mtarejeshwa?”(2:28)

Kwa hivyo, Mwenye Kuweza Kuanzisha uumbaji ni Muweza wa Kuurejesha kwa njia ya awali na ya uhakika zaidi,

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

“Na Yeye Ndiye Anayeanzisha Uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake.” (30:27)

ثُمَّ يَجْمَعُكُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ

“...kisha Anakukusanyeni Siku ya Kiyama isiyo na shaka.”

Maana yake: Atakapokukusanyeni katika Siku ya Kiyama, Hatakurejesheni duniani, hata msembe:

اتُّمُوا بِآبَائِنَا إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ

“Waleteni baba zetu, ikiwa nyinyi ni wasemao kweli.”

يَوْمَ يَجْمَعُكُمْ لِيَوْمِ الْجَمْعِ

“Siku Atakayokukusanyeni kwa ajili ya Siku ya Mkusanyiko...” (64:9)

لَأَيِّ يَوْمٍ أُجِّلَتْ لِيَوْمِ الْفَضْلِ

“Kwa siku gani hiyo wamewekewa muda huo? Kwa siku ya kupambanua!” (77:12-13) na

وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مُّعَدودٍ

“Na Sisi Hatuiakhirishi ila kwa muda unaohisabiwa.” (11:104)

Katika Aya hii, Allah تعالى Amesema:

ثُمَّ يَجْمَعُكُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ

“...kisha Anakukusanyeni Siku ya Kiyama isiyo na shaka.”

Maana yake: Haina utata kutukuka kwake,

وَلَيْكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾

“...Lakini watu wengi hawajui.”

Kwa hivyo, wanakanusha kurejea na wanaona suala la kufufuliwa viwiliwili liko mbali. Allah تعالى Amesema:

إِنَّمَا يَرَوْنَهُ بَعِيدًا ﴿٦٨﴾ وَنَزَلَهُ قَرِيبًا ﴿٦٩﴾

“Hakika wao wanaiona iko mbali. Na Sisi Tunaiona iko karibu.”
(70:6-7)

Maana yake: Wanaona kutuka kwake kuko mbali, huku Waumini wanaona kwamba ni sahali na kuko karibu.

وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُنْحَسِرُ الْمُبْطِلُونَ ﴿٧٠﴾
وَتَرَى كُلَّ أُمَّةٍ جَائِيَةً ۗ كُلُّ أُمَّةٍ تُدْعَىٰ إِلَىٰ كِتَابِهَا الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٧١﴾ هَذَا
كِتَابُنَا يَنْطِقُ عَلَيْكُمْ بِالْحَقِّ ۗ إِنَّا كُنَّا نَسْتَنسِخُ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٧٢﴾

27. “Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi. Na siku itaposimama Saa ya Kiyama, siku hiyo wataangamia wenye kushikamana na upotovu.”

28. “Na utauona kila umma umepiga magoti, na kila umma utaitwa kwenda soma kitabu chake: Leo mtalipwa mliyokuwa mkiyatenda.”

29. “Kitabu chetu hiki kinasema juu yenu kwa haki. Hakika Sisi Tulikuwa Tukiyaandika mliyokuwa mkiyatenda.”

Baadhi ya Hali za Siku ya Kiyama na Vitisho Vyake

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye Ndiye Mmiliki wa mbingu na ardhi na Ndiye Mtawala katika maisha haya na ya Akhera. Kauli ya Allah تعالى:

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ

“Na siku itaposimama Qiyama...”

Maana yake: Siku ya Kiyama.

يَخْضِرُ الْمُبْطِلُونَ

“...siku hiyo wataangamia wenye kushikamana na upotovu.”

Hawa ni wanaomkataa Allah تعالى, wanayapinga Aliyoteremshiwa Mtume ﷺ katika hoja na dalili za wazi. Kisha, Allah تعالى Alisema:

وَتَرَى كُلَّ أُمَّةٍ جَائِيَةً

“Na utauona kila umma umepiga magoti...”

Kwa magoti yao kutokana na taabu na ukubwa wa jambo hilo, na kusemwa hali hii ni baada ya kuletwa Jahannamu na kupumua mara moja, na hakuna hata mmoja atakayesalia, bali atapiga magoti, hata Nabii Ibrahim *Al-Khalil* عليه السلام, atasema: “Nafsi yangu, nafsi yangu, nafsi yangu! Leo sitakuomba (Ya Allah تعالى), isipokuwa nafsi yangu.” Hata Nabii Isa عليه السلام, atasema: “Leo sitakuomba isipokuwa nafsi yangu, sitakuomba juu ya Maryam ambaye amenizaa.” Kauli ya Allah تعالى:

كُلُّ أُمَّةٍ تُدْعَى إِلَى كِتَابِهَا

“...na kila umma utaitwa kwenda kusoma kitabu chake...”

Maana yake: Kitabu cha amali zao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَوُضِعَ الْكِتَابُ وَجِئَءَ بِالنَّبِيِّنَ وَالشُّهَدَاءِ

“...na Kitabu kitawekwa, na wataletwa Manabii na mashahidi...”

(39:69)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

“Leo mtalipwa mliyokuwa mkiyatenda.”

Mtalipwa kutokana na amali zenu, za kheri na za shari. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يُنذِرُوا الْإِنْسَانَ يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ﴿١٣﴾ بَلِ الْإِنْسَانُ عَلَىٰ نَفْسِهِ بَصِيرَةٌ ﴿١٤﴾ وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ ﴿١٥﴾

“Siku hiyo ataambiwa mtu aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha. Bali mtu ni hoja juu ya nafsi yake. Na ingawa atatoa nyudhuru nyingi.” (75:13-15)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

هَذَا كِتَابُنَا يَنْطِقُ عَلَيْكُمْ بِالْحَقِّ

“Kitabu Chetu hiki kinasema juu yenu kwa haki.”

Maana yake: Kimeandika amali zenu zote, bila ya ziada wala upungufu. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَوُضِعَ الْكِتَابُ فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا مَالِ هَذَا الْكِتَابِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا وَلَا يَظْلُمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿١٨﴾

“Na kitawekwa kitabu. Basi utawaona wakosefu wanavyoogopa kwa yale yaliomo humo. Na watasema: Ole wetu! Kitabu hiki kina nini! Hakiachi dogo wala kubwa ila huliandika? Na watayakuta yote waliyoyatenda yamehudhuria hapo. Na Mola Wako Mlezi Hamdhulumu yeyote.” (18:49)

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّا كُنَّا نَسْتَنْسِخُ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

“Hakika Sisi Tulikuwa Tukiyaandika mliyokuwa mkiyatenda.”

Maana yake: Sisi Tulikuwa Tukiwaamuru Malaika waandishi waandike amali zenu. Bin ‘Abbas رضي الله عنهما na wengine wamesema: “Malaika huandika amali

za waja, kisha wanapanda nazo mbinguni. Wanazipokea Malaika ambao wamepewa majukumu ya kuzishughulikia amali zilizoandikwa na (Malaika) waandishi ambazo zilikwishadhihirishwa kwao kutoka katika *Al-Lawh Al-Mahfudh* (ubao uliohifadhi matendo yote ya waja na makadirio yao) katika kila *Laylatul-Qadr* (usiku wenye cheo) ambapo yale ambayo Allah تعالی Alikwishayaandika tangu azali (enzi) kabla Hajawaumba wanadamu yatatendeka kwa waja. Haitazidi wala kupungua hata herufi moja.

Akasoma Aya ifuatayo,

إِنَّا كُنَّا نَسْتَنسِخُ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

“Hakika Sisi Tulikuwa Tukiyaandika mliyokuwa mkiyatenda.”

* * *

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُدْخِلُهُمْ رَبُّهُمْ
 فِي رَحْمَتِهِ ۗ ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْمُبِينُ ﴿٣٠﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا
 أَفَلَمْ تَكُنْ ءَايَتِي تُنزَّلُ عَلَيْكُمْ فَاسْتَكْبَرْتُمْ وَكُنْتُمْ قَوْمًا مُّجْرِمِينَ
 ﴿٣١﴾ وَإِذَا قِيلَ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَالسَّاعَةُ لَا رَيْبَ فِيهَا
 قُلْتُمْ مَا نَدْرِي مَا السَّاعَةُ إِنْ نَظُنُّ إِلَّا ظَنًّا وَمَا نَحْنُ
 بِمُستَقْبِرِينَ ﴿٣٢﴾ وَبَدَا لَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا عَمِلُوا وَحَاقَ بِهِم
 مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٣٣﴾ وَقِيلَ الْيَوْمَ نَنسَلِكُمَا
 نَسِيتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا وَمَأْوَاكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُم مِّنْ
 نَّصِيرِينَ ﴿٣٤﴾ ذَٰلِكُمْ بِأَنكُم مَّاتَّخَذْتُمْ ءَايَاتِ اللَّهِ هُزُوًا
 وَعَرَّيْتُمْ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا ۗ فَالْيَوْمَ لَا تُخْرَجُونَ مِنْهَا وَلَا هُمْ
 يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٣٥﴾ فَلِلَّهِ الْحَمْدُ رَبِّ السَّمٰوٰتِ وَرَبِّ
 الْأَرْضِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٦﴾ وَلَهُ الْكِبْرِيَاءُ فِي السَّمٰوٰتِ
 وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٣٧﴾

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا
 الصَّالِحَاتِ فَيُدْخِلُهُمْ رَبُّهُمْ فِي
 رَحْمَتِهِ ۗ ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْمُبِينُ ﴿٣٠﴾
 وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا أَفَلَمْ تَكُنْ ءَايَتِي
 تُنزَّلُ عَلَيْكُمْ فَاسْتَكْبَرْتُمْ وَكُنْتُمْ قَوْمًا
 مُّجْرِمِينَ ﴿٣١﴾ وَإِذَا قِيلَ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ
 حَقٌّ وَالسَّاعَةُ لَا رَيْبَ فِيهَا قُلْتُمْ مَا
 نَدْرِي مَا السَّاعَةُ إِنْ نَظُنُّ إِلَّا ظَنًّا
 وَمَا نَحْنُ بِمُستَقْبِرِينَ ﴿٣٢﴾ وَبَدَا
 لَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا عَمِلُوا وَحَاقَ بِهِم مَا
 كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٣٣﴾ وَقِيلَ
 الْيَوْمَ نَنسَلِكُمَا كَمَا نَسِيتُمْ لِقَاءَ
 يَوْمِكُمْ هَٰذَا وَمَأْوَاكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُم

مِّنْ نَّصِيرِينَ ﴿٣٤﴾ ذَٰلِكُمْ بِأَنكُم مَّاتَّخَذْتُمْ ءَايَاتِ اللَّهِ هُزُوًا
 وَعَرَّيْتُمْ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا ۗ فَالْيَوْمَ لَا تُخْرَجُونَ
 مِنْهَا وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٣٥﴾ فَلِلَّهِ الْحَمْدُ رَبِّ السَّمٰوٰتِ وَرَبِّ
 الْأَرْضِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٦﴾ وَلَهُ
 الْكِبْرِيَاءُ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٣٧﴾

30. "Ama walioamini na wakatenda mema, Mola wao Mlezi Atawatia katika Rehema Yake. Huko ndiko kufanikiwa kuliko wazi."

31. "Na ama waliokufuru, wataambiwa: Kwani hamkuwa mkisomewa Aya Zangu nanyi mkajivuna, na mkawa watu waovu?"

32. ***“Na ikisemwa: Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, na Qiyama hakina shaka, nyinyi mkisema: Hatukijui hicho Qiyama, tunadhania dhana tu, wala hatuna yakini.”***

33. ***“Basi ubaya wa waliyoyatenda utawadhihirikia, na yatawazunguka waliyoyafanyia mashara.”***

34. ***“Na itasemwa: Leo Tunakusahauni kama nyinyi mlivyosahau mkutano wa siku yenu hii; na mahali penu ni Motoni, wala hamna wa kukunusuruni.”***

35. ***“Hayo ni kwa sababu nyinyi mlizifanyia mzaha Aya za Mwenyezi Mungu; na maisha ya dunia yakakudanganyeni. Basi leo hawatatolewa humo wala hao hawatakubaliwa nyudhuru wao.”***

36. ***“Basi sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa mbingu, na Mola Mlezi wa ardhi, na Mola Mlezi wa walimwengu wote.”***

37. ***“Na Ukubwa ni Wake Yeye tu, mbinguni na ardhini, Naye ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”***

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Hukumu Yake kwa Kuiumba Siku ya Kiyama, kwa Kusema:

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Ama walioamini na wakatenda wema...”

Maana yake: Nyoyo zao zimeamini, na viungo vyao vikatenda amali nzuri, zilizotakasika na zinazoafikiana na sheria,

فَيُدْخِلُهُمْ رَبُّهُمْ فِي رَحْمَتِهِ

“...Mola Wao Mlezi Atawatia katika Rehema Yake.”

Hiyo ni Pepo, kama ilivyothibiti katika Sahih Mbili, (Bukhari na Muslim). Allah تعالى Aliiambia Pepo;

أَنْتِ رَحْمَتِي، أَرْحَمُ بِكَ مِنْ أَشَاءِ؛

“Wewe ni Rehema Yangu. Kwako Mimi Humrehemu Nimtakaye.”¹

¹ Fath Al-Bari 8:460.

ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْمُبِينُ

“Huko ndiko kufuzu kuliko wazi.” Maana yake: Kufaulu kuliko wazi.

Kisha, Allah تعالى Alisema:

وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا أَفَلَمْ تَكُنْ ءآيَاتِي تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فَاسْتَكْبَرْتُمْ

“Na ama waliokufuru, wataambiwa: Kwani hamkuwa mkisomewa Aya Zangu nanyi mkapanda kichwa...”

Wataambiwa hayo kwa njia ya kukaripiwa, ‘nyinyi mlisomewa Aya za Allah تعالى, mkafanya jeuri kwa kutokuzifuata, na mkakataa kuzisikiliza?’

وَكُنْتُمْ قَوْمًا مُّجْرِمِينَ

“...na mkawa watu waovu?” Katika matendo yenu, pamoja na ukanushaji mlioukusanya katika nyoyo zenu?.

وَإِذَا قِيلَ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَالسَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيهَا

“Na ikisemwa: Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, na Qiyama hakina shaka...”

Maana yake: Pindi Waumini walipokuambieni hayo,

قُلْتُمْ مَا نَدْرِي مَا السَّاعَةُ

“...nyinyi mkisema: Hatukijui hicho Qiyama...” Maana yake: Hatukitambui,

إِن نَّظُنُّ إِلَّا ظَنًّا

“...tunadhania dhana tu...” Inamaanisha, sisi hatujui kutuka kwake, bali tunakisia tu, yaani hatuna hakika na jambo hilo. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَمَا نَحْنُ بِمُستَقْبِرِينَ

“...wala hatuna yakini.”

وَنَدَا هُمْ سَيِّئَاتٍ مَا عَمِلُوا

“Basi ubaya wa waliyoyatenda utawadhihirikia...” Na adhabu ya amali zao mbaya itadhihirika,

وَحَاقَ بِهِم

“...*na yatawazunguka...*” Maana yake: Hawatapata pa kukimbilia,

مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ

“...*waliyoyafanyia maskhara.*”

Maana yake: Miongoni mwa adhabu na majanga,

وَقِيلَ الْيَوْمَ نَنْسَدُكُمْ

“*Na itasemwa: Leo Tunakusahauni...*”

Inamaanisha, Tutakufanyieni muamala wa mwenye kukusahauni katika Moto wa Jahanamu,

كَمَا نَسِيتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَذَا

“...*kama nyinyi mlivyosahau mkutano wa siku yenu hii...*”

Maana yake: Hamkujiandaa, kwa sababu nyinyi hamkuusadiki,

وَمَاؤْنِكُمْ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِنْ نَّاصِرِينَ

“...*na mahali penu ni Motoni, wala hamna wa kukunusuruni.*”

Imethibiti katika Bukhari na Muslim kwamba Allah تعالى Atawaambia baadhi ya waja Siku ya Kiyama:

«أَلَمْ أَرْوِّجْكَ؟ أَلَمْ أُحْرِمْنَاكَ؟ أَلَمْ أَسْخَرْ لَكَ الْخَيْلَ وَالْإِبِلَ، وَأَذْرَكَ نِزَاسُ وَتَرْبِيعَ؟
فَيَقُولُ: بَلَى يَا رَبِّ. فَيَقُولُ: أَفَطَنَّتْ أَنْكَ مُلَائِمِي؟ فَيَقُولُ: لَا. فَيَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى:
فَأَلْبِسْكُمْ أَنْسَاكَ كَمَا نَسِيتُنِي»

“Je sikukuozesha mke? Sikukutiishia, sikukudhalilishia farasi na ngamia, na kukuacha uwe na cheo?” Atajibu: ‘Ndiyo, ewe Mola Wangu.’ Allah Atasema: ‘Je, ulidhani kuwa utakutana Nami?’ Atajibu: ‘Hapana.’ Allah Taala Atasema: ‘Basi, leo, Nitakusahau kama ulivyonisahau Mimi’¹”

¹ Muslim 9:2279.

Amesema Allah تعالی:

ذَلِكُمْ بِأَنكُمْ أَخَذْتُمْ ءَايَاتِ اللَّهِ هُزُوًا

“Hayo ni kwa sababu nyinyi mlizifanyia mzaha Aya za Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Tumekulipeni jaza hii kwa sababu nyinyi mlizifanyia masikhara hoja za Allah juu yenu, mkazikejeli na kuzifanyia stihizai,

وَعَزَّيْتُمْ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا

“...na maisha ya dunia yakakudanganyeni.”

Yamekukhadaeni, mkayatumainia, mkawa katika wenye hasara. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema:

فَالْيَوْمَ لَا تُخْرَجُونَ مِنْهَا

“Basi leo hawatatolewa humo...”

Maana yake: Motoni,

وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ

“...wala hao hawatakubaliwa nyudhuru zao.”

Maana yake: Udhuru wao hautahitajika, bali wataadhibiwa pasi na hesabu wala kupewa udhuru. Ni kama ambavyo, kundi la Waumini litaingia Peponi pasi na adhabu wala hesabu.

Kisha, baada ya Kutaja hukumu Yake kwa Waumini na makafiri, Allah تعالی Akasema:

فَلِلَّهِ الْحَمْدُ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَرَبِّ الْأَرْضِ

“Basi sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa mbingu, na Mola Mlezi wa ardhi...”

Maana yake: Mmiliki wa hivyo na vilivyomo humo. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema:

رَبِّ الْعَالَمِينَ

“...na Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

Kisha, Allah تعالى Akasema:

وَلَهُ الْكِبْرِيَاءُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Na Ukubwa ni Wake Yeye tu, mbinguni na ardhini...”

Mujahid amesema: “Inamaanisha, utawala.” Maana yake: Yeye ni Adhimu, Anayestahiki sifa, na kila kitu kinamnyenyekea Yeye na kuhitaji Kwake.

Ilinukuliwa katika Hadithi Sahih kuwa, Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ اللهُ تَعَالَى: الْعِظْمَةُ إِزَارِي، وَالْكَبْرِيَاءُ رِدَائِي، فَمَنْ تَارَعَنِي وَاجِدَا مِنْهُمَا
أَسْكَنَتْهُ نَارِي»

“Allah Taala Anasema: ‘Ukuu ni Kikoi Changu, Kiburi ni Shuka Yangu, basi yeyote mwenye kupokonyana na Mimi mojawapo ya hizo mbili, Nitamkalisha katika Moto Wangu.’¹

Muslim amepokea Hadithi kama hii.² Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ الْعَزِيزُ

“...Naye ni Mwenye Nguvu...”

Ambaye Hashindwi na chochote wala Hazuiliwi Kufanya Anachotaka,

الْحَكِيمُ

“...Mwenye Hikima.”

Katika Kauli na Matendo Yake, Sharia na Kudura Yake, ni Mtukuka na Mwenye Sifa Njema, hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye tu.

Mwisho wa tafsiri ya *Surat Al-Jathiyah*. Sifa njema zinamstahiki Allah تعالى, na Kwake Ndiko kwenye taufiki na hifadhi.

* * *

¹ Abu Dawud 4:350.

² Muslim 4:2023.

Tafsiri ya Suratul Ahqaaf

Sura ya 46

Iliteremshwa Makkah

سُورَةُ الْأَخْفَافِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمَّ ۝ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ۝ مَا
 خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَأَجَلٍ
 مُّسَمًّى ۚ وَالَّذِينَ كَفَرُوا عَمَّا أُنذِرُوا مُّعْرِضُونَ ۝ قُلْ أَرَأَيْتُمْ
 مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرُونَا مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ
 لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَوَاتِ ۖ أَتَتَوَكَّلُونَ عَلَىٰ بَعْضِ الْأَشْيَاءِ
 مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝ وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن
 يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ
 وَهُمْ عَنْ دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ۝ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ
 أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ۝ وَإِذَا تَنَادَىٰ عَلَيْهِمْ
 آئِنَّا مِنَ الْبُيُوتِ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ هَذَا سِحْرٌ
 مُّبِينٌ ۝ أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۖ قُلْ إِنْ أَفْتَرَيْتُهُ فَلَا تَمْلِكُونَ لِي
 مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۖ هُوَ أَعْلَمُ بِمَا تُفِيضُونَ فِيهِ ۖ كَفَىٰ بِهِ شَهِيدًا
 بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۖ وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ۝ قُلْ مَا كُنْتُ بِدَعَا
 مِنْ الرُّسُلِ وَمَا أَدْرَىٰ مَا يُفْعَلُ بِي وَلَا بِكُمْ ۖ إِنْ أَتَيْتُمْ إِلَّا مَا
 يُوحَىٰ إِلَيَّ وَمَا أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ۝

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi
 wa Rehema Mwenye
 Kurehemu

حَمَّ ۝ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ
 الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ۝ مَا خَلَقْنَا
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا
 بِالْحَقِّ وَأَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ وَالَّذِينَ كَفَرُوا
 عَمَّا أُنذِرُوا مُّعْرِضُونَ ۝ قُلْ أَرَأَيْتُمْ
 مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرُونَا
 مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ
 لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَوَاتِ ۖ أَتَتَوَكَّلُونَ
 عَلَىٰ بَعْضِ الْأَشْيَاءِ مِنْ دُونِ اللَّهِ
 إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝ وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن
 يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ
 لَهُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنْ
 دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ۝ وَإِذَا حُشِرَ
 النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا
 بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ۝

1. "HA MIM

2. ***“Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”***
3. ***“Hatukuziumba mbingu na ardhi wala yaliyomo baina yao ila kwa haki na kwa muda maalumu. Na waliokufuru wanayapuuza yale wanayoonywa.”***
4. ***“Je! Mnawaona wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu? Nionesheni wameumba nini katika ardhi; au hao wanayo shirika katika mbingu? Nileteeni Kitabu kilichokuwa kabla ya hiki, au alama yoyote ya elimu (inayokubali hayo mnayoyasema, ikiwa mnasema kweli.”***
5. ***“Na nani mpotovu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wao kutokana na maombi yao wameghafilika.”***
6. ***“Na ambao watu watakapokusanywa watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.”***

Qur’an ni Uteremsho kutoka kwa Allah تعالى na Ulimwengu Ameuumba Yeye kwa Njia ya Haki

Allah تعالى Anaeleza kuwa Aliteremsha Kitabu kwa mja na Mtume Wake, Muhammad, Rehema za Allah تعالى zimshukie daima mpaka Siku ya Malipo. Pia, Allah تعالى Ameisifu Nafsi Yake Yenye Utukufu mkubwa sana usioweza kufikirika (kiakili). Pia Amesifia Hikima Yake katika Kauli na Matendo Yake. Akasema:

مَا خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ

“Hatukuziumba mbingu na ardhi wala yaliyomo baina yake ila kwa haki...”

Maana yake: Si katika njia ya mchezo na ubatilifu,

وَأَجَلٍ مُّسَمًّى

“...na kwa muda maalumu.” Katika muda maalumu uliowekwa, hauzidi wala haupungui. Kauli ya Allah تعالى:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا عَمَّا أُنذِرُوا مُعْرِضُونَ

“Na waliokufuru wanayapuuza yale wanayoonywa.”

Maana yake: Wamevutwa mawazo juu ya kilichokusudiwa kwao, wamepumbazika na kuacha walichoambiwa. Allah تعالى Alikwishawateremshia Kitabu na Alishawapelekea Mitume, lakini wameyakataa yote hayo. Hivi karibuni watatambua matokeo ya tabia hiyo.

Kubainisha Uwongo wa Washirikina

Halafu, Allah تعالى Akasema:

قُلْ

“Sema...”

Kuwaambia hao washirikina wenye kumshirikisha Allah تعالى,

أَرَأَيْتُمْ مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ أُوْنِي مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ

**“Je! Mwawaona wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu?
Nionesheni wameumba nini katika ardhi...” (46:4)**

Maana yake: Nielekezeni sehemu waliyohusika kuiumba katika ardhini,

أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَوَاتِ

“...au hao wanayo shirika katika mbingu?”

Maana yake: Wala hawana ushirika wa mbinguni wala ardhini, wala hawamiliki japo uzi wa kokwa ya tende. Ufalme na Mamlaka yote ni ya Allah تعالى, ‘basi vipi mnamuabudu Allah تعالى pamoja na mwingine na pia mnamshirikisha? Ni nani aliyekuelekezeni haya? Ni nani aliyekuiteni mfanye hivyo? Yeye Ndiye Aliyekuamrisheni hivyo? Ama hilo ni jambo mliloliamua nyinyi wenyewe?’ Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

أَتُؤْنِي بِكِتَابٍ مِّن قَبْلِ هَذَا

“Nileteeni Kitabu kilichokuwa kabla ya hiki...”

Nileteeni kitabu kimojawapo cha Allah تعالى kilichoteremshwa kwa Mitume, Rehema na amani ziwe juu yao, ambacho kinakuamrisheni kuyaabudu masanamu haya,

أَوْ أَتْرَقَ مِن عِلْمٍ

“...au alama yoyote ya elimu...”

Inamaanisha, dalili bayana ya kuthibitisha njia hii mnayoipitia,

إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

“...ikiwa mnasema kweli.”

Kwa kuwa hamna dalili ya maandishi wala ya kiakili. Kwa ajili hii, wengine walisoma hivi,

(أَوْ أَثَرَةٍ مِنْ عِلْمٍ)

“...au atharatin min ‘ilmin (au alama yoyote ya elimu)...”

Maana yake ‘Au katika elimu sahihi mliyoirithi kutoka kwa mmojawapo wa watu wa kabla yenu.” Ni kama alivyosema Mujahid juu ya Kauli ya Allah تعالى:

أَوْ أَثَرَةٍ مِنْ عِلْمٍ

“...au alama yoyote ya elimu...”

Kuwa ni, ‘au yeyote aliyerithi elimu.”¹ Kauli ya Allah تعالى:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنِ
دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ﴿٦٠﴾ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴿٦١﴾

“Na nani mpotovu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao.”

Maana yake: Hapana aliye mpotovu zaidi kuliko mwenye kuyaomba masanamu badala ya Allah تعالى, na anahitaji kutoka kwao mambo ambayo hayo masanamu hayawezi kuyafanya, mpaka Siku ya Kiyama. Masanamu hayatambui anayoyasema, hayasikii, hayaoni, wala hayashiki. Ni kwa sababu, hayo ni mawe yasiyo hai wala hayasemi. Kauli ya Allah تعالى:

وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴿٦١﴾

“Na ambapo watu watakapokusanywa watakuwa maadui zao, na watakataa ibada yao.”

¹ At-Tabari 22:94.

Ni sawa na Kauli Yake nyingine,

وَاتَّخِذُوا مِن دُونِ اللَّهِ إِلَهَةً لِّيَكُونُوا لَهُمْ عِزًّا ﴿٤٦﴾ كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادِهِمْ وَيَكُونُونَ
عَلَيْهِمْ ضِدًّا ﴿٤٧﴾

“Na wamejaalia miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili ati iwape nguvu. Sivyoo kabisa! Wataikataa hiyo ibada yao, na watakuwa ndio dhidi yao.” (19:81-82)

Kwamba watawasaliti baada ya kuwa watawahitaji sana. *Al-Khalil* alisema:

وَقَالَ إِنَّمَا اتَّخَذْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ أَوْثِنًا مَّوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
يَكْفُرُ بَعْضُكُم بِبَعْضٍ وَيَلْعَنُ بَعْضُكُم بَعْضًا وَمَأْوَأَتُكُم النَّارُ وَمَا لَكُم مِّن
نَّاصِرِينَ ﴿٢٩﴾

“Hakika nyinyi mmejaalia masanamu waungu badala ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yaliyo baina yenu katika uhai wa duniani. Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi, na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi. Na makaazi yenu yatakuwa ni Motoni. Wala hamtapata wa kukunusuruni.” (29:25)

وَإِذَا تَتَلَىٰ عَلَيْهِمْ ءَايَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٣٠﴾
أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ قُلْ إِنِ افْتَرَيْتُهُ فَلَا تَمْلِكُونَ لِي مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۗ هُوَ أَعْلَمُ بِمَا
تُفِيضُونَ فِيهِ كَفَىٰ بِهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۗ وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٣١﴾ قُلْ مَا كُنْتُ بِدَعَا
مِّنَ الرُّسُلِ وَمَا أَدْرَىٰ مَا يُفَعَّلُ بِي وَلَا يَكْرَهُ إِنِ اتَّبِعْتُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ وَمَا أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ
مُّبِينٌ ﴿٣٢﴾

7. “Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, waliokufuru husema juu ya haki inapowajia: Huu ni uchawi ulio dhahiri.”

8. “Au wanasema: Ameyazua mwenyewe! Sema: Ikiwa nimeyazua mimi, basi nyinyi hamuezi kunifaa chochote mbele ya Mwenyezi

Mungu. Yeye Anajua zaidi hayo mnayoyasukuma; Anatosha kuwa Shahidi baina yangu na nyinyi. Na Yeye Ndiye Mwingi wa Msamaha, Mwingi wa Rehema.”

9. “Sema: Mimi si mpya miongoni mwa Mitume. Wala sijui nitakavyofanywa mimi wala nyinyi. Mimi nafuata niliyofunuliwa tu kwa Wahyi, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji wa wazi wazi.”

Kubainisha Uwongo wa Kauli za Washirikina Dhidi ya Qur’an na Mtume ﷺ na Majibu yao

Allah تعالى Anaeleza kuhusu ukafiri na ufidhuli wa washirikina, kuwa wanaposomewa waziwazi Aya za Allah تعالى bainifu, wao husema:

هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ

“Huu ni uchawi dhaahiri.”

Maana yake: Ni uchawi ulio wazi, wameongopa, wamezua, wamepotea na wamekufuru,

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَيْنَاهُ

“Au wanasema: Ameizua mwenyewe!”

Wakimkusudia Muhammad ﷺ. Allah تعالى Anawajibu:

قُلْ إِنْ افْتَرَيْتُمْ فَلَا تَمْلِكُونَ لِي مِنَ اللَّهِ شَيْئًا

“Sema: Ikiwa nimeizua mimi, basi nyinyi hamuezi kunifaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Inamaanisha, ikiwa nimemuongopea na nikadai kuwa Amenituma, basi Ataniadhibu vikali. Wala hataweza yeyote wa ardhini – nyinyi au wengine – kunikinga dhidi Yake,

قُلْ إِنِّي لَنْ يُجِيرَنِي مِنَ اللَّهِ أَحَدٌ وَلَنْ أَجِدَ مِنْ دُونِهِ مُلْتَحَدًا ﴿٤٦﴾ إِلَّا بَلَاغًا مِنَ اللَّهِ

وَرِسَالَتِي ۗ

“Sema: Hakika hapana yeyote awezae kunilinda na Mwenyezi Mungu, wala sitapata pa kukimbilia isipokuwa Kwake Yeye tu. Ila nifikishe Ujumbe utokao kwa Mwenyezi Mungu na risala Zake.” (72:22-23) Na,

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ ﴿٦٨﴾ لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٦٩﴾ ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ ﴿٧٠﴾
فَمَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ ﴿٧١﴾

“Na lau kama angelituzulia baadhi ya maneno tu. Bila ya shaka Tungemuadhibu kwa Mkono wa Kulia. Kisha kwa hakika Tungelimkata mshipa mkubwa wa moyo! Na hapana yeyote katika nyinyi ambaye angeliweza kutuzuia.” (69:44-47)

Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema katika Aya hii:

قُلْ إِنْ أَفْتَرَيْتُهُ، فَلَا تَمْلِكُونَ لِي مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۗ هُوَ أَعْلَمُ بِمَا تُفِيضُونَ فِيهِ ۗ كَفَىٰ بِهِ
شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۗ

“Sema: Ikiwa nimeizua mimi, basi nyinyi hamuezi kunifaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Yeye Anajua zaidi hayo mnayoropokwa; Anatosha kuwa Shahidi baina yangu na nyinyi.”

Hili ni karipio na onyo kali kwao wao. Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

“Na Yeye Ndiye Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Huku ni kuwabembeleza wafanye toba na warudi. Yaani, pamoja na haya yote, mkirudi na kutubu Ataipokea toba yenu, Atakuacheni, Atakughufurieni na Atakurehemuni. Aya hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى ndani ya Surat Al-Furqaan:

وَقَالُوا أَسْطِطِيرُ الْأَوَّلِينَ ۚ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّىٰ عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٦٧﴾ قُلْ أَنْزَلَهُ
الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ إِنَّهُ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٦٨﴾

“Na wakasema: Hivi ni visa vya watu wa kale alivyoviandika, anavyosomewa asubuhi na jioni. Sema: Ameyateremsha haya Ajuaye siri za mbinguni na ardhini. Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.” (25:5-6)

Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ مَا كُنْتُ بِدَعَاٍ مِّنَ الرُّسُلِ

“Sema: Mimi si mpya miongoni mwa Mitume.”

Inamaanisha, ‘Mimi si Mtume wa kwanza kuja duniani, bali Mitume wengi walikuja, kwa hivyo mimi sikuja na jambo lisilo na mfano wake, mpaka mfikie hatua ya kunikanusha (na mkauweka mbali utume wangu kwenu). Kabla yangu, Allah تعالى Aliwatuma Manabii katika umma mbalimbali.

Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا أَدْرِى مَا يُفَعِّلُ بِي وَلَا يَكْرَهُ

“Wala sijui nitakavyofanywa wala nyinyi.”

Ibn Abu Twalhah amesema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alitoa rai kuhusu Aya hii: “Baada yake” ikashuka aya ifuatayo,

لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ

“Ili Mwenyezi Mungu Akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo...” (48:2)¹

‘Ikrimah, Al-Hasan na Qatadah wamesema hivyo hivyo, kuwa Aya hiyo hukumu yake imefutwa na aya ifuatayo,

لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ

“Ili Mwenyezi Mungu Akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo...” (48:2)

¹ At-Tabari 22:99.

Wamesema: Iliposhuka Aya hii, mtu mmoja miongoni mwa Waislamu alisema, “Hapa, Allah تعالى Amebainisha Atakachokufanyia wewe, ewe Mjumbe wa Allah تعالى! Atatufanyia nini sisi?”

Allah تعالى Akashusha Aya:

لِيُدْخِلَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Ili Awaingize Waumini wanaume na Waumini wanawake katika Bustani zipitazo mito kati yake”. (48:5)¹

Hivyo ndivyo Alivyosema. Kilichothibiti ndani ya Sahih ni kuwa Waumini walisema: “Pongezi kwako ewe Mjumbe wa Allah! Sisi je?” Allah تعالى Akashusha Aya hii.²

Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Khaarijah bin Zayd bin Thabit kutoka kwa Umm Al-'Alaa رضي الله عنها mwanamke wa Kianswaar ambaye alipata kumuunga mkono Mtume ﷺ alimpa habari: “Answaar walipiga kura ya kuwapa makazi Muhajiruna. Kura yangu ilimuangukia 'Uthmaan bin Madh'un, ambaye maradhi yalimsumbua alipokuwa nyumbani kwetu, hivyo tukamuuguza mpaka akafariki dunia kisha tukamkafini. Mtume ﷺ akaja kwetu, nami nikasema: “Rehema za Allah تعالى zikushukie ewe Abu Sa-ib! Natoa ushuhuda wangu juu yako kwamba Allah تعالى Amekupa utukufu.”

Mtume ﷺ akasema:

«وَمَا يُذْرِكُ أَنَّ اللَّهَ تَعَالَى أَكْرَمُهُ»

“Ni nini kilichokujulisha kuwa Allah Taala Amemkirimu?”

Nikajibu: “Sijui – baba na mama yangu wawe ni fidia kwako!” Mtume ﷺ akasema:

«أَمَّا هُوَ فَقَدْ جَاءَهُ الْيَقِينُ مِنْ رَبِّهِ، وَإِنِّي لَأَرْجُو لَهُ الْخَيْرَ. وَاللَّهِ مَا أَدْرِي وَأَنَا رَسُولُ
اللَّهِ مَا يُفْعَلُ بِي»

¹ At-Tabari 22:99,100.

² Fath Al-Bari 7:516.

“Ama kumhusu yeye, yakini (kifo) imemujia kutoka kwa Mola Mlezi Wake, nami namtarajia kheri. Wallah! Ingawa mimi ni Mjumbe wa Allah, sijui nitafanywa nini (baada ya kufariki).”

Nikasema: “Wallah! Abadani sitamtakasa yeyote baada Yake milele.” Tukio hilo likanihuzunisha, nikalala, nikaota kwamba ‘Uthman anamiliki chemchem inayobubujika. Nikaja kwa Mtume ﷺ na nikampa habari hiyo. Mtume ﷺ akasema:

«ذَٰكَ عَمَلُهُ»

“Hiyo ni amali yake.”¹ Ameipokea Bukhari peke yake. Muslim hakuinukuu. Ama kuhusu kauli yake,

«مَا أَدْرِي وَأَنَا رَسُولُ اللَّهِ مَا يَفْعَلُ بِهِ»

“Ingawa mimi ni Mjumbe wa Allah, sijui nitakachofanywa (baada ya kufariki).”²

Hadithi hiyo na mithili yake ni ushahidi kwamba, hairuhusiwi kutamka kwamba mtu fulani ni wa Peponi, isipokuwa wale waliotajwa na Allah تعالى. Hao ni kama wale Masahaba kumi³ na Ibn As-Salaam, Al-Ghumaysaa, Bilaal, Suraaqah, ‘Abdullah bin ‘Umar bin Haraam (baba wa Jaabir), waliohifadhi Qur’an sabini waliouawa vita ya *Biiri Mauna*, Zayd bin Harithah, Ja’far, Ibn Rawaahah na mfano wao, Allah تعالى Awaridhie nao. Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ

“Mimi nafuata niliyo funuliwa tu kwa Wahyi...”

Inamaanisha, ‘Mimi nafuata wahyi Alionifunulia Allah تعالى’

وَمَا أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ مُّبِينٌ

“...wala mimi si chochote ila ni mwonyaji wa wazi wazi.”

Maana yake, ‘Maonyo yangu yako dhahiri kwa kila mtu mwenye uelewa.’ Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

¹ Ahmad 6 436 na *Fath al-Bari* 7:310.

² *Fat’h al-Bari* 3: 137.

³ Wao ni Abu Bakr, ‘Umar, ‘Uthman, ‘Ali, Talhah, Az-Zubayr, ‘Abdur-Rahman bin ‘Awf, ‘Sa’d bin Abi Waqqas, Sa’id bin Zayd, na Abu ‘Ubaydah bin Al-Jarrah.

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كَانَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَكَفَرْتُمْ بِهِ وَشَهِدَ شَاهِدٌ
 مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَىٰ مِثْلِهِ فَقَامَنَ وَأَسْتَكْبَرْتُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠﴾ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ
 ءَامَنُوا لَوْ كَانَ خَيْرًا مَا سَبَقُونَا إِلَيْهِ وَإِذْ لَمْ يَهْتَدُوا بِهِ
 فَسَيَقُولُونَ هَذَا إِنْكَارٌ قَدِيمٌ ﴿١١﴾ وَمِنْ قَبْلِهِ كَتَبَ مُوسَىٰ
 إِمَامًا وَرَحْمَةً ۗ وَهَذَا كِتَابٌ مُصَدِّقٌ لِسَانًا عَرَبِيًّا لِيُنذِرَ
 الَّذِينَ ظَلَمُوا وَيُشْرَىٰ لِلْمُحْسِنِينَ ﴿١٢﴾ إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا
 رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَفْتَمُوا فَلَا خَوْفَ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ
 يَحْزَنُونَ ﴿١٣﴾ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ خَالِدِينَ فِيهَا جَزَاءً
 بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾ وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا
 ۗ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا ۗ وَحَمَلُهُ وَفِصْلُهُ ثَلَاثُونَ
 شَهْرًا ۗ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَبَلَغَ أَرْبَعِينَ سَنَةً قَالَ رَبِّ
 أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ
 وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِي ۗ إِنِّي تُبْتُ
 إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٥﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ نَتَقَبَّلُ عَنْهُمْ
 أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَتَتَجَاوَزُ عَنْ سَيِّئَاتِهِمْ فِي أَصْحَابِ الْجَنَّةِ ۗ
 وَعَدَ الصَّادِقِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿١٦﴾

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كَانَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ
 وَكَفَرْتُمْ بِهِ وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِنْ بَنِي
 إِسْرَائِيلَ عَلَىٰ مِثْلِهِ فَقَامَنَ
 وَأَسْتَكْبَرْتُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي
 الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠﴾ وَقَالَ الَّذِينَ
 كَفَرُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا لَوْ كَانَ خَيْرًا
 مَا سَبَقُونَا إِلَيْهِ وَإِذْ لَمْ يَهْتَدُوا بِهِ
 فَسَيَقُولُونَ هَذَا إِنْكَارٌ قَدِيمٌ ﴿١١﴾
 وَمِنْ قَبْلِهِ كَتَبَ مُوسَىٰ إِمَامًا
 وَرَحْمَةً ۗ وَهَذَا كِتَابٌ مُصَدِّقٌ لِسَانًا
 عَرَبِيًّا لِيُنذِرَ الَّذِينَ ظَلَمُوا وَيُشْرَىٰ
 لِلْمُحْسِنِينَ ﴿١٢﴾ إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا
 رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَفْتَمُوا فَلَا خَوْفَ
 عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٣﴾
 أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ خَالِدِينَ فِيهَا
 جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

10. "Sema: Mnaonaje ikiwa kitabu hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi mkaikataa, na akashuhudia shahidi miongoni mwa Wana wa Israeli mfano wake, na wakayaamini, na nyinyi mnafanya kiburi? Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wenye kudhulumu."

11. *“Na waliokufuru waliwaambia walioamini: Lau ingekuwa ni ya kheri, wasingelitutangulia. Na walipokosa kuongoka wakasema: Huu ni uzushi wa zamani.”*

12. *“Na kabla yake kilikuwapo Kitabu cha Musa, chenye uwongozi na rehema. Na hiki ni Kitabu ni chenye kusadikisha kilichokuja kwa lugha ya Kiarabu, ili kiwaonye waliodhulumu, na kiwe ni bishara kwa watendao wema.”*

13. *“Hakika waliosema: Mola Wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu; kisha wakawa na msimamo, hawatakuwa na khofu, wala hawatahuzunika.”*

14. *“Hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo, hali ya kuwa ni malipo kwa waliyokuwa wakiyatenda.”*

Qur’an ni Maneno ya Kweli ya Allah تعالى na Namna Wanavyoichukulia Makafiri na Waumini.

Allah تعالى Anasema:

قُلْ

“Sema...”

Ewe Muhammad! Kuwaambia hawa washirikina wanaoikataa Qur’an,

أَرَأَيْتُمْ إِنْ كَانَ

“Mnaonaje ikiwa (Qur’an)...” Qur’an hii,

مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَكَفَرْتُمْ بِهِ

“...(ni kweli) imetoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi mkaikanusha...”

Maana yake: Mnadhani Allah تعالى Atakufanyieni kitu gani ikiwa Kitabu hiki nilichokujieni nacho, ni kweli kilishushwa kwangu ili nikufikishieni, nanyi mumekikataa na kukipinga,

وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَىٰ مِثْلِهِ

“...na akakishuhudia shahidi miongoni mwa Wana wa Israeli mfano wake...”

Wameshuhudia ukweli na kimesadikishwa na Vitabu vilivyotangulia ambavyo viliteremshwa kwa Manabii (Rehema na amani ziwashukie) kabla yangu. Nimetoa bishara na nimeeleza mithili ya vile ilivyoeleza hii Qur'an. Kauli ya Allah تعالى:

فَقَامَنَ

"...na akaamini..."

Huyu aliyasadiki ukweli wake, kutoka kwa Wana wa Israel kwa sababu ya kufahamu kwake kwamba ni cha kweli,

وَأَسْتَكْبِرُكُمْ

"...na nyinyi mnafanya kiburi?"

Mkaacha kukifuata. Masruq alisema: "Shahidi huyu akakiamini Kitabu na Mtume Wake, nanyi mkamkataa Nabii wenu na Kitabu chenu."¹

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

"Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wenye kudhulumu."

Na shahidi huyu anaweza akawa 'Abdullah bin Salaam¹ رضي الله عنه, au mtu mwingine kwani Aya hii ilishuka Makkah kabla 'Abdullah bin Salaam رضي الله عنه hajasilimu. Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَإِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ قَالُوا ءَأَمَنَّا بِهِ ءِ إِنَّهُ الْحَقُّ مِن رَّبِّنَا إِنَّا كُنَّا مِن قَبْلِهِ مُسْلِمِينَ ﴿٥٣﴾

"Na wanaposomewa wanasema: Tunaiamini. Hakika hii ni Haki inayotoka kwa Mola Wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa ni Waislamu, tulionyenyekea." (28:53)

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِن قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلْآذَانِ سُجَّدًا ﴿٥٤﴾ وَيَقُولُونَ سُبْحَانَ رَبِّنَا إِن كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿٥٥﴾

¹ At-Tabari 22: 103-104.

“Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake, wanaposomewa Qur’an, huanguka kifudifudi wanasujudu. Na wanasema: Subhana Rabbina, Ametakasika Mola Wetu Mlezi! Hakika ahadi ya Mola Wetu Mlezi lazima itimizwe!” (17:107-108)

Sa’d رضي الله عنه amesema: “Sijapata kumsikia Mtume ﷺ akimuambia yeyote akiwa angali anatembea juu ya uso wa dunia kwamba ni miongoni mwa watu wa Peponi, isipokuwa ‘Abdullah bin Salaam رضي الله عنه, na ilishuka Aya hii kumhusu yeye,

وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَىٰ مِثْلِهِ

“...na akashuhudia shahidi miongoni mwa Wana wa Israeli juu ya mfano wake...”

Hadithi hii ameipokea Bukhari, Muslim na An-Nasai.² Ibn ‘Abbas, Mujahid, Adh-Dhahhak, Qatadah, ‘Ikrimah, Yusuf bin ‘Abdullah bin Salaam, Hilaal bin Yasaaf, As-Suddi, Ath-Thawri, Malik bin Anas na Ibn Zaid, wote wamesema: “Ni ‘Abdullah bin Salaam رضي الله عنه.”³ Kauli ya Allah تعالى:

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا لَوْ كَانَ خَيْرًا مَا سَبَقُونَا إِلَيْهِ

“Na waliokufuru waliwaambia walioamini: Lau ingelikuwa hii ni kheri, wasingelitutangulia.”

Maana yake: Makafiri waliwaambia wenye kuiamini Qur’an: “Kama Qur’an ingelikuwa na kheri yoyote, basi wasingelitutangulia kwenye hilo.” Kwa maneno hayo, wanawakusudia Bilal, ‘Ammar, Suhayb na Khabbab, Allah تعالى Awaridhie wote. Pia na wengine wenye kushabihiana nao waliokuwa wanyonge, watumwa na vijakazi. Kwa ujumla hawana jingine, bali kwa sababu wanadhani kwamba wana hadhi ya juu mbele ya Allah تعالى, na kwamba Anawapa hifadhi. Kwa kufanya kwao hivyo, wamefanya kosa kubwa sana.

¹ Msomi wa Kiyahudi aliyesilimu mbele ya Mtume ﷺ.

² At-Tabari 22:104. Hayo yamenukuliwa na Al-Bukhari (*Fat’h Al-Bari* 7:160), Muslim 4:1930, na An-Nasai katika *Al-Kubra* 5:70.

³ At-Tabari 22:104-105, na Al-Qurtubi 16:188.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَكَذَلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لِيَقُولُوا أَهَؤُلَاءِ مَنَّ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنْ بَيْنِنَا ﴿٥٣﴾

“Na hivi ndivyo Tunavyowajaribu wao kwa wao, ili waseme: Ni hao ndio Mwenyezi Mungu Amewafadhilisha miongoni mwetu?”
(6:53)

Wanastaajabu, ‘vipi hao waongoke bila ya sisi?’ kwa minajili hiyo, walisema:

لَوْ كَانَ خَيْرًا مَّا سَبَقُونَا إِلَيْهِ ﴿٥٤﴾

“Lau ingelikuwa hii ni kheri, wasingelitutangulia.”

Ama Ahlus-Sunnah Wal-Jama’ah wanasema kuwa kila kauli au kitendo ambacho hakikuthibiti kutoka kwa Masahaba, Allah تعالى Awaridhie: “ni bidaa (uzushi) kwani kama ingelikuwemo kheri ndani yake, basi wangelitutangulia kuitenda kheri hiyo, kwani wao hawakuacha hata jambo moja miongoni mwa mambo ya kheri, isipokuwa wameharakisha kuitenda.’ Kauli ya Allah تعالى:

وَإِذْ لَمْ يَهْتَدُوا بِهِ

“Na walipokosa kuongoka...” Kwa Qur’an,

فَسَيَقُولُونَ هَذَا إِفْكٌ قَدِيمٌ

“...Wakasema: Huu ni uzushi wa zamani.”

Kwamba ni uongo wa zamani. Wanamaanisha kuwa Qur’an ni mapokeo ya watu wa zamani, wanaitia ila Qur’an na wanaoifuata. Hicho ni kiburi alichokisema Mtume ﷺ:

«بَطَرُ الْحَقِّ وَغَمَطُ النَّاسِ»

“(Kiburi) ni kukataa ukweli na kuwadharau watu.”¹

¹ Imeandikwa na Muslim 1:93.

Halafu, Allah تعالى Alisema:

وَمِن قَبْلِهِ كِتَابُ مُوسَىٰ

“Na kabla yake kilikuwapo Kitabu cha Musa...”

Ambacho ni Taurati,

إِمَامًا وَرَحْمَةً ۗ وَهَذَا كِتَابٌ

“...kuwa chenye uwongozi na rehema. Na Kitabu hiki...”

Maana yake: Qur’an,

مُصَدِّقٌ

“...ni chenye kusadikisha...”

Vitabu vilivyokuja kabla yake,

لِسَانًا عَرَبِيًّا

“...na kilichokuja kwa lugha ya Kiarabu.”

Maana yake: Fasaha, bayana na wazi,

لِيُنذِرَ الَّذِينَ ظَلَمُوا وَيُشْرَىٰ لِلْمُحْسِنِينَ

“ili kiwaonye waliodhulumu, na kiwe ni bishara kwa watendao wema.”

Kwamba, kimekusanya maonyo kwa makafiri na bishara kwa Waumini. Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا

“Hakika waliosema: Mola Wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu; kisha wakawa na msimamo.”

Tafsiri yake imeshatangulia katika Surat As-Sajdah, (angalia (41:30)).

Kisha Allah تعالى Anasema:

فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ

“...hawatakuwa na khofu...” Kuhusu mustakabali wao,

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ

“...wala hawatahuzunika.”

Kwa yaliyopita,

﴿١٥﴾ أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ خَالِدِينَ فِيهَا جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

“Hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo, hali ya kuwa ni malipo kwa waliyokuwa wakiyatenda.”

Kwamba, amali ni sababu ya wao kupata rehema na yaliyofungamana nayo - Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا ۖ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا ۖ وَحَمَلُهُ وَفِصْلُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا ۚ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ أَشُدَّهُ ۖ وَبَلَغَ أَرْبَعِينَ سَنَةً قَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِي ۗ إِنِّي تُثِيبُ إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٥﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ نَتَقَبَّلُ عَنْهُمْ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَنَتَجَاوَزُ عَنْ سَيِّئَاتِهِمْ فِي أَصْحَابِ الْجَنَّةِ ۖ وَعَدَّ الصَّدَقِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿١٦﴾

15. “Na Tumemuusia mwanaadamu awatendee wema wazazi wake wawili. Mama yake amechukua ujauzito wake kwa taabu, na akamzaa kwa taabu. Na kuchukua ujauzito wake hadi kumuachisha ziwa ni miezi thelathini. Hata anapofika utuuzima wake, na akafikisha miaka arubaini, husema: Mola Wangu Mlezi! Niwezeshe nishukuru neema Zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na nitende wema Unaoupenda. Na Unitengenezee kizazi changu. Hakika mimi nimetubu Kwako, na mimi ni miongoni mwa Waislamu.”

16. “Hao ndio Tunaowakubalia mazuri waliotenda, na Tunayasamehe makosa yao. Watakuwa miongoni mwa watu wa Peponi. Miadi hiyo waliyoahidiwa ni ya kweli.”

Wasia wa Allah تعالى kwa Wazazi Wawili

Allah تعالى Alipotaja katika Aya ya kwanza kumpwekesha Yeye, kufanya ikhilasi katika ibada na kuwa na msimamo Kwake Yeye, Allah تعالى Alifuatishia hayo kwa Kutoa maagizo kuhusu wazazi wawili sawa na Alivyoyataja mambo hayo mawili kwa pamoja katika Aya nyingi za Qur'an. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

“Na Mola Wako Mlezi Amehukumu kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema.” (17:23) na,

أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَيَّ الْمَصِيرُ ﴿١٤﴾

“Nishukuru Mimi na wazazi Wako. Ni Kwangu Mimi ndiyo marudio.” (31:14)

Kuna Aya nyingine nyingi kama hii. Allah تعالى Alisema pia,

وَوَصَّيْنَا الْآلَ نَسْنِ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا ط

“Na Tumemuusia mwanaadamu awatendee wema wazazi wake wawili.” (46:15)

Maana yake: Tumemuamrisha kuwafanyia ihsani wazazi wawili na kuwa na huruma kwao. Abu Dawud At-Twayaaliys ameipokea kutoka kwa Sa'd alisema: mama yake alimuambia: “Allah تعالى Aameamuru kuwatii wazazi wawili, kwa hivyo, sitakula wala kunywa mpaka umkufuru Allah تعالى.” Akajizuia kula na kunywa mpaka watu wakawa wanajaribu kufungua kinywa chake kwa fimbo.

Ikashuka Aya hii:

وَوَصَّيْنَا الْآلَ نَسْنِ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا ط

“Na Tumemuusia mwanaadamu awatendee wema wazazi wake wawili.”¹

¹ Musnad At-Tayalis (28). Masimulizi haya yanamhusu Luqman 31:14-15. Pia angalia na. 6238 ya Muslim.

Ameipokea Muslim na waandishi wengine wa Suna isipokuwa Ibn Majah,¹

حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا

“Mama yake amechukua ujauzito wake kwa taabu...”

Maana yake: Mama yake alikumbana na mashaka na taabu katika hali ya ujauzito wake, kama vile, uchovu, homa, kutapika, uzito na dhiki na ghairi ya hayo katika taabu na mashaka yanayoambatana na ujauzito,

وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا

“...na akamzaa kwa taabu.”

Pia kwa maana ya mashaka ya kujifungua na shida zake,

وَحَمَلَهُ وَفَضَّلَهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا

“Na kuchukua ujauzito wake mpaka kumwachisha ziwa ni miezi thalathini.”

Uthibitisho wa Hukumu ya Muda wa Ujauzito Kuwa Miezi Sita.

‘Ali رضي الله عنه aliitolea dalili Aya hii pamoja na iliyo katika Surat Luqman:

وَفَضَّلَهُ فِي عَامَيْنِ

“...na kumuachisha ziwa baada ya miaka miwili.” (31:14) Na,

وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُتِمَّ الرَّضَاعَةَ

“Na wazazi wanawake wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili kwa anayetaka kutimiza kunyonyesha.” (2:233)

Maana yake: Uchache wa muda wa ujauzito ni miezi sita. Huu ni unyambuaji wenye nguvu na sahihi, na uliafikiwa hilo na ‘Uthman na Masahaba wengi,

¹ Muslim 4:1878, Abu Dawud 3:177, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:48, na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:348.

Allah رحمته الله تعالى Awe radhi nao. Muhammad bin Is-haq bin Yasaar¹ alisimulia kutoka kwa Ba'jah bin 'Abdullah Al-Juhaniy amesema: "Mmoja wetu alimuoa mwanamke wa kutoka Juhaynah. Akamzalia mtoto baada ya kutimia miezi sita. Akaenda kwa 'Uthman رضي الله عنه na akamtajia jambo hilo. Akatuma ujumbe kwa mwanamke huyo. Na aliposimama kuvaa vizuri nguo zake, dada yake akalia. Akamuuliza: "Nini kinachokuliza? Wallah! Hapana kiumbe yeyote wa Allah تعالى Aliyenikaribia (kwa jimai) kamwe, isipokuwa yeye (mume). Basi, Allah تعالى Anihukumu Atakavyo Yeye." Alipopelekwa Mwanamke huyo kwa Uthman رضي الله عنه aliamuru apigwe mawe. Habari hiyo ikamfikia 'Ali رضي الله عنه Akaja kwa 'Uthman رضي الله عنه na kumuuliza: "Unataka kufanya nini?" Akasema: "Amejifungua baada ya ujauzito kutimiza miezi sita kamili. Hilo linawezekana?" 'Ali رضي الله عنه akamuuliza: "Umesoma Qur'an?" Akajibu: "Ndiyo." Akauliza tena: "Umesikia kuwa Allah تعالى Amesema:

وَحَمَلُهُ وَفَصَلَّهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا

"Na kuchukua ujauzito wake mpaka kumuachisha ziwa ni miezi thalathini."

Na Kauli Yake nyengine,

حَوْلِينَ كَامِلِينَ

"...miaka miwili kamili..." (2:233)

Tunakuta kuwa unapotoa miaka miwili ya kunyonyesha ambayo ni sawa na miezi 24 inabaki miezi sita katika miezi 30, ya muda wa ujauzito na umuachishe mtoto. 'Uthman رضي الله عنه akanena: "Wallah! Hili sikulijua. Mrejesheni mwanamke." Lakini wakamkuta kauawa. Ba'jah akaendelea: Wallah! Si kunguru kwa kunguru, wala yai kwa yai vinavyoweza kushabihiana na jinsi alivyokuwa mtoto yule na baba yake. Baada ya baba yake kuona hivyo, alisema: "Wallah! Ni mwanangu, wala hapana mashaka hata kidogo." Baadaye, Allah تعالى Alimpa mateso ya kuwa na donda lenye usaha usoni mwake (kwa sababu ya kumsingizia mkewe). Liliendelea kumla mpaka akafariki.²

¹ Masimulizi haya hayakufikishwa kiusahihi

² Ibn Abi Hatim na Ibn Al-Mundhir kwa mujibu wa *Ad-Dur Al-Manthur* 6:9. Kama ilivyoelezwa hapo juu, haya ni masimulizi dhaifu.

Aliyanukuu haya Ibn Abu Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى. Ibn Abu Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى kutoka kwa 'Ikrimah alimsikia Ibn 'Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا kuwa alisema: "Mwanamke akizaa baada ya kutimia miezi tisa, basi inamtosha mtoto kunyonyeshwa kwa miezi ishirini na mmoja, akizaa baada ya miezi saba, miezi ishirini na tatu itamtosha na ikiwa ni baada ya miezi sita, basi ni miaka miwili kamili. Ni kwa sababu, Allah تَعَالَى Amesema:

وَحَمَلُهُ وَفَصْلُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا حَتَّى إِذَا بَلَغَ أَشُدَّهُ

"Na kuchukua ujauzito wake hata kumuachisha ziwa ni miezi thalathini. Hata anapopata nguvu zake..."¹

Maana yake: Akawa mwenye nguvu, kijana na akapevuka.

وَبَلَغَ أَرْبَعِينَ سَنَةً

"...na akafikilia miaka arubaini..."

Ilisemwa pia kuwa, kwa kawaida, mtu hatabadilika kutoka vile alivyo, mara afikiapo umri wa miaka arubaini.

قَالَ رَبِّ أَوْزَعْنِي

"...husema: Mola Wangu Mlezi! Niwezeshe..."

Inamaanisha, 'Nipe ilhamu.'

أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ

"...nishukuru neema Zako Ulizo nineemesha mimi na wazazi wangu, na nitende mema unayo yapenda."

Maana yake: Kwa hapo baadaye,

وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِي

"Na Unitengenezee dhuria wangu."

Kwa maana ya kizazi changu na wanaonifuata,

¹ Al-Bayhaqi 7:332.

إِنِّي تُبْتُ إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ

“Hakika mimi nimetubu Kwako, na mimi ni miongoni mwa Waislamu.”

Hii ina mwongozo kwa mwenye kufikisha miaka arubaini kwamba atubu upya na kujirudi kumuelekea Allah تعالى na aliazimie hilo kwa dhati. Allah تعالى Amesema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ نَتَقَبَّلُ عَنْهُمْ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَتَتَجَاوَزُ عَنْ سَيِّئَاتِهِمْ فِي أَصْحَابِ الْجَنَّةِ ۗ

“Hao ndio Tunawakubalia mazuri waliotenda, na Tunayasamehe makosa yao. Watakuwa miongoni mwa watu wa Peponi.”

Kwamba hao wenye sifa zilizotajwa, wenye kutubu kwa Allah تعالى na kujirudi kwa kumuelekea, wenye kutumia toba na istighfari kwa ajili ya kuyadiriki yaliyowapita, ndio, tunawakubalia vitendo vyao bora walivyovitenda, na Tunayasamehe makosa yao. Wataghufuriwa mengi waliyoteleza na Tutawakubalia amali zao chache.

فِي أَصْحَابِ الْجَنَّةِ ۗ

“...miongoni mwa watu wa Peponi.”

Kwamba, wao ni katika jumla ya watu wa Peponi. Hii ndiyo hukumu yao kwa Allah تعالى. Ni sawa na Alivyowaahidi wenye kutubu na kujirudi. Kwa minajili hii, Allah تعالى Alisema:

وَعَدَ الْصِّدْقِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ

“Miadi hiyo walioahidiwa ni ya kweli.”

* * *

وَالَّذِي قَالَ لِيَوْلَادِهِ أَفِ لَكُمْ مَا تُعَدِّانِي أَنْ أُخْرَجَ وَقَدْ
 خَلَتْ الْقُرُونُ مِنْ قَبْلِي وَهُمَا يَسْتَفِغِيَانِ اللَّهَ وَبَلِّغْ لَهُمُ الْآيَاتِ
 مَا هُنَّ لِقَوْمِهِمْ إِلَّا لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٧﴾
 أُولَئِكَ الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي أَمْرٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ
 قَبْلِهِمْ مِنَ الْإِنْسِ وَالْإِنْسِ عَلَيْهِمْ لَكِبٌ إِنَّهُمْ كَانُوا خَاسِرِينَ ﴿١٨﴾
 وَلِكُلِّ دَرَجَةٍ عَمَلٌ يُعْمَلُ وَلِيُؤْفِقَهُمْ اللَّهُ فِي مَا كَانُوا
 يَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾ وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ أَلَيْسَ
 لَكُمْ فِي حَيَاتِكُمْ الدُّنْيَا وَاسْتَمْتَعْتُمْ بِهَا فَالْيَوْمَ يُجْزَوْنَ
 عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ
 وَبِمَا كُنتُمْ تَفْسُقُونَ ﴿٢٠﴾ * وَأَذْكُرْ أَخَا عَادٍ إِذْ أَنْذَرَ قَوْمَهُ
 بِالْأَحْقَابِ وَقَدْ خَلَتْ أَلْدُنُورُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ
 أَلَّا يُعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ
 ﴿٢١﴾ قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَأْفِكَنَا عَنْ آلِهَتِنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِنْ
 كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٢٢﴾ قَالَ إِنَّمَا أَلِمْ عِنْدَ اللَّهِ
 وَأُبْلِغُكُمْ مَا أُرْسِلْتُ بِهِ وَلَكِنِّي أَرَأَيْتُمْ قَوْمًا جَاهِلُونَ ﴿٢٣﴾
 فَلَمَّا رَأَوْهُ عَارِضًا مُسْتَقْبِلَ أَوْدِيَّتِهِمْ قَالُوا هَذَا عَارِضٌ
 مُمَطَّرٌ نَا بَلْ هُوَ مَا اسْتَعْجَلْتُمْ بِهِ رِيحٌ فِيهَا عَذَابٌ أَلِيمٌ
 ﴿٢٤﴾ تُدِيرُ كُلَّ شَيْءٍ بِأَمْرِ رَبِّهَا فَأَصْبَحُوا لَا يُرَى إِلَّا
 مَسَكِبُهُمْ كَذَلِكَ نُجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿٢٥﴾

وَالَّذِي قَالَ لِيَوْلَادِهِ أَفِ لَكُمْ مَا تُعَدِّانِي أَنْ أُخْرَجَ وَقَدْ
 خَلَتْ الْقُرُونُ مِنْ قَبْلِي وَهُمَا يَسْتَفِغِيَانِ اللَّهَ وَبَلِّغْ لَهُمُ الْآيَاتِ
 مَا هُنَّ لِقَوْمِهِمْ إِلَّا لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٧﴾
 أُولَئِكَ الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي أَمْرٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ
 قَبْلِهِمْ مِنَ الْإِنْسِ وَالْإِنْسِ عَلَيْهِمْ لَكِبٌ إِنَّهُمْ كَانُوا خَاسِرِينَ ﴿١٨﴾
 وَلِكُلِّ دَرَجَةٍ عَمَلٌ يُعْمَلُ وَلِيُؤْفِقَهُمْ اللَّهُ فِي مَا كَانُوا
 يَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾ وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ أَلَيْسَ
 لَكُمْ فِي حَيَاتِكُمْ الدُّنْيَا وَاسْتَمْتَعْتُمْ بِهَا فَالْيَوْمَ يُجْزَوْنَ
 عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ
 وَبِمَا كُنتُمْ تَفْسُقُونَ ﴿٢٠﴾ * وَأَذْكُرْ أَخَا عَادٍ إِذْ أَنْذَرَ قَوْمَهُ
 بِالْأَحْقَابِ وَقَدْ خَلَتْ أَلْدُنُورُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ
 أَلَّا يُعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ
 ﴿٢١﴾ قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَأْفِكَنَا عَنْ آلِهَتِنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِنْ
 كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٢٢﴾ قَالَ إِنَّمَا أَلِمْ عِنْدَ اللَّهِ
 وَأُبْلِغُكُمْ مَا أُرْسِلْتُ بِهِ وَلَكِنِّي أَرَأَيْتُمْ قَوْمًا جَاهِلُونَ ﴿٢٣﴾
 فَلَمَّا رَأَوْهُ عَارِضًا مُسْتَقْبِلَ أَوْدِيَّتِهِمْ قَالُوا هَذَا عَارِضٌ
 مُمَطَّرٌ نَا بَلْ هُوَ مَا اسْتَعْجَلْتُمْ بِهِ رِيحٌ فِيهَا عَذَابٌ أَلِيمٌ
 ﴿٢٤﴾ تُدِيرُ كُلَّ شَيْءٍ بِأَمْرِ رَبِّهَا فَأَصْبَحُوا لَا يُرَى إِلَّا
 مَسَكِبُهُمْ كَذَلِكَ نُجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿٢٥﴾

17. "Na ambaye amewa-
 fyonya wazazi wake na
 akawaambia: Ati ndio
 mnanitisha kuwa nita-
 fufuliwa, na hali vizazi vingi
 vimekwisha pita kabla

yangu! Na hao wazazi humuomba msaada Mwenyezi Mungu (na humuambia mtoto wao): Ole wako! Amini! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Na yeye husema: Hayakuwa haya ila ni visa vya watu wa kale."

18. "Hao ndio ambao imehakikishwa hukumu juu yao kama mataifa yaliyokwishapita kabla yao miongoni mwa majini na watu. Hakika hao wamepata hasara."

19. "Na wote watakuwa na daraja zao mbalimbali kwa waliyoyatenda, na ili awalipe kwa vitendo vyao, na wala hawatadhulumiwa."

20. "Na siku watakapoletwa waliokufuru kwenye Moto wataambiwa: Nyinyi mlitwaa vitu vyenu vizuri katika uhai wa duniani, na mkastareheshwa navyo. Basi leo ndio mnalipwa adhabu ya fedheha kwa mlivyokuwa mkitakabari katika ardhi bila ya haki, na kwa sababu mlikuwa mkifanya upotovu."

Kutaja Hatma ya Watoto Wakosefu kwa Wazazi wao na Hatima Yao

Baada ya Allah تعالى Kutaja watoto wenye kuwaombea dua nzuri wazazi wawili na kuwafanyia wema, kwamba wamefuzu na kufaulu, Allah تعالى Anageukia katika Kueleza hali ya watoto wakosefu kwa wazazi wao wawili.

Allah تعالى Anasema:

وَالَّذِي قَالَ لَوْلَا دَيْهِ أَفٍّ لَكُمْ

"Na ambaye amewafyonya wazazi wake..."

Neno "Uff" lililotumika katika Aya hii linajumuisha kila mwenye kuwatusi na kuwatolea lugha mbaya wazazi wake. Ama wenye kudai kuwa Aya hii ilishuka kumhusu 'Abdur-Rahman bin Abubakr رضي الله عنهما kauli yao ni dhaifu yenye kupingwa. Kwa sababu 'Abdur-Rahman bin Abubakr رضي الله عنهما alisilimu baada ya kushuka kwa Aya hiyo, akafanya vyema katika Uislamu wake na akawa miongoni mwa waliokuwa bora katika zama zake.

Imamu Bukhari amepokea kutoka kwa Yusuf bin Maahak kwamba Marwan (bin Al-Hakam) alikuwa kadhi wa Hijaz baada ya kuteuliwa na Mu'awiyah bin

Abu Sufyan رضي الله عنه (Marwan) akahutubu huku akimtaja Yazid bin Mu'awiyah ili watu wamuunge mkono (wam-ba'i) baada ya baba yake. 'Abdur-Rahman bin Abubakr رضي الله عنهما, akamuambia jambo (kuhusu hao wawili). Akasema: "Mchukueni." Akaingia nyumbani kwa 'Aishah رضي الله عنها na wakashindwa kumkamata. Marwan akasema: "Huyu ndiye ambaye Aya ifuatayo ilishuka kumhusu yeye,

وَالَّذِي قَالَ لَوْلَايَهُ أَفٍ لَّكُمْ أَتَعِدَانِي أَنْ أُخْرَجَ وَقَدْ خَلَتِ الْقُرُونُ مِنْ قَبْلِي

"Na ambaye amewafyonya wazazi wake na akawaambia: Ati ndio mnanitisha kuwa nitafufuliwa, na hali vizazi vingi vimekwisha pita kabla yangu!"

'Aishah رضي الله عنها akamjibu kutokea nyuma ya pazia: "Allah تعالى Hakuteremsha Aya yoyote kutuhusu (wana wa Abubakr رضي الله عنهم) isipokuwa tamko la kunitetea."¹

Katika simulizi nyingine, An-Nasai aliandika kuwa Muhammad bin Ziyaad alisema: Wakati Mu'awiyah alipokuwa akiwasihi watu wamuunge mkono (wam-ba'i) kwa ajili ya mwanaye, Marwan alitamka: "Huu ni mwenendo wa Abubakr na 'Umar." Baada ya kuyasikia haya, 'Abdur-Rahman bin Abubakr رضي الله عنهما alisema, "Bali huu ni mwenendo wa Kisultani, Hiraqli na Kaiser." Marwan akasema: "Huyu ndiye Ambaye Allah تعالى Alishusha Aya ifuatayo kumhusu yeye,

وَالَّذِي قَالَ لَوْلَايَهُ أَفٍ لَّكُمْ

"Na ambaye amewafyonya wazazi wake..."

Habari hiyo ikamfikia 'Aishah رضي الله عنها, akasema: "Marwan ameongopa. Wallah! Aya hiyo haihusiani kabisa na Abdurrahmani. Lau ningelitaka kumtaja mtu mwenye kusemwa katika Aya hiyo ningelifanya hivyo. Lakini, Mtume ﷺ alimlaani baba yake Marwan (Al-Hakam bin Abu Al-'As) wakati Marwan akiwa angali mgongoni mwake. Kwa hiyo, Marwan ni matokeo ya laana ya Allah تعالى."² Kauli ya Allah تعالى:

أَتَعِدَانِي أَنْ أُخْرَجَ

"Ati ndio mnanitisha kuwa nitafufuliwa..." Maana yake: Nifufuliwe.

¹ Fath Al-Bari 8:439. Alikuwa akirejea katika Surat An-Nur 24:11-18.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:458.

وَقَدْ خَلَّتِ الْقُرُونُ مِنْ قَبْلِي

“...na hali vizazi vingi vimekwisha pita kabla yangu!”

Kwamba watu wameondoka wala hajarejea mmoja wao mwenye kutoa habari,

وَهُمَا يَسْتَعِيثَانِ اللَّهَ

“Na hao wazazi humuomba msaada Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Wanamuomba Allah تعالى Amuongoze na wanamuambia mtoto wao,

وَيْلَكَ ءَامِنٌ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ فَيَقُولُ مَا هَذَا إِلَّا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ

**“Ole wako! Amini! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli.
Na yeye husema: Hayakuwa haya ila ni visa vya watu wa kale.”**

Kauli ya Allah تعالى:

أُولَئِكَ الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي أَمْرٍ قَدْ خَلَّتْ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ إِنَّهُمْ
كَانُوا خَاسِرِينَ ﴿٥٦﴾

**“Hao ndio ambao imehakikishwa hukumu juu yao kama mataifa
yaliyo kwisha pita kabla yao miongoni mwa majini na watu. Hakika
hao wamekuwa wamepata hasara.”**

Maana yake: Katika kundi hilo wanaingia wenye kushabihiana nao na wa rika lao, miongoni mwa makafiri wenye kuzitia hasara nafsi zao na ahli zao Siku ya Kiyama. Kauli ya Allah تعالى:

أُولَئِكَ

“Hao...”

Baada ya Kauli Yake,

وَالَّذِي قَالَ

“Na ambaye amesema...”

Ni dalili ya yale tuliyoyaeleza, kuwa ni maelezo yanayomgusa kila mwenye sifa kama hizo.

Al-Hasan na Qatadah walisema: “Ni kafiri mwovu mwenye kuwakosea adabu wazazi wake, mwenye kukadhibisha ufufuo.”¹

Kauli ya Allah تعالى:

وَلِكُلِّ دَرَجَةٍ مِّمَّا عَمِلُوا

“...Na wote watakuwa na daraja zao mbali mbali kwa waliyoyatenda...”

Kwamba kila adhabu italingana na amali yake,

وَلِيُؤْفِقَهُمْ أَعْمَالَهُمْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

“...na ili awalipe kwa vitendo vyao, na wala hawatadhulumiwa.”

Maana yake: Hatawadhulumu japo uzito wa chembe ya vumbi au chini zaidi ya hapo. ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam amesema, “Daraja za moto huwa zinakwenda chini na zile za Peponi hupanda juu.”² Kauli ya Allah تعالى:

وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ أَدَّهَبْتُمْ طَيِّبَاتِكُمْ فِي حَيَاتِكُمُ الدُّنْيَا وَأَسْتَمْتَعْتُمْ بِهَا

“Na siku watakapoletwa waliokufuru kwenye Moto wataambiwa: Nyinyi mlitwaa vitu vyenu vizuri katika uhai wa duniani, na mkastareheshwa navyo.”

Wataambiwa hayo kwa namna ya kushutumiwa na kukaripiwa. Amiri wa Waumini, ‘Umar bin Al-Khattwab رضي الله عنه aliyaacha mazuri mengi katika vyakula na vinywaji, na akajiepusha navyo. Akasema: “Nachelea nisije nikawa kama wale Aliowaeleza Allah تعالى, Akawashutumumu na Kuwafedhehesha,

أَدَّهَبْتُمْ طَيِّبَاتِكُمْ فِي حَيَاتِكُمُ الدُّنْيَا وَأَسْتَمْتَعْتُمْ بِهَا

“Nyinyi mlitwaa vitu vyenu vizuri katika uhai wa duniani, na mkastareheshwa navyo.”

Abu Mijlaz alisema: “baadhi ya watu watapoteza amali njema walizokuwa wakizifanya duniani, na wataambiwa,

¹ At-Tabari 20:118.

² At-Tabari 20:119.

أَذْهَبْتُمْ طَيِّبَاتِكُمْ فِي حَيَاتِكُمُ الدُّنْيَا

“Nyinyi mlitwaa vitu vyenu vizuri katika uhai wa duniani...” na,

فَالْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنْتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَإِذَا كُنْتُمْ
تَفْسُقُونَ

“Basi leo ndio mnalipwa adhabu ya fedheha kwa mlivyo kuwa mkitakabari katika ardhi bila ya haki, na kwa sababu mlikuwa mkifanya upotovu.”

Kwa hivyo watalipwa kulingana na jinsi ya amali zao. Walipozifurahia nafsi zao na wakafanya kiburi dhidi ya kuifuata haki, wakajishirikisha na dhambi na maasi. Allah تعالى Atawapa adhabu ya kufedhehesha, ambayo ni kudhalilishwa, khizaya, maumivu yenye machungu na majuto yenye kufuatana na vituo katika vina vya moto vyenye kutisha (huko Jahanam). Allah تعالى Atukinge dhidi ya hayo yote.

وَأَذْكُرْ أَحَا عَادٍ إِذْ أَنْذَرَ قَوْمَهُ بِالْأَحْقَابِ وَقَدْ خَلَّتِ الْأَنْدُرُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ إِلَّا
تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٧﴾ قَالُوا أَجِئْنَا لِنَتَأَفَّكُنَا عَنْ
ءَاهِتِنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٨﴾ قَالَ إِنَّمَا أَلْعَلُّمُ عِنْدَ اللَّهِ وَأُبَلِّغُكُمْ
مَا أُرْسِلْتُ بِهِ وَلَيْكِنِّي أَرَأَيْتُمْ قَوْمًا تَجْهَلُونَ ﴿١٩﴾ فَلَمَّا رَأَوْهُ عَارِضًا مُسْتَقْبِلَ أَوْدِيَّتِهِمْ
قَالُوا هَذَا عَارِضٌ مُمْطِرُنَا بَلْ هُوَ مَا اسْتَعْجَلْتُمْ بِهِ رِيحٌ فِيهَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢٠﴾ تَدْمِيرٌ
كُلُّ شَيْءٍ بِأَمْرِ رَبِّهَا فَأَصْبَحُوا لَا يُرَى إِلَّا مَسَكِنُهُمْ كَذَلِكَ نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿٢١﴾

21. *“Na mtaje ndugu wa kina A’di, alipowaonya watu wake kwenye bonde la Ardhi. Na kwa yakini waonyaji wengi walitokea kabla yake na baada yake kuwaambia: Msimuabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi nakukhofieni isikupateni adhabu ya siku iliyo kuu.”*

22. *“Wakasema: Je! Umetujia ili ututenge mbali na miungu yetu? Basi tulettee hayo unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.”*

23. ***“Akasema: Hakika Elimu iko kwa Mwenyezi Mungu. Mimi nakufikishieni niliyotumwa. Lakini nakuoneni kuwa nyinyi mnafanya ujinga.”***

24. ***“Basi walipoliona wingu likielekea kwenye mabonde yao, walisema: Wingu hili la kutunyeshea mvua! Kumbe sivyo, haya ni hayo mliyoyahimiza, upepo ambao ndani yake imo adhabu chungu iumizayo!”***

25. ***“Unaoangamiza kila kitu kwa Amri ya Mola Wake Mlezi. Wakawa hawaonekani tena ila nyumba zao tu. Hivyo ndivyo Tuwalipavyo wakosefu!”***

Kisa cha ‘Ad

Allah تعالی Anamliwaza Mtume Wake kuhusu ukadhibishaji wa baadhi ya watu wake,

وَأَذْكُرُ أَخَا عَادٍ

“Na mtaje ndugu wa kina A’di...”

Huyo ni Hud عليه السلام ambaye Allah تعالی Alimpeleka kwa watu wa ‘Ad na walikuwa wakiishi Al-Ahqaaf. Neno Al-Ahqaaf ni wingi wa *Hiqf* ambao ni mlima wa mchanga. Ameyasema hayo Ibn Zayd.¹ ‘Ikrimah amesema: “Al-Ahqaaf ni mlima na pango.” Qatadah amesema: “Tulifahamishwa kuwa ‘Ad lilikuwa ni kabila mojawapo la Yemen, lililoishi baina ya milima ya mchanga na mkabala na bahari, katika ardhi iliyoitwa Ash-Shihr.”²

Chini ya mlango usemao, “Mwenye kuomba anatakiwa aanze na nafsi yake”, Ibn Majah aliandika kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: Mjumbe wa Allah ﷻ aliomba dua:

يَرْحَمُنَا اللَّهُ وَأَخَا عَادٍ

“Namuomba Allah Aturehemu na ndugu wa kina ‘Ad.”³

Kauli ya Allah تعالی :

¹ At-Tabari 22:125.

² At-Tabari 22:124.

³ Abu Dawud na. 3984, na Ibn Majah 2:1266. Al-Albani ameipa Hadithi hii daraja la dhaifu. Al-Busayri amesema kuwa Hadithi hiyo ni sahihi.

وَقَدْ خَلَّتِ الْأُنْدُرُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ

“Na kwa yakini waonyaji wengi walitokea kabla yake na baada yake...”

Maana yake: Allah تعالى Aliwapeleka Mitume na waonyaji katika miji iliyozunguka maeneo ya Ad. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَجَعَلْنَاهَا نَكَالًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهَا وَمَا خَلْفَهَا

“Kwa hivyo Tukayafanya hayo kuwa onyo kwa wale waliokuwa katika zama zao na waliokuja baada yao...” (2:66) na,

فَإِنْ أَعْرَضُوا فَقُلْ أَنْذَرْتُكُمْ صَاعِقَةً مِثْلَ صَاعِقَةِ عَادٍ وَثَمُودَ ﴿٤١﴾ إِذْ جَاءَهُمُ الرُّسُلُ مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ

“Basi wakipuuza wewe sema: Nakuhadharisheni adhabu mfano wa adhabu ya A’di na Thamudi. Walipowajia Mitume mbele yao na nyuma yao wakawaambia: Msimuabudu ila Mwenyezi Mungu!” (41:13-14)

Kauli ya Allah تعالى:

إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ

“Hakika mimi nakukhofieni isikupateni adhabu ya siku iliyo kuu.”

Maana: Hud عليه السلام aliwaambia hayo. Kaumu yake wakamjibu kwa kusema:

أَجِئْتَنَا لِتَأْفِكَنَا عَنْ آهَتِنَا

“Je! Umetujia ili ututenge mbali na miungu yetu?”

Kwa maana kwamba, ili utuzuie,

عَنْ آهَتِنَا

“...mbali na miungu yetu?”

فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ

“Basi tulettee hayo unayo tuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.”

Waliihimiza adhabu ya Allah تعالى na mateso Yake, kwa kudhani kuwa haitatokea.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا

“Wasioamini huihimiza Saa hiyo ifike upesi...” (42:18)

قَالَ إِنَّمَا أَلْغَلُمُ عِنْدَ اللَّهِ

“Akasema: Hakika ujuzi uko kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Allah تعالى Anakujueni zaidi ikiwa mnastahiki kuharakishiwa adhabu, basi Atakufanyieni hayo. Ama mimi, jukumu langu ni kukufikishieni yale niliyotumwa kwenu,

وَلَيْكِنِّي أَرْزَكُمُ قَوْمًا تَجْهَلُونَ

“Lakini nakuoneni kuwa nyinyi mnafanya ujinga.”

Kwamba, ninyi hamtii akilini wala hamfahamu. Kauli ya Allah تعالى:

فَلَمَّا رَأَوْهُ عَارِضًا مُسْتَقْبِلَ أَوْدِيَّتِهِمْ

“Basi walipoliona wingu likielekea kwenye mabonde yao...”

Maana yake: Walipoona kuwa adhabu iko mbele yao, walidhani kuwa ni mawingu yenye mvua. Wakafurahi na wakapeana bishara, na wakati huo walikuwa na ukame na walihitaji mvua. Allah تعالى Alisema:

بَلْ هُوَ مَا اسْتَعْجَلْتُمْ بِهِ رِيحٌ فِيهَا عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Kumbe sivyo, haya ni hayo mliyoyahimiza, upepo ambao ndani yake imo adhabu chungu!”

Maana yake: Hiyo ndiyo adhabu mliyosema, “Basi tulettee hayo unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.”

تُدْمِرُ كُلَّ شَيْءٍ

“Unaangamiza kila kitu...”

Katika miji yao ambayo kwa kawaida ingeliweza kuharibiwa,

بِأَمْرِ رَبِّهَا

“...*kwa Amri ya Mola Wake Mlezi.*” Maana yake: Kwa Idhini ya Mola Wake Mlezi juu ya hilo. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

مَا تَذُرُّ مِنْ شَيْءٍ أَتَتْ عَلَيْهِ إِلَّا جَعَلْتَهُ كَالرَّمِيمِ ﴿٤٢﴾

“Haukuacha chochote ulichokifikia ila ulikifanya kama kilicho nyambuka.” (51:42)

Maana yake: Kama kitu kilichooza. Kwa minajili hii, Allah تعالى Alisema:

فَأَصْبَحُوا لَا يُرَى إِلَّا مَسَكِنُهُمْ^٤

“Wakawa hawaonekani ila nyumba zao tu.”

Kwamba wote walihilikishwa, na hapana yeyote katika wao aliyesalia,

كَذَلِكَ نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ

“Hivyo ndivyo Tuwalipavyo waovu!”

Kwamba hiyo ndiyo Hukumu Yetu kwa waliowakadhibisha Mitume Wetu na wakakhalifu Amri Yetu.

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى aliandika kuwa ‘Aishah رضي الله عنها alisema: “Sikupata kumuona Mtume ﷺ akiwa mwenye kucheka sana mpaka nikaweza kukiona kidakatonge chake, alikuwa mara nyingi akitabasamu.” Akasema: Mtume ﷺ alipokuwa akiona mawingu au upepo, hutokea mabadiliko usoni mwake. Naye ‘Aishah رضي الله عنها alikuwa akimuambia kuhusu hilo, “Ewe Mjumbe wa Allah! Watu wakiyaona hayo, hufurahi kwa kutarajia mvua, mimi nakuona unapoyaona, huwa unajisikia vibaya.” Mtume ﷺ akasema:

«يَا عَائِشَةُ، مَا يُؤْمِنُنِي أَنْ يَكُونَ فِيهِ عَذَابٌ، قَدْ عَذَّبَ قَوْمَ بِالرَّيْحِ، وَقَدْ رَأَى قَوْمَ الْعَذَابِ وَقَالُوا: هَذَا عَارِضٌ مُمِطِرُنَا»

“Ewe ‘Aishah! Inanitumainisha vipi kuwa hali hiyo haitaleta adhabu. Kuna kaumu iliadhibiwa kwa upepo, hakika walipoiona adhabu hiyo, wakasema, ‘Haya ni mawingu ya kutuletea mvua.”¹

¹ Ahmad 6:66, Fat’h Al-Bari 8:441, na Muslim 2:616.

Bukhari na Muslim wameikusanya.¹ Imamu Ahmad ameandika kwamba 'Aishah رضي الله عنها amesema: "Mtume ﷺ alipokuwa akiona mawingu katika sehemu mojawapo angani, aliacha amali zake, hata kama alikuwa ndani ya Sala, na husema:

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا فِيهِ»

"Ewe Mola! Mimi najikinga Kwako dhidi ya shari iliyomo ndani yake."

Allah تعالى Akiyaondoa mawingu hayo, basi alimhimidi Allah تعالى, na ikinyesha, Mtume ﷺ huomba dua pia,

«اللَّهُمَّ صَيِّبًا نَافِعًا»

"Ewe Mola! Ijaalie inyeshe na iwe na manufaa."

Muslim alinukuu ndani ya Sahih yake, kwamba 'Aishah رضي الله عنها alisema: Wakati upepo ulipokuwa ukivuma, Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَهَا وَخَيْرَ مَا فِيهَا وَخَيْرَ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا، وَشَرِّ مَا فِيهَا، وَشَرِّ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ»

"Ewe Mola! Ninakuomba kheri yake na iliyomo ndani yake, na iliyoletwa nayo. Na ninajikinga Kwako dhidi ya shari yake na iliyomo ndani yake na iliyoletwa nayo."

Akasema kwamba mbingu zilipokuwa zikitanda na mawingu kubadilika, alikuwa akitoka nje na kuingia, kuja na kuondoka na pindi inaponyesha hufurahishwa nayo. 'Aishah رضي الله عنها alipoitambua hali hiyo, akamuuliza, Mtume ﷺ akamjibu:

«لَعَلَّهُ يَا عَائِشَةُ كَمَا قَالَ قَوْمُ عَادٍ: ﴿فَلَمَّا رَأَوْهُ عَارِضًا مُسْتَقْبِلَ أَوْدِيَّتِهِمْ قَالُوا هَذَا عَارِضٌ مُّطْرًا﴾»

"Ewe 'Aishah! Huenda mawingu haya yakawa sawa na walivyosema

¹ Ahmad 6:190.

kaumu 'Ad: "Basi walipoliona wingu likielekea kwenye mabonde yao, walisema: Wingu hili la kutunyeshea mvua!"¹

Tulikwisha kieleza kisa cha kuhiliki kaumu ya 'Ad ndani ya Sura mbili, Al-A'raaf na Huud² kwa kiasi cha kutosha na kuondoa haja ya kukirejea hapa. Na sifa njema ni za Allah تعالی.



¹ Muslim 2:616.

² Angalia juzu ya 4, Tafsir ya Surat Al-Araf (7:66-72) na juzu ya 5, Tafsir ya Surat Hud (11:50-60).

وَلَقَدْ مَكَّنَّهُمْ فِيمَا إِن مَكَّنَّكُمْ فِيهِ
 وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَأَبْصَرًا وَأَفِيدَةً
 فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ سَمْعُهُمْ وَلَا أَبْصَرُهُمْ
 وَلَا أَفِيدَتُهُمْ مِّنْ شَيْءٍ إِذْ كَانُوا
 يَجْحَدُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَحَاقَ بِهِم مَّا
 كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٢٦﴾ وَلَقَدْ
 أَهْلَكْنَا مَا حَوْلَكُمْ مِّنَ الْقُرَىٰ وَصَرَّفْنَا
 الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٧﴾ فَلَوْلَا
 نَصْرُهُمُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِ اللَّهِ
 قُرْبَانًا ؕ إِلَهًا بَلْ ضَلُّوا عَنْهُمْ
 وَذَلِكَ إِفْكُهُمْ وَمَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢٨﴾
 وَإِذْ صَرَّفْنَا
 إِلَيْكَ تَفْرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ
 فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوا أَنصِتُوا
 فَلَمَّا قُضِيَ وَلَّوْا إِلَىٰ قَوْمِهِمْ مُنْذِرِينَ ﴿٢٩﴾
 قَالُوا يَا قَوْمَنَا إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا
 أُنزِلَ مِن بَعْدِ مُوسَىٰ مُصَدِّقًا
 لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَدْعَىٰ إِلَىٰ الْحَقِّ
 وَإِلَىٰ طَرِيقِ مُسْتَقِيمٍ ﴿٣٠﴾ يَنْقُومَنَا
 أَجِيبُوا دَاعِيَ اللَّهِ وَآمِنُوا بِهِ
 يَغْفِرَ لَكُمْ مِّن ذُنُوبِكُمْ وَيُجِرْكُمْ
 مِّن عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٣١﴾ وَمَنْ لَا يُجِيبِ
 دَاعِيَ اللَّهِ فَلَيْسَ بِمُعْجِزٍ فِي الْأَرْضِ
 وَلَيْسَ لَهُ مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءُ
 ؕ أُولَٰئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٣٢﴾ أَوَلَمْ
 يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْزُبْ
 عَنْهُ سِجِّينَ السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ عَلَيَّ قَدِيرٌ ﴿٣٣﴾ عَلَيَّ
 أَن يَنْحِيَ السَّمَواتِ بَلَىٰ إِنَّهُ
 عَلَيَّ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٤﴾ وَيَوْمَ
 يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ
 أَلَيْسَ هَذَا بِالْحَقِّ قَالُوا بَلَىٰ
 وَرَبِّنَا قَالَ فَذُوقُوا الْعَذَابَ
 بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٥﴾ فَاصْبِرْ
 كَمَا صَبَرَ أُولُو الْعَرْشِ مِنَ الرُّسُلِ
 وَلَا تَسْتَعْجِلْ لَهُمْ كَأَنَّهُمْ
 يَوْمَ يَرَوْنَ مَا يُوعَدُونَ لَمْ
 يَلْبُثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّن نَّهَارٍ
 بَلَّغْ فَهَلْ يُهْلَكُ إِلَّا الْقَوْمُ
 الْفَاسِقُونَ ﴿٣٦﴾

وَلَقَدْ مَكَّنَّهُمْ فِيمَا إِن مَكَّنَّكُمْ فِيهِ
 وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَأَبْصَرًا وَأَفِيدَةً
 فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ سَمْعُهُمْ وَلَا أَبْصَرُهُمْ
 وَلَا أَفِيدَتُهُمْ مِّنْ شَيْءٍ إِذْ كَانُوا
 يَجْحَدُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَحَاقَ بِهِم مَّا
 كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٢٦﴾ وَلَقَدْ
 أَهْلَكْنَا مَا حَوْلَكُمْ مِّنَ الْقُرَىٰ وَصَرَّفْنَا
 الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٧﴾ فَلَوْلَا
 نَصْرُهُمُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِ اللَّهِ
 قُرْبَانًا ؕ إِلَهًا بَلْ ضَلُّوا عَنْهُمْ
 وَذَلِكَ إِفْكُهُمْ وَمَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢٨﴾

26. "Na bila ya shaka Tuliwaweka vizuri sio kama Tulivyokuwekeni nyinyi; na Tuliwapa masikio, na macho, na nyoyo. Na hayakuwafaa kitu masikio yao, wala macho yao, wala nyoyo zao kwa lolote. Kwani hao walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na yale waliyokuwa wakiyafanyia mas-khara ndiyo yakawazunguka."

27. “Na hakika Tuliangamiza miji iliyokuwa jirani zenu, na Tulizitumia Ishara ili wapate kurejea.”

28. “Basi mbona wale waliowashika badala ya Mwenyezi Mungu, kuwa ati hao ndio wawakurubishe, hawakuwanusuru? Bali waliwapotea! Na huo ndio uwongo waliokuwa wakiuzua.”

Allah تعالى Anasema, “Umma zilizotangulia duniani, Tuliwapatia mali, watoto na vinginevyo ambavyo Hatukuwapatieni nyinyi kilicholingana au kinachokaribiana navyo.”

وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَأَبْصَرًا وَأَفْئِدَةً فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ سَمْعُهُمْ وَلَا أَبْصَرُهُمْ وَلَا أَفْئِدَتُهُمْ مِنْ شَيْءٍ إِذْ كَانُوا يَجْحَدُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ

“...na Tuliwapa masikio, na macho, na nyoyo. Na hayakuwafaa kitu masikio yao, wala macho yao, wala nyoyo zao kwa lolote. Kwani hao walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na yale waliyokuwa wakiyafanyia maskhara ndiyo yakawazunguka.”

Maana yake: Adhabu na majanga zikawazingira ambazo kwa ujumla wake walikuwa wakizikadhibisha na wakizitilia mashaka juu ya kutukia kwake. Basi tahadharini enyi wasikilizaji msije mkawa mithili yao, na mkapatwa na adhabu zilizowasibu duniani na Akhera. Kauli ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا مَا حَوْلَكُمْ مِنَ الْقُرَىٰ

“Na hakika Tuliangamiza miji iliyokuwa jirani zenu...”

Anamaanisha watu wa Makkah. Allah تعالى Aliuhilikisha umma uliokadhibisha Mitume ambao ulikuwa jirani na mji huo, kama vile ‘Ad ambao walikuwa katika Al-Ahqaaf huko Hadhramawt, karibu na Yemen; na Thamud ambao makazi yao yalikuwa baina ya Makkah na Sham. Kadhalika, Saba-i (Sheba) ambao ni watu wa Yemen; na Madyan walikuwa katika njia yao ya kuelekea Ghazzah (Palestina ya Magharibi); na kaumu ya Lut عليه السلام, ambao waliishi karibu na ziwa (Dead Sea) ambapo walikuwa wakipita (kwenda Jordan) pia. Kauli ya Allah تعالى:

وَصَرَّفْنَا الْآيَاتِ

“...na Tulizitumia Ishara...”

Maana yake: Tulizibainisha na kuzifafanua,

لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٦﴾ فَلَوْلَا نَصَرَهُمُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ قُرْبَانًا ءِالِهَةً

“...ili wapate kurejea. Basi mbona wale waliowashika badala ya Mwenyezi Mungu, kuwa ati hao ndio wawakurubishe hawakuwanusu?...”

Kwamba, je waliwasaidia wakati walipokuwa wakiwahitaji?

بَلْ ضَلُّوا عَنْهُمْ

“Bali waliwapotea!” Bali waliwaacha peke yao kabisa, pindi walipokuwa na haja nao zaidi,

وَذَلِكَ إِفْكُهُمْ

“Na huo ndio uwongo wao...” Maana yake: Uzushi na tuhuma zao,

وَمَا كَانُوا يَفْقَهُونَ

“...waliokuwa wakiuzua.” Maana yake: Walizusha uongo kwa kuwafanya wao miungu, na wakapotea na kupata hasara kwa kuwaabudu na kuwatumaini. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوا أَنصِتُوا فَلَمَّا قُضِيَ وَلَّوْا إِلَىٰ قَوْمِهِمْ مُنْذِرِينَ ﴿٢٧﴾ قَالُوا يَنْقُومَنَا إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا أُنزِلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَىٰ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ وَإِلَىٰ طَرِيقٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٢٨﴾ يَنْقُومَنَا أَجِيبُوا دَاعِيَ اللَّهِ وَءَامِنُوا بِهِ يَغْفِرَ لَكُمْ مِّن ذُنُوبِكُمْ وَيُجِرْكُمْ مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٢٩﴾ وَمَنْ لَا يُجِبْ دَاعِيَ اللَّهِ فَلَيْسَ بِمُعْجِزٍ فِي الْأَرْضِ وَلَيْسَ لَهُ مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءُ ؕ أُولَٰئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٣٠﴾

29. “Na wakati Tulipowaleta kundi la majini kuja kwako kusikiliza Qur’ani. Basi walipoihudhuria walisema: Sikilizeni! Na ilipokwisha somwa, walirudi kwa kaumu yao kwenda kuwaonya.”

30. “Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi Tumesikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa, kinacho sadikisha yaliyokuwa

kabla yake, na kinachoongoza kwenye Haki na kwenye Njia Iliyonyooka.”

31. “Enyi kaumu yetu! Muitikieni Mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu, na muaminini, Mwenyezi Mungu Atakusameheni, na Atakulingeni na adhabu chungu iumizayo.”

32. “Na wasiomuitikia Muitaji wa Mwenyezi Mungu basi hao hawatashinda katika ardhi, wala hawatakuwa na walinzi mbele yake. Hao wamo katika upotovu uliodhaahiri.”

Kisa cha Majini Kusikiliza Qur’an

Imam Ahmad aliasimulia kutoka kwa Az-Zubayr رضي الله عنه kuwa alitoa rai kuhusu Aya:

وَأَذِّبْ صَرْفَتَنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ

“Na wakati Tulipowaleta kundi la majini kuja kwako kusikiliza Qur’ani.”

“Walikuwa katika sehemu iliyokuwa ikiitwa Nakhlah¹, wakati Mtume ﷺ alipokuwa akisali Sala ya Isha, na,

كَأَدْوَا يُكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا

“...walikuwa karibu kumzonga!” (72:19)

Sufyaan alisema: “Wengine walisimama juu ya wenzao kama manyoya.”² Ahmad amenukuu haya peke yake. Imamu Ahmad na Imamu mashuhuri, Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bayhaqi رحمه الله تعالى ndani ya kitabu chake, *Dalaailun-Nubuwwah* waliandika kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema: “Mtume wa Allah ﷺ hakuwasomea majini wala hakuwaona. Mjumbe wa Allah ﷻ alikwenda Twaif akiwa pamoja na kikundi cha Masahaba wake kuelekea katika soko la ‘Ukaadh. Wakati huohuo, mashetani wakarejea wamezuiliwa kupata habari za mbinguni na wakashambuliwa na miale ya moto iunguzayo. Mashetani wakarejea kwa kaumu zao. Wakawauliza: “Mumepatwa na nini?” Wakajibu: “Tumezuiliwa dhidi ya kuvizia habari za mbinguni, na tumeletewa

¹ Nakhlah ni jina la bonde lililo baina ya Makkah na At-Taif.

² Ahmad 1:167.

myenge iunguzayo." Wakawaambia: "Mlichoziuliwa ni uvizaji wa habari za mbinguni kwa sababu ya tukio kubwa (lililotukia). Basi piteni duniani kote, mashariki na magharibi ili muone kilichokuzuilieni dhidi ya kuzivizia habari za mbinguni. Wakasafiri duniani kote, mpaka mashariki na magharibi kwa ajili ya kutafuta kilichowazuilia kuvizia habari za mbinguni. Kikundi chao kimojawapo kilielekea Tihamah¹ na wakamkuta Mtume ﷺ akiwa mahali palipoitwa *Nakhlah*, akiwa njiani kwenda katika soko la 'Ukaadh, akiwa anawaongoza Masahaba wake katika Sala ya *As-Subh*. Walipoisikia Qur'an ikisomwa, waliisikiliza, kisha wakasema, "Wallah! Hiki ndicho kilichokuzieni kuzisikiliza habari za mbinguni." Waliporejea kwa kaumu yao, walisema, "Enyi kaumu yetu! Sisi tumekisikia kisomo cha kustaajabisha (Qur'an), kinaongoza kwenye uongofu, nasi tukakiamini, wala hatutamshirikisha Allah تعالى na kitu chochote." Allah تعالى Akamshushia Nabii Wake:

قُلْ أَوْحَىٰ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِّنَ الْجِنِّ

"Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza..." (72:1)

Hivyo, kilichofunuliwa kwake kilihusu mazungumzo waliyoyafanya majini.² Al-Bukhari alipokea mfano wa hayo, na Muslim na imenukuliwa na At-Tirmidhi na An-Nasai katika Tafsir.³ 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema: "Majini yalikuja kwa Mtume ﷺ akiwa anasoma Qur'an mahali paitwapo *Nakhlah*. Baada ya kumsikia,

قَالُوا أَنْصِتُوا

"...walisema: Sikilizeni!"

Kwamba, nyamazeni! Walikuwa tisa, mmoja wao alikuwa akiitwa Zawba'ah. Allah تعالى Akashusha:

وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوا أَنْصِتُوا فَلَمَّا

قُضِيَ وَلَوْا إِلَىٰ قَوْمِهِمْ مُنْذِرِينَ ﴿٧٢﴾

¹ Kijiji kilicho umbali wa kadiri ya maili mbili magharibi mwa Al-Madinah.

² Ahmad 1:252 na *Dalail An-Nubuwwah* 2:252.

³ Al-Bukhari na. 771, 9921, Muslim 1:331, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9: 168 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:499.

“Na wakati Tulipowaleta kundi la majini kuja kwako kusikiliza Qur’ani. Basi walipoihudhuria walisema: Sikilizeni! Na ilipokwishasomwa, walirudi kwa kaumu yao kwenda kuwaonya.” Mpaka,

فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ

“...upotovu uliodhaahiri.”¹

Masimulizi haya na yaliyotangulia yanatokana na Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما yanaonesha kuwa Mtume ﷺ hakutambua kuhudhuria kwao katika mara ya kwanza. Wao walikisikiliza kisomo chake kisha wakarejea kwa kaumu yao. Baadaye, waliwatuma wajumbe kwake ambao walikuja kikundi baada ya kikundi. Kauli ya Allah تعالى:

وَلَوْ إِلَى قَوْمِهِمْ مُنْذِرِينَ

“...walirudi kwa kaumu yao kwenda kuwaonya.”

Kwamba walirejea kwa kaumu yao na wakawaonya kuhusu walichokisikia kutoka kwa Mtume ﷺ. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لِيَتَفَقَّهُوْا فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ

“...wakajifunze vyema Dini, na kisha waje kuwaonya wenzao watakapowarejea, ili wapate kujihadharisha?” (9:122)

Kuna walioitumia Aya hii kama ushahidi kwa kusema kuwa majini wana maonyo tu, hawana Mitume. Hapana shaka kuwa Allah تعالى Hakutuma miongoni mwa majini Mitume, ni kutokana na Kauli Yake:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُوْحِي إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ

“Na Hatukuwatuma Mitume kabla yako isipokuwa watu wanaume Tuliowafunulia wahyi miongoni mwa wakazi wa mijini.” (12:109)

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لِيَأْكُلُوا الطَّعَامَ وَيَشْرَبُونَ فِي الْآسْوَاقِ

“Na Hatukuwatuma kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakienda masokoni.” (25:20)

¹ Al-Hakim 2:456.

Pia, Allah تعالى Anaeleza kuhusu Ibrahim, Al-Khalil عليه السلام :

وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

“Na Tukajaalia katika dhuria wake Unabii na Kitabu...” (29:27)

Kwa hivyo, kila Nabii aliyetumwa na Allah تعالى baada ya Ibrahim عليه السلام alitokana na watoto na uzao wake. Ama kuhusu Kauli ya Allah تعالى ndani ya Surat Al-An'aam:

يَمْعَشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ

“Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakukujieni Mitume kutokana na nyinyi wenyewe...” (6:130)

Makusudio ni kwa namna zote mbili kwa pamoja, bali hususan inafungamana na kimojawapo, ambacho ni watu. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

تَخْرُجُ مِنْهَا اللَّوْلُؤُ وَالْمَرْجَانُ

“Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani.” (55:22)¹

Maana yake kimojawapo. Kisha, Allah تعالى Akatoa maana ya majini kuwatahadharisha kaumu yao, Alisema:

قَالُوا يَنْقُومَنَا إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا أُنزِلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَىٰ

“Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi tumesikia Kitabu kilichotemshwa baada ya Musa...”

Hawakumtaja 'Isa عليه السلام kwa sababu injili aliyoshushiwa ina maonyo na mahimizo machache katika masuala ya halali na haramu. Kwa hakika, ilikuwa inatimiliza sharia ya Taurat. Kwa minajili hii, walisema:

أُنزِلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَىٰ

“...kilicho teremshwa baada ya Musa...”

Hivi ndivyo pia alivyosema Waraqah bin Nawfal, pindi Mtume ﷺ alipompa habari ya kushuka Malaika Jibril عليه السلام katika mara ya kwanza. Alisema, “Bakh, Bakh (vizuri sana, vizuri sana)! Huyu ni An-Namus ambaye alikuwa akimuendea Musa عليه السلام, natamani ningelikuwa kijana bado (ili nikusaidie).”²

¹ Angalia maelezo ya aya hiyo.

² Angalia *Fat'h Al-Bari* 1:30, lakini bila ya neno “Bakh, Bakh” (vyema, vyema).

مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ

“...kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake...” Maana yake: Katika Vitabu vilivyoshushwa kabla yake,

يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ

“...na kinachoongoza kwenye Haki...” Inamaanisha, imani na habari,

وَأِلَى طَرِيقِ مُسْتَقِيمٍ

“...na kwenye Njia Iliyo Nyooka.”

Katika amali, kwani Qur’an inajumuisha mambo ya namna mbili, habari na amri. Habari zake ni za kweli na amri zake ni za uadilifu. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

“Na yametimia Maneno ya Mola Mlezi Wako kwa kweli na uadilifu.” (6:115)

Allah تعالى Alisema pia,

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ

“Yeye Ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa uwongofu na Dini ya Haki...” (9:33)

Maana yake, Uongofu ni elimu yenye manufaa, na dini ya haki ni amali njema. Hivi ndivyo majini walivyosema,

يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ

“...kinachoongoza kwenye Haki...” Katika mambo ya imani,

وَأِلَى طَرِيقِ مُسْتَقِيمٍ

“...na kwenye Njia Iliyonyooka.” Katika mambo ya amali.

يَنْقُومَنَا أَجِيبُوا دَاعِيَ اللَّهِ

“Enyi kaumu yetu! Muitikieni Mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu...”

Huu ni uthibitisho kuwa Allah تعالى Alimtuma Muhammad ﷺ kwa viumbe mbea mbili, majini na wanaadamu. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema:

أَجِيبُوا دَاعِيَ اللَّهِ وَآمِنُوا بِهِ

“Muitikieni Mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu, na muaminini...”

Kauli ya Allah تعالى: يَغْفِرْ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبِكُمْ

“Mwenyezi Mungu Atakusameheni madhambi yenu...”

Katika nadharia ya kanuni ya lugha ya kiarabu Neno “Min,” husemwa limezidi, lakini nadharia hiyo ina mapungufu kwani kuzidi kwake ni mara chache sana kutumiwa katika kuthibitisha. Husemwa: katika nadharia nyingine “Min” maana yake ni kuonesha kuwa ni baadhi tu ya kitu (si chote),

وَيُجْرَتُمْ مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ

“...na Atakulingeni na adhabu chungu.”

Kwamba Atakuhifadhini dhidi ya adhabu iumizayo. Kisha, Allah تعالى Alieleza habari zao,

وَمَنْ لَا يُجِبْ دَاعِيَ اللَّهِ فَلَيْسَ بِمُعْجِزٍ فِي الْأَرْضِ

“Na wasiomuitikia Muitaji wa Mwenyezi Mungu basi hao hawatashinda katika ardhi...”

Yaani, bali Kudura ya Allah تعالى inamjumuisha na inamzingira,

وَلَيْسَ لَهُ مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءُ

“...wala hawatakuwa na walinzi mbele yake.”

Kwamba, hapana wa kumlinda dhidi ya Allah تعالى:

أُولَئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ

“Hao wamo katika upotovu uliodhaahiri.”

Hii ni karipio kali na onyo, waliwalingania kaumu yao kwa njia ya kuwatia moyo na kuwaonya. Kwa ajili hii, majini wengi walinufaika, wakaja kwa Mtume ﷺ vikundi vikundi.

Allah تعالى Ndiye Anayestahiki Sifa njema, Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْزِمْنِي بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ مَحْيَىٰ
 الْمَوْتَىٰ بَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٦﴾ وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ أَلَيْسَ
 هَذَا بِالْحَقِّ قَالُوا بَلَىٰ وَرَبِّنَا قَالَ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٢٧﴾ فَاصْبِرْ كَمَا
 صَبَرَ أُولُو الْعَزْمِ مِنَ الرُّسُلِ وَلَا تَسْتَعْجِلْ لَهُمْ كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَ مَا يُوعَدُونَ لَمْ يَلْبَثُوا
 إِلَّا سَاعَةً مِّن نَّهَارٍ بَلَّغٌ فَبَلَّغْ فَهَلْ يَهْلِكُ إِلَّا الْقَوْمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٢٨﴾

33. *“Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, Aliye ziumba mbingu na ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba, kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.”*

34. *“Na siku watakapoletwa makafiri Motoni wakaambiwa: Je! Haya si kweli? Watasema: Kwanini? Tunaapa kwa Mola Wetu Mlezi, ni kweli! Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya kule kukataa kwenu.”*

35. *“Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume waliovumilia kukubwa, wala usiwafanyie haraka. Siku watakayoyaona waliyoahidiwa itakuwa kama kwamba hawakukaa ulimwenguni ila saa moja ya mchana. Huu ndio ufikisho! Kwani hawaangamizwi isipokuwa walio waovu tu?”*

Dalili ya Kuwepo Maisha baada ya Mauti

Allah تعالى Anasema, wale wanaokanusha juu ya kufufuliwa katika Siku ya Kiyama na wanalifanya mbali jambo la kurejea, hawaoni,

أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْزِمْنِي بِقَدِيرٍ

“...kwamba Mwenyezi Mungu, Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba...”

Maana yake, wala Kuviumba hivyo Hakukumchosha, bali Aliviambia, “Kuweni, na vikawa pasi na kizuizi wala kukhalifu. Bali vilitii, viliitika kwa unyenyekevu na hofu. Je, Huyo Hawezi Kuwahuisha wafu?.

Ni sawa na Kauli Yake katika Aya nyingine,

لَخَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَئِنْ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

“Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.” (40:57)

Kwa minajili hii, Allah تعالى Amesema:

بَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Kwanini? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.”

Halafu, Allah تعالى Ametoa vitisho na Kuwaonya wenye kumkufuru:

وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ أَلَيْسَ هَذَا بِالْحَقِّ ۗ

“Na siku watakapoletwa makafiri Motoni wakaambiwa: Je! Haya si kweli?”

Maana yake: “Si ya kweli haya? Hii ni sihiri ama hamuoni?”

قَالُوا بَلَىٰ وَرَبِّنَا

“Watasema: Kwanini? Tunaapa kwa Mola Wetu Mlezi, ni kweli!”

Hawatakuwa na khiyari, isipokuwa kusema:

قَالَ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ

“Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya kule kukataa kwenu.”

Amri kwa Mtume ﷺ Awe na Subira

Halafu, Allah تعالى Alimuamuru Mtume Wake awe na subira juu ya waliomkadhibisha miongoni mwa watu wa kaumu yake,

فَأَصْبِرْ كَمَا صَبَرْنَا وَأُولُوا الْعَزْمِ مِنَ الرُّسُلِ

“Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume waliovumilia Kukubwa...”

Maana yake: Juu ya umma wao kuwakadhibisha wao. Mitume wenye uvumilivu mkubwa (*Ulul-'Azm*) ni Nuh عليه السلام, Ibrahim عليه السلام, Musa عليه السلام, 'Isa عليه السلام na mwisho wa Manabii wote, Muhammad ﷺ. Allah تعالى Ameyataja majina yao ndani ya Aya mbili katika Sura mbili, Al-Ahzaab (33:7) na Ash-Shura (42:13).

وَلَا تَسْتَعْجِلْ لَهُمْ

"...wala usiwafanyie haraka."

Maana yake: Usiwaharakishie kushuka adhabu. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَذَرْنِي وَالْكَذِبِينَ أَُولِيَ النَّعْمَةِ وَمَهَلْهُمْ قَلِيلًا ﴿٧٣﴾

"Na niache Mimi na hao wanaokanusha, walioneemeka; na wape muhula kidogo!" (73:11) na,

فَمَهَلِ الْكَافِرِينَ أَهْمَلَهُمْ زُؤِيدًا ﴿٨٦﴾

"Basi wape muhula makafiri - wape muhula polepole." (86:17)

Kauli ya Allah تعالى:

كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَ مَا يُوعَدُونَ لَمْ يَلْبُثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّنْ نَّهَارٍ

"Siku watakayoyaona waliyoahidiwa itakuwa kama kwamba hawakukaa ulimwenguni ila saa moja ya mchana."

Inalingana na Kauli Yake nyingine,

كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبُثُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحَاهَا ﴿٧٩﴾

"Ni kama kwamba wao siku watapokiona Qiyama hawakukaa ila jioni moja tu, au mchana wake." (79:46) na,

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ كَأَن لَّمْ يَلْبُثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّنَ النَّهَارِ يَتَعَارَفُونَ بَيْنَهُمْ

"Na Siku Atakapowakusanya, itakuwa kama kwamba hawakukaa ila saa moja tu ya mchana! Watatambuana." (10:45)

Kauli ya Allah تعالى:

بَلِّغْ

“Huu ndio ufikisho!”

Inamaanisha kuwa Qur’an hii ndiyo ufikisho. Kauli ya Allah تعالى:

فَهَلْ يُهْلِكُ إِلَّا الْقَوْمَ الْفَاسِقُونَ

“Kwani hawaangamizwi isipokuwa walio waovu tu?”

Kwamba, Allah تعالى Hamhilikishi yeyote, isipokuwa aliyejichagulia hivyo. Hii ni sehemu ya Uadilifu Wake, kwamba Hamuadhibu yeyote, isipokuwa mwenye kustahiki. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Mwisho wa tafsiri ya *Surat Al-Ahqaaf*, Himdi na Shukurani ni za Allah تعالى, Kwake Ndiko kwenye taufiki na hifadhi.

* * *

Tafsiri ya Suratu Muhammad

Suratul Qitaal¹

Sura ya 47

Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ أَضَلَّ أَعْمَلُهُمْ ﴿١﴾
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَءَامَنُوا بِمَا نُزِّلَ عَلَى
 مُحَمَّدٍ وَهُوَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ كَفَّرَ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَأَصْلَحَ بَالَهُمْ
 ﴿٢﴾ ذَلِكَ بِأَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا اتَّبَعُوا الْبَاطِلَ وَأَنَّ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا اتَّبَعُوا الْحَقَّ مِنْ رَبِّهِمْ ۚ كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ لِلنَّاسِ
 أَمْثَلَهُمْ ﴿٣﴾ فَإِذَا لَقِيتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبِ الرِّقَابِ
 حَتَّىٰ إِذَا أَخْنَثْتُمْهُمْ فَشُدُّوا آلَوتِقًا فَإِذَا مَتَّ بَعْدُ وَإِنَّمَا
 فِدَاءٌ حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا ۚ ذَلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ
 لَآتَتْكُمْ مِنْهُمُ الْوَالِدَاتُ وَالَّذِينَ قَتَلُوا
 فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَنْ يُضِلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٤﴾ سَيِّئَاتِهِمْ وَيُضِلَّهُمْ
 بِأَهْلِهِمْ ﴿٥﴾ وَيُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ ﴿٦﴾ يَتَأَيَّمُوا الَّذِينَ
 ءَامَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُؤْتِنِمْ أَقْدَامَكُمْ ﴿٧﴾
 وَالَّذِينَ كَفَرُوا فَتَعَسَا لَهُمْ وَأَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٨﴾ ذَلِكَ
 بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ ﴿٩﴾

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi
 wa Rehema Mwenye
 Kurehemu

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ
 أَضَلَّ أَعْمَلَهُمْ ﴿١﴾ وَالَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَءَامَنُوا
 بِمَا نُزِّلَ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ وَهُوَ الْحَقُّ مِنْ
 رَبِّهِمْ كَفَّرَ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَأَصْلَحَ
 بَالَهُمْ ﴿٢﴾ ذَلِكَ بِأَنَّ الَّذِينَ
 كَفَرُوا اتَّبَعُوا الْبَاطِلَ وَأَنَّ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا اتَّبَعُوا الْحَقَّ مِنْ رَبِّهِمْ ۚ كَذَلِكَ
 يَضْرِبُ اللَّهُ لِلنَّاسِ أَمْثَلَهُمْ ﴿٣﴾

1. "Waliokufuru wakajizua na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, Yeye Atavipondoa vitendo vyao."

2. "Na walioamini, na wakatenda mema, na wakaamini aliyoteremshiwa

¹ Sura hii kwa umaarufu inaitwa Surah Muhammad.

Muhammad - nayo ni Haki iliyotoka kwa Mola Wao Mlezi - Atawafutia makosa yao na Ataitengeneza hali yao."

3. "Hayo ni kwa sababu waliokufuru wamefuata upotovu, na walioamini wamefuata Haki iliyotoka kwa Mola Wao Mlezi. Hivyo Ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyowapigia watu mifano yao."

Malipo ya Makafiri na Waumini

Allah تعالیٰ Anasema:

الَّذِينَ كَفَرُوا

"Waliokufuru..."

Aya za Allah تعالیٰ:

وَصَدُّوا

"...na wakazuilia..."

Maana yake: Watu wengine,

عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ أَضَلَّ أَعْمَلَهُمْ

"...njia ya Mwenyezi Mungu, Yeye Atavipotoa vitendo vyao."

Maana yake: Atavibadilisha na Kuvifuta, na wala hatavihesabu kuwa ni thawabu na malipo:

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنْ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَنْثُورًا ﴿٢٣﴾

"Na Tutayaendea yale waliyoyatenda katika vitendo vyao, Tuvifanye kama mavumbi yaliyotawanyika." (25:23)

Kisha, Allah تعالیٰ Amesema:

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

"Na walioamini, na wakatenda mema..."

Maana yake: Nyoyo na dhamiri zao ziliamini, viungo vyao na miili yao, siri na dhahiri ikafuata Shariah ya Allah تعالیٰ,

وَأَمْتُوا بِمَا نَزَّلَ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ

“...na wakaamini aliyoteremshiwa Muhammad...”

Hii ni nadharia ya kanuni ya kilugha ambayo inaruhusu kuunganisha jambo mahususi katika jambo la jumla, huu ni uthibitisho kwamba hilo ni sharti la kusihi imani, baada ya kutumwa Muhammad ﷺ.

Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّهِمْ

“...nayo ni Haki iliyotoka kwa Mola Wao Mlezi...”

Ni nzuri iliyoingia katikati ya maneno. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

كَفَرْنَا عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَأَصْلَحَ بَالَهُمْ

“...Atawafutia makosa yao na Ataitengeneza hali yao.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, Maana yake, “Aliwaamuru.” Mujahid alisema: “Jambo lao.” Qatadah na Ibn ‘Zaydi walisema: “Hali yao.” Maneno yote hayo yamekaribiana. Maana yake imekuja katika Hadithi ya kumrehemu mwenye kupiga chafya:

«يَهْدِيكُمْ اللَّهُ وَيُصْلِحُ بِالْكُفْرِ»

“Allah Akuongozeni na Ayatengeneze mambo yenu.”¹

Kisha, Allah تعالى Akasema:

ذَٰلِكَ بِأَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا اتَّبَعُوا الْبَاطِلَ

“Hayo ni kwa sababu waliokufuru wamefuata upotovu...”

Maana yake: Tumezibatilisha amali za makafiri, na Tumesamehe maovu ya wachamungu. Tukatengeneza mambo yao, kwa sababu makafiri walifuata upotofu, yaani walikhitari ubatilifu dhidi ya ukweli,

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:11.

وَأَنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّبَعُوا الْحَقَّ مِن رَّبِّهِمْ ۚ كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ لِلنَّاسِ أَمْثَلَهُمْ ﴿٤٧﴾

*“...na walioamini wame fuata Haki iliyotoka kwa Mola Wao Mlezi.
Hivyo Ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyowapigia watu mifano yao.”*

Maana yake: Anawabainishia mwisho wa amali zao na mahali watakapoishia katika kurejea kwao. Allah تعالى ni Mjuzi.

فَإِذَا لَقِيتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَخْتُمْتُمُوهُمْ فَشُدُّوا الْوَتَاقَ فَإِمَّا مَنًّا بَعْدَ
وَأِمَّا قِتْلًا حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا ۚ ذَٰلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَانتَصَرْنَا مِنْهُمْ وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَ
بَعْضَكُمْ بِبَعْضٍ ۗ وَالَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَن يُضِلَّ أَعْمَلَهُمْ ﴿٤٨﴾ سَيَجْزِيهِمْ وَيُصَلِّحُ
بِهِمْ ۗ ﴿٤٩﴾ وَيُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ ﴿٥٠﴾ يَتَأَيُّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَنَّصَرُوا أَنَّ اللَّهَ يَنْصُرْكُمْ
وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ ﴿٥١﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا فَتَعَسَا لَهُمُ الْوُجُوهُ ۗ وَأَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٥٢﴾ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ
كَرَهُوا مَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ ﴿٥٣﴾

4. Basi mnapokutana (vitani) na wale waliokufuru wakateni shingo zao, mkiwadhoofisha na kuwashinda wafungeni pingu (muwachukue kwenu mateka). Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vitue mizigo yake (vipoe). Ndio hivyo. Na lau angelitaka Mwenyezi Mungu Angeliwashinda Mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu Akutieni mitihani nyinyi kwa nyinyi. Na waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu hayatapotea matendo yao.”

5. “Atawaongoza na Awatengezee hali yao.”

6. “Na Atawaingiza katika Pepo Aliyowajulisha.”

7. “Enyi mliaoamini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu Naye Atakunusuruni na Ataithibitisha miguu yenu.”

8. “Na waliokufuru, basi kwao ni maangamizo, na Atavipoteza vitendo vyao.”

9. “Hayo ni kwa sababu waliyachukia Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi Akaviangusha vitendo vyao.”

Amri ya Kupigana na Maadui, na Kuwashika Mateka, Kisha Kuwaachia huru ima kwa Hisani au Fidia.

Allah تعالى Anawaelekeza Waumini kuhusu kitu cha kukitumia katika vita vyao dhidi ya washirikina,

فَإِذَا لَقِيتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ

“Basi mnapokutana (vitani) na wale waliokufuru wakateni shingo zao...”

Maana yake: Mtakapowakuta muwavune kwa mapanga,

حَتَّىٰ إِذَا أَخْنَثْتُمْهُمْ

“...mkiwadhoofisha na kuwashinda...”

Maana yake: Mmewahiliki kabisa kwa kuwaua,

فَشُدُّوا أَلْوَتَاقَ

“...wafungeni pingu.”

Mateka mnaowateka, kisha nyinyi, baada ya kumalizika vita, mnapewa hiyari katika jambo lao, mkitaka wafanyieni huruma na muwaachilie huru, bure, na mkitaka watozeni fidia ya mali ambayo mtaichukua kutoka kwao na kuwapa masharti. Jambo la kuzingatiwa hapa, ni kwamba aya hii ilishuka baada ya vita vya Badri. Allah تعالى Aliwalaumu waumini siku hiyo kwa kushikilia mateka wengi ili kuchukua fidia kutoka kwao.

مَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَنْ يَكُونَ لَهُ أَسْرَىٰ حَتَّىٰ يُثْخِرَ فِي الْأَرْضِ ۚ تُرِيدُونَ عَرَضَ الدُّنْيَا
وَاللَّهُ يُرِيدُ الْآخِرَةَ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧٧﴾ لَوْلَا كِتَابٌ مِّنَ اللَّهِ سَبَقَ لَمَسَّكُمْ فِيمَا
أَخَذْتُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٧٨﴾

“Haimfalii Nabii yeyote kuwa na mateka mpaka awe ameshinda baraabara katika nchi. Mnataka vitu vya dunia, na Mwenyezi Mungu Anataka Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima. Lau isingelikuwa hukumu iliyokwisha tangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu ingelikupateni adhabu kubwa kwa vile mlivyochukua.” (8:67-68)

Kauli ya Allah تعالى:

حَتَّى تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا

"...mpaka vita vipoe."

Mujahid alisema: "Mpaka 'Isa bin Maryam عليه السلام ateremke."¹ Yeye ni kama kwamba ameyachukua kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

«لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي ظَاهِرِينَ عَلَى الْحَقِّ حَتَّى يُقَاتِلَ آخِرُهُمُ الدَّجَالَ»

*"Halitaacha kuwepo kundi katika umma wangu ambalo litashinda juu ya haki, mpaka wa mwisho wao apigane na Dajjal."*²

Imamu Ahmad alimnukuu Jubayr bin Nafiyr kwamba Salamah bin Nufayl alimjia Mtume ﷺ, na kusema: "Mimi nimemuachilia farasi aende, nikaitupa chini silaha, kwa kuwa vita vimekwisha." Nami nikasema: "Hakuna vita tena." Mtume ﷺ akamuambia:

«الآنَ جَاءَ الْقِتَالُ، لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي ظَاهِرِينَ عَلَى النَّاسِ، يُرِيدُ اللَّهُ تَعَالَى قُلُوبَ أَقْوَامٍ، فَيُقَاتِلُونَهُمْ وَيَرْزُقُهُمُ اللَّهُ مِنْهُمْ حَتَّى يَأْتِيَ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ عَلَى ذَلِكَ، أَلَا إِنَّ عَفْرَةَ دَارِ الْمُؤْمِنِينَ الشَّامُ، وَالْحَيْلُ مَعْفُودَةٌ فِي نَوَاصِيهَا الْخَيْرُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

*"Hivi sasa, mapigano yamekuja, halitaacha kundi katika umma wangu kuwashinda watu. Allah Atazigeuza nyoyo za (baadhi ya) watu, watapigana nao, na Allah Atawaruzuku miongoni mwao, mpaka ije Amri ya Allah, ilhali wako katika hilo. Hakika, kituo cha makazi ya Waumini ni Shaam, na farasi aliyefungwa, katika utosi wake kuna kheri mpaka Siku ya Kiyama."*³

Kama hivi amepokea An-Nasai.⁴

¹ At-Tabari 22:157.

² Abu Dawud 3:11.

³ Ahmad 4:104.

⁴ An-Nasai 6:215, na katika *Al-Kubra* 5:218.

Kauli ya Allah تعالى:

ذَٰلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَانتَصَرَ مِنْهُمْ

“Ndio hivyo. Na lau Angelitaka Mwenyezi Mungu Angeliwashinda Mwenyewe...”

Maana yake: Allah تعالى Angelitaka Angeliwalipizia kisasi dhidi ya makafiri kwa adhabu na maafa kutoka Kwake,

وَلٰكِنْ لِّيَبْلُوٓا۟ بَعْضَڪُمْ بِبَعْضٍ

“...lakini haya ni kwa sababu Akutienu mitihani nyinyi kwa nyinyi.”

Lakini Amekuwekeeni Shariah ya Jihadi na kupigana na maadui, ili Akujaribuni na kupatikana habari zenu, kama Alivyotaja hikima Yake katika kuileta Shariah ya Jihadi katika Sura mbili, Aali 'Imraan na Baraa-ah (At-Tawbah).

Katika Kauli ya Allah تعالى:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٢﴾

“Je! Mnadhani mtaingia Peponi na hali Mwenyezi Mungu Hajawapambanua wale miongoni mwenu waliopigana Jihadi, na Hajawapambanua waliosubiri?” (3:142)

Allah تعالى Amesema katika Surat Baraa-ah:

فَتِلْوَهُمْ يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَتُخْزِيهِمْ وَيَنْصُرُكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِي صُدُورَ قَوْمٍ مُّؤْمِنِينَ ﴿١٤١﴾
وَيُدْهَبُ غِيْظَ قُلُوْبِهِمْ وَيَتُوبُ اللَّهُ عَلٰى مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٤٢﴾

“Piganeni nao, Mwenyezi Mungu Awaadhibu kwa mikono yenu, na Awafedheheshe wao na Akunusuruni muwashinde, na Avipoze vifua vya kaumu ya Waumini. Na Aondoe hasira ya nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu Humkubalia toba ya Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hikima.” (9:14-15)

Fadhila za Mashahidi

Kwa kuwa ni katika shani ya vita, kuuawa Waumini wengi, Allah تعالى Amesema:

وَالَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَنْ يُضِلَّ أَعْمَالَهُمْ

“Na waliuliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu Hatazipoteza amali zao.”

Maana yake: Hataziacha amali zao nzuri zipotee, bali Atazikithirisha, Kuzizalisha na Kuziongeza. Miongoni mwao, wapo wanaolipwa kwa muda wao wote wa kuishi katika kaburi *Al-Barzakh*.¹

Ni sawa na ilivyoeleza hivyo Hadithi iliyosimuliwa na Imamu Ahmad katika Musnad yake kutoka kwa Kathir bin Murrah, naye, kutoka kwa Qays bin Al-Judhaami – mtu ambaye alikuwa na usahibu naye alisema, Mtume ﷺ alisema:

«يُعْطَى الشَّهِيدُ سِتَّ خِصَالٍ عِنْدَ أَوَّلِ قَطْرَةٍ مِنْ دَمِهِ: تُكَفَّرُ عَنْهُ كُلُّ خَطِيئَةٍ، وَيَرَى مَقْعَدَهُ مِنَ الْجَنَّةِ، وَيُرَوِّجُ مِنَ الْحُورِ الْعِينِ، وَيَأْمُنُ مِنَ الْفَزَعِ الْأَكْبَرِ، وَيَمُنَّ عَذَابِ الْقَبْرِ، وَيُحَلِّي حُلَّةَ الْإِيمَانِ»

“Shahidi atapewa mambo sita: Katika tone la kwanza la damu yake, hufutiwa kila tone moja kosa lake, anaona makazi yake Peponi, ataozwa mahurul a’ini, atasalimika na mfazaiko mkubwa, na atasalimika dhidi ya adhabu ya kaburi, na atapambwa pambo la Imani.”

Ahmad peke yake aliinukuu Hadithi hii.²

Abu Ad-Dardai رضي الله عنه Amesema, Mtume ﷺ Amesema:

«يُسْمَعُ الشَّهِيدُ فِي سَبْعِينَ مِنْ أَهْلِ بَيْتِهِ»

“Shahidi atawaombea watu sabini katika jamaa zake.”

Ilinukuliwa na Abu Dawud.³

¹ Hali ya mpito baina ya maisha ya duniani na Akhera.

² Ahmad 4:104.

³ Abu Dawud na. 2522.

Na Hadithi zinazoeleza fadhila za mashahidi ni nyingi. Kauli ya Allah تعالى:

سَيَلِيمٌ

“Atawaongoza...”

Kwenda Peponi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ يَهْدِيهِمْ رَبُّهُمْ بِإِيمَانِهِمْ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمُ
الْأَنْهَارُ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٩﴾

“Hakika walioamini na wakatenda mema, Mola Wao Mlezi Atawaongoa kwa sababu ya Imani yao. Itakuwa inapita mito kati yao katika Mabustani yenye neema.” (10:9)

Kauli ya Allah تعالى:

وَيُصَلِّحُ بِأَهَمِّ

“...na Awatengezee hali yao.”

Maana yake: Jambo lao na hali yao,

وَيُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ عَرَفَهَا هُمْ

“Na Atawaingiza katika Pepo Aliyowajulisha.”

Maana yake: Aliwajulisha na Kuwaongoza kwenda peponi. Mujahid alisema: “Atawaongoza wakazi wake kwenda katika nyumba na maskani yao, na mahali ambapo Allah تعالى Aliwagawanyia humo, hawatakosea, kana kwamba ni wakazi wa huko tangu walipoumbwa, hawatamuuliza yeyote wa kuwaelekeza.”¹

Bukhari amepokea kutoka kwa Abuu Said Al-Khudri عنه رضي الله عنه kwamba; Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا خَلَصَ الْمُؤْمِنُونَ مِنَ النَّارِ حُبِسُوا بِقَنْطَرَةٍ بَيْنَ الْجَنَّةِ وَالنَّارِ، يَتَمَاصُونَ مَطَالِمَ
كَانَتْ بَيْنَهُمْ فِي الدُّنْيَا، حَتَّى إِذَا هُدُّوا وَنُقُوا أُذِنَ لَهُمْ فِي دُخُولِ الْجَنَّةِ، وَالَّذِي
نَفْسِي بِيَدِهِ! إِنَّ أَحَدَهُمْ بِمَنْزِلِهِ فِي الْجَنَّةِ أَهْدَى مِنْهُ بِمَنْزِلِهِ الَّذِي كَانَ فِي الدُّنْيَا»

¹ At-Tabari 22:160.

“Waumini wakishaokoka na Moto, watazuiwa katika daraja lililo baina ya Pepo na Moto, wakilipiana dhuluma zilizokuwa baina yao duniani, mpaka watakaposafishwa na kutakata kabisa, wataruhusiwa kuingia Peponi. Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Kila mmoja kati yao, atakwenda katika makazi yake Peponi akiwa ameongoka zaidi kuliko makazi yake aliyokuwemo duniani.”¹

Mnusuruni Allah تعالیٰ, Atakunusuruni

Kisha, Allah تعالیٰ Amesema:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَنْصُرُوا اللَّهَ يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ ﴿٧﴾

“Enyi mliaoamini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu Naye Atakunusuruni na Ataithibitisha miguu yenu.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ:

وَلْيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَن يَنْصُرُهُ

“Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu Humsaidia yule anayemsaidia Yeye.” (22:40)

Kwani malipo ni kwa jinsi ya amali yenyewe. Kwa ajili hii, Allah تعالیٰ Alisema:

وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ

“...na Ataithibitisha miguu yenu.”

Kama ilivyokuja katika Hadithi, kuwa Mwenye kumfikishia mwenye mamlaka haja ya mtu asiyoweza kumfikishia, Allah تعالیٰ Atathibitisha nyayo zake katika *Swirat* (njia nyoofu), Siku ya Kiyama. Kisha, Allah تعالیٰ Akasema:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا فَتَعَسَا لَهُم

“Na waliokufuru, basi kwao ni maangamizo...”

¹ Al-Bukhari na. 6535.

Hiki ni kinyume cha nyayo za Waumini wanaomnusuru Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ kuwa madhubuti. Kuna Hadithi iliyothibiti kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alisema:

تَعِسَ عَبْدُ الدِّيَارِ، تَعِسَ عَبْدُ الدِّرْهَمِ، تَعِسَ عَبْدُ القَطِيفَةِ، تَعِسَ وَاتَّكَسَ وَإِذَا
شَيْكَ فَلَا انْتَفَسَ،

“Ameangamia mtu anayeabudu dinari; Ameangamia mtu anayeabudu dirhamu; Ameangamia mtumwa wa nguo, ameangamia na ameanguka akichomwa na mwiba, asipate wa kuutoa.”¹

Maana yake Allah تعالى Asimponye. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ

“...na Atavipoteza vitendo vyao.”

Maana yake: Avibatilishe na Kuvikosesha matunda. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أُنزَلَ اللَّهُ

“Hayo ni kwa sababu waliyachukia Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu...”

Inamaanisha, hawayataki wala hawayapendi,

فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ

“...basi Akaviangusha vitendo vyao.”

* * *

¹ Fat'h Al-Bari 6:95 na Ibn Majah 2:1386

* أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ
 مِنْ قَبْلِهِمْ ۖ دَمَّرَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ ۗ وَلِلْكَافِرِينَ أَمْثَلُهَا ﴿١٠﴾ ذَلِكَ
 بِأَنَّ اللَّهَ مَوْلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَأَنَّ الْكَافِرِينَ لَا مَوْلَى لَهُمْ ﴿١١﴾
 إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ
 تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ
 كَمَا تَأْكُلُ الْأَنْعَامُ وَالنَّارُ مَثْوًى لَهُمْ ﴿١٢﴾ وَكَأَيِّنْ مِنْ قَرْيَةٍ
 هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِنْ قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجْتِكَ أَهْلَكَنَّهُمْ فَلَا
 نَاصِرَ لَهُمْ ﴿١٣﴾ أَفَمَنْ كَانَ عَلَىٰ بَيْتِهِ مِنْ رَبِّهِ كَمَنْ زُيِّنَ
 لَهُ سُوءُ عَمَلِهِ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ﴿١٤﴾ مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي
 وُعدَ الْمُتَّقُونَ ۗ فِيهَا أَنْهَارٌ مِنْ مَاءٍ غَيْرِ ءَاسِنٍ وَأَنْهَارٌ مِنْ لَبَنٍ
 لَمْ يَتَغَيَّرْ طَعْمُهُ وَأَنْهَارٌ مِنْ خَمْرٍ لَذَّةٍ لِلشَّارِبِينَ وَأَنْهَارٌ مِنْ
 عَسَلٍ مُصَفًّى ۗ وَهُمْ فِيهَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَمَغْفِرَةٌ مِنْ رَبِّهِمْ ۗ
 كَمَنْ هُوَ خَلِيدٌ فِي النَّارِ وَسُقُوا مَاءً حَمِيمًا فَقَطَّعَ أَمْعَاءَهُمْ
 ﴿١٥﴾ وَمِنْهُمْ مَنْ يَسْتَمِعُ إِلَيْكَ حَتَّىٰ إِذَا خَرَجُوا مِنْ عِنْدِكَ
 قَالُوا لِلَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مَاذَا قَالَ ءَايِنَا ۚ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ
 طَبَعَ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ﴿١٦﴾ وَالَّذِينَ
 آهْتَدُوا زَادَهُمْ هُدًى وَءَاتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ ﴿١٧﴾ فَهَلْ
 يَنْظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَنْ تَأْتِيَهُمْ بَغْتَةً ۗ فَقَدْ جَاءَ أَشْرَاطُهَا ۗ
 فَأَنَّىٰ لَهُمْ إِذَا جَاءَهُمْ ذِكْرُهُمْ ﴿١٨﴾ فَاعْلَمُوا أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا
 اللَّهُ ۗ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنْبِكَ ۗ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ
 مُتَقَلِّبِكُمْ ۗ وَمَثُونَكُمْ ﴿١٩﴾

* أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا
 كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۖ
 دَمَّرَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ ۗ وَلِلْكَافِرِينَ أَمْثَلُهَا
 ﴿١٠﴾ ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ مَوْلَى الَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَأَنَّ الْكَافِرِينَ لَا مَوْلَى لَهُمْ
 ﴿١١﴾ إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا
 وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ
 تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَتَمَتَّعُونَ
 وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ الْأَنْعَامُ وَالنَّارُ
 مَثْوًى لَهُمْ ﴿١٢﴾ وَكَأَيِّنْ مِنْ قَرْيَةٍ
 هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِنْ قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجْتِكَ
 أَهْلَكَنَّهُمْ فَلَا نَاصِرَ لَهُمْ ﴿١٣﴾

10. "Kwani hawakutembea katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa waliokuwa kabla yao? Mwenyezi Mungu Aliwangamiza, na kwa makafiri hawa itakuwa mfano wa hayo."

11. "Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Na makafiri hawana mlinzi."

12. ***“Hakika Mwenyezi Mungu Atawaingiza walioamini na wakatenda wema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake. Na waliokufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao.”***

13. ***“Na miji mingapi iliyokuwa na nguvu zaidi kuliko mji wako huu waliokutoa; nao Tuliwateketeza na wala hawakupata wa kuwanusuru.”***

Moto ni kwa Ajili ya Makafiri, na Pepo ni kwa Ajili ya Wachamungu

Allah تعالى Anasema:

أَفَلَمْ يَسِيرُوا

“Kwani hawakutembea...”

Maana yake: Wanaomshirikisha Allah تعالى, na wanamkanusha Mjumbe Wake,

فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَنِقَةَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ دَمَّرَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ

“...katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa waliokuwa kabla yao? Mwenyezi Mungu Aliwaangamiza...”

Maana yake: Aliwaadhibu kwa sababu ya ukadhibishaji na ukafiri wao. Ina maana pia akawaokoa Waumini kutoka miongoni mwao. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَلِلْكَافِرِينَ أَمْثَلُهَا

“...na kwa makafiri hawa itakuwa mfano wa hayo.”

Kisha, Akasema:

ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ مَوْلَى الَّذِينَ آمَنُوا وَأَنَّ الْكَافِرِينَ لَا مَوْلَى لَهُمْ

“Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Na makafiri hawana mlinzi wao.”

Kwa ajili hii, Abuu Sufian Swakhr bin Harb, kiongozi wa washirikina, alipouliza katika siku ya Uhud kuhusu Mtume ﷺ, Abubakr na ‘Umar رضي الله عنهما, bila ya kujibiwa, alisema: “Hakika wameshakufa.” ‘Umar bin Al-Khattwab رضي الله عنه

akamjibu: “Umeongopa, Ewe adui wa Allah! Bali, Allah تعالى Amewanusuru wale watakaokuchukiza. Kwa hakika! Wote uliowataja wangali hai bado.” Abu Sufyan akasema: “Siku hii ya leo inailipiza ile ya Badr, na vita hupanda na kushuka. Hakika nyinyi, mtapata madhara ambayo sikuyaamuru wala kuyakataza.” Akaondoka huku akiimba mashairi, “Utukufu ni wa Hubal (sanamu lao kubwa kabisa), utukufu ni wa Hubal.” Mtume ﷺ akasema:

«أَلَا نُجِيبُوهُ؟»

“Mbona hamumjibu.”

Wakauliza: “Ewe Mtume! Tutajibu vipi?” Akawaambia,

«قُولُوا: اللَّهُ أَغْلَى وَأَجَلُّ»

“Semeni, ‘Allah Ndiye Aliye juu kabisa, na Mwenye Utisho zaidi.’”

Kisha, Abu Sufyan alisema: “Sisi tunaye Al-‘uzza (sanamu la pili), wala ninyi hamna ‘uzza (utukufu).” Mtume ﷺ akasema:

«أَلَا نُجِيبُوهُ؟»

“Mbona hamumjibu?”

Wakauliza: “Ewe Mtume! Tutajibu vipi?” Akawaambia,

«قُولُوا: اللَّهُ مَوْلَانَا وَلَا مَوْلَى لَكُمْ»

“Semeni, ‘Allah ni Mlinzi Wetu, wala nyinyi hamna mlinzi.’”¹

Kisha, Allah تعالى Anasema:

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Atawaingiza walioamini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake.”

Maana yake: Siku ya Kiyama,

¹ Fath Al-Bari 6:188.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ الْأَنْعَامُ

“Na waliokufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama...”

Maana yake: Katika maisha yao ya duniani, wana starehe nayo na wanakula humo kama ulaji wa wanyama kwa kutafuna kwa nguvu na kuguguna, wala hawana malengo mengine, isipokuwa hayo. Kwa hivyo, ilithibiti katika Hadithi Sahih:

«الْمُؤْمِنُ يَأْكُلُ فِي مَعَى وَاحِدٍ، وَالْكَافِرُ يَأْكُلُ فِي سَبْعَةِ أَنْعَاءٍ»

“Muumini hula katika utumbo mmoja na kafiri hula katika tumbo saba.”¹

Halafu, Allah تعالى Alisema,

وَالنَّارُ مَثْوًى لَهُمْ

“...na Moto ndio makaazi yao.”

Katika siku ya malipo yao. Kauli ya Allah تعالى Anasema:

وَكَايِنٍ مِّن قَرْيَةٍ هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِّن قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجْتِكَ

“Na miji mingapi iliyokuwa na nguvu zaidi kuliko mji wako huu walio kutoa...”

Maana yake: Makka,

أَهْلَكْنَاهُمْ فَلَا نَاصِرَ لَهُمْ

“...nao Tuliwateketeza na wala hawakuwa wa kuwanusuru.”

Hili ni karipio kali na ahadi yenye msisitizo kwa wakazi wa Makkah, kwa kumkanusha Mtume ﷺ, na yeye ndiye mkuu wa Mitume na Nabii wa mwisho. Ikiwa, Allah تعالى Aliziangamiza kaumu zilizowakadhibisha Mitume kabla yake, kwa sababu ya hao Mitume, na ilhali wao walikuwa na nguvu kubwa zaidi yao, basi wana dhana gani Allah تعالى Kuwafanyia hayo duniani na Akhera? Na

¹ Fat'h Al-Bari 9:446.

ikiwa wengi katika wao wataondolewa adhabu duniani mintarafu ya baraka ya kuwepo kwa Mtume ﷺ, Nabii wa rehema, basi adhabu itakuwa kubwa kwa makafiri katika marejeo yao,

يُضَعَفُ لَهُمُ الْعَذَابُ مَا كَانُوا يَسْتَطِيعُونَ السَّمْعَ وَمَا كَانُوا يُبْصِرُونَ ﴿١١﴾

“Watazidishiwa adhabu. Hawakuwa wakiweza kusikia wala hawakuwa wakiona.” (11:20)

Kauli ya Allah تعالى:

مِنْ قَرِيْبِكَ الَّتِي أَخْرَجْتَنِي

“...kuliko mji wako huu waliokutoa...”

Maana yake: Waliokutoa katika maeneo yao. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisema, Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alieleza kwamba Mtume ﷺ alipotoka Makkah kwenda katika pango. Alipofika aligeuka kuangalia Makkah na akasema,

«أَنْتِ أَحَبُّ بِلَادِ اللَّهِ إِلَيَّ، وَأَنْتِ أَحَبُّ بِلَادِ اللَّهِ إِلَيَّ، وَلَوْلَا أَنَّ الْمُسْرِكِينَ
أَخْرَجُونِي لَمْ أَخْرُجْ مِنْكَ»

“Wewe ni mji unaopendwa sana na Allah miongoni mwa miji ya Allah, na wewe ndio mji niupendao sana kati ya miji ya Allah, lau kama si kunitoa washirikina, mimi nisingelitoka kwako.”

Kisha Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Adui mbaya zaidi ni yule mwenye kumfanyia uadui Yeye katika mahali Pake Patukufu, au akamuua mtu asiyepegana naye au akaua kwa sababu ya kisasi cha Jahiliyyah.”

Allah تعالى Akamteremshia Nabii Wake Aya ifuatayo:

وَكَايْنٍ مِّنْ قَرِيْبٍ هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِّنْ قَرِيْبِكَ الَّتِي أَخْرَجْتَنِي أَهْلَكْنَهُمْ فَلَا نَاصِرَ لَهُمْ ﴿١٢﴾

“Na miji mingapi iliyo kuwa na nguvu zaidi kuliko mji wako huu waliokutoa; nao Tuliwateketeza na wala hawakuwa wa kuwanusuru.”¹

¹ At-Tabari 22:165.

أَفَمَنْ كَانَ عَلَىٰ بَيْنَةٍ مِّن رَّبِّهِ كَمَنْ زُيِّنَ لَهُ سُوءُ عَمَلِهِ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ﴿١٤﴾ مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وَعَدَ الْمُتَّقُونَ ۚ فِيهَا أَنْهَارٌ مِّن مَّاءٍ غَيْرِ آسِنٍ وَأَنْهَارٌ مِّن لَّبَنٍ لَّمْ يَتَغَيَّرَ طَعْمُهُ وَأَنْهَارٌ مِّن خَمْرٍ لَّذَّةٍ لِلشَّارِبِينَ وَأَنْهَارٌ مِّن عَسَلٍ مُّصَفًّى ۚ وَهُمْ فِيهَا مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَمَغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ ۚ كَمَنْ هُوَ خَالِدٌ فِي النَّارِ وَسُقُوا مَاءً حَمِيمًا فَقَطَّعَ أَمْعَاءَهُمْ ﴿١٥﴾

14. *“Je! Mwenye kuwa na ubainifu kutoka kwa Mola Wake Mlezi ni kama aliyepambiwa uovu wa vitendo vyake, na wakafuata matamano ya nafsi zao?”*

15. *“Mfano wa Pepo walioahidiwa wachamungu ina mito ya maji yasiyovunda, na mito ya maziwa isiyo haribika ladha yake, na mito ya mvinyo yenye ladha kwa wanywao, na mito ya asali iliyosafishwa. Na wao humo watakuwa na kila namna ya matunda, na msamaha kutoka kwa Mola Wao Mlezi. Basi hao ni kama watakaodumu Motoni na wakinyweshwa maji yanayochemka ya kuwakata matumbo yao?”*

Hawalingani Wenye Kuabudu Haki na Wenye Kuabudu Matamano.

Allah تعالیٰ Anasema:

أَفَمَنْ كَانَ عَلَىٰ بَيْنَةٍ مِّن رَّبِّهِ

“Je! Mwenye kuwa na bayana kutoka kwa Mola Wake Mlezi...”

Maana: Kwa mwenye busara na yakini kuhusu Amri za Allah تعالیٰ na Dini Yake kwa sababu ya uongofu na ilimu iliyo ndani ya Kitabu Chake Alichokiteremsha, na kutokana na umbo nyooфу Alilomuumbia Allah تعالیٰ,

كَمَنْ زُيِّنَ لَهُ سُوءُ عَمَلِهِ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ

“...ni kama aliyepambiwa uovu wa vitendo vyake, na wakafuata pumbao lao?”

Maana yake: Huyu si kama huyu. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ:

أَفَمَنْ يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَىٰ

“ Je! Anaye jua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola Wako Mlezi ni Haki ni sawa na aliye kipofu?...”, (13:19)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٥٩﴾

“Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.” (59:20)

Sifa za Pepo na Mito Yake

Kisha, Allah تعالى Amesema:

مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وَعَدَ الْمُتَّقُونَ ۗ

“Mfano wa Pepo waliyoahidiwa wachamngu...”

‘Ikrimah amesema,

مَثَلُ الْجَنَّةِ

“Mfano wa Pepo...”

Maana yake: Sifa zake,

فِيهَا أَنْهَارٌ مِنْ مَاءٍ غَيْرِ آسِنٍ

“...ina mito ya maji yasiyovunda...”

Ibn ‘Abbas , Al-Hasan na Qatadah wamesema: “Yaani, Haibadiliki.”¹ Qatadah, Adh-Dhahhak, na ‘Ata Al-Khuraasani walisema: “Si yenye kunuka.”² Waarabu husema, “Asinal-Ma-u (maji yamevunda).” ikibadilika harufu yake.

وَأَنْهَارٌ مِنْ لَبَنٍ لَمْ يَتَغَيَّرَ طَعْمُهُ

“...na mito ya maziwa isiyoharibika ladha yake...”

¹ At-Tabari 22:166.

² At-Tabari 22:167.

Maana yake: Bali yatakuwa katika ukomo wa weupe, utamu na virutubisho. Na katika Hadithi ya Mtume ﷺ, 'Hayakutoka katika viwele vya mnyama.'

وَأَهْتَرُّ مِّنْ خَمْرٍ لَّدَىٰ لِلشَّرِيرِينَ

"...na mito ya mvinyo yenye ladha kwa wanywao..."

Maana yake: Si yenye ladha wala harufu mbaya ya kukirahisha kama ulivyo mvinyo wa duniani, bali ni nzuri katika mtazamo, ladha, harufu na utendaji.

Allah تعالیٰ Anasema:

لَا فِيهَا غَوْلٌ وَلَا هُمْ عَنْهَا يُنْزَفُونَ ﴿٣٧﴾

"Hakina madhara, wala hakiwaleweshi." (37:47)

Na Kauli ya Allah تعالیٰ,

لَا يُصَدَّعُونَ عَنْهَا وَلَا يُنْزَفُونَ ﴿٣٨﴾

"Hawataumwa kichwa kwa vinywaji hivyo wala hawatoleweshwa." (56:19)

Na Kauli ya Allah تعالیٰ,

بَيِّضَاءَ لَّدَىٰ لِلشَّرِيرِينَ ﴿٣٩﴾

"Kinywaji cheupe, kitamu kwa wanywao." (37:46)

Imeelezwa katika Hadithi "Marfu" kuwa, 'Watu hawakuikamua kwa miguu yao.'

وَأَهْتَرُّ مِّنْ عَسَلٍ مُّصَفًّى

"...na mito ya asali iliyosafishwa."

Maana yake: Ipo safi kabisa, rangi nzuri, ladha na harufu ya kutamanisha. Katika Hadithi 'Marfu' nyingine, "Haikutoka katika matumbo ya nyuki."¹

Imamu Ahmad amesimulia kuwa Hakim bin Mu'awiyah alipokea toka kwa baba yake kuwa alisema, nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

¹ Masimulizi haya na maana ya yaliyo kabla yake yameandikwa na Al-Mundhir kama lafudhi ya Sa'id bin Jubayr kwa mujibu wa *Ad-Dur Al-Manthur* 6:25.

«فِي الْجَنَّةِ بَحْرُ اللَّبَنِ وَبَحْرُ الْمَاءِ وَبَحْرُ الْعَسَلِ وَبَحْرُ الْخَمْرِ، ثُمَّ تُشَقَّقُ الْأَنْهَارُ مِنْهَا بَعْدُ»

“Peponi kuna bahari ya maziwa, ya maji, ya asali, ya pombe. Kisha mito inabubujika kutokea huko.”¹

At-Tirmidhi aliyankuu masimulizi haya kuhusu wasifu wa Pepo, na amesema; “Hadithi ina daraja ya Hasan Sahih.”²

Katika Sahih imekuja Hadithi isemayo;

«إِذَا سَأَلْتُمْ اللَّهَ تَعَالَى فَاسْأَلُوهُ الْفِرْدَوْسَ فَإِنَّهُ أَوْسَطُ الْجَنَّةِ، وَأَعْلَى الْجَنَّةِ، وَمِنْهُ تُفَجَّرُ أَنْهَارُ الْجَنَّةِ، وَفَوْقَهُ عَرْشُ الرَّحْمَنِ»

“Mnapomuomba Allah Taala, basi muombeni pepo ya Al-Firdaws, kwani hiyo ndio pepo yenye hadhi ya kati na ya juu zaidi na pepo hiyo hutiririka mito ya Peponi, na juu yake ipo Arshi ya Ar-Rahman.”³

Kauli ya Allah تعالی:

وَهُمْ فِيهَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ

“Na wao humo watakuwa na kila namna ya matunda...”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

يَدْعُونَ فِيهَا بِكُلِّ فَاكِهَةٍ آمِنِينَ ﴿٥٥﴾

“Humo watataka kila aina ya matunda, na wakae kwa amani.”
(44:55)

Na Kauli ya Allah تعالی:

فِيهِمَا مِنْ كُلِّ فَاكِهَةٍ زَوْجَانِ ﴿٥٢﴾

“Humo katika kila matunda zimo namna mbili.” (55:52)

Kauli ya Allah تعالی:

¹ Ahmad 5:5.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 7:287.

³ Fat'h Al-Bari 6:14.

وَمَغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ

"...na maghufira kutoka kwa Mola Wao Mlezi."

Maana yake: Pamoja na hayo yote. Kauli ya Allah تعالى:

كَمَنْ هُوَ خَلِدٌ فِي النَّارِ

"...ni kama watakaodumu Motoni..."

Inamaanisha, je, hao Tuliowataja, makazi yao katika Pepo, ni sawa na watakaoka milele Motoni? hawa sio kama hao, na walio katika daraja za juu (peponi), hawalingani na watakaokuwa katika tabaka za chini (motoni).

وَسُقُوا مَاءً حَمِيمًا

"...na wakinyweshwa maji yanayochemka..."

Maana yake: Ya moto mno, asiyoyamudu mtu,

فَقَطَّعَ أَمْعَاءَهُمْ

"...ya kuwakata matumbo yao?"

Maana yake: Kakata matumbo yao na yaliyomo ndani ya matumbo yao – Tunamuomba Allah تعالى Atukinge na shari hiyo.

وَمِنْهُمْ مَّن يَسْتَمِعُ إِلَيْكَ حَتَّىٰ إِذَا خَرَجُوا مِنْ عِندِكَ قَالُوا لِلَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مَاذَا قَالَ
ءَانفَاءً ۗ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ طَبَعَ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ﴿١٦﴾ وَالَّذِينَ اهْتَدَوْا زَادَهُمْ
هُدًى ۖ وَآتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ ﴿١٧﴾ فَهَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَن تَأْتِيَهُمْ بَغْتَةً ۖ فَقَدْ جَاءَ
أَشْرَاطُهَا ۗ فَأَنَّىٰ لَهُمْ إِذَا جَاءَهُمْ ذِكْرُهُمْ ﴿١٨﴾ فَأَعْلَمَ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ۖ وَأَسْتَغْفِرُ
لِدُنْيَاكَ ۖ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مُتَقَلَّبَكُمْ وَمَثْوَاكُمْ ﴿١٩﴾

16. "Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza, mpaka wakiondoka kwako huwauliza waliopewa ilimu: Amesema nini sasa hivi? Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu Amepiga muhuri juu ya nyoyo zao, na wakafuata matamania ya nafsi zao."

17. ***“Na wale walioongoka Anawazidishia uongofu na Anawapa uchamungu wao.”***

18. ***“Kwani wanangojea jengine isipokuwa iwafikie Saa (ya Kiyama) kwa ghafla? Na hakika alama zake zimekwisha kuja. Na itapowajia kutawafaa wapi kukumbuka hapo?”***

19. ***“Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu, na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu Anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa.”***

Ubainifu wa Hali za Wanafiki na Agizo la Tauhidi na Kuomba Maghifira.

Allah تعالى Anaeleza kuhusu ujinga wa wanafiki na uchache wa ufahamu wao, kwamba walikuwa wakikaa kumzunguka Mtume ﷺ kwa kumsikiliza pasi na kuelewa chochote kutoka kwake, wakishaondoka katika hadhara yake,

قَالُوا لِلَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ

“...huwauliza waliopewa ilimu...” Katika Masahaba,

مَاذَا قَالَ ءَايِنْفًا

“Amesema nini sasa hivi?” Maana yake: Sasa hivi. Hawakijui alichokisema, wala hawakizingatii. Allah تعالى Anasema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ طَبَعَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ

“Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu Amepiga muhuri juu ya nyoyo zao, na wakafuata pumbao lao.”

Maana yake: Hawana fahamu sahihi wala nia sahihi. Kisha, Allah تعالى Amesema:

وَالَّذِينَ أَهْتَدُوا زَادَهُمْ هُدًى

“Na wale walioongoka Anawazidishia uongofu...”

Inamaanisha, waliokusudia uongofu, basi Allah تعالى Huwawafikisha kwa uongofu huo, na Kuwaongoza kuufikia, Akawathubutisha juu yake na Kuwazidishia kutokana nao,

وَأَتَنَّهُمْ تَقْوَلُهُمْ

“...*na Anawapa uchamungu wao.*”Maana yake: Huwapa ilhamu ya kuongoka.

Kauli ya Allah تعالى،

فَهَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَنْ تَأْتِيَهُمْ بَغْتَةً

“Kwani wanangojea jengine isipokuwa kiwafikie Qiyama kwa ghafla?”

Maana yake: Wakiwa wameghafilika nayo،

فَقَدْ جَاءَ أَشْرَاطُهَا

“Na hakika alama Zake zimekwisha kuja.”

Maana yake: Alama za kukaribia kwake. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

هَذَا تَذِيرٌ مِّنَ الْتَذِيرِ الْأُولَى ﴿٥٦﴾ أُرِفَتِ الْأَرْفَةُ ﴿٥٧﴾

“Hili ni Onyo katika maonyo yale yale ya zamani. Kiyama kimekaribia!” (53:56-57)

Na kama Kauli Yake Allah تعالى،

أَقْرَبَتِ السَّاعَةُ وَأَدْنَى الْقَمَرُ ﴿٥٨﴾

“Kiyama kimekaribia, na mwezi umepasuka!” (54:1)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

أَنَّى أَمْرٌ اللَّهُ فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ

“Amri ya Mwenyezi Mungu itafika tu. Basi msiihimize (16:1)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

أَقْرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ مُّعْرِضُونَ ﴿٢١﴾

“Imewakaribia watu hisabu yao, nao wamo katika mghafala wanapuza.”(21:1)

Kwa hivyo, kutumwa Mtume ﷺ ni miongoni mwa alama Zake, kwa sababu yeye ndiye mwisho wa Mitume. Kwake yeye, Allah تعالى Ameikamilisha Dini na

Kusimamisha ushahidi juu ya walimwengu. Mtume ﷺ alishaeleza ishara za Kiyama, akazibainisha na kuziweka wazi kuliko Nabii yeyote wa kabla yake, kama ilivyofafanuliwa kwa kirefu mahali pake panapostahiki.

Al-Bukhari alimnukuu Sahl bin Sa'd عنه رضي الله kuwa alisema: "Nilimuona Mtume ﷺ akiviambatanisha vidole vyake, cha kati na kinachokifuata, na akasema:

«بُعِثْتُ أَنَا وَالسَّاعَةَ كَهَاتَيْنِ»

*"Nimetumwa mimi na Qiyama ni kama (vidole) hivi viwili."*¹

Kisha, Allah تعالى Amesema:

فَأَنى لَهُمْ إِذَا جَاءَهُمْ ذِكْرُهُمْ

"Na itapowajia kutawafaa wapi kukumbuka hapo?"

Yaani, kukumbuka kutawafaa nini makafiri baada ya kufika kwa Kiyama? Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يَوْمَئِذٍ يَجْهَنَّمُ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ الْإِنسَانُ وَأَنى لَهُ الذِّكْرُ ﴿٢٣﴾

"Siku hiyo mtu atakumbuka! Lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?" (89:23) na,

وَقَالُوا ءَأَمْنَا بِهِ ءَأَنى لَهُمُ التَّنَافُسُ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٥٢﴾

"Na watasema: Tunaiamini! Lakini wataipata wapi kutoka huko mahala mbali?" (34:52)

Kauli ya Allah تعالى:

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

"Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu..."

Haya ni maelezo kwamba hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى. Si jambo jepesi yeye Kuwaamuru watu walijue hilo. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alifuatishia na Kauli Yake:

¹ Fat'h Al-Bari 8:560.

وَأَسْتَغْفِرُ لِدُنْبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ¹

“...na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake.”

Hadithi iliyoandikwa katika Sahih, inaeleza kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ amesema,

«اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي خَطِيئَتِي وَجَهْلِي وَإِسْرَافِي فِي أَمْرِي وَمَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي هَزْلِي وَجِدِّي، وَخَطِيئِي وَعَمْدِي، وَكُلُّ ذَلِكَ عِنْدِي»

“Ewe Allah! Nighufirie madhambi yangu, kutokujua kwangu, israfu yangu katika mambo yangu, na yote ambayo, Wewe unayajua zaidi kuliko mimi. Ewe Allah! Nighufirie mizaha yangu, umakini wangu, makosa yangu ya makusudi au bahati mbaya, na yote hayo yakitokana nami.”¹

Kuna Hadithi katika Sahih, kwamba Mtume ﷺ alikuwa akisema ndani ya Sala,

«اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي مَا قَدَّمْتُ وَمَا أَخَّرْتُ، وَمَا أَسْرَرْتُ وَمَا أَعْلَنْتُ، وَمَا أَسْرَفْتُ، وَمَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي، أَنْتَ إِلَهِي لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ»

“Ewe Allah! Nighufirie niliyoyatanguliza na niliyoyaakhirisha, niliyoyafanya siri, niliyoyadhihirisha, niliyoyafuja, na yote ambayo Wewe Unayajua zaidi kuliko mimi. Wewe ni Mola Wangu, hapana wa kuabudiwa isipokuwa Wewe.”²

Pia katika Sahih kuna Hadithi:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ تَوْبُوا إِلَيَّ رَبِّكُمْ، فَإِنِّي أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ فِي النَّيِّمِ أَكْثَرَ مِنْ سَبْعِينَ مَرَّةً»

“Enyi watu! Tubuni kwa Mola wenu, kwani mimi huwa naomba maghufira na kutubu Kwake zaidi mara sabini kwa siku.”³

¹ Fat’h Al-Bari 11:200.

² Fat’h Al-Bari 13:473.

³ Fat’h Al-Bari 11:104.

Kauli ya Allah تعالى:

وَاللَّهُ يَعْلَمُ مُتَقَلَّبِكُمْ وَمَثَوْلَكُمْ

“Na Mwenyezi Mungu Anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa.”

Maana yake: Anajua mnachokifanya wakati wa mchana na mnapopitisha usiku. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّنَكُمْ بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ بِالنَّهَارِ

“Naye Ndiye Anayekufisheni usiku, na Anakijua mlichofanya mchana.”

Na Kauli ya Allah تعالى,

* وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي

كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦﴾

“Na hakuna kiumbe chochote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye Anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.” (11:6)

* * *

وَيَقُولُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَوْلَا نُزِّلَتْ سُورَةٌ ۗ فَإِذَا أُنزِلَتْ
 سُورَةٌ مُحْكَمَةٌ وَذُكِرَ فِيهَا الْقِتَالُ ۗ رَأَيْتَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ
 مَرَضٌ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ نَظَرَ الْمَغْشِيِّ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ فَأَوْلَىٰ
 لَهُمْ ۗ طَاعَةٌ وَقَوْلٌ مَّعْرُوفٌ ۗ فَإِذَا عَزَمَ الْأَمْرُ فَلَوَّ
 صَدَقُوا اللَّهَ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ ۗ فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ تَوَلَّيْتُمْ
 أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ ۗ أُولَٰئِكَ
 الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فَأَصَمَّهُمْ وَأَعَمَّىٰ أَبْصَرَهُمْ ۗ أَفَلَا
 يَتَذَكَّرُونَ الْفُرْعَانَ ۗ أَمْ عَلَىٰ قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا ۗ إِنَّ
 الَّذِينَ آزَنُوا عَلَىٰ أَذْبَانِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ
 الْهُدَىٰ ۗ الشَّيْطَانُ سَوَّلَ لَهُمْ وَأَمَلَىٰ لَهُمْ ۗ ذَلِكَ
 بِأَنَّهُمْ قَالُوا لِلَّذِينَ كَرِهُوا مَا نَزَّلَ اللَّهُ سَنُطِيعُكُمْ فِي
 بَعْضِ الْأَمْرِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِسْرَارَهُمْ ۗ فَكَيْفَ إِذَا تَوَفَّتْهُمُ
 الْمَلَائِكَةُ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَذْبَرَهُمْ ۗ ذَلِكَ
 بِأَنَّهُمْ اتَّبَعُوا مَا أَسْخَطَ اللَّهَ وَكَرِهُوا رِضْوَانَهُ ۗ فَأَحْبَطَ
 أَعْمَلَهُمْ ۗ أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ أَنْ
 لَنْ يُخْرِجَ اللَّهُ أَصْغَبَهُمْ ۗ وَلَوْ نَشَاءُ لَأَرَيْنَاكُمْ
 فَلَعَرَفْتَهُمْ بِسِيمَتِهِمْ ۗ وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ ۗ وَاللَّهُ
 يَعْلَمُ أَعْمَالَكُمْ ۗ وَلَتَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ الْمُجْهِدِينَ
 مِنْكُمْ وَالصَّابِرِينَ وَتَبْلُوَ أَخْبَارَكُمْ ۗ

وَيَقُولُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَوْلَا نُزِّلَتْ
 سُورَةٌ ۗ فَإِذَا أُنزِلَتْ سُورَةٌ مُحْكَمَةٌ
 وَذُكِرَ فِيهَا الْقِتَالُ ۗ رَأَيْتَ الَّذِينَ فِي
 قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ نَظَرَ
 الْمَغْشِيِّ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ فَأَوْلَىٰ
 لَهُمْ ۗ طَاعَةٌ وَقَوْلٌ مَّعْرُوفٌ ۗ فَإِذَا
 عَزَمَ الْأَمْرُ فَلَوَّ صَدَقُوا اللَّهَ لَكَانَ
 خَيْرًا لَهُمْ ۗ فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ
 تَوَلَّيْتُمْ أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ
 وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ ۗ أُولَٰئِكَ
 الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فَأَصَمَّهُمْ وَأَعَمَّىٰ
 أَبْصَرَهُمْ ۗ

20. "Na Waumini wana-
 sema: kwa nini haite-
 remshwi Sura? Na inapote-
 remshwa Sura madhubuti
 na ikatajwa ndani yake
 habari ya vita, utawaona
 wenye maradhi katika
 nyoyo zao wanakutazama
 mtazamo wa anayezimia
 kwa mauti. Basi ole wao."

21. "Ut'iifu na kauli njema.
 Na jambo likishaazimiwa,
 basi wakiwa ni wakweli

kwa Mwenyezi Mungu, bila ya shaka itakuwa ni kheri kwao.”

22. “Basi yanayotarajiwa kwenu mkikataa (kupigana Jihad) ndio mfidisi katika nchi na mvunje undugu wenu?”

23. “Hao ndio Mwenyezi Mungu Aliowalaani, na Akawatia uziwi, na Akawapofoa macho yao.”

Hali ya Muumini Wakweli na Wanafiki Wakati wa Kuteremka Amri ya Kupigana Jahadi

Allah تعالى Anawaeleza Waumini kuwa wao walikuwa wakitamani sheria ya Jahadi. Lakini, baada ya Allah تعالى Kuifaradhisha na Kuiamuru, watu wengi walikataa. Kama Allah تعالى Anavyosema:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ قِيلَ لَهُمْ كُفُّوا أَيْدِيَكُمْ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ
الْقِتَالُ إِذَا فَرِيقٌ مِنْهُمْ يَخْشَوْنَ النَّاسَ كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً وَقَالُوا رَبَّنَا لِمَ كَتَبْتَ
عَلَيْنَا الْقِتَالَ لَوْلَا أَخَّرْتَنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ قُلْ مَتَّعْتُ الدُّنْيَا قَلِيلًا وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِّمَنِ اتَّقَىٰ
وَلَا تُظَلَّمُونَ فِتْيَلًا ﴿٧٧﴾

“Je, huwaoni wale walioambiwa: Izuieni mikono yenu, na mshike Sala na mtoe Zaka. Na walipoamrisha kupigana, mara kundi moja kati yao liliwaogopa watu kama kumuogopa Mwenyezi Mungu, au kwa khofu kubwa zaidi. Na wakasema: Mola Mlezi Wetu! kwa nini umetuamrisha kupigana? Laiti ungetuakhirishia kiasi ya muda kidogo hivi! Sema: Starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa mwenye kumchamungu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi wa kokwa ya tende.” (4:77)

Katika Aya hii, Allah تعالى Anasema:

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَتْ سُورَةٌ

“Na Waumini wanasema: kwa nini haiteremshwi Sura?”

Maana yake Yenye kukusanya hukumu ya kupigana vita.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

فَإِذَا أَنْزَلَتْ سُورَةً مُحْكَمَةً وَذُكِرَ فِيهَا الْقِتَالُ رَأَيْتَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ
نَظَرَ الْمَغْشِيِّ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ

“Na inapoteremshwa Sura madhubuti na ikatajwa ndani yake habari ya vita, utawaona wenye maradhi katika nyoyo zao wanakutazama mtazamo wa anayezimia kwa mauti.”

Maana yake: Kwa sababu ya hofu na woga wao juu ya kukabiliana na maadui. Akawashajiisha kwa Kusema:

فَأُولَىٰ لَهُمْ ۖ طَاعَةٌ وَقَوْلٌ مَّعْرُوفٌ

“Basi ni bora kwao. Utiifu na kauli nzuri.”

Maana yake: Lililo bora kwao wasikie na wawe watiifu katika hali iliyopo sasa,

فَإِذَا عَزَمَ الْأَمْرُ

“Na jambo likishaazimiwa...”

Maana yake: Hali inapotinga na mapigano yakawadia,

فَلَوْ صَدَقُوا اللَّهَ

“...basi wakiwa ni wakweli kwa Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Wamsafishie Yeye nia,

لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ

“...bila ya shaka itakuwa ni kheri kwao.” Kauli ya Allah تعالى:

فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ تَوَلَّيْتُمْ

“Basi yanayotarajiwa kwenu mkikataa (kupigana Jihadi)...” Dhidi ya Jihadi na mkajitoa,

أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتَقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ

“...ndio mfididi katika nchi na mvunje undugu wenu?”

Inamaanisha, ndio mrudi katika ujahili wa majahili mliokuwemo? Ambapo mnamwaga damu na mnauvunja undugu. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

﴿أُولَئِكَ الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فَأَصَمَّهُمْ وَأَعَمَّى أَبْصَرَهُمْ﴾

“Hao ndio Mwenyezi Mungu Aliowalaani, na Akawatia uziwi, na Akawapofoa macho yao.”

Hili ni katazo la ujumla dhidi ya ufisadi ardhini, na hususan dhidi ya kuuvunja undugu, bali Allah تعالى Aliamuru kufanya katika ardhi wema na kuunga undugu, ambako ni kuwafanyia ihsani ndugu, kwa kauli, vitendo na kuwapa mali. Kuna Hadithi nyingi kutoka kwa Mjumbe wa Allah ﷺ ambazo zina daraja ya Hasan na Sahih zikizungumzia jambo hilo ambazo zina isnadi na njia nyingi. Al-Bukhari alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنہ kuwa Mtume ﷺ amesema:

«خَلَقَ اللهُ تَعَالَى الْخَلْقَ فَلَمَّا فَرَّغَ مِنْهُ قَامَتِ الرَّحْمُ فَأَخَذَتْ بِحَقْوِ الرَّحْمَنِ عَزَّ وَجَلَّ فَقَالَ: مَهْ، فَقَالَتْ: هَذَا مَقَامُ الْعَائِدِ بِكَ مِنَ الْقَطِيعَةِ، فَقَالَ تَعَالَى: أَلَا تَرْضَيْنِ أَنْ أَصِلَ مِنْ وَصْلِكَ وَأَقْطَعَ مَنْ قَطَعَكَ؟ قَالَتْ: بَلَى، قَالَ: فَذَلِكَ لَكَ،

“Allah Taala Aliumba viumbe. Alipomaliza, Uzao (udugu) ulisimama na kushika vazi la chini la Ar-Rahman. Akasema: “Acha.” Ukasema: ‘Kisimamo hiki ni cha mwenye kutaka hifadhi Kwako dhidi ya kukatwa.’ Allah Taala Akasema: ‘Hauridhii kwamba Nitamuunga mwenye kukuunga na Kumkataa mwenye kukukataa?’ Ukasema: ‘Naam.’ Akasema: ‘Basi, hayo sasa ni yako.” (Umepata ulichoomba)

Abu Hurayrah عنه رضي الله عنہ aliendelea kusema: Mkitaka, someni,

﴿فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ تَوَلَّيْتُمْ أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ﴾

“Basi yanayotarajiwa kwenu mkikataa (kupigana Jihadi) ndio mfisidi katika nchi na mvunje undugu wenu?”

Halafu, Bukhari aliinukuu kwa tamshi jingine kuwa Mtume ﷺ alisema:

﴿افْرءُوا إِنْ شِئْتُمْ ﴿فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ تَوَلَّيْتُمْ أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ﴾﴾

“Mkipenda, someni, **“Basi yanayotarajiwa kwenu mkikataa (Kupigana Jihadi) ndio mfisidi katika nchi na mvunje undugu wenu?”**

Pia Muslim aliinukuu. Imamu Ahmad alimnukuu Abu Bakrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا مِنْ ذَنْبٍ أُخْرَى أَنْ يُعَجَّلَ اللَّهُ تَعَالَى عُقُوبَتَهُ فِي الدُّنْيَا، مَعَ مَا يَدَّخِرُ لِصَاحِبِهِ فِي
الْآخِرَةِ، مِنَ الْبُغْيِ وَقَطِيعَةِ الرَّجْمِ»

*"Hapana dhambi yenye haki ya Allah kuiharakishia adhabu yake duniani, pamoja na kumuhifadhia muhusika wake huko akhera kuliko dhambi ya uasi na kukata undugu."*¹

Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibn Majah waliandika Hadithi hii, na At-Tirmidhi akasema: "Hadithi hii ni Sahih."²

Imamu Ahmad alimnukuu Thawbaan عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ سَرَّهُ النَّسَاءُ فِي الْأَجَلِ وَالزِّيَادَةُ فِي الرُّزْقِ، فَلْيَصِلْ رَجْمَهُ»

"Mwenye kupenda umri wake uongezwe na kuzidishwa kipato cha riziki, basi aunge undugu wake."

Ahmad peke yake aliinukuu, na ina masimulizi kutoka katika Sahih yanayoiunga mkono.³

Imamu Ahmad aliandika kutoka kwa 'Abdullah bin 'Amri عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ الرَّجْمَ مُعَلَّقَةٌ بِالْعَرْشِ، وَلَيْسَ الرَّاصِلُ بِالْمُكَافِي، وَلَكِنَّ الرَّاصِلَ الَّذِي إِذَا
قُطِعَتْ رَجْمُهُ وَصَلَّهَا»

"Kwa hakika! Uzao (udugu) umeambatanishwa na Arshi ya Allah. Kulipa Fadhila hakumaanishi kuunga udugu. Bali mwenye kuunga udugu ni yule ambaye udugu wake unapokatwa anauunga."

Hadithi hii Ameipokea Bukhari.⁴

¹ Ahmad 5:38.

² Abu Dawud 5:208, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 7:213, Ibn Majah 2:1408.

³ Ahmad 5:279, kadhalika na Al-Bukhari 5985.

⁴ *Fat'h Al-Bari* 10:437, na Ah 163.

«تُوضَعُ الرَّجِمُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ لَهَا [حُجْنَةٌ كَحُجْنَةِ] الْمِنْزَلِ تَكَلِّمُ بِلِسَانِ طَلِقٍ ذَلِي،
تَنْقَطِعُ مِنْ قَطْعِهَا وَتَصِلُ مِنْ وَصْلِهَا»

“Siku ya Kiyama, kizazi kitawekwa (kikiwa kimepindwa kama) gurudumu la kusokotea nyuzi, likizungumza kwa lugha fasaha na litamuacha aliyekata undugu na kumuunga aliyeuunga.”¹

Imamu Ahmad aliandika kuwa ‘Abdullah bin ‘Amri رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema:

«الرَّاجِمُونَ يَرْحَمُهُمُ الرَّحْمَنُ، ارْحَمُوا أَهْلَ الْأَرْضِ يَرْحَمَكُمُ أَهْلُ السَّمَاءِ، وَالرَّجِمُ
شُجْنَةٌ مِنَ الرَّحْمَنِ، مَنْ وَصَلَهَا وَصَلَتْهُ وَمَنْ قَطَعَهَا بَتَّهْ»

“Wenye rehema watarehemewa na Ar-Rahman. Wahurumieni wakazi wa ardhini, watakurehemuni watu wa mbinguni. Ar-Rahim (kizazi) hutoka kwa Ar-rahman, basi mwenye kukiunga nacho humuunga, na mwenye kukikata hukikata.”²

Abu Dawud na At-Tirmidhi waliinukuu Hadithi hii, na imesimuliwa kwa isnadi iliyo bora. At-Tirmidhi alisema, “Ni Hasan Sahih.”³ Hadithi zinazohusiana na suala hili ni nyingi sana.

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ أَمْرَ عَلَى قُلُوبٍ أَقْفَالَهَا ﴿٢٤﴾ إِنَّ الَّذِينَ أَرْتَدُّوا عَلَىٰ أَدْبَارِهِمْ
مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْهُدَىٰ الشَّيْطَانُ سَوَّلَ لَهُمْ وَأَمَلَىٰ لَهُمْ ﴿٢٥﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ
قَالُوا لِلَّذِينَ كَرِهُوا مَا نَزَّلَ اللَّهُ سَنطِيعُكُمْ فِي بَعْضِ الْأَمْرِ ط وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِسْرَارَهُمْ
﴿٢٦﴾ فَكَيْفَ إِذَا تَوَفَّتْهُمُ الْمَلَائِكَةُ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَارَهُمْ ﴿٢٧﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ
أَتَّبَعُوا مَا اسْحَطَّ اللَّهُ وَكَرِهُوا رِضْوَانَهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَلَهُمْ ﴿٢٨﴾

24. “Je! Hawaizingatii hii Qur’ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?”

25. “Kwa hakika wanaorudi nyuma baada ya kuishawabainikia uwongofu, Shetani huyo amewapambia juu ya hilo na amewarefushia muda wa matamano yao.”

¹ Ahmad 2:189.

² Ahmad 2:160.

³ Abu Dawud 5:231, na Tuhfat Al-Ahwadhi 6:51.

26. *“Hayo ni kwa sababu waliwaambia waliochukia Aliyoya-teremsha Mwenyezi Mungu: Tutakut’iini katika baadhi ya mambo. Na Mwenyezi Mungu Anajua siri zao.”*

27. *“Basi itakuwaje Malaika watakapowafisha wakawa wanawapiga nyuso zao na migongo yao!”*

28. *“Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyomchukiza Mwenyezi Mungu na wakachukia yanayomridhisha, basi Akaviangusha vitendo vyao.”*

Amri ya Kuzingatia Qur’an

Allah تعالى Anaamuru suala la kuitafakari na kuifahamu Qur’an na Akakataza kuipa mgongo. Kwa Kusema:

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ أَمْ عَلَى قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا ﴿٢٧﴾

“Je! Hawaizingatii hii Qur’ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?”

Maana yake: Kuna kufuli juu ya nyoyo zinazozifunga, hapana maana yoyote ya Qur’an inayozifikia. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Hisham bin ‘Urwah kuwa baba yake alisema: Siku moja Mtume ﷺ alisoma,

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ أَمْ عَلَى قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا ﴿٢٧﴾

“Je! Hawaizingatii hii Qur’ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?”

Kijana mmoja kutokea Yemen akasema, “Naam, juu yake kuna kufuli, mpaka Allah تعالى Ayafungue kabisa au kidogo.” Baada ya hapo, ‘Umar رضي الله عنه hakuacha kumpenda kijana huyo, mpaka akamteua katika kazi, na akamsaidia.”¹

Lawama Dhidi ya Kuritadi

Kisha, Allah تعالى Akasema:

إِنَّ الَّذِينَ آذَنُوا عَلَىٰ آذَانِهِمْ

“Kwa hakika wanaorudi nyuma...” Maana yake: Wakaiacha imani na wakarejea katika ukafiri,

¹ Tabari 22:180.

مَنْ بَعْدَ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْهُدَىٰ ۗ الشَّيْطَانُ سَوَّلَ لَهُمْ

“...baada ya kwisha wabainikia uwongofu, Shetani huyo amewashawishi...”

Maana yake: Walipambiwa hayo na wakapendezeshewa,

وَأَمَلَىٰ لَهُمْ

“...na amewaghuri.” Amewadanganya na kuwahadaa,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لِلَّذِينَ كَرِهُوا مَا نَزَّلَ اللَّهُ سَنَطِيعُكُمْ فِي بَعْضِ الْأُمْرِ

“Hayo ni kwa sababu waliwaambia waliochukia Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu: Tutakut’iini katika baadhi ya mambo.”

Inamaanisha, waliwajuza na wakawanasihi kwa siri katika upotofu uliofichamana. Hivi ndivyo wanafiki walivyo, wanayoyadhihirisha ni kinyume cha wanayoyaficha. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِسْرَارَهُمْ

“Na Mwenyezi Mungu Anajua siri zao.”

Maana yake Siri zao na wanayoyaficha, Allah تعالى Ana habari hizo na Anazijua.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَاللَّهُ يَكْتُبُ مَا يُبَيِّنُونَ

“Na Mwenyezi Mungu Anayaandika yote hayo wanayoyapangia njama za usiku.” (4:81)

Kisha, Allah تعالى Alisema:

فَكَيْفَ إِذَا تَوَفَّتْهُمُ الْمَلَائِكَةُ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَرَ هُمْ

“Basi itakuwaje Malaika watakapowafisha wakawa wanawapiga nyuso zao na migongo yao!”

Maana yake: Itakuwaje hali yao, pindi watakapowajia Malaika kutoa roho zao, nazo zikang’ang’ania katika viwiliwili vyao, na Malaika wakazitoa kwa ukali, nguvu na kipigo. Inalingana na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ يَتَوَفَّى الَّذِينَ كَفَرُوا الْمَلَائِكَةُ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَرَهُم

“Na laiti ungeliona Malaika wanapowafisha wale walio kufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao...” (8:50) na,

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُوا أَيْدِيَهُم

“Na lau ungeliliwaona madhalimu wanavyokuwa katika mfadhaiko wa mauti, na Malaika wamewanyoosha mikono...” (6:93)

Maana yake: Kwa kipigo,

أَخْرِجُوا أَنْفُسَكُمْ يَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهَوْنِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ
وَكُنْتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٧٣﴾

“Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyo ya haki, na mlivyokuwa mkizifanyia kiburi Ishara Zake.” (6:93)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Anasema katika Aya hii,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ اتَّبَعُوا مَا أَسْخَطَ اللَّهَ وَكَرَهُوا رِضْوَانَهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَلَهُمْ ﴿٧٤﴾

“Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyomchukiza Mwenyezi Mungu na wakachukia yanayomridhisha, basi Akaviangusha vitendo vyao.”

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ أَنْ لَنْ نُخْرِجَ اللَّهُ أَصْغَنِيمَ ﴿٧٥﴾ وَلَوْ نَشَاءُ
لَأَرْبِنَنَّكُمْ فَلَعَرَفْتَهُمْ بِسِمَتِهِمْ ۗ وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ أَعْمَالَكُمْ ﴿٧٦﴾
وَلَتَبْلُؤَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ الْمُجَاهِدِينَ مِنْكُمْ وَالصَّابِرِينَ وَتَبْلُؤَ أَخْبَارَكُمْ ﴿٧٧﴾

29. “Je! Wenye maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu Hatazidhihirisha chuki zao?”

30. "Na Tungelipenda Tungelikuonesha hao na ungeliwatambua kwa alama zao, lakini bila ya shaka utawajua kwa namna ya msemo wao. Na Mwenyezi Mungu Anavijua vitendo vyenu."

31. "Na bila ya shaka Tutakujaribuni mpaka Tuwajue wapiganao Jihadi katika nyinyi na wanaosubiri. Nasi Tutazifanyia mtihani habari zenu."

Kufichua Siri Zilizofichika za Wanafiki

Allah تعالى Anasema:

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ أَنْ لَنْ نُخْرِجَ اللَّهُ أَضْغَانَهُمْ ﴿٣٠﴾

"Je! Wenye maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu Hatazidhihirisha chuki zao?"

Maana yake: Je, wanafiki wanadhani kwamba Allah تعالى Hatayafichua mambo yao kwa waja wake Waumini, La hashah! bali Atayaweka wazi na kuyadhihirisha, mpaka wafahamu wenye busara. Allah تعالى Aliiteremsha katika shauri hilo Surat Tawba Akabainisha humo kashfa zao na matendo yao wanayoyaegemea, ambayo yanaonesha unafiki wao.

Kwa sababu hii, *Surat Baraa-a (At-Tawbah)* huitwa pia, *Al-Faadhwihah* (Yenye kuumbua). Neno *Adhwighan*, ni wingi wa *Dhwighn*, ambayo maana yake ni yaliyo katika nafsi kama vile husuda na chuki kwa Uislamu, Waislamu na wanaounusuru.

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَوْ نَشَاءُ لَأَرَيْنَاكَهُمْ فَלَعَرَفْتَهُمْ بِسِيمَاهُمْ ۗ

"Na Tungelipenda Tungelikuonesha hao na ungeliwatambua kwa alama zao..."

Allah تعالى Anasema, "Lau Tungelitaka, ewe Muhammad ﷺ, Tungelikuonesha watu wenyewe khasa, ambao ni wanafiki ili uwajue wazi wazi." Lakini, Allah تعالى Hakufanya hivyo, kwa wanafiki wote, kwa ajili ya kuwasitiri viumbe Wake, na Kuyaacha mambo yaende kwa amani na Kuzirudisha siri kwa Mjuzi wake,

وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ^٤

“...lakini bila ya shaka utawajua kwa namna ya msemu wao.”

Maana yake: Katika maneno yao wanayoyadhihirisha ambayo yanaonesha makusudio yao, utajua kuwa mzungumzaji yuko katika kundi lipi kati ya mawili. Ni kutokana na kauli zake na makosa yake. Ni sawa na alivyosema Amiri wa Waumini, ‘Uthman رضي الله عنه: “Hapana yeyote afichaye siri, isipokuwa Allah تعالى Ataidhihirisha kwenye paji la uso wake na makosa ya ulimi wake.” Kauli ya Allah تعالى:

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ

“Na bila ya shaka Tutakujaribuni...”

Maana yake: Tutakufanyieni mtihani, kwa maamrisha na makatazo,

حَتَّى نَعْلَمَ الْمُجَاهِدِينَ مِنْكُمْ وَالصَّادِقِينَ وَنَبْلُوا أَحْبَابَكُمْ

**“...mpaka Tuwajue wapiganao Jihadi katika nyinyi na wanao subiri.
Nasi Tutazifanyia mtihani habari zenu.”**

Maana yake: Hapana shaka kuwa Ilimu ya Allah تعالى Ilikwishatangulia kabla ya kutukia jambo, kwamba litatukia pasi na shaka ya aina yoyote ile. Makusudio ya “**mpaka Tuwajue.**” ni kutokea kwake. Kwa ajili hii, Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما anasema kuhusu hili: “**Isipokuwa Tuwajue**” maana yake “ili Tuone.”

* * *

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَشَاقُّوا الرَّسُولَ
 مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أُضِلُّوا لَنْ يُضِرُّوا اللَّهَ شَيْئًا
 وَسَيُحِيطُ أَعْمَلُهُمْ ﴿٣٢﴾ * يَتَأَيُّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا
 اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٣﴾ إِنَّ الَّذِينَ
 كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ مَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَنْ
 يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ ﴿٣٤﴾ فَلَا تَهِنُوا وَتَدْعُوا إِلَى السَّلْمِ وَأَنْتُمْ
 الْأَعْلَوْنَ وَاللَّهُ مَعَكُمْ وَلَنْ يَبْرِكُمْ أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٥﴾ إِنَّمَا
 الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَلَهُوَ^٤ وَإِنْ تُؤْمِنُوا وَتَتَّقُوا يُؤْتِكُمْ
 أُجُورَكُمْ وَلَا يَسْأَلْكُمْ أَمْوَالَكُمْ ﴿٣٦﴾ إِنْ يَسْأَلْكُمْوهَا
 فَيُخْفِئْكُمْ تَبَخَّلُوا وَبَخْرَجِ أَصْفَعْتُمْ ﴿٣٧﴾ هَتَأْتُمْ هَتُولًا^٥
 تَدْعُونَ لِتُنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَمِنْكُمْ مَنْ يَبْخُلُ^٦
 وَمَنْ يَبْخُلْ فَإِنَّمَا يَبْخُلْ عَنِ نَفْسِهِ^٧ وَاللَّهُ الْغَنِيُّ وَأَنْتُمْ
 الْفُقَرَاءُ^٨ وَإِن تَتَوَلَّوْا يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا
 أَمْثَلَكُمْ ﴿٣٨﴾

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ
 اللَّهِ وَشَاقُّوا الرَّسُولَ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ
 لَهُمْ أَنَّهُمْ أُضِلُّوا لَنْ يُضِرُّوا اللَّهَ شَيْئًا
 وَسَيُحِيطُ أَعْمَلُهُمْ ﴿٣٢﴾ * يَتَأَيُّبُ
 الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا
 الرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٣﴾
 إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ
 اللَّهِ ثُمَّ مَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَنْ يَغْفِرَ
 اللَّهُ لَهُمْ ﴿٣٤﴾ فَلَا تَهِنُوا وَتَدْعُوا إِلَى
 السَّلْمِ وَأَنْتُمْ الْأَعْلَوْنَ وَاللَّهُ مَعَكُمْ
 وَلَنْ يَبْرِكُمْ أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٥﴾

32. "Kwa hakika walio-
 kufuru na wakazuilia njia ya
 Mwenyezi Mungu na
 wakapinzana na Mtume
 baada ya kuisha wabai-

nikia uwongofu, hao hawatamdhuru Mwenyezi Mungu kwa lolote. Naye Ataviangusha vitendo vyao."

33. "Enyi mlioamini! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu."

34. "Hakika waliokufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakafa na hali ni makafiri, Mwenyezi Mungu Hatawasamehe makosa yao."

35. "Basi msijihisi unyonge na kutaka suluhu, maana nyinyi ndio mtakaoshinda. Na Mwenyezi Mungu Yu pamoja nanyi, wala Hatakunyimeni malipo ya vitendo vyenu."

Kufutwa Amali za Makafiri na Amri ya Kupigana Nao

Allah تعالى Anaeleza kuwa yeyote aliyekufuru, akazuia njia ya Allah تعالى, akamkhalifu Mtume ﷺ na akapambana naye, akaiacha imani baada ya uongofu kumbainikia kwamba hatamdhuru Allah تعالى chochote. Bali ataidhuru nafsi yake mwenyewe na ataitia hasara siku ya marejeo yake.

Allah تعالى Atafuta amali zake, hivyo Hatampa thawabu kwa amali zake zilizotangulia baada ya kuritadi kwake – hata japo kheri yenye uzito wa mbu, bali atazifuta zote, kama ambavyo wema hufuta maovu.

Imamu Ahmad bin Nasr Al-Marwazi amesimulia katika Kitabu *As-Swalaah* (Kitabu cha Sala) kuwa Abu Al-'Aliyah amesema: “Masahaba wa Mtume ﷺ walikuwa wakidhani kuwa hapana dhambi itakayodhuru iwapo mtu ametamka *Laailaha illallah*, kama ambavyo haitanufaisha amali yoyote pamoja na ushirikina.

Ikateremka Aya,

أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ

“Mtiini Mwenyezi Mungu na mt’iini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu.”

Wakawa na khofu kuwa, “madhambi yatabatilisha amali.”¹

Kisha, ikapokewa kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما kuwa alisema: “Sisi, kongamano la Masahaba wa Mtume ﷺ tulikuwa tukidhani kuwa hapana jambo lolote jema bali litakubaliwa, mpaka ilipoteremka Aya,

أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ

“Mt’iini Mwenyezi Mungu na mt’iini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu.”

Tukasema, ‘Ni nini kinachoharibu amali zetu?’ Tukasema: ‘Ni madhambi makubwa ya kutuingiza Motoni na maovu.’ Ikateremka Kauli ya Allah Taala,

¹ *As-Salah* cha Al-Marwazi 2:645.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ^٤

“Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehe kushirikishwa, na Husamehe yaliyo duni ya hilo kwa Amtakaye.” (4:48)

Baada ya kuteremshwa, tukajizua kusema hivyo, na tukawa tunamkhofia mwenye kufanya madhambi makubwa na maovu na kuvutiwa na asiyeyatenda.¹ Kisha, Allah تعالی Aliwaamuru waja wake Waumini kumtii Yeye na kumtii Mjumbe Wake na kwamba hayo ndiyo furaha ya Dunia na Akhera. Akawakataza kuritadi ambako ndiko kwenye kuziharibu amali. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَلَكُمْ

“...wala msiviharibu vitendo vyenu.”

Maana yake: Kwa kuritadi. Akasema baada yake,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ مَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ ﴿٤٨﴾

“Hakika waliokufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakafa na hali ni makafiri, Mwenyezi Mungu Hatawasamehe makosa yao.”

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ^٤

“Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehe kushirikishwa, na Husamehe yaliyo chini ya hilo kwa Amtakaye.” (4:48)

Halafu, Allah تعالی Akasema,

فَلَا تَهِنُوا

“Basi msijihisi unyonge...”

Maana yake: Msiwe dhaifu juu ya maadui,

¹ As-Salah cha Al-Marwazi 2:645.

وَتَدْعُوا إِلَى السَّلْمِ

“...*na kutaka suluhu...*” Maana yake: Maafikiano, kuweka suluhu na kukomesha mapigano baina yenu na makafiri, ilhali mko katika nguvu na wingi wa idadi yenu na maandalizi. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

فَلَا تَهِنُوا وَتَدْعُوا إِلَى السَّلْمِ وَأَنْتُمْ الْأَعْلَوْنَ

“Basi msijihisi unyonge na kutaka suluhu, maana nyinyi ndio mtakaoshinda.”

Maana yake: Katika hali ya kuwa nyinyi mpo juu ya maadui zenu kwa nguvu. Kama makafiri wanakuwa na nguvu zaidi yenu na idadi yao kubwa kuliko Waislamu wote, na kiongozi akaona kuwa maafikiano yana maslahi (kwa Waislamu), basi anaweza kufanya hivyo. Ni kama alivyofanya Mtume ﷺ wakati makafiri wa kikuraishi walipomzuia kuingia Makkah na wakamuomba afanye mkataba wa maafikiano, waache vita baina yao na yeye kwa miaka kumi. Akawakubalia hayo. Kauli ya Allah تعالى:

وَاللَّهُ مَعَكُمْ

“Na Mwenyezi Mungu Yu pamoja nanyi...” Ndani yake kuna bishara kuhusu nusura na ushindi juu ya maadui,

وَلَنْ يَزِيدَكُمْ أَعْمَلَكُمْ

“...wala hatakunyimeni malipo ya amali zenu.”

Maana yake: Hataziharibu, kuzibatilisha, wala kukupokonyeni amali zenu, bali Atakulipeni thawabu Zake, wala Hatapunguza chochote katika hizo. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi,

إِنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَلَهْوٌ وَإِنْ تُؤْمِنُوا وَتَتَّقُوا يُؤْتِكُمْ أَجُورَكُمْ وَلَا يَسْأَلْكُمْ أَمْوَالَكُمْ
 ﴿٦٦﴾ إِنْ يَسْأَلْكُمْوهَا فَيُحْفِكُمْ تَبَخَّلُوا وَخَرَجَ أَصْغَنَكُمْ ﴿٦٧﴾ هَاتَتْهُ هَتُولَاءُ
 تَدْعُونَ لِتُنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَمِنْكُمْ مَنْ يَبْخَلُ وَمَنْ يَبْخَلْ فَإِنَّمَا يَبْخَلْ عَنِ
 نَفْسِهِ ۗ وَاللَّهُ الْغَنِيُّ وَأَنْتُمُ الْفُقَرَاءُ ۗ وَإِن تَتَوَلَّوْا يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا
 أَمْثَلَكُمْ ﴿٦٨﴾

36. "Hakika uhai wa duniani ni mchezo na pumbao. Na mkiamini na mkamuogopa Mwenyezi Mungu Atakupeni ujira wenu, wala Hakutakeni mali yenu."

37. "Na Akikutakeni hayo na Kukushikilieni mtafanya ubakhili, na Atatoa undani wa chuki zenu."

38. "Angalieni! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wapo katika nyinyi wanaofanya ubakhili. Na Anayefanya ubakhili basi Anajifanyia ubakhili mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu Si Mhitaji, na nyinyi ndio wahitaji. Na mkipinga Atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi."

Ubainifu wa udhalili wa Dunia na Uhamasishaji katika Kutoa

Allah تعالى Anazungumzia uhakiri wa mambo ya kidunia na uduni wa shani yake,

إِنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَلَهْوٌ

"Hakika uhai wa duniani ni mchezo na pumbao."

Maana yake: Hayo ndio matokeo yake, isipokuwa kitakachofanywa kwa ajili ya Allah تعالى. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَإِنْ تُوْمِنُوا وَتَتَّقُوا يُؤْتِكُمْ أَجْرَكُمْ وَلَا يَسْأَلْكُمْ أَمْوَالَكُمْ

"Na mkiamini na mkamuogopa Mwenyezi Mungu Atakupeni ujira wenu, wala Hakutakeni mali yenu."

Maana yake: Yeye hana haja kwenu, hana anachotafuta kutoka kwenu, na Amekufaradhisieni Sadaka kutoka katika mali zenu kwa ajili ya kuwasaidia ndugu zenu mafakiri, ili manufaa yake yarudi kwenu na thawabu zake zirejee kwenu. Kisha, Allah تعالى Amesema:

إِنْ يَسْأَلْكُمْوهَا فَيُحْفِكُمْ تَبَخَّلُوا

"Na Akikutakeni hayo na Kukushikilieni mtafanya ubakhili..."

Inamaanisha, ikiwa Atakusihini sana, mngelifanya ubahili,

وَيُخْرِجُ أَضْغَنْتَكُمْ

“...na Atatoa undani wa chuki zenu.”

Qatadah amesema: “Allah تعالى Anajua kwamba katika kutoa mali ni kuondoa chuki.”¹ Hakika, Qatadah alisema kweli pale aliposema: ‘Mali ni yenye kupendwa, wala (mtu) haitumii isipokuwa kwa kile anachokipenda zaidi mtu huyo kuliko mali.’ Kauli ya Allah تعالى:

هَاتَتْهُمْ هَتُؤَلَاءِ تَدْعُونَ لِنُفُوقِ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَمِنْكُمْ مَنْ يَبْخُلُ

“Angalieni! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wapo katika nyinyi wanao fanya ubakhili.”

Inamaanisha, hawayakubali hayo,

وَمَنْ يَبْخُلْ فَإِنَّمَا يَبْخُلُ عَنِ نَفْسِهِ

“Na anayefanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe.”

Maana yake: Yeye mwenyewe huyapunguza malipo yake, na athari yake mbaya inamrudia yeye.

وَاللَّهُ الْغَنِيُّ

“Na Mwenyezi Mungu Si Mhitaji...”

Wa chochote ghairi yake, na kila kitu ni chenye kumhitajia Yeye daima. Kwa minajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَأَنْتُمْ الْفُقَرَاءُ

“...na nyinyi ndio wahitaji.”

Kwake Yeye khasa, basi wasifu Wake kwamba ni ‘Al-Ghaniy’ Mwenye Kujitosheleza kwa kila kisichokuwa Yeye, na kila kitu kinahitajia Kwake.

Kauli ya Allah تعالى:

وَإِن تَتَوَلَّوْا

“Na mkipinga...” Dhidi ya kumtii na kufuata Shariah Yake,

¹Abdur-Razzaq 3:224.

يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَلَكُمْ

“...Atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi.”

Maana yake: Watakuwa wasikivu, wenye kutii amri Zake.

Mwisho wa tafsiri ya *Suratu Al-Muhammad*, Hamdi na shukrani zinamstahiki Allah تعالى.

* * *

Tafsiri ya Suratul Fat'h Sura ya 48 Iliteremshwa Madinah

Fadhila za *Suratu Al-Fat'h*

Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa 'Abdullah bin Mughaffal رضي الله عنه kuwa alisema: "Mtume ﷺ alisoma *Suratul-Fat'h* akiwa amepanda ngamia katika safari yake ya kuikomboa Makkah, akawa anairudiarudia kuisoma. Mu'awiyah رضي الله عنه akasema: "Kama si kuchelea watu kunikusanyikia, ningefuatishia usomaji wake."

* * *

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

سُورَةُ الْفَاتِحَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُبِينًا ﴿١﴾ لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ
 مِن ذُنُوبِكُمْ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ
 صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٢﴾ وَيَنْصُرَكَ اللَّهُ نَصْرًا عَظِيمًا ﴿٣﴾
 أَنْزَلَ السَّكِينَةَ فِي قُلُوبِ الْمُؤْمِنِينَ لِيَزْدَادُوا إِيمَانًا مَعَ
 إِيمَانِهِمْ ۗ وَاللَّهُ جُنُودَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا
 حَكِيمًا ﴿٤﴾ لِيُدْخِلَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي
 مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَيُكَفِّرُ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ ۗ
 وَكَانَ ذَلِكَ عِنْدَ اللَّهِ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٥﴾ وَيُعَذِّبُ
 الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْمُشْرِكِينَ وَالْمُشْرِكَاتِ الظَّالِمِينَ
 بِاللَّهِ ظُلْمًا أَلْسِنَهُمْ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ ۗ وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ
 وَلَعَنَهُمْ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَهَنَّمَ ۗ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٦﴾ وَاللَّهُ
 جُنُودَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيمًا حَكِيمًا ﴿٧﴾

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُبِينًا ﴿١﴾
 لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذُنُوبِكُمْ
 وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ
 وَيَهْدِيَكَ صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٢﴾
 وَيَنْصُرَكَ اللَّهُ نَصْرًا عَظِيمًا ﴿٣﴾

1. "Hakika Tumekufungulia Ushindi wa dhaahiri."

2. "Ili Mwenyezi Mungu Akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo, na Akutimizie neema Zake, na Akuongoe katika Njia Iliyonyooka,"

3. "Na Mwenyezi Mungu Akunusuru nusura yenye nguvu."

Sababu ya Kushuka Aya Hii

Sura hii tukufu iliteremka wakati Mtume ﷺ aliporejea

kutoka Hudaybiyyah, katika mwezi wa Dhul-qa'dah, mwaka wa sita baada ya Hijrah, wakati washirikina walipomzuia kufika Al-Masjid Al-Haraam, kwa ajili ya kutekeleza ibada yake ya 'Umrah aliyoikusudia kuifanya ndani yake. Wakamzuia kufika Makkah, wakaelekea katika kutaka suluhu na mwafaka, na kwamba, mwaka huu warejee na waje mwaka uliofuata. Akawakubalia hayo,

licha ya Masahaba wengi kutokuyapenda hayo. Miongoni mwao ni ‘Umar bin al-Khattaab رضي الله عنه, kama itakavyoelezwa katika mahala pake katika tafsiri ya Sura hii, Inshaa Allah. Baada ya Mtume ﷺ kuchinja wanyama wake wa dhabihu mahali hapo walipozuiliwa, akarejea, Allah تعالى Aliiteremsha Sura hii kuelezea jambo lake na wao lilivyokuwa, na Akaijaalia suluhu ile kuwa ni ushindi kwa kuyazingatia masilahi na matokeo yake. Kama alivyosimulia Ibn Mas’ud رضي الله عنه na wengine, kwamba alisema: “Nyinyi mnachukulia kuwa kuifungua Makkah ndio ushindi, nasi tunachukulia kwamba ushindi ni mkataba wa Hudaybiyyah.”¹ Bukhari alinukuu kutoka kwa Baraa alisema kuwa, nyinyi mnachukulia *Fat-h* kuikomboa Makkah ndio ushindi, naam, hiyo ilikuwa *Fat-h* kuikomboa Makkah, sisi tunachukulia kwamba ushindi ni baina ya *Ar-Ridhwaan* uungaji mkono katika siku ya Hudaybiyyah. Tulikuwa watu mia nne, pamoja na Mtume ﷺ. Huko Hudaybiyyah kulikuwa na kisima, tukanywa maji yake, na hatukuacha hata tone moja ndani yake. Hayo yakamfikia Mjumbe wa Allah, akatujia na kukaa katika ukingo wake akaomba aletewe chombo cha maji. Akatawadha, akasukutua, akaomba dua, akayamimina kisimani. Tukakiacha kwa muda mfupi, halafu kikatupatia maji kiasi cha kututosha sisi na wanyama wetu.²

Imamu Ahmad alimnukuu ‘Umar رضي الله عنه kuwa alisema: “Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ safarini. Nikamuuliza kuhusu jambo fulani, mara tatu, bila ya kunijibu. Basi nikajisemea katika nafsi yangu, “Umeshapata hasara, ewe Ibn Al-Khattaab! Umemuita Mtume ﷺ mara tatu wala hakukujibu?” Nikapanda juu ya mnyama wangu, nikasonga mbele na farasi wangu kwa kukhofia kuteremshwa Aya kunihusu mimi. Nikamsikia mlinganiaji akiita, “Ewe ‘Umar!” Nikarejea huku nikidhani kuwa imeshateremka Aya kunihusu. Mtume ﷺ akasema:

«نَزَلَ عَلَيَّ الْبَارِحَةَ سُورَةٌ هِيَ أَحَبُّ إِلَيَّ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا فِيهَا: ﴿إِنَّا مَعَنَا لَكَ نَتَانَا
 مُبِينًا﴾ لِيَتَغَيَّرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ»

“Jana niliteremshiwa Sura ambayo ninaipenda kuliko dunia nzima na vilivyomo: **“*Hakika Tumekufungulia Ushindi wa dhaahiri. Ili Mwenyezi Mungu Akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo...*”**³

¹ At-Tabari 22:201.

² *Fat’h Al-Bari* 7:505.

³ Ahmad 1:31.

Aliinukuu Bukhari, Tirmidhi na Nasai kupitia njia nyingi kutoka kwa Malik, Allah تعالى Amrehemu.¹ 'Ali bin Al-Madini alitoa rai, "Hii ni isnadi nzuri ya Madinah ambayo hatuipati isipokuwa kutoka kwa Maulamaa wa Madinah." Imamu Ahmad alimnukuu Anas bin Malik رضي الله عنه ambaye alisema: "Iliteremshwa kwa Mtume ﷺ:

لَيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ

"Ili Mwenyezi Mungu Akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo..."

Wakati akirejea kutoka Hodaybiyyah. Mtume ﷺ amesema:

«لَقَدْ أَنْزِلْتُ عَلَيَّ اللَّيْلَةَ آيَةً أَحَبُّ إِلَيَّ مِمَّا عَلَى الْأَرْضِ»

"Usiku wa leo, nimeteremshiwa Aya ninayoipenda kuliko vyote vya ardhini."

Mtume ﷺ akawasomea, na wakasema: "Hongera, ewe Mtume ﷺ! Allah تعالى Amebainisha Atakachokufanyia, sisi je, Atatufanyia nini?" Ikamteremka Aya,

لَيَدْخُلَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

"Ili Awaingize Waumini wanaume na Waumini wanawake katika Bustani zipitazo mito kati yake,..." Mpaka,

فَوْزًا عَظِيمًا

"...kufuzu kukubwa..."² Hadithi hii imenukuliwa katika Sahih Mbili.³ Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Al-Mughirah bin Shu'bah رضي الله عنه, ambaye alisema: "Mtume ﷺ alikuwa akisali, mpaka miguu yake yote miwili ikivimba. Akaulizwa, "Kwani Allah تعالى Hakukughufiria dhambi zako zilizopita na za wakati ujao?" Akajibu:

«أَفَلَا أَكُونُ عَبْدًا شَكُورًا؟»

"Kwa nini nisiwe mja mwenye shukurani?"⁴ Sahih Mbili na wokusanyaji wengine wa Hadithi wameiandika, isipokuwa Abu Dawud.⁵ Kauli ya Allah تعالى:

¹ Fat'h Al-Bari 8:675, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:167, An-Nasai katika Al-Kubra 6:461

² Ahmad 3:197

³ Fat'h Al-Bari 7:516, Muslim 3:1413

⁴ Ahmad 4:55

⁵ Al-Bukhari na. 4836, Muslim na. 2819, At-Tirmidhi na. 412, An-Nasai 3:219 na Ibn Majah na. 1419

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿١٠٠﴾

“Hakika Tumekufungulia Ushindi wa dhahiri.”

Maana yake: Bayana na dhahiri. Makusudio yake ni mkataba wa Hudaybiyyah, kwani umesababisha kupatikana kwa kheri tele, watu wakaamini, wakaweza kukutana wao kwao. Na Muumini akaweza kuzungumza na kafiri. Elimu ya manufaa ikaenea pamoja na Imani. Kauli ya Allah تعالى:

لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ

“Ili Mwenyezi Mungu Akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo...”

Haya ni katika mambo yanayomuhusu Mtume ﷺ tu, hayamshirikishi mwingine, wala hakuna katika Hadithi Sahih kwamba kuna mtu mwingine ameghufiriwa madhambi yake yaliyotangulia na ya baadaye. Hii ni Hadhi na Utukufu mkubwa kwa Mtume ﷺ ambaye katika mambo yake yote yuko katika twaa, wema na msimamo ambao hakuwa nao mwanaadamu yeyote isipokuwa yeye tu. Si hao wa awali wala wa nyuma yake. Mtume ﷺ ndiye mwanaadamu mkamilifu zaidi, tena ni kiongozi wao duniani na Akhera. Kwa kuwa ndiye mtiifu zaidi katika viumbe wa Allah تعالى, na ndiye anayeheshimu sana Amri na makatazo ya Allah تعالى. Alisema pindi ngamia wake aliposhikilia kupiga magoti,

«حَبَسَهَا حَاسِبُ الْفِيلِ»

“Amemzuia mzuiaji wa Tembo.”

Kisha, Mtume ﷺ amesema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَا يَسْأَلُونِي النَّوْمَ شَيْئًا يُعْظَمُونَ بِهِ حُرْمَاتِ اللَّهِ إِلَّا أَجَبْتُهُمْ إِلَيْهَا»

“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Ikiwa wataniomba kitu watakachokitumia kuheshimu matukufu ya Allah, nitawapa.”¹

Mtume ﷺ alipomtii Allah تعالى katika hilo na kukubali kufanya mkataba wa muafaka, Allah تعالى Alisema:

¹ Fat'h Al-Bari 5:388.

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿١﴾ لِيُغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ
نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ

“Hakika Tumekufungulia Ushindi wa dhaahiri. Ili Mwenyezi Mungu Akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo, na Akutimizie Neema Zake juu yako...” (48:1-2)

Maana yake: Duniani na Akhera,

وَيَهْدِيكَ صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٢﴾

“...na Akuongoe katika Njia Iliyonyooka,”

Maana yake: Kwa Shariah tukufu na Dini iliyonyooka, Anayokufaradhishia,

وَيَنْصُرَكَ اللَّهُ نَصْرًا عَظِيمًا ﴿٣﴾

“Na Mwenyezi Mungu Akunusuru nusura yenye nguvu.”

Inamaanisha, kwa sababu ya unyenyekevu wako kwa amri za Allah تعالیٰ, Atakunyanyua na Kukupa ushindi juu ya maadui zako.

Ni sawa na ilivyo katika Hadithi Sahih:

«وَمَا زَادَ اللَّهُ عَبْدًا بِعَفْوٍ إِلَّا عِزًّا. وَمَا تَوَاضَعَ أَحَدٌ لِلَّهِ إِلَّا رَفَعَهُ اللَّهُ تَعَالَى»

“Allah hajamzujisha mja yoyote kwa msamaha, isipokuwa humpa utukufu. Wala hajanyenyekea yeyote kwa Allah Taala ila Allah humnyanyua (daraja).”¹

‘Umar bin Al-Khattwaab رضي الله عنه amesema: “Hutaweza kumuadhibu yeyote anayemuasi Allah تعالیٰ, kwa mithili ya wewe unavyomtii Allah تعالیٰ.”

¹ Muslim 2001.

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ السَّكِينَةَ فِي قُلُوبِ الْمُؤْمِنِينَ لِيَزْدَادُوا إِيمَانًا مَعَ إِيْمَانِهِمْ ۗ وَلِلَّهِ جُنُودُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٤٨﴾ لِيُدْخِلَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَيُكَفِّرُ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ ۗ وَكَانَ ذَلِكَ عِنْدَ اللَّهِ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٤٩﴾ وَيُعَذِّبُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْمُشْرِكِينَ وَالْمُشْرِكَاتِ الظَّالِمِينَ ۗ بِاللَّهِ ظَنِّ السَّوءِ ۗ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوءِ ۗ وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَلَعَنَهُمْ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَهَنَّمَ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٥٠﴾ وَلِلَّهِ جُنُودُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٥١﴾

4. *“Yeye Ndiye Aliyeteremsha utulivu katika nyoyo za Waumini ili wazidi Imani juu ya Imani yao. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Ujuzi, Mwenye Hikima.”*

5. *“Ili Awaingize Waumini wanaume na Waumini wanawake katika Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo, na Awafutie makosa yao. Na huko ndiko kufuzu kukubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.”*

6. *“Na Awape adhabu wanaafiki wanaume na wanaafiki wanawake, na washirikina wanaume na washirikina wanawake, wanaomdhanja Mwenyezi Mungu dhana mbaya. Utawafikia mgeuko mbaya, na Mwenyezi Mungu Awakasirikie, na Awalaani, na Awaandalie Jahannamu. Na hayo ni marudio maovu kabisa.”*

7. *“Na Mwenyezi Mungu Ana majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”*

Allah تعالیٰ Aliteremsha na Kujaalia Utulivu katika Nyoyo za Waumini

Allah تعالیٰ Amesema:

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ السَّكِينَةَ

“Yeye Ndiye Aliyeteremsha utulivu...”

Maana yake: Amejaalia utulivu. Qatadah alisema: “Ni rehema nyoyoni mwa Waumini”, hao ni Masahaba, Allah تعالیٰ Awe radhi nao. Katika siku ya

Hudaybiyyah walipokea wito wa Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ na wakafuata amri ya Allah تعالى na Mjumbe Wake. Nyoyo zao zilipopata matumaini kwa hilo na kutulia, imani ilizidi mara dufu juu ya waliyokuwa nayo. Bukhari na maimamu wengine, waliitumia Aya hii kuonesha kuwa imani huongezeka na kupungua nyoyoni.

Kisha, Allah تعالى Alitaja kuwa Angelitaka Waislamu wangeliwashinda makafiri. Allah تعالى Amesema:

وَاللَّهُ جُنُودُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ^٤

“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye majeshi ya mbingu na ardhi.”

Maana yake: Lau kama Angewapelekea Malaika mmoja juu yao angeangamiza uoto wao mzuri wa rangi ya kijani, lakini Allah تعالى Aliwapa Shariah ya jihadi na vita waja wake waumini, kutokana na Hikima Yake kubwa, hoja zisizopingika, na ushahidi wa wazi. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Ujuzi, Mwenye Hikima.”

Kisha, Allah تعالى Amesema,

لِيَدْخُلَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا

“Ili Awaingize Waumini wanaume na Waumini wanawake katika Bustani zipitazo mito kati yake....”

Hadithi ya Anasi رضي الله عنه imekwishatangulia, pindi Masahaba waliposema: “Hongera zako, ewe Mjumbe wa Allah ﷺ! Haya ni kwa ajili yako, vipi kuhusu sisi?”

Allah تعالى Akateremsha Aya ifuatayo:

لِيَدْخُلَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا

“Ili Awaingize Waumini wanaume na Waumini wanawake katika Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo...”¹

¹ Fat'h Al-Bari 7:516.

Maana yake: Watakaa humo milele.

وَيُكَفِّرُ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ^٤

“...na awafutie makosa yao.”

Maana yake: Makosa na madhambi yao. Hatawaadhibu juu ya hayo, bali Allah تعالى Ataacha, Atasamehe, Atasitiri, Atarehemu na Kuthamini.

وَكَانَ ذَلِكَ عِنْدَ اللَّهِ فَوْزًا عَظِيمًا

“Na huko ndiko kufuzu kukubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَمَنْ زُحِرَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ^٥

“Na atakayeepushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu.” (3:185)

Allah تعالى Amesema:

وَيُعَذِّبُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْمُشْرِكِينَ وَالْمُشْرِكَاتِ الظَّالِمِينَ بِاللَّهِ ظُلْمًا سَوِيًّا^٤

“Na Awape adhabu wanafiki wanaume na wanafiki wanawake, na washirikina wanaume na washirikina wanawake, wanaomdhania Mwenyezi Mungu dhana mbaya.”

Wanamtuhumu Allah تعالى katika Hukumu Yake na kumdhania vibaya Mtume ﷺ na Sahaba zake رضي الله عنهم. Allah تعالى Awaangamize na wamalizike kabisa. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

عَلَيْهِمْ دَابِرَةُ السَّوْءِ^٥ وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَلَعَنَهُمْ

“Utawafikia mgeuko mbaya, na Mwenyezi Mungu Awakasirikie, na Awalaani...”

Maana yake: Awaweke mbali na Rehema Zake.

وَأَعَدَّ لَهُمْ جَهَنَّمَ^٥ وَسَاءَتْ مَصِيرًا

“...na Awaandalie Jahannamu. Na hayo ni marudio maovu kabisa.”

Halafu, Akisisitizia Uwezo Wake wa Kuwalipizia kisasi maadui wa Uislamu, miongoni mwa washirikina na wanafiki, Allah تعالى Alisema:

وَاللَّهُ جُنُودُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

“Na Mwenyezi Mungu Ana majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

* * *

إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَهِيدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿١٥﴾ لِيُتُومِنُوا بِاللَّهِ
 وَرَسُولِهِ وَيُؤَدُّوا لَهُ الْوُفَىٰ وَيُقَرِّبُوا الْقُرْبَىٰ وَيَنْفِرُوا فِي أَدْبَارِ
 الْأَعْرَابِ يَوْمَ تُبَايَعُونَ أَنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ
 أَيْدِيهِمْ ۖ فَمَن نَّكَثَ فَإِنَّمَا يَنكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۗ وَمَن أَوْفَىٰ
 بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهِ اللَّهُ فَسَيُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٦﴾ سَيَقُولُ
 لَكَ الْمُخَلَّفُونَ مِنَ الْأَعْرَابِ شَغَلَتْنَا أَمْوَالُنَا وَأَهْلُونَا
 فَاسْتَغْفِرْ لَنَا ۖ يَقُولُونَ بِالَّذِينَ نَحْنُ فِي قُلُوبِهِمْ ۗ قُلْ
 فَمَن يَمْلِكُ لَكُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ بِكُمْ ضَرًّا أَوْ
 أَرَادَ بِكُمْ نَفْعًا ۗ بَلْ كَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١٧﴾ بَلْ
 ظَنَنْتُمْ أَن لَّن يَنْقَلِبَ الرَّسُولُ وَالْمُؤْمِنُونَ إِلَىٰ أَهْلِيهِمْ أَبَدًا
 وَزَيَّنَّ ذَٰلِكَ فِي قُلُوبِكُمْ ۖ وَظَنَنْتُمْ ظَنًّا سَئِيئًا
 وَكُنْتُمْ قَوْمًا بُورًا ﴿١٨﴾ وَمَن لَّمْ يُؤْمِنْ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ
 فَإِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَعِيرًا ﴿١٩﴾ وَ لِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ
 وَالْأَرْضِ ۖ يَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ ۗ وَكَانَ
 اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٢٠﴾ سَيَقُولُ الْمُخَلَّفُونَ إِذَا
 انطَلَقْتُمْ إِلَىٰ مِغَاذٍ لِّتَأْخُذُوا ذُرُوعًا ۖ نَتَّبِعْكُمْ ۗ
 يُرِيدُونَ أَن يُبَدِّلُوا كَلِمَةَ اللَّهِ ۗ قُلْ لَن نَّتَّبِعُونَ
 كَذٰلِكُمْ قَالِ اللَّهُ مِّن قَبْلِ ۗ فَسَيَقُولُونَ بَلْ نَحْسُدُونَكَ
 بَلْ كَانُوا لَا يَفْقَهُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢١﴾

إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَهِيدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا
 ﴿١٥﴾ لِيُتُومِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَيُؤَدُّوا
 لَهُ الْوُفَىٰ وَيُقَرِّبُوا الْقُرْبَىٰ وَيَنْفِرُوا فِي
 أَدْبَارِ الْأَعْرَابِ يَوْمَ تُبَايَعُونَ أَنَّمَا
 يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ ۖ
 فَمَن نَّكَثَ فَإِنَّمَا يَنكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۗ
 وَمَن أَوْفَىٰ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهِ اللَّهُ ۗ
 فَسَيُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٦﴾

8. "Hakika Tumekutuma wewe uwe Shahidi, na Mtoaji wa habari za kheri, na Muonyaji wa habari za shari."

9. "Ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mumsaidie, na Mumhishimu, na Mumtakase asubuhi na jioni."

10. "Bila ya shaka wanao fungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu Uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi hizi anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na anayetekeleza aliyomuahidi Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Atamlipa ujira mkubwa."

Sifa za Mtume ﷺ

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ, Muhammad ﷺ,

إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَهِيدًا

“Hakika Tumekutuma wewe uwe Shahidi...”

Kwa viumbe,

وَمُبَشِّرًا

“...na Mbashiri...”

Kwa Waumini,

وَنَذِيرًا

“...na Mwonyaji,”

Kwa makafiri. Tumeshazielezea maana ya maneno haya katika tafsiri ya *Surat Al-Ahzaab*.¹

لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُعَزِّرُوهُ

“Ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mumsaidie...”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na wengine kadha walisema, “Mumtukuze.”¹

وَتُؤَيِّرُوهُ

“...na Mumhishimu...”

Maana ya *Tawqiyir* ni kuheshimu, kutukuza, kuadhimisha,

وَتُسَيِّحُوهُ

“...na Mumtakase...”

Maana yake: Mumtukuze Allah تعالى.

بُكَرَةً وَأَصِيلًا

“...asubuhi na jioni.” Maana yake: Mwanzo wa mchana na mwisho wake.

¹ Angalia juzuu ya saba, Tafsiri ya *Surat Al-Ahzaab*.

Uungaji Mkono (*Bai'h*) wa Arridhwaani

Kisha, Allah تعالى Alimuambia Mjumbe Wake kwa kumtukuza, kumheshimu na kumuadhimisha,

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ

“Bila ya shaka wanao fungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

مَنْ يُطِيعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ

“Mwenye kumt’ii Mtume basi ndio amemt’ii Mwenyezi Mungu.”
(4:80)

Kauli ya Allah تعالى,

يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ

“Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao.”

Maana yake: Yuko pamoja nao, Anasikia kauli zao na Anaona mahala pao, Anajua dhamiri zao na dhahiri zao. Kwa hivyo, Allah تعالى Ndiye Aliyekuwa Akipokea uungaji mkono wao “*bai’ah* yao” kupitia kwa Mjumbe Wake.

إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنْفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنْ لَّهُمُ الْجَنَّةَ يُفْتَلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبْشِرُوا بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu - wanaua na wanauawa. Hii ni ahadi Aliyojilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur’ani. Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa

¹ At-Tabari 22:207.

biashara yenu mliyofanya Naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.”
(9:111)

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهِ اللَّهُ فَمِئُتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا

“...na anayetekeleza Aliyomuahidi Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Atamlipa ujira mkubwa.”

Maana yake: Thawabu nyingi. Uungaji mkono huu ni (*Bai'ah*) *Baitu Ridhwaan* na ilifanyika chini ya mti, Samurah, katika eneo la Hudaybiyah. Na Masahaba, Allah تعالى Awe radhi nao, siku hiyo ndio waliomsapoti Mtume ﷺ, husemwa kwamba idadi yao ilikuwa elfu moja na mia tatu, ilitajwa pia kuwa ni elfu moja na mia nne, na ilisemwa tena, ilikuwa elfu moja na mia tano. Ya kati ndiyo sahihi zaidi.

Kutaja Hadithi Zinazosimulia Suala la ‘*Bai'ah*’ Uungaji Mkono wa Mkataba wa Hudaybiyah

Bukhari alinukuu kutoka kwa Jabir رضي الله عنه، kuwa alisema: “Katika siku ya Hudaybiyah, tulikuwa watu elfu moja na mia nne.”¹ Pia, Muslim ameipokea Hadithi hii.² Aidha Bukhari na Muslim wamepokea kutoka kwa Jabir رضي الله عنه kuwa, “Siku hiyo tulikuwa watu elfu moja na mia nne, Mtume ﷺ aliweka mkono wake katika maji yale, yakawa yanabubujika kutoka vidoleni mwake mpaka kila mmoja akakata kiu yake.”³ Huu ni mukhtasari wa hadithi nyingine. Wakati iliposimuliwa kiu yao katika siku ya Hudaybiyah, maji yalimiminika mpaka yakawatosheleza wote. Jabir رضي الله عنه akaambiwa, “Siku hiyo mlikuwa wangapi?” Akasema: “Tulikuwa elfu moja na mia nne, na hata kama tungekuwa laki moja, yangetutosha sote.”⁴ Katika maelezo mengine, Walikuwa elfu moja na mia tano kwa wakati huo.⁵

Bukhari aliandika pia, kutokana na maelezo ya Qatadah, “Nilimuuliza Sa'id bin Musayyib, ‘Ni watu wangapi walioshiriki katika *Bai'ah*, uungaji mkono wa

¹ *Fat'h Al-Bari* 8:451.

² Muslim 3:1484.

³ *Fat'h Al-Bari* 7:505 na Muslim 3:1484.

⁴ *Fat'h Al-Bari* 7:504.

⁵ *Fat'h Al-Bari* 7:507 na Muslim 1484.

Ridhwaan?" Akajibu: 'Elfu moja na mia tano.' Nikasema: "Jabir رضي الله عنه alisema, walikuwa elfu moja mia nne." Sa'id akasema: "Alisahau, aliniambia mimi kuwa walikuwa Elfu moja na mia tano."¹ Bayhaqi alisema: "Masimulizi haya yanajulisha kwamba zamani walikuwa wakisema Elfu moja na mia tano. Kisha ikakumbukwa idadi sahihi kwamba walikuwa elfu moja mia nne."²

Kutaja Sababu za *Bai'ah* Uungaji mkono huu Mkubwa

Muhammad bin Is-haq bin Yasaar رحمه الله تعالى aliandika katika kitabu chake, *As-Siyrah*: "Mtume ﷺ akamuita 'Umar bin Al-Khattwaab رضي الله عنه ili amtume kwenda Makkah, kuwafikishia wakuu wa Kikuraishi, kuhusu aliyoyajia. Akasema: 'Ewe Mtume! Ninawakhofu Makuraishi juu ya nafsi yangu, wala huko Makkah hakuna mkuu yeyote katika Banu 'Adi bin Ka'b atakayenizuia, na Makuraishi wanaufahamu uadui na ukali wangu kwao. Hata hivyo, ninakujulisha mtu mwenye nguvu kwao kuliko mimi, ni 'Uthman bin 'Affaan رضي الله عنه. Tumtume kwenda kwa Abu Sufyaan na wakuu wa Kikuraishi kuwajulisha kwamba, hukuja kivita, bali kuizuru Nyumba na kuitukuza. 'Uthmaan رضي الله عنه akaelekea Makkah. Njiani alikutana na Abaan bin Sa'id bin Al-'As alipokuwa akiingia Makkah au kabla kidogo. Akamchukua na kumhifadhi ili afikishe habari ya Mtume ﷺ. 'Uthman akaenda mpaka kwa Abu Sufyaan na wakuu wa Kikuraishi. Akafikisha ujumbe aliotumwa na Mtume ﷺ. Baada ya 'Uthman رضي الله عنه kuufikisha ujumbe wa Mtume ﷺ, walimuambia: 'Ukitaka kufanya *Twawaf* katika Nyumba, basi fanya.' Akawajibu: 'Sitafanya hivyo, mpaka Mtume ﷺ afanye hivyo.' Wakamzuia Makkah kwa hilo. Habari zikamfikia Mtume ﷺ na Waislamu kuwa 'Uthman رضي الله عنه kauawa." Ibn Is-haq رحمه الله تعالى anaendelea kueleza: 'Abdullah bin Abubakr رضي الله عنه alinisimulia kwamba baada ya habari kwamba 'Uthman رضي الله عنه kauawa, Mtume ﷺ alisema,

«لَا تَبْرُحُ حَتَّى نَتَاجَزَ الْقَوْمَ»

"Hatutaondoka, mpaka tuwapige watu hawa."³

¹ *Fat'h Al-Bari* 7:507.

² *Dalail An-Nubuwwah* 4:97.

³ Ibn Hisham 3:329-330. Sehemu hii ya usimulizi si sahihi lakini maana ya ujumla ipo katika rejea inayofuata.

Ibn Is-haq رحمه الله تعالى aliendelea, Mtume ﷺ akawaita watu wamuunge mkono, hivyo basi ndio ikapatikana "*Bai'ah Ridhwani*" uungaji mkono wa Ridhwani, ilifanyika chini ya mti. Watu wakawa wanasema, "Mtume ﷺ alikubaliana nao kupigana hadi kufa." Jabir bin 'Abdullah رضي الله عنه akawa anasema: "Mtume ﷺ hakusema tupambane hadi kufa, bali tulimbai kwamba tusikimbie vita."¹ Watu wakamsapoti, wala hakuna Muislamu yeyote aliyekuwepo ambaye alibaki nyuma, isipokuwa Jadd bin Qays, kaka yake Abu Salamah. Baadaye, Jabir رضي الله عنه alikuwa akisema: "Wallah! Hivi sasa, najihisi kama vile namuona akiwa karibu kabisa na bega la ngamia wake, akijificha nyuma yake dhidi ya watu. Halafu ikamfikia Mtume ﷺ kwamba habari ya kifo cha 'Uthman haikuwa ya kweli."²

Al-Hafidh Abuu Bakri رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Anasi bin Malik رضي الله عنه amesema; "Mtume ﷺ pindi alipoamrisha kupata uungwaji mkono wa pamoja. Uthman bin Affan رضي الله عنه alikuwa ni mwakilishi wa Mtume ﷺ, kwa watu wa Makka. Hivyo basi watu wakamuunga mkono Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akasema; "Ewe Mola Wangu hakika Uthman yupo katika kufuatilia jambo la Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ." Hivyo basi Mtume ﷺ akakamata mkono mmoja wa Uthman juu ya mwingine. Ikawa kushikana mikono, Mtume ﷺ na Uthman ni bora kuliko mikono ya Masahaba wengine wanaoshikana wao kwa wao.

Bukhari alisema kuwa Nafi' alieleza, "Watu wanazungumza kwamba Ibn 'Umar رضي الله عنه alisilimu kabla ya 'Umar رضي الله عنه, ilhali sivyo. Lakini, katika siku ya Hodaybiyyah, 'Umar رضي الله عنه alimtuma 'Abdullah رضي الله عنه kwenda kumchukua farasi kutoka kwa mtu mmoja wa kiansari, ili amtumie katika mapigano. Wakati huo, Mtume ﷺ alikuwa chini ya mti akipokea uungwaji mkono - *bai'ah*, huku 'Umar رضي الله عنه akiwa hajalijua hilo. Kwa hivyo, 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنه akamuunga mkono Mtume ﷺ, akamfuata farasi, na akamletea 'Umar رضي الله عنه ambaye alikuwa akijiandaa kwa ajili ya vita. 'Abdullah رضي الله عنه akamjulisha 'Umar رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ anapokea uungwaji mkono chini ya mti. Akaenda pamoja naye, na akamuunga mkono. Hiyo ndiyo sababu iliyowafanya watu waseme kwamba 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما alisilimu kabla ya 'Umar رضي الله عنه."³

¹ Angalia rejea ya Muslim itakayofuata

² Ibn Hisham 3:329-330.

³ *Fat'h Al-Bari* 7:521.

Tena, Bukhari aliandika kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa alisema: "Watu waliokuwa pamoja na Mtume ﷺ walikuwa wamesambaa katika vivuli vya miti. Ghafila, watu wakakusanyika kumzunguka Mtume ﷺ, 'Umar رضي الله عنه akasema, 'Ewe 'Abdullah! Angalia, kwanini watu wamemzunguka Mtume ﷺ." Akawakuta wakimsapoti, na yeye akafanya hivyo. Akarejea kwa 'Umar رضي الله عنه, na yeye akaenda kumsapoti."¹

Jabir رضي الله عنه alisema: "Siku ya Hudaybiyyah, tulikuwa watu elfu moja na mia nne. Tukamuunga mkono Mtume ﷺ, huku 'Umar رضي الله عنه akiwa ameshika mkono wa Mtume ﷺ chini ya mti, ambao ulikuwa Samurah (namna ya mti wenye miba). Tulimsapoti kwamba tusikimbie, wala hatukufanya hivyo juu ya kufa." Aliandika Muslim.² Muslim alimnukuu Ma'qil bin Yasaar رضي الله عنه kuwa alisema: "Katika siku ya Mti, wakati Mtume ﷺ akipokea uungwaji mkono na watu, mimi nilikuwa nimelinyanyua tawi mojawapo la mti huo mbali na kichwa chake. Tulikuwa watu elfu moja na mia nne. Wala hatukula kiapo juu ya kufa, bali kutokimbia."³ Bukhari aliandika kutoka kwa Salamah bin Ak-wa' رضي الله عنه kuwa alisema: "Mlikula kiapo kwa Mtume ﷺ chini ya mti." Yazid aliuliza: "Wakati huo mlikuwa mkimuunga mkono juu ya jambo gani?" Akajibu: "Juu ya mauti."⁴ Bukhari aliandika tena: Salah alinena: "Siku ya Hudaybiyyah, nilikula kiapo kwa Mtume ﷺ, halafu nikasimama pembeni. Mtume ﷺ akasema:

«يَا سَلْمَةُ أَلَا تَتَّبِعُ؟»

"Ewe Salamah! Kwanini hutaki kuchukua ahadi pamoja nami?"

Nikamjibu, 'Tayari nimeshafanya hivyo.' Mtume ﷺ akasema:

«أَتَبِلُ تَبَايِعُ؟»

"Njoo ule kiapo." Nikamsogelea na nikachukua ahadi kwake." Nikauliza: "Mlichukua ahadi juu ya jambo gani ee Salamah?" Akajibu: "Juu ya mauti."⁵ Pia, Muslim aliinukuu Hadithi hii,⁶ ambapo Bukhari aliihusanya kutoka kwa 'Abbad bin Tamim kwamba ahadi waliyoitoa ilikuwa juu ya mauti.⁷

¹ Fat'h Al-Bari 7:521.

² Muslim 3:1483.

³ Muslim 3:1485.

⁴ Fat'h Al-Bari 6:136.

⁵ Fat'h Al-Bari 13:211.

⁶ Muslim 3:1486.

⁷ Fat'h Al-Bari 6:136.

Bayhaqi aliandika kutoka kwa Salamah bin Akwa'a رضي الله عنه kuwa alisema: Tuliwasili Hudaybiyah pamoja na Mtume ﷺ huku tukiwa watu elfu moja na mia nne na tulikuwa na kondoo khamsini wenye kiu.

Mtume ﷺ akaketi katika ukingo wa kisima, ama aliomba dua au alitema mate ndani yake, maji yakatiririka, tukanywa na kuwanyweshwa wanyama. Halafu, Mtume ﷺ akatuita kwa ajili ya kula kiapo chini ya mti. Mimi nikawa katika watu wa kwanza kuchukua ahadi. Watu wakaendelea kumbai. Baada ya kiasi cha nusu ya watu kufanya hivyo, Mtume ﷺ aliniambia,

«بَايَعَنِي يَا سَلَمَةُ»

“Chukua ahadi juu yangu ewe Salamah!

Nikamjibu: “Ewe Mjumbe wa Allah ﷺ, mimi tayari nimeshachukua ahadi juu yako katika watu wa mwanzoni kabisa.” Akasema:

«وَأَيْضًا»

“Na tena.”

Nikarudia. Kisha, akaniona nimejitenga pembeni, akanipatia ngao iliyote-ngenezwa na ngozi. Akaendelea kuungwa mkono na watu, walipokaribia kumalizika, akaniambia:

«أَلَا تَبِيعُ يَا سَلَمَةُ؟»

“Ewe Salamah! Kwanini hutaki kuniunga mkono?”

Nikamjibu, “Ewe Mtume! Nimeshachukua ahadi juu yako katika watu wa mwanzo, pia na wa katikati yao.” Mtume ﷺ akasema:

«وَأَيْضًا»

“Na tena.”

Nikamuunga mkono kwa mara ya tatu. Kisha Mtume ﷺ akasema:

¹ Fat'h Al-Bari 13:211.

² Muslim 3:1486.

³ Fat'h Al-Bari 6:136.

«يَا سَلْمَةُ أَيْنَ حَجَمْتِكِ أَوْ دَرَقْتِكِ الَّتِي أُعْطِيتُكَ؟»

“Ewe Salamah! Iko wapi ngao yako niliyokupa?”

Nikasema: “Ewe Mjumbe wa Allah! Nilikutana na ‘Amir ambaye hakuwa na ngao, nami nikampatia.” Mtume ﷺ akacheka na kusema:

«إِنَّكَ كَالَّذِي قَالَ الْأَوَّلُ اللَّهُمَّ ابْنِعِي حَيًّا هُوَ أَحَبُّ إِلَيَّ مِنْ نَفْسِي»

“Hakika Wewe ni sawa na alivyosema mtu wa mwanzo, ‘Ewe Allah! Nipatie mtu aliyependwa zaidi kwangu kuliko nafsi yangu.”

Halafu, washirikina wa Makkah wakatutumia ujumbe wa suluhu tukajadiliana sisi kwa sisi na kufikia makubaliano. Mimi nilikuwa mtumishi wa Twalhah bin ‘Ubaydullah wa kumpatia maji farasi wake na kumtunza. Na Twalhah alikuwa akinipatia chakula. Niliacha familia na mali yangu kwa ajili ya kuhamia kwa Allah تعالى na Mjumbe Wake. Baada ya sisi na watu wa Makkah kuwekeana mkataba, na baadhi yetu wakawa wanachanganyika baina yao, nikaenda kwenye mti na kuondoa miba yake, nikajilaza kivulini karibu na shina. Wakanjia washirikina wanne kutokea Makkah, wakaanza kumsema vibaya Mtume ﷺ, nami nikachukia kuwa karibu nao. Nikahamia kwenye mti mwingine, wakatandika silaha zao na wakajilaza. Wakati walipokuwa katika hali hiyo, mtu mmoja alinadi kutokea bondeni: “Enyi Muhajiriina! Ibn Zunaym ameuawa, nikaukamata upanga wangu na kuwaendea washirikina wale wane, ilhali wakiwa bado wamelala. Nikazichukua silaha zao mkononi kwangu, halafu nikasema: “Naapa kwa Aliyeupa utukufu uso wa Muhammad! Yeyote katika nyinyi hatanyanyua uso wake, bali nitakipiga kinachoyahifadhi macho yake.” Kisha nikawaswaga mpaka kwa Mtume ﷺ. Ami yangu ‘Amir naye, alimleta mshirikina mmoja ambaye alikuwa akiitwa Mikraz. Tukawasimamisha wao pamoja na washirikina wengine sabini, mbele ya Mtume ﷺ. Mtume ﷺ aliwaangalia, akasema:

«دَعُوهُمْ يَكُنْ لَهُمُ بَدْءُ الْفُجُورِ وَرِثَاةُ»

“Waacheni waende, kwani wao watakuwa chanzo cha maovu na mwisho wake.”

Hivyo, Mtume ﷺ akawasamehe. Allah تعالى Akateremsha:

وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ مِنْ بَعْدِ أَنْ أَظْفَرْتُمْ عَلَيْهِمْ^٤

“Na Yeye Ndiye Aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya Kukupeni Ushindi juu yao.”
(48:24)¹

Muslim alinukuu masimulizi yaliyolingana au yaliyo sawa na haya.² Katika Sahih Mbili kumeandikwa kuwa, Sa'd bin al-Musayyab alisema: “Baba yangu alikuwa miongoni mwa waliochukua ahadi ya maridhiano na Mtume ﷺ chini ya mti. Alisema: ‘Mwaka uliofuatia tukaenda kuhiji, lakini pakafichika mahali ulipokuwepo mti huo. Kwa hivyo, ikiwa nyinyi mtabainikiwa mahali ulipo, basi mtakuwa ni wenye ujuzi zaidi.”³

Abu Bakr Humaydi alisimulia kwamba Jabir رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ alipowaita watu kwa ajili ya kula kiapo, tulimkuta mtu mmoja miongoni mwetu, kwa jina akiitwa Jadd bin Qays akiwa amejificha chini ya bega la ngamia wake.”⁴ Hadithi hii alinukuu Muslim.⁵ Humaidi alisimulia tena kutoka kwa ‘Amri kuwa alimsikia Jabir رضي الله عنه amesema: “Katika siku ya Hodaybiyyah, tulikuwa watu elfu moja na mia nne, Mtume ﷺ akatuambia.

«أَنْتُمْ خَيْرُ أَهْلِ الْأَرْضِ الْيَوْمَ»

“Leo, nyinyi ndio watu walio bora zaidi wa ardhini.”

Jabir رضي الله عنه aliendelea kusema, “Kama ningelikuwa bado ninaona, ningelikuonesha huo mti.”⁶ Sufyan alisema: “Wao (Masahaba) walikhitilafiana kuhusu mahali pa mti huo.” Wameipokea Hadithi hiyo Bukhari na Muslimu.⁷

Imamu Ahmad alimnukuu Jabir رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

¹ *Dalail An-Nubuwwah* 4:138.

² Muslim 1807.

³ *Fat'h Al-Bari* 7:512, Muslim 1485.

⁴ *Musnad Al-Humaydi* 2:537.

⁵ Muslim 3:1483.

⁶ *Musnad Al-Humaydi* 2:514, Muslim na. 4811.

⁷ *Fat'h Al-Bari* 7:507, Muslim 3:1484.

«لَا يَدْخُلُ النَّارَ أَحَدٌ يَمِّنَ بَايَعِ تَحْتِ الشَّجَرَةِ»

*"Hataingia Motoni, mtu yeyote miongoni mwa waliochukua ahadi ya maridhiano chini ya mti."*¹

'Abdullah bin Ahmad alisimulia kutoka kwa Jabir رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَنْ يَصْعَدُ النَّيَّةَ نَيْتَةَ الْمُرَارِ فَإِنَّهُ يُحِطُّ عَنْهُ مَا حُطُّ عَنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ»

"Anayekwea Thaniyyah (njia ya mlimani), Thaniyyah ya Muraar, atafutiwa dhambi zake kama dhambi walizofutiwa Wana wa Israel."

Wakawa wa kwanza kuukwea mlima huo wapanda farasi (wa kabila la kiansari) wa Banu Khazraj. Kisha Waislamu wakafuata baada yao. Mtume ﷺ alisema:

«كُلُّكُمْ مَغْفُورٌ لَهُ إِلَّا صَاحِبَ الْجَمَلِ الْأَحْمَرِ»

"Nyote mmesamehewa isipokuwa mmiliki wa ngamia mwekundu."

Tukamuambia: "Njoo, ili Mtume ﷺ akuombe maghufira kwa Allah تعالى."

Akasema: "Wallahi! Kumpata ngamia wangu aliyepotea ni jambo litakalonipendeza zaidi kuliko sahibu yenu kuniombe maghufira."

Ghafla tukamsikia mtu huyo akinadi kupotelewa na ngamia wake. Muslim alikusanya Hadithi hii kutoka kwa 'Ubaydullah (kutoka kwa Jaabir رضي الله عنه).²

Kutoka kwa Abu Zubayr, amesema kuwa Jabir رضي الله عنه anasema: Ummu Mubashir رضي الله عنها alinieleza kwamba alimsikia Mtume ﷺ akimuambia Hafsa رضي الله عنها,

«لَا يَدْخُلُ النَّارَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ تَعَالَى مِنْ أَصْحَابِ الشَّجَرَةِ الَّذِينَ بَايَعُوا تَحْتَهَا، أَحَدٌ»

"Inshaallah, hataingia Motoni yeyote miongoni mwa watu waliochukua ahadi ya maridhiano chini ya mti."

Akasema: "Hapana Ewe Mtume!" Mtume ﷺ akamkaripia. Hafsa رضي الله عنها akasema:

«وَأِنْ مَنَعَكَ إِلَّا وَارِدَهَا»

"Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia." (19:71)

¹ Ahmad 3:350.

² Muslim 4:2144.

Mtume ﷺ akasema:

«قَدْ قَالَ اللَّهُ تَعَالَى: ﴿مَنْ تَبِعَى الَّذِينَ اتَّقُوا وَنَدَّرَ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثًا﴾»

“Allah تعالى Ameshasema: **Kisha Tutawaokoa wale waliomchamungu; na Tutawaacha madhaalimu humo wamepiga magoti.**”

Aliandika Muslim.¹ Pia kuna masimulizi kutoka kwa Jabir رضي الله عنه, “Mtumwa wa Hatib bin Balta’ah alikuja kumshitakia Hatib, akasema, ‘Kwa hakika, Hatib ataingia Motoni.’ Mtume ﷺ akamjibu:

«كَذَّبَتْ لَا يَدْخُلُهَا فَإِنَّهُ قَدْ شَهِدَ بَدْرًا وَالْحُدَيْبِيَّةَ»

“Umeongopa, hataingia, kwani yeye alishiriki Badr na Hudaibiyyah.”²

Kwa ajili hii, Allah تعالى Aliwasifu kwa kusema:

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ فَمَنْ نَكَتَ فَإِنَّمَا يَنْكُثْ عَلَى نَفْسِهِ ۗ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهِ اللَّهُ فَمَسِيئَتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٨﴾

“Bila ya shaka wanaofungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi hizi anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na anayetekeleza Aliyomuahidi Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Atamlipa ujira mkubwa.”

Ni sawa na Kauli nyingine:

﴿لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا﴾ ﴿٤٨﴾

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amewapa radhi Waumini walipofungamana nawe chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi Akateremsha utulivu juu yao, na Akawalipa kwa Ushindi wa karibu.” (48:18)

¹Muslim 4:1942.

²Muslim 4:1942.

سَيَقُولُ لَكَ الْمُخَلَّفُونَ مِنَ الْأَعْرَابِ شَغَلَتْنَا أَمْوَالُنَا وَأَهْلُونَا فَاسْتَغْفِرْ لَنَا ؕ يَقُولُونَ
بِأَلْسِنَتِهِمْ مَا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ ؕ قُلْ فَمَنْ يَمْلِكُ لَكُمْ مِنْ اللَّهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ بِكُمْ ضَرًّا أَوْ
أَرَادَ بِكُمْ نَفْعًا ؕ بَلْ كَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١١﴾ بَلْ ظَنَنْتُمْ أَنْ لَنْ يَنْقَلِبَ الرَّسُولُ
وَالْمُؤْمِنُونَ إِلَىٰ أَهْلِيهِمْ أَبَدًا وَزُيِّنَ ذَٰلِكَ فِي قُلُوبِكُمْ وَظَنَنْتُمْ ظَنًّا سَوِيًّا وَكُنْتُمْ
قَوْمًا بُورًا ﴿١٢﴾ وَمَنْ لَمْ يُؤْمِنْ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ فَإِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَعِيرًا ﴿١٣﴾ وَلِلَّهِ مُلْكُ
السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ يَغْفِرُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ ۚ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١٤﴾

11. *“Watakuambia mabedui waliobaki nyuma: Zimetushughulisha mali zetu na ahali zetu, basi tuombe msamaha. Wanasema kwa ndimi zao yasiyokuwamo katika nyoyo zao. Sema: Ni nani awezaye Kukusaidieni chochote kwa Mwenyezi Mungu Akitaka Yeye Kukudhuruni au Akitaka Kukunufaisheni? Bali Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda.”*

12. *“Lakini mlidhani kwamba Mtume na Waumini hawatarudi kabisa kwa ahali zao, na mkapambiwa hayo katika nyoyo zenu, na mkadhania dhana mbaya, na mkawa watu wanaoangamia.”*

13. *“Na asiyemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi kwa hakika Sisi Tumewaandalia makafiri Moto mkali.”*

14. *“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi. Humsamehe Amtakaye, na Humuadhibu Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”*

Udhuru wa Uongo kwa Waliojitenga na Mkatiba wa Hudaibiyah na Kemeo la Allah تعالی Kwao.

Allah تعالی Anaeleza kuhusu udhuru wanaoutoa mabedui ambao walichagua kubakia na familia na shughuli zao, wakaacha kwenda pamoja na Mtume ﷺ. Wakatoa udhuru juu ya shughuli zao, na wakaomba kwamba Mtume ﷺ awaombe maghufira, ilhali, hiyo ni kauli yao tu, haikuwa katika itikadi ya kweli, bali katika namna ya kujihami na kujifanyisha. Allah تعالی Amesema:

يَقُولُونَ بِأَلْسِنَتِهِمْ مَا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ ۚ قُلْ فَمَنْ يَمْلِكُ لَكُمْ مِنْ أَلَلهِ شَيْئًا إِنَّ أَرَادَ بِكُمْ ضَرًّا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ نَفْعًا

“Wanasema kwa ndimi zao yasiyokuwamo katika nyoyo zao. Sema: Ni nani awezaye kukusaidieni chochote kwa Mwenyezi Mungu Akitaka Yeye Kukudhuruni au Akitaka Kukunufaisheni?”

Maana yake: Hapana yeyote awezaye kuyazuia yale Aliyokutakieni Allah تعالى. Yeye ni Mjuzi wa siri na dhamira zenu, hata kama mtajisingizia na kutufanyia unafiki. Kwa minajili hii, Allah تعالى Amesema:

بَلْ كَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا

“Bali Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda.”

Halafu, Allah تعالى Akasema,

بَلْ ظَنَنْتُمْ أَنْ لَنْ يَنْقَلِبَ الرَّسُولُ وَالْمُؤْمِنُونَ إِلَىٰ أَهْلِيهِمْ أَبَدًا

“Lakini mlidhani kwamba Mtume na Waumini hawatarudi kabisa kwa ahali zao...”

Maana yake: Kubakia kwenu nyuma, hakukusababishwa na udhuru, au uasi, bali ni unafiki. Na mkadhani Waislamu watauawa na kuhilikishwa, maisha yao yatahilikishwa na hatarejea yeyote katika wao mwenye kusimulia.

وَوَظَنَنْتُمْ ظَنَّ السَّوْءِ وَكُنْتُمْ قَوْمًا بُورًا

“...na mkadhania dhana mbaya, na mkawa watu wanaoangamia.”

Inamaanisha kuwa waliangamia. Kwa mujibu wa ‘Abdullah bin ‘Abbas, Mujahid na wengine.¹ Qatadah alilitafsiri kwa maana ya wenye kuharibu. Na husemwa kwamba ni lugha ya watu wa Omani.² Allah تعالى Anasema:

¹ At-Tabari 22:214.

² At-Tabari 22:214.

وَمَنْ لَّمْ يُؤْمِنْ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ

“Na asiyeuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake...”

Maana yake: Wasiotakasa amali zao kwa dhahiri na kwa siri, basi, Allah تعالی Atawaadhibu kwa Moto, hata kama watawadhihirishia watu itikadi yao iliyo kinyume na ukweli wa jambo lenyewe.

Baada ya hapo, Allah تعالی Alibainisha kuwa Yeye Ndiye Mwenye Mamlaka, Mfalme, Mdhibiti wa wakazi wa mbinguni na ardhini.

يَغْفِرُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا

“Humsamehe Amtakaye, na Humuadhibu Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Maana yake: Kwa mwenye kutubu na kujirudi na akanyenyekea Kwake.

سَيَقُولُ الْمُخَلَّفُونَ إِذَا انطَلَقْتُمْ إِلَىٰ مَغَائِمٍ لَتَأْخُذُواهَا ذُرُونًا نَتَّبِعْكُمْ يُرِيدُونَ
 أَنْ يُبَدِّلُوا كَلِمَ اللَّهِ ۗ قُلْ لَنْ تَتَّبِعُونَا كَذَّبْتُمْ كَذَّالِكُمْ قَالَ اللَّهُ مِنْ قَبْلُ ۗ فَسَيَقُولُونَ بَلْ
 نَحْسَدُونَكَ ۗ بَلْ كَانُوا لَا يَفْقَهُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٥﴾

15. “Waliobaki nyuma watasema: Mtapokwenda kuchukua ngawira, tuacheni tukufuateni! Wanataka kuyabadili maneno ya Mwenyezi Mungu. Sema: Hamtatufuata kabisa. Mwenyezi Mungu Alikwishasema kama hivi zamani. Hapo watasema: Bali nyinyi mnatuhusudu. Siyo, bali walikuwa hawafahamu ila kidogo.”

Allah تعالی Anaeleza kuhusu mabedui waliobakia nyuma ya Mtume ﷺ wakati wa ‘Umra ya Hudaybiyyah, wakisema kwamba, pindi Mtume ﷺ na Masahaba wake walipokwenda kufungua mji wa Khaybar, mabedui walitaka wafuatane nao kwenye ghanima, na hawakuwepo kwenye mapigano na maadui, kuvumilia na kusubiri. Allah تعالی Akamuamuru Mtume ﷺ kwamba asiwaruhusu katika hayo, kwa kuwaadhibu kwa jinsi ya madhambi yao, kwani Allah تعالی Aliwaahidi washiriki wa Hudaybiyyah peke yao ndio wa kupewa ngawira za Khaybar. Katika hilo, wasishirikiane na mabedui wanaobakia nyuma. Kwa hivyo, hilo

halikuwezekana kisharia wala kikudura ya Allah تعالى. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

يُرِيدُونَ أَنْ يُبَدِّلُوا كَلِمَ اللَّهِ^ع

“...Wanataka kuyabadili Maneno ya Mwenyezi Mungu...”

Mujahid, Qatadah, Juwaybir walitoa rai, kuwa, hiyo ni ahadi waliyoahidiwa watu wa Hudaybiyyah. Kauli hii ndiyo ambayo Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameikubali.¹

قُلْ لَنْ تَتَّبِعُونَا كَذَلِكُمْ قَالَ اللَّهُ مِنْ قَبْلُ^ه

“Sema: Hamtatufuata kabisa. Mwenyezi Mungu Alikwisha sema kama hivi zamani.”

Maana yake: Allah تعالى Aliwaahidi washiriki wa Hudaybiyah kabla ya ombi lenu la kutoka pamoja nao,

فَسَيَقُولُونَ بَلْ نَحْسُدُونَنَا^ع

“Hapo watasema: Bali nyinyi mnatusudu.”

Maana yake: Katika kukushirikisheni katika ghanima.

بَلْ كَانُوا لَا يَفْقَهُونَ إِلَّا قَلِيلًا

“Siyo, bali walikuwa hawafahamu ila kidogo.”

Maana yake: Mambo si kama walivyodai, lakini hawana fahamu.

* * *

¹ At-Tabari 22:215.

قُلْ لِلْمُخَلَّفِينَ مِنَ الْأَعْرَابِ سُدْعُونَ إِلَىٰ قَوْمِ أُولَىٰ بِأَسِ
 شَدِيدٍ تَقْتُلُوهُمْ أَوْ يُسْلِمُونَ ۗ فَإِنْ تُطِيعُوا يُؤْتِكُمُ اللَّهُ أَجْرًا
 حَسَنًا ۗ وَإِنْ تَتَوَلَّوْا كَمَا تَوَلَّيْتُمْ مِنْ قَبْلُ يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا
 أَلِيمًا ﴿١٦﴾ لَيْسَ عَلَى الْأَعْمَىٰ حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْأَعْرَجِ
 حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْمَرِيضِ حَرْجٌ ۗ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
 يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۗ وَمَنْ يَتَوَلَّ يَعْذِْبْهُ
 عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٧﴾ * لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ
 إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ
 السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿١٨﴾ وَمَغَانِمَ كَثِيرَةً
 يَأْخُذُونَهَا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٩﴾ وَعَدَّكُمْ اللَّهُ
 مَغَانِمَ كَثِيرَةً تَأْخُذُونَهَا فَعَجَلَ لَكُمْ هَذِهِمُ ۗ وَكَفَّ أَيْدِيَ
 النَّاسِ عَنْكُمْ وَلِتَكُونَ آيَةً لِلْمُؤْمِنِينَ وَيَهْدِيَكُمْ صِرَاطًا
 مُسْتَقِيمًا ﴿٢٠﴾ وَأُخْرَىٰ لَمْ تَقْدِرُوا عَلَيْهَا قَدْ أَحَاطَ اللَّهُ
 بِهَا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ﴿٢١﴾ وَلَوْ قَتَلْتُمْ
 الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلُوا الْأَدْبَرُ ثُمَّ لَا تِجْدُونَ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا
 ﴿٢٢﴾ سُنَّةَ اللَّهِ الَّتِي قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلُ ۗ وَلَنْ يَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّهِ
 تَبْدِيلًا ﴿٢٣﴾ وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ
 عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ مِنْ بَعْدِ أَنْ أَظْفَرَكُمْ عَلَيْهِمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ

بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا ﴿٢٤﴾

قُلْ لِلْمُخَلَّفِينَ مِنَ الْأَعْرَابِ
 سُدْعُونَ إِلَىٰ قَوْمِ أُولَىٰ بِأَسِ
 شَدِيدٍ تَقْتُلُوهُمْ أَوْ يُسْلِمُونَ ۗ
 فَإِنْ تُطِيعُوا يُؤْتِكُمُ اللَّهُ
 أَجْرًا حَسَنًا ۗ وَإِنْ تَتَوَلَّوْا
 كَمَا تَوَلَّيْتُمْ مِنْ قَبْلُ يُعَذِّبْكُمْ
 عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٦﴾ لَيْسَ عَلَى
 الْأَعْمَىٰ حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْأَعْرَجِ
 حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْمَرِيضِ حَرْجٌ ۗ
 وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
 يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ
 تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۗ وَمَنْ يَتَوَلَّ
 يَعْذِْبْهُ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٧﴾

16. "Waambie walioachwa
 nyuma katika mabedui:
 Karibuni hivi mtakujaitwa
 kwenda pigana na watu
 wakali kwa vita, mpigane
 nao au wasalimu amri. Basi
 mkimt'ii, Mwenyezi Mungu
 Atakupeni ujira mzuri. Na
 mkipinga kama mlivyo-
 pinga kwanza, Ataku-
 adhibuni kwa adhabu
 iliyochungu."

17. "Kipofu hana lawama,
 wala kiguru hana lawama,

wala mgonjwa hana lawama. Na mwenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Atamuingiza katika bustani zipitazo mito kati yake. Na atakayepinga Atamuadhibu kwa adhabu chungu."

Allah تعالیٰ Anatoa Tangazo la Kuendelea na Jihadi na kwamba Ndio Inayotofautisha baina ya Waumini na Wanafiki

Wafasiri wa Qur'an wamekuwa na rai nyingi kuhusu watu wanaotakiwa kwenda kukabiliana na wanaowaita, ambao ni wakali wa vita. Kwanza wao ni watu wa kabila la Hawaazin, kama Shu'bah alivyosimulia kutoka kwa Abu Bishr, kutoka kwa Sa'd bin Jubayr, au 'Ikrimah, au wote wawili.¹ Hushaym ametoa maelezo haya kutoka kwa Abu Bishr, kutoka kwa wote wawili, Sa'd bin Jubayr na 'Ikrimah.² Qatadah, kama ilivyosimuliwa kutoka kwake, katika masimulizi mojawapo, alikuwa na rai sawa na hiyo.³ Pili, ni Thaqif, kwa mujibu wa adh-Dhahaak. Tatu, Banuu Hanifah. Hayo aliyasema Juwaybir na pia ni kwa mujibu wa Muhammad bin Is-haq alivyosimulia kutoka kwa Az-Zuhri.⁴ Masimulizi sawa na hayo, yalitolewa na Sa'd bin Jubayr na 'Ikrimah.⁵ Nne, Wafursi. Aliyasimulia 'Ali bin Abu Twalhah, kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما. Haya pia ni maoni ya 'Ataa, Mujahid na 'Ikrimah, katika moja ya masimulizi yake.⁶ Ka'b Ahbaar amesema kuwa hao ni Warumi.⁷ Abu Laylaa, 'Atwaa, Al-Hasan na Qatadah walisema kuwa ni Waajemi na Warumi.⁸ Mujahid amesema: "Hao ni wanaoabudu masanamu."⁹

Mujahid amesema tena: "Hao ni watu wapenda vita, wala kundi lao halikuainishwa." Ibn Jurayj anatoa rai hiyo pia, na Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameikubali.

Kauli ya Allah تعالیٰ:

¹ At-Tabari 22:220.

² At-Tabari 22:220.

³ At-Tabari 22:220.

⁴ At-Tabari 22:220.

⁵ At-Tabari 22:220.

⁶ At-Tabari 22:219, Al-Qurtubi 16:272.

⁷ At-Tabari 22:221.

⁸ At-Tabari 22:219.

⁹ Ad-Dur Al-Manthur 7:520.

تُقَاتِلُونَهُمْ أَوْ يُسَلِّمُونَ^ط

“...mpigane nao au wasalimu amri.”

Maana yake: Amekuwekeeni Shariah ya Jihadi dhidi yao na kupigana bila ya kuacha. Ushindi ni wenu, au wasilimu na kuingia katika Dini yenu, bila ya mapigano, ila kwa khiyari. Kisha, Allah تعالى Alisema:

فَإِنْ تَطِيعُوا

“Basi mkimtii...”

Maana yake: Mnaitika na kujiandaa kwa ajili ya Jihadi na kutekeleza wajibu wenu katika hili,

يُؤْتِكُمْ اللَّهُ أَجْرًا حَسَنًا وَإِنْ تَتَوَلَّوْا كَمَا تَوَلَّيْتُمْ مِنْ قَبْلُ^ط

“Mwenyezi Mungu Atakupeni ujira mzuri. Na mkipinga kama mlivyopinga kwanza...”

Inamaanisha, katika zama za ujahili, mlipoitwa kwa ajili ya Jihadi, nanyi mkabakia nyuma.

يُعَذِّبُكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا

“...Atakuadhibuni kwa adhabu iliyo chungu.”

Udhuru wa Kisharia wa Kuacha Jihadi pamoja na Agizo la Utii

Halafu, Allah تعالى Alitaja nyudhuru za kuacha Jihadi. Miongoni mwake ni za lazima kama vile upofu na ulemavu. Nyingine ni za kwa muda, kama vile maradhi yanayozuka kwa siku kadha, kisha yanaondoka. Mtu akiwa katika hali ya kuugua kwake anajumuishwa na wenye udhuru wa kisheria mpaka apone. Halafu, katika kuifarahisha Jihadi na kumtii Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ, Allah تعالى Amesema:

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَمَنْ يَتَوَلَّ

“Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Atamuingiza katika bustani yapitayo mito kati yake. Na atakayepinga upande...”

Maana yake: Atakayejitenga na Jihadi akajishughulisha na maisha yake,

يُعَذِّبُكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا

“...atamuadhibu kwa adhabu chungu.”

Kwa mateso ya duniani na Moto huko Akhera. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ
السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿١٦﴾ وَمَعَانِمَ كَثِيرَةً يَأْخُذُونَهَا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا
حَكِيمًا ﴿١٧﴾

18. “Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amewapa radhi Waumini walipofungamana nawe chini ya mti, na Alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi Akateremsha utulivu juu yao, na Akawalipa kwa Ushindi wa karibu.”

19. “Na ngawira nyingi watakazozichukua. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Bishara ya Radhi na Ghanima kwa Ajili ya Watu wa Bai’ah ya Ridhwaan.

Watu waliochukua ahadi siku ya Hudaibiyah wapata Bishara ya Bidhaa na Ghanima. Allah تعالى Anaeleza kuhusu kuwaridhia Waumini waliochukua ahadi ya maridhiano kwa Mtume ﷺ chini ya mti. Idadi yao ilikwishatajwa kwamba walikuwa elfu moja na mia nne, na kwamba mti huo ulikuwa ni Samurah uliokuwa mahali paitwapo *Hudaybiyah*. Bukhari alinukuu kutoka kwa Twariq kwamba ‘Abdur-Rahman alisema: “Nilikwenda kuhiji, nikawakuta njiani watu wakisali.” Nikasema: “Ni msikiti gani huu.” Wakajibu: “Hapa ni pale ambapo Mtume ﷺ alipokea uungwaji mkono.” Nikamuendea Said bin Musayyab, nikamueleza, akasema: “Baba yangu aliniambia kuwa yeye alikuwa miongoni mwa waliokula kiapo kwa Mtume ﷺ chini ya mti. Tukatoka katika mwaka uliofuatia, tukapasahau mahali pale, na hatukukubaliana kuwa ulikuwa mti gani hasa.” Sa’id akasema: “Masahaba wa Muhammad hawakuujua, lakini nyinyi mmeujua, basi nyinyi mna elimu bora kuliko wao.”¹ Kauli ya Allah تعالى:

¹ *Fat’h Al-Bari* 7:512.

فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ

“...na Alijua yaliyomo nyoyoni mwao.”

Maana yake: Katika masuala ya kusadiki, kutekeleza, kusikia na kutii,

فَأَنْزَلَ السُّكِينَةَ

“Basi Akateremsha utulivu...”

Maana yake: Amani,

عَلَيْهِمْ وَأَنْبَهُهُمْ فَتَحًا قَرِيبًا

“...juu yao, na Akawalipa kwa Ushindi wa karibu.”

Nayo ni yale Aliyoyapitisha Allah تعالى kwa Masahaba baada ya mkataba baina yao na maadui wao, pamoja na kheri ya kuendelea iliyoambatana na ushindi wa Khaybar na wa Makkah, halafu ushindi katika miji na maeneo mengine, na nguvu, ushindi na kuwa juu duniani na Akhera. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

وَمَغَانِمَ كَثِيرَةً يَأْخُذُونَهَا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٢٠﴾

“Na ngawira nyingi watakazozichukua. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

وَعَدَّكُمْ اللَّهُ مَغَانِمَ كَثِيرَةً تَأْخُذُونَهَا فَعَجَّلَ لَكُمْ هَذِهِ ۚ وَكَفَّ أَيْدِيَ النَّاسِ عَنْكُمْ
وَلِتَكُونَ آيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ وَيَهْدِيَكُمْ صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا ﴿٢١﴾ وَأُخْرَى لَمْ تَقْدِرُوا عَلَيْهَا قَدْ
أَحَاطَ اللَّهُ بِهَا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ﴿٢٢﴾ وَلَوْ فَتَلَّكُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوَلَّوْا
الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يَجِدُونَ وِلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿٢٣﴾ سُنَّةَ اللَّهِ الَّتِي قَدْ خَلَّتْ مِنْ قَبْلُ ۗ وَلَنْ يَجِدَ
لِسُنَّةِ اللَّهِ تَبْدِيلًا ﴿٢٤﴾ وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ مِنْ
بَعْدِ أَنْ أَظْفَرَكُمْ عَلَيْهِمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا ﴿٢٥﴾

20. “Mwenyezi Mungu Anakuahidini ngawira nyingi mtakazo-zichukua, basi Amekutangulizieni hizi kwanza, na Akaizuia mikono ya watu isikufikieni, na ili hayo yawe ni Ishara kwa Waumini, na Akakuongozeni njia Iliyonyooka.”

21. *“Na mengine hamuezi kuyapata bado, Mwenyezi Mungu Amekwishayazingia. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”*

22. *“Na lau makafiri wangelipigana nanyi basi bila ya shaka wangeligeuza migongo, kisha wasingelipata mlinzi wala msaidizi.”*

23. *“Huo ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu uliokwishapita zamani, wala hutapata mabadiliko katika mwenendo wa Mwenyezi Mungu.”*

24. *“Na Yeye Ndiye Aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya Kukupeni Ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona myatendayo.”*

Bishara ya Ghanima Nyingi za Vita

Mujahid alitoa rai kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَعَدَكُمْ اللَّهُ مَغَايِمَ كَثِيرَةً تَأْخُذُوهَا

“Mwenyezi Mungu Anakuahidini ngawira nyingi mtakazozichukua...”

Hizo ni ghanima zote, mpaka leo,

فَعَجَّلَ لَكُمْ هُنْدِمْ

“...basi Amekutangulizieni hizi kwanza...”

Maana yake: Ushindi wa Khaybar.¹ ‘Awfi alinukuu kutoka kwa Ibn ‘Abbas

رضي الله عنهما

فَعَجَّلَ لَكُمْ هُنْدِمْ

“...basi Amekutangulizieni hizi kwanza...”

Maana yake: “Mkataba wa Hudaybiyah.”²

وَكَفَّ أَيْدِيَ النَّاسِ عَنْكُمْ

“...na Akaizuia mikono ya watu isikufikieni...”

¹ At-Tabari 22:230.

² At-Tabari 22:230.

Maana yake: Hamkapatwa na uovu walioudhamiria maadui zenu juu ya kukupigeni vita na kukuueni. Kadhalika, mikono ya watu ilizuiwa kuwafikia wanafamilia na ndugu zenu mliowaacha nyuma ya migongo yenu katika jamaa na wake zenu,

وَلَتَكُونَ آيَةً لِلْمُؤْمِنِينَ

“...na ili hayo yawe ni Ishara kwa Waumini...”

Maana yake: Wayazingatie hayo, kwani Allah تعالى Amewahifadhi na Kuwapa ushindi dhidi ya maadui wengine, licha ya uchache wao, na ili walijue jambo hili walilofanyiwa na Allah تعالى, kwamba Yeye Ndiye Ajuaye ukomo wa mambo, tena, kheri imo katika jambo Analowachagulia waja Wake Waumini, hata kama kwa dhahiri yake watalichukia.

وَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ

“Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu.” (2:216)

Allah تعالى Amesema,

وَيَهْدِيكُمْ صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا

“...na Akakuongozeni Njia Iliyonyooka.”

Maana yake: Kwa sababu ya kufuata kwenu amri Zake, na Kumtii, pamoja na kuafikiana kwenu na Mjumbe Wake.

Bishara ya Kupata Ushindi Waislamu Mpaka Siku ya Kiyama

Kauli ya Allah تعالى:

وَأُخْرَىٰ لَمْ تَقْدِرُوا عَلَيْهَا قَدْ أَحَاطَ اللَّهُ بِهَا وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ﴿٦٠﴾

“Na mengine hamuezi kuyapata bado, Mwenyezi Mungu Amekwishayazingia. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”

Maana yake: Na ghanima nyingine na ushindi mwingine ulio bayana, ambao hamkuwa mkiuweza. Allah تعالى Amekurahisishieni na Ameyazingira yote hayo kwa ajili yenu, kwani Yeye, Allah تعالى, Huwaruzuku waja Wake wamchao, kwa

namna ambayo wasiyoweza kuihesabu. Wafasiri wamekuwa na rai mbalimbali kuhusu maana ya ghanima hii ni nini. Al-'Awfi alisema kuwa alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما: "Ni mji wa Khaybar."¹ Rai yake hii imetokana na Kauli ya Allah تعالى:

فَعَجَّلَ لَكُمْ هَذِهِ

"...basi Amekutangulizieni hizi kwanza..."

Kwamba hii inamaanisha, mkataba wa Hudaybiyyah. Pia ni rai ya 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam.² Qatadah amesema, "Ni Makkah." Ibn Jarir رحمه الله تعالى.³ Ibn Abu Laylaa na Al-Hasan Al-Basri walisema: "Ni Waajemi na Warumi".⁴ Mujahid alisema: "Ni kila ushindi, mpaka Siku ya Kiyama."⁵ Abu Dawud At-Twayaalisi alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, kuwa,

وَأُخْرَى لَمْ تَقْدِرُوا عَلَيْهَا قَدْ أَحَاطَ اللَّهُ بِهَا

"Na mengine hamuezi kuyapata bado. Mwenyezi Mungu Amekwishayazingia...."

"Ni ushindi huu unaoendelea kupatikana, hadi Siku ya Kiyama."⁶

Kama Makafiri wa Makkah Wangelipigana Hudaybiyah, Wangelikimbia na Wasingeliweza Kupambana.

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَوْ فَتَلَكُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوَلَّوْا الْأَدْبَرَ ثُمَّ لَا يَجِدُونَ وِلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿٦٧﴾

"Na lau makafiri wangelipigana nanyi basi bila ya shaka wangeligeza migongo, kisha wasingelipata mlinzi wala msaidizi."

¹ At-Tabari 22:233.

² At-Tabari 22:233-234.

³ At-Tabari 22:234.

⁴ At-Tabari 22:233.

⁵ At-Tabari 22:233.

⁶ At-Tabari 22:233 alieleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema. "Ni ushindi dhini ya Uajemi na Roma." Mujahid akaongeza, "Basi endeleeni kupata ushindi mpaka Siku ya Kiama."

Allah تعالی Anawapa bishara waja Wake Waumini, kwamba, washirikina wangelipigana nao, basi, Allah تعالی Angelimpa ushindi Mjumbe Wake na Waumini. Halafu, jeshi la makafiri lingelikimbia kwa kugeuka wasingelipata msaidizi wala wa kuwanusuru, kwa sababu wanapigana vita dhidi ya Allah تعالی, Mjumbe Wake ﷺ na kundi lake la Waumini. Kisha, Allah تعالی Akasema:

سُنَّةَ اللَّهِ الَّتِي قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلُ وَلَنْ تَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّهِ تَبْدِيلًا ﴿١٦﴾

“Huo ndio mwenendo wa Mwenyezi Mungu uliokwisha pita zamani, wala hutapata mabadiliko katika mwenendo wa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Huu ni mwenendo na ada ya Allah تعالی kwa viumbe Wake, pindi kufuru na Imani vinapokabiliana mahali, basi nusura kutoka kwa Allah تعالی huja kuifanya Imani iwe juu ya kufuru, na Akainua haki na Akaiangusha batili. Ni kama siku ya Badr ambapo, Allah تعالی Aliwapa ushindi wapenzi Wake, Waumini dhidi ya maadui Wake, washirikina. Licha ya uchache wa idadi na zana za Waislamu dhidi ya idadi kubwa ya washirikina.

Hekima ya Allah تعالی Kuzuia Vita

Kauli ya Allah تعالی:

وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ مِنْ بَعْدِ أَنْ أَظْفَرَكُمْ عَلَيْهِمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا ﴿١٧﴾

“Na Yeye Ndiye Aliyezuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya Kukupeni Ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona myatendayo.”

Huu ni ukumbusho wa Allah تعالی kwa waja Wake Waumini, pindi Alipozuia mikono ya washirikina kuwafikia na kuwadhuru kwa ubaya wowote, na Akaizuia mikono ya waumini dhidi ya washirikina katika Masjid Al-Haraam. Bali Allah تعالی Aliyahifadhi makundi yote mawili na Akawezesha mapatano baina yao, yaliyokuwa ya kheri kwa Waumini, na wao ndio wenye mwisho mzuri duniani na Akhera. Hadithi ya Salamah bin Al-Akwa رضي الله عنه, pindi alipoleta mateka sabini, wakafungwa mbele ya Mtume ﷺ. Aliwatazama, akasema:

«أَرْسِلْهُمْ يَكُنْ لَهُمُ بَدَأُ الْفُجُورِ وَثَنًا»

“Waachilieni, ili iwe ni mwanzo wa uovu na mwisho wake.”¹

Na Aya ikashuka kuhusu jambo hilo:

وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ

“Na Yeye Ndiye Aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao...”

Imamu Ahmad aliandika kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه, kuwa amesema: “Katika siku ya Hudaybiyah, watu themanini kutoka Makkah wakiwa na silaha waliteremka bondeni alikokuweco Mtume ﷺ na Masahaba Wake, kwa kupitia upande wa mlima Tan'im. Nia ya watu hao ilikuwa kumshambulia Mtume ﷺ, akaomba dua dhidi yao, wakakamatwa mateka. 'Affan alisema, akawasamehe, halafu, ikashuka Aya hii:

وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ مِنْ بَعْدِ أَنْ أَظْفَرْتُمْ عَلَيْهِمْ²

“Na Yeye Ndiye Aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya Kukupeni Ushindi juu yao.”²

Muslim ameipokea Hadithi hiyo, na Abu Dawud ameipokea katika sunani yake pamoja na Tirmidhi chini ya mlango wa Tafsiri.³

* * *

¹ Hayo yalishatokea.

² Ahmad 3:122.

³ Muslim 3:1442, Abu Dawud 3:137, *Tuhfat Al-Ahwadhi*, An-Nasai katika *Al-Kubra* 9:149.

هُم الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ
 وَالْهَدْيِ مَعْكُوفًا أَنْ يَبْلُغَ حِجْلَهُ^٤ وَلَوْلَا رِجَالٌ مُؤْمِنُونَ وَنِسَاءٌ
 مُؤْمِنَاتٌ لَمَّ تَعَلَّمُوهُمْ أَنْ تَطْعُوهُمْ فَتُصِيبَكُمْ مِنْهُمْ مَعْرَةٌ بَغَيْرِ
 عِلْمٍ^٥ لِيَدْخُلَ اللَّهُ فِي رَحْمَتِهِ مَنْ يَشَاءُ^٦ لَوْ تَزَيَّلُوا لَعَذَّبْنَا
 الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٢٥﴾ إِذْ جَعَلَ الَّذِينَ
 كَفَرُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْحَمِيَّةَ الْجَنْهَلِيَّةَ فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ
 عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ التَّقْوَى
 وَكَانُوا أَحَقَّ بِهَا وَأَهْلَهَا^٧ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٢٦﴾
 لَقَدْ صَدَقَ اللَّهُ رَسُولَهُ الرُّؤْيَا بِالْحَقِّ^٨ لَتَدْخُلَنَّ الْمَسْجِدَ
 الْحَرَامَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ ءَامِينَ الْمُحَلِّقِينَ رُءُوسَكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا
 تَخَافُونَ^٩ فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا فَجَعَلَ مِنْ دُونِ ذَلِكَ فَتْحًا
 قَرِيبًا ﴿٢٧﴾ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَى وَدِينِ الْحَقِّ
 لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ^{١٠} وَكَفَى بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾ مُحَمَّدٌ
 رَسُولُ اللَّهِ^{١١} وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ^{١٢}
 تَرَاهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا سِيمَاهُمْ
 فِي وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثَرِ السُّجُودِ^{١٣} ذَلِكَ مَنْطَلُهُمْ فِي التَّوْرَةِ^{١٤} وَمَنْطَلُهُمْ
 فِي الْإِنْجِيلِ كَرْنَعٍ أَخْرَجَ شَطَطَهُ فَفَازَرَهُ فَاسْتَعْلَظَ فَاسْتَوَى
 عَلَى سُوْقِهِ يُعْجِبُ الزُّرَّاعَ لِيُغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ^{١٥} وَعَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾

هُم الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوكُمْ عَنِ
 الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَالْهُدَى مَعْكُوفًا
 أَنْ يَبْلُغَ حِجْلَهُ^٤ وَلَوْلَا رِجَالٌ مُؤْمِنُونَ
 وَنِسَاءٌ مُؤْمِنَاتٌ لَمَّ تَعَلَّمُوهُمْ أَنْ
 تَطْعُوهُمْ فَتُصِيبَكُمْ مِنْهُمْ مَعْرَةٌ بَغَيْرِ
 عِلْمٍ^٥ لِيَدْخُلَ اللَّهُ فِي رَحْمَتِهِ مَنْ
 يَشَاءُ^٦ لَوْ تَزَيَّلُوا لَعَذَّبْنَا
 الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٢٥﴾
 إِذْ جَعَلَ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي قُلُوبِهِمُ
 الْحَمِيَّةَ الْجَنْهَلِيَّةَ فَأَنْزَلَ اللَّهُ
 سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى
 الْمُؤْمِنِينَ وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ
 التَّقْوَى وَكَانُوا أَحَقَّ بِهَا وَأَهْلَهَا^٧
 وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٢٦﴾

25. "Hao ndio waliokufuru
 na wakakuzieni msiingie
 Msikiti Mtakatifu, na
 wakawazuilia wanyama
 wa kuchinjwa kufika
 mahala pao. Na lau si
 wanaume Waumini na
 wanawake Waumini msio-
 wajuah mkawasaga na

mkaingia makosani kuto- kana nao bila ya kujua Mwenyezi Mungu (Amefanya haya) ili Amuingize Amtakae katika Rehema Yake. Lau wangelitengana bila ya shaka Tungeliwaadhibu waliokufuru kwa adhabu chungu."

26. "Pale waliokufuru walipotia katika nyoyo zao hasira, hasira za kijinga, Mwenyezi Mungu Aliteremsha utulivu juu ya Mtume Wake na juu ya Waumini, na Akawalazimisha neno la kuchamungu. Na wao walikuwa ndio wenye haki nalo na wenye kustahili. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."

Miongoni mwa Faida za Sulhu ya Hudaybiyah, Licha ya Kuwa Waumini ndio wenye Haki na Ushindi

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu makafiri wa kishirikina katika Waarabu wa Kikuraishi na waliowasaidia wao dhidi ya Mtume ﷺ:

هُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا

"Hao ndio waliokufuru..."

Maana yake: Hao ndio makafiri, si wengine.

وَصَدُّكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ

"...na wakakuziieni msiingie Msikiti Mtakatifu..."

Maana yake: ilhali, nyinyi ndio mnaostahiki zaidi msikiti huo, na ndio watu wake kabisa, katika jambo hilo.

وَأَهْدَىٰ مَعَكُمْ أَنْ يَبْلُغَ حَجَّهِ^٤

"...na wakawazuilia dhabihu kufika mahala pao."

Inamaanisha, wakawazuia wanyama wa kuchinjwa wasifike mahala pao. Haya ni kutokana na uasi na ukaidi wao. Wanyama hao walikuwa ngamia sabini, kama itakavyoelezwa, Inshaa Allah. Kauli ya Allah تعالیٰ:

¹ Ahmad 3:122.

² Muslim 3:1442, Abu Dawud 3:137, *Tuhfat Al-Ahwadhi*, An-Nasai katika *Al-Kubra* 9:149.

وَلَوْلَا رِجَالٌ مُّؤْمِنُونَ وَنِسَاءٌ مُّؤْمِنَاتٌ

“Na lau si wanaume Waumini na wanawake Waumini...”

Maana yake: Baina ya migongo yao kuna anayeficha imani yake dhidi yao kwa kuzikhofia nafsi zao dhidi ya kaumu yao, lakini Sisi Tulikupeni mamlaka juu yao (huko Makkah) na mngeliweza kuwaua na kuwamaliza kabisa, lakini miongoni mwao kulikuwemo Waumini wa kiume na wa kike ambao msingeliwajua katika kipindi cha mauaji. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

لَمْ تَعْلَمُوهُمْ أَنْ تَطُوهُمْ فَتُصِيبَكُمْ مِنْهُمْ مَعْرَةٌ

“...msiowajua mkawasaga na mkaingia makosani kutokana nao...”

Maana yake: Madhambi na gharama.

بِغَيْرِ عِلْمٍ لِّيُدْخِلَ اللَّهُ فِي رَحْمَتِهِ مَنْ يَشَاءُ

“...bila ya kujua ...Mwenyezi Mungu (Amefanya haya) ili Amuingize Amtakaye katika Rehema Yake.”

Maana yake: Anaakhirisha adhabu yao ili Awaokoe Waumini walio baina yao, na ili wengi katika wao warejee katika Uislamu. Kisha, Allah تعالى Akasema:

لَوْ تَرَىٰ

“Lau wangelitengana...”

Maana yake: Lau kama ingelikuwepo upambanuzi baina ya makafiri na Waumini waliokuwa wakiishi pamoja nao,

لَعَذَّبْنَا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا

“...bila ya shaka Tungeliwaadhibu waliokufuru kwa adhabu chungu.”

Basi, Tungelikupeni mamlaka juu yao, na kuweza kuwaua pasi na udhuru wowote.

إِذْ جَعَلَ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْحَمِيَّةَ الْحَمِيَّةَ الْجَاهِلِيَّةَ

“Pale waliokufuru walipotia katika nyoyo zao hasira, hasira za kijinga...”

Hayo, ni kipindi walipokataa kuandikwa *Bismillahir Rahmanir Rahiym* (Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu), pia wakakataa kuyaandika, "Haya ndiyo aliyoyapitisha Mtume ﷺ."

فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ التَّقْوَى

"...Mwenyezi Mungu Aliteremsha utulivu juu ya Mtume Wake na juu ya Waumini, na Akawalazimisha neno la kumchamungu."

Mujahid alisema: "*Kalimatut-Taqwa* (Neno la uchamungu) lina maana ya ikhilasi.¹ 'Ataa bin Abu Rabaah alisema, ni, "*Laa ilaaha illallah Wahdahu laa sharika lahu, lahul-Mulku, walahul-Hamd, Wahuwa 'Alaa kulli shay-in Qadiyr.* (Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki, isipokuwa Allah تعالى, Peke Yake, Hana mshirika, Ufalme ni Wake, Hamdi ni Zake, na Yeye ni Mwenye Uwezo wa Kufanya kila kitu."² Yunus bin Bakiyr alilieleza toka kwa Ibn Is-haq, toka kwa Zuhri, toka kwa 'Urwah, toka kwa Maswar, juu ya Aya:

وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ التَّقْوَى

"...na Akawalazimisha neno la kuchamungu."

Kuwa ni, "*Laa ilaaha illallah Wahdahu, laa shariyka lahu,*" Hapana Mola anayepaswa kuabudiwa kwa haki, isipokuwa Yeye Peke Yake, Asiy na mshirika.

Hizi ni Hadithi Zilizokuja Katika Kisa cha Hundaybiyah na Suluhu Yake.

Imamu Bukhari, Allah تعالى Amrehemu, ameeleza chini ya "Kitabu cha Masharti," katika Sahih yake, kuwa, Miswar bin Makhramah na Marwan bin Hakam, kila mmoja akisadikisha Hadithi ya mwenzake. Walisema: "Mtume ﷺ alitoka katika zama za Hundaybiyyah, akiwa na Masahaba kiasi cha elfu moja ushei. Alipofika Dhul-Hulayfah, aliwakokota wanyama wa kuchinjwa na kuwatia alama, akatia nia kwa ajili ya ibada ya Umra "Hija ndogo." Akatuma wapelelezi kadha kutoka kabila la Khuza'ah, na akaendelea. Baada ya kufika katika kijiji

¹ At-Tabari 22:255.

² At-Tabari 22:256.

cha Ash-Taata, mpelelezi wake alimjia, akasema: 'Makuraishi wamekusanya Makabila ya Kinana na Khuzaa, wamejikusanya mahali paitwapo "Hunshiyu" nao ni mlima uliopo sehemu ya chini ya Makka na wakala kiapo¹ dhidi yako. Wao wanakusudia kupigana na kukuzuia.' Mtume ﷺ akasema:

«أَشِيرُوا أَيُّهَا النَّاسُ عَلَيَّ، أَتُرُونَ أَنْ نَمِيلَ عَلَى عِيَالِهِمْ وَذَرَارِيَّ هَؤُلَاءِ، الَّذِينَ يُرِيدُونَ أَنْ يَصُدُّوَنَا عَنِ النَّبِيِّ؟»

"Nipeni ushauri, enyi watu! Mnaonaje kwamba tuzishambulie familia na dhuriya wao hao wanaotaka kutuzuia kufika kwenye Nyumba Tukufu (Al-Kaaba)?"

Katika matamshi mengine,

«[أ]تُرُونَ أَنْ نَمِيلَ عَلَى ذَرَارِيَّ هَؤُلَاءِ الَّذِينَ أَعَانُوهُمْ، فَإِنْ يَأْتُونَنَا كَانَ اللَّهُ فَذَقَطَعَ عُنُقًا مِنَ الْمُشْرِكِينَ، وَإِلَّا تَرَكْنَاهُمْ مَحْزُونِينَ»

"Mnadhani kwamba tuzishambulie familia za hao waliowasaidia. Na wakitujia, basi Allah Atakuwa Amezivunja shingo za washirikina. Vinginevyo, tutawaacha na watakuwa ni wenye kuhuzunika."

«فَإِنْ قَعَدُوا قَعَدُوا مُؤْتَرِبِينَ مَجْهُودِينَ مَحْزُونِينَ، وَإِنْ نَجَّوْا يَكُنْ عُنُقًا قَطَمَهَا اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ. أَمْ تَرُونَ أَنْ نُؤَمَّ النَّبِيَّ فَمَنْ صَدَّنَا عَنْهُ فَأَتَلْنَا»

"Wakibakia (katika mahali walipokusanyika) watakaa wakiwa na fedheha, wamechoka na wamehuzunika. Kama watazinusuru familia zao, basi itakuwa kwamba shingo zao zimekatwa na Allah. Ama mnadhani tuelekee katika Nyumba Tukufu (Al-Ka`aba), na watakaotuzuia, tutapigana nao."

Abubakr رضي الله عنه akasema: "Ewe Mjumbe wa Allah ﷺ! Umetoka kwa makusudio ya Nyumba hii, ukiwa hutaki kupigana vita na yeyote, basi ielekee, na atakayetuzuia, tutapigana naye." Katika riwaya nyingine, Abubakr رضي الله عنه

¹ Makabila yaliyoishi katika viunga vya Makkah.

akasema: "Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ wanajua zaidi, kwa hakika! Tulikuja kufanya 'Umrah, (Hija ndogo) si kupigana na yeyote, lakini atakayezuia baina yetu na Ka'aba (nyumba tukufu ya Allah تعالى) tutapigana naye." Mtume ﷺ akasema:

«فَرُّوْهُرَا اِذْنُ»

"Basi nendeni."

Katika tamshi jingine,

«فَامُضُّوْا عَلٰى اِسْمِ اللّٰهِ تَعَالٰى»

"Basi nendeni kwa Jina la Allah Taala."

Mpaka walipokuwa katika baadhi ya njia, Mtume ﷺ akasema:

«اِنَّ خَالِدَ بْنَ الْوَلِيْدِ فِيْ خَيْلٍ لِّقُرَيْشٍ طَلِيْعَةٌ، فَخُدُوْا ذَاتَ الْاَيْمِيْنَ»

"Hakika Khalid bin Al-Waliyd anaongoza kikosi cha askari farasi wa Kikuraishi akiwa katika mstari wao wa mbele, basi, tumieni njia ya upande wa kulia."

Basi, Wallahi, Khalid hakutambua kuingia kwa Waislamu, mpaka wakakutana na vumbi la jeshi la Waislamu, akarudi mbio kuwaonya Makuraishi. Mtume ﷺ akaenda, mpaka alipofika Thaniyyah (njia ya mlimani) ambayo ingeweza kumfikisha, ngamia wa Mtume akapiga magoti. Watu wakasema, 'Hima hima!' lakini akatulia mahala pake. Basi, wakasema: 'Al-Qaswaa analeta usumbufu, Al-Qaswaa analeta usumbufu.' Mtume ﷺ akasema:

«مَا خَلَّاتِ الْقِسْوَاءُ وَمَا دَاكَ لَهَا بِخُلُقِيْ، وَلَكِيْنَ حَبَسَهَا حَابِسُ النَّبِيْلِ»

"Al-Qaswaa hajawahi kusumbua, na hiyo si tabia yake, lakini amemzuia Yule Ambaye Alimzuia ndovu."

Halafu, akasema:

«وَالَّذِيْ نَفْسِيْ بِيَدِهِ! لَا يَسْأَلُوْنِيْ خُطَّةً يُعْظَمُوْنَ فِيْهَا حُرْمَاتِ اللّٰهِ تَعَالٰى اِلَّا اَعْطَيْتُهُمْ
اِيَّاهَا»

*“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake!
Hawataniomba kitu chochote ambacho watatukuza nacho matukufu
ya Allah, isipokuwa nitawapatia.”*

Kisha, akamkemea ngamia, akasimama, na Mtume ﷺ akabadili mwelekeo, mpaka akateremka katika sehemu ya mbali zaidi katika Hudaybiyyah katika shimo lililokuwa na maji machache ambayo watu huyatumia kwa kiasi kidogo. Baada ya muda mfupi, watu waliyamaliza maji hayo, wakalalamika kiu kwa Mtume ﷺ. Akachomoa mshale, akawaamuru kutia maji ndani yake. Basi, Wallahi! Hakikuacha kububujisha maji, mpaka watu wote wakakata kiu yao na wakatoshika.

Wakiwa bado katika hali hiyo, alikuja Budayl bin Warqaa Al-Khuza'i, alikuja pamoja na baadhi ya watu wa kabila lake, Al-Khuza'ah. Walikuwa ni washauri wa Mtume ﷺ, na ni watu waliokuwa wakiishi Tihamah.¹ Budayl akasema: “Mimi nimemuacha Ka'b bin Luayy, na 'Amir bin Luayy wakiwa wamepiga kambi katika sehemu yenye maji mengi ya Hudaybiyyah. Walikuwa pamoja na ngamia wa maziwa, na wao wamejiandaa kupigana vita dhidi yako na kukuzuia dhidi ya Nyumba Tukufu (Al-Kaaba). Mtume ﷺ akasema:

«إِنَّا لَمْ نَجِءَ لِقِتَالِ أَحَدٍ، وَلَكِنْ جِئْنَا مُتَعَمِّرِينَ، وَإِنْ قُرَيْنَا قَدْ نَهَكْتَهُمُ الْحَرْبُ،
وَأَضْرَتْ بِهِمْ، فَإِنْ شَاؤُوا مَادَدْتُهُمْ مُدَّةً وَيُحْلُوا بَيْنِي وَبَيْنَ النَّاسِ، فَإِنْ أَظْهَرُوا، فَإِنْ
شَاءُوا أَنْ يَدْخُلُوا فِيمَا دَخَلَ فِيهِ النَّاسُ فَعَلُوا، وَإِلَّا فَقَدْ جَمَّوْا، وَإِنْ هُمْ أَبَوْا
فَوَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَأَقَابِلَنَّاهُمْ عَلَى أَمْرِي هَذَا حَتَّى تَنْفِرَ سَالِقَتِي أَوْ لِيُنْفِرَنَّ اللَّهُ
أَمْرُهُ»

*“Sisi hatukuja kupigana na yeyote, bali tumekuwa kwa ajili ya kufanya
'Umrah (hija ndogo). Kwa hakika, vita vimewadhoofisha Makuraishi
na wamepata khasara kubwa. Kwa hivyo, wakitaka nitawapa muda
(mkataba) ambapo wataniacha huru baina yangu na watu.
Nikishinda, wakitaka wataingia (katika Uislamu), katika yale
waliyoyaingia watu. Vinginevyo, watakuwa wamejumuika kwa ajili
ya kupigana. Na kama watakataa, basi, naapa kwa Ambaye nafsi*

¹ Sehemu kadiri ya masafa ya maili sabini na mbili Magharibi mwa Al-Madinah.

yangu iko Mkononi Mwake nitapigana nao juu ya jambo langu hili, mpaka niuawe, au Allah Apatishe Amri Yake."

Budayl akasema: 'Nitawapa habari za hayo unayoyasema.' Akaenda mpaka akawafikia Makuraishi, akawaambia: 'Sisi tumekuja kutokea kwa mtu huyu, na tumemsikia akitoa kauli ambayo, mkitaka tukwambieni, tutafanya hivyo.' Wapumbavu wao wakakataa kuwa: 'Hatuna haja ya nyinyi kutupa habari yoyote kutoka kwake.' Hata hivyo, waliokuwa na busara miongoni mwao walisema: 'Yalete uliyoyasikia kutoka kwake.'" Akaeleza, kwamba nilimsikia akisema kadha wa kadha. Akawasimulia aliyoyasema Mtume ﷺ. Urwah bin Mas'ud رضي الله عنه akasimama na kuuliza: "Enyi watu! Nyinyi si wazazi?" Wakasema: "Ndiyo." Akaongeza: "Mimi si mtoto?" Wakasema: "Ndiyo." Akasaili: "Mnaituhumu jambo?" Wakasema: "Hapana." Akahoji tena: "Je, mnajua kwamba nimewaita watu wa 'Ukkaz kwa ajili ya kukusaidieni, na walipokataa, nikawaleteeni ahali na jamaa zangu na watoto, pamoja na walionitii?" Wakasema: "Ndiyo." Akasema: 'Mtu huyu amekuleteeni pendekezo zuri, ni vyema mkalikubali, na mniruhusu nikutane naye.' Wakamuambia: 'Kakutane naye.'

Akamjia na kuanza kuzungumza naye. Mtume ﷺ akamuambia kama alivyomuambia Budayl bin Waraqaa. Baada ya hayo, 'Urwah akasema: 'Ewe Muhammad! Hupati mashaka yoyote kwa kuhatarisha uhusiano wako? Je, umewahi kumsikia Mwarabu yeyote wa kabla yako anayeangamiza mahusiano yake?' Kama ni vinginevyo, basi mimi, Wallah! Mimi sioni nyuso zenye hadhi hapa, bali, nawaona watu wa makabila mbalimbali wakikimbia na kukuacha wewe peke yako.' Abubakr رضي الله عنه akamuambia: 'Nenda kanyonye maziwa ya Latah!, Sisi tukimbie tumuache?' 'Urwah akauliza: 'Ni nani huyu?' Wakamjibu: 'Ni Abubakr رضي الله عنه.' Akamuambia Abubakr رضي الله عنه, 'Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Ingekuwa si fadhila ulizonifanyia ambazo siwezi kuzilipa, ningekujibu.' Akaendelea kumuambia Mtume ﷺ huku akizishika ndevu za Mtume wakati wa kuzungumza kwake, huku Mughirah bin Shu'bah akiwa amesimama karibu na kichwa cha Mtume ﷺ, na akiwa na upanga na juu yake (kichwani) akiwa na kofia ya vita. Kila mara 'Urwah alipounyoosha mkono wake kwenye ndevu za Mtume ﷺ, Mughirah aliupiga kwa mpini wa upanga na kumuambia: 'Ondoa mkono wako mbali na Mtume ﷺ.' 'Urwah akainua kichwa chake na kusaili: 'Huyu ni nani?' Akamjibu: "Ni

Mughirah bin Shu'bah.' Akasema: 'Ewe msaliti, je, sifanyi vyema kuondosha madhara ya usaliti wako?'

Katika zama za Ujahili, Mughirah bin Shu'bah alikuwa sahibu wa kaumu hiyo. Akaua na kuchukua mali zao, akaja Madinah na kusilimu. Mtume ﷺ akasema:

«أَمَّا الْإِسْلَامُ فَأَقْبَلُ، وَأَمَّا الْمَالُ فَلَسْتُ مِنْهُ فِي شَيْءٍ»

"Ama Uislamu, nakubali, ama kuhusu mali, sichukui chochote kutokana nayo."

Kisha, "Urwah akaanza kuwatazama Masahaba wa Mtume ﷺ, akasema: 'Wallahi! Mtume hajatema kohozi lolote isipokuwa, huangukia katika kiganja cha mmojawapo miongoni mwao, ambaye hulipangusia usoni mwake na katika ngozi yake, na anapowaamuru huharakisha amri yake, na anapotawadha hukaribia kuuana kwa ajili ya kugombania maji ya udhu wake, na anapooonea, hushusha sauti zao, na hawamkazii macho usoni kwa sababu ya kumuadhimisha." 'Urwah akarejea kwa watu wake na kusema: 'Enyi watu! Wallahi! Nimewahi kupeleka ujumbe kwa wafalme, na kuongoza ujumbe kwa Kisra, Kaisar na Najjash. Wallahi!, Kamwe sijapata kumuona Mfalme anayeheshimiwa na watu wake kama jinsi Masahaba wa Muhammad wanavyomuheshimu Muhammad. Wallahi! Akitema kohozi, huangukia mkononi mwa mmoja wao na kulisugua usoni na katika ngozi yake, na anapowaamuru jambo, hulitekeleza haraka, akitawadha hukaribia kuuana kwa kugombania maji ya udhu wake, anapozungumza, basi wao hushusha sauti zao mbele yake, wala hawamkazii macho yao, kwa wanavyomuadhimisha. Hakika yeye amekuleteeni pendekezo zuri, basi lipokeeni.'

Mtu mmoja kutoka kabila la Banu Kinanah akasema: 'Niruhusuni nimuendee.' Wakamkubalia: 'Muendee.' Alipotokeza kwa Mtume ﷺ na masahaba zake, Mtume ﷺ akasema:

«هَذَا فُلَانٌ وَهُوَ مِنْ قَوْمٍ يُعْظَمُونَ الْبَدَنَ فَاْبَعَثُوا لَهُ»

"Huyu ni fulani, ambaye anatoka kwa watu wanatukuza wanyama wa dhabihu, basi waleteni mbele yake."

Wakaletwa, na watu wakawapokea huku wakisoma Talbiyah. Alipoyaona hayo, akasema: 'Subhanallah! Wale hawatakiwi kuwazuia Nyumba Tukufu (Al-

Kaabah).’ Aliporudi kwa jamaa zake, aliwaambia: ‘Nimeona wanyama wakiwa wamekutwa na alama, basi sioni haja ya kuzuiliwa Nyumba Tukufu (Al-Kaabah).’ Mtu mmoja kati yao, aliyetitwa Mikraz bin Hafis akasimama na kusema: ‘Niruhusuni nimuendee.’ Wakamuambia: ‘Muendee.’ Alipowakaribia, Mtume ﷺ akasema:

«هَذَا مِكْرَزٌ وَهُوَ رَجُلٌ فَاجِرٌ»

“Huyu ni Mikraz, ambaye ni mtu mwovu.”

Mikraz alianza kumueleza Mtume ﷺ. Akiwa katikati ya mazungumzo, Suhayl bin ‘Amr alikuja.”

Ma’mar alisema, Ayyub amenieleza kuwa ‘Ikrimah alisema: “Baada ya Suhayl bin ‘Amr kuja, Mtume ﷺ alisema:

«قَدْ سَهَّلَ لَكُمْ مِنْ أَمْرِكُمْ»

“Sasa, jambo lenu limekuwa sahali.”

Az-Zuhri رحمه الله تعالى alieleza katika Hadithi yake: “Akaja Suhayl bin ‘Amr, amesema: “Andika mkataba baina yetu na wewe.” Mtume ﷺ akamuita ‘Ali رضي الله عنه na akamuambia:

«اَكْتُبْ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ»

“Andika: ‘Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwingi wa Kurehemu.’”

Suhayl akasema: “Ama hakika, mimi, Wallah! *Ar-Rahman* sijui ni nani, bali andika hivi: ‘Kwa Jina Lako, ewe Allah تعالی,’ kama mlivyokuwa mkiandika zamani. Waislamu wakasema: “Wallah! Hatutaandika, isipokuwa, ‘Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwingi wa Kurehemu.’” Mtume ﷺ akasema:

«اَكْتُبْ بِاسْمِكَ اللّٰهُمَّ»

“Andika: ‘Kwa Jina Lako, ewe Allah.’”

Halafu, akasema:

«هَذَا مَا قَاضَىٰ عَلَيْهِ مُحَمَّدٌ رَّسُولُ اللّٰهِ»

“Huu ni mkataba wa amani ambao, Muhammad, Mjumbe wa Allah ameupitisha.”

Suhayl akasema: "Wallah! Kama sisi tungekuwa tunajua kwamba wewe ni Mtume, tusingekuzuia dhidi ya Nyumba ya Allah ﷻ wala tusingepigana nawe, bali, andika, Muhammad bin 'Abdullah." Mtume ﷻ akamuambia:

«وَاللّٰهُ اِنِّي لَرَسُوْلٌ اَللّٰهُ وَاِنْ كَذَّبْتُمْوَنِيْ، اَكْتُبْ مُحَمَّدٌ بِنُ عَبْدِ اَللّٰهِ»

*"Wallah! Mimi ni Mjumbe wa Allah, hata kama mnanikanusha.
Andika Muhammad bin 'Abdullah."*

Az-Zuhri رحمه الله تعالى alisema, haya ni kutokana na kauli yake, "Mtume ﷻ aliyakubali yote hayo, kwani alishasema kuwa angekubali chochote ambacho watamtukuza Allah تعالى." Mtume ﷻ akamuambia:

«عَلَىٰ اَنْ تُخَلُّوْا بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْبَيْتِ فَنَطُوْفٌ بِهٖ»

"Kwa sharti kwamba mtuachilie baina yetu na Ka'aba ili tuweze kutufu - Kuzunguka Ka'aba"

Suhayl akajibu: "Wallah! Hatutafanya hivyo, ili Waarabu wasiseme tumelazimishwa, lakini hilo tutakuruhusuni mwakani." Akaandika, halafu Suhayl akasema: "Asikujie mtu wetu yeyote, hata kama ni mfuasi wa dini yako, isipokuwa umrudishe kwetu." Waislamu wakasema: "Subhanallah! Atarudishwa vipi kwa washirikina, ilhali amekuja akiwa Muislamu?"

Huku wangali katika hali hiyo, aliwajia Abu Jandal bin Suhayl bin 'Amr رضي الله عنه alikuja kutokea katika bonde la Makkah, akiyumbayumba na minyororo yake na akajitupa baina ya Waislamu. Suhayl akasema: "Ewe Muhammad! Huu ndio mwanzo wa mkataba wetu, hivyo, huyu mtu utamrudisha kwetu."

Mtume ﷻ akasema:

«اِنَّا لَم نَقْضِ الْكِتَابَ بَعْدُ»

"Mkataba hatujauandika bado."

Akasema: "Basi, Wallah! Kamwe, sitaandikiana na wewe, mkataba wowote wa amani." Mtume ﷻ akasema:

«فَاَجْزُهُ لِيْ»

"Muachilie aje kwangu."

Suhayl akajibu: "Mimi sitaliachilia hilo jambo kwako." Mtume ﷺ akasema:

«بَلَىٰ فَاَفْعَلْ»

"Kwanini! Fanya hivyo."

Akamjibu: "Sifanyi." Mikraz akasema: "Ndiyo, tumeshapitisha Mkataba." Abu Jandal رضي الله عنه akasema: "Enyi kundi la Waislamu! Narudishwa kwa washirikina, ilhali nimekuja huku nikiwa ni Muislamu, hamu yao ni niliyokutana nayo?" Alikuwa ameteswa vikali kabisa juu ya Allah تعالى.

'Umar رضي الله عنه amesema: "Nikamuendea Mtume ﷺ na kumuambia: "Wewe si Mjumbe wa kweli wa Allah?" Mtume ﷺ akanijibu:

«بَلَىٰ»

"Ndiyo." Nikauliza tena: "Je, sisi si ndio tulio katika ukweli, na adui yetu katika upotevu?" Akajibu:

«بَلَىٰ»

"Ndiyo." Nikauliza tena: "Basi, ni kwa nini tujidhalilisha Dini yetu?" Mtume ﷺ akasema:

«إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ وَلَسْتُ أَغْصِيهِ وَهُوَ نَاصِرِي»

"Hakika mimi ni Mjumbe wa Allah wala simuasi, na Yeye ni Mwenye Kuninusuru."

Nikauliza: "Je, hukuwa ukituambia kwamba tutakwenda katika Nyumba na kutufu "kuzunguka" humo?" Akajibu:

«بَلَىٰ أَفَأَخْبِرْتُكَ أَنَّا نَأْتِيهِ الْعَامَ؟»

"Ndiyo, lakini, je, nilikuambieni kwamba sisi tunaiendea mwaka huu?"

Nikajibu: "Hapana." Mtume ﷺ akasema:

«فَإِنَّكَ آتِيهِ وَمُطَوَّفٌ بِهِ»

"Basi, utaiendea na utatufu."

'Umar رضي الله عنه aliendelea kueleza: Basi nikamuendea Abubakr رضي الله عنه na kumuambia, "Ewe Abu Bakr! Kwani huyu si Nabii wa kweli wa Allah?" Akajibu:

“Ndiyo.” Nikauliza: “Kwani sisi hatuko katika ukweli, na adui yetu katika upotevu?” Akajibu: “Ndiyo.” Nikasema: “Basi, ni kwanini tunajidhalilisha katika Dini yetu.” Akasema: “Ewe Mtu, ni Mtume, wala yeye hamuasi Mola wake, na Yeye Atamnusuru, kwa hivyo shikamana naye, kwani, Wallahi! Yeye yuko katika ukweli.” Nikasema: “Kwani hakuwa akitueleza kwamba tutaijia Ka’aba na kutufu?” Akajibu: “Ndiyo, kwani alikuambia kwamba utaiendea mwaka huu?” Nikajibu: “Hapana.” Akasema: “Basi, iendelee na ukatufu.” Zuhri رحمه الله تعالى alieleza: “‘Umar رضي الله عنه alisema, ‘basi nikafanya amali nyingi njema (kwa ajili ya kufutiwa maswali yasiyofaa niliyouliza).”

Baada ya kumalizika kuandikwa kwa mkataba wa amani, Mtume ﷺ aliwaambia Masahaba wake:

«قَوْمُوا فَأَنْحَرُوا ثُمَّ اخْلِقُوا»

“Simameni mchinje, kisha mnyoe.”

Akaendelea kusema: “Wallah! Hakusimama yeyote katika wao, mpaka akayakariri hayo mara tatu. Baada ya kutosimama yeyote katika wao, Mtume ﷺ aliwaacha na kuingia kwa Umm Salamah رضي الله عنها. Akamuambia walichofanya watu. Ummu Salamah رضي الله عنها akamuuliza, “Ewe Nabii wa Allah! Unayapenda hayo?” Toka, wala usimsemeshe yeyote katika wao, na umchinje mnyama wako, na umuite kinyozi wako akunyoe.” Mtume ﷺ akafanya hivyo. Watu walipoona hivyo, walisimama, wakachinja, wakaanza kunyoana wao kwa wao. Walifanya haraka na kuhuzunika mpaka wakakaribia kuuana. Kisha wakaja wanawake Waumini. Allah تعالى Akateremsha Aya:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا جَاءَكُمْ الْمُؤْمِنَاتُ

“Enyi mlioamini! Wakikujilieni wanawake Waumini...” (60:10) mpaka,

بِعَصِمِ الْكَوَافِرِ

“Msiwarudishe kwa Makafiari”

Basi, siku hiyo, ‘Umar رضي الله عنه aliwapa talaka wakeze wawili ambao walikuwa katika ushirikina. Mmoja wao akaolewa na Mu’awiyah bin Abu Sufyan, na mwingine aliolewa na Swaf-waan bin Umayyah.

Mtume ﷺ akarejea Madinah, akajiwa na Abu Baswiir رضي الله عنه, kutoka kwa Makuraishi, akiwa amesilimu. Makuraishi wakawatuma watu wawili kumfuatilia. Wakasema: "Shikilia ahadi uliyotupa." Akawapa, na wakaondoka naye, mpaka wakafika Dhul-Hulayfah. Wakapiga kambi ili kula tende zao. Abu Baswiir رضي الله عنه akamuambia mmojawapo kati ya watu hao wawili: "Wallahi! Ewe fulani, mimi naona upanga wako huu ni mzuri sana." Mwenzake akauchomoa wa kwake na kusema, "Ndiyo, ni mzuri, nami nilishujaribu mara kadha." Abu Baswiir رضي الله عنه akasema: "Hebu niuangalie." Alipompa, alimpiga nao na kumuua. Mwenzake akakimbilia Madinah na kuingia mbio msikitini. Mtume ﷺ alipomuona, alisema:

«لَقَدْ رَأَىٰ هَذَا دُغْرًا»

"Mtu huyu ameona kitisho."

Alipofika kwa Mtume ﷺ, alisema: "Wallahi! Sahibu yangu kauawa, nami ningeuawa pia." Akaja Abu Baswiir na kusema: "Ewe Mtume ! Wallahi! Allah تعالى Ametimiza wajibu wako, umenirudisha kwao, kisha Allah تعالى Akaniokoa dhidi yao." Mtume ﷺ akasema:

«وَيْلٌ أُمَّوٍ وَسَعَرَ حَرْبٍ لَوْ كَانَ مَعَهُ أَحَدٌ»

"Ole wake mama yake! Angelikuwa mchocheaji wa vita, iwapo angelikuwa pamoja na mtu mwingine."

Alipoyasikia hayo, alijua kwamba Mtume ﷺ atamrudisha kwao. Akaondoka, mpaka akafika ufukweni mwa bahari. Abu Jandal bin Suhayl رضي الله عنه naye alijiondoa kwa washirikina, akakutana na Abu Baswiir. Ikawa kwamba, hapana mtu anayesilimu na kutoka kwa Makuraishi, isipokuwa aliungana na Abu Baswiir رضي الله عنه, mpaka wakakusanyika kundi lenye nguvu. Basi, Wallahi! Walikuwa hawausikii msafara wa Makuraishi uliotoka kwenda Sham, isipokuwa waliusimamisha, wakawaua na kuchukua mali zao. Makuraishi wakatuma ujumbe kwenda kwa Mtume ﷺ wakimuomba kwa ajili ya Allah تعالى na undugu kwamba awatumie ujumbe (Abu Baswiir na wenzake), yeyote atakayetoka kwao na kumuendea Mtume, atakuwa yuko katika amani. Mtume ﷺ akawatumia ujumbe. Allah تعالى Akateremsha Aya:

«وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ

"Na Yeye Ndiye Aliyezuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka..." mpaka,

حَمِيَّةَ الْجَاهِلِيَّةِ

“...hasira za kijinga...”

Hasira zao ni kuwa, hawakukubali kwamba yeye ni Mtume ﷺ wala kuikubali *Bismillahir Rahmanir Rahim*, na wakawazuia Waislamu kuiendea Nyumba Tukufu “Ka’bah.”¹ Haya ni masimulizi ambayo Bukhari aliyakusanya katika mlango wa Tafsiri,² na chini ya mlango wa Umrat Al-Hudaybiyyah,³ na katika mlango wa Hajj na kadhalika.⁴ Allah تعالى Ndiye Pekee wa Kuombwa msaada, na Kutegemewa ni Kwake tu, wala hapana hila wala nguvu isipokuwa kutoka kwa Allah تعالى, Mwingi wa Hikima.

Bukhari amenukuu katika mlango wa Tafsir kwamba Habib bin Abu Thabit amesema: Nilikuja kwa Abu Waail kumuuliza jambo, akajibu: “Tulikuwa mahali palipoitwa Swiffin, mtu mmoja akasema, ‘Je huwaoni wale wanaolingania kwenda katika Kitabu cha Allah?’ ‘Ali bin Abu Twalib رضي الله عنه akajibu: ‘Ndiyo.’ Sahl bin Hunayf akasema: ‘Msizitegemee rai kwa kuwa hazifai. Katika siku ya Hudaybiyyah, ambapo mkataba wa amani uliwekwa baina ya Mtume ﷺ na washirikina, tungelipata fursa ya kupigana, tungelifanya hivyo.” “Akaja ‘Umar رضي الله عنه na kusema: ‘Je sisi hatuko katika haki, na wao wako katika batili? Je maiti wetu si wa kwenda Peponi na maiti wao ni wa Motoni?’ Akajibu: ‘Ndiyo.’ Akasema ‘Basi ni kwa vipi tunajidhalilisha katika Dini yetu? Na tunarejea, ilhali, bado Allah تعالى Hajahukumu baina yetu sisi na wao?’ Mtume ﷺ akajibu:

«يَا ابْنَ الْخَطَّابِ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ وَلَنْ يُضَيِّعَنِي اللَّهُ أَبَدًا»

“Ewe Mwana wa Al-Khattwaab! Mimi ni Mjumbe wa Allah, wala Allah Hatanipoteza kamwe.”

‘Umar رضي الله عنه akarejea akiwa amekasirika, mpaka alipokuja Abubakr رضي الله عنه alisema: ‘Ewe Abu Bakr! ‘Je sisi hatuko katika haki, na wao wako katika batili?’ Abubakr رضي الله عنه akamjibu: ‘Ewe Mwana wa Khattab! Yeye ni Mtume ﷺ, wala Hatampoteza kamwe.’ Ikateremka *Surat Al-Fat-h*.” Bukhari aliinukuu tena katika sehemu nyingine, na Muslim na An-Nasai kupitia isnadi

¹ *Fat’h Al-Bari* 5:388.

² *Fat’h Al-Bari* 8:451.

³ *Fat’h Al-Bari* 7:518.

⁴ *Fat’h Al-Bari* 3:634.

kadha, kutoka kwa Abu Waail, Sufyan bin Salamah, kutoka kwa Sahl bin Hunayf. Baadhi yake, zina matamshi haya: “Enyi watu! Msizitegemee rai kuwa hazifai. Katika siku ambayo Abu Jandal رضي الله عنه alikuja, nilijiona nikitaka kuikataa amri ya Mtume ﷺ, kama ningelikuwa na fursa.” Katika masimulizi mingine: “Ikateremka *Surat Al-Fat-h*. Mtume ﷺ akamuita ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه, akamsomea.”¹

Imamu Ahmad alimnukuu Anas رضي الله عنه kuwa alisema: “Makuraishi waliwekeana mkataba wa amani na Mtume ﷺ. Kwa wakati huo, Suhayl bin ‘Amr alikuwa miongoni mwa washirikina. Mtume ﷺ alimuambia ‘Ali رضي الله عنه,

«اَكْتُبْ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ»

“Andika, ‘Bismillahir Rahmanir Rahim.’”

Suhayl akasema: “Sisi hatujui ni nini ‘Bismillahir Rahmanir Rahim’. Lakini andika [tunachokifahamu], ‘Kwa Jina lako ewe Allah تعالی.’” Mtume ﷺ akasema:

«اَكْتُبْ مِنْ مُحَمَّدٍ رَسُولِ اللَّهِ»

“Andika, ‘Kutoka kwa Muhammad, Mjumbe wa Allah.’”

Akasema: “Lau kama tungelijua kuwa wewe ni Mtume, tungelikufuata, lakini andika jina lako na la baba yako.” Mtume ﷺ akasema:

«اَكْتُبْ مِنْ مُحَمَّدِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ»

“Andika, ‘Kutoka kwa Muhammad bin ‘Abdullah.’”

Wakampa sharti Mtume ﷺ kwa kumuambia, “Yeyote atakayekuja kutokea kwenu hatutamrudisha kwenu, na atayewajieni kutokea kwetu, mrudisheni.” ‘Ali رضي الله عنه akauliza: “Ewe Mtume! Je tuliandike hili?” Mtume ﷺ akamjibu:

«نَعَمْ، إِنَّهُ مِنْ ذَهَبٍ مِثًا إِلَيْهِمْ فَأَبْعَدَهُ اللَّهُ»

“Ndiyo. Kwa hakika, wale watakaondoka kwetu na kwenda kwao, basi Allah Awaweke mbali.”² Muslim pia aliikusanya Hadithi hii.³

¹ *Fat’h Al-Bari* 8:451.

² Ahmad 8:268.

³ Muslim 3:1411.

Imamu Ahmad alinukuu tena, kutoka kwa 'Abdullah bin 'Abbas رضي الله عنه, kuwa alisema: "Pindi Al-Haruriyyah alipoasi, waliwaandalia kambi tofauti, nikawaambia, Mtume ﷺ alikubali kuwekeana mkataba na washirikina. Alimuambia 'Ali رضي الله عنه:

«اَكْتُبْ يَا عَلِيُّ، هَذَا مَا صَلَّحَ عَلَيْهِ مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ»

"Andika ewe 'Ali, haya ndiyo aliyokubaliana nayo Muhammad, Mjumbe wa Allah."

Washirikina wakasema: "Lau kama tungelijua kuwa wewe ni Mjumbe wa Allah, tusingepigana nawe." Mtume ﷺ akasema:

«امْحُ يَا عَلِيُّ، اللَّهُمَّ إِنَّكَ تَعْلَمُ أَنِّي رَسُولُكَ، امْحُ يَا عَلِيُّ وَارْتَضِ: هَذَا مَا صَلَّحَ عَلَيْهِ مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ»

"Ifute ewe 'Ali. Eee Allah! Hakika Wewe unajua kwamba mimi ni Mjumbe Wako. Futa ewe 'Ali, na uandike hivi: Haya ndiyo aliyokubaliana nayo Muhammad bin 'Abdullah."

Wallah! Mtume ﷺ ni mbora zaidi kuliko 'Ali رضي الله عنه, na amefuta mahali pa cheo chake, hata hivyo, kufuta cheo chake haikumaanisha kuwa umefutwa Utume wake. Wakasema, 'Ndiyo.'"¹ Abu Dawud pia, alinukuu masimulizi sawa na haya.²

Imam Ahmad alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema: "Katika siku ya Hudaybiyyah, Mtume ﷺ alichinja wanyama sabini, akiwemo Ngamia aliyekuwa wa Abu Jahl. Ngamia alipozuiliwa kwenda katika Nyumba, alilia kama aliavyo pindi anapomuona mwanawe."³

لَقَدْ صَدَقَ اللَّهُ رَسُولَهُ الرُّؤْيَا بِالْحَقِّ لَتَدْخُلُنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ
ءَامِنِينَ مُحَلِّقِينَ رُءُوسِكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا تَخَافُونَ فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا فَجَعَلَ مِنْ دُونِ
ذَلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿٧٧﴾ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظَاهِرَهُ عَلَى
الدِّينِ كُلِّهِ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٧٨﴾

¹ Ahmad 1:342.

² Abu Dawud 3:317.

³ Ahmad 1:314.

27. "Hakika Mwenyezi Mungu Amemtimizia Mtume Wake ndoto ya haki. Bila ya shaka nyinyi mtauingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, kwa amani, na hali mmenyoa vichwa vyenu na mmepunguza nywele. Hamtakuwa na khofu. Yeye Anajua msiyoyajua. Basi Atakupeni kabla ya haya Ushindi karibuni."

28. "Yeye Ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa uwongofu na Dini ya Haki, ili Aitukuze juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Shahidi."

Kubainisha Ukweli wa Ndoto ya Mtume ﷺ

Mtume ﷺ aliona usingizini kuwa ameingia Makkah na kufanya tawafu katika Nyumba ya Allah تعالى (Ka'aba). Akawasimulia hilo Masahaba wake akiwa Madinah. Pindi walipoelekea Makkah, katika siku ya Hudaybiyah, hapana yeyote miongoni mwao, aliyekuwa na mashaka kwamba ndoto ya Mtume ﷺ itakuwa kweli katika mwaka huo.

Baada ya kadhia ya mkataba, na mwaka huo wakarejea kwa maagano kuwa warudi katika mwaka uliofuata, baadhi ya Masahaba hawakuyapenda hayo, hadi 'Umar bin Khattab رضي الله عنه akauliza juu ya jambo hilo. Miongoni mwa maswali aliyoyatoa ni: "Je, haukuwa ukitueleza kuwa tutaiendea Ka'aba na kufanya Tawafu?" Akamjibu,

«بَلَىٰ أَفَأَخْبِرُكَ أَنْتَ تَأْتِيهِ عَامُكَ هَذَا؟»

"Ndiyo, lakini je, nilikujulisha kuwa utakwenda katika mwaka huu?"

Akajibu: "Hapana." Mtume ﷺ akasema,

«فَإِنَّكَ آتِيهِ وَمُطَوِّفٌ بِهِ»

"Kwa hakika utakwenda na kufanya Tawaf hapo."

Umar رضي الله عنه alipokea jibu sawa na hilo kutoka kwa Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه, neno kwa neno.¹ Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

¹ Fat'h Al-Bari 5:390.

لَقَدْ صَدَقَ اللَّهُ رَسُولَهُ الرُّؤْيَا بِالْحَقِّ لَتَدْخُلُنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ إِن شَاءَ اللَّهُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Amemtimia Mtume Wake ndoto ya haki. Bila ya shaka nyinyi mtauingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah...”

Hii ni katika kuithibitisha habari na kuipa nguvu, wala si katika kuiondolea chochote. Kauli ya Allah تعالى:

ءَامِنِينَ

“...kwa amani...” Maana: Wakati wa kuingia kwenu. Kauli ya Allah تعالى:

مُخْلِفينَ رُءُوسِكُمْ وَمُقْصِرِينَ

“...na hali mmenyoa vichwa vyenu na mmepunguza nywele.”

Walikuwepo katika wao, walionyoo na waliopunguza nywele zao. Iliandikwa ndani ya Sahih Mbili kwamba Mtume ﷺ alisema:

«رَجِمَ اللَّهُ الْمُخْلِفينَ»

“Allah Awarehemu wenye kunyoo nywele.”

Wakasema: “Ewe Mtume ﷺ! Na wenye kuzipunguza.” Mtume ﷺ akasema:

«رَجِمَ اللَّهُ الْمُخْلِفينَ»

“Allah Awarehemu wenye kunyoo.”

Wakasema tena: “Ewe Mjumbe wa Allah! Na wenye kuzipunguza.” Mtume ﷺ akarudia kusema:

«رَجِمَ اللَّهُ الْمُخْلِفينَ»

“Allah Awarehemu wenye kunyoo.”

Wakasema: “Ewe Mtume! Na wenye kuzipunguza.” Mtume ﷺ akasema (katika mara ya tatu au ya nne):

«وَالْمُقْصِرِينَ»

“Na wenye kupunguza.”¹

¹ Fat'h Al-Bari 3:656, Muslim 2:946.

Kauli ya Allah تعالى:

لَا تَخَافُونَ

“Hamtakuwa na khofu..”

Allah تعالى Aliwathibitishia kuwepo amani wakati wa kuingia, Akawaondolea khofu wakati wa kuwepo kwao katika mji huo. Hawatamkhofu yeyote. Haya yalitokea katika Hija ndogo ‘Umrah” iliyofanywa katika mwaka uliofuatia, mwaka wa saba baada ya Al-Hijrah.

Mtume ﷺ aliporejea kutoka Hundaybiyyah, katika mwezi wa *Dhul-Qa’dah*, (mfungo pili) mwaka wa sita baada ya Hijrah. Akakaa huko Madinah, mwezi wa *Dhul-Hijah* (mfungo tatu) na *Muharram* (mfungo nne). Katika mwezi wa *Swafar* (mfungo tano) alikwenda Khaybar. Allah تعالى Akamfungulia mji huo, baadhi yake kwa nguvu, na baadhi kwa watu kujisalimisha kwake. Khaybar lilikuwa jimbo kubwa lililokuwa na wingi wa mitende na mazao. Mtume ﷺ aliwaweka baadhi ya Mayahudi waliokuwepo huko kushughulikia sehemu ya mashamba kwa masharti na sehemu ya jimbo iliyosalia iligawanywa kwa wale tu walioshiriki Hundaybiyah, wala hawakujumuishwa wengine katika mgao huo, isipokuwa Ja’far bin Abu Twalib na wenzake رضي الله عنهم ambao walikwenda Habashah (Ethiopia) hapo kabla, na Abu Musa Al-Ash’ari na wenzake رضي الله عنهم. Hapana yeyote katika wao ambaye hakuwepo. Ibn Zayd alisema: Isipokuwa Abu Dujanah Simaak bin Kharshah رضي الله عنه.¹ Kama ilivyothibitishwa hilo. Kisha Mtume ﷺ alirejea Madinah.

Baada ya kufika mwezi wa Dhul-Hijjah katika mwaka wa saba, Mtume ﷺ alielekea Makkah kwa ajili ya kufanya ‘Umrah. (Hija ndogo). Alifuatana na washiriki wa Hundaybiyah. Akahirimia (kutia nia ya lbada) mahali palipoitwa Dhul-Hulayfah na alikuwa pamoja na wanyama wa kuchinja. Ilisemekana kuwa walikuwa ngamia sitini. Alisoma *Talbiyah* akaenda pamoja na Masahaba wake ambao nao walisoma *Talbiyah* kwa sauti. Mtume ﷺ alipokaribia kufika Marr Adh-Dhahraan, alimtuma Muhammad bin Maslamah رضي الله عنه atangulie pamoja na farasi na silaha. Washirikina walipomuona, waliogopa sana, wakadhani Mtume ﷺ amekuja kupigana nao vita, na ameamua kuuvunja mkataba uliokuwepo baina yao wa kutokuwepo mapigano kwa muda wa miaka kumi. Wakaenda kuwapa habari wakazi wa Makkah.

¹ At-Tabari 22:259.

Baada ya Mjumbe ﷺ kuteremka na kupiga kambi hapo Marr Adh-Dhahran, mahali alipoweza kuyaona masanamu yaliyowekwa katika Al-Haram, alipeleka silaha mbalimbali, kama vile mipinde, mishale na mikuki kwenda katika bonde la Ya-'jaj. Akashika njia ya kwenda Makkah huku mapanga yao yakiwa ndani ya ziaka zake. Makuraishi wakamtuma Mikraz bin Hafs, ambaye alisema: "Ewe Muhammad! Hatukujua kuwa wewe utavunja mkataba." Mtume ﷺ akauliza:

«وَمَا ذَاكَ؟»

"Kwani imekuaje?"

Mikraz akajibu: "Umeingia kwetu ukiwa na silaha, mipinde na mikuki." Mtume ﷺ akasema:

«لَمْ يَكُنْ ذَلِكَ وَقَدْ بَعَثْنَا بِهِ إِلَى يَأْجِجٍ»

"Si hivyo, zote hizo tumekwishazipeleka huko Ya-'jaj."

Mikraz akasema: "Hivi ndivyo tunavyokujua ulivyo, kwa kufanya wema na kutekeleza ahadi." Wakuu wa makafiri wakatoka Makkah ili waweze kumuona Mtume ﷺ na Masahaba wake kwa namna ya hasira na hamaki.

Watu wengine wa Makkah, wakiwemo wanaume, wanawake na watoto, walikaa njiani na juu ya majumba, wakimtazama Mjumbe wa Allah na Masahaba wake. Mtume ﷺ na Masahaba wake, wakaingia katika mji wa Makkah huku wakisoma *Talbiyah*. Halikadhalika, alipeleka wanyama wa kuchinjwa, mahali palipoitwa, Dhu Tuwa, huku akiwa juu ya ngamia wake, Al-Qaswaa, ambaye ndiye pia aliyekuwa juu yake, katika siku ya Hudaybiyah. Wakati huo, 'Abdullah bin Rawaahah رضي الله عنه alikuwa akizishikilia zimamu za ngamia wa Mtume ﷺ huku akilikariri shairi hili:

"Kwa Jina la Ambaye hapana dini ya haki, isipokuwa Dini Yake. Kwa Jina la Ambaye, Muhammad ﷺ ndiye Mjumbe Wake. Enyi wana wa makafiri, ondokeni katika njia yake. Leo, tutatakupigeni. Ni sawa na tulivyokupigeni juu ya uteremsho Wake. Pigo ambalo hukiondoa kichwa kutoka katika matulizano yake, na kumuelemea rafiki dhidi ya kumzuru rafiki yake. Allah تعالى Ameteremsha katika ufunuo Wake ndani ya kurasa zisomwazo mbele ya Mjumbe Wake. Kwamba kifo kilicho bora ni ambacho hutoka katika njia Yake, ndani ya kurasa zisomwazo mbele ya Mjumbe Wake ﷺ. Kwa hivyo, ee Allah! Mimi ninaziamini kauli zake." Kisa hiki kimekusanywa katika masimulizi mbalimbali.

Ahmad alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, kuwa amesema: "Mtume ﷺ na Masahaba wake walifika Makkah, huku, homa ya Yathrib (Madinah) ikiwa imewadhoofisha na kuwasumbua. Washirikina wakasema, 'Wanakujieni watu ambao wameshadhoofishwa na homa ya Yathrib, na wakapata madhara kutokana nayo.' Washirikina wakakaa katika upande ulio jirani na Al-Hijr. Allah تعالى Alimfikishia Mtume Wake waliyoyasema washirikina. Mtume ﷺ akawaamuru Masahaba wake kufanya mchakamchaka raundi tatu za mwanzoni, ili washirikina washuhudie nguvu zao. Masahaba wakafanya hivyo katika mizunguko mitatu ya awali. Pia aliwaamuru watembe kwa namna ya kawaida baina ya nguzo mbili, ambapo washirikina hawawaoni. Wala hakuwaamuru kwenda mchakamchaka katika raundi zote za Tawafu kwa sababu ya kuwahurumia. Washirikina wakasema: 'Hawa ndio mllosema kwamba homa imewadhoofisha! ni wenye nguvu kuliko fulani na fulani.'" Imeandikwa ndani ya Sahih Mbili.¹

Katika masimulizi mengine, "Mtume ﷺ na Masahaba walikuja Makkah katika asubuhi ya tarehe nne ya mwezi wa Dhul-Qa'dah. Washirikina wakasema: 'Yeye anakuleteeni kundi la watu ambao homa ya Yathrib imekwishawafanya madhaifu.' Mtume ﷺ akawaamuru waende mchakamchaka raundi tatu za awali za Tawaf, na kwa kuwahurumia, hakuwaamuru kufanya hivyo katika raundi zote."²

Bukhari aliandika kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kwamba alisema: "Baada ya Mtume ﷺ kufika, kama ilivyowafikiwa katika mkataba wa amani, alisema: "*nendeni mchakamchaka,*" ili washirikina ambao walikuwa katika eneo la Qu'ayqi'an³ waone nguvu zao."⁴ Pia, kwa mujibu wa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, kwamba alisema: "Mtume ﷺ alienda mbiombio⁵ katika Ka'aba na baina ya Swafaa na Marwah ili washirikina waone ukakamavu wake."⁶

Bukhari, alimnukuu tena Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa alisema: "Mtume ﷺ alitoka kwa ajili ya kufanya 'Umrah (Hija ndogo), makafiri wa Kikuraishi wakazuia

¹ Ahmad 1:294.

² *Fat'h Al-Bari* 7:581, Muslim 2:923.

³ *Fat'h Al-Bari* 3:548.

⁴ Mlima mdogo kuelekea katika *Hijr*.

⁵ *Fat'h Al-Bari* 7:581.

⁶ Kutembea haraka haraka.

njia baina yake na Kaaba. Akachinja mnyama wake na akanyoa nywele za kichwani kwake katika sehemu ya Hudaybiyyah. Akakubaliana nao kwamba atafanya 'Umrah (Hija ndogo) katika mwaka uliofuatia, wala asibebe silaha wakati huo, isipokuwa mapanga, wala asikae zaidi huko, isipokuwa kwa kipindi walichokiruhusu. Mtume ﷺ akafanya 'Umrah katika mwaka uliofuatia, akaingia kama alivyopatana nao. Baada ya kupita siku tatu humo, walimuamuru aondoke, na akaondoka.”¹ Kauli ya Allah تعالى:

فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا فَجَعَلَ مِنْ دُونِ ذَلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿٢٧﴾

“...Yeye Anajua msiyoyajua. Basi, Hivi karibuni Atakupeni Ushindi.”

Maana yake: Allah تعالى Alikuwa Akijua kheri na manufaa ya Kukuzuieni dhidi ya Makkah na Kukukatazeni kuingia katika mwaka wenu huo. Aliyajua msiyoyajua nyinyi,

فَجَعَلَ مِنْ دُونِ ذَلِكَ

“...Basi Atakupeni kabla ya haya...”

Kabla hamjaingia Makkah, kama mlivyoahidiwa kupitia ndoto ya Mtume ﷺ, Alitoa ushindi wa karibu, ambao ni mapatano yaliyofanyika baina yenu na maadui zenu wa kishirikina.

Bishara ya Ushindi wa Waislamu Ulimwenguni

Halafu, Allah تعالى Aliwapa bishara Waumini, kwamba Mjumbe atawashinda maadui wake, na watu wengine wote duniani,

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ

“Yeye Ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa uwongofu na Dini ya Haki...”

Kwa elimu yenye manufaa na amali njema, kwani Sheria ina mambo mawili, elimu na amali. Hivyo, elimu ya kisheria ni sahihi na amali ya kisheria ni yenye kupokelewa. Halikadhalika, habari yake ni ya kweli, na amri zake ni uadilifu,

¹ Fat'h Al-Bari 7:581.

لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

“...ili Aitukuze juu ya dini zote.”

Maana yake: Kwa watu wa dini zote, katika ardhi yote, kwa Waarabu na wasio hao, wapagani na washirikina.

وَكَفَى بِاللَّهِ شَهِيدًا

“Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Shahidi.”

Inamaanisha, kuwa yeye ni Mjumbe Wake na Yeye Ndiye wa Kumnusuru. *Allahu Aalam.*

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ ۗ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ ۖ تَرَاهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا ۖ سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثَرِ السُّجُودِ ۗ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التَّوْرَةِ ۗ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ كَرَزَعٍ أُخْرِجَ شَطْنُهُ فَأَزْرَهُ فَأَسْتَغْلَظَ فَاسْتَوَىٰ عَلَىٰ سَوْفِهِ ۗ يُعْجَبُ الْزَّرَّاعُ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ ۗ وَعَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾

29. “Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama na kusujudu wakitafuta Fadhila na Radhi za Mwenyezi Mungu. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili ni kama mmea uliotoa matawi yake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya shina lake, ukawafurahisha wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri. Mwenyezi Mungu Amewaahidi walioamini na wakatenda wema katika wao msamaha na ujira mkubwa.”

Sifa za Waumini

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Muhammad ﷺ kuwa yeye ni Mjumbe Wake, bila ya shaka yoyote. Allah تعالى Amesema:

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ

“Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.”

Huu ni utangulizi wa habari inayojumuisha kila sifa nzuri. Kisha, Allah تعالى Akafuatishia sifa za Masahaba, Allah تعالى Awe radhi nao. Akasema:

وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءَ بَيْنَهُمْ

“Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ

“...basi Mwenyezi Mungu Atakuja leta watu Anaowapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa Waumini na wenye nguvu juu ya makafiri ...” (5:54)

Hizi ni sifa za waumini, kwamba ni wakakamavu juu ya makafiri, lakini ni wapole na wema kwa Waumini; ni wenye ghadhabu na hasira kali mbele ya makafiri na tabasamu na wenye bashasha katika nyuso za ndugu zao, Waumini.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَتِلُوا الَّذِينَ يَلُونَكُمْ مِنَ الْكُفَّارِ وَلَيَجِدُوا فِيكُمْ غِلظَةً

“Enyi mlioamini! Piganeni na wale makafiri walio karibu yenu, na wakute ukakamavu kwenu.” (9:123)

Mtume ﷺ amesema:

«مَثَلُ الْمُؤْمِنِينَ فِي تَوَادُّهِمْ وَتَرَاحِيهِمْ كَمَثَلِ الْجَسَدِ الْوَاحِدِ، إِذَا اشْتَكَى مِنْهُ عُضْوٌ تَدَاعَى لَهُ سَائِرُ الْجَسَدِ بِالْحَمَى وَالسَّهْرِ»

“Mfano wa Waumini katika kupendana kwao na kuhurumiana kwao ni kama kiwiliwili kimoja, kiungo chake kimoja kikiugulia maumivu, basi mwili mzima unapokea kwa kupata homa na kukesha.”¹

Mtume ﷺ alisema tena:

«الْمُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِ كَالْبُنْيَانِ يَشُدُّ بَعْضُهُ بَعْضًا»

“Muumini kwa Muumini mwenzake, ni kama jengo moja ambapo inatiana nguvu baina yake na baadhi nyingine .”

Akafumbanisha baina ya vidole vyake.² Hadithi zote mbili ziko ndani ya Sahih.

Kauli ya Allah تعالى:

تَرْنَهُمْ رُكْعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا^ط

“Utawaona wakiinama na kusujudu wakitafuta fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu.”

Allah تعالى Ameeleza kuwa sifa zao ni kukithirisha amali na Sala. Pia alieleza ikhilasi yao huwa ni kwa ajili ya Allah تعالى Peke Yake, na kutarajia malipo makubwa mbele ya Allah تعالى. Nayo ni Pepo ambayo ina fadhila tele za Allah تعالى, na ina ukunjufu wa riziki juu yao, Radhi Zake Allah تعالى. Radhi ni malipo makubwa zaidi ya hayo yaliyotajwa awali. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ أَكْبَرُ

“...na Radhi za Mwenyezi Mungu ndio kubwa kuliko yote.” (9:72)

Kauli ya Allah تعالى:

سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِمْ مِّنْ أَثَرِ السُّجُودِ

“Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu.”

¹ Muslim 4:1999.

² Fat’h Al-Bari 5:119.

'Ali bin Abu Twalhah amesema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alitoa rai kuwa maana ya 'Alama zao ziko katika nyuso zao, ni haiba nzuri.¹ Mujahid na wengine wamesema kuwa maana yake, 'unyenyekavu na uchaji.²

Baadhi yao walisema: "Amali njema huleta nuru moyoni na uangavu katika wajihi, na ukunjufu wa riziki na mapenzi katika nyoyo za watu."

Amiri wa Waumini, 'Uthman رضي الله عنه amesema: "Hapana yeyote afichaye siri yoyote, bali Allah تعالى Ataidhirisha katika wajihi wake, au kwa kuteleza ulimi wake." Imamu Ahmad alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ الْهُدَى الصَّالِحِ، وَالسَّمْتَ الصَّالِحِ، وَالْأَفِصَادَ، جُزْءٌ مِنْ خَمْسَةٍ وَعِشْرِينَ
جُزْءًا مِنَ التَّبَوُّةِ»

"Kwa hakika, tabia njema, muonekano mzuri na matumizi mazuri, ni sehemu ya mafungu ishirini na matano ya Utume."³

Abu Dawud pia, aliinukuu Hadithi hii.⁴ Kwa hivyo, Masahaba walizitakasa nia zao, wakafanya amali njema. Kwa ajili hiyo, kila aliyewatazama alipendezwa nao kwa haiba yao na tabia yao. Malik amesema: "Ilinifikia habari kuwa, pindi Manasara walipowaona Masahaba ambao waliifungua Shamu, walisema, 'Wallahi! Hawa ni wabora zaidi kuliko wanafunzi [wa 'Isa عليه السلام], kwa mujibu wa habari zilizotufikia.'" Kauli yao hiyo ni ya kweli, kwani, umma huu umetukuzwa ndani ya Vitabu vilivyotangulia, na walio na heshima na fadhila zaidi ni Masahaba wa Mtume ﷺ. Allah تعالى Aliwasifu kwa kuwataja ndani ya Vitabu vilivyoteremshwa habari zinazosimuliwa. Kwa minajili hii, Allah تعالى Anasema katika Aya hii:

ذَلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التَّوْرَةِ

"Huu ndio mfano wao katika Taurati." Akasema:

وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ كَرَزَعٍ أُخْرِجَ شَطَطُهُ

"Na mfano wao katika Injili ni kama mmea uliotoa chipukizi lake..."

¹ At-Tabari 22:263.

² At-Tabari 22:263.

³ Ahmad 1:296.

⁴ Abu Dawud 5:136.

Maana yake: Chipukizi lake.

فَفَازَرَهُ

“...kisha ukalitia nguvu...”

Maana yake: Kukomaa kwake.

فَأَسْتَغْلَظَ

“...ukawa mnene...”

Inamaanisha, ukakua na kurefuka.

فَأَسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوْقِهِمْ يُعْجِبُ الزُّرَّاعَ

“...ukasimama sawa juu ya ubuwa wake, ukawafurahisha wakulima...”

Maana yake: Kadhalika, Masahaba wa Mtume ﷺ, walimpa nguvu, wakamsaidia, na kupata ushindi, kama vile chipukizi katika mmea.

لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ

“...ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri.”

Kwa kuitegemea Aya hii, Imamu Malik alizungumzia kikundi cha *Ar-Rawafidh* (Shia) ¹ ambao huwachukia Masahaba. Imamu Malik رضي الله عنه alisema: “Kwa kuwa wanawachukia Masahaba, na kwa mujibu wa Aya hii, Mwenye kuwachukia Masahaba ni kafiri.” Maulamaa wengi waliafikiana naye juu ya hili. Kuna Hadithi nyingi zinazozungumzia fadhila za Masahaba na kukataza kuwapinga kutokana na makosa yao. Inawatosha kwamba Allah تعالى Aliwasifu na Akawa Radhi nao. Kisha, Allah تعالى Akasema:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْهُمْ مَغْفِرَةً

“Mwenyezi Mungu Amewaahidi walioamini na wakatenda wema katika wao msamaha...”

¹ Kikundi cha Shia.

Kwa ajili ya madhambi yao,

وَأَجْرًا عَظِيمًا

“...na ujira mkubwa.”

Maana yake: Thawabu nyingi na riziki tukufu. Ahadi ya Allah تعالى ni ya kweli, haikhalifiwi wala kubadilishwa. Kila mwenye kufuata mwendo wa Masahaba, watakuwa katika hukumu yao. Masahaba wana fadhila zaidi, kutangulia kwao katika Dini na ukamilifu wa tabia, ambao hapana wa kuweza kuwafikia katika umma huu. Allah تعالى Awe radhi nao, na Awafanye wao nao wawe radhi, Ajaalie makazi yao yawe katika Pepo za Firdaus. Naam, Amekwisha yafanya yote haya.

Muslim aliandika ndani ya Sahih yake, kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alieleza: Mtume ﷺ amesema:

«لَا تَسُبُّوا أَصْحَابِي، فَوَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ أَنْفَقَ مِثْلَ أُحُدٍ ذَهَبًا، مَا أَذْرَكَ مُدًّا أَحَدِهِمْ وَلَا نَصِيفَهُ»

“Msiwatukane Masahaba wangu, kwani, naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Iwapo mmoja wenu angelitoa dhahabu mfano wa Uhud, kiasi hicho kisingefikia kibaba cha mmoja wao wala nusu yake.”¹

Mwisho wa tafsiri ya *Surat Al-Fat-h*. Himdi na Shukurani zinamstahiki Allah تعالى.

* * *

¹ Kipimo kidogo cha vitu vikavu, Muslim 4:1967.

Tafsiri ya Suratul Hujuraat

Sura ya 49

Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehema Mwingi wa Kurehemu

سُورَةُ الْحُجُرَاتِ

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيْ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ^ط
 وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا
 تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ
 كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا
 تَشْعُرُونَ ﴿٢﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ
 أُولَئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَىٰ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ
 عَظِيمٌ ﴿٣﴾ إِنَّ الَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِن وَرَاءِ الْحُجُرَاتِ
 أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٤﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ صَبَرُوا حَتَّىٰ تَخْرُجَ
 إِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٥﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ
 ءَامَنُوا إِن جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَأٍ فَتَبَيَّنُوا أَن تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهْلَةٍ
 فَتُصِيبُكُمْ عَلَىٰ مَا فَعَلْتُمْ نَسِيئِينَ ﴿٦﴾ وَأَعْلَمُوا أَن فِيكُمْ
 رَسُولَ اللَّهِ ۗ لَوْ يُطِيعُكُمْ فِي كَثِيرٍ مِّنَ الْأَمْرِ لَعَنِيمٌ وَلَٰكِنَ اللَّهُ
 حَبَّبَ إِلَيْكُمُ الْإِيمَانَ وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ
 وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ ۗ أُولَئِكَ هُمُ الرَّشِيدُونَ ﴿٧﴾ فَضَلًّا
 مِّنَ اللَّهِ وَنِعْمَةً ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٨﴾

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُقَدِّمُوا بَيْنَ
 يَدَيْ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ^ط وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ
 اللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١﴾ يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ
 ءَامَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ
 صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ
 بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ
 أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا
 تَشْعُرُونَ ﴿٢﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ
 أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَئِكَ
 الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَىٰ
 لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٣﴾

1. "Enyi mlioamini! msita-ngulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua."

2. *“Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa sauti ya juu kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui.”*

3. *“Kwa hakika wanaoteremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu Amezisafisha nyoyo zao kwa uchamungu. Hao watakuwa na msamaha na ujira mkubwa.”*

Kukatazwa Kumtangulia Allah تعالی na Mjumbe Wake ﷺ, na Amri ya Kumuadhimisha na Kumfanyia Adabu Mtume ﷺ.

Katika Aya hizi, Allah تعالی Anawafundisha adabu waja Wake, Waumini katika kuamiliiana na Mjumbe kwa kumtukuza, kumheshimu, kumuenzi na kumuadhimisha. Allah تعالی Amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْدِمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ^ط

“Enyi mlioamini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake...”

Maana yake: Msifanye haraka katika masuala yoyote mbele yake, kabla yake, bali muwe mnamfuata katika mambo yote. ‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالی:

لَا تَقْدِمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ

“Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake...”

Kwamba, “Msitoe kauli iliyo kinyume na Qur’an na Sunnah.”¹ Qatadah amesema: “Tuliambiwa kwamba watu walikuwa wakisema, ‘Lau ingeliteremshwa kadha na kadha au ingelikuwa sahihi jambo kadha. Allah تعالی Akachukia hilo.”² Allah تعالی Amesema katika Aya hiyo,

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“...na mcheni Mwenyezi Mungu.”

¹ At-Tabari 22:275.

² At-Tabari 22:276.

Katika Alivyokuamrisheni,

إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia...”

Kauli zenu,

عَلِيمٌ

“...Mwenye Kujua.”

Nia zenu. Kauli ya Allah تعالى:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ

“Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii...”

Hii ni adabu ya pili, ambayo Allah تعالى Anawafundisha Waumini, wasizipaze sauti zao mbele ya Mtume ﷺ kuliko sauti yake. Ilisimuliwa kwamba Aya hii ilishuka kuwahuu wazee wawili, Abubakr na ‘Umar رضي الله عنهما.

Bukhari alinukuu kwamba Mulaykah alisema: “Wachamungu wawili walikaribia kuhiliki, ni Abubakr na ‘Umar رضي الله عنهما, ambao waliinua sauti zao mbele ya Mtume ﷺ pindi msafara wa Banu Tamim ulipofika. Mmoja kati ya wawili hao, alimuashiria Aqra’ bin Habis, mmoja wapo katika ndugu wa Banu Mujaashi’, huku mwenzake akimuashiria mtu mwingine.”

Nafi’, mmoja wa wasimulizi, amesema: “Sikumbuki jina lake.” Abubakar رضي الله عنه alimuambia ‘Umar رضي الله عنه, ‘Ulichotaka wewe si kingine, isipokuwa kunikhalifu.’ Akamjibu, ‘Mimi sikukusudia kukukhalifu.’ Sauti zao zikapaa katika mazungumzo hayo.

Allah تعالى Akateremsha Aya:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٥٩﴾

“Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui.”

Ibnu Zubayr رضي الله عنه amesema: “Baada ya hayo, sauti ya ‘Umar رضي الله عنه ilikuwa ya chini kiasi kwamba Mjumbe wa Allah ﷺ alikuwa akimtaka kurudia usemi, ili aweze kuelewa alichokisema.” Wala, Zubayr رضي الله عنه hakulitaja jambo hilo kuhusu baba yake, yaani, Abubakr¹ رضي الله عنه² Muslim hakuandika Hadithi hii.

Katika masimulizi yaliyokusanywa na Bukhari, kutoka kwa Zubayr رضي الله عنه. Amesema kuwa, wajumbe kutoka kwa Banu Tamim walikuja kwa Mtume ﷺ. Abubakr رضي الله عنه akasema: “Mchague Al-Qa’qa’ bin Ma’bad awe amiri wao.” ‘Umar رضي الله عنه akasema: “Bali, mchague Aqra’ bin Habis.”³ Masimulizi haya pia, yalinukuliwa na Bukhari peke yake.

Bukhari aliandika kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa Mjumbe wa Allah ﷺ alimkosa Thabit bin Qays رضي الله عنه. Mtu mmoja akasema: “Ewe Mjumbe wa Allah! Mimi nitatafuta habari zake kwa ajili yako.” Akamuendea nyumbani kwake, akamkuta akiwa ameinamisha kichwa chake. Akamuuliza: “Nini kilichokusibu?” Akajibu: “Jambo baya.” Alikuwa akipaza sauti yake zaidi ya ile ya Mtume ﷺ, kwa hivyo akakhofia kwamba amali zake hazikuweza kuwa na manufaa na kwamba yeye ni katika watu wa Motoni. Mtu yule akarudi kwa Mtume ﷺ na akampa habari kuwa amesema kadha wa kadha. Akaenda tena kwa Thabit رضي الله عنه huku akiwa na bishara kubwa. Mtume ﷺ alimtuma:

«اذْمَبْ إِلَيْهِ فَقُلْ لَهُ: إِنَّكَ لَنْتَ مِنْ أَهْلِ النَّارِ، وَلَكِنَّكَ مِنْ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

“Muendee na umuambie hivi, ‘Wewe si katika watu wa Motoni, bali wewe ni wa Peponi.”

Bukhari peke yake aliinukuu Hadithi hii kwa maneno haya yalivyo.¹

Imamu Ahmad alimnukuu Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa alisema: “Iliposhuka Aya hii:

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ

“Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii...” mpaka,

¹ Maana yake: Babu yake.

² Fat’h Al-Bari 8:454.

³ Fat’h Al-Bari 8:457.

وَأَتُّمَّرَ لَا تَشْعُرُونَ

“...na hali hamtambui.”

Thabit bin Qays bin Shammaas رضي الله عنه alikuwa ndiye mwenye kunyanyua sauti, amesema, ‘Mimi ndiye niliyekuwa nikiipaza sauti zaidi ya Mtume ﷺ, basi mimi ni katika watu wa Motoni, amali zangu hazina manufaa tena.’ Akakaa pamoja na ahali wake akiwa mwenye huzuni. Mtume ﷺ akawa ana shida naye. Watu wakamuendea na kumuuliza: “Mtume ﷺ anakutafuta, ni nini kilichokusibu?” Akawajibu: “Mimi ndiye mwenye kunyanyua sauti yangu juu ya ile ya Mtume ﷺ, pia nilikuwa nikimdhihirishia kauli. Amali zangu zimekuwa zenye khasara, mimi ni katika wakazi wa Motoni.” Wakamuendea Mtume ﷺ, wakamuambia aliyoyasema Thabit رضي الله عنه. Mtume ﷺ akasema:

«لَا، بَلْ هُوَ مِنْ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

“Hapana, bali yeye ni katika watu wa Peponi.”

Anas bin Malik رضي الله عنه alisema: “Basi, tukawa tunamuona akitembea katika maeneo yetu, huku tukijua kwamba yeye ni miongoni mwa watu wa Peponi. Ilipofika siku ya vita vya Al-Yamamah, kulikuwa na baadhi yetu walioonesha kurudi nyuma. Akaja Thabit bin Qays bin Shammaas رضي الله عنه akiwa amejikafini na kujitia *Hanut* (uturi unaotiwa katika sanda),² akasema, “Ni vibaya mnavyowazo esha maadui zenu.” Akaendelea kupigana mpaka akauawa shahidi, Allah تعالى Awe radhi naye.”³ Kisha ikakatazwa kumdhihirishia Mtume ﷺ kauli kama uzungumzaji wa anayekomea kumfanyia uadui. Bali, aseme naye kwa utulivu, heshima na taadhima. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ

“...msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi...”

Ni sawa na Alivyosema Allah تعالى katika Kauli nyingine:

¹ *Fat’h Al-Bari* 8:454.

² Manukato yanayotumika wakati wa kumkafini maiti.

³ Ahmad 3:137. Kadhalika imenukuliwa na Muslim na. 119

لَا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا

“Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi.” (24:63)

Kauli ya Allah تعالى:

أَنْ تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ

“...visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui.”

Maana yake: Tumekukatazeni dhidi ya kupaza sauti mbele yake, kwa kukhofia kwamba angeweza kughadhibika na kwa hivyo, Allah تعالى Naye Akaghadhabika. Matokeo yake, ni kuharibika kwa amali za aliyeghadhibikiwa ilhali yeye mwenyewe hajui. Ni sawa na ilivyoeleza Hadithi Sahih,

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيَتَكَلَّمُ بِالْكَلِمَةِ مِنْ رِضْوَانِ اللَّهِ تَعَالَى لَا يُلْقِي لَهَا بَالًا، يُكْتَبُ لَهُ بِهَا الْجَنَّةُ، وَإِنَّ الرَّجُلَ لَيَتَكَلَّمُ بِالْكَلِمَةِ مِنْ سَخَطِ اللَّهِ تَعَالَى لَا يُلْقِي لَهَا بَالًا، يَهْرِي بِهَا فِي النَّارِ أَبَعَدَ مَا بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ»

“Kwa hakika, mtu anaweza kutamka kauli ya kumridhisha Allah Taala, bila ya kujua ukubwa wa neno lake, na kuandikiwa Pepo kwa ajili hiyo. Pia, mtu anaweza kutamka neno zito la Kumghadhibisha Allah. Bila ya kujali uzito wake. Hivyo kumtumbukiza katika shimo la moto lenye kina kirefu kama baina ya mbingu na ardhi.”¹

Halafu, Allah تعالى Akaamuru kushusha sauti mbele yake na Akahimiza Kushajiisha na Kubainisha jambo hilo.

إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَى

“Kwa hakika wanaoteremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu Amezisafisha nyoyo zao kwa uchamungu.”

Maana yake: Alizitakasa, Akazifanya ndio makazi ya Taqwa,

¹ Fat'h Al-Bari 11:314.

لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ

“Hao watakuwa na maghufira na ujira mkubwa.”

Imamu Ahmad aliandika katika mlango wa Az-Zuhd kwamba Mujahid amesema, “Umar رضي الله عنه aliandikiwa na mtu: ‘Ewe Amiri wa Waislamu! Mtu ambaye hana matamania ya kufanya maasi, wala hayafanyi ni bora, au mtu mwenye kuwa na matamania ya kufanya maasi lakini hayatendi.’ Umar رضي الله عنه akaandika majibu: ‘Hakika, ni wale wenye matamania ya maasi, lakini hawayatendi.’”

أُولَئِكَ الَّذِينَ أَمْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَىٰ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ

“...hao ndio Mwenyezi Mungu Amezisafisha nyoyo zao kwa uchamungu. Hao watakuwa na maghufira na ujira mkubwa.”

إِنَّ الَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِنَ وَرَاءِ الْحُجُرَاتِ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٤١﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ صَبَرُوا حَتَّى تَخْرُجَ إِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٤٢﴾

4. “Hakika hao wanaokuita nawe uko nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili.”

5. “Na lau wao wangelingojea mpaka uwatokee ingelikuwa kheri kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghufira, Mwenye Kurehemu.”

Karipio kwa Wanaomuita Mtume ﴿٤١﴾ Nyuma ya Vyumba

Kisha, Allah تعالى Aliwakemea wale ambao humuita kutokea nyuma ya vyumba vya wakeze, kama wafanyavyo mabedui wasiostaarabika. Amesema:

أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ

“...wengi wao hawana akili.”

Halafu, Allah تعالى Alielekeza adabu za kuyafanya hayo, kwamba,

وَلَوْ أَنَّهُمْ صَبَرُوا حَتَّى تَخْرُجَ إِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ ۗ

“Na lau wao wangelingojea mpaka uwatokee ingelikuwa kheri kwao.”

Maana yake: Katika hayo, wangelipata kheri na maslahi ya dunia na Akhera. Katika kuwaita katika toba na kujirudi, Allah تعالى Alisema:

وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira, Mwenye Kurehemu.”

Ilielezwa kwamba Aya hii, ilishuka kumhusu Aqra’ bin Haabis Tamimi katika masimulizi yaliyotolewa na zaidi ya mtu mmoja. Imamu Ahmad aliandika kutoka kwa Aqra’ bin Haabis kwamba yeye alimuita Mtume ﷺ kutokea nyuma ya vyumba. Alisema: “Ewe Muhammad! Ewe Muhammad!” Katika masimulizi mengine: “Ewe Mtume!” Hakumuitika. Aqra’ akasema: “Ewe Mtume! Sifa zangu (kwa wengine) ni nzuri, na karipio langu ni baya.” Mtume ﷺ akamjibu:

«ذَكَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ»

“Huyo ni Allah Taalaa (Ndiye Aliyebainisha hivyo).”¹

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَأٍ فَتَبَيَّنُوا أَن تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهَالَةٍ فَتُصْحَبُوا عَلَىٰ مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ ﴿٦٦﴾ وَأَعْلَمُوا أَن فِيكُمْ رَسُولَ اللَّهِ ؕ لَوْ يُطِيعُكُمْ فِي كَثِيرٍ مِّنَ الْأَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ حَبَّبَ إِلَيْكُمُ الْإِيمَانَ وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ ؕ أُولَٰئِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ ﴿٦٧﴾ فَضَلَّأَ مِّنَ اللَّهِ وَنِعْمَةً ؕ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٨﴾

6. “Enyi mlioamini! Akikujieni muovu na habari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyoyatenda.”

7. “Na jueni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko nanyi. Lau angelikut’iini katika mambo mengi, bila ya shaka mngelitaabika. Lakini Mwenyezi Mungu Amekupendezeeni Imani, na Akaipamba katika nyoyo zenu, na Amekufanyeni muuchukie ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walioongoka.”

8. “Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na Neema Zake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Hikima.”

¹ Ahmad 3:488.

Agizo la Kuifanyia Uchunguzi Habari ya Fasiki

Allah **تعالى** Anaamuru kufanyiwa uchunguzi habari ya fasiki, ili hukumu isitolewe kwa kuegemea kauli yake tu, ilhali, kumbe jambo lenyewe ni la uongo au la bahati mbaya, kumfanyia hakimu kushawishika na kauli ya Fasiki.

Allah **تعالى** Alikwishakataza kufuata njia ya mafisadi. Kwa sababu hii, maulamaa wengi wamejizuia dhidi ya kukubali rai za wasiojulikana mazingira yao kwa kuchelea kuwepo ufasiki katika mambo yao.

Kimesimuliwa kisa kupitia njia kadha za usimulizi, ambacho kinaeleza sababu za kuteremshwa kwa Aya hii. Kisa kizuri zaidi ni alichoeleza Imamu Ahmad katika kitabu chake cha *Musnad*, kupitia kwa kiongozi wa Banu Mustwaliq. Huyu ni Al-Harith bin Abu Dhiraar, baba yake Juwayriyah bint Al-Harith, Mama wa Waumini **رضي الله عنها**,

Al-Harith bin Dhiraar Al-Khuza'i amesema: "Nilikwenda kwa Mtume **ﷺ**, akanilingania katika Uislamu. Nikaingia na kuukubali. Akaniita katika kutoa Zaka, nikakubali, nikasema: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Mimi narejea kwa watu wangu na kuwaita katika Uislamu na kutoa Zaka. Atakayenikubalia, nitaikusanya Zaka yake. Pia ewe Mjumbe wa Allah! Umtume mjumbe katika wakati kadha wa kadha ili akuletee Zaka nitakayoikusanya."

Baada ya Al-Harith kukusanya Zaka kutoka kwa waliomkubalia na muda wa kupelekewa Zaka hiyo kwa Mtume **ﷺ** ukawadia. Mjumbe aliyetumwa alijizuia na hakuja. Harith akadhani kuwa imetokea ghadhabu ya Allah **تعالى** na Mjumbe Wake **ﷺ**. Akawaita watukufu katika kaumu yake na kuwaambia: "Mtume **ﷺ** aliniwekea muda maalumu ambapo atamtuma mjumbe wake kunijia ili akabidhiwe Zaka kutoka kwangu, wala Mtume **ﷺ** hawezi halifu, wala sidhani kuwa yeye amemzuia mjumbe wake, bali ni kwa sababu ya kukasirika. Twendeni kwa Mtume **ﷺ**."

Wakati huo huo, Mtume **ﷺ** alikwisha mtuma Walid bin 'Uqbah kwenda kwa Harith ili apokee Zaka aliyokusanya. Baada ya Walid kwenda hadi njiani, alishikwa na khofu. Akarejea na kumuendea Mtume **ﷺ**. Akamuambia: "Ewe Mjumbe wa Allah! Harith amezuia kunipa Zaka na akataka kuniua."

Mtume **ﷺ** akaghadhibika akawatuma watu kumuendea Harith **رضي الله عنه**. Harith **رضي الله عنه** alikuwa ameshatoka pamoja na wenzake, na baada ya kutoka nje ya mji, alikutana na wajumbe wa Mtume **ﷺ**. Wakasema: "Harith huyu hapa."

Alipowafikia aliwauliza: “Mmetumwa kwenda kwa nani?” Wakajibu: “Kwako.” Akauliza tena: “Kwa ajili ya jambo gani?” Wakasema: “Mtume ﷺ alimtuma Walid bin ‘Uqbah kuja kwako, akadai kuwa wewe umezuia kumkabidhi Zaka na ukataka kumuua.” Harith akasema: “Hapana. Naapa kwa Aliyemtuma Muhammad kwa ukweli! Sikumuona wala hakunijia.” Al-Harith رضي الله عنه alipoingia kwa Mtume ﷺ alisema:

«مَنْعَتِ الزَّكَاةَ وَأَرَدْتَ قَتْلَ رَسُولِي؟»

“Umezuia Zaka na ukataka kumuua mjumbe wangu?”

Akajibu: “Hapana. Naapa kwa Aliyekutuma kwa haki! Sikumuona, wala hakunijia. Wala sikuja, isipokuwa baada ya kutomuona mwakilishi wa Mtume ﷺ kwa kukhofia kwamba yaweza kuwa ni ghadhabu kutoka kwa Allah na Mjumbe Wake.” Kwa hiyo ikateremka aya ya 6 mpaka ya 8 za Sura hii.¹ Hayo pia yamenukuliwa na Ibn Abu Hatim na At-Tabarani.²

Uamuzi wa Mtume ﷺ ni Bora Zaidi

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَعْلَمُوا أَنَّ فِيكُمْ رَسُولَ اللَّهِ

“Na jueni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko nanyi.”

Maana yake: Tambueni kwamba kati yenu, yuko Mtume ﷺ, basi mtukuzeni, muheshimuni na muwe na adabu kwake na mfuata amri yake, kwani yeye anajua zaidi manufaa yenu na anakuoneeni huruma kuliko nyinyi wenyewe. Na rai yake kwenu ni timilifu zaidi kuliko zenu wenyewe. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

النَّبِيُّ أَوْلَىٰ بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنفُسِهِمْ

“Nabii ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao.” (33:6)

¹ Ahmad 4:279.

² At-Tabrani 22:274. Kutajwa jina la Walid bin ‘Uqbah katika kisa hiki ni makosa, kwa sababu kisa hiki kilitokea baada ya vita vya Bani Mustaliq ambavyo vilifanyika katika mwezi wa Shaaban mwaka wa 5H au 6H ambapo alisilimu Walid bin ‘Uqbah baada ya ushindi, yaani katika mwezi wa Ramadhan ya mwaka wa 8H.

Akabainisha kwamba maoni yao si kamilifu katika kuyachunga maslahi yao,

لَوْ يُطِيعُكُمْ فِي كَثِيرٍ مِّنَ الْأَمْرِ لَعَنِتُّمْ

“Lau angelikut’iini katika mambo mengi, bila ya shaka mngelitaabika.”

Maana yake: Kama angelikutiini katika yote mnayoyataka, mngelipata matata na taabu. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَلَوْ أَتَبَعَ الْحَقُّ أَهْوَاءَهُمْ لَفَسَدَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ وَمَن فِيهِنَّ ۗ بَلْ أَتَيْنَهُمْ
بِذِكْرِهِمْ فَهُمْ عَن ذِكْرِهِمْ مُعْرِضُونَ ﴿٧١﴾

“Na lau kuwa Haki ingelifuata matamano yao, basi zingeliharibika mbingu na ardhi na waliomo ndani. Bali Tumewaleta ukumbusho wao, nao wanajitenga mbali na ukumbusho wao.” (23:71)

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَٰكِنَّ اللَّهَ حَبِيبٌ إِلَيْكُمْ ۖ إِلَيْمَنَّا وَإِلَيْكُمْ ۗ وَزَيْنَهُ ۗ فِي قُلُوبِكُمْ

“Lakini Mwenyezi Mungu Amekupendezeeni Imani, na Akaipamba katika nyoyo zenu...”

Maana: Ataipendezesha katika nafsi zenu na Kuifanya nzuri katika nyoyo zenu.

Tofauti Baina ya Uislamu na Imani

Kauli ya Allah تعالى:

وَكُرْهُ إِلَيْكُمْ ۖ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ ۗ

“...na Amekufanyeni muuchukie ukafiri, upotovu, na uasi.”

Maana yake: Amekufanyeni muuchukie ukafiri na ufasiki, ambayo ni madhambi makubwa; na maasi – ambayo ni madhambi ya namna zote. Kauli hii inaelekeza katika neema kamilifu. Kauli ya Allah تعالى:

أَوْلَيْتِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ

“Hao ndio walioongoka.”

Maana yake: Wenye sifa hii ndio walioongoka ambao Allah تعالى Ameshawapa uongofu wao.

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Rifa'ah Az-Zuraqi kuwa baba yake alisema: “Ilipowadia siku ya vita vya Uhud, pindi washirikina walipokimbia, Mtume ﷺ alisema:

«اسْتَوُوا! حَتَّىٰ أَنْتَهِيَ عَلَىٰ رَبِّي عِزًّا وَجَلًّا»

“Jipangeni safu, ili nimsifu Mola Wangu.”

Wakajipanga nyuma yake, akasema:

«اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ كُلُّهُ، اللَّهُمَّ لَا قَائِضَ لِمَا بَسَطْتَ وَلَا بَاسِطَ لِمَا قَبَضْتَ، وَلَا هَادِيَ لِمَنْ أَضَلَلْتَ، وَلَا مُضِلَّ لِمَنْ هَدَيْتَ، وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ وَلَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ، وَلَا مُقَرَّبَ لِمَا بَاعَدْتَ، وَلَا مُبَاعِدَ لِمَا قَرَّبْتَ. اللَّهُمَّ ابْسُطْ عَلَيْنَا مِنْ بَرَكَاتِكَ وَرَحْمَتِكَ وَفَضْلِكَ وَرِزْقِكَ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ التَّيِّمَ الْمُقِيمَ الَّذِي لَا يَحُولُ وَلَا يَزُولُ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ التَّيِّمَ يَوْمَ الْعَيْلَةِ وَالْأَمْنِ يَوْمَ الْخَوْفِ. اللَّهُمَّ إِنِّي عَائِدٌ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا أَعْطَيْتَنَا وَمِنْ شَرِّ مَا مَنَعْتَنَا. اللَّهُمَّ حَبِّبْ إِلَيْنَا الْإِيمَانَ وَزَيِّنْهُ فِي قُلُوبِنَا وَكَرِّهْ إِلَيْنَا الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ وَاجْعَلْنَا مِنَ الرَّاشِدِينَ. اللَّهُمَّ تَوَقَّنَا مُسْلِمِينَ وَأَخِينَا مُسْلِمِينَ وَأَلْجِئْنَا بِالصَّالِحِينَ غَيْرِ خَرَايَا وَلَا مَقْتُونِينَ، اللَّهُمَّ قَاتِلِ الْكُفْرَةَ الَّذِينَ يُكْذِبُونَ رُسُلَكَ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِكَ وَاجْعَلْ عَلَيْهِمْ رِجْزَكَ وَعَذَابَكَ، اللَّهُمَّ قَاتِلِ الْكُفْرَةَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَهَ الْحَقِّ»

“Ewe Allah! Hamdi zote ni Zako. Ewe Allah! Hapana wa kukifunga Ulichokikunjua, wala wa kukikunjua Ulichokifunga, wala wa kumuongoa Uliyemuacha apotee, wala wa kumpoteza Uliyemuongoa, wala wa kumpa Uliyemzuilia, wala wa kumzuilia Uliyempa; wala wa kumsogeza karibu Uliyemueka mbali, wala wa kumueka mbali Uliyemueka karibu. Ewe Allah! Tukunjulie Baraka Zako, Rehema Zako, Fadhila Zako na Riziki Zako. Ewe Allah! Ninakuomba Neema za kudumu, zisizobadilika wala kuondoka. Ewe

Allah! Ninakuomba Neema katika Siku ya kukosekana; Amani katika Siku ya khofu. Ewe Allah! Ninajilinda Kwako dhidi ya shari ya Ulivyotupa na dhidi ya shari ya Ulivyotunyima. Ewe Allah! Tujaalie tuipende Imani na Utupambie nyoyoni mwetu, na Utufanye kuuchukia ukafiri, ufasiki na maasi; na Utujaalie tuwe katika walioongoka. Ewe Allah! Utufishe tukiwa ni Waislamu, na Utuhishe tukiwa ni Waislamu, na Utufikishe daraja za waja Wema, pasi na khizaya wala fitina. Ewe Allah! Wapige makafiri ambao wanawakana Mitume Wako na wanazuia dhidi ya Njia Yako na Uwapelekee mateso na adhabu Yako. Ewe Allah! wapige makafiri waliopewa Kitabu, ee Mola wa kweli.”¹

Nasai aliikusanya Hadithi hii katika mlango wa *Al-Yawm Wal-Laylah*.²

Kisha Allah تعالی Akasema:

فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَنِعْمَةً

“Kwa Fadhila za Mwenyezi Mungu na neema Zake.”

Maana yake: Haya Aliyokupeni ni Fadhila na Neema Zake kwenu,

وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Hikima.”

Maana yake: Ni Mwenye Kujua zaidi wanaostahiki kupotoka, ni Mwenye Hikima katika Kauli, Matendo na Sharia Zake.

* * *

¹ Ahmad 3:424.

² An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:156.

وَإِنْ طَافِيَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَقْتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا ۖ فَإِنْ
 بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَىٰ فَقْتُلُوا الَّتِي تَبَغَىٰ حَتَّىٰ تَبْغِيَ
 إِلَىٰ أَمْرِ اللَّهِ ۚ فَإِنْ فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا ۚ
 إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٩﴾ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ
 فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٠﴾
 يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّن قَوْمٍ عَسَىٰ أَن يَكُونُوا
 خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِّن نِّسَاءٍ عَسَىٰ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ ۚ
 وَلَا تَلْمِزُوا أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا بِاللِّقَابِ ۚ بئسَ الآسَمُ
 الْفُسُوقِ بَعْدَ الْإِيمَانِ ۚ وَمَن لَّمْ يَتُبْ فَأُولَئِكَ هُم
 الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ
 إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ ۚ وَلَا تَجَسَّسُوا ۚ وَلَا يَغْتَب بَّعْضُكُم
 بَعْضًا ۚ أَيُّحِبُّ أَحَدُكُمْ أَن يَأْكُلَ لَحْمَ أَخِيهِ مَيْتًا
 فَكَرِهْتُمُوهُ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾ يَا أَيُّهَا
 النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا
 وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا ۚ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ

عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

وَإِنْ طَافِيَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَقْتَلُوا
 فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا ۖ فَإِنْ بَغَتْ
 إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَىٰ فَقْتُلُوا الَّتِي
 تَبَغَىٰ حَتَّى تَبْغِيَ إِلَى أَمْرِ اللَّهِ ۚ فَإِنْ
 فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ
 وَأَقْسِطُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ
 الْمُقْسِطِينَ ﴿٩﴾ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ
 إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۚ وَاتَّقُوا
 اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٠﴾

9. "Na ikiwa makundi mawili katika Waumini yanapigana, basi yapatanisheni. Na likiwa kundi moja linamdhulumu mwenzie, basi lipigeni linalodhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu. Na likirudi basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wanaohu kumu kwa haki."

10. "Hakika Waumini ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe."

Amri ya Kusuluhisha Waumini Wanaopigana na Kulipiga Kundi Lililoasi

Allah تعالی Anaamuru jambo la kusuluhisha vikundi viwili vyenye kukhasimiana wao kwa wao,

وَإِنْ طَآئِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا ط

“Na ikiwa makundi mawili katika Waumini yanapigana basi yapatanisheni.”

Allah تعالی Ameyaita makundi yote hayo mawili kwa jina la Waumini, ingawa wanapigana. Kwa ajili hii, Bukhari na wengine wameeleza kwamba kufanya maasi hata kama yatakuwa makubwa hakumtoi mtu katika Imani. Si kama wasemavyo watu wa madhehebu ya Khawarij na wafuasi wao, kama vile Mu'tazilah na mfano wao. Kwa ajili hii, ndani ya Sahih Bukhari imethibiti Hadithi Hasan kuwa Abubakr رضي الله عنه amesema, siku moja Mtume ﷺ alikhutubu, huku akiwa katika mimbari pamoja na Al-Hasan bin 'Ali رضي الله عنه. Akawa mara anamuangalia Hasan رضي الله عنه, na mara nyingine anawaangalia watu huku akisema:

«إِنَّ ابْنِي هَذَا سَيِّدٌ وَلَعَلَّ اللَّهَ تَعَالَى أَنْ يُضْلِحَ بِهِ بَيْنَ فِتْنَتَيْنِ عَظِيمَتَيْنِ مِنَ الْمُسْلِمِينَ»

“Kwa hakika, mwanangu huyu ni bwana, na huenda kwa kupitia kwake, Allah Akayasuluhisha makundi mawili makubwa ya Waislamu.”¹

Kwa hivyo, kama alivyosema Mtume ﷺ, Allah تعالی Aliwasuluhisha watu wa Sham na wa Iraq kupitia kwa Hasan رضي الله عنه baada ya vita vya muda mrefu na matukio ya kutisha.

Kauli ya Allah تعالی:

فَإِنْ بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَى فَقْتُلُوا الَّتِي تَبَغَتْ حَتَّى تَبْغِيَ إِلَى أَمْرِ اللَّهِ

“Na likiwa kundi moja la hao linamdhulumu mwenzie, basi lipigeni linalo dhulumu mpaka lirejee kwenye Amri ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Mpaka (kundi lenye kuasi) lirudi katika amri ya Allah تعالی na Mjumbe Wake ﷺ, lisikie ukweli na kuutii. Ni kama ilivyoandikwa katika Sahih kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«انصُرْ أَخَاكَ ظَالِمًا أَوْ مَظْلُومًا»

“Mnusuru nduguyo akiwa dhalimu au mwenye kudhulumiwa.”

Nikamuuliza: “Ewe Mjumbe wa Allah! Huyu anayedhulumiwa ni sawa nimnusuru, lakini vipi nimnusuru mwenye kudhulumu?” Akajibu:

«تَمَنَعُهُ مِنَ الظُّلْمِ فَذَاكَ نَصْرُكَ إِيَّاهُ»

“Unamzuia kudhulumu, huko ndiko kumnusuru kwako.”²

Sa’id bin Jubayr رضى الله عنه alisema kuwa makabila ya Aws na Khazraj yalikuwa na mapigano kwa kutumia matawi ya mitende na viatu. Allah تعالى Akaiteremsha Aya hii na Akawaamuru wawe na suluhu baina yao.³

As-Suddi amesema tena, alikuwepo mtu mmoja katika Answaar aliyekuwa akiitwa ‘Imraan, alikuwa na mke aliyetitwa Mama Zayd. Mkewe alitaka kuzuru watu wake, mumewe akamfungia katika chumba cha sehemu ya juu ambacho yeyote katika watu wake hakuweza kumtembelea. Mke huyo akatuma ujumbe kwa watu wake ambao walikuja kumfungulia ili waondoke naye, na wakati huo mumewe alikuwa ametoka. Watu wake wakawaita watu wa mumewe. Wakaja watoto wa ami yake ili wamzuie mke asiondoke na watu wa kwao. Wakasukumana wakashindana nguvu na kuwafanya wapigane kwa viatu. Aya hii ikashuka kuwahuu wao. Mtume ﷺ akamtuma mtu kuwasuluhisha, na wote walikubaliana kufuata hukumu ya Allah تعالى.⁴ Kauli ya Allah تعالى:

فَإِنْ فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا إِنَّ اللَّهَ سُبْحٌ الْمُقْسِطِينَ

“Na likirudi basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wanao hukumu kwa haki.”

Maana yake: Fanyeni uadilifu baina yao katika yaliyowasibu, kwa kutenda haki, ambayo ndiyo uadilifu,

¹ Fat’h Al-Bari 3:361.

² Fat’h Al-Bari 5:118.

³ Ad-Dur Al-Manthur 7:560.

⁴ At-Tabari 22:294. Hii na kauli iliyotangulia zipo katika kundi la masimulizi yaliyotajwa mwanzoni mwa kitabu hiki.

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wanaohukumu kwa haki.”

Ibn Abu Hatim رضي الله عنه aliandika kuwa ‘Abdullah bin ‘Amri رضي الله تعالى عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ الْمُقْسِطِينَ فِي الدُّنْيَا عَلَى مَنَابِرٍ مِنْ لَوْلُو بَيْنَ يَدَيِ الرَّحْمَنِ عَزَّ وَجَلَّ بِمَا أَفْسَطُوا فِي الدُّنْيَا»

“Kwa hakika, wenye kufanya haki duniani watakuwa katika mimbari za lulu mbele ya Ar-Rahman kutokana na uadilifu wao duniani.”

Nasai aliikusanya Hadithi hii.¹ Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ

“Hakika Waumini ni ndugu...”

Maana yake Waumini wote ni ndugu katika Dini. Ni sawa na kauli ya Mtume ﷺ:

«الْمُسْلِمُ أَخُو الْمُسْلِمِ لَا يَظْلِمُهُ وَلَا يُسْلِمُهُ»

“Muislamu ni ndugu wa Muislamu, hamdhulumu wala hamkoseshi amani.”²

Na katika Sahih, ipo Hadithi:

«وَاللَّهُ فِي عَوْنِ الْعَبْدِ مَا كَانَ الْعَبْدُ فِي عَوْنِ أَخِيهِ»

“Allah Yuko katika Kumsaidia mja maadam mja huyo yuko katika kumsaidia nduguye.”³

Pia Hadithi nyingine ndani ya Sahih,

¹ An-Nasai katika *Al-Kubra* 5917.

² *Fat'h Al-Bari* 5:116.

³ *Muslim* 4:2074.

«إِذَا دَعَا الْمُسْلِمُ لِأَخِيهِ بِظَهْرِ الْغَيْبِ قَالَ الْمَلَكُ: آمِينَ وَلَكَ بِمِثْلِهِ»

“Muislamu akiomba dua kwa ajili ya nduguye ambaye hayupo (mahali hapo) basi Malaika huitikia, ‘Amin, nawe unapata mithili yake.’”¹

Hadithi juu ya mada hii ni nyingi. Ndani ya Sahih kuna Hadithi:

«مَثَلُ الْمُؤْمِنِينَ فِي تَوَادُّهِمْ وَتَرَاحُمِهِمْ وَتَوَاضُعِهِمْ كَمَثَلِ الْجَسَدِ الْوَاحِدِ، إِذَا اشْتَكَى مِنْهُ عُضْوٌ تَدَاعَى لَهُ سَائِرُ الْجَسَدِ بِالنَّحْمَى وَالسَّهْمِ»

“Mfano wa Waumini katika kupendana, kuhurumiana na kuungana kwao ni kama mwili mmoja, kiungo kimoja kikiugua, basi mwili wote huitikia kwa homa na kukesha.”² Na,

«الْمُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِ كَالْبَيْتِ إِذَا بَدَأَ بَعْضُهُ بَعْضًا»

“Muumini kwa Muumini ni sawa na jengo moja, hutiana nguvu baadhi yake kwa baadhi ya nyingine.”

Kisha, Mtume ﷺ aliambatanisha baina ya vidole vyake.³

Kauli ya Allah تعالى:

فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخْوَابِكُمْ

“...basi patanisheni baina ya ndugu zenu...”

Maana yake: Vikundi viwili vinavyopigana,

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“...na mcheni Mwenyezi Mungu...”

Katika mambo yenu yote.

¹ Muslim 4:2094.

² Muslim 4:1999.

³ Fat’h Al-Bari 5:119.

لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

“...ili mrehemewe.”

Huu ni uthibitisho toka kwa Allah تعالى juu ya kuwarehemu wanaomcha.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَسْخَرُونَ مِنْ قَوْمٍ عَسَىٰ أَنْ يَكُونُوا خَيْرًا مِنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِنْ نِسَائِهِمْ
عَسَىٰ أَنْ يَكُنَّ خَيْرًا مِنْهُنَّ وَلَا تَلْمِزُوا أَنْفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا بِاللِّقَابِ بِئْسَ الْإِسْمُ الْفُسُوقُ
بَعْدَ الْإِيمَانِ ۚ وَمَنْ لَمْ يَتُبْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾

11. “Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu.”

Kukatazwa Kejeli na Dharau

Allah تعالى Anakataza jambo la dharau ambayo ni pamoja na kejeli na stihizai. Ni sawa na ilivyoandikwa katika Sahih kuwa Mtume ﷺ alisema:

«الْكِبْرُ بَطْرُ الْحَقِّ وَعَمَصُ النَّاسِ»

“Kiburi ni kukataa ukweli na kuwadhalilisha watu.”¹

Katika masimulizi mengine,

«عَمَطُ النَّاسِ»

“...na kuwadharau watu.”

Maana yake: Ni kuwahakiri na kuwadunisha, na hili ni haramu, kwani yawezekana mwenye kudharauliwa akawa na cheo kikubwa mbele ya Allah تعالى, na pia akawa ni mpendwa zaidi Kwake kuliko mdhalilishaji na mwenye kumdharau. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

¹ Muslim 1:93.

يَتَّيِبُهُمُ اللَّهُ لِيَأْتِيَهُمْ خَيْرٌ مِّنْ قَوْمٍ عَسَىٰ أَن يَكُونُوا خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِّنْ نِّسَاءِ
عَسَىٰ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ

“Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao.”

Onyo hili limetolewa kwa wanaume, kisha wanawake. Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَلْمِزُوا أَنفُسَكُمْ

“Wala msivunjiane hishima...”

Maana yake: Msiwavunjie watu heshima. Mtu mwenye kukashifu na kusengenywa katika wanaume amelaaniwa. Ni sawa na kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَدَلَّ لِكُلِّ هُمْزَةٍ لُّمَزَةٍ

“Ole wake kila safihi, msengenyaji!” (104:1)

Kusafihi ni kwa kitendo na huku kusengenywa ni kwa kauli. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine:

هَمَّازٍ مَّشَاءٍ بِنَمِيمٍ

“Mtapitapi, apitae akifitini.” (68:11)

Maana yake: Anawadharau watu na anawakashifu pamoja na kueneza fitina baina yao. Huko ni kusengenywa kwa kauli. Kwa minajili hii, Allah تعالى Amesema katika Aya hii:

وَلَا تَلْمِزُوا أَنفُسَكُمْ

“Wala msivunjiane hishima...” Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ

“Wala msjiuwe.” (4:29)

Ibn ‘Abbas, Mujahid, Sa’id bin Jubayr, Qatadah na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم walisema kuwa:

وَلَا تَلْمِزُوا أَنْفُسَكُمْ

“...wala msivunjiane heshima.”

Maana yake: Msikashifiane. Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَنَابَزُوا بِاللِّقَبِّ^ط

“...wala msiitane kwa majina ya kejeli.”

Maana yake: Msiitane kwa majina ya utani, yaani yale yanayomchukiza mtu anapoyasikia. Imamu Ahmad alisimulia kutoka kwa Jubayr bin Adh-Dhahhak رضي الله عنه kuwa: “Aya hii ilishuka kutuhusu sisi, Banu Salamah,

وَلَا تَنَابَزُوا بِاللِّقَبِّ^ط

“...wala msiitane kwa majina ya kejeli.”

Alisema: “Mtume ﷺ alipohamia Madinah, alitukuta kila mtu akiwa na majina, ama mawili au matatu. Ikawa kwamba, Mtume ﷺ alipomuita mmojawapo kwa moja ya majina hayo, watu walimuambia: ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Huyo halipendi jina hilo.’” Ikateremshwa Aya:

وَلَا تَنَابَزُوا بِاللِّقَبِّ^ط

“...wala msiitane kwa majina ya kejeli.”¹

Abu Dawud pia aliikusanya Hadithi hii.² Kauli ya Allah تعالى:

بئسَ الْإِسْمُ الْفُسُوقُ بَعْدَ الْإِيمَانِ^ع

“Ni uovu kutumia jina baya baada ya kuisha amini.”

Maana yake: Sifa na jina baya ni ufasiki. Nayo ni kuitana kwa majina ya utani ambayo watu wa enzi za ujahili walikuwa wakiitana, baada ya kuingia kwenu ndani ya Uislamu na mkauelewa.

¹ Abu Dawud 4:460.

² Abu Dawud 5:246.

وَمَنْ لَّمْ يَتُوبْ

“Na wasiotubu...”

Dhidi ya dhambi hii,

فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

“...hao ndio wenye kudhulumu.”

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَبَ بَعْضُكُم بَعْضًا أَنُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَن يَأْكُلَ لَحْمَ أَخِيهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوهُ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾

12. “Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anayependa kuila nyama ya nduguye aliyekufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kupokea toba, Mwenye Kurehemu.”

Kukatazwa Dhana

Allah تعالیٰ Anawakataza waja Wake Waumini dhidi ya kukithirisha dhana. Hiyo ni kuwatuhumu na kuwafanyia khiyana wanafamilia, ndugu na watu wengine mahali wasipopastahiki kwani hayo huwa ni madhambi yaliyo wazi kabisa. Kwa hivyo, Waislamu wanatakiwa wajiepushe dhidi ya kukithirisha dhana pasi na msingi. Amiri wa Waumini, ‘Umar bin Al-Khattwab رضي الله عنه alisema: “Kamwe usilidhanie vyovyote neno lolote litokalo kwa nduguyo Muumini isipokuwa kheri, hali yakuwa wewe unaweza ukalichukulia vizuri”.¹ Imamu Malik رحمه الله تعالیٰ aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِيَّاكُمْ وَالظَّنَّ فَإِنَّ الظَّنَّ أَكْذَبُ الْحَدِيثِ، وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا تَحَسَّسُوا، وَلَا تَنَافَسُوا وَلَا تَحَاسَدُوا، وَلَا تَبَاغَضُوا وَلَا تَدَابَرُوا، وَكُونُوا عِبَادَ اللَّهِ إِخْوَانًا»

¹ Az-Zubd cha Imam Ahmad, Ad-Dur Al-Manthur 6:99

“Nakutahadharisheni na dhana, kwani hayo ni masimulizi ya uongo zaidi, wala msipelelezane, msihisiane vibaya, msioneane wivu, msihusudiane, msichukiane, msiamane, na enyi waja wa Allah! kuweni ndugu.”¹

Bukhari, Muslim na Abu Dawud wameipokea Hadithi hii.² Anas رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا تَقَاطَعُوا وَلَا تَدَابَرُوا وَلَا تَبَاغَضُوا وَلَا تَحَاسَدُوا، وَكُونُوا عِبَادَ اللَّهِ إِخْوَانًا، وَلَا يَجِلُّ لِلْمُسْلِمِ أَنْ يَهْجَرَ أَخَاهُ فَوْقَ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ»

“Wala msikatane, wala msipeane migongo, msichukiane, msihusudiane na muwe ndugu, enyi waja wa Allah! Wala si halali kwa Muislamu kumhama nduguye kwa zaidi ya siku tatu.”

Muslim na At-Tirmidhi amesema ni sahihi.³

وَلَا تَجَسَّسُوا

“Wala msipelelezane...”

Nyinyi kwa nyinyi. Mara nyingi, neno *“Tajassus”* katika lugha ya kiarabu hutumika katika shari, na mpelelezi huitwa *Jaasus*. Ama neno *“Tahassus”* katika nadharia ya lugha ya kiarabu mara nyingi huwa ni katika kheri. Ni sawa na Alivyosema Allah تعالى wakati alipoeleza habari kumhusu Yaqub عليه السلام kwamba alisema:

يَبْنِيَّ أَذْهَبُوا فَتَحَسَّسُوا مِنْ يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَأْتَسُوا مِنْ رُوحِ اللَّهِ

“Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye, wala msikate tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu.” (12:87)

Wakati mwingine, yote mawili hayo yanaweza kutumika katika shari. Ni kama ilivyokuja katika Sahih Mbili, kwamba Mtume ﷺ amesema:

¹ Al-Muwatta' 2:907.

² Fat'h Al-Bari 10:499.

³ Muslim:1983, Tuhfat Al-Ahwadhi 6:46.

«لَا تَجَسَّسُوا وَلَا تَحَسُّسُوا، وَلَا تَبَاغَضُوا وَلَا تَدَابَّرُوا، وَكُنُوا عِبَادَ اللَّهِ إِخْوَانًا»

“Wala Msipelelezane, msihisiane vibaya, msichukiane, wala msipeane migongo na kuweni waja wa Allah mliondugu!”¹

Awza’i رحمه الله تعالى amesema: “Maana ya *At-Tajassus* ni kutafuta kitu, na *At-Tahassus* ni kusikiliza mazungumzo ya watu ilhali wao hawapendi au kusikiliza milangoni mwao, na *At-Tadaabur* ni kitendo cha kila mtu kutokumjali mwenzake.” Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى aliyataarifu haya. Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا يَغْتَب بَّعْضُكُم بَعْضًا

“...wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi.”

Hii inakataza usengenyaji. Sharia imelifasiri hilo, kama ilivyotaarifiwa katika Hadithi ambayo aliiandika Abu Dawud kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ aliulizwa, “Kusengenyana ni nini?” Akajibu:

«ذُكْرُكَ أَخَاكَ بِمَا يَكْرَهُ»

“Kumtaja kwako nduguyo kwa anayoyachukia.”

Akaulizwa tena: “Unaonaje ikiwa hayo ninayoyasema kumhusu ndugu yangu ni ya kweli?” Akajibu:

«إِنْ كَانَ فِيهِ مَا تَقُولُ فَقَدْ اغْتَبْتَهُ، وَإِنْ لَمْ يَكُنْ فِيهِ مَا تَقُولُ فَقَدْ بَهْتَهُ»

“Ikiwa anayo unayosema, utakuwa umemsengenyana, na kama atakuwa sivyo ulivyosema, basi utakuwa umemzushia.”¹

Al-Tirmidhi aliitaarifu na akasema, “Ni Hasan Sahih.”²

Usengenyaji umekemewa vikali sana, kwa minajili hiyo, Allah تعالى Ameushabihisha na kula nyama ya mtu aliyefariki. Kauli ya Allah تعالى:

¹ *Fat’h Al-Bari* 10:496.

² Abu Dawud 5:191.

³ Muslim na. 2589, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:63.

أَتُحِبُّ أَحَدَكُمْ أَنْ يَأْكُلَ لَحْمَ أَخِيهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوهُ

“Je! Yupo katika nyinyi anayependa kuila nyama ya nduguye aliyekufa? Mnalichukia hilo!”

Maana yake: Kama ambavyo mnachukia kula nyama ya mtu kimaumbile, basi lichukieni hilo kisheria, kwani adhabu yake ni kali kuliko hilo la kwanza. Aya hii ni katika njia ya kuliogopesha na kulitahadharisha. Ni sawa na kauli ya Mtume ﷺ kuhusu mtu mwenye kurudia sadaka yake alioitoa,

«كَالْكَلْبِ يَبْقَىٰ ثُمَّ يَرْجِعُ فِي فَنِيهِ»

“Ni sawa na mbwa anayetapika, halafu anakula tena matapishi yake.”

Baada ya kutangulia kusema,

«لَيْسَ لَنَا مَثَلُ السَّوءِ»

“Sisi hatuna mfano mbaya.”¹

Imethibiti ndani ya vitabu kadha vya Sahih, Musnad kutokana na isnadi, njia za upokezi Hadithi mbalimbali. kwamba Mtume ﷺ alisema katika Khutuba ya Hija ya Kuaga:

«إِنَّ دِمَاءَكُمْ وَأَمْوَالَكُمْ وَأَعْرَاضَكُمْ عَلَيْكُمْ حَرَامٌ كَحُرْمَةِ يَوْمِكُمْ هَذَا، فِي شَهْرِكُمْ هَذَا، فِي بَلَدِكُمْ هَذَا»

“Kwa hakika, damu, mali na vyeo vyenu ni vitukufu kwenu sawa na utukufu wa siku yenu hii katika mwezi wenu huu na ndani ya mji wenu huu.”²

Abu Dawud aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema:

¹ Fat’h Al-Bari 5:278.

² Fat’h Al-Bari 3:670, Muslim 3:1306, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:481 na Ahmad 1:230.

«كُلُّ الْمُسْلِمِ عَلَى الْمُسْلِمِ حَرَامٌ مَالُهُ وَعِرْضُهُ وَدَمُهُ، حَسْبُ امْرِئٍ مِنَ الشَّرِّ أَنْ
يَخْتَرِ أَخَاهُ الْمُسْلِمَ»

"Kila Muislamu kwa Muislamu mwenzake ni haramu mali yake, cheo chake na damu yake. Inatosha kuwa katika shari mtu kumdharau nduguye Muislamu."¹

Tirmidhi aliikusanya Hadithi hii na akasema ni Hasan Gharib.²

Hafidh Abu Ya'laa رحمه الله تعالى alinukuu kuwa binamu yake Abu Hurayra رضي الله عنه amesema kuwa Ma'iz رضي الله عنه alikuja kwa Mtume ﷺ na kusema: "Ewe Mjumbe wa Allah! Mimi nimezini." Mtume ﷺ akageuza uso wake upande mwingine mpaka Ma'iz aliporudia maneno hayo mara nne. Ilipofikia mara ya tano, akamhoji:

«رُئِيتَ؟»

"Umezini?"

Akajibu: "Ndiyo." Akamsaili tena:

«وَتَذَرِي مَا الزُّنَا؟»

"Unajua zina ni nini?"

Ma'iz رضي الله عنه akajibu: "Nimefanya na mwanamke kwa njia ya haramu ambalo mume hufanya na mkewe kihalali." Mtume ﷺ akamuuliza:

«مَا تُرِيدُ إِلَىٰ هَذَا الْقَوْلِ؟»

"Kwa kauli hii unamaanisha nini."

Akajibu "Ninataka unitakase." Mtume ﷺ akamuuliza:

«أَدْخَلْتَ ذَلِكَ بَيْنَكَ فِي ذَلِكَ بَيْنَهَا كَمَا يَغِيبُ الْمَيْلُ فِي الْمُكْحَلَةِ وَالرَّشَا فِي الْبُرِّ؟»

"Umemuvingia kama kijiti kinavyoingia ndani ya kichupa cha wanja na kama kamba inavyoingia kisimani?"

¹ Abu Dawud 5:195.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:54.

Akajibu: “Ndiyo ewe Mjumbe wa Allah!” Mtume ﷺ akaamuru apigwe mawe. Akarujumiwa. Mtume ﷺ akawasikia watu wawili, mmoja akimuambia mwenzake: “Je umemuona mtu ambaye Allah تعالى Amemfichia siri yake, lakini moyo wake haukumpa fursa, mpaka akarujumiwa kama mbwa hadi akafariki.” Mtume ﷺ akaendelea kwenda, mpaka akapita karibu ya mzoga wa punda, akauliza:

«أَيْنَ فُلَانٌ وَفُلَانٌ؟ انْزِلَا فَكَلَّا مِنْ جِيفَةِ هَذَا الْجَمَارِ»

“Yuko wapi fulani na fulani? Teremkeni na mle mzoga wa punda huyu.”

Wakasema: “Allah تعالى Akughufirie, ewe Mjumbe wa Allah ﷺ! Kwani huyu analiwa?” Akajibu:

«فَمَا بَلْتُمَا مِنْ أَخِيكُمَا إِنَّمَا أَشَدُّ أَكْثَلًا مِنِّي، وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! إِنَّهُ الْآنَ لَعَنِي أَنْهَارِ الْجَنَّةِ يَنْغَمِسُ فِيهَا»

“Basi, mlichokipata kutokana na kumsengenya ndugu yenu hivi punde ni chakula kibaya zaidi kuliko hiki. Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Huyu kwa sasa anaogelea katika mito ya Pepo.”¹

Isnadi (njia ya upokezi) wa Hadithi hii ni Sahih. Imamu Ahmad alimnukuu Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنه kuwa alisema: Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ, upepo ukapeperusha harufu mbaya ya uvundo. Mtume ﷺ akasema:

«أَتَدْرُونَ مَا هَذِهِ الرِّيحُ؟ هَذِهِ رِيحُ الَّذِينَ يَغْتَابُونَ النَّاسَ»

“Je mnajua harufu hii ni ya nini? Hii ni harufu ya wenye kuwasengenya watu.”²

¹ Musnad Abu Ya'la 6:524, kadhalika iliandikwa na Abu Dawud, na. 4428.

² Ahmad 3:351

Katika Kukubaliwa Toba ya Msengenyaji na Mfitinishi

Kauli ya Allah تعالى:

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu.”

Katika Aliyokuamrisheni kuyafanya na Aliyokukatazeni. Muwe makini katika kuyachunga hayona muogopeni Yeye,

إِنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ رَّحِيمٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.”

Maana yake: Ni Mwenye Kukubali toba ya mwenye kutubia Kwake, ni Mwenye Huruma kwa mwenye kurejea Kwake na kumtegemea Yeye. Maulamaa wengi wamesema: Namna ya toba ya mwenye kuwasengenywa watu ni kuiacha tabia hiyo na kuazimia kwamba hatarudia. Je ni sharti kuyajutia yaliyopita? Hilo lina rai nyingi, pia kuhusu iwapo akaombe msamaha kwa aliwasengenywa? Wengine wamesema kwamba si sharti kuwaomba msamaha, kwani akifanya hivyo, huenda wakaumia zaidi kuliko asipofanya hivyo. Kwa hivyo, ni bora, awasifie katika vikao ambavyo alikuwa akiwafanyia dhambi hiyo. Pia awatetee dhidi ya kusengenywa zaidi, kwa uwezo wake wote ili hiyo iweze kuyafuta madhambi yaliyopita.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاهُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا ۗ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقَىٰكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

13. “Enyi watu! Hakika Sisi Tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na Tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamungu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Habari.”

Wanaadamu Wote ni Wazao wa Adam عليه السلام na Hawa

Allah تعالى Anawatangazia watu kwamba Aliwaumba kutokana na mtu mmoja na kutokana naye, alimuambia mkewe. Hao ni Adam عليه السلام na Hawa na kutokana nao akafanya mataifa yenye makabila ambayo yamegawanyika tena katika makundi, koo na kadhalika. Ilisemwa pia, kuwa maana ya *Shu'uub* ni wasio Waarabu na *Kabaa-il* ni Waarabu. Ni sawa na ilivyo kwamba *Asbaat* ni Waisrael. Kauli nyingi juu ya hili zilikusanywa katika utangulizi wa kitabu, Al-Ashbaah cha Abu 'Umar bin 'Abdul-Bar رحمه الله تعالى na kitabu kingine, *Al-Qasd Wal-Umam Fiy Ma'rifat Ansaab Al-'Arab wal—'Ajam*.

Kwa hivyo, watu wote, kwa nasaba ya udongo, wanatokana na Adam عليه السلام na Hawa wana hadhi sawa. Kinachowafanya wazidiane kwa fadhila ni mambo ya dini, ambayo ni kumtii Allah تعالى na kumfuata Mjumbe Wake .

Kwa hivyo, baada ya kukataza mambo ya usengenyi na dharau baina ya watu, Allah تعالى Ameerza juu ya usawa wao katika utu. Allah تعالى Amesema:

يَتَأْتِيَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاهُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا^٤

“Enyi watu! Hakika Sisi Tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na Tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane.”

Maana yake: ili kuwepo kujuana kwamba kila mmoja anarejea kwenye kabila lake. Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

لِتَعَارَفُوا^٤

“...ili mjuane.”

Kama ambavyo huitwa, “Fulani bin fulani kutoka katika kabila fulani.”¹

Sufyan Thawri رحمه الله تعالى amesema: “*Wa-Himyar* (ambao waliishi Yemen) walikuwa wakijinasibisha na majimbo yao na Waarabu wa Hijaz walijitambulisha kwa makabila yao.”

¹ At-Tabari 22:312.

Utukufu Hupatikana kwa Uchamungu

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقَنُّكُمْ^٤

“Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamungu zaidi katika nyinyi.”

Wanapata heshima mbele ya Allah تعالى kwa uchamungu, si kwa koo. Kuna Hadithi nyingi za Mtume ﷺ zinazolizungumzia hilo.

Bukhari alitaarifu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ aliulizwa, ‘Ni nani mtukufu zaidi miongoni mwa watu?’ Akajibu:

«أَكْرَمُهُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقَاهُمْ»

“Mtukufu wao mbele ya Allah ni mchamungu wao zaidi.”

Wakasema: “Hatukuulizi juu ya hilo.” Akasema:

«فَأَكْرَمُ النَّاسِ يُوسُفُ نَبِيُّ اللَّهِ، ابْنُ نَبِيِّ اللَّهِ، ابْنِ نَبِيِّ اللَّهِ ابْنِ خَلِيلِ اللَّهِ»

“Mtukufu zaidi kwa watu ni Nabii wa Allah, Yusuf mwana wa Nabii wa Allah, mwana wa Nabii wa Allah, mwana wa Khalil wa Allah.”

Wakasema: “Hatukuulizi juu ya hilo.” Akawauliza:

«فَعَنْ مَعَادِنِ الْعَرَبِ تَسْأَلُونِي؟»

“Je mnaniuliza juu ya asili ya Waarabu?”

Wakajibu: “Ndiyo.”

«فَخِيَارُكُمْ فِي الْجَاهِلِيَّةِ خِيَارُكُمْ فِي الْإِسْلَامِ إِذَا فَتَهُرَا»

“Wabora wenu katika zama za ujahili ndiyo wabora wenu katika Uislamu wakijua dini.”¹

¹ Fat’h Al-Bari 8:212.

Bukhari aliihusanya Hadithi hii katika sehemu nyingi ndani ya Sahih yake,¹ pia Nasai katika sehemu ya Tafsir.²

Muslim aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ اللَّهَ لَا يَنْظُرُ إِلَى صُورِكُمْ وَأَمْوَالِكُمْ وَلَكِنْ يَنْظُرُ إِلَى قُلُوبِكُمْ وَأَعْمَالِكُمْ»

“Hakika Allah Hazitizami sura na mali zenu, bali Anaangalia nyoyo zenu na amali zenu.”³

Ibn Majah aliihusanya Hadithi hii.⁴ Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما amesema: Katika siku ya kuikomboa Makkah, Mtume ﷺ alitufu akiwa juu ya Ngamia wake, Al-Qaswaa, na alikuwa akizigusa nguzo kwa fimbo aliyokuwa nayo mkononi. Hakupata mahali ndani ya msikiti ambapo ngamia wake angekaa na Mtume ﷺ akateremka katika mikono ya watu. Akamuongoza ngamia wake bondeni ambapo alikaa. Baadaye, Mtume ﷺ aliwakhutubia huku akiwa juu ya ngamia wake. Alimshukuru Allah تعالى na akamsifu kama Anavyostahiki, akasema:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ! إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى قَدْ أَذْهَبَ عَنْكُمْ عِبَّةَ الْجَاهِلِيَّةِ وَتَعَظَّمَهَا بِأَبَائِهَا، فَالنَّاسُ رَجُلَانِ: رَجُلٌ بَرٌّ تَقِيٌّ كَرِيمٌ عَلَى اللَّهِ تَعَالَى، وَرَجُلٌ فَاجِرٌ شَقِيٌّ هَيْنٌ عَلَى اللَّهِ تَعَالَى، إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يَقُولُ: ﴿يَتَأْتِيَ النَّاسُ إِنَّا خَلَقْتُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقْوَمُ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ﴾»

“Enyi watu! Allah Taala Amekuondoleeni kujifakharisha kwa kijahili wa kijahiliya na desturi zao za kutukuza baba zao. Watu ni wa namna mbili, mtu mwema, mchamungu na mwenye heshima kwa Allah Taala, mwingine ni mtu muovu, mtenda dhambi na duni kwa Allah. Allah Taala Anasema: ‘Enyi watu! Hakika Sisi Tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na Tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu

¹ Fat’h Al-Bari 6:477 na 481.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:367.

³ Muslim 4:1987.

⁴ Ibn Majah 2:1388.

zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamungu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Habari.'"

Akasema:

«أَقُولُ قَوْلِي هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللَّهَ لِي وَلَكُمْ»

"Ninaitamka kauli yangu hii, na ninamuomba Allah Anighufirie mimi na nyinyi."

Hii ilinukuliwa na 'Abd bin Humayd.¹ Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ

"Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Habari."

Maana yake: Anakujueni na Anayajua mambo yenu, basi Yeye Humuongoa Amtakaye na Humpoteza Amtakaye, Humrehemu Amtakaye na Humuadhibu Amtakaye na Humfadhilisha Amtakaye juu ya Awatakao.

Yeye ni Mwingi wa Hekima, Mwingi wa Kujua, Mwingi wa Habari katika hayo yote.

Maulamaa kadha wameitegemea Aya hii na Hadithi hizi tukufu kwamba suala la *kufu* si sharti katika nikahi², sharti ni Dini tu. Ni kutokana na Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ

"Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamungu zaidi katika nyinyi."

* * *

¹ Al-Muntakhab cha 'Abd bin Humayd 793.

² Kuhusiana na hadhi katika jamii, mali, familia, ukoo n.k.

* قَالَتِ الْأَعْرَابُ ءَأَمْنَا ۗ قُلْ لَمْ تُوْمِنُوا وَلَكِنْ قُولُوا
 * قَالَتِ الْأَعْرَابُ ءَأَمْنَا ۗ قُلْ لَمْ تُوْمِنُوا وَلَكِنْ قُولُوا
 أَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ الْإِيْمَانُ فِي قُلُوْبِكُمْ ۗ وَإِنْ تُطِيعُوا اللَّهَ
 وَرَسُوْلَهُ لَا يَلْتَكُم مِّنْ أَعْمَالِكُمْ شَيْءًا ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ
 ﴿١٤﴾ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُوْلِهِ ثُمَّ
 لَمْ يَرْتَابُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيْلِ اللَّهِ ۗ
 أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّٰدِقُونَ ﴿١٥﴾ قُلْ أَتَعْلَمُونَ اللَّهَ
 بِدِيْنِكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ
 وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿١٦﴾ يٰمُنُوْنَ عَلَيْكَ أَنْ أَسْلَمُوا ۗ قُلْ
 لَا تَمْنُوا عَلَيَّ إِسْلَمَكُمْ ۗ بَلِ اللَّهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ أَنْ هَدَيْتُكُمْ
 لِلْإِيْمَانِ ۖ إِنَّ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿١٧﴾ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ غَيْبَ
 السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ بَصِيْرٌ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٨﴾

* قَالَتِ الْأَعْرَابُ ءَأَمْنَا ۗ قُلْ لَمْ
 تُوْمِنُوا وَلَكِنْ قُولُوا أَسْلَمْنَا
 وَلَمَّا يَدْخُلِ الْإِيْمَانُ فِي قُلُوْبِكُمْ ۗ وَإِنْ
 تُطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُوْلَهُ لَا يَلْتَكُم مِّنْ
 أَعْمَالِكُمْ شَيْءًا ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ
 ﴿١٤﴾ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُوْلِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا
 وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي
 سَبِيْلِ اللَّهِ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ
 الصَّٰدِقُونَ ﴿١٥﴾ قُلْ أَتَعْلَمُونَ
 اللَّهَ بِدِيْنِكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا فِي
 السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ

شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿١٦﴾ يٰمُنُوْنَ عَلَيْكَ أَنْ أَسْلَمُوا ۗ قُلْ لَا تَمْنُوا عَلَيَّ إِسْلَمَكُمْ ۗ بَلِ اللَّهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ أَنْ هَدَيْتُكُمْ
 لِلْإِيْمَانِ ۖ إِنَّ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿١٧﴾ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ غَيْبَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ بَصِيْرٌ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٨﴾

14. "Mabedui wamesema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani Imani haijaingia katika nyoyo zenu. Na mkimtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Hatakupunguzieni chochote katika vitendo vyenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."

15. "Hakika Waumini ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wakweli."

16. "Sema: Ati ndio mnamfundisha Mwenyezi Mungu Dini yenu, na hali Mwenyezi Mungu Anayajua ya katika mbingu na ardhi, na Mwenyezi Mungu Anajua kila kitu?"

17. “Wanakusimbulia kuwa wamesilimu! Sema: Msinisimbulie kwa kusilimu kwenu. Bali Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekufanyieni hisani kwa Kukuongoeni kwenye Imani, ikiwa nyinyi ni wakweli.”

18. “Hakika Mwenyezi Mungu Anajua siri za mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu Anayaona myatendayo.”

Tofauti Baina ya Muumini na Muislamu

Allah تعالى Anawaambia mabedui ambao baada tu ya kuingia katika Uislamu walidai kuwa wana imani ya kweli, ilhali, bado imani ilikuwa haijamakinika katika nyoyo zao,

قَالَتِ الْأَعْرَابُ ءَأَمَّنَّا قُلْ لَمْ تُؤْمِنُوا وَلَكِنْ قُولُوا أَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ الْإِيمَانُ فِي قُلُوبِكُمْ

“Mabedui wamesema: Tumeamini.Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani Imani haijaingia katika nyoyo zenu.”

Aya hii tukufu imeleta faida kuwa Imani ni jambo makhususi zaidi kuliko Uislamu, kwa mujibu wa maulamaa wa *Sunna wal-Jama'ah*. Hadithi ya Jibril عليه السلام inajulisha jambo hilo, pindi alipouliza kuhusu Uislamu, halafu juu ya Imani, na baadaye kuhusu Ihsan. Kwa hivyo alikuwa akihama kutoka katika jambo la ujumla na kuliendea lililo makhususi zaidi.

Imamu Ahmad alimnukuu Sa'd bin Abu Waqqaas رضي الله عنه kuwa amesema Mtume ﷺ aliwapa watu kitu, wala hakumpatia mtu mmoja miongoni mwao. Sa'd رضي الله عنه akasema: “Ewe Mjumbe wa Allah! Umempa kitu fulani na fulani, wala fulani hukumpa, ilhali yeye pia ni Muumini.” Mtume ﷺ akasema:

«أَوْ مُسْلِمٍ؟»

“Au Muislamu?”

Mpaka Sa'd رضي الله عنه akarudia kusema hivyo mara tatu, na Mtume ﷺ anasema:

«أَوْ مُسْلِمٍ؟»

“Au Muislamu.”

Kisha, Mtume ﷺ akasema:

«إِنِّي لَأَعْطِي رَجَالًا وَأَدْعُ مَنْ هُوَ أَحَبُّ إِلَيَّ مِنْهُمْ، فَلَمْ أُعْطِهِ شَيْئًا مَخَافَةَ أَنْ يُكْبَرُوا فِي النَّارِ عَلَيَّ وَجُودِهِمْ»

“Hakika mimi ninaweza kuwapa watu, na nikamuacha nimpandaye zaidi kuliko wao, wala sikumpa yeye kitu, kwa kuchelea kwamba wasije kutupwa Motoni kwa kuangukia juu ya nyuso zao.”¹

Hadithi hii imenukuliwa katika Sahih Mbili.²

Mtume ﷺ amepambanua baina ya Muumini na Muislamu, na akajulisha kuwa Imani ni makhususi zaidi kuliko Islam. Haya tumeyakariri pamoja na ushahidi wake, ndani ya Kitabu cha Imani katika Sahih Al-Bukhari. Hamdi na shukrani zinamstahiki Allah تعالى.

Hili linaonesha kwamba mabedui waliotajwa katika Aya hii, hawakuwa wanafiki, bali Waislamu ambao Imani ilikuwa bado haijawa imara katika nyoyo zao. Wakadai kufikia hadhi ya juu kuliko waliyoifikia, wakapewa mafunzo kuhusu hilo. Hii ndiyo maana iliyomo katika kauli ya Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Ibrahim Nakha’i رحمه الله تعالى na Qatadah رحمه الله تعالى. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amehitari. Na kwa hakika, hao waliambiwa kwa njia ya mafunzo:

قُلْ لَمْ تَوْفِنُوا وَلَكِنْ قُولُوا أَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ الْإِيمَانُ فِي قُلُوبِكُمْ
“...Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu.”

Maana yake: Bado hamjaifikia Imani ya uhakika. Kisha, Allah تعالى Akasema:

وَأَنْ تُطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ، لَا يَلْتَمِسُ مِنْكُمْ شَيْئًا

“Na mkimt’ii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Hatakupunguzieni chochote katika vitendo vyenu.”

Maana yake: Hakitapungua kitu katika malipo yenu. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

¹ Ahmad 1:176.

² Fat’h Al-Bari 1:99, Muslim 1:132.

وَمَا أَلْتَنَّهُمْ مِّنْ عَمَلِهِمْ مِن شَيْءٍ^ع

**“...na wala Hatutawapunja hata kidogo katika vitendo vyao.”
(52:21)**

Kauli ya Allah تعالی:

إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Maana yake: Kwa mwenye kutubu Kwake na kurejea Kwake.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ

“Hakika Waumini...”

Maana yake: Hakika waumini wakamilifu.

الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا

“...ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake tena wasitie shaka kabisa...”

Inamaanisha, hawawi na mashaka, wala hawatetereki, bali huwa imara katika hali moja, ambayo ni kusadikisha kwa wazi.

وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ^ع

“...na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao.”

Maana yake: Na wakayatoa maisha yao na mali zao za thamani kubwa katika kumtii Allah تعالی na kutafuta Radhi Zake,

أُولَئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

“Hao ndio wakweli.” Maana yake: Katika kauli zao, pindi wasemapo kwamba wao ni Waumini. Si kama baadhi ya mabedui ambao hawakuwa na chochote katika Imani, zaidi ya kauli ya juu juu tu.

Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ أَتُعَلِّمُونَ اللَّهَ بِدِينِكُمْ

“Sema: Ati ndio mnamfundisha Mwenyezi Mungu Dini yenu...”

Maana yake: Je, mnampa Allah تعالى habari za yaliyo katika dhamiri zenu?,

وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

“...na hali Mwenyezi Mungu Anayajua ya katika mbingu na Ardhi...”

Maana yake: Hakifichami dhidi Yake kitu chochote hata cha uzito wa mdudu chungu, ardhini wala mbinguni, wala kidogo au kikubwa zaidi,

وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“...na Mwenyezi Mungu Anajua kila kitu?”

Kisha, Allah تعالى Akasema:

يَمُنُونَ عَلَيْكَ أَنْ أَسْلَمُوا قُلْ لَا تَمُنُوا عَلَيَّ إِسْلَمَكُمْ

“Wanakusimbulia kuwa wamesilimu! Sema: Msinisimbulie kwa kusilimu kwenu.”

Maana yake: Mabedui ambao wanaomsimanga kwa kusilimu kwao, kumfuata na kumsaidia Mtume ﷺ, Allah تعالى Anawajibu:

قُلْ لَا تَمُنُوا عَلَيَّ إِسْلَمَكُمْ

“Sema: Msinisimbulie kwa kusilimu kwenu.”

Kwani manufaa yake yanakurudieni nyinyi, na juu yenu ni kumshukuru Allah تعالى ndani yake.

بَلِ اللَّهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ أَنْ هَدَيْتُمُوهَا لِلْإِيمَانِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

“Bali Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekufanyieni hisani kwa Kukuongoeni kwenye Imani, ikiwa nyinyi ni wakweli.”

Maana yake: Katika madai yao hayo. Ni sawa na kauli ya Mtume ﷺ kuwaambia Answaar katika siku ya vita vya Hunayn,

«يَا مَعْشَرَ الْأَنْصَارِ! أَلَمْ أَجِدْكُمْ ضَلَّالًا فَهَدَاكُمْ اللَّهُ بِبِي؟ وَكُنْتُمْ مُتَمَرِّقِينَ فَأَلْفَكُمُ اللَّهُ بِبِي؟ وَكُنْتُمْ عَالَةً فَأَغْنَاكُمْ اللَّهُ بِبِي؟»

“Enyi kundi la Answaar! Je, sikukukuteni mkiwa wapotevu, Allah Akakuongoeni, kupitia kwangu? Mlikuwa mliofarakana, Allah Akakuunganisheni, kupitia kwangu? Na mlikuwa masikini, Allah Akakutajirisheni, kupitia kwangu?”

Kila mara Mtume ﷺ aliponena jambo, walisema, “Allah تعالى na Mjumbe Wake ni wenye fadhila nyingi.”¹

Hafidh Abu Bakr Bazzar رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Banu Asad walikuja kwa Mtume ﷺ wakasema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Sisi tumesilimu, na Waarabu wamepigana dhidi yako, lakini sisi hatukupigana nawe.” Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ فِيهِمْ قَلِيلًا وَإِنَّ الشَّيْطَانَ يَنْطِقُ عَلَىٰ أَلْسِنِهِمْ»

“Kwa hakika, wewevu wao ni wachache na Shetani anaongea kupitia katika ndimi zao.”

Ikateremshwa Aya hii:

يَمُنُونَ عَلَيْكَ أَنْ أَسْلَمُوا ۗ قُلْ لَا تَمُنُوا عَلَيَّ إِسْلَمَكُمْ ۗ بَلِ اللَّهُ يَمُنُ عَلَيْكُمْ أَنْ هَدَاكُمْ لِلْإِيمَانِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧٧﴾

“Wanakusimbulia kuwa wamesilimu! Sema: Msinisimbulie kwa kusilimu kwenu. Bali Mwenyezi Mungu ndiye Aliyekufanyieni hisani kwa Kukuongoeni kwenye Imani, ikiwa nyinyi ni wakweli.”²

Kisha, Allah تعالى Alikumbusha kwamba, Yeye Ana ilimu juu ya viumbe wote na pia Anazona amali zao zote. Allah تعالى Alisema:

¹ Fat’h Al-Bari 7:644.

² An-Nasai katika Al-Kubra 11519.

إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ غَيْبَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Anajua siri za mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu Anayaona myatendayo.”

Mwisho wa tafsiri ya *Suratu Al-Hujurat*. Hamdi na Shukurani zinamstahiki Allah تعالیٰ, na Kwake Ndiko kwenye taufiki na Kuhifadhika dhidi ya makosa.

* * *

Tafsiri ya Suratu Qaf Sura ya 50 Iliteremshwa Makkah

Mwanzo wa Sehemu ya *Mufasswal*¹ katika Qur'an:

Sura hii ndiyo ya mwanzo katika fungu la *Mufasswal* (Sura zenye Aya fupi fupi) katika Qur'an, kwa mujibu wa rai sahihi. Husemwa kuwa sehemu ya *Mufasswal* inaanzia katika *Surat Al-Hujurat*. Baadhi ya watu wasiokuwa na utambuzi wa elimu na Dini wanasema kuwa *Mufasswal* inaanzia katika Sura 'Amma" yaani sura *An-Naba*, (sura ya 78), hata hivyo, hiyo si kweli kwa sababu hakuna yeyote katika wanazuoni aliyeiunga mkono rai hii wanaozingatwa katika elimu (Allah ﷻ Awarehemu). (Bin Hudhayfah) amesema; "Niliwauliza Masahaba wa Mtume ﷺ namna walivyogawa mafungu ya Qur'an." Wakajibu; 'Sehemu tatu, tano, saba, tisa, kumi na moja, kumi na tatu na sehemu ya *Mufasswal* kuwa ni moja.' Haya yameandikwa na Ibn Majah na Imamu Ahmad.²

Ikiwa utahesabu sura arubaini na nane, basi itakayofuata itakuwa *Qaf*. Ufafanuzi wake ni huu ufuatao: Sura tatu za mwanzo: *Al-Baqarah*, *Ali 'Imran* na *An-Nisa'*. Sura tano ni *Al-Ma'idah*, *Al-An'am*, *Al-Araf*, *Al-Anfal* na *Bara'ah* (au *At-Tawbah*). Sura saba zinazofuata ni *Yunus*, *Hud*, *Yusuf*, *Ar-Ra'd*, *Ibrahim*, *Al-Hijr* na *An-Nahl*. Sura tisa baada ya hizo ni *Subhan* (au *Al-Isra'*), *Al-Kahf*, *Maryam*, *Ta Ha*, *Al-Anbiya'*, *Al-Hajj*, *Al-Mu'minun*, *An-Nur* na *Al-Furqan*. Sura kumi na moja baada ya hizo ni *Ash-Shu'ara*, *An-Naml*, *Al-Qasas*, *Al-Ankabut*, *Ar-Rum*, *Luqman*, *Alif Lam Mim As-Sajdah*, *Al-Ahzab*, *Saba'*, *Fatir* na *Ya Sin*. Sura kumi na tatu baada ya hizo ni *As-Saffat*, *Sad*, *Az-Zumar*, *Ghafir*, *Ha Mim As-Sajdah* (au *Fussilat*), *Ash-Shura*, *Az-Zukhruf*, *Ad-Dukhan*, *Al-Jathiyah*, *Al-Ahqaf*, *Al-Qital* (au *Muhammad*), *Al-Fath* na *Al-Hujurat*. Baada ya hapo inakuja sehemu ya *Mufasswal*, kwa mujibu wa Masahaba. Hivyo, *Surat Qaf* ni ya awali katika sehemu ya *Mufasswal*, kama tulivyoeleza, kila Sifa Njema Inamstahiki Allah ﷻ na fadhila zote ni kutoka Kwake.

¹ *Mufassal* hapa inamaanisha sura fupi fupi zinaanzia Surah Qaf mpaka mwisho wa Qur'an

² Abu Dawud 2:114, Ibn Majah 1:422 na Ahmad 4:9. Hii ni sehemu ya Hadithi dhaifu ambayo iliondolewa.

Fadhila za *Surat Qaf*

Imamu Ahmad ameandika kuwa, 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alimuuliza Abu Waqid Al-Laythi رضي الله عنه, "Mtume ﷺ alisoma nini katika Sala za Idi?" Abu Waqid رضي الله عنه akajibu, "*Surat Qaf na Surat Iqtarabat (yaani Surat Al-Qamar).*" Muslim na wakusanyaji wane wa Sunan waliikusanya Hadithi hii.¹

Hadithi nyingine:

Imamu Ahmad aliandika kuwa Umm Hisham bint Harithah رضي الله عنها alisema, "Tanuri letu na la Mtume ﷺ lilikuwa moja kwa kadiri ya miaka miwili, au mwaka mmoja na zaidi, nami sikuhifadhi Surat,

ق وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ ﴿١﴾

Qaaf. Naapa kwa Qur'ani Tukufu!

Isipokuwa kutoka katika ulimi wa Mtume ﷺ ambaye alikuwa akiisoma kila siku ya Ijumaa huku akiwa amesimama juu ya Mimbari akiwahutubia watu.² Muslim aliikusanya Hadithi hii.³

Abu Dawud pia aliandika kuwa binti wa Al-Harith bin An-Nu'man رضي الله عنها amesema, "Mimi nilihifadhi *Surat Qaf* kutoka katika mdomo wa Mtume ﷺ ambaye alikuwa akiisoma katika kila hotuba ya Ijumaa. Tanuri letu na Mtume ﷺ lilikuwa moja."⁴ Muslim na An-Nasa'i waliikusanya Hadithi hii.⁵

Hivyo, Mtume ﷺ alikuwa akiisoma Sura hii wakati wa mikusanyiko mikubwa kama vile hotuba za Idi na Ijumaa. Alifanya hivyo kwa sababu Sura hii ina habari za kuanza kwa Uumbaji, Ufufuo, Kurejea, Kusimama (mbele ya Allah تعالى), Hesabu, Pepo, Moto, Malipo kutoka kwa Allah تعالى na Adhabu, Kuhamasisha na Kuogopesha. Allah ni تعالى Mjuzi zaidi.

* * *

¹ Ahmad 5:217, Muslim 2:607, Abu Dawud 1:683, *Tuhfat Al-Ahwadhi*, An-Nasai katika *Al-Kubra* 3:79, 3:183 na Ibn Majah 1:408.

² Ahmad 6:435.

³ Muslim 2:595.

⁴ Abu Dawud 1:660.

⁵ Muslim 2:595, An-Nasai katika *Al-Kubra* 3:107.

سُورَةُ الْقَافِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قَافٌ وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ ﴿١﴾ بَلْ عَجِبُوا أَنْ جَاءَهُمْ مُنْذِرٌ
 مِنْهُمْ فَقَالَ الْكٰفِرُونَ هَذَا شَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٢﴾ أَوَدَا مِثْنَا
 وَكُنَّا تُرَابًا ۗ ذٰلِكَ رَجْعٌ بَعِيدٌ ﴿٣﴾ قَدْ عَلِمْنَا مَا تَنْقُصُ
 الْأَرْضُ مِنْهُمْ ۗ وَعِنْدَنَا كِتَابٌ حَفِيفٌ ﴿٤﴾ بَلْ كَذَّبُوا
 بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ فَهُمْ فِي أَمْرٍ مَرِيجٍ ﴿٥﴾ أَقَلَّمْ يَنْظُرُوا
 إِلَى السَّمَاءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنَاهَا وَزَيَّنَّاهَا وَمَا لَهَا مِنْ فُرُوجٍ
 ﴿٦﴾ وَالْأَرْضَ مَدَدْنَاهَا وَأَلْقَيْنَا فِيهَا رَوَاسِيَ وَأَوْبَقْنَا فِيهَا
 مِنْ كُلِّ زَوْجٍ بَهِيجٍ ﴿٧﴾ تَبَصَّرَةٌ وَذِكْرَىٰ لِكُلِّ عَبْدٍ مُّبِينٍ
 ﴿٨﴾ وَنَزَّلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً مُّبْرَكًا فَأَنْبَتْنَا بِهِ جَنَّاتٍ
 وَحَبَّ الْحَصِيدِ ﴿٩﴾ وَالنَّخْلَ بَاسِقَاتٍ لَهَا طَلْعٌ نَضِيدٌ ﴿١٠﴾
 رِزْقًا لِّلْعِبَادِ ۗ وَأَحْيَيْنَا بِهِ بَلَدَةً مَيِّتًا ۗ كَذٰلِكَ الْخُرُوجُ ﴿١١﴾
 كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَأَصْحَابُ الرَّسِّ وَثَمُودُ ﴿١٢﴾ وَعَادُ
 وَفِرْعَوْنُ وَإِخْوَانُ لُوطٍ ﴿١٣﴾ وَأَصْحَابُ الْأَيْكَةِ وَقَوْمُ تُبَّعٍ
 كُلٌّ كَذَّبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ وَعِيدِ ﴿١٤﴾ أَفَعَيَيْنَا بِالْخَلْقِ الْأَوَّلِ
 بَلْ لَمْ يَكُنِ فِي لَبْسٍ مِّنْ خَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٥﴾

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi
 wa Rehema Mwenye
 Kurehemu

قَافٌ وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ ﴿١﴾ بَلْ
 عَجِبُوا أَنْ جَاءَهُمْ مُنْذِرٌ مِنْهُمْ فَقَالَ
 الْكٰفِرُونَ هَذَا شَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٢﴾
 أَوَدَا مِثْنَا وَكُنَّا تُرَابًا ۗ ذٰلِكَ رَجْعٌ
 بَعِيدٌ ﴿٣﴾ قَدْ عَلِمْنَا مَا تَنْقُصُ
 الْأَرْضُ مِنْهُمْ ۗ وَعِنْدَنَا كِتَابٌ حَفِيفٌ
 ﴿٤﴾ بَلْ كَذَّبُوا بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ
 فَهُمْ فِي أَمْرٍ مَرِيجٍ ﴿٥﴾

1. Qaaf. Naapa kwa Qur'ani
 Tukufu!

2. Bali wanastaajabu
 kwamba amewafikia
 mwonyaji kutoka miongoni
 mwao, na wakasema
 makafiri: Hili ni jambo la
 ajabu!

3. Ati tukifa na tukawa
 udongo? Kurejea huko kuko
 mbali!

4. Hakika Sisi Tunajua kiasi cha kila kinachopunguzwa na ardhi kutokana nao. Na Kwetu kipo Kitabu kinachohifadhi yote.

5. Lakini waliikanusha Haki ilipowajia; kwa hivyo wamo katika mambo yenye mchanganyiko na mgongano.

ق

“Qaaf.” Ambayo ni mojawapo katika herufi za alfabeti zinazotajwa mwanzoni mwa baadhi ya Sura, kama vile,

ص

“Sad.” (38:1)

ن

“Nun.” (68:1)

الم

“Alif Lam Mim.” (2:1)

حم

“Ha Mim.” (40:1) na

طسم

“Twa Sin Mim” (28:1)

Na kadhalika. Mujahid na wengine kadha wamesema hivyo. Pia tulizungumzia jambo hili mwanzoni mwa maelezo ya *Surat Al-Baqarah* kiasi cha kutosha kutoyarudia hapa.

Makafiri Wanaustaajabia Ujumbe na Ufufuo

Allah تعالى Amesema,

وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ

“Naapa kwa Qur’ani Tukufu!”

Maana yake, ‘Naapa kwa Qur’an Tukufu na yenye hadhi.’

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ ۚ تَنْزِيلٌ مِنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

“Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye Hikima, Mwenye Kutukuzwa.” (41:42)

Jawabu la kiapo hiki katika Aya hii ndio madhumuni ya maneno baada ya kiapo, nayo ni kufafanua Utume, Ufufuo na kuthibitisha kuwa hayo ni ya kweli,

japokuwa kiapo hiki hakikubeba tamko la wazi. Mifano hii ni mingi ndani ya Qur'an, kama ilivyotangulia katika Kauli Yake,

ص وَالْقُرْآنِ ذِي الذِّكْرِ ﴿١٠﴾ بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي عِزَّةٍ وَشِقَاقٍ ﴿١١﴾

“S’ad, Naapa kwa Qur’ani yenye mawaidha. Lakini waliokufuru wamo katika majivuno na upinzani.” (38:1-2)

Allah تعالى Amesema katika Aya hii,

ق وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ ﴿١٢﴾ بَلْ عَجِبُوا أَنْ جَاءَهُمْ مُنذِرٌ مِنْهُمْ فَقَالَ الْكٰفِرُونَ هَذَا شَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿١٣﴾

“Qaaf. Naapa kwa Qur’ani Tukufu! Bali wanastaajabu kwamba amewafikia mwonyaji kutoka miongoni mwao, na wakasema makafiri: Hili ni jambo la ajabu!”

Waliistaajabia Hikima ya Kumtuma Mtume ﷺ ambaye ni mwanadamu. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ رَجُلٍ مِنْهُمْ أَنْ أَنْذِرِ النَّاسَ

“Je! Imekuwa ajabu kwa watu kwamba Tumemfunulia mmoja wao kuwa: Waonye watu”. (10:2)

Maana yake: Hili si ajabu kwa Allah تعالى, Yeye Huteua Mitume katika Malaika na wanadamu. Allah تعالى Alieleza kuhusu makafiri kushangaa ufufuo na kukanusha kuja kwake,

أَءِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا ذَلِكُمْ رَجْعٌ بَعِيدٌ ﴿١٤﴾

“Ati tukifa na tukawa udongo? Kurejea huko kuko mbali!”

Walisema, ‘baada ya kufariki kwetu, kusagika, huku viungo vikiwa vimekatika vipande na tukawa mavumbi, tunawezaje kurejeshwa katika umbo na miili yetu ya awali,’

ذَلِكُمْ رَجْعٌ بَعِيدٌ ﴿١٥﴾

“Kurejea huko kuko mbali!” ‘Hakuonekani kama kweli kunaweza kutokea.’ Walidhani kuwa Ufufuo ulikuwa mbali na jambo la kuwepo na kamwe hautatokea. Allah تعالى Aliwajibu kauli yao kwa Kusema,

قَدْ عَلِمْنَا مَا تَنْقُصُ الْأَرْضُ مِنْهُمْ^ط

“Hakika Sisi Tunajua kiasi cha kila kinachopunguzwa na ardhi kutokana nao.

Inamaanisha, ‘Tunakijua kinachochukuliwa na ardhi kutokana na miili yao iliyokufa.’ Wapi na kwa namna gani miili yao imesagika, imebadilika kuwa kitu gani na imekuwa hivyo kwa namna gani, yote haya katu hayakosekani katika Ujuzi wa Allah تعالى.

وَعِدْنَا كِتَابَ حَفِيفٍ^ط

“Na Kwetu kipo Kitabu kinacho hifadhi yote.”“Chenye kuhifadhi kumbukumbu zote. Hivyo, Ujuzi Wetu ni wenye kuenea na Kitabu cha Hukumu kina kila kitu kikiwa kimeandikwa kwa ufasaha.” Al-’Awfi alisimulia kuwa ‘Abdullah bin ‘Abbas رضي الله عنها alitoa rai juu ya Kauli ya Allah تعالى,

قَدْ عَلِمْنَا مَا تَنْقُصُ الْأَرْضُ مِنْهُمْ^ط

“Hakika Sisi Tunajua kiasi cha kila kinachopunguzwa na ardhi kutokana nao.”

“Inarejea katika kinacholiwa na ardhi miongoni mwa nyama, ngozi, mifupa na nywele.”¹ Maoni sawa na haya yameandikwa kutoka kwa Mujahid, Qatadah, Adh-Dhahhak na wengine.²

Allah تعالى Ameeleza sababu zao nyuma ya ukafiri wao, uasi na kupuuzia kwao, uwezekano wa lile ambalo kwa ukweli ni lenye kuwezekana,

بَلْ كَذَّبُوا بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ فَهُمْ فِي أَمْرٍ مَرِيجٍ^ط

“Lakini waliikanusha Haki ilipowajia; kwa hivyo wamo katika mambo ya mkorogo.”

Hii ndio hali ya wenye kuukataa ukweli, chochote wanachokisema baada ya kuukataa Ukweli si sahihi kabisa. Maana ya neno *Marij*, katika vurugu, hali ya kuchanganyikiwa na tabia za ukataaji Ukweli. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

¹ At-Tabari 22:328.

² At-Tabari 22:329.

إِنكُم لَئِي قَوْلٍ مُّخْتَلِفٍ ﴿٥٨﴾ يُؤَفِّكُ عَنْهُ مَن أُوَفِّكَ ﴿٥٩﴾

“Hakika nyinyi bila ya shaka mmo katika kauli inayokhitalifiana. Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa.” (51:8-9)

أَفَلَمْ يَنْظُرُوا إِلَى السَّمَاءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنَاهَا وَزَيَّنَّاهَا وَمَا هِيَ مِنْ فُرُوجٍ ﴿٦٠﴾ وَالْأَرْضَ
مَدَدْنَاهَا وَأَلْقَيْنَا فِيهَا رَوَّسِيَّ وَأُنْبِتْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍ بَهِيجٍ ﴿٦١﴾ تَبَصَّرَةٌ وَذَكَرَى لِكُلِّ
عَبْدٍ مُّنبِئٍ ﴿٦٢﴾ وَنَزَّلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً مُّبْرَكًا فَأَنْبَتْنَا بِهِ جَنَّاتٍ وَحَبَّ الْحَصِيدِ ﴿٦٣﴾
وَالنَّخْلَ بَاسِقَاتٍ لِّهَا طَلْعٌ نَّضِيدٌ ﴿٦٤﴾ رِزْقًا لِّلْعِبَادِ ۗ وَأَحْيَيْنَا بِهِ بَلَدَةً مِّمَّا كَذَّبَكَ
الْخُرُوجُ ﴿٦٥﴾

6. Je! Hawaangalii mbingu zilizo juu yao! Vipi Tulivyoziyenga, na Tukazipamba. Wala hazina nyufa.

7. Na ardhi Tumeitandaza na Tukaiwekea milima, na Tukaiotesha mimea mizuri ya kila namna.

8. Yawe haya ni kifumbua macho na ukumbusho kwa kila mja mwenye kuelekea.

9. Na Tumeteremsha kutoka mbinguni maji yaliyobarikiwa, na kwa hayo Tukaotesha mabustani na nafaka za kuvunwa.

10. Na mitende mirefu yenye makole yaliyozaa kwa wingi,

11. Ili iwe ni riziki kwa waja wangu. Na Tukaifufua kwa maji nchi iliyokuwa imekufa. Kama hivyo ndivyo utakavyokuwa ufufuaji.

Ubainifu wa Uwezo wa Allah تعالى Juu ya Jambo Kubwa Kuliko Ufufuo

Allah تعالى Anawatanabahisha waja Wake juu ya Nguvu Zake zisizo na ukomo, Alizozidhihirisha kwa Kuumba vilivyo vikubwa kuliko walichokistaajabia na kupuuzia uwezekano wake,

أَفَلَمْ يَنْظُرُوا إِلَى السَّمَاءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنَاهَا وَزَيَّنَّاهَا

“Je! Hawaangalii mbingu zilizo juu yao! Vipi Tulivyoziyenga, na Tukazipamba.”

Kwa mataa;

وَمَا هَا مِنْ فُرُوجٍ

“Wala hazina nyufa.” Maana yake: Mianya, kwa mujibu wa Mujahid.¹ Wengine wamesema kuwa maana ya neno *“Furuji”* ni nyufa au mianya. Maana zote hizi zinakaribiana. Allah تعالى Amesema,

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٠﴾ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا ۗ مَا تَرَىٰ فِي خَلْقِ الرَّحْمَنِ مِن تَفَوتٍ ۗ فَأَرْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَىٰ مِن فُطُورٍ ﴿١١﴾ ثُمَّ أَرْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنقَلِبْ إِلَيْكَ الْبَصَرُ حَاسِمًا ۗ وَهُوَ حَسِيرٌ ﴿١٢﴾

“Ambaye Ameumba mauti na uhai ili Kujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye Nguvu na Mwenye Msamaha. Aliyeumba mbingu saba kwa matabaka. Huoni tafauti yoyote katika Uumbaji wa Mwingi wa Rehema. Hebu rudisha nadhari! Unaona kosa lolote? Tena rudisha nadhari mara mbili, nadhari yako itakurejea mwenyewe hali ya kuwa imehizika nayo imechoka.” (67:2-4)

Amechoka, hawezi kugundua ila au udhaifu wowote. Kauli ya Allah تعالى

وَالْأَرْضَ مَدَدْتَهَا

“Na ardhi Tumeitandaza.” Inamaanisha, ‘Tuliipanua na kuitandika,’

وَأَلْقَيْنَا فِيهَا رَوْسِيَ

“Na Tukaiwekea milima.” Ya kuizua dunia isiyumbe pamoja na wakazi wake.

وَأُنَبِّتْنَا فِيهَا مِن كُلِّ زوجٍ بهيجٍ

“na Tukaiotesha mimea mizuri ya kila namna.”

Kila aina na sampuli ya mmea, tunda na majani.

وَمِن كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿١٤﴾

“Na katika kila kitu Tumeumba kwa jozi ili mzingatie.” (51:49)

¹ At-Tabari 22:332

Kauli ya Allah تعالى 'Bahij', inamaanisha mtazamo mzuri,

تَبَصَّرَةٌ وَذِكْرَىٰ لِكُلِّ عَبْدٍ مُّنِيبٍ ﴿٥٠﴾

“Yawe haya ni kifumbua macho na ukumbusho kwa kila mja mwenye kuelekea.”

Allah تعالى Anasema, kwa kuangalia Uumbaji wa mbingu na ardhi na vitu vyote vikubwa Alivyoviweka vyenye kuleta utambuzi, ushahidi na fundisho kwa kila mja mwenye kutubu anayejinyenyekeza na toba kwa Allah تعالى huku akimuogopa. Allah تعالى Amesema:

وَنَزَّلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً مُّبْرَكًا

“Na Tumeteremsha kutoka mbinguni maji yaliyobarikiwa.”

Inamaanisha yenye manufaa.

فَأَنْبَتْنَا بِهِمِ الْجَنَّاتِ

“Na kwa hayo Tukaotesha bustani.”

Maana yake: Bustani, mashamba na kadhalika.

وَحَبَّ الْخَبِيدِ

“Na nafaka za kuvunwa.”

Nafaka zinazovunwa kwa ajili ya chakula na kwa kutunzwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

وَالنَّخْلَ بَاسِقَاتٍ

“Na mitende mirefu”

Inamaanisha, mirefu, kwa mujibu wa maelezo yaliyosimuliwa kutoka kwa Ibn 'Abbas, Mujahid, 'Ikrimah, Al-Hasan, Qatadah As-Suddi رضي الله عنهم¹. Allah تعالى Amesema,

هَذَا طَلْعٌ نَّضِيدٌ

“Yenye makole yaliyozaa kwa wingi.”

Ikizaa matunda yaliyopangwa katika makole.

¹ At-Tabari 22:335.

رِزْقًا لِلْعِبَادِ

“Ili iwe ni riziki kwa waja Wangu.” Kwa ajili ya viumbe (wa Allah تعالى),

وَأَحْيَيْنَا بِهِ بَلَدَةً مَّيْتًا

“Na Tukaifufua kwa maji nchi iliyokuwa imekufa.”

Hii ni ardhi iliyokuwa kame. Hata hivyo, ikanyesha mvua juu yake, inatikiswa na kuwa hai, inavimba na kuzalisha namna zote za jozi kama vile maua na mingine – inayovutia kutokana na uzuri wake. Yote haya huwepo baada ya ardhi kukosa rangi ya chanikiwiti, lakini ikatikiswa kurejeshwa kuwa hai na ikawa kijani kibichi. Kwa hakika, hii ni dalili ya Ufufuo baada ya kifo na kusagika; hivyo, Allah تعالى Huwafufua wafu. Alama hii ya uwezo wa Allah تعالى ambayo huonekana na kushuhudiwa ni kubwa kuliko ukanushaji wa wapingaji wa Ufufuo. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

لَخَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

“Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.” (40:57),

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْ يَخْلُقْهُنَّ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقِيَ

الْمَوْتَىٰ ۗ بَلَىٰ ۗ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٥٨﴾

“Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba, kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.” (46:33) na,

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ تَرَى الْأَرْضَ خَاشِعَةً فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ ۗ إِنَّ الَّذِي

أَحْيَاهَا لَمُخِي الْمَوْتَىٰ ۗ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٥٩﴾

“Na katika Ishara Zake ni kwamba unaiona ardhi nyonge, lakini Tunapoteremshia maji mara unaiona inataharaki na kuumuka. Bila ya shaka Aliyeihuisha ardhi Ndiye Atakayehuisha wafu. Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.” (41:39)

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَأَصْحَابُ الرَّسِّ وَثَمُودُ ﴿١٢﴾ وَعَادٌ وَفِرْعَوْنُ وَإِخْوَانُ لُوطٍ ﴿١٣﴾
 وَأَصْحَابُ الْأَيْكَةِ وَقَوْمُ تُبَيْعٍ ۚ كُلٌّ كَذَّبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ وَعِيدِ ﴿١٤﴾ أَفَعَيَّبْنَا بِالْخَلْقِ الْأَوَّلِ ۚ بَلْ
 هُمْ فِي لَبْسٍ مِّنْ خَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٥﴾

12. *Walikadhibisha kabla yao kaumu ya Nuhu na wakaazi wa visimani na Thamudi.*

13. *Na A'di na Firauni na nduguze Lut'i.*

14. *Na wakaazi wa Misituni, na watu wa Yemeni'. Wote hao waliwakanusha Mitume, kwa hivyo onyo langu likathibitika juu yao.*

15. *Kwani Tulichoka kwa Kuumba mara ya kwanza. Bali wao wamo katika shaka tu juu ya umbo jipya.*

Makuraishi Wakumbushwa Juu ya Kuhilikishwa Mataifa Yaliyotangulia

Allah تعالى Anawaonya makafiri wa kikuraishi yaliyowakuta watu kama wao miongoni mwa waliokufuru kabla yao, kutokana na Kuwapa wao adhabu kali hapa duniani kama watu wa Nuh عليه السلام kwa kuwagharikisha katika mafuriko yaliyoenea na kuwasibu watu wote duniani. Adhabu hii pia iliwakumba watu wa Ar-Rass, na tulieleza habari yao katika Surat Al-Furqan.¹

وَتَمُودُ ﴿١٢﴾ وَعَادٌ وَفِرْعَوْنُ وَإِخْوَانُ لُوطٍ ﴿١٣﴾

“Na Thamud. Na A'di na Firauni na kaumu ya Lut'i”.

Watu wa Sadum (Sodom) na maeneo yaliyozunguka, ambapo Lut عليه السلام alitumwa. Allah تعالى Aliitikisa dunia chini yao na eneo lao likageuzwa kuwa ziwa lenye harufu mbaya, ikinuka kama ulivyokuwa ukafiri, uasi na ukanaji ukweli,

وَأَصْحَابُ الْأَيْكَةِ

“Na wakaazi wa Machakani.”

Hao ni umma wa Shu'ayb عليه السلام.

¹ Angalia juzu ya tano, Tafsiri ya Surat Al-Furqan (25:38)

وَقَوْمُ تَبَعٍ

“Na watu wa Yemeni”. Mfalme wa Yemen; tulishaeleza habari yake katika Tafsiri ya *Surat Ad-Dukhan*,¹ kwa kiasi cha kutosha kutoirudia hapa. Kila Sifa Njema ni za Allah تعالى.

كُلٌّ كَذَّبَ الرُّسُلَ

“Wote hao waliwakanusha Mitume.”

Inamaanisha, umma zote hizi na vizazi vyao waliwaita Mitume wao waongo, na kila mwenye kumkataa japo Mtume mmoja, ni kama amewakana wote. Allah تعالى Amesema,

كَذَّبَتْ قَوْمُ نُوحٍ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٠٥﴾

“Kaumu ya Nuhu waliwakadhibisha Mitume.” (26:105)

Japokuwa Mtume mmoja tu alitumwa kwao, na kwa hakika, hata kama wangewajia Mitume wote wasingewaamini pia. Allah تعالى Amesema,

حَقٌّ وَعَيْدٌ

“Kwa hivyo onyo likathibitika.”

Maana yake: Ahadi ya adhabu na mateso Aliyowapa Allah تعالى kutokana na ukanushaji wao. Hivyo, wale wote wenye kukhofia mwisho kama huo wataonyeka. Hususan kwa kuwa hawa nao wamemkana Mtume, kama walivyofanya hao wa awali.

Kurudia Uumbaji ni Rahisi Zaidi

Allah تعالى Amesema,

أَفَعَيْنَا بِالْخَلْقِ الْأَوَّلِ

“Kwani Tulichoka kwa Kuumba mara ya kwanza.”

Inamaanisha, ‘kuanza Uumbaji kulituchosha kiasi cha kuwapa wao mashaka kuwa kurudia Uumbaji ni jambo lisilowezezana.’

¹ Angalia juzu ya nane, Tafsiri ya *Surat Ad-Dukhan* (44:37)

بَلْ هُمْ فِي لَبْسٍ مِّنْ خَلْقٍ جَدِيدٍ

“Bali wao wamo katika shaka tu juu ya umbo jipya.”

Maana yake: ‘Kuanza Uumbaji hakukutuchosha, na Kuurejesha ni rahisi zaidi.’
Allah تعالیٰ Amesema,

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

“Na Yeye Ndiye Anayeanzisha Uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake.” (30:27),

Na Allah تعالیٰ Amesema,

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾

“Na akatupigia mfano, na akasahau Kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakayeihusha mifupa nayo imekwisha chakaa? Sema: Ataihuisha huyo huyo Aliyeiumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila Kuumba.” (36:78-79)

Tulishataja hapo awali Hadithi iliyokusanywa katika Sahihi,

«يَقُولُ اللهُ تَعَالَى يُؤْذِنِي ابْنُ آدَمَ يَقُولُ: لَنْ يُعِيدَنِي كَمَا بَدَأَنِي. وَلَيْسَ أَوَّلُ الْخَلْقِ بِأَهْوَنَ عَلَيَّ مِنْ إِعَادَتِهِ»

“Allah Mtukuka Anasema, ‘Mwanaadamu ananiudhi pale anaposema, ‘(Mwenyezi Mungu) Hatanifufua mimi kama Alivyoniumba mwanzo!’ Ilhali kumrejesha duniani (kwa kumkusanya mabaki yake yaliyopo ardhini) ni rahisi zaidi kuliko uumbaji wake wa mwanzo.”¹

* * *

¹ Fat’h Al-Bari 8:611.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ وَنَعَلَهُ مَا تُوَسَّوَسُ بِهِ نَفْسُهُ ۗ^ط
 وَخَنُّ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ ﴿١٦﴾ إِذْ يَتَلَقَّى
 الْمُتَلَقِّيَانِ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ قَعِيدٌ ﴿١٧﴾ مَا يَلْفِظُ
 مِنْ قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٨﴾ وَجَاءَتْ سَكْرَةُ
 الْمَوْتِ بِالْحَقِّ ۗ ذَٰلِكَ مَا كُنْتَ مِنْهُ تَحِيدُ ﴿١٩﴾ وَنُفِخَ فِي
 الصُّورِ ۗ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْوَعِيدِ ﴿٢٠﴾ وَجَاءَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَعَهَا
 سَابِقٌ وَسَّيِّدٌ ﴿٢١﴾ لَقَدْ كُنْتَ فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَٰذَا فَكَشَفْنَا
 عَنْكَ غِطَاءَكَ فَبَصَرُكَ الْيَوْمَ حَدِيدٌ ﴿٢٢﴾ وَقَالَ قَرِينُهُ
 هَٰذَا مَا لَدَىٰ عَتِيدٍ ﴿٢٣﴾ أَلْقِيَا فِي جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ
 عَابِدٍ ﴿٢٤﴾ مِّنَاعٍ لِلْخَيْرِ مُعْتَدٍ مُّرِيبٍ ﴿٢٥﴾ الَّذِي جَعَلَ
 مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ فَالْقِيَا فِي الْعَذَابِ الشَّدِيدِ ﴿٢٦﴾ *
 قَالَ قَرِينُهُ رَبَّنَا مَا أَطَّغَيْتُهُ وَلَٰكِن كَانَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ
 ﴿٢٧﴾ قَالَ لَا تَخْتَصِمُوا لَدَىٰ وَقَدْ قَدَّمْتُ إِلَيْكُمْ بِالْوَعِيدِ
 ﴿٢٨﴾ مَا يُبَدِّلُ الْقَوْلُ لَدَىٰ وَمَا أَنَا بِظَلْمٍ لِلْعَبِيدِ ﴿٢٩﴾
 يَوْمَ نَقُولُ لِجَهَنَّمَ هَلِ امْتَلَأَتْ وَتَقُولُ هَلْ مِنْ مَّزِيدٍ ﴿٣٠﴾
 وَأُزْلِفَتِ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِينَ غَيْرَ بَعِيدٍ ﴿٣١﴾ هَٰذَا مَا تُوعَدُونَ
 لِكُلِّ أَوَّابٍ حَفِيظٍ ﴿٣٢﴾ مَّن حَشَى الرَّحْمَنَ بِالْغَيْبِ وَجَاءَ
 بِقَلْبٍ مُنِيبٍ ﴿٣٣﴾ ادْخُلُوهَا بِسَلَامٍ ۗ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْخُلُودِ ﴿٣٤﴾
 هُمْ مَا يَشَاءُونَ فِيهَا وَلَدَيْنَا مَزِيدٌ ﴿٣٥﴾

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ وَنَعَلَهُ مَا تُوَسَّوَسُ بِهِ نَفْسُهُ ۗ^ط
 وَخَنُّ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ ﴿١٦﴾ إِذْ
 يَتَلَقَّى الْمُتَلَقِّيَانِ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ
 الشِّمَالِ قَعِيدٌ ﴿١٧﴾ مَا يَلْفِظُ مِنْ
 قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٨﴾
 وَجَاءَتْ سَكْرَةُ الْمَوْتِ بِالْحَقِّ ۗ ذَٰلِكَ
 مَا كُنْتَ مِنْهُ تَحِيدُ ﴿١٩﴾ وَنُفِخَ فِي
 الصُّورِ ۗ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْوَعِيدِ ﴿٢٠﴾
 وَجَاءَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَعَهَا سَابِقٌ
 وَسَّيِّدٌ ﴿٢١﴾ لَقَدْ كُنْتَ فِي غَفْلَةٍ
 مِّنْ هَٰذَا فَكَشَفْنَا عَنْكَ غِطَاءَكَ
 فَبَصَرُكَ الْيَوْمَ حَدِيدٌ ﴿٢٢﴾

16. Na hakika Tume-
 muumba mtu, nasi Tuna-
 yajua yanayompitikia katika
 nafsi yake. Na Sisi Tuko
 karibu naye kuliko mshipa
 wa shingoni mwake.

17. Wanapopokea wapo-
 keaji wawili, wanaokaa
 kuliani na kushotoni.

- 18. Hatamki neno ila karibu yake yupo mwangalizi tayari.**
- 19. Na uchungu wa kutoka roho utamjia kwa haki. Hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia.**
- 20. Na litapulizwa baragumu. Hiyo ndiyo Siku ya Miadi.**
- 21. Na kila nafsi itakuja na pamoja nayo mchungaji na shahidi.**
- 22. (Aambiwe): kwa hakika ulikuwa umeghafilika na haya; basi leo Tumekuondolea pazia lako, na kwa hivyo kuona kwako leo ni kukali.**

Ujuzi wa Allah تعالی Huangazia Kila Jambo la Mwanaadamu

Allah تعالی Anathibitisha Utawala Wake juu ya mwanaadamu, kuwa Yeye ni Muumbaji wao na Anajua kila linalowahusu. Allah تعالی Ana Ujuzi kamili kuhusu fikra zote zinazopita akilini mwa mwanadamu, nzuri au mbaya. Katika Sahih, Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى تَجَاوَزَ لِأُمَّتِي مَا حَدَّثَتْ بِهِ أَنْفُسَهَا مَا لَمْ تَقُلْ أَوْ تَعْمَلْ»

“Hakika, Allah Mtukufu Ameusamehe Umma wangu (Waislamu) kwa kile wanachozungumza (kufikiri) katika nafsi zao, ilimradi hawakitaji au kukitenda.”

Kauli ya Allah تعالی وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ

“Na Sisi Tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake.”

Maana yake: Malaika Wake wako karibu zaidi na mwanaadamu kuliko mshipa wa shingoni mwake. Walioelezea neno ‘Sisi’ lililotajwa katika Aya kumaanisha ‘Ujuzi Wetu,’ wamefanya hivyo kuepuka kuangukia katika jambo la kuwa na mwili au kitu chenye kukaa ndani (au moyoni); lakini kanuni hizi mbili za imani si sahihi kwa mujibu wa itifaki ya Waislamu. Allah تعالی Ametakasika, na Kujiweka mbali na sifa wanazompachikia. Maneno yaliyo katika Aya hii hayahitaji maelezo haya (kuwa ‘Sisi’ inaelezea Ujuzi wa Allah), kwani Allah تعالی Hakusema, ‘Nami Niko karibu naye kuliko mshipa wake wa shingoni,’ Bali, Amesema,

وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ

“Na Sisi Tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake.”

Ni sawa na Alivyosema kuhusu mtu anayefariki,

وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْكُمْ وَلَكِنْ لَا تُبْصِرُونَ ﴿٥٦﴾

“Na Sisi Tuko karibu zaidi naye kuliko nyinyi, lakini hamuoni.” (56:85),

Akiwazungumzia Malaika Wake (wanaotoa roho). Allah تعالى Amesema,

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٥٩﴾

“Hakika Sisi Tumeteremsha ukumbusho na hakika Sisi ndio Wenye Kuulinda” (15:9)

Hivyo, Malaika walishusha ufunuo, Qur'an, kwa idhini ya Allah تعالى. Hivyo, Malaika wako karibu na mwanadamu kuliko mshipa wa shingoni mwake, kwa nguvu na idhini ya Allah تعالى.¹ Wakati huo huo, Malaika ana ukaribu kwa wanadamu kama ukaribu wa mashetani, Aidha shetani huingia kwa mwanadamu katika mishipa yao ya damu, kama alivyohabarisha hilo Mtume ﷺ, ambaye ni mkweli kuliko watu wote akatuambia sisi. Kauli ya Allah تعالى katika Aya hii,

إِذْ يَتَلَقَى الْمُتَلَقِيَانِ

“Wanapopokea wapokeaji wawili.” Inarejea kwa Malaika wawili wanaopokea na kuandika amali za mwanaadamu,

عَنِ الَّتِيْمِيْنَ وَعَنِ الشِّمَالِ قَعِيْدٌ

“Ambao hukaa kuliani na kushotoni.”

Wakiwa tayari kuandika.

مَا يَلْفِظُ

“Hatamki” Maana yake: Mwanaadamu.

¹ Fat'h Al-Bari 11:557

مِنْ قَوْلٍ

“*Neno*”, Lolote analolisema.

إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ

“*ila karibu yake yupo mwangalizi tayari.*” Inamaanisha, yupo mwandishi mwenye kazi ya kuliandika, asiyeacha kunukuu neno au kitendo chochote. Allah تعالى Amesema,

وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لَحَافِظِينَ ﴿١٠﴾ كِرَامًا كَاتِبِينَ ﴿١١﴾ يَعْمُونَ مَا تَفْعَلُونَ ﴿١٢﴾

“*Na hakika bila ya shaka wapo walinzi juu yenu. Waandishi wenye hishima. Wanayajua mnayoyatenda.*” (82:10-12)

Hivyo, mwandishi anaandika kila neno linalotamkwa, kwa mujibu wa maelezo ya Al-Hasan na Qatadah.¹ Pia haya ndiyo maana ya wazi ya Aya hii. Bin Abbas رضي الله عنهما katika mtazamo wake anasema: ‘Malaika huandika madhambi na thawabu tu.’ Imamu Ahmad aliandika kuwa Bilal bin Al-Harith Al-Muzani رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيَتَكَلَّمُ بِالْكَلِمَةِ مِنْ رِضْوَانِ اللَّهِ تَعَالَى مَا يَظُنُّ أَنْ تَبْلُغَ مَا بَلَغَتْ يَكْتُبُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ لَهُ بِهَا رِضْوَانَهُ إِلَى يَوْمِ يَلْقَاهُ، وَإِنَّ الرَّجُلَ لَيَتَكَلَّمُ بِالْكَلِمَةِ مِنْ سَخَطِ اللَّهِ تَعَالَى مَا يَظُنُّ أَنْ تَبْلُغَ مَا بَلَغَتْ، يَكْتُبُ اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ بِهَا سَخَطَهُ إِلَى يَوْمِ يَلْقَاهُ»

“*Hakika, mtu anatamka neno lenye kumridhisha Allah, bila ya kujua namna litakavyokuwa utukufu wake na kwa sababu yake Allah Mtukufu Anamuandikia Radhi Zake mpaka Siku ya kukutana Naye. Pia mtu anatamka neno la kumkasirisha Allah bila ya kujua ukubwa wa ubaya wake na Allah Anamuandikia Hasira Zake mpaka Siku ya kukutana Naye.*”

‘Alqamah alikuwa akisema, “Maneno mangapi sikuyatamka kwa sababu ya Hadithi aliyosimulia Bilal bin Al-Harith.”² At-Tirmidhi, An-Nasa’i na Ibn Majah wameikusanya Hadithi hii. At-Tirmidhi alisema, “Hasan Sahih.”³ Kuna Hadithi inayolingana na hii katika Sahih.

¹ At-Tabari 22:345.

² Ahmad 3:469. ³ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:610, *Tuhfat Al-Ashraf* 2:555 na Ibn Majah 2:1312.

Kuwakumbusha Wanadamu Juu ya Uchungu wa Umauti, Kupulizwa Parapanda na Siku ya Kukusanywa Watu.

Allah تعالى Amesema,

وَجَاءَتْ سَكْرَةُ الْمَوْتِ بِالْحَقِّ ذَٰلِكَ مَا كُنْتَ مِنْهُ تَحِيدُ ﴿٥٠﴾

“Na uchungu wa kutoka roho utamjia kwa haki. Hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia”.

Allah تعالى Anasema, ‘Ewe mwanaadamu! Mfazaiko na uchungu wa umauti umekujia kweli, kwa maana sasa Nimekuleteeni uhakika mliokuwa mnabishania.’

ذَٰلِكَ مَا كُنْتَ مِنْهُ تَحِيدُ

“Hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia.” Inamaanisha, ‘huu ndio mwisho mliokuwa mkijaribu kuukimbia, umekufikieni! Hivyo, hamtakuwa na hifadhi wala kimbilio.’ Na imethibiti katika Sahih kwamba, Mtume ﷺ, alivyojiwa na hali ya kutoka roho alikuwa akifuta jasho usoni mwake huku akisema;

«سُبْحَانَ اللَّهِ! إِنَّ لِلْمَوْتِ لَسَكْرَاتٍ»

“Ametakasika Allah! Hakika mauti yana kilevi.”¹

Ama kuhusu Aya,

ذَٰلِكَ مَا كُنْتَ مِنْهُ تَحِيدُ

“Hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia.” Yaweza kuwa na maana mbili. Mojawapo ni hii: ‘mlichokuwa mkijaribu kukikwepa na kukikimbia kimekujieni na kuingia majumbani mwenu!’ Maana ya pili: ‘Hamna namna ya kuukwepa au kuukimbia mwisho huu.’ At-Tabarani aliandika Hadithi katika *Al-Mu’jam Al-Kabir*² kuwa Samurah alisimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

مَثَلُ الَّذِي يَقْرَأُ مِنَ الْمَوْتِ مَثَلُ الثَّغْلِبِ تَطْلُبُهُ الْأَرْضُ بِدَيْنِهِ، فَجَاءَ يَسْعَى حَتَّى إِذَا
أُغْيِيَ وَأَسْهَرَ دَخَلَ جُحْرَهُ وَقَالَتْ لَهُ الْأَرْضُ: يَا ثَغْلِبُ، دَيْنِي. فَخَرَجَ وَلَهُ
حُصَاصٌ، فَلَمْ يَزَلْ كَذَلِكَ حَتَّى تَقَطَّعَتْ عُنُقُهُ وَمَاتَ»

¹ Fat’h Al-Bari 11:369.

² At-Tabarani 7:222. Masimulizi haya ni *Mawquf*, yaani, ni sahihi kutoka kwa sahaba peke yake.

"Mfano wa mtu anayeyakimbia mauti kama Bweha anayeridhiwa na ardhi. Bweha akakimbia na alipochoka na muda wa kulala ukawadia, akaingia shimoni mwake. Ardhi ikamuambia: 'Ewe Bweha! Nilipe deni langu,' akatoka huku akilia sana. Akaendelea hivyo mpaka shingo yake ikakatika na akafa."

Mfano huu unajulisha kuwa kama namna Bweha alivyokosa namna ya kuikimbia na kuikwepa ardhi, ndivyo hivyo pia, mwanadamu hana namna ya kukikimbia kifo. Allah تعالى Amesema,

وَتُفِخَ فِي الصُّورِ ذَٰلِكَ يَوْمَ الْوَعِيدِ ﴿٥٠﴾

"Na litapulizwa baragumu. Hiyo ndiyo Siku ya Miadi."

Hapo awali tulieleza kuhusu kupulizwa kwa parapanda, hofu inayofuatia, kufariki kwa kila kitu na kufufuliwa, haya yote yatatokea Siku ya Kiama.¹ Pia tulitaja kuwa Mtume ﷺ amesema katika Hadithi,

«كَيْفَ أَنْعَمَ وَصَاحِبُ الْقُرْنِ قَدِ النَّعَمَ الْقُرْنَ، وَحَنَى جَبْهَتَهُ، وَانْتَظَرَ أَنْ يُؤَدَّنَ لَهُ»

"Nitafarijika vipi ilhali Mwenye Parapanda ameliweka mdomoni mwake na ameinamisha paji la uso wake akisubiri kupewa idhini (na Allah ili apulize)."

Wakauliza, "Ewe Mtume, tuseme nini?" Akawajibu:

«قُولُوا حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ»

*"Semeni: 'Allah Anatutosha Naye ni Mbora wa Kutegemewa.'"*²

Masahaba waliikariri dua hii kwa kusema, "Allah تعالى Anatutosha Naye ni Mbora wa Kutegemewa." Allah تعالى Amesema,

وَجَاءَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَعَهَا سَاقِقٌ وَشَهِيدٌ ﴿٥١﴾

"Na kila nafsi itakuja na pamoja nayo mchungaji na shahidi."

Maana yake: Malaika mchungaji mwenye kumpeleka kwenye kukusanywa na Malaika wa kushuhudia amali zake. Hii ndiyo maana ya dhahiri ya Aya hii

¹ Angalia juzu ya sita, Tafsiri ya Surat Ta Ha (20:102).

² Tuhfat Al-Ahwadhi 7:117.

tukufu na ndiyo maana aliyoikubali Ibn Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى¹. Iisimuliwa kutoka kwa Yahya bin Rafi رَضِيَ اللهُ عَنْهُ، Mtumwa aliyeachwa huru na Thaqif, kuwa alimsikia 'Uthman bin 'Affan رَضِيَ اللهُ عَنْهُ، akitoa hotuba na akasoma Aya,

وَجَاءَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَعَهَا سَائِقٌ وَشَهِيدٌ ﴿٣٨﴾

“Na kila nafsi itakuja na pamoja nayo mchungaji na shahidi.”

Akasema, “mchungaji anaipeleka nafsi kwa Allah تَعَالَى، na shahidi wa kutoa ushahidi dhidi yake kwa aliyoyafanya.”² Kauli ya Allah تَعَالَى،

لَقَدْ كُنْتَ فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَذَا فَكَشَفْنَا عَنْكَ غِطَاءَكَ فَبَصَرُكَ الْيَوْمَ حَدِيدٌ ﴿٣٩﴾

“(Aambiwe): kwa hakika ulikuwa umeghafilika na haya; basi leo Tumekuondolea pazia lako, na kwa hivyo kuona kwako leo ni kukali.”

Tamko hili anaambiwa Mwanadamu, Allah تَعَالَى Amesema,

لَقَدْ كُنْتَ فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَذَا

“(Aambiwe): kwa hakika ulikuwa umeghafilika na haya.”

Kuhusu Siku hii.

فَكَشَفْنَا عَنْكَ غِطَاءَكَ فَبَصَرُكَ الْيَوْمَ حَدِيدٌ

“Basi leo Tumekuondolea pazia lako, na kwa hivyo kuona kwako leo ni kukali.”

Maana yake: ‘Una nguvu.’ Kila mmoja Siku ya Kiama ataona sana, hata makafiri watakuwa na msimamo Siku ya Kiama, lakini hilo halitawasaidia, kwani Allah تَعَالَى Amesema,

أَسْمِعْ بِهِمْ وَأَبْصِرْ يَوْمَ يَأْتُونَنَا ۗ

“Watasikia na wataona vizuri vilioje Siku watakayotufikia!” (19:38),

¹ At-Tabari 22:347.

² At-Tabari 22:347.

Na Allah تعالی Amesema,

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا
تَعْمَلْ صَالِحًا إِنَّا مُوقِنُونَ ﴿٣٢﴾

“Na ungeliswaona wakosefu wanavyoinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao Mlezi, (wakisema): Mola wetu Mlezi! Tumeshona, na tumeshasikia. Turejesho tukatende mema, kwani hakika sisi tumekwishakuwa na yakini sasa.” (32:12)

وَقَالَ قَرِينُهُ هَذَا مَا لَدَىٰ عَتِيدٍ ﴿٣٣﴾ أَلْقِيَا فِي جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ عَانِدٍ ﴿٣٤﴾ مَنَاعٍ
لِّلْخَيْرِ مُعْتَدٍ مُّرِيبٍ ﴿٣٥﴾ الَّذِي جَعَلَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ فَأَلْقِيَاهُ فِي الْعَذَابِ الشَّدِيدِ
﴿٣٦﴾ * قَالَ قَرِينُهُ رَبَّنَا مَا أَطَّغَيْتُهُ وَلَكِن كَانَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿٣٧﴾ قَالَ لَا تَخْتَصِمُوا
لَدَىٰ وَقَدْ قَدَّمْتُمُ الْيَكْرَ بِالْوَعِيدِ ﴿٣٨﴾ مَا يُبَدَّلُ الْقَوْلُ لَدَىٰ وَمَا أَنَا بِظَلَمٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٣٩﴾

23. Na mwenzake atasema: Huyu niliye naye nimekwisha mtayarisha.

24. Mtupeni katika Jahannamu kila kafiri muovu.

25. Akatazae kheri, arukae mipaka, mwenye kutia shaka.

26. Aliyeweka mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu. Basi mtupeni katika adhabu kali.

27. Mwenzake aseme: Ee Mola Wetu Mlezi! Sikumpoteza mimi, bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotovu wa mbali.

28. (Mwenyezi Mungu) Aseme: Msigombane mbele Yangu. Nilikuleteni mbele onyo Langu.

29. Mbele Yangu haibadilishwi kauli, wala Mimi Siwadhulumu waja Wangu.

Ushahidi wa Malaika; na Amri ya Allah تعالی Kuamuru Makafiri Watupwe Motoni

Allah تعالی Anaeleza kuwa Malaika mwandishi, aliyepewa kazi ya kuandika matendo ya mwanadamu, atatoa ushahidi dhidi yake juu ya matendo aliyoyafanya. Atasema,

هَذَا مَا لَدَىٰ عَيْنِي

“Huyu niliye naye mimi kesho tayarishwa.”

Bila ya nyongeza wala upungufu. Huu ni wakati ambapo Allah تعالی Mtukuka Atawahukumu viumbe kwa uadilifu. Aliposema,

أَلْقِيَا فِي جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ عَنِيدٍ ﴿١٦﴾

“Mtupeni katika Jahannamu kila kafiri mwenye inda.”

Inaonekana kuwa Allah تعالی Atayasema maneno haya Kuwaambia Malaika Mchungaji na Shahidi; huyo *Sa'iq* ndiye aliyemchunga mwanaadamu kwenda katika uwanja ambapo Hesabu inafanyika na ushahidi unatolewa.

Allah تعالی Atawaamuru wamtupie katika moto wa Jahanamu, na ndio makazi mabaya mno,

أَلْقِيَا فِي جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ عَنِيدٍ ﴿١٧﴾

“Mtupeni katika Jahannamu kila kafiri mwenye inda.”

Maana yake: Ambaye kufuru yake na kukana kwake ukweli kulikuwa kwa kutisha, ambao kwa ukaidi waliukataa ukweli, huku kwa makusudi wakiuchanganya na uwongo,

مَنَاعٍ لِلْخَيْرِ

“Akatazae kheri.”


Kwa kuwa hakutimiza wajibu alioamrisha, wala hakuwajibika kuhifadhi undugu wala kutoa Sadaka,

مُعْتَدٍ

“Arukae mipaka.”

Maana yake: Aliruka mipaka katika matumizi. Qatadah yeye amesema, “Ni mwenye kuruka mipaka katika kauli, tabia na mambo yake.”¹

Allah تعالى Amesema,



“Mwenye kutia shaka.”

Maana yake: Anatia shaka na anazidisha mashaka kwa wanaoichunguza tabia yake.

الَّذِي جَعَلَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ

“Aliyeweka mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu.”

Anawashirikisha wengine kwa Allah تعالى na anaabudu asiyekuwa Yeye.

فَأَلْفَيْاهُ فِي الْعَذَابِ الشَّدِيدِ

“Basi mtupeni katika adhabu kali”.

Imamu Ahmad aliandika kuwa Abu Sa’id Al-Khudri رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«يَخْرُجُ عَنْهُ مِنَ النَّارِ يَتَكَلَّمُ يَقُولُ: وَكُلْتُ الْيَوْمَ بِثَلَاثَةِ: بِكُلِّ جَبَّارٍ غَنِيْدٍ، وَمَنْ جَعَلَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ، وَمَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ، فَتَنْطَوِي عَلَيْهِمْ فَتَقْدِفُهُمْ فِي عَمْرَاتِ جَهَنَّمَ»

“Shingo itajitokeza Motoni na itazungumza kwa kusema, ‘Leo nimewakilishwa mambo matatu: Kila mwasi mwenye kiburi, na mwenye kujaalia mungu mwingine pamoja na Allah na mwenye kuuu nafsi pasi na haki.’ Kisha shingo hiyo itawazunguka na kuwatupia katikati ya Jahanamu.”²

¹ At-Tabari 22:356.

² Ahmad 3:40.

Kugombana Mwanaadamu na Shetani Mbele ya Allah تعالى

Kauli ya Allah تعالى;

قَالَ قَرِينُهُ

“Mwenzake aseme.” Inamkusudia shetani aliyewakilishwa kwa kila mtu, kwa mujibu wa maelezo ya ‘Abdullah bin ‘Abbas رضي الله عنها, Mujahid, Qatadah na wengine.¹ Atasema,

رَبَّنَا مَا أَطَعَيْتُهُ

“Ee Mola Wetu Mlezi! Sikumpoteza mimi.”

Maana yake: Shetani atayasema haya kumhusu mwanaadamu atakayekuja Siku ya Ufufuo akiwa kafiri. Shetani atamkana kwa kumuambia,

رَبَّنَا مَا أَطَعَيْتُهُ

“Ewe Mola Wetu Mlezi! Sikumpoteza mimi.”

Maana yake: “Sikumuangamiza, sikumhiliki na sukumtelezesha.”

وَلَيْكِن كَانَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ

“Bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotovu wa mbali.”

Maana yake: Yeye mwenyewe alikuwa mpotevu, akikubali upotovu na kuukataa ukweli. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَقَالَ الشَّيْطَانُ لَمَّا قُضِيَ الْأَمْرُ إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعَدَ الْحَقِّ وَوَعَدْتُكُمْ فَأَخْلَفْتُكُمْ وَمَا كَانَ لِي عَلَيْكُمْ مِنْ سُلْطَانٍ إِلَّا أَنْ دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ لِي ۗ فَلَا تُلْمُونِي وَلَوْلَا أَنْفُسُكُمْ ۗ مَا أَنَا بِمُصْرِخِكُمْ وَمَا أَنْتُمْ بِمُصْرِخِي ۗ إِنِّي كَفَرْتُ بِمَا أَشْرَكْتُمُونِ مِنْ قَبْلُ ۗ إِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٥٠﴾

“Na Shet’ani atasema itapokatwa hukumu: Hakika Mwenyezi Mungu Alikuahidini ahadi ya kweli. Nami nalikuahidini; lakini sikukutimizieni. Na sikuwa na mamlaka juu yenu, isipokuwa nilikuiteni, nanyi mkaniitikia. Basi msinilaumu mimi, bali jilaumuni wenyewe. Mimi siwezi kuwa mtetezi wenu, wala nyinyi hamuezi kuwa watetezi wangu. Hakika mimi nilikataa tangu zamani

¹ At-Tabari 22:357.

kunishirikisha na Mwenyezi Mungu. Hakika madhaalimu watakuwa na adhabu chungu.”(14:22)

Allah تعالى Amesema,

قَالَ لَا تَخْتَصِمُوا لَدَيَّ

“Msigombane mbele yangu.”

Mola Mtukuka Atamuambia haya mwanaadamu na shetani wake ambao watakuwa wakibishana mbele yake. Mwanaadamu atasema, “Ewe Mola Wangu Mlezi! Huyu Shetani amenipotosha mbali dhidi ya onyo baada ya kunifikia.’ Ambapo shetani atasema,

رَبَّنَا مَا أَطَعْتَهُرْ وَلَكِنْ كَانِ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ

“Ee Mola Wetu Mlezi! Sikumpoteza mimi, bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotovu wa mbali.”

Mbali na njia ya ukweli. Mola Mtukufu Atawaambia,

لَا تَخْتَصِمُوا لَدَيَّ

“(Mwenyezi Mungu) Aseme: Msigombane mbele Yangu.”

وَقَدْ قَدَّمْتُ إِلَيْكُم بِالْوَعِيدِ

“Nilikuleteeni mbele onyo langu.”

Nimekupeni hoja za kutosha kupitia kwa Mitume, na Nimeteremsha vitabu vitukufu, basi shuhuda, dalili na hoja zimekwisha simama dhidi yenu.

مَا يُبَدِّلُ الْقَوْلُ لَدَيَّ

“Mbele Yangu haibadilishwi kauli.”

“Nimeshapitisha Uamuzi.” Kwa mujibu wa maelezo ya Mujahid.¹

وَمَا أَنَا بِظَلَمٍ لِلْعَبِيدِ

“Wala Mimi siwadhulumu waja wangu.”

¹ At-Tabari 22:359.

يَوْمَ نَقُولُ لِجَهَنَّمَ هَلِ امْتَلَأَتْ وَتَقُولُ هَلْ مِنْ مَزِيدٍ ﴿٣٠﴾ وَأَزْلَفَتْ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِينَ غَيْرَ
 بَعِيدٍ ﴿٣١﴾ هَذَا مَا تُوْعَدُونَ لِكُلِّ أَوَّابٍ حَفِيظٍ ﴿٣٢﴾ مَنْ حَثِيءَ الرَّحْمَنِ بِالْغَيْبِ وَجَاءَ
 بِقَلْبٍ مُنِيبٍ ﴿٣٣﴾ ادْخُلُوهَا بِسَلَامٍ ۗ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْخُلُودِ ﴿٣٤﴾ هُمْ مَا يَشَاءُونَ فِيهَا وَلَدَيْنَا
 مَزِيدٌ ﴿٣٥﴾

30. Siku Tutapoiambia Jahannamu: Je! Umejaa? Nayo itasema: Je! Kuna ziada?

31. Na Pepo italetwa karibu kwa ajili ya wachamngu, haitakuwa mbali.

32. Haya ndiyo mnayoahidiwa kwa kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu na akajilinda.

33. Mwenye kumuogopa Mwingi wa Rehema hali kuwa hamuoni, na akaja kwa moyo ulioelekea.

34. (Ataambiwa) ingieni kwa salama. Hiyo ndiyo siku ya daima dawamu.

35. Humo watapata wakitakacho, na Kwetu yako ya ziada.

Hali za Jahanamu na Pepo Pamoja na Wakazi Wake

Allah تعالى Anaeleza kuwa Ataiambia Jahanamu katika Siku ya Kiama, "Je, umejaa?" Allah تعالى Ameiahidi Jahanamu kuwa itajazwa na majini na wanaadamu. Allah تعالى Atahukumu nani wa kutupwa Motoni nayo itakuwa inasema, "Je kuna ziada?" Au, 'Je kuna ziada Utakayonipa?" Hii ndiyo maana dhahiri ya Aya hii inayothibitishwa na Hadithi nyingi.

Imamu Ahmad aliandika kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا تَزَالُ جَهَنَّمُ يُلْقَى فِيهَا وَتَقُولُ: هَلْ مِنْ مَزِيدٍ؟ حَتَّى يَضَعَ رَبُّ الْعِزَّةِ قَدَمَهُ فِيهَا، فَيَتَرَوَى بَعْضَهَا إِلَى بَعْضٍ وَتَقُولُ: قَطُّ قَطُّ وَعِزَّتِكَ وَكَرَمِكَ. وَلَا يَزَالُ فِي الْجَنَّةِ فَضْلٌ حَتَّى يُنْسِيَ اللَّهُ لَهَا خَلْقًا آخَرَ فَيُسْكِنَهُمُ اللَّهُ تَعَالَى فِي فُضُولِ الْجَنَّةِ»

*"Haitaachwa Jahanamu kujazwa ndani yake, na itakuwa inasema, 'Je kuna ziada? Mpaka Mola Mlezi Aweke Mguu Wake juu yake na hapo itajikusanya pamoja na itasema, 'Inatosha, inatosha, kwa Utukufu na Ukarimu Wako!' Na Peponi hakutaacha kuwa na nafasi kubwa mpaka Allah Aumbe viumbe wengine na kuwafanya wakazi wa maeneo yaliyo matupu ya Peponi' kwa fadhila Zake."*²

Muslim pia ameikusanya Hadithi hii. Al-Bukhari aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

«يَقَالُ لِبَهَنَمَ هَلِ امْتَلَأَتْ؟ وَتَقُولُ: هَلْ مِنْ مَزِيدٍ؟ فَيَضَعُ الرَّبُّ تَبَارَكَ وَتَعَالَى قَدَمَهُ عَلَيْهَا فَتَقُولُ: قَطَّ قَطَّ»

*"Jahanamu itaulizwa, 'Je umejaa?' Nayo itasema, 'Je kuna ziada? Mola Mlezi Mtukufu Ataweka Mguu Wake juu yake ndipo itasema, 'Inatosha, inatosha!'"*³

Al-Bukhari aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«تَحَاجَّتِ الْجَنَّةُ وَالنَّارُ فَقَالَتِ النَّارُ: أُورِثُ بِالْمُتَكَبِّرِينَ وَالْمُتَجَبِّرِينَ. وَقَالَتِ الْجَنَّةُ: مَا لِي لَا يَدْخُلُنِي إِلَّا ضُعَفَاءُ النَّاسِ وَسَقَطُهُمْ. قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ لِلْجَنَّةِ: أَنْتِ رَحِمَتِي أَرْحَمُ بِكَ مِنْ أَشَاءِ مِنْ عِبَادِي. وَقَالَ لِلنَّارِ: إِنَّمَا أَنْتِ عَذَابِي أُعَذِّبُ بِكَ مَنْ أَشَاءُ مِنْ عِبَادِي وَلِكُلِّ وَاحِدَةٍ مِنْكُمَا مِلْؤُهَا، فَأَمَّا النَّارُ فَلَا تَمْتَلِيءُ حَتَّى يَضَعَ رِجْلَهُ فِيهَا فَتَقُولُ: قَطَّ قَطَّ، فَهَذَا لِكَ تَمْتَلِيءُ وَيَنْزَوِي بَعْضُهَا إِلَى بَعْضٍ وَلَا يَطْلِمُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ مِنْ خَلْقِهِ أَحَدًا، وَأَمَّا الْجَنَّةُ فَإِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يُشِيءُ لَهَا خَلْقًا آخَرَ»

"Pepo na Moto vilibishana. Moto ulisema, 'Nimefadhilishwa kwa kupewa wenye kiburi na wenye majivuno.' Pepo ikasema, 'Kwa nini kwangu waingie wanyonge na walio dhalili.' Allah Mtukuka Akaiambia Pepo, 'Wewe ni Rehema Yangu Ninayowarehemu wale Niwatakao katika waja Wangu.' Akaiambia Jahanamu, 'Wewe ni Adhabu Yangu Ninayowaadhibu wale Niwatakao katika waja Wangu."

¹ Ahmad 3:234

² Muslim 4:2187 na 2188

³ Fat'h Al-Bari 8:460

Kila kimoja kati yenu kina ujazo wake.” Moto hautajaa isipokuwa mpaka Allah Aweke Mguu Wake humo, nao utasema, ‘Inatosha, inatosha.’ Hapo Moto utajaa na kujikusanya wenyewe. Allah Hatamdhulumu yeyote katika viumbe wake. Kuhusu Pepo, Allah Ataumba viumbe wengine wa kuijaza.”¹

Allah تعالیٰ Amesema,

وَأَزَلَفْتِ الْجَنَّةَ لِلْمُتَّقِينَ غَيْرَ بَعِيدٍ ﴿٥٠﴾

“Na Pepo italetwa karibu kwa ajili ya wachamngu, haitakuwa mbali.”

Maana yake: Pepo italetwa karibu kwa wachamungu, kwa mujibu wa Qatadah, Abu Malik na As-Suddi رضي الله عنهما,²

غَيْرَ بَعِيدٍ

“Haitakuwa mbali.”

Na hili litafanyika katika Siku ya Ufufuo, ambayo haiko mbali. Kwa hakika, Siku hiyo itafika na yote yaliyoambatana nayo yapo karibu,

هَذَا مَا تُوْعَدُونَ لِكُلِّ أَوَّابٍ

“Haya ndiyo mnayoahidiwa kwa kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu na akajilinda.”

Anayerudi kwa Allah تعالیٰ kwa toba ya kweli akikusudia kutokurejea katika dhambi.

حَفِيظٍ

(Hafidh), Anayetunza ahadi yake na Allah تعالیٰ, wala haivunji au kusaliti,

مَنْ حَثِيَ الرَّحْمَنَ بِالْغَيْبِ

“Mwenye kumuogopa Mwingi wa Rehema hali kuwa hamuoni.”

Waliomuogopa Allah تعالیٰ kwa siri, ambapo Allah تعالیٰ Pekee Ndiye Aliyewaona. Mtume ﷺ amesema,

¹ Fat'h Al-Bari 8:460

² At-Tabari 22:363

وَرَجُلٌ ذَكَرَ اللَّهَ تَعَالَى خَالِيًا، فَفَاضَتْ عَيْنَاهُ

“Na mtu aliyemtaja Allah Mtukufu huku akiwa peke yake. Mpaka macho yake yakabubujika machozi.”¹

Allah تَعَالَى Amesema,

وَجَاءَ بِقَلْبٍ مُنِيبٍ

“Na akaja kwa moyo ulioelekea.”

Atakutana na Allah تَعَالَى katika Siku ya Kiama huku akiwa na moyo ulioelekea katika kutubia Kwake pia ukiwa huru (dhidi ya Shiriki) na umemnyenyekea Yeye,

أَدْخُلُوهَا

“(Wataambiwa) ingieni.” Maana yake: Peponi.

بِسَلَامٍ

“Kwa salama.” Watasalimika dhidi ya adhabu ya Allah تَعَالَى, na Malaika wa Allah تَعَالَى watawasalimia kwa kuwaambia Salaam, kwa mujibu wa maelezo ya Qatadah.² Kauli ya Allah تَعَالَى:

ذَلِكَ يَوْمُ الْخُلُودِ

“Hiyo ndiyo siku ya daima dawamu.”

Maana yake: Watakaa Peponi milele na hawatakufa, hawatahamishwa hata mmoja wao hatatamani kuhamishwa. Kauli ya Allah تَعَالَى,

هُمْ مَا يَشَاءُونَ فِيهَا

“Humo watapata wakitakacho.”

Inamaanisha, neema zozote watakazoitaka na kuzitamani watazikuta wameshaletewa mbele yao. Kauli ya Allah تَعَالَى,

وَلَدَيْنَا مَزِيدٌ

“Na Kwetu yako ya ziada.”

¹ Fat'h Al-Bari 2:168. Maana yake: Katika kivuli cha Kiti cha Enzi.

² At-Tabari 22:356

Ni sawa na Kauli Yake nyingine,

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ

“Kwa wafanyao wema ni wema na zaidi.” (10:26)

Katika Sahih, Muslim ameandika kuwa Suhayb bin Sinan Ar-Rumi alisema kuwa ‘zaidi’ inamaanisha kuangalia Uso Mtukufu wa Allah تعالى.¹

* * *

¹ Muslim 1:163

وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْنٍ هُمْ أَشَدُّ مِنْهُمْ بَطْشًا فَنَقَّبُوا
 فِي الْبِلَادِ هَلْ مِنْ مَّجِيسٍ ﴿٣٦﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى
 لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ ﴿٣٧﴾ وَلَقَدْ
 خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا
 مَسَّنَا مِنْ لُغُوبٍ ﴿٣٨﴾ فَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَسَبِّحْ
 بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ ﴿٣٩﴾ وَمِنَ
 اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَأَدْبَرَ السُّجُودِ ﴿٤٠﴾ وَأَسْمِعْ يَوْمَ يُنَادِ
 الْمُنَادِ مِنْ مَكَانٍ قَرِيبٍ ﴿٤١﴾ يَوْمَ يَسْمَعُونَ الصَّيْحَةَ
 بِالْحَقِّ ۚ ذَلِكَ يَوْمَ الْخُرُوجِ ﴿٤٢﴾ إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي وَنُمِيتُ
 وَإِلَيْنَا الْمَصِيرُ ﴿٤٣﴾ يَوْمَ نَشَقُّقُ الْأَرْضَ عَنْهُمْ سِرَاعًا
 ۗ ذَٰلِكَ حَشْرٌ عَلَيْنَا يَسِيرٌ ﴿٤٤﴾ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ ۗ وَمَا
 أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِجَبَّارٍ ۗ فَذَكِّرْ بِالْقُرْآنِ مَن يَخَافُ وَيَعِيدُ ﴿٤٥﴾

وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْنٍ هُمْ أَشَدُّ
 مِنْهُمْ بَطْشًا فَنَقَّبُوا فِي الْبِلَادِ هَلْ مِنْ
 مَّجِيسٍ ﴿٣٦﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى
 لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ
 شَهِيدٌ ﴿٣٧﴾ وَلَقَدْ خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا
 مَسَّنَا مِنْ لُغُوبٍ ﴿٣٨﴾ فَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا
 يَقُولُونَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ
 طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ ﴿٣٩﴾
 وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَأَدْبَرَ السُّجُودِ ﴿٤٠﴾

**36. Na kaumu ngapi
 Tuliziangamiza kabla yao
 waliokuwa na nguvu zaidi
 kuliko hawa! Nao wali-
 tangatanga katika nchi**

nyingi. Je! Walipata pa kukimbilia?

37. Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia.

38. Na bila ya shaka Sisi Tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yao siku sita; na wala hayakutugusa machofu.

39. Basi vumilia kwa hayo wasemayo, na mtakase kwa kumsifu Mola Wako Mlezi kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa.

40. Na katika usiku pia mtakase, na baada ya kusujudu.

Makafiri Waonywa Kupewa Adhabu na Mtume ﷺ Agizwa kuwa na Subira na Kusali.

Allah تعالى Anauliza, 'Wangapi Tuliowahilikisha kabla ya makafiri hawa wanaokana.'

مِنْ قَرْنٍ هُمْ أَشَدُّ مِنْهُمْ بَطْشًا

"Na kaumu ngapi Tuliziangamiza kabla yao waliokuwa na nguvu zaidi kuliko hawa."

Walikuwa wengi zaidi, wenye nguvu zaidi kuliko wao na ambao walijenga duniani kuliko wao. Kauli ya Allah تعالى,

فَتَقَبُّوْا فِي الْبَلَدِ هَلْ مِنْ مَّحِيصٍ

"Nao walitanga tanga katika nchi nyingi. Je! Walipata pa kukimbilia?"

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alitoa rai, "Waliacha alama katika ardhi,"¹ Qatadah amesema, "Walisafiri ardhini kutafuta fadhila kwa njia ya biashara, zaidi kuliko nyinyi." Kauli ya Allah تعالى,

هَلْ مِنْ مَّحِيصٍ

"Je! Walipata pa kukimbilia?"

Inamaanisha, 'walimudu kupata kimbilio dhidi ya hukumu na kudura ya Allah? Je walivyovikusanya viliwanufaisha au kuwaepushia adhabu ya Allah تعالى ilipowafikia kutokana na kitendo chao cha kuwakataa Mitume, kamwe hamtaweza kuikwepa, kuiepuka wala kupata kimbilio (mbali na adhabu Yake).' Allah تعالى Amesema,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرٍ

"Hakika katika hayo upo ukumbusho."

Na fundisho,

لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ

"Kwa mwenye moyo." Maana yake: Uelewa mzuri unaomfanya afahamu, au, akili nzuri, kwa mujibu wa Mujahid.

¹ At-Tabari 22:371.

أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ

“Au akatega sikio naye yupo anashuhudia”.

Maana yake: Anasikia kauli, anaiielewa na kuifahamu akilini mwake na anapata ishara zake kwa akili yake. Mujahid amesema kuwa,

أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ

“Au akatega sikio.”

Inamaanisha, haiambii nafsi yake bali anasikiliza kwa moyo makini.¹ Adh-Dhahhak alitoa rai, “Waarabu huweza kusema kuwa fulani ametoa sikio wakati anaposikia kwa masikio yake, huku moyo wake upo hapo na haukosekani.”² Ath-Thawri na wengine kadha wamesema sawa na hayo.³ Kauli ya Allah تعالى;

وَلَقَدْ خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا مَسَّنَا مِنْ لُغُوبٍ ﴿١٧٦﴾

“Na bila ya shaka Sisi Tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yao katika siku sita; na wala hayakutugusa machofu”.

Ni msisitizo juu ya Ufufuo kwa sababu Yule Mwenye Uwezo wa Kuumba mbingu na ardhi pasi na kuchoka, kwa hakika basi, Anaweza Kufufua wafu. Qatadah amesema, “Mayahudi, laana ya Allah تعالى iwashukie, walisema kuwa Allah تعالى Aliumba mbingu na ardhi kwa siku sita na Akapumzika katika siku ya saba, ambayo ilikuwa Sabato. Hii ndiyo sababu wanaiita siku ya mapumziko. Allah تعالى Mtukufu baadaye Aliteremsha Aya ya Kuwakanusha kauli yao na mtazamo wao potofu.”⁴ Allah تعالى Amesema,

وَمَا مَسَّنَا مِنْ لُغُوبٍ

“Na wala hayakutugusa machofu”. Inaonesha kuwa hakuna kulala, wala kuchoka au athari za uchofu zinazoweza kumpata. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

¹ At-Tabari 22:378.

² At-Tabari 22:374.

³ At-Tabari 22:374.

⁴ At-Tabari 22:376.

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْزُبْ عَنْهُم مِّنْ قَدْرٍ عَلَىٰ أَنْ يُحْيِيَ
الْمَوْتَىٰ بَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٦﴾

Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba, kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.” (46:33),

لَخَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

“Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.” (40:57)

Na Allah تعالى Amesema,

ءَأَنْتُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءُ بَنَاهَا ﴿٧٩﴾

“Je! Ni vigumu zaidi Kukuumbeni nyinyi au mbingu? Yeye Ndiye Aliyeijenga!” (79:27)

Allah تعالى Amesema,

فَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ

“Basi vumilia kwa hayo wasemayo.”

Katika kuwataja waliomkataa Mtume ﷺ, maana yake: wanakanusha, wavumilie wao na ujitenge nao kwa namna nzuri.

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ

“Na mtakase kwa kumsifu Mola Wako Mlezi kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa.”

Kulikuwa na Sala mbili za faradhi kabla ya safari ya Israa. Moja ilikuwa kabla ya jua kuchomoza na nyingine kabla ya jua kuzama wakati wa magharibi. Sala ya *Qiyam Al-Layl*, wakati wa usiku iliamrisha kwa Mtume ﷺ na wafuasi wake kwa muda fulani lakini baadaye iliondoshwa hukumu yake kwa ajili ya

umma. Baadaye, wakati wa safari ya Israa, Allah تعالى Aliziondosha amri zote za nyuma kuhusu Sala kwa kufaradhisha Sala tano, ikiwa ni pamoja na Sala ya Alfajri kabla ya kuchomoza jua, na Alasiri wakati wa jioni. Imamu Ahmad ameandika kuwa Jarir bin 'Abdullah رضي الله عنه amesema, "Kipindi fulani tukiwa tumeketi pamoja na Mtume ﷺ, aliutazama mwezi ulioangaza kwa mbalamwezi kali, akasema,

«أَمَا إِنَّكُمْ سَتُعْرَضُونَ عَلَى رَبِّكُمْ فَتَرَوْنَهُ كَمَا تَرَوْنَ هَذَا الْقَمَرَ لَا تُضَامُونَ فِيهِ، فَإِنْ اسْتَطَعْتُمْ أَنْ لَا تُغْلَبُوا عَلَى صَلَاةٍ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ غُرُوبِهَا فَافْعَلُوا»

"Kwa hakika nyinyi mtapelekwa mbele ya Mola Wenu Mlezi na mtamuona Yeye kama mnavyouona mwezi huu, wala hamtakuwa na kizuizi katika kumuona. Kwa hiyo, ikiwa mnaweza kutekeleza Sala kabla ya kuchomoza jua na kabla ya magharibi, fanyeni hivyo."

Akasoma Kauli ya Allah تعالى،

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ

"Na mtakase kwa kumsifu Mola Wako Mlezi kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa."¹

Bukhari na Muslim na kundi la waandishi wa Hadithi wakusanyaji waliinukuu Hadithi hii kupitia isnadi ya Isma'il.²

Agizo la Kumtakasa Allah تعالى Baada ya Sala

Allah تعالى Amesema،

وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ

"Na katika usiku pia mtakase."

Inamaanisha, muombe Yeye dua. Allah تعالى Amesema katika Aya،

¹ Ahmad 4:365

² *Fat'h Al-Bari* 8:462, *Muslim* 1:439. Abu Dawud 5:97, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 7:265, An-Nasai katika *Al-Kubra*, 6:469 na Ibn Majah 1:63.

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٣٦﴾

**“Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunna khasa kwako wewe.
Huenda Mola Wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinachosifika.”
(17:79)**

Ibn Abu Najih alisimulia kuwa Mujahid amesema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema,

وَأَدْبَرَ السُّجُودِ

“Na baada ya kusujudu.”

Inamaanisha *Tasbih*, yaani, kutaja sifa za Allah تعالى, baada ya Sala.¹ Kuna Hadithi iliyokusanywa ndani ya Sahihi Mbili inayoithibitisha maana hii. Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, “Baadhi ya Muhajirina masikini walikuja na wakasema, ‘Ewe Mtume! Matajiri watapata daraja za juu na watakuwa na furaha ya milele.’ Mtume ﷺ akawajibu,

«وَمَا ذَاكَ؟»

“Ni kitu gani hicho?”

Wakasema, ‘Wanasali sawa na sisi, wanafunga kama sisi, tena wanatoa Sadaka, lakini sisi hatumudu. Wanawaacha huru watumwa, sisi hatuwezi.’ Mtume ﷺ akasema,

«أَفَلَا أَعَلَّمْتُمْ شَيْئًا إِذَا فَعَلْتُمُوهُ سَبَقْتُمْ مِنْ بَعْدِكُمْ وَلَا يَكُونُ أَحَدٌ أَفْضَلَ مِنْكُمْ إِلَّا مَنْ فَعَلَ مِثْلَ مَا فَعَلْتُمْ؟ تُسَبِّحُونَ وَتُحَمِّدُونَ وَتُكَبِّرُونَ دُبُرَ كُلِّ صَلَاةٍ ثَلَاثًا وَثَلَاثِينَ»

“Je nikufundisheni jambo ambalo mkilifanya mtawa shinda wale wa baada yenu na wala hakutakuwa mbora zaidi yenu isipokuwa watakaofanya kama nyinyi, semeni ‘Subhana Allah, Alhamdulillah, Allahu Akbar,’ mara thelathini na tatu baada ya kila Sala.”

Baadaye, walirudi na kusema, ‘Ewe Mtume! Ndugu zetu, Waislamu matajiri, wamesikia tulivyofanya, na wao wanafanya vivyo hivyo.’ Mtume ﷺ amesema,

¹ At-Tabari 22:381.

«ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ»

“Hizo ni fadhila za Allah Humpa amtakaye”.¹

Na kauli ya pili, ni kwamba kusudio la Allah تعالى katika Kauli Yake,

وَأَدْبَرَ السُّجُودِ

“Na baada ya kusujudu.”

Inakusudia Rakaa mbili baada ya Sala ya Magharibi. Haya yamesimuliwa kutoka kwa ‘Umar bin Al-Khattab, ‘Ali bin Abi Talib na mwanaye Al-Hasan, ‘Abdullah bin ‘Abbas, Abu Hurayrah na Abu Umamah رضي الله عنهم.

Pia hii ni kauli ya Mujahid, ‘Ikrimah, Ash-Sha’bi, An-Nakha’i, Al-Hasan Al-Basri, Qatadah, na wengine.

وَأَسْتَمِعَ يَوْمَ يُنَادِ الْمُنَادِ مِنْ مَّكَانٍ قَرِيبٍ ﴿٤١﴾ يَوْمَ يَسْمَعُونَ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ ذَٰلِكَ
 يَوْمَ الْخُرُوجِ ﴿٤٢﴾ إِنَّا نَحْنُ نُحْيِيهِمْ وَنُمِيتُهُمْ وَإِلَيْنَا الْمَصِيرُ ﴿٤٣﴾ يَوْمَ نَشْفِقُ الْأَرْضَ عَنْهُمْ
 سِرَاعًا ذَٰلِكَ حَشْرٌ عَلَيْنَا يَسِيرٌ ﴿٤٤﴾ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ ط وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِجَبَّارٍ ط فَذَكِّرْ
 بِالْقُرْآنِ مَن يَخَافُ وَعِيدِ ﴿٤٥﴾

41. Na sikiliza siku ataponadi mwenye kunadi kutoka pahala karibu.

42. Siku watakaposikia ukelele wa haki. Hiyo ndiyo siku ya kufufuka.

43. Hakika Sisi Tunahuisha na Tunafisha, na Kwetu Sisi ndio marejeo.

44. Siku itapowapasukia ardhi haraka haraka! Mkusanyo huo kwetu ni mwepesi.

45. Sisi Tunajua kabisa wayasemayo. Wala wewe si mwenye kuwatawalia kwa ujabari. Basi mkumbushe kwa Qur’ani anayeliogopa onyo.

¹ Fat’h Al-Bari 2:378.

Kukumbushwa Baadhi ya Yatakayotukia Siku ya Ufufuo

Allah تعالى Amesema,

وَأَسْتَمِعْ

“Na sikiliza”

‘Ewe Muhammad ﷺ’

يَوْمَ يُنَادِ الْمُنَادِ مِنْ مَكَانٍ قَرِيبٍ

“Siku ataponadi mwenye kunadi kutoka pahala karibu.”

Kwenda katika mkusanyiko wa Siku ya Hukumu.

يَوْمَ يَسْمَعُونَ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ

“Siku watakaposikia ukelele wa haki”.

Inamaanisha mpulizo wa Parapanda litakaloleta ukweli ambao wengi wao waliupuuza na wakaukataa,

ذَلِكَ يَوْمَ الْخُرُوجِ

“Hiyo ndiyo siku ya kufufuka.”

Kutoka makaburini.

إِنَّا نَحْنُ نُحْيِيهِمْ وَنُمِيتُهُمْ وَإِلَيْنَا الْمَصِيرُ ﴿٥٠﴾

“Hakika Sisi Tunahuisha na Tunafisha, na Kwetu Sisi ndio marejeo.”

Allah تعالى Ndiye Anayeanzisha Uumbaji na Ndiye Anayeurejesha tena, na hili la mwisho ni jepesi Kwake; Kwake Yeye ndio marejeo ya viumbe wote. Kwa wakati huu Atamlipa kila mmoja kwa mujibu wa amali zake, wema kwa wema na ubaya kwa ubaya. Allah تعالى Amesema,

يَوْمَ تَشَقُّقُ الْأَرْضُ عَنْهُمْ سِرَاعًا

“Siku itapowapasukia ardhi mbiombio! Mkusanyo huo Kwetu ni mwepesi.”

Allah تعالی Atateremsha mvua toka mbinguni. Kutokana na mvua hiyo, viwiliwili vya viumbe vitamea kutoka makaburini mwao mithili ya mbegu zinavyoota katika udongo baada ya kunyesha mvua. Viwiliwili vikishamea na kukamilika, Allah تعالی Atamuamuru Malaika Israfil عليه السلام na ambaye atapuliza parapanda (kwa mara ya pili). Roho zitakuwa zimezungushiwa katika tundu lililo katika parapanda. Israfil عليه السلام atakapopuliza katika tundu la parapanda, roho zitatoka kupitia kwenye parapanda hilo na zitaruka baina ya mbingu na ardhi.

Allah تعالی Atanadi, "Naapa kwa Utukufu Wangu na Nguvu Zangu, kila roho itarejea katika kiwiliwili kilimokuwa ikiishi, na kwa kweli, kila roho itarudi katika kiwiliwili chake kilekile. Roho itaingia katika kiwiliwili chake kama sumu iingiavyo mwilini, halafu udongo utaondolewa kutoka juu yao, na wote watasimama na kuelekea kwenye mahali pa Hesabu kwa kuharakisha kutii amri ya Allah تعالی,

مُهْطِعِينَ إِلَى الدَّاعِ يَقُولُ الْكٰفِرُونَ هٰذَا يَوْمٌ عَسِرٌ ﴿٥٨﴾

"Wanamkimbililia muitaji, na makafiri wanasema: Hii ni siku ngumu." (54:8),

Na Allah تعالی Amesema,

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَظُنُّونَ اِنْ لَبِثْتُمْ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿٥٩﴾

"Siku atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru, na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mdogo tu". (17:52)

Katika Sahih, kumeandikwa kuwa Anas رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«أَنَا أَوَّلُ مَنْ تَنَسَّقُ عَنْهُ الْأَرْضُ»

"Mimi nitakuwa wa kwanza kupasukiwa na ardhi."¹

Allah تعالی Amesema,

¹ Muslim 4:1782.

ذَلِكَ حَشْرٌ عَلَيْنَا يَسِيرٌ

“Mkusanyo huo Kwetu ni mwepesi.”

Maana yake: ‘Huko Kuwarejesha hai ni rahisi Kwetu wala hakuna juhudi yoyote.’
Ni kama Kauli nyingine ya Allah تعالى،

وَمَا أَمْرًا إِلَّا وَاحِدَةً كَلِمَةٍ بِالْبَصْرِ ﴿٥٠﴾

“Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.” (54:50),

Na Allah تعالى Amesema,

مَا خَلَقُكُمْ وَلَا بَعَثُكُمْ إِلَّا كَنَفْسٍ وَاحِدَةٍ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٣١﴾

“Hakukuwa Kuumbwa kwenu, wala Kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona. (31:28)

Kumfariji Mtume ﷺ

Kauli ya Allah تعالى،

لَحْنٌ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ ط

“Sisi Tunajua kabisa wayasemayo.”

Inamaanisha, ‘Elimu Yetu inayazunguka wanayokuambia washirikina miongoni mwa uzushi na ukadhibishaji, hivyo usijihangaishe.’ Katika Aya nyingine, Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّكَ يَضِيقُ

صَدْرُكَ بِمَا يَقُولُونَ ﴿١٥﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُنْ مِنَ السَّاجِدِينَ ﴿١٦﴾ وَأَعْبُدْ رَبَّكَ

حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿١٧﴾

“Na Sisi Tunajua kwa hakika kuwa wewe kifua chako kinaona dhiki kwa hayo wayasemayo. Basi mtakase Mola Wako Mlezi kwa kumhimidi, na uwe miongoni wanaomsujudia. Na muabudu Mola Wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini. ” (15:97-99)

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِجَبَّارٍ ط

“Wala wewe si mwenye kuwatawalia kwa ujabari.”

Anasema, ‘si wewe unayewalazimisha kupokea uongofu, hii si sehemu ya kazi yako.’ Allah تعالى Amesema,

فَذَكِّرْ بِالْقُرْآنِ أَنْ مِّنْ تَخَافُ وَعِيدِ

“Basi mkumbushe kwa Qur’ani anayeliogopa onyo.”

Maana yake: ‘Fikisha Ujumbe wa Mola Wako, kwani ni wale tu wanaomuogopa Allah تعالى na adhabu Zake, na wana matumaini na ahadi Yake ndio watakaokumbuka na kutia maanani.’

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ

“Juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu yetu ni hisabu.” (13:40),

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ﴿٥٨﴾ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ﴿٥٩﴾

“Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia.” (88:21-22)

لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ؕ

“Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakae”. (2:272)

Na Allah تعالى Amesema hapa,

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ؕ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿٥٨﴾

“Kwa hakika wewe humuongoi umpendaye, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye. Na Yeye Ndiye Anawajua zaidi waongokao.” (28:56)

Kauli ya Allah تعالى katika Aya hii,

وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِجَبَّارٍ ۖ فَذَكِّرْ بِالْقُرْآنِ مَن يَخَافُ وَعِيدِ

“Wala wewe si mwenye kuwatawalia kwa ujabari. Basi mkumbushe kwa Qur’ani anayeliogopa onyo.”

Qatadah alikuwa akiomba, “Ewe Allah! Tujaalie tuwe miongoni mwa wanaoogopa Kitisho Chako na wana Matumaini na Ahadi Yako, ewe Mwema, ewe Mwenye Kurehemu.”¹

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Surat Qaf*. Kila Sifa njema ni za Allah تعالی. Naye ni Mbora wa kumtawakali.



¹ Al-Qurtubi 17:29.

Tafsiri ya Suratu Adh-Dhaariyaat

Sura ya 51

Iliteremshwa Makkah

سُوْرَةُ الدَّارِيَااتِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالدَّارِيَاتِ ذُرْوًا ﴿١﴾ فَالْحَمَلَاتِ ﴿٢﴾ وَالْجُرِيَاتِ يُسْرًا ﴿٣﴾
 وَالْمَقْسَمَاتِ أَمْرًا ﴿٤﴾ إِنَّمَا تُوعَدُونَ لَصَادِقٍ ﴿٥﴾
 وَإِنَّ الَّذِينَ لَوْفَعُ ﴿٦﴾ وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْحُبُكِ ﴿٧﴾ إِنَّكُمْ
 لَفِي قَوْلٍ مُخْتَلِفٍ ﴿٨﴾ يُؤَفِّكُ عَنْهُ مَنَ أُوْفِكَ ﴿٩﴾ قَتَلَ
 الْحَرَصُونَ ﴿١٠﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي عَمْرٍو سَاهُونَ ﴿١١﴾
 يَسْأَلُونَ أَيَّانَ يَوْمِ الدِّينِ ﴿١٢﴾ يَوْمَ هُمْ عَلَى النَّارِ يُفْتَنُونَ ﴿١٣﴾
 ذُوقُوا فِتْنَتَكُمْ هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِمِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿١٤﴾
 إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿١٥﴾ ءَاخِذِينَ مَا ءَاتَاهُمْ
 رَبُّهُمْ إِنَّهُمْ كَانُوا قَبْلَ ذَلِكَ مُحْسِنِينَ ﴿١٦﴾ كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ
 آلِئِلِ مَا يَهْجُونَ ﴿١٧﴾ وَبِالْآسْتِحَارِ هُمْ يَسْتَعْجِرُونَ ﴿١٨﴾ وَفِي
 أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿١٩﴾ وَفِي الْأَرْضِ ءَايَاتٌ
 لِّلْمُوقِنِينَ ﴿٢٠﴾ وَفِي أَنْفُسِكُمْ ءَآفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٢١﴾ وَفِي
 السَّمَاءِ رِزْقُكُمْ وَمَا تُوعَدُونَ ﴿٢٢﴾ فَوَرَبِّ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ
 إِنَّهُ لَحَقٌّ مِّثْلَ مَا أَنَّكُمْ تَنْطِقُونَ ﴿٢٣﴾

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi
wa Rehema Mwenye
Kurehemu.

وَالدَّارِيَاتِ ذُرْوًا ﴿١﴾ فَالْحَمَلَاتِ ﴿٢﴾
 وَالْجُرِيَاتِ يُسْرًا ﴿٣﴾ وَالْمَقْسَمَاتِ أَمْرًا ﴿٤﴾
 إِنَّمَا تُوعَدُونَ لَصَادِقٍ ﴿٥﴾ وَإِنَّ الَّذِينَ لَوْفَعُ ﴿٦﴾
 وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْحُبُكِ ﴿٧﴾ إِنَّكُمْ لَفِي قَوْلٍ مُخْتَلِفٍ ﴿٨﴾
 يُؤَفِّكُ عَنْهُ مَنَ أُوْفِكَ ﴿٩﴾ قَتَلَ الْحَرَصُونَ ﴿١٠﴾
 الَّذِينَ هُمْ فِي عَمْرٍو سَاهُونَ ﴿١١﴾ يَسْأَلُونَ أَيَّانَ يَوْمِ
 الدِّينِ ﴿١٢﴾ يَوْمَ هُمْ عَلَى النَّارِ يُفْتَنُونَ ﴿١٣﴾
 ذُوقُوا فِتْنَتَكُمْ هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِمِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿١٤﴾

1. Naapa kwa pepo zinazo tawanya.

2. Na zinazobeba mizigo.

3. Na zinazokwenda kwa wepesi.

4. Na zinazogawanya kwa amri.
5. Hakika mnayoahidiwa bila ya shaka ni kweli.
6. Na kwa hakika malipo bila ya shaka yatatokea.
7. Naapa kwa mbingu zenye njia.
8. Hakika nyinyi bila ya shaka mmo katika kauli inayokhitalifiana.
9. Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa.
10. Wazushi wameangamizwa.
11. Ambao wameghafilika katika ujinga.
12. Wanauliza: Ni lini hiyo siku ya malipo?
13. Hiyo ni siku watakayoadhibiwa Motoni.
14. Onjeni adhabu yenu! Haya ndiyo mliyokuwa mkiyahimiza.

Kuthibitisha Habari za Ufufuo na Hesabu

'Ali bin Abu Talib رضي الله عنه, alipanda juu ya Mimbari katika mji wa Kufah, akatangaza, "Aya yoyote katika Kitabu cha Allah تعالى na Sunnah yoyote kutoka kwa Mtume ﷺ mtakayoniuliza leo nitakujibuni." Ibn Al-Kawwa amesema, "Ewe amiri wa Waumini! Ni nini maana ya Kauli ya Allah تعالى,

وَأَلذَّيْبَتِ ذُرْوًا

"Naapa kwa pepo zinazotawanya."

'Ali رضي الله عنه amesema, "Upepo". Mmoja akauliza,

فَأَحْمَلَتِ وَقْرًا

"Na zinazobeba mizigo."

'Ali رضي الله عنه alisema, "mawingu." Yule mtu aliuliza tena,

فَأَجْرَيْتِ يُسْرًا

"Na zinazokwenda kwa wepesi."

'Ali رضي الله عنه amesema, "majahazi." Yule mtu aliuliza,

فَالْمُقَسَّمَتِ أَمْرًا ﴿١٠﴾

"Na zinazogawanya kwa amri."

'Ali رضي الله عنه amesema, inamaanisha "Malaika."¹ Baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa zinazokwenda kwa wepesi *Yusra* ina maana ya nyota zinazopita katika njia zake kwa wepesi ili ziwe zikipanda kwa mpangilio kwa kuanzia chini na kuja juu. Pepo huleta mawingu, nyota ziko juu yake na malaika ambao hupeleka amri ya Allah تعالى wako juu yake, na hushuka kwa amri na hukumu ya Allah تعالى. Aya hizi zina kiapo kutoka kwa Allah تعالى kuwa Ufufuo utatukia. Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّمَا تُوْعَدُونَ لَصَادِقٌ

"Hakika mnayohidiwa bila ya shaka ni kweli."

Ni ahadi ya kweli,

وَإِنَّ الدِّينَ

"Na kwa hakika malipo"

(Kwa kweli, *Ad-Din*) ni hesabu ya malipo.

لَوْ قَعٌ

"Bila ya shaka yatatokea."

Kwa hakika hilo litafanyika. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْحُبُوبِ ﴿١١﴾

"Naapa kwa mbingu zenye njia."

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema; "Zimejaa uzuri, huba, sifa na ubora."² Mujahid, 'Ikrimah, Sa'id bin Jubayr, Abu Malik, Abu Swalih, As-Suddi, Qatadah, 'Atiyah, Al-'Awfi, Ar-Rabi' bin Anas na wengine wamesema sawa na hivyo.³

¹ At-Tabari 22:389-392 na 'Abdur-Razzaq 3:41.

² At-Tabari 22:395-396.

³ At-Tabari 22:396-397.

Adh-Dhahak, Al-Minhal bin 'Amr na wengine wamesema, "inamaanisha kupindapinda kwa maji, mchanga na mimea pindi upepo unapopita juu yake; huku ikitengeneza njia humo, hiyo ndiyo *Hubuk*." Kazi zote hizi zinamaanisha kitu hicho hicho kimoja, yaani uzuri na ubora. Mbingu iko juu yetu, safi na nene, imesimamishwa imara, kubwa, yenye huba, huku ikiwa imependezeshwa na nyota zilizotulia na zinazotembea kama vile sayari zenye kuzunguka katika njia zao kama vile mwezi na sayari zilizo katika mfumo wa jua.

Kutofautiana kauli za Washirikina

Allah تعالی Amesema,

﴿إِنكُم لَفِي قَوْلٍ مُّخْتَلِفٍ﴾

"Hakika nyinyi bila ya shaka mmo katika kauli inayokhitalifiana."

Allah تعالی Anasema, 'nyinyi makafiri mnaowakana Mitume mna mitazamo yenye kutofautiana ambayo haiungani au kuwa sambamba. 'Qatadah alitoa rai juu ya Ayah, "Mna rai tofauti kuhusu Qur'an. Baadhi yenu mnakubali kuwa ni ya kweli ilhali wengine mnaukataa ukweli huu."¹ Allah تعالی Akasema,

﴿يُؤْفِكُ عَنْهُ مَنَ أُولَئِكَ﴾

"Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa."

Allah تعالی Anasema, maoni haya yaliyochanganyika na kutofautiana huwapumbaza tu wale wasioongoka. Hakika, upotovu huu hukubaliwa, hukumbatiwa na unakuwa chanzo cha uharibifu wa wasioongoka na waongo, wapumbavu ambao hawana uelewa sahihi, sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی,

﴿فَإِنكُم مَّا تَعْبُدُونَ﴾ مَّا أَنتُمْ عَلَيْهِ بِفَعْتِينَ ﴿١٦١﴾ إِلَّا مَن هُوَ صَالٍ الْجَحِيمِ ﴿١٦٢﴾

"Basi hakika nyinyi na mnaowaabudu. Hamuezi kuwapoteza. Isipokuwa yule atakayeingia Motoni." (37:161-163)

¹Abdur-Razzaq 4242

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na As-Suddi wamesema:

يُؤْفِكُ عَنْهُ مَنْ أُفِكَ ﴿٥١﴾

“Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa.”

“Yule asiyeongoka hupotoka kutokana nayo.” Allah تعالى Akasema;

قُتِلَ الْخَرَّاصُونَ ﴿٥٢﴾

“Wazushi wameangamizwa.”

Mujahid alisema; “waongo” Hii inalingana na kilichotajwa katika (Surah) 'Abasa:

قُتِلَ الَّذِينَ مَآ أَكْفَرَهُ ﴿٥٣﴾

“Ameangamia mwanaadamu! Nini kinachomkufurisha?” (80:17)

Al-Kharrasun, “wazushi” ni wale wanaodai kuwa hawatafufuliwa, wakitilia mashaka Ufufuo.’¹ ‘Ali bin Abu Talhah alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa;

قُتِلَ الْخَرَّاصُونَ ﴿٥٤﴾

“Wazushi wameangamizwa”.

Wamelaaniwa wenye kutia shaka. Mu’adh رضي الله عنه amesema sawa na hivyo. Katika mojawapo ya hotuba zake amesema, “Wameangamia wenye mashaka.”² Qatadah amesema, “*Al-Kharrasun*” ni watu wenye mashaka na wasiwasi.’³ Allah تعالى Amesema;

الَّذِينَ هُمْ فِي عَمْرَةٍ سَاهُونَ ﴿٥٥﴾

“Ambao wameghafilika katika ujinga”.

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, na wengine wamesema; “katika ukafiri na mashaka, wao ni wazembe na wanafanya mchezo.”⁴ Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 22:400.

² At-Tabari 22:399.

³ At-Tabari 22:400.

⁴ At-Tabari 22:400-401.

يَسْأَلُونَ أَيَّانَ يَوْمِ الَّذِينَ ﴿٥١﴾

“Wanauliza: Ni lini hiyo siku ya malipo?”

Wao hutamka kauli hii katika ukanaji, ukaidi, mashaka na wasiwasi.

Allah تعالى Akajibu,

يَوْمَ هُمْ عَلَى النَّارِ يُفْتَنُونَ ﴿٥٢﴾

“Hiyo ni siku watakayoadhibiwa Motoni.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Mujahid, Al-Hasan na wengine kadha wamesema kuwa *Yuftanun* inamaanisha wenye kupewa adhabu.¹ Mujahid: “Kama ambavyo dhahabu hulainishwa kwenye moto.”² Kundi jingine pia akiwemo Mujahid, ‘Ikrimah, Ibrahim An-Nakha’i, Zayd bin Aslam, na Sufyan Ath-Thawri wamesema, “Watachomwa moto.”

ذُوقُوا فِتْنَتَكُمْ ﴿٥٣﴾

“Onjeni adhabu yenu!”

Mujahid amesema, “Kuchomwa kwenu motoni,”³ ilhali wengine wamesema, “Adhabu yenu.”

هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٥٤﴾

“Haya ndiyo mliyokuwa mkiyahimiza”

Hii ni kauli ya kuwaonya, kuwadhibu, kuwafedhehesha na kuwadhalilisha.

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٥٥﴾ ءَأَخِذِينَ مَا ءَاتَاهُمْ رَبُّهُمْ ءِإِنَّهُمْ كَانُوا قَبْلَ ذَلِكَ
مُحْسِنِينَ ﴿٥٦﴾ كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ ﴿٥٧﴾ وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿٥٨﴾ وَفِي
أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٥٩﴾ وَفِي الْأَرْضِ ءَايَاتٌ لِّلْمُوقِنِينَ ﴿٦٠﴾ وَفِي أَنْفُسِكُمْ
أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٦١﴾ وَفِي السَّمَاءِ رِزْقُكُمْ وَمَا تُوعَدُونَ ﴿٦٢﴾ فَوَرَبِّ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِنَّهُ
لَحَقٌّ مِّثْلَ مَا أَنَّكُمْ تَنْطِقُونَ ﴿٦٣﴾

¹ At-Tabari 22:402.

² At-Tabari 22:402.

³ At-Tabari 22:403.

15. *Hakika wachamngu watakuwa katika bustani na chemchem.*
16. *Wanapokea aliyowapa Mola Wao Mlezi. kwa hakika hao walikuwa kabla ya haya wakifanya wema.*
17. *Walikuwa wakilala kidogo tu usiku.*
18. *Na kabla ya alfajiri wakiomba maghufira.*
19. *Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na anayejizua kuomba.*
20. *Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini.*
21. *Na pia katika nafsi zenu - Je! Hamuoni?*
22. *Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyoahidiwa.*
23. *Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, hakika haya ni kweli kama ilivyo kweli kuwa nyinyi mnasema.*

Sifa za Wachamungu na Malipo Yao

Allah تعالیٰ Anajulisha kuhusu wale wenye kumchamungu *Taqwa*, kuwa katika siku ya Kurejeshwa kwao watakuwa katika bustani na chemchemi. Tofauti na hivyo, wenye hasara watakuwa katika mateso, adhabu, moto na minyororo. Allah تعالیٰ Amesema,

ءَاخِذِينَ مَا آتَيْنَهُمْ نُهُمْ

“Wanapokea aliyowapa Mola wao Mlezi”

Kauli Yake Allah تعالیٰ;

ءَاخِذِينَ

“Wanapokea”

Inaelezea hali za wachamungu katika bustani na chemchemi. Wao watapokea kile ambacho Mola wao Mlezi Atawapa wote, furaha na fadhila. Allah تعالیٰ Amesema,

إِنَّمَا كَانُوا قَبْلَ ذَلِكَ

“Kwa hakika hao walikuwa kabla ya haya.”

Katika maisha ya dunia.

مُحْسِنِينَ

“Wakifanya mema.”

Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine,

كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ ﴿٦٩﴾

“Waambiwe: Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya mlivyotanguliza katika siku zilizo pita.” (69:24)

Allah تعالى Ameeleza amali nzuri walizozifanya,

كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ ﴿٧٠﴾

“Walikuwa wakilala kidogo tu usiku.”

Wanazuoni wa Tafsiri wana rai mbili juu ya hili:

Rai ya Kwanza

Kwanza ni kuwa, walikuwa wakitumia sehemu ndogo ya usiku bila ya kulala. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema, “Kila usiku, walikuwa wakimuabudu Allah تعالى, hata wakati wa sehemu ndogo ya usiku.”¹

Qatadah alisimulia kuwa Mutarrif bin ‘Abdullah amesema, “Ni vigumu wao kupitwa na usiku pasi na wao kumuomba Allah تعالى, ama mwanzoni au katikati yake.”² Mujahid amesema, “Ni nyakati chache tu za usiku, kama zipo, ambapo wao hulala usiku kucha mpaka asubuhi, bila ya kusali *Tahajjud*.”³ Qatadah amesema sawa na hayo.⁴ Anas bin Malik رضي الله عنه na Abu Al-‘Aliyah رضي الله عنه wamesema, “Wamekuwa wakisali baina ya *Al-Maghrib* na *Al-‘Isha*.”⁵

¹ At-Tabari 22:407.

² At-Tabari 22:407.

³ At-Tabari 22:408.

⁴ At-Tabari 22:408.

⁵ At-Tabari 22:407-408.

Rai ya Pili

Walikuwa wakitumia sehemu ndogo ya usiku kwa kulala. Rai hii ni ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى amesema:

كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ ﴿٥١﴾

“Walikuwa wakilala kidogo tu usiku.”

“Walikuwa wakisali Sala za suna za usiku na hawakulala usiku isipokuwa kidogo. Walikuwa wakikeshwa na kuendelea huku wakiomba msamaha muda wa kabla ya alfajiri.”³

‘Abdullah bin Salam amesema, “Mtume ﷺ alipowasili Madinah, kwa haraka watu walikusanyika kumzunguka nami nikawa miongoni mwao pindi nilipouona uso wake, nilijua kuwa haukuwa uso wa mwenye kuongopa. Kwanza kauli niliyoisikia kutoka kwake ilikuwa,

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ! أَطْعَمُوا الطَّعَامَ، وَصَلُّوا الْأَرْحَامَ، وَأَنْفُسُوا السَّلَامَ، وَصَلُّوا بِاللَّيْلِ
وَالنَّاسُ نِيَامٌ، تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ بِسَلَامٍ»

“Enyi watu! lisheni chakula, ungeni undugu, enezeni Salamu, salini usiku ilhali watu wakiwa wamelala, mtaingia Peponi kwa amani.”⁴

Imamu Ahmad alinukuu kuwa ‘Abdullah bin ‘Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ عُرْقًا يُرَى ظَاهِرُهَا مِنْ بَاطِنِهَا وَبَاطِنُهَا مِنْ ظَاهِرِهَا»

“Hakika, Peponi kuna vyumba vya juu ambamo nje yake huonekana kwa ndani yake na ndani yake huonekana kwa nje yake.”

Abu Musa Al-Ash‘ar رضي الله عنه aliuliza, “Kwa ajili ya akina nani, Ewe Mjumbe wa Allah?” Akajibu,

¹ At-Tabari 22:408-409.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 7:187.

«يَمَنْ أَلَانَ الْكَلَامَ، وَأَطْعَمَ الطَّعَامَ، وَبَاتَ لِلَّهِ قَائِمًا وَالنَّاسُ نِيَامًا»

“Kwa ajili ya yule aliyelainisha maneno na wakalisha chakula, na wanaupitisha usiku kwa kusimama kusali ilhali watu wamelala.”¹

Allah تعالی Amesema:

وَيَا لَأَسْحَارٍ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿١٧﴾

“Na kabla ya alfajiri wakiomba maghfira”.

Mujahid na wengine kadha wamesema: “Walikuwa wakisali.”² Wengine wakasema walikuwa wakisimama kusali usiku na wakachelewa wakiwa wanamuomba Allah تعالی msamaha mpaka muda wa baadaye kabisa kabla ya alfajiri. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی;

وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ ﴿١٧﴾

“Na wanaomba maghfira kabla ya alfajiri.” (3:17);

Hii ni kwa sababu ni vizuri kuomba msamaha wakati wa kusali. Imethibitishwa katika vitabu vya Hadithi Sahih kadhalika na vingine, kutoka kwa Masahaba kadha, kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يَنْزِلُ كُلَّ لَيْلَةٍ إِلَى سَمَاءِ الدُّنْيَا حِينَ يَبْقَى ثُلُثُ اللَّيْلِ الْآخِرِ، فَيَقُولُ هَلْ مِنْ تَائِبٍ فَأَتُوبُ عَلَيْهِ. هَلْ مِنْ مُسْتَغْفِرٍ فَأَغْفِرَ لَهُ. هَلْ مِنْ سَائِلٍ فَيُعْطَى سَوْأَهُ حَتَّى يَطْلُعَ الْفَجْرُ»

“Allah, Mtukuka, Huteremka kila usiku mpaka katika mbingu ya chini wakati wa theluthi ya mwisho ya usiku. Anasema, “Kuna yoyote anayetubu ili Niipokee toba yake? Kuna yoyote mwenye kuomba msamaha, Nimsamehe? Kuna yoyote anayeniomba ili Nimpe? Hadi alfajiri iingie.”⁵

Wengi miongoni mwa wanazuoni wa Tafsiri wamesema kuwa pindi Mtume Ya'qub عليه السلام alipowaambia wanawe:

¹ Ahmad 2:173.

² At-Tabari 22:413.

³ Fat'h Al-Bari 3:35, 11:133 na 13:473, Muslim 1:521 na 523, Abu Dawud 2:77 na 5:101. Tuhfat Al-Ahwardhi 9:471, An-Nasai katika Al--Kubra, 4:24 na Ibn Majah 1:435.

سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي

“Akasema, Nitakuja kuombeeni msamaha kwa Mola Wangu Mlezi.” (12:98),

Alichelewesha kufanya hivyo mpaka muda mfupi kabla ya alfajiri. Allah تعالى Amesema,

وَفِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٩٨﴾

“Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiyeomba.”

Baada ya Allah تعالى Kutaja sifa zao za kusali, alitaja sifa zao zingine katika Sadaka, wema na kuenzi undugu,

وَفِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ

“Na katika mali yao ipo haki.”

Fungu ambalo wao huwatengea *Sa'il* na *Mahrum*. *Sa'il* ni masikini anayewaomba watu, naye ana fungu lake ni vivyo hivyo pia kwa *Mahrum*, Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na Mujahid amesema, “Ni masikini mtu asiyepokea ujira.”¹ Ikimaanisha hapokei kipato kutoka Baytulmal, wala hana namna ya kujipatia kipato, wala ujuzi.

Mama wa Waumini, 'A'ishah رضي الله عنها, amesema kuhusu *Mahrum*, “Aliyelazimishwa na hali, asiye na ujuzi wa kujipatia kipato.” Qatadah na Az-Zuhri: “*Mahrum* ni asiyeomba watu kwa ajili ya kitu chochote.”² Az-Zuhri aliongeza kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَيْسَ الْمَسْكِينُ بِالطَّوَّابِ الَّذِي تَرُدُّهُ اللَّقْمَةُ وَاللَّقَمَاتِ وَالثَّمَرَةُ وَالثَّمَرَاتِ، وَلَكِنَّ الْمَسْكِينُ الَّذِي لَا يَجِدُ غِنَى يُغْنِيهِ وَلَا يُفْطِنُ لَهُ فَيَتَصَدَّقَ عَلَيْهِ،»

“Masikini si yule ambaye huwazungukia watu na kuwaomba kitonge kimoja au viwili au tende moja au mbili. Bali, masikini ni yule asiye na kiasi cha kukidhi haja zake huku hali yake haifahamiki kwa wengine, ili waweze kumpa Sadaka.”³

¹ At-Tabari 22:414.

² At-Tabari 22:416.

³ An-Nasai 5:85.

Hadithi hii imeandikwa katika Sahih Mbili kwa kutumia isnadi nyingine ya masimulizi.¹

Ishara za Allah تعالی Duniani na Ndani ya Nafsi

Kauli Yake Allah تعالی,

وَفِي الْأَرْضِ آيَاتٌ لِّلْمُوقِنِينَ ﴿٥١﴾

“Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini.”

Maana yake: Ndani yake kuna ishara zinazoonesha nguvu kubwa ya Muumba na Uweza Wake mkubwa. Ishara hizi ni pamoja na vitu ambavyo Allah تعالی Ameviweka duniani, namna kadha wa kadha miongoni mwa mimea, wanyama, mabonde, milima, majangwa, mito na bahari. Pia Amemuumba mwanadamu na Kumuwzesha kuzungumza lugha mbalimbali, kuwa na tofauti ya rangi, utashi na uwezo. Na wengi miongoni mwao kutofautiana uwezo wa uelewa, ufahamu, kujituma, wema na uovu. Allah تعالی Ameweka kila kiungo katika miili yao katika mahali sahihi kabisa ambapo ndipo penye haja kubwa zaidi ya kuwepo hapo. Kwa hivyo Akasema:

وَفِي أَنفُسِكُمْ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٥٢﴾

“Na pia katika nafsi zenu - Je! Hamuoni?”

Qatadah amesema, “Mwenye kutafakari juu ya kuumbwa kwake yeye mwenyewe atagundua kuwa aliumbwa awe na maungo laini ili iwe wepesi kwake kufanya matendo ya kiibada.”² Kisha, Allah تعالی Akasema,

وَفِي السَّمَاءِ رِزْقُكُمْ

“Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyoahidiwa”

Maana yake: Mvua.

¹ Fat'h Al-Bari 3:399 na Muslim 2:719.

² Al-Qurtubi 17:40.

³ At-Tabari 22:420.

وَمَا تُوعَدُونَ

“Na mliyoahidiwa”.

Maana yake: Pepo. Rai hii imesemwa na Ibn ‘Abbas, Mujahid na wengine رضي الله عنهم³. Allah تعالى Amesema:

فَوَرَبِّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ إِنَّهُ لَحَقٌّ مِّثْلَ مَا أَنَّكُمْ تَنْطِقُونَ ﴿٥١﴾

“Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, hakika haya ni kweli kama ilivyo kweli kuwa nyinyi mnasema.”

Allah تعالى Anaapa kwa Nafsi Yake Tukufu, maana yake masuala ya Hukumu, Ufufuo, na Malipo kuwa ahadi zote zilizotolewa zititimia kwa hakika. Kwa hiyo, ni ukweli usio na shaka, basi msiwe na mashaka juu ya kuja kwake. Kama mtu asivyokuwa na mashaka ya kuweza kuzungumza na mmojawapo kati ya marafiki zake. Mu’adh رضي الله عنه alikuwa akisema: “Ninachokisema ni cha kweli kama ambavyo nyinyi mko hapa.”

* * *

هَلْ أَتٰنَكَ حَدِيثٌ ضَیْفِ اِبْرٰهِيْمَ ۝۱۱۱ ۝۱۱۲ اِذْ
 دَخَلُوْا عَلَيْهِ فَقَالُوْا سَلٰمًا ۝۱۱۳ قَالَ سَلٰمٌ قَوْمٌ مُّٰنِكُوْنَ ۝۱۱۴
 فَرٰغَ اِلٰى اٰهْلِيْهِ فَجَآءَ بِعِجْلٍ سَمِيْنٍ ۝۱۱۵ فَفَرَّقَتْهُ اِلَيْهِمْ
 قَالَ اَلَا تٰكْلُوْنَ ۝۱۱۶ فَاَوْجَسَ مِنْهُمْ خِیْفَةً ۝۱۱۷ قَالُوْا لَا
 تَخَفْ ۝۱۱۸ وَبَشِّرُوْهُ بِغُلٰمٍ عَلِيْمٍ ۝۱۱۹ فَاَقْبَلَتْ اَمْرٰتُهُ فِيْ صِرٰةٍ
 فَصَكَّتْ وَجْهَهَا وَقَالَتْ عَجُوْزٌ عَقِيْمٌ ۝۱۲۰ قَالُوْا كَذٰلِكَ
 قَالَ رَبُّكَ ۝۱۲۱ اِنَّهُ هُوَ الْحَكِيْمُ الْعَلِيْمُ ۝۱۲۲ * قَالَ فَمَا
 خَطْبُكُمْ اَيُّهَا الْمُرْسَلُوْنَ ۝۱۲۳ قَالُوْا اِنَّا اُرْسِلْنَا اِلٰى قَوْمٍ
 مُّٰجْرِمِيْنَ ۝۱۲۴ لِتُرْسَلَ عَلَيْهِمْ حِجَارَةٌ مِّنْ طِيْنٍ ۝۱۲۵ مُّسَوَّمَةٌ
 عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُسْرِفِيْنَ ۝۱۲۶ فَاَخْرَجْنَا مَنْ كَانَ فِيْهَا مِّنَ
 الْمُؤْمِنِيْنَ ۝۱۲۷ فَمَا وَجَدْنَا فِيْهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِّنَ الْمُتَسَلِّمِيْنَ
 ۝۱۲۸ وَتَرَكْنَا فِيْهَا اٰيَةً لِّلَّذِيْنَ يَخٰفُوْنَ الْعَذَابَ الْاَلِيْمَ ۝۱۲۹
 وَفِيْ مُوسٰى اِذْ اُرْسَلْنَاهُ اِلٰى فِرْعَوْنَ بِسُلْطٰنٍ مُّبِيْنٍ ۝۱۳۰
 فَتَوَلٰى بِرُكْبٰتِهٖ وَقَالَ سِحْرٌ اَوْ مَجْنُوْنٌ ۝۱۳۱ فَاَخَذْنَاهُ
 وَجُنُوْدَهُ فَتَبَدَّنٰهُمْ فِيْ اَلِيْمٍ وَهُوَ مُلِيْمٌ ۝۱۳۲ وَفِيْ عَادٍ اِذْ
 اُرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الرِّيْحَ الْعَقِيْمَ ۝۱۳۳ مَا تَدْرُوْنَ مِنْ شَيْءٍ اَنْتَ
 عَلَيْهِ اِلَّا جَعَلْتَهُ كَالرَّمِيْمِ ۝۱۳۴ وَفِيْ نُوْحٍ اِذْ قِيْلَ لَهُمْ
 تَمَتُّعُوْا حَتّٰى حِيْنٍ ۝۱۳۵ فَعَتَوْا عَنْ اَمْرِ رَبِّيْهِمْ فَاَخَذْنَا مِنْهُمُ
 الصَّبْعَةَ وَهُمْ يَنْظُرُوْنَ ۝۱۳۶ فَمَا اسْتَبْعُوْا مِنْ قِيٰمٍ وَمَا
 كَانُوْا مُّنتَصِرِيْنَ ۝۱۳۷ وَقَوْمَ نُوْحٍ مِّنْ قَبْلِ اِيْنِهِمْ كَانُوْا قَوْمًا
 فٰسِقِيْنَ ۝۱۳۸

هَلْ أَتٰنَكَ حَدِيثٌ ضَیْفِ اِبْرٰهِيْمَ
 اِذْ دَخَلُوْا عَلَيْهِ ۝۱۱۱ ۝۱۱۲ اِذْ دَخَلُوْا عَلَيْهِ
 فَقَالُوْا سَلٰمًا ۝۱۱۳ قَالَ سَلٰمٌ قَوْمٌ
 مُّٰنِكُوْنَ ۝۱۱۴ فَرٰغَ اِلٰى اٰهْلِيْهِ فَجَآءَ
 بِعِجْلٍ سَمِيْنٍ ۝۱۱۵ فَفَرَّقَتْهُ اِلَيْهِمْ
 قَالَ اَلَا تٰكْلُوْنَ ۝۱۱۶ فَاَوْجَسَ
 مِنْهُمْ خِیْفَةً ۝۱۱۷ قَالُوْا لَا
 تَخَفْ ۝۱۱۸ وَبَشِّرُوْهُ
 بِغُلٰمٍ عَلِيْمٍ ۝۱۱۹ فَاَقْبَلَتْ
 اَمْرٰتُهُ فِيْ صِرٰةٍ فَصَكَّتْ
 وَجْهَهَا وَقَالَتْ عَجُوْزٌ
 عَقِيْمٌ ۝۱۲۰ قَالُوْا كَذٰلِكَ
 قَالَ رَبُّكَ ۝۱۲۱ اِنَّهُ هُوَ
 الْحَكِيْمُ الْعَلِيْمُ ۝۱۲۲

24. Je! Imekufikia hadithi ya wageni wa Ibrahim wanao-hishimiwa?

25. Walipoingia kwake wakasema: Salama! Na yeye akasema: Salama! Nyinyi ni watu nisio kujueni.

26. Akenda kwa ahali yake na akaja na ndama aliye-nona.

27. Akawakaribisha, aka-sema: Mbona hamli?

28. Akahisi kuwaogopa katika nafsi yake. Wakasema: Usiwe na khofu, nao wakambashiria kupata kijana mwenye ilimu.

29. Ndipo mkewe akawaelekea, na huku anasema na akijipiga usoni kwa mastaajabu, na kusema: Mimi ni kikongwe na tasa!

30. Wakasema: Ndivyo vivyo hivyo Alivyosema Mola Wako Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye Hikima na Mwenye Kujua.

Wageni wa Nabii Ibrahim عليه السلام

Tumeeleza habari hii hapo awali katika Surah Hud na Al-Hijr.¹ Allah تعالى Amesema,

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثٌ ضَيْفٍ إِتْرَاهِيمَ الْمُكْرَمِينَ ﴿١١﴾

“Je! Imekufikia hadithi ya wageni wa Ibrahim wanaohishimiwa?”

Ambao Ibrahim عليه السلام aliwakarimu na wao,

فَقَالُوا سَلَامًا قَالَ سَلَامٌ

“Wakasema: Salama! Na yeye akasema: Salama!”

وَإِذَا حُيِّتُمْ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا بِأَحْسَنَ مِنْهَا أَوْ رُدُّوهَا

“Na mnapo amkiwa kwa maamkio yoyote, basi nanyi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo.” (4:86)

Hivyo, Rafiki wa Allah تعالى alichagua jibu lililokuwa bora katika kuitikia salamu yao, kwa kutekeleza amri ya Allah تعالى : Kuitikia maamkizi. Malaika watatu; Jibril عليه السلام, Mika'il عليه السلام na Israfil عليه السلام walikuja kwa Ibrahim عليه السلام wakiwa katika sura za vijana wazuri, wanaadamu wazuri sana. Ndiyo sababu iliyompelekea Ibrahim عليه السلام kusema,

قَوْمٌ مُنْكَرُونَ

“Ni watu nisiokujueni.”

¹ Angalia, Tafsiri ya Surat Hud (11:69) na Tafsiri ya Surat Al-Hijr (15:51).

Allah تعالى Amesema,

فَرَاغَ إِلَىٰ أَهْلِهِ

“Akenda kwa ahali yake.”

Ibrahim عليه السلام aliingia ndani peke yake kwa haraka.

فَجَاءَ بِعَجَلٍ سَمِينٍ

“Na akaja na ndama aliyenona.”

Kutokana na aina bora zaidi ya chakula chake, na katika Aya nyingine kumeandikwa.

فَمَا لَبِثَ أَنْ جَاءَ بِعَجَلٍ حَيْنٍ ﴿٦٩﴾

“Hakukaa ila mara akaleta ndama wa kuchoma.” (11:69)

Maana yake: ilikuwa imebanikwa katika makaa ya moto.

فَقَرَّبَهُ إِلَىٰ آلِهِمْ

“Akawakaribisha.”

Aliwasogezea na akasema,

قَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ

“Mbona hamli?”

Ibrahim عليه السلام aliyasema hayo kwa upole na ukarimu kuwaambia wageni wake, na hakika, Ayah hii inaashiria tabia sahihi katika kuwakirimu wageni. Kwa ajili hiyo aliwaletea chakula wageni wake haraka, ilhali wao walikuwa hawatambui kuwa kilikuwa kikiandaliwa kwa ajili yao, hakuanza kuwatajia fadhila hii kabla kwa kusema, “Tutakuandalieni chakula.” Bali, kisirisiri, kilitayarishwa na kikawekwa mbele yao.

Aliandaa chakula bora kabisa alichokuwa nacho, ndama mdogo mnene aliyeokwa.

Hakukiweka chakula mbali nao na kuwaalika wakiendee. Bali, alikiweka karibu yao ili kukwepa jambo la wao kukataa kula. Badala yake aliwakaribisha kwa heshima.

أَلَا تَأْكُلُونَ

“Mbona hamli?”

Kauli hii inalingana na mmojawapo miongoni mwenu kumuambia mgeni wake, “Tafadhali kwa ukarimu wako unaweza kufanya kitu kadha wa kadha.”

Allah تعالی Amesema,

فَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً ط

“Akahisi kuwaogopa katika nafsi yake.”

Aya hii imeelezwa na Kauli ya Allah تعالی,

فَلَمَّا رَأَىٰ أَيْدِيَهُمْ لَا تَصِلُ إِلَيْهِ نَكِرَهُمْ وَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً قَالُوا لَا تَخَفْ إِنَّا أُرْسِلْنَا
إِلَىٰ قَوْمٍ لُّوطٍ ﴿٥١﴾ وَأَمْرُهُمْ قَائِمَةٌ فَضَحِكْتِ

“Basi alipoona mikono yao haifikilii aliwatilia shaka, na akawaogopa. Wakasema: Usiogope! Hakika sisi tumetumwa kwa kaumu ya Lut’. Na mkewe alikuwa kasimama wima, akacheka. Basi tukambashiria (kuzaliwa) Is-haq, na baada ya Is-haq Yaaqub.” (11:70-71),

Maana yake: Alifurahi kuwa watu wa Lut عليه السلام wanaangamizwa kwa sababu ya uasi wao kwa Allah تعالی. Haya ni pindi Malaika walipompa bishara ya kupata mwana, Is-haq عليه السلام; na Ya’qub عليه السلام baada ya Is-haq عليه السلام,

قَالَتْ يَنْوِيْلَتِي ۗ أَلِدُ وَأَنَا عَجُوزٌ وَهَذَا بَعْلِي شَيْخًا ۗ إِنَّ هَذَا لَشَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٥٢﴾ قَالُوا
أَتَعْجَبِينَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ ۗ رَحِمْتُ اللَّهُ وَبَرَكَتُهُ ۗ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ ۗ إِنَّهُ حَمِيدٌ مَّجِيدٌ ﴿٥٣﴾

“Akasema: Je, hivyo mimi nizae, na hali kuwa ni kikongwe na huyu mume wangu ni kizee? Hakika haya ni mambo ya ajabu! Wakasema: Je, unastaajabia Amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye Ndiye Msifiwa wa kutukuzwa.” (11:72-73)

Allah تعالى Amesema hapa;

وَنَشْرُوهُ بِغُلْمٍ عَلِيمٍ

“Na wakambashiria kupata kijana mwenye ilimu.”

Habari hizi zilikuwa nzuri kwa Ibrahim عليه السلام kwa kuwa zilimhusu mkewe, kwa hivyo, mtoto angekuwa wao na wao wote wawili walikuwa wakipewa bishara hiyo. Allah تعالى Amesema,

فَأَقْبَلَتِ امْرَأَتُهُ فِي صَرَافٍ

“Ndipo mkewe akawaelekea, na huku anasema.”

Alipiga kelele, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas, Mujahid, ‘Ikrimah, Abu Swalih, Adh-Dhahhak, Zayd bin Aslam, Ath-Thawri na As-Suddi رضي الله عنهم.¹ Akasema ile ilikuwa kauli yake,

يَا وَيْلَتَى

“Ee Ole wangu!” (25:28)

Kisha,

فَصَكَّتْ وَجْهَهَا

“Na akijipiga usoni kwa mastaajabu.”

‘Alijipiga katika paji lake la uso, kwa mujibu wa Mujahid na Ibn Saabit.² Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa alijipiga usoni kwake wanawake wafanyavyo pindi wanapozongwa na jambo la kushangaza.³

وَقَالَتْ عَجُوزٌ عَقِيمٌ

“Na kusema: Mimi ni kikongwe na tasa!”

“Nawezaje kuzaa ilhali mimi ni kikongwe na hata nilipokuwa msichana nilikuwa tasa na sikuweza kuzaa.”

¹ At-Tabari 22:426 na Al-Qurtubi 17:46.

² At-Tabari 22:428.

³ At-Tabari 22:427.

قَالُوا كَذَلِكَ قَالَ رَبُّكَ إِنَّهُ هُوَ الْحَكِيمُ الْعَلِيمُ ﴿٦٠﴾

“Wakasema: Ndivyo vivyohivyo Alivyosema Mola Wako Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye Hikima na Mwenye Kujua”

‘Yeye Ndiye Mjuzi zaidi wa heshima unayostahiki na Yeye ni Mwingi wa Hikima katika kauli na hukumu Zake.’

* قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ أَيُّهَا الْمُرْسَلُونَ ﴿٥٩﴾ قَالُوا إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ ﴿٦٠﴾ لِنُرْسِلَ عَلَيْهِمْ حِجَابًا مِّنَ طِينٍ ﴿٦١﴾ مُّسَوَّمَةً عِندَ رَبِّكَ لِلْمُسْرِفِينَ ﴿٦٢﴾ فَأَخْرَجْنَا مَن كَانَ فِيهَا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٣﴾ فَمَا وَجَدْنَا فِيهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِّنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٦٤﴾ وَتَرَكْنَا فِيهَا آيَةً لِلَّذِينَ يَخَافُونَ الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٦٥﴾

31. Akasema: Basi ujumbe wenu ni nini, enyi mliotumwa?

32. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwa watu waovu.

33. Tuwatupie mawe ya udongo.

34. Yaliyotiwa alama kutoka kwa Mola Wako Mlezi kwa ajili ya wanaopindukia mipaka.

35. kwa hivyo Tukawatoa katika hao wale walioamini.

36. Lakini hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu!

37. Na Tukaacha humo Ishara kwa ajili ya wanaoigopa adhabu chungu.

Malaika Walipelekwa Kuangamiza Kaumu ya Nabii Lut عليه السلام

Allah تعالى Amesema kumhusu Ibrahim عليه السلام

فَلَمَّا ذَهَبَ عَن إِبْرَاهِيمَ الرَّوْعُ وَجَاءَتْهُ الْبُشْرَىٰ مُجْتَدِلًا فِي قَوْمٍ لُّوطٍ ﴿٦٦﴾ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَحَلِيمٌ أَوَّهٌ مُّنِيبٌ ﴿٦٧﴾ يَتْلُو آيَاتِهِمْ فَأَخْرَجْنَا إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَهَارُونَ ﴿٦٨﴾ فَجَاءَ أَمْرُ رَبِّكَ ﴿٦٩﴾ وَإِنَّمَا آتَيْنَاهُمُ عَذَابَ غَيْرِ مَرْدُودٍ ﴿٧٠﴾

“Basi khofu ilipomuondoka Ibrahim, na ikawa ile bishara imemfikia, alianza kujadiliana nasi juu ya kaumu ya Lut’. Hakika Ibrahim alikuwa mpole, ana huruma, na mwepesi wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu. (Akaambiwa): Ewe Ibrahim! Wachilia mbali haya! kwa hakika Amri ya Mola Wako Mlezi imekwisha kuja, na hakika hao itawafikia adhabu isiyorudi nyuma.” (11:74-76)

Allah تعالى Amesema:

قَالَ فَمَا حَطْبُكُمْ أَيُّهَا الْمُرْسَلُونَ ﴿٧٤﴾

“Akasema: Basi ujumbe wenu ni nini, enyi mliotumwa?”

‘Ni ujumbe gani mliotumwa kuupeleka?’

قَالُوا إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ ﴿٧٥﴾

“Wakasema: Hakika sisi Tumetumwa kwa watu wakosefu”

Maana: Kaumu ya Lut عليه السلام,

لُرْسِلَ عَلَيْهِمْ حِجَارَةٌ مِّن طِينٍ ﴿٧٦﴾ مُسَوَّمَةٌ

“Tuwatupie mawe ya udongo Yaliyotiwa alama.”

Au yameandikwa,

عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُسْرِفِينَ

“Kutoka kwa Mola Wako Mlezi kwa ajili ya wanao pindukia mipaka.”

Majina yao yameandikwa kwa Allah تعالى; kila jiwe likiwa na jina la sahibu wake. Allah تعالى Amesema katika Surat Al-Ankabut,

قَالَ إِنَّ فِيهَا لُوطًا قَالُوا نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَنْ فِيهَا لَنَنْجِيَنَّهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا أُمَّرَأَتَهُ كَانَتْ

مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٧٧﴾

“Akasema: Hakika humo yumo Lut’i. Wao wakasema: Sisi Tunajua zaidi nani yumo humo. Hapana shaka Tutamuokoa yeye na ahali wake, isipokuwa mkewe aliye miongoni mwa wataokaa nyuma.” (29:32),

Na amesema katika Aya hii,

فَأَخْرَجْنَا مَنْ كَانَ فِيهَا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

“Kwa hivyo Tutawatoa katika hao wale walioamini.”

Wao ni: Lut عليه السلام na familia yake, isipokuwa mkewe,

فَمَا وَجَدْنَا فِيهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٢٥﴾

“Lakini hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu!”

Allah تعالى Amesema,

وَتَرَكْنَا فِيهَا آيَةً لِلَّذِينَ يَخَافُونَ الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٢٦﴾

“Na Tukaacha humo Ishara kwa ajili ya wanaoiogopa adhabu chungu.”

‘Tumeacha ushahidi wa adhabu, mateso na mawe yaliyotengenezwa kwa *Sijjil* (udongo uliochomwa moto). Tuliowapelekea juu yao; Tuliyaifanya makazi yao kuwa eneo lililovunda, baya, bahari iliyokufa, ili liwe fundisho kwa waumini.’

لِلَّذِينَ يَخَافُونَ الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٢٦﴾

“Kwa ajili ya wanaoiogopa adhabu chungu”

وَفِي مُوسَى إِذْ أَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ بِسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٢٧﴾ فَتَوَلَّىٰ بِرُكْبَيْهِ ۖ وَقَالَ سَاحِرٌ أَوْ

مَجْنُونٌ ﴿٢٨﴾ فَأَخَذْتُهُ وَجُنُودَهُ فَنَبَذْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ وَهُوَ مُلِيمٌ ﴿٢٩﴾ وَفِي عَادٍ إِذْ أَرْسَلْنَا

عَلَيْهِمُ الرِّيحَ الْعَقِيمَ ﴿٣٠﴾ مَا تَذُرُّ مِنْ شَيْءٍ أَنْتَ عَلَيْهِ إِلَّا جَعَلْتَهُ كَالرِّيمِ ﴿٣١﴾ وَفِي

نَمُودٍ إِذْ قِيلَ لَهُمْ تَمَتَّعُوا حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٣٢﴾ فَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ فَأَخَذَتْهُمُ الصَّيْقَةُ وَهُمْ

يَنْظُرُونَ ﴿٣٣﴾ فَمَا اسْتَطَبُّعُوا مِنْ قِيَامٍ وَمَا كَانُوا مُنْتَصِرِينَ ﴿٣٤﴾ وَقَوْمَ نوحٍ مِّن قَبْلُ ۗ

إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَسِقِينَ ﴿٣٥﴾

38. Na katika habari za Musa. Tulipomtuma kwa Firauni na hoja wazi.

39. Lakini alipuuza kwa sababu ya nguvu zake na akasema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu!

40. Basi Tukamkamata yeye na majeshi yake na Tukawatupa baharini, na yeye ndiye wa kulaumiwa.

41. Na katika habari za A'di Tulipowapelekea upepo wa kukata uzazi.

42. Haukuacha chochote ulichokifikia ila ulikifanya kama kilicho chakaa na kuangamia.

43. Na katika habari za Thamudi walipoambiwa: Jifurahisheni kwa muda mdogo tu.

44. Wakaasi amri ya Mola wao Mlezi. Basi uliwanyakua roho zao moto wa radi nao wanaona.

45. Basi hawakuweza kusimama wala hawakuwa wenye kujitetea.

46. Na kaumu ya Nuhu hapo mbele. Hakika hao walikuwa watu wapotovu.

Mafundisho na Mazingatio Kutokana na Kuangamizwa kwa Firauni, 'Ad, Thamud, na Kaumu ya Nuh عليه السلام

Allah تعالى Amesema,

وَفِي مُوسَىٰ إِذْ أَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ بِسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٢٤﴾

“Na katika habari za Musa. Tulipomtuma kwa Firauni na hoja za wazi.”

Maana yake: Na dalili dhahiri na ushahidi wa waziwazi,

فَتَوَلَّىٰ بِرُكْبٰهٖ

“Lakini alipuuza kwa sababu ya nguvu zake...”

Maana yake: Katika uasi na kiburi, Fir'auni aliupinga ukweli dhahiri aliotumwa nao Musa,

ثَانِي عَطْفِهِ لِيُضِلَّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ^ط

“Anayegeuza shingo yake ili kupoteza watu waache Njia ya Mwenyezi Mungu.” (22:9),

Maana yake: Kuukimbia ukweli kutokana na kiburi.

وَقَالَ سَلْحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ

“Huyu ni mchawi au mwendawazimu!”

Maana yake: Fir’auni alimuambia Musa عليه السلام, “Kuhusu ujumbe ulioniletea, wewe, ama ni mchawi au mwendawazimu.” Allah تعالى Akajibu,

فَأَخَذْنَاهُ وَجُنُودَهُ فَنَبَذْنَاهُمْ

“Basi Tukamkamata yeye na majeshi yake na Tukawatupa...”

Maana yake: ‘Tuliwavurumiza.’

فِي الْيَمِّ

“Baharini, (katika Yamm)”,

Baharini,

وَهُوَ مُلِيمٌ

“Na yeye ndiye wa kulaumiwa.”

Maana yake Fir’auni alikuwa mkanaji mwenye dhambi na kafiri mkaidi mwenye kulaumiwa, Allah تعالى Amesema,

وَفِي عَادٍ إِذْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الرِّيحَ الْعَقِيمَ ﴿٥١﴾

“Na katika habari za A’di Tulipowapelekea upepo wa kuhilikisha ukoo.”

Unaoharibu kila kitu na hauzalishi kitu chochote. Haya yalisemwa na Adh-Dhahhak, Qatadah na wengine.¹ Kauli ya Allah تعالى,

¹ At-Tabari 22:434

مَا تَذُرُّ مِنْ شَيْءٍ أَتَتْ عَلَيْهِ

“Haukuacha chochote ulichokifikia...”

Maana yake: Kila kitu ambacho upepo uliweza kukiharibu.

إِلَّا جَعَلْتُهُ كَأَلْرَمِيمِ

“Ila ulikifanya kama kilionyambuka.”

Maana yake: Ukakifanya kama kitu kilichooza na kuhiliki. Sa'id bin Al-Musayyab na wengine walitoa rai juu ya:

إِذْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الرِّيحَ الْعَقِيمَ

“Tulipowapelekea upepo wa kukata uzazi.”

“Pepo za kusi.”¹ Hata hivyo, kuna Hadithi katika Sahih kutoka kwa Shu'bah bin Al-Hakam, kutoka kwa Mujahid, kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, ambaye alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«نُصِرْتُ بِالصَّبَا وَأُهْلِكْتُ عَادًا بِالدُّبْرِ»

“Nimepewa ushindi kwa Saba (upepo utokao mashariki), na watu wa 'Ad walihilikishwa kwa Dabur (upepo uvumao toka magharibi).”²

Kauli ya Allah تعالى،

وَفِي نَمُودٍ إِذْ قِيلَ لَهُمْ تَمَتَّعُوا حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٥١﴾

“Na katika habari za Thamudi walipoambiwa: Jifurahisheni kwa muda mdogo tu.”

Ni sawa na Kauli Yake katika Aya nyingine,

وَأَمَّا نَمُودٌ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمَىٰ عَلَىٰ الْهُدَىٰ فَأَخَذَتْهُمُ صَاعِقَةُ الْعَذَابِ الْهُونِ بِمَا

كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٥٢﴾

¹ At-Tabari 22:433

² Fat'h Al-Bari 2:604 na Muslim 2:617

“Na ama Thamudi Tuliwaongoza. Lakini walipenda upofu kuliko uwongofu. Basi uliwachukua moto wa adhabu ya kuwafedhehesha kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.” (41:17)

Allah تعالى Amesema hapa,

وَفِي ثَمُودَ إِذْ قِيلَ لَهُمْ تَمَتَّعُوا حَتَّىٰ حِينٍ ﴿١٦﴾ فَعْتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ فَأَخَذَتْهُمُ الصَّاعِقَةُ
وَهُمْ يَنْظُرُونَ ﴿١٧﴾

“Na katika habari za Thamudi walipoambiwa: Jifurahisheni kwa muda mdogo tu. Wakaasi amri ya Mola wao Mlezi. Basi uliwanyakua moto wa radi nao wanaona.”

Thamud walipewa muda wa siku tatu, ambapo walingojea adhabu. Katika asubuhi ya siku ya nne, adhabu ikawajia.

فَمَا اسْتَطَبُّعُوا مِنْ قِيَامٍ

“Basi hawakuweza kusimama.”

Hawakuweza kutoroka na kuikimbia,

وَمَا كَانُوا مُنْتَصِرِينَ

“Wala hawakuwa wenye kujitetea.”

Wala hawa kumudu kujiokoa dhidi ya adhabu iliyowaangukia. Allah تعالى Amesema,

وَقَوْمَ نُوحٍ مِّن قَبْلُ ۗ

“Na kaumu ya Nuhu hapo mbele...”

Maana yake: ‘Tulia ngamiza kaumu ya Nuh عليه السلام kabla ya watu hawa (Fir’auni, ‘Ad na Thamud).’

إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَاسِقِينَ

“Hakika hao walikuwa watu wapotovu.”

Maelezo haya yametajwa katika maelezo ya tafsiri za Sura kadha.

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا بِأَيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ ﴿٤٧﴾ وَالْأَرْضَ
 فَرَشْنَاهَا فَنِعْمَ الْمَاهِدُونَ ﴿٤٨﴾ وَمِن كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا
 زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٤٩﴾ فَفِرُّوا إِلَى اللَّهِ إِنِّي لَكَرِمَةٌ
 نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥٠﴾ وَلَا تَجْعَلُوا مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ إِنِّي لَكَرِمٌ
 مِنَّهُ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥١﴾ كَذَلِكَ مَا أَتَى الَّذِينَ مِن قَبْلِهِم مِّن
 رَّسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ ﴿٥٢﴾ أَتَوَاصَوْا بِهِ ؕ بَلْ
 هُمْ قَوْمٌ طَآغُونَ ﴿٥٣﴾ فَتَوَلَّ عَنْهُمْ فَمَا أَنت بِمَلُومٍ ﴿٥٤﴾
 وَذَكَرْ فَإِنَّ الذِّكْرَى تَنفَعُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٥﴾ وَمَا خَلَقْتُ
 الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾ مَا أُرِيدُ مِنْهُمْ مِن رِزْقٍ
 وَمَا أُرِيدُ أَنْ يُطْعَمُوا ﴿٥٧﴾ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ
 الْعَمِيمِ ﴿٥٨﴾ فَإِنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُنُوبًا مِّثْلَ ذُنُوبِ أَصْحَابِهِمْ
 فَلَا يَسْتَعْجِلُونَ ﴿٥٩﴾ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِن يَوْمِهِمُ
 الَّذِي يُوْعَدُونَ ﴿٦٠﴾

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا بِأَيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ
 ﴿٤٧﴾ وَالْأَرْضَ فَرَشْنَاهَا فَنِعْمَ
 الْمَاهِدُونَ ﴿٤٨﴾ وَمِن كُلِّ شَيْءٍ
 خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٤٩﴾
 فَفِرُّوا إِلَى اللَّهِ إِنِّي لَكَرِمَةٌ
 نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥٠﴾ وَلَا تَجْعَلُوا مَعَ اللَّهِ
 إِلَهًا آخَرَ ﴿٥١﴾ كَذَلِكَ مَا أَتَى الَّذِينَ
 مِن قَبْلِهِم مِّن رَّسُولٍ إِلَّا قَالُوا
 سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ ﴿٥٢﴾ أَتَوَاصَوْا
 بِهِ ؕ بَلْ هُمْ قَوْمٌ طَآغُونَ ﴿٥٣﴾
 فَتَوَلَّ عَنْهُمْ فَمَا أَنت بِمَلُومٍ ﴿٥٤﴾
 وَذَكَرْ فَإِنَّ الذِّكْرَى تَنفَعُ الْمُؤْمِنِينَ
 ﴿٥٥﴾ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ
 إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾ مَا أُرِيدُ مِنْهُمْ
 مِن رِزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَنْ يُطْعَمُوا
 ﴿٥٧﴾ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو
 الْقُوَّةِ الْعَمِيمِ ﴿٥٨﴾ فَإِنَّ لِلَّذِينَ
 ظَلَمُوا ذُنُوبًا مِّثْلَ ذُنُوبِ أَصْحَابِهِمْ
 فَلَا يَسْتَعْجِلُونَ ﴿٥٩﴾ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ
 كَفَرُوا مِن يَوْمِهِمُ الَّذِي يُوْعَدُونَ
 ﴿٦٠﴾

47. Na mbingu Tumezifanya kwa Nguvu na Uweza na hakika Sisi bila ya shaka ndio wenye Uweza wa Kuzitanua.

48. Na ardhi Tumeitandaza; basi watandazaji wazuri namna gani Sisi!

49. Na katika kila kitu Tumeumba dume na jike na

vinyume vyake ili mpate kuzingatia.

50. Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu, hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae kwake.

51. Wala msijaalie mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu. Hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae Kwake.

Ushahidi wa Upweke wa Allah ﷻ Umo Katika Kuumbwa kwa Mbingu na Ardhi na Uumbaji wa Kila Kitu Aina Mbili.

Allah ﷻ Anatumkumbusha juu ya Kuumbwa kwa ulimwengu wa juu na wa chini,

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا

“Na mbingu Tumeijenga...”

Maana yake: ‘Tumeifanya kama dari iliyozuiliwa isianguke.’

بِأَيْدِي

“Kwa Nguvu na Uweza.”

Maana yake: Kwa Kawi, Satua, Mamlaka, Fosi na Amri, kwa mujibu wa ‘Abdullah bin ‘Abbas, Mujahid, Qatadah, Ath-Thawri na wengine,¹

وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ

“Na hakika Sisi bila ya shaka ndio wenye Uweza wa Kuzitanua.”

Maana yake: ‘Tumeikunjua na Tukainyanyua dari yake juu pasi na nguzo za kutegemeza, hivyo zinaning’inia zenyewe tu.’

وَالْأَرْضَ فَرَشْنَاهَا

“Na ardhi Tumeitandaza.”

Maana yake: ‘Tumeifanya kuwa mahali pa kupumzika kwa ajili ya viumbe.’

فَنِعْمَ الْمُنْهَدُونَ

“Basi watandazaji wazuri namna gani Sisi!”

Maana yake: ‘Tumeitandaza kwa ajili ya wakazi wake.’

وَمِنْ كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ

“Na katika kila kitu Tumeumba kwa jozi.”

¹ At-Tabari 22:438

Maana yake: Viumbe wote wako katika jozi, mbingu na ardhi, usiku na mchana, jua na mwezi, nchi na bahari, nuru na kiza, imani na ukafiri, kifo na uhai, taabu na furaha, Pepo na Moto, hadi wanyama na mimea. Kauli ya Allah تعالى

لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

“Ili mzingatie.”

Na ujue kuwa, Muumbaji, Allah تعالى, ni Mmoja, asiye na washirika.

فَفِرُّوا إِلَى اللَّهِ^ط

“Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Tafuteni Kwake hifadhi na salama juu ya mambo yenu.

إِنِّي لَكُمْ مِّنْهُ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥١﴾ وَلَا تَجْعَلُوا مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ^ط

**“Hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae Kwake.
Wala msijaalie mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu.”**

Msimshirikishe na chochote,

إِنِّي لَكُمْ مِّنْهُ نَذِيرٌ مُّبِينٌ

“Hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae Kwake.”

كَذَلِكَ مَا آتَى الَّذِينَ مِن قَبْلِهِم مِّن رَّسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ ﴿٥٢﴾ أَتَوَاصَوْا بِهِمْ^ع
بَلْ هُمْ قَوْمٌ طَآغُونَ ﴿٥٣﴾ فَتَوَلَّوْا عَنْهُمْ فَمَا أَنْتَ بِمَلْمُومٍ ﴿٥٤﴾ وَذَكَرْنَا لَكَ الذِّكْرَىٰ تَنْفَعُ
الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٥﴾ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾ مَا أُرِيدُ مِنْهُمْ مِن رِّزْقٍ
وَمَا أُرِيدُ أَنْ يُطْعَمُوا ﴿٥٧﴾ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ ﴿٥٨﴾ فَإِنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا
ذُنُوبًا مِّثْلَ ذُنُوبِ أَصْحَابِهِمْ فَلَا يَسْتَعْجِلُونَ ﴿٥٩﴾ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِن يَوْمِهِمُ الَّذِي
يُوعَدُونَ ﴿٦٠﴾

52. Basi ndio hivyo hivyo, hakuwajia kabla yao Mtume ila walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu.

53. Je! Wameambizana kwa haya? Bali hawa ni watu waliovuka mpaka wa waasi.

54. Basi waachilie mbali, nawe hutalaumiwa.

55. Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa Waumini.

56. Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.

57. Na sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishe.

58. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kuruzuku, Mwenye Nguvu, Madhubuti.

59. Hakika waliodhulumu wana fungu lao la adhabu kama fungu la wenzao. Basi wasinihimize.

60. Kuangamia ni kwa wale walioikanusha siku yao waliyoahidiwa.

Mitume Wote Walipingwa na Mataifa Yao

Allah تعالى Anamfariji Mtume Wake ﷺ kwa kumuambia, 'kama walivyokukataa hawa washirikina, makafiri wa zamani nao walitumia maneno sawa na hayo kuwaambia Mitume wao.'

كَذَلِكَ مَا أَتَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مُجْنُونٌ ﴿٥١﴾

"Basi ndio hivyo hivyo, hakuwajia kabla yao Mtume ila walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu."

Allah تعالى Amesema,

أَتَوَصَّوْا بِهِمْ

"Je! Wameambizana kwa haya?"

Maana yake: Kwani hao wa zamani wamewafundisha haya hawa wa sasa?

بَلْ هُمْ قَوْمٌ طَآغُونَ

"Bali hawa ni watu waasi."

Wao ni madhalimu ambao nyoyo zao zinalingana. Kwa hivyo, hawa leo wamesema sawa na yaliyosemwa na wa kabla yao. Allah تعالى Amesema,

فَقَوْلٌ عَنَّهُمْ

“Basi waachilie mbali.”

Maana yake: ‘Ewe Muhammad ﷺ, achana nao washirikina wa Kikuraishi,’

فَمَا أَنْتَ بِمَلُومٍ

“Nawe hulaumiwi.”

Maana yake: ‘Hatutakulaumu ikiwa utawapa kisogo.’

وَذَكِّرْ فَإِنَّ الذِّكْرَى تَنْفَعُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥١﴾

“Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa Waumini.”

Maana yake: Manufaa ni kwa ajili ya nyoyo zenye kuamini tu.

Allah تعالى Ndiye Aliyewaumba Wanaadamu na Majini ili Wamuabudu Yeye tu.

Allah تعالى Amesema,

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٢﴾

“Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.”

Maana yake: ‘Mimi, Allah تعالى, Ndimi Pekee Niliyewaumba ili waniabudu Mimi, si kuwa Nina haja nao.’ ‘Ali bin Abu Talhah amesimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alitoa rai juu ya Aya hii,

إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٢﴾

“ila waniabudu Mimi.” Maana yake: “Ili waniabudu, kwa hiyari au kwa nguvu.”

Allah تعالى Amesema,

مَا أُرِيدُ مِنْهُمْ مِنْ رِزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَنْ يُطْعَمُونِ ﴿٥٣﴾ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ ﴿٥٤﴾

“Na Sitaki kwao riziki, wala Sitaki wanilishe. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kuruzuku, Mwenye Nguvu, Madhubuti.”

Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ alifundisha yafuatayo:

(إِنِّي أَنَا الرَّزَاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينِ)

“Hakika, Mimi Ndimi Mpaji, Mwenye Nguvu Sana.”¹

Abu Dawud, At-Tirmidhi na An-Nasa'i nao waliikusanya Hadithi hii. At-Tirmidhi amesema, “Hasan Sahih.”² Maana ya Aya hii (51:56) ni kuwa, Allah تعالى, Aliwaumba viumbe ili wamuabudu Yeye Peke Yake pasi na washirika. Wale wanaomuabudu watapata ujira mzuri, ilhali wasiomtii watapata adhabu kali kutoka Kwake. Allah تعالى Alieleza kuwa Hana haja na viumbe, lakini kinyume chake, wao ni wenye kumhitaji katika hali zote. Yeye ni Mpweke, Muumba wao na Mpaji. Imamu Ahmad amenukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«قَالَ اللهُ تَعَالَى: يَا ابْنَ آدَمَ تَفَرَّغْ لِعِبَادَتِي أَمَلًا صَدْرَكَ غِنَى وَأَسَدُ فَقْرَكَ، وَإِلَّا تَفَعَّلْ، مَلَأْتُ صَدْرَكَ شُغْلًا وَلَمْ أَسَدُ فَقْرَكَ»

*“Allah Mtukufu Amesema, ‘Ewe mwanaadamu! Jishughulishe na kuniabudu, Nitakijaza kifua chako utajiri na Kuuondoa ufakiri wako. Vinginevyo, Nitakijaza kifua chako mambo ya kuhangaisha na wala Nisiuondoe ufakiri wako.”*³

At-Tirmidhi na Ibn Majah wameikusanya Hadithi hii na At-Tirmidhi alisema, “Hasan Gharib.”⁴ Kauli ya Allah تعالى,

فَإِنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُنُوبًا

“Hakika waliodhulumu wana fungu lao la adhabu.”

Inajulisha kuwa watapokea adhabu yao.

¹ Ahmad 418

² Abu Dawud 4:290, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:261 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:469

³ Ahmad 2:358

⁴ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 7:166 na *Ibn Majah* 2:1376

مِثْلَ ذُنُوبِ أَصْحَابِهِمْ فَلَا يَسْتَعْجِلُونَ

“Kama fungu la wenzao. Basi wasinihimize.”

Waache kuomba kuharakishiwa adhabu hiyo, kwani, kwa hakika, itakuja.

فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ يَوْمِهِمُ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿٦٠﴾

“Kuangamia ni kwa wale walioikanusha siku yao waliyoahidiwa.”

Maana yake: Siku ya Ufufuo.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Adh-Dhariyat*; Sifa zote Njema ni za Allah تعالى na Fadhila zote ni kutoka Kwake, Peke Yake.

* * *

Tafsiri ya Suratu At-Tur Sura ya 52 Iliteremshwa Makkah

Fadhila za *Suratu At-Tur*

Malik رضي الله عنه amesimulia kuwa Jubayr bin Mut'im رضي الله عنه amesema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akisoma *Surat At-Tur* akiwa katika Sala ya Magharibi. Hakika, sikuwahi kusikia sauti nzuri zaidi au kisomo kizuri kama cha usomaji wake."¹ Hadithi hii imeandikwa katika Sahih Mbili kwa njia ya Malik.² Al-Bukhari alinukuu kuwa Ummu Salamah رضي الله عنها amesema, "Nilishitakia kuumwa kwangu mbele ya Mtume ﷺ, akasema,

«طُوفِي مِنْ وَرَاءِ النَّاسِ وَأَنْتِ رَاجِيَةٌ»

"Tufu (zunguka Ka'bah) nyuma ya watu hali ya kuwa uko juu ya mnyama."

Kwa hivyo, nilitufu na wakati huo Mtume ﷺ akiwa anasali kando ya Ka'aba, huku anasoma At-Tur.³

* * *

¹ *Al-Muwatta* 1:78

² *Fat'h Al-Bari* 2:289 na *Muslim* 1:338

³ *Fat'h Al-Bari* 8:468

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

سُورَةُ الطُّورِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالطُّورِ ۝ وَكِتَابٍ مُّسْتَوِرٍ ۝ فِي رَقٍ مَّنشُورٍ ۝
 وَاللَّبَّيَّتِ الْمَعْمُورِ ۝ وَالسَّقْفِ الْمَرْفُوعِ ۝ وَالْبَحْرِ الْمَسْجُورِ ۝ إِنَّ
 عَذَابَ رَبِّكَ لَوَاقِعٌ ۝ مَا لَهُ مِنْ دَافِعٍ ۝ يَوْمَ تَمُورُ السَّمَاءُ مَوْرًا ۝
 وَتَسِيرُ الْجِبَالُ سَيْرًا ۝ فَوَيْلٌ لِلْمُكذِّبِينَ ۝ الَّذِينَ هُمْ فِي
 خَوْضٍ يَلْعَبُونَ ۝ يَوْمَ يُدْعَوْنَ إِلَى نَارٍ جَهَنَّمَ دَعَاً ۝
 هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكذِّبُونَ ۝ أَفَسِحْرٌ هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تُبْصِرُونَ ۝ أَصَلَوْهَا فَاصْبِرُوا أَوْ لَا
 تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ ۝ إِنَّمَا تُحْزَنُونَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ۝
 إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَنَعِيمٍ ۝ فَنَكِهِينَ بِمَا آتَاهُمْ
 رِزْقَهُمْ وَوَقَّهْتُمْ رَهُمَ عَذَابِ الْجَحِيمِ ۝ كُلُوا وَاشْرَبُوا
 هَيْهَاتَ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ۝ مُتَّكِئِينَ عَلَى سُرُرٍ مَّصْفُوفَةٍ
 وَزَوَّجْنَاهُمْ بِحُورٍ عِينٍ ۝

وَالطُّورِ ۝ وَكِتَابٍ مُّسْتَوِرٍ ۝ فِي رَقٍ مَّنشُورٍ ۝ وَاللَّبَّيَّتِ
 الْمَعْمُورِ ۝ وَالسَّقْفِ الْمَرْفُوعِ ۝ وَالْبَحْرِ الْمَسْجُورِ ۝ إِنَّ
 عَذَابَ رَبِّكَ لَوَاقِعٌ ۝ مَا لَهُ مِنْ دَافِعٍ ۝ يَوْمَ تَمُورُ السَّمَاءُ مَوْرًا
 وَتَسِيرُ الْجِبَالُ سَيْرًا ۝ فَوَيْلٌ لِلْمُكذِّبِينَ ۝ الَّذِينَ
 هُمْ فِي خَوْضٍ يَلْعَبُونَ ۝ يَوْمَ يُدْعَوْنَ إِلَى نَارٍ جَهَنَّمَ دَعَاً
 هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكذِّبُونَ ۝ أَفَسِحْرٌ هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا
 تُبْصِرُونَ ۝ أَصَلَوْهَا فَاصْبِرُوا أَوْ لَا تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ ۝
 إِنَّمَا تُحْزَنُونَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ۝

1. Naapa kwa mlima wa T'ur.

2. Na Kitabu kilichoandikwa.

3. *Katika karatasi ya ngozi iliyokunjuliwa.*
4. *Na kwa Nyumba iliyojengwa.*
5. *Na kwa Mbingu iliyonyanyuliwa.*
6. *Na kwa bahari iliyojazwa.*
7. *Hakika adhabu ya Mola Wako Mlezi hapana shaka itatokea.*
8. *Hapana wa kuizuia.*
9. *Siku zitakapotikisika mbingu kwa mtikiso.*
10. *Na milima iwe inakwenda kwa mwendo mkubwa.*
11. *Basi adhabu kali siku hiyo itawapata hao wanaokadhibisha.*
12. *Ambao wanacheza katika mambo ya upuuzi.*
13. *Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu.*
14. *(Waambiwe): Huu ndio Moto ule mliokuwa mkiukanusha!.*
15. *Je! Huu ni uchawi, au hamuoni tu?.*
16. *Uingieni, mkistahamili au msistahamili - ni mamoja kwenu. Hakika mnalipwa kwa mliyokuwa mkiyatenda.*

Kiapo cha Allah تعالی Juu ya Kutokea Adhabu

Allah تعالی Anaapa kwa viumbe Wake, kama ni ushahidi wa Uweza Wake mkubwa, kuwa Adhabu Yake, kwa hakika itawaangukia maadui Wake; hawatakuwa na namna ya kuikwepa.

At-Tur ni mlima wenye miti, kama ule ambao Allah تعالی Alizungumza na Nabii Musa عليه السلام huku akiwa juu ya mlima huo, na mlima ambao Allah تعالی Alimpa Utume Nabii Isa عليه السلام. Mlima usio na miti yaani *Jabal*, hauitwi kwa jina la *Tur*. Allah تعالی Amesema:

وَكُنْتُمْ مَّسْطُورِينَ

“Na Kitabu kilichoandikwa.” Inamaanisha *Al-Lawh Al-Mahfudh*, pia amesema kuwa ina maana ya Kitabu Alichoteremsha Allah تعالی ili watu wakosome.

Na hii ndiyo sababu Allah تعالی Akasema,

فِي رَقِيٍّ مَّنْشُورٍ ﴿٦٦﴾ وَالْبَيْتِ الْمَعْمُورِ ﴿٦٧﴾

“Katika ngozi iliyokunjuliwa. Na kwa Nyumba iliyojengwa.”

Katika Sahih Mbili imethibitishwa kuwa Mtume ﷺ amesema katika Hadithi ya *Al-Isra'*, baada ya kupanda hadi mbingu ya saba:

«ثُمَّ رُفِعَ بِي إِلَى الْبَيْتِ الْمَعْمُورِ، وَإِذَا هُوَ يَدْخُلُهُ كُلُّ يَوْمٍ سَبْعُونَ أَلْفًا، لَا يَعُودُونَ إِلَيْهِ آخِرَ مَا عَلَيْهِمْ»

“Kisha nilinyanyuliwa hadi Al-Bayt Al-Ma'mur ambayo kila siku wanaingia Malaika elfu sabini ambao hawarejei hadi mwisho wa wajibu wao.”¹

Malaika wanamuabudu Allah تعالی katika *Al-Bayt Al-Ma'mur* na wanatufu kuizunguka kama watu wa ardhi wanavyotufu kuzunguka Ka'bah. *Al-Bayt Al-Ma'mur* ni Ka'bah ya wakazi wa mbingu ya saba. Wakati wa Safari ya *Isra'*, Mtume ﷺ alimuona Nabii Ibrahim *Al-Khalil* عليه السلام, ambaye alikuwa ameegemeza mgongo wake katika *Al-Bayt Al-Ma'mur*. Nabii Ibrahim عليه السلام ndiye aliyejenga Ka'bah ya duniani, na Hakika, malipo ni kutokana na jinsi ya amali ya mtu.

Al-Bayt Al-Ma'mur iko sambamba na Ka'bah; kila mbingu ina nyumba ambayo wakazi wake hufanyia ibada na ndicho kibla chao. Nyumba iliyo katika mbingu ya dunia inaitwa *Bayt Al-'Izzah*. na Allah تعالی Anajua zaidi. Kauli ya Allah تعالی,

وَالسَّقْفِ الْمَرْفُوعِ ﴿٦٨﴾

“Na kwa dari iliyonyanyuliwa.”

Sufyan Ath-Thawri, Shu'bah, na Abu Al-Ahwas, wote wamesimulia kutoka kwa Simak, kutoka kwa Khalid bin 'Ar'arah, kutoka kwa 'Ali bin Abu Talib رضي الله عنه:

وَالسَّقْفِ الْمَرْفُوعِ ﴿٦٨﴾

“Na kwa dari iliyonyanyuliwa.” Maana yake: “mbingu.” Sufyan aliongeza.

¹ *Fat'h Al-Bari* 6:349 na *Muslim* 1:50

Kisha 'Ali رضي الله عنه akasoma,

وَجَعَلْنَا السَّمَاءَ سَقْفًا مَحْفُوظًا ۖ وَهُمْ عَنْ آيَاتِهَا مُعْرَضُونَ ﴿٣٢﴾

“Na Tukaifanya mbingu kuwa dari iliyohifadhiwa, lakini wanazipuuza Ishara Zake.” (21:32)¹

Maelezo sawa na hayo yalisemwa na Mujahid, Qatadah, As-Suddi na Ibn Jurayj, Ibn Zayd na ameyakubali Ibn Jarir رحمه الله تعالى.² Kauli ya Allah تعالى،

وَالْبَحْرِ الْمَسْجُورِ ﴿٦٠﴾

“Na kwa bahari iliyojazwa.”

Wanazuoni wengi wamesema, inamaanisha bahari hii ya duniani. *Masjur*, maana yake, 'Bahari itawashwa moto Siku ya Kiama.'

Kama alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine،

وَإِذَا الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ﴿٦١﴾

“Na bahari zikawaka moto.” (81:6)

Maana yake: Itawashwa moto na utakuwa moto utakaowazunguka watu kuwapeleka katika eneo la kukusanyika. Haya yalisimuliwa na Sa'id bin Al-Musayyab kutoka kwa 'Ali bin Abu Talib رضي الله عنه.³ Pia yalisimuliwa kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما. Hii pia ni rai ya Sa'id bin Jubayr, Mujahid, 'Abdullah bin 'Ubayd bin 'Umayr na wengine. Qatadah amesema, “*Masjur* ni bahari iliyojazwa.” Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameyakubali maelezo haya kwa kusema, “Bahari haziwaki moto kwa sasa, kwa hivyo imejazwa.” Kauli ya Allah تعالى؛

إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ لَوَاقِعٌ ﴿٦٢﴾

“Hakika adhabu ya Mola Wako Mlezi hapana shaka itatokea.”

Hiki ndicho kinachoapiwa, Yaani hapana shaka adhabu itawafika makafiri, sawa na alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine؛

¹ At-Tabari 22:257-258.

² At-Tabari 22:458.

³ At-Tabari 22:58.

مَا لَهُ مِنْ دَافِعٍ ﴿٥٢﴾

“Hapana wa kuizuia.”

Ikiwa na maana kuwa, pindi Allah تعالى Anapoamua kupeleka adhabu juu yao hakuna wa kuizuia au kuisimamisha ili isiwapate. Al-Hafidh Abu Bakr Ibn Abu Ad-Dun'ya amenukuu kuwa Ja'far bin Zayd Al-'Abdi amesema, “Usiku mmoja, katika mji wa Madinah, ‘Umar رضي الله عنه alitoka kwenda kuchunguza hali za Waislamu, akapita katika nyumba ya mtu ambaye alikuwa amesimama akisali Sala ya Sunnah. ‘Umar رضي الله عنه akasimama kimya, akisikiliza kisomo chake; alikuwa akisoma:

وَالطُّورِ ﴿٥٢﴾

“Naapa kwa mlima wa Tur.” Mpaka alipoifikia Aya,

إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ لَوَاقِعٌ ﴿٥٢﴾ مَا لَهُ مِنْ دَافِعٍ ﴿٥٢﴾

“Hakika adhabu ya Mola Wako Mlezi hapana shaka itatokea. Hapana wa kuizuia.”

‘Umar رضي الله عنه amesema, ‘Naapa kwa Mola wa Ka’bah, hiki ni kiapo cha kweli.’ ‘Umar رضي الله عنه akateremka kutoka juu ya punda wake, akaketi jirani na ukuta kwa muda kidogo. Akarudi nyumbani kwake na akaugua kwa mwezi mzima. Wakati wa kuumwa kwake, watu walimzuru bila ya kujua sababu ya maradhi yake,” Allah تعالى Amuwie radhi Sayyidina Umar رضي الله عنه.¹

Maelezo ya Siku ya Adhabu, ambayo Ndio Siku ya Kiama

Allah تعالى Amesema;

يَوْمَ تَمُورُ السَّمَاءُ مَوْرًا ﴿٥٢﴾

“Siku zitakapotikisika mbingu kwa mtikiso.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na Qatadah wamesema: “Kutikisika kwa nguvu.”² Pia Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema, “Kupasuka.” Mujahid amesema: “itazunguka.” Adh-Dhahhak alisema, “Dunia itazunguuka na kutikisika kwa Amri ya Allah تعالى, na mawimbi yataingiliana yenyewe kwa yenyewe kwa nguvu.”³ Rai hii imekubaliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى, kuwa ni kutikisika katika mzunguko wake.”

¹ Ameitaja Mwandishi katika Musnadi wa Umar 2:608.

² At-Tabari 22:462.

³ At-Tabari 22:362.

Allah تعالیٰ Amesema,

وَدَسِيرُ الْجِبَالِ سَيْرًا ﴿١٠﴾

“Na milima iwe inakwenda kwa mwendo mkubwa.”

Itaondoka na kuwa chembechembe za vumbi zilizotawanyika na kupeperushwa na upepo,

فَوَيْلٌ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١١﴾

“Basi ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha.”

Ole wao Siku hiyo kutokana na adhabu ya Allah تعالیٰ na hilaki Atakayoielekeza kwao.

الَّذِينَ هُمْ فِي حَوْضٍ يَلْعَبُونَ ﴿١٢﴾

“Ambao wanacheza katika mambo ya upuuzi.”

Maana yake: Duniani wanazama katika batili na wanaifanyia dini yao dhihaka na mchezo,

يَوْمَ يَدْعُوبُ ﴿١٣﴾

“Siku wataposukumwa.”

Maana yake: Watakapokokotwa kwa nguvu na kusukumwa.

إِلَى نَارٍ جَهَنَّمَ دَعَا ﴿١٤﴾

“Kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu.”

Mujahid, Ash-Sha’bi, Muhammad bin Ka’b, Adh-Dhahhak, As-Suddi na Ath-Thawri wamesema kuwa maana ya Aya hii, “Watabimbirishwa humo kwa nguvu.”¹ Allah تعالیٰ Amesema,

هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿١٥﴾

“(Waambiwe): Huu ndio Moto ule mliokuwa mkiukanusha!”

Maana yake: Malaika wa adhabu watawaambia haya kwa kuwakemea na kuwafedhehesha,

أَفْسِحْزُ هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تَبْصُرُونَ ﴿١٦﴾ أَصَلَوْهَا

“Je! Huu ni uchawi, au hamuoni tu? Uingieni.”

¹ At-Tabari 22:464 na Ad-Dur Al-Manthur 7:631.

Maana yake: Ingieni katika Moto, 'utakaokuzingireni kila upande.'

فَاصْبِرُوا أَوْ لَا تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ^ط

"Mkistahamili au msistahamili - ni mamoja kwenu."

'Ikiwa mtavumilia adhabu na hilaki zake au hamtavumilia, katu hamna pa kuikwepea wala hamna pa kujiokoa dhidi yake.'

إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

"Hakika mnalipwa kwa mliyokuwa mkiyatenda."

Na Hakika, Allah تعالى si dhalimu kwa yeyote. Kwa hakika, Allah تعالى Atamjazi kila mmoja kulingana na amali zake.

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَنَعِيمٍ ﴿١٧﴾ فَتَكْبِهِينَ بِمَا آتَيْنَهُمْ رَبُّهُمْ وَوَقَّعَهُمْ رَبُّهُمْ عَذَابَ
الْجَحِيمِ ﴿١٨﴾ كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾ مُتَّكِنِينَ عَلَى سُرُرٍ مَّصْفُوفَةٍ^ط
وَزَوَّجْنَاهُمْ بِحُورٍ عِينٍ ﴿٢٠﴾

17. Hakika wachamungu watakuwa katika bustani na neema.

18. Wakifurahi kwa yale Aliyowapa Mola wao Mlezi. Na Mola wao Mlezi Atawalinda na adhabu ya Moto.

19. Kuleni na kunyweni kwa raha kabisa kwa sababu ya mliyokuwa mkiyatenda.

20. Watakuwa wameegemea juu ya viti vya enzi vilivyopangwa kwa safu. Na Tutawaoza wanawake wa peponi.

Maelezo ya Makazi ya Watu Wema

Allah تعالى Anaeleza kuhusu makazi ya watu wema,

إِنَّ الْأَمْتَقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَنَعِيمٍ ﴿١٧﴾

"Hakika wachamungu watakuwa katika bustani na neema."

Na hilo ni tofauti na hao watakaokuwa katika adhabu na mateso;

فَيَكْفُرُونَ بِمَا آتَاهُمْ رَبُّهُمْ

“Wakifurahi kwa yale aliyowapa Mola wao Mlezi.”

Maana yake: Kwa kufurahia namna kadha wa kadha ya neema Alizowapa Allah تعالیٰ, kama vile aina mbali mbali za vyakula, vinywaji, mavazi, makazi na kadhalika,

وَوَقَلْنَاهُمْ رُبُّهُمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ

“Na Mola wao Mlezi Atawalinda na adhabu ya Motoni.”

Amewaokoa wao na adhabu ya Moto, ambapo kuepushwa huko ni neema. Zaidi ya hilo, wataingia Peponi, kwenye neema ambazo hakuna jicho lililopata kuziona wala kupita katika fikra za watu.

Kauli ya Allah تعالیٰ,

كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٦﴾

“Kuleni na kunyweni kwa raha kabisa kwa sababu ya mliyokuwa mkiyatenda.”

Inalingana na kauli Yake nyingine,

كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ ﴿٦٧﴾

“Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya mlivyotanguliza katika siku zilizopita.” (69:24)

Maana yake: Haya ni malipo stahiki kutokana na amali zenu; Hakika, hizi zote ni fadhila za Allah تعالیٰ na jaza Yake. Allah تعالیٰ Amesema,

مُتَكِبِينَ عَلَىٰ سُرُرٍ مَّصْفُوفَةٍ

“Watakuwa wameegemea juu ya viti vya enzi vilivyopangwa kwa safu.”

Ath-Thawri رحمه الله تعالیٰ amesimulia kutoka kwa Husayn, kutoka kwa Mujahid, kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: “Viti vya enzi vyenye miamvuli.” Na maana ya, *Masfufah* ni kuwa vitakuwa vikielekeana,

عَلَىٰ سُرُرٍ مُّتَقَابِلِينَ ﴿٤٤﴾

“Wako juu ya viti wamekabiliiana.” (37:44)

Kisha Allah تعالی Akasema,

وَرَوَّحْتُهُمْ مَّجُورٍ عَيْنٍ ﴿٤٥﴾

“Na Tutawaoza mahuru-l-aini.”

Tumewaozesha *Al-Hur Al-Ayn*. wasifu wao umetangulia zaidi ya sehemu moja. Inatosheleza na wala hakuna haja ya kurudia tena hapa.¹

* * *

¹ Angalia *Tafsir ya Surat Ar-Rahman* (55:56 na 72) na *As-Saffat* (37:48-49), na *Ad-Dukhan* (44:54)

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِإِذْنِ الْحَقِّنَا يَمَّا كَسَبَ
وَمَا آتَيْنَاهُمْ مِنْ عَمَلِهِمْ مِنْ شَيْءٍ ۚ كُلُّ امْرِئٍ بِمَا كَسَبَ
رَهِيْنٌ ﴿٢١﴾ وَأَمَدَدْنَاهُمْ بِفِكَهٍ وَلَحْمٍ مِمَّا يَشْتَهُونَ ﴿٢٢﴾
يَتَنَزَّعُونَ فِيهَا كَأَسَا لَا لَغْوَ فِيهَا وَلَا تَأْتِيْمٌ ﴿٢٣﴾ * وَيَطُوفُ
عَلَيْهِمْ غِلْمَانٌ هُمْ كَأَنَّهُمْ لُؤْلُؤٌ مَكْنُونٌ ﴿٢٤﴾ وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ
عَلَىٰ بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٢٥﴾ قَالُوا إِنَّا كُنَّا قَبْلُ فِي أَهْلِنَا
مُشْفِقِينَ ﴿٢٦﴾ فَمَنْ أَلَّهٖ عَلَيْنَا وَوَقَّانَا عَذَابَ السَّمُورِ ﴿٢٧﴾
﴿٢٨﴾ إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلُ نَدْعُوهُ ۗ إِنَّهُ هُوَ الْبَرُّ الرَّحِيْمُ ﴿٢٩﴾
﴿٣٠﴾ فَذَكَرْ فَمَا أَنْتَ بِبِعَمَتِ رَبِّكَ بِكَاهِنٍ وَلَا مَجْنُونٍ ﴿٣١﴾
﴿٣٢﴾ أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ نَّتَرَبَّصُ بِهِ رَيْبَ الْمُنُونِ ﴿٣٣﴾
﴿٣٤﴾ فَلَنْ تَرَبَّصُوا فَلِئِي مَعَكُمْ مِنَ الْأَمْتَرِيصِينَ ﴿٣٥﴾ أَمْ
تَأْمُرُهُمْ أَحْلَمُهُمْ بِهَذَا ۗ أَمْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُونَ ﴿٣٦﴾ أَمْ
يَقُولُونَ نَقَوْلُهُ ۗ بَلْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٣٧﴾ فَلْيَأْتُوا بِحَدِيثٍ
مِثْلِهِ ۗ إِنْ كَانُوا صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ
بِإِذْنِ الْحَقِّنَا يَمَّا كَسَبَتْ وَمَا
آتَيْنَاهُمْ مِنْ عَمَلِهِمْ مِنْ شَيْءٍ ۚ كُلُّ
امْرِئٍ بِمَا كَسَبَ رَهِيْنٌ ﴿٢١﴾
وَأَمَدَدْنَاهُمْ بِفِكَهٍ وَلَحْمٍ مِمَّا
يَشْتَهُونَ ﴿٢٢﴾ يَتَنَزَّعُونَ فِيهَا كَأَسَا لَا
لَغْوَ فِيهَا وَلَا تَأْتِيْمٌ ﴿٢٣﴾ * وَيَطُوفُ
عَلَيْهِمْ غِلْمَانٌ هُمْ كَأَنَّهُمْ لُؤْلُؤٌ مَكْنُونٌ
﴿٢٤﴾ وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ
يَتَسَاءَلُونَ ﴿٢٥﴾ قَالُوا إِنَّا كُنَّا قَبْلُ
فِي أَهْلِنَا مُشْفِقِينَ ﴿٢٦﴾ فَمَنْ أَلَّهٖ
عَلَيْنَا وَوَقَّانَا عَذَابَ السَّمُورِ ﴿٢٧﴾
﴿٢٨﴾ إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلُ نَدْعُوهُ ۗ إِنَّهُ
هُوَ الْبَرُّ الرَّحِيْمُ ﴿٢٩﴾

21. Na walioamini na wakafuatwa na vizazi vyao kwa Imani Tutawakutanisha nao vizazi vyao, na wala Hatutawapunja hata kidogo katika vitendo vyao. Kila mtu lazima atafunguliwa au kufungwa kwa alichokichuma.

22. Na Tutawapa matunda, na nyama kama watavyopenda.

23. Watapeana humo bilauri zisio na vinywaji vya kuleteana maneno ya upuuzi wala dhambi.

24. Iwe wanawapitia watumishi wao kama kwamba ni lulu zilizomo katika chaza.

25. Wataelekeana wakiulizana.

26. Waseme: Tulikuwa zamani pamoja na ahali wetu tukiogopa;

27. Basi Mwenyezi Mungu Akatufanyia hisani na Akatulinda na adhabu ya upepo wa Moto.

28. Hakika sisi zamani tulikuwa tukimuomba Yeye tu. Hakika Yeye Ndiye Mwema Mwenye Kurehemu.

Kizazi cha Muumini Kitakutanishwa Nae Katika Makazi (Peponi)

Katika Aya hii, Allah تعالی Anathibitisha Fadhila Zake, Ukirimu, Rehema na wema kwa waja Wake. Pindi Waumini watakapowafuata wao dhuria wao katika imani, Allah تعالی Atanyanyua daraja zao kufikia za wazazi wao, ingawa watoto hao hawakufanya amali kubwa kama za wazazi wao. Allah تعالی Atayafariji macho ya wazazi kwa kuwaona watoto wao wamenyanyuliwa mpaka wakafikia daraja zao. Hakika, Allah تعالی Atawakutanisha katika namna nzuri wala hatapunguza malipo wala daraja za walio na hadhi ya juu kwa ajili ya kuwaunganisha pamoja. Hivyo, Kauli Yake,

أَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَمَا أَلَتْنَاهُمْ مِنْ عَمَلِهِمْ مِنْ شَيْءٍ^٤

“Tutawakutanisha nao dhuria wao, na wala Hatutawapunja hata kidogo katika vitendo vyao.”

Ath-Thawri رحمه الله تعالی amesimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema, “Hakika, Allah تعالی Atanyanyua daraja za kizazi cha Muumini mpaka kufikia daraja za amali yake, japokuwa wao hawakufanya amali kama za wazazi wao, ili macho ya wazazi hao yafarijike.” Kisha, Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما akasoma Aya hii,

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِإِيمَانٍ أَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَمَا أَلَتْنَاهُمْ مِنْ عَمَلِهِمْ مِنْ شَيْءٍ

“Na walioamini na dhuriya wao wakawafuata kwa Imani Tutawakutanisha nao dhuriya wao, na wala Hatutawapunja hata kidogo katika vitendo vyao.”^١

Ibn Jarir رحمه الله تعالی na Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالی waliinukuu kauli hii kutoka

¹ Tafsir Ath-Thawri 283.

kwa Sufyan Ath-Thawri رضي الله عنهما kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله تعالى¹

Ibn Abu Hatim رضي الله عنهما pia alinukuu kuwa Ibn 'Abbas رضي الله تعالى alisema juu ya Kauli ya Allah تعالى،

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِإِيمَانٍ أَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ

“Na walioamini na wakafuatwa na vizazi vyao kwa Imani Tutawakutanisha nao vizazi vyao.”

Kwa kusema, “Hao ni watoto wa Waumini waliokufa wakiwa katika imani. Ikiwa daraja za wazazi wao ni za juu kuliko zao, wataunganishwa na wazazi wao. Hakuna sehemu ya malipo ya wazazi wao itakayopunguzwa kwa ajili yao. “Abdullah, mtoto wa Imamu Ahmad, amenukuu kutoka kwa Ali رضي الله عنه amesema, Mama Khadijah رضي الله عنها alimuuliza Mtume ﷺ kuhusu wanawe wawili waliofariki wakati wa Jahiliyyah, Mtume ﷺ akamjibu;

«هُمَا فِي النَّارِ»

“Wao wawili ni wa Motoni.”

Alipoona huzuni usoni mwake, akamuambia,

«لَوْ رَأَيْتَ مَكَانَهُمَا لَأَبْغَضْتَهُمَا»

“Lau ungeliyaona makazi yao ungewachukia.”

Akauliza, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Vipi kuhusu wanao?’ Akamjibu,

«فِي الْجَنَّةِ»

“Wao ni wa Peponi.”

Mtume ﷺ akasema,

«إِنَّ الْمُؤْمِنِينَ وَأَوْلَادَهُمْ فِي الْجَنَّةِ، وَإِنَّ الْمُنْشَرِكِينَ وَأَوْلَادَهُمْ فِي النَّارِ»

“Hakika, Waumini na watoto wao watakaa Peponi, hali washirikina na watoto wao watakaa Motoni.”

¹ At-Tabari 22:467.

Kisha Mtume ﷺ akasoma Aya,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِإِيمَانٍ

“Na walioamini na dhuria wao wakawafuata Kwa Imani...”¹

Kwa hakika, ni Rehema na Fadhila za Allah تعالى kwamba Anawapa watoto neema hii kwa sababu ya amali njema za wazazi wao. Yeye pia Anawapa Fadhila Zake wazazi kutokana na Baraka za dua za watoto wao. Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ اللَّهَ تَرَفُّعَ الدَّرَجَةِ لِلْعَبْدِ الصَّالِحِ فِي الْجَنَّةِ يَقُولُ: يَا رَبِّ أَنْتَ لِي هُدًى؟ يَقُولُ:
بِاسْتِغْفَارٍ وَلَدَيْكَ لَكَ»

“Hakika, Allah Atanyanyua daraja za mja mwema Peponi, atauliza, “Ewe Mola Mlezi! Nimeipataje hii?” Allah Atajibu, “Kwa kuombewa msamaha na watoto wako”²

Hadithi hii ina isnadi sahihi ya usimulizi, lakini haikunukuliwa katika Sahih. Hata hivyo, kuna masimulizi yenye kuipa nguvu Isnadi hiyo katika Sahih Muslim, kutokana na Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه, aliyesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا مَاتَ ابْنُ آدَمَ انْقَطَعَ عَمَلُهُ إِلَّا مِنْ ثَلَاثٍ: صَدَقَةٍ جَارِيَةٍ، أَوْ عِلْمٍ يُنْتَفَعُ بِهِ، أَوْ وَلَدٍ صَالِحٍ يَدْعُو لَهُ»

“Mwanaadamu anapofariki, hukatika amali zake isipokuwa (mambo) matatu: Sadaka yenye kuendelea, elimu yenye kunufaisha, au mtoto mwema mwenye kumuomba.”³

¹ Ahmad 1:135.

² Ahmad 2:509.

³ Muslim 3:1255.

Uadilifu wa Allah تعالیٰ kwa Wenye Madhambi

Allah تعالیٰ Amesema,

كُلُّ أَمْرٍ بِمَا كَسَبَ رَهِينٌ

“Kila mtu lazima atapata alichokichuma.”

Baada ya Allah تعالیٰ Kutaja Fadhila Zake kwa Kunyanyua daraja za kizazi kupitia wazazi wao, kwamba hata kama amali zao hazikuwafikia, Amethibitisha uadilifu Wake katika hilo, Hamuadhibu yeyote kutokana na makosa ya wengine,

كُلُّ أَمْرٍ بِمَا كَسَبَ رَهِينٌ

“Kila mtu lazima atapata alichokichuma.”

Kwa hivyo, kila mtu atawajibika kwa matendo yake mwenyewe. Hakuna dhambi iliyofanywa na mwingine itakayoongezwa katika mzigo wa mwingine, hata kama ilifanywa na wazazi au watoto. Sawa na Kauli Yake nyingine,

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ﴿٣٨﴾ إِلَّا أَصْحَابَ الْيَمِينِ ﴿٣٩﴾ فِي جَنَّاتٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٤٠﴾
عَنِ الْمُجْرِمِينَ ﴿٤١﴾

“Kila nafsi imo rahanini kwa mabaya iliyoyachuma. Isipokuwa watu wa kuliani. Hao watakuwa katika bustani, wawe wanaulizana. Habari za wakosefu.” (74:38-41)

Wasifu wa Pombe ya Peponi na Neema za Wakazi Wake.

Allah تعالیٰ Amesema,

وَأَمَدَدْنَاهُمْ بِفِكَهَةٍ وَلَحْمٍ مِّمَّا يَشْتَهُونَ ﴿٣٨﴾

“Na Tutawapa matunda, na nyama kama watavyopenda.”

Maana yake: ‘Tutawapa aina mbali mbali za matunda na nyama, na chochote watakachokitamani.’

يَتَنَزَّعُونَ فِيهَا كَأْسًا

“Watapeana humo bilauri”

Maana yake: Watapewa glasi za pombe, kwa mujibu wa Adh-Dhahhak.

لَا لَعُوٌّ فِيهَا وَلَا تَأْتِيمٌ

“Zisio na vinywaji vya kuleta maneno ya upuuzi wala dhambi.”

Yaani, pindi watakapokunywa hawatasema maneno yoyote ya kipuuzi, au ya ovyo au kauli chafu au zenye dhambi kama wafanyavyo walevi wa duniani. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa maana ya *Laghwni* ‘upotovu’ na *Taa’thim* ni ‘kuongopa.’¹ Mujahid amesema, “Hawatukanani wala kufanya dhambi.” Qatadah amesema, “ulevi wa aina hiyo ulikuwa duniani pamoja na Shetani. Allah تعالی Ameiepusha pombe ya Akhera dhidi ya ila na madhara yanayosababishwa na pombe ya duniani.”² Kwa hivyo, Allah تعالی Ameitakasa pombe ya Akhera dhidi ya machafu na adha kama ilivyo pombe ya duniani. Ameiondolea matatizo ya maumivu ya kichwa, maumivu ya tumbo na sumu iliyo katika pombe ya duniani. Allah تعالی Ameeleza kuwa pombe ya Akhera haitawasababishia wanywaji waseme maneno yasiyostahili, ya ovyo au yasiyowanufaisha, yaliyojaa upuuzi na uovu. Pia, Allah تعالی Ameeleza kuhusu pombe ya Akhera kuwa ina uzuri na ladha yake ni nzuri. Na Kauli Yake:

بَيْضَاءَ لَذَّةٍ لِلشَّارِبِينَ ﴿٣٧﴾ لَا فِيهَا غَوْلٌ وَلَا هُمْ عَنْهَا يُنزَفُونَ ﴿٣٨﴾

“Kinywaji cheupe, kitamu kwa wanywao. Hakina madhara, wala hakiwaleweshi.” (37:46-47)

Aidha Amesema,

لَا يُصَدَّعُونَ عَنْهَا وَلَا يُنزَفُونَ ﴿٥٦﴾

“Hawataumwa kichwa kwa vinywaji hivyo wala hawatoleweshwa.” (56:19)

Allah تعالی Amesema katika Aya hii,

يَتَنَزَّعُونَ فِيهَا كَأْسًا لَا لَعُوٌّ فِيهَا وَلَا تَأْتِيمٌ ﴿٥٧﴾

“Watapeana humo bilauri zisio na vinywaji vya kuleta maneno ya upuuzi wala dhambi.”

¹ At-Tabari 22:474.

² At-Tabari 22:474.

Allah تعالیٰ Amesema,

وَيَطُوفُ عَلَيْهِمْ غِلْمَانٌ هُمْ كَأَنَّهُمْ لَوْلُؤُا مَكْنُونٌ ﴿٥٦﴾

“Iwe wanawapitia watumishi wao kama kwamba ni lulu zilizomo katika chaza.”

Haya ni maelezo ya watumishi na huduma nzuri, watakayo- pewa Waumini Peponi. Watumishi wao watakuwa wazuri, wakarimu, wenye mavazi mazuri, hali uzuri na mvuto wao ni kama lulu zilizohifadhiwa vyema. Ni sawa na Kauli Yake:

يَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخْلِذُونَ ﴿٥٧﴾ بِأَكْوَابٍ وَأَبَارِيقٍ وَكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿٥٨﴾

“Wakitumikiwa na wavulana wa ujana wa milele. Kwa vikombe na birika na bilauri za vinywaji kutoka chemchem safi.” (56:17-18)

Allah تعالیٰ Amesema,

وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ

“Wataelekeana wakiulizana.”

Maana yake: Waumini wataelekeana au wakiongea na kukumbuka amali na hali zao humu duniani, kama wafanyavyo watu wa humu duniani wanapokuwa katika unywaji, hasa pindi wanapokuwa katika ulevi,

قَالُوا إِنَّا كُنَّا قَبْلُ فِي أَهْلِنَا مُشْفِقِينَ ﴿٥٩﴾

“Waseme: Tulikuwa zamani pamoja na ahali wetu tukiogopa”

Maana yake: ‘Katika maisha ya duniani na katika familia zetu, tulikuwa katika kumcha Mola Wetu Mlezi na tukiogopa adhabu Yake.’

فَمَرَّ بِاللَّهِ عَلَيْنَا وَوَقْنَا عَذَابَ السُّمُورِ ﴿٦٠﴾

“Basi Mwenyezi Mungu Akatufanyia hisani na Akatulinda na adhabu ya upepo wa Moto.”

Maana yake: ‘Ametupa fadhila na Ametunusuru dhidi ya tulichokiogopa.’

إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلُ نَدْعُوهُ^ط

“Hakika sisi zamani tulikuwa tukimuomba Yeye tu.”

Maana yake: ‘Tulikuwa tukimuomba Yeye kwa unyenyekevu, na Yeye Alitutakabalia na Akatupa tulichokitamani,’

إِنَّهُ هُوَ الْبَرُّ الرَّحِيمُ^ط

“Hakika Yeye Ndiye Mwema Mwenye Kurehemu.”

فَذَكَرَ فَمَا أَنْتَ بِبِعَمَتِ رَبِّكَ بِكَاهِنٍ وَلَا مَجْنُونٍ^ط أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ نَتَرَبَّصُ بِهِ
رَبِّبَ الْمُنُونِ^ط قُلْ تَرَبَّصُوا فَإِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُنْتَرِبِينَ^ط أَمْ تَأْمُرُهُمْ أَحْلِمُهُمْ
بِهَذَا أَمْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُونَ^ط أَمْ يَقُولُونَ تَقْوَاهُ^ط بَلْ لَا يُؤْمِنُونَ^ط فَلْيَأْتُوا بِحَدِيثٍ
مِثْلِهِ إِنْ كَانُوا صَادِقِينَ^ط

29. Basi kumbusha! Kwani wewe, kwa neema ya Mola Wako Mlezi, si kuhani wala mwendawazimu.

30. Au wanasema: Huyu ni mtunga mashairi, tunamtarajia kupatilizwa na zama.

31. Sema: Tarajieni, na mimi pia ni pamoja nanyi katika kutarajia.

32. Au hizo akili zao ndio zinawaamrisha haya, au wao basi ni watu majeuri tu?

33. Au ndio wanasema: Ameitunga hii! Bali basi tu hawaamini!

34. Basi nawalete masimulizi kama haya ikiwa wao wanasema kweli.

Mtume ﷺ ni Mtu Safi Dhidi ya Tuhuma za Washirikina na Adhabu Kali Inawangojea Wao

Allah تعالى Anamuamuru Mjumbe Wake awafikishie waja Wake Ujumbe Wake na awakumbushe Alichowateremshia. Kisha, Allah تعالى Anakanusha madai ya uongo waliyotoa wazushi na watenda dhambi dhidi ya Mtume ﷺ, Akasema,

فَذَكِّرْ فَمَا أَنْتَ بِنِعْمَتِ رَبِّكَ بِكَاهِنٍ وَلَا مَجْنُونٍ ﴿٥٢﴾

“Basi kumbusha! Kwani wewe, kwa neema ya Mola Wako Mlezi, si kuhani wala mwendawazimu.”

Allah تعالى Anasema: Kwa neema ya Allah تعالى, wewe, Ewe Muhammad, si kuhani, kama washirikina wajinga wa Kikuraishi wanavyodai. Kuhani ni mtabiri ambaye hupokea maelezo kutoka kwa Majini wanaopata habari za siri, habari za mbinguni.

وَلَا مَجْنُونٍ

“Wala mwendawazimu.” Ambaye Shetani amempagawisha kwa kichaa. Allah تعالى Amesema, huku akiwakanusha wapagani kutokana na Shutuma zao dhidi ya Mtume ﷺ.

أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ نَّتَرْتِيبُ بِهِ رَبِّبَ الْمُتُونِ ﴿٥٣﴾

“Au wanasema: Huyu ni mtunga mashairi tunamtarajia kupatilizwa na dahari.”

Maana yake: Balaa ya dahari na mauti. Wamesema, ‘Tunamngoja mpaka kifo kimfike, kwa hivyo, tuondokane na usumbufu wake na Ujumbe wake.’ Allah تعالى Amesema,

قُلْ تَرْتَبُوا فَإِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُتَرْتِبِينَ ﴿٥٤﴾

“Sema: Tarajieni, na Mimi pia ni pamoja nanyi katika kutarajia.”

‘Ngojeni, Nami pia Nitangojea pamoja nanyi, na mtakuja kujua nani mwenye mwisho mwema na kupata ushindi humu duniani na Akhera.’ Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى amesimulia kuwa ‘Abdullah bin Abu Najih kutoka kwa Mujahid amesema, Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema, “Pindi Makuraishi walipokusanyika katika Dar An-Nadwah (sehemu yao ya kukutana) kujadiliana suala la Mtume ﷺ, mmoja wao akasema, ‘Mfungeni jela katika minyororo. Halafu tutangojea

kwa muda, balaa litampata, atakufa kama walivyokufa washairi waliokuwa kabla yake Zuhayr na An-Nabighah, kwa kuwa na yeye ni mshairi kama wao.’ Allah تعالى Amesema katika kujibu kauli yao,

أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ نَّتَرْتِصُ بِهِ رَيْبَ الْمُنُونِ ﴿٤٤﴾

“Au wanasema: Huyu ni mtunga mashairi, tunamtarajia kupatilizwa na dahari”.¹

Allah تعالى Amesema,

أَمْ تَأْمُرُهُمْ أَحْلِمُهُمْ بِهَذَا

“Au hizo akili zao ndio zinawaamrisha haya.”

‘Akili zao ndizo zinazowaamuru wao wakuzushie uongo huu (Ewe Muhammad), ingawa wanajua kutoka katika nyoyo zao kuwa wao ni waongo na wapotovu.’

أَمْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُونَ

“Au wao basi ni watu majeuri tu?”

‘Hakika, wao ni watu wapotevu, wakaidi na madhalimu, ndiyo sababu wanayasema wayasemayo kukuhusu (Ewe Muhammad).’

‘Allah تعالى Amesema,

أَمْ يَقُولُونَ تَقْوَاهُ

“Au ndio wanasema: Ameitunga hii!”

Wamesema, ‘Qur’an hii ameibuni ameizua yeye mwenyewe.’ Allah تعالى Aliwajibu,

بَلْ لَا يُؤْمِنُونَ

“Bali basi tu hawaamini!”

Maana yake: Ukafiri wao huwafanya watoe kauli hizi.

فَلْيَأْتُوا بِحَدِيثٍ مِّثْلِهِ إِنْ كَانُوا صَادِقِينَ ﴿٤٥﴾

“Basi nawalete masimulizi kama haya ikiwa wao wanasema kweli.”

¹ At-Tabari 22:479, Isnadi yake ni dhaifu.

Maana yake: Ikiwa wao wakweli katika kauli yao kuwa Muhammad ﷺ ameitunga Qur'an hii na ameizua yeye mwenyewe, basi walete kitu chenye kufanana na alichokileta, na hata kama wataunganisha nguvu zao na walio duniani, majini na wanaadamu, kamwe hawatamudu kuleta kitu kama Qur'an, au Sura kumi au hata Sura moja tu!

* * *

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمْ
 الْخَالِقُونَ ﴿٣٥﴾ أَمْ خُلِقُوا
 خَلْقُوا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ^ع بَلْ لَا يُوقِنُونَ ﴿٣٦﴾ أَمْ
 عِنْدَهُمْ خَزَائِنُ رِزْقِ أَمْ هُمْ
 الْمَصْطَرُونَ ﴿٣٧﴾ أَمْ هُمْ
 سَلَمٌ يَسْتَمِعُونَ فِيهِ^ط فَلَيَاتِ مُسْتَمِعُهُمْ
 بِسُلْطَانٍ مُبِينٍ ﴿٣٨﴾ أَمْ لَهُ
 الْآبِنَتُ وَلَكُمْ الْبَنُونَ ﴿٣٩﴾ أَمْ تَسْأَلُهُمْ
 أَجْرًا فَهُمْ مِّنْ مَّغْرَمٍ مُّثْقَلُونَ ﴿٤٠﴾ أَمْ
 عِنْدَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُمُونَ ﴿٤١﴾ أَمْ
 يُرِيدُونَ كَيْدًا^ط فَالَّذِينَ كَفَرُوا هُمُ
 الْمَكِيدُونَ ﴿٤٢﴾ أَمْ هُمْ
 إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ^ع سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٤٣﴾ وَإِن يَرَوْا
 كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ سَاقِطًا يَقُولُوا سَحَابٌ مَّرْكُومٌ ﴿٤٤﴾
 فَذَرَهُمْ حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي فِيهِ يُصْعَقُونَ ﴿٤٥﴾ يَوْمَ
 لَا يُغْنِي عَنْهُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٤٦﴾ وَإِنَّ
 لِلَّذِينَ ظَلَمُوا عَذَابًا دُونَ ذَلِكَ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ
 ﴿٤٧﴾ وَأَصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا^ط وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ
 حِينَ تَقُومُ ﴿٤٨﴾ وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَإِدْبَارَ النُّجُومِ ﴿٤٩﴾

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمْ
 الْخَالِقُونَ ﴿٣٥﴾ أَمْ خُلِقُوا
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ^ع بَلْ لَا يُوقِنُونَ
 ﴿٣٦﴾ أَمْ عِنْدَهُمْ خَزَائِنُ رِزْقِ أَمْ هُمْ
 الْمَصْطَرُونَ ﴿٣٧﴾ أَمْ هُمْ
 سَلَمٌ يَسْتَمِعُونَ فِيهِ^ط فَلَيَاتِ مُسْتَمِعُهُمْ
 بِسُلْطَانٍ مُّبِينٍ ﴿٣٨﴾ أَمْ لَهُ
 الْآبِنَتُ وَلَكُمْ الْبَنُونَ ﴿٣٩﴾ أَمْ تَسْأَلُهُمْ
 أَجْرًا فَهُمْ مِّنْ مَّغْرَمٍ مُّثْقَلُونَ ﴿٤٠﴾ أَمْ
 عِنْدَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُمُونَ ﴿٤١﴾ أَمْ
 يُرِيدُونَ كَيْدًا^ط فَالَّذِينَ كَفَرُوا هُمُ
 الْمَكِيدُونَ ﴿٤٢﴾ أَمْ هُمْ
 إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ^ع سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ
 ﴿٤٣﴾

35. Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji?

36. Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini.

37. Au wanazo khazina za Mola Wako Mlezi au wao ndio wenye madaraka?

38. Au wanazo ngazi za kusikilizia? Basi msikilizaji wao huyo na alete hoja iliowazi!

39. Au Mwenyezi Mungu ana wasichana, na nyinyi ndio mna wavulana?

40. Au wewe unawaomba ujira, na kwa hivyo ndio wanaelemewa na uzito wa gharama?

41. Au wanayo elimu ya ghaibu, nao wameandika?

42. Au wanataka kufanya vitimbi tu? Lakini hao waliokufuru ndio watakaotegeka.

43. Au wanae mungu asiyekuwa Mwenyezi Mungu? Subhanallah! Ametakasika Mwenyezi Mungu na hao wanaowashirikisha Naye.

Yanayothibitisha Tawhidi na Kutengua Hila za Washirikina

Aya hizi zinathibitisha "Tauhid Ar-Rubuubiya" Tauhid ya umiliki Wake Mola Mlezi. Na Tawhid ya mamlaka ya kiuungu. Allah تعالى Amesema,

﴿أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ﴾

"Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji?"

Allah تعالى Anawauliza ikiwa waliumbwa bila ya muumba au walijiumba wenyewe, yote si sahihi. Allah تعالى Peke Yake ndiye Aliyewaumba na Akawapatisha, wakati walikuwa hawajulikani kabisa. Al-Bukhari amenukuu kutoka kwa Jubayr bin Mut'im amesema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akisoma Surat At-Tur katika Sala ya Al-Maghrib na alipofikia Aya hii,

﴿أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ﴾ ﴿أَمْ خُلِقُوا مِنَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ بَلْ لَّا يُوقِنُونَ﴾ ﴿أَمْ عِنْدَهُمْ خَزَائِنُ رَيْكِ أَمْ هُمُ الْمُصِيطِرُونَ﴾

"Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji? Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini. Au wanazo khazina za Mola Wako Mlezi au wao ndio wenye madaraka?"¹

¹ Fat'h Al-Bari 8:469

Nilihisi moyo wangu ukikaribia kuruka.” Hadithi hii imekusanywa katika Sahih Mbili kwa isnadi nyingi.¹ Jubayr bin Mut’im alikwenda kwa Mtume ﷺ baada ya vita ya Badr kuwakomboa washirikina wenzake waliotekwa. Wakati huo alikuwa bado mshirikina. Akamsikia Mtume ﷺ akisoma Aya hii ilikuwa moja ya Aya ambayo ilimfanya baadaye aingie katika Uislamu. Allah تعالى Amesema,

﴿أَمْ خَلَقُوا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بَلْ لَا يُوقِنُونَ﴾

“Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini.”

Maana yake: Allah تعالى Anawakaripia washirikina kutokana na ushirikina wao, huku Akiwauliza kama wameumba mbingu na ardhi. Walijua kuwa Allah تعالى Peke Yake Ndiye Muumba pasi na washirika. Hata hivyo, kukosekana uyakinifu ndiko kuliko sababisha wafanye hilo,

﴿أَمْ عِنْدَهُمْ خَزَائِنُ رَيْكَ أَمْ هُمُ الْمُصِيطِرُونَ﴾

“Au wanazo khazina za Mola Wako Mlezi au wao ndio wenye madaraka?”

Inamaanisha, je, wana mamlaka ya kufanya chochote wanachotaka katika Ufalme Wake, je, mikononi mwao wanazo funguo za hazina Zake.

﴿أَمْ هُمُ الْمُصِيطِرُونَ﴾

“Au wao ndio wenye madaraka?”

Inamaanisha, je, wao ni wenye kuhesabu viumbe? Sivyo, bali Allah تعالى Ndiye Mmiliki Mwenye Kuendesha (ulimwengu), Mwenye Kufanya Atakalo.

Allah تعالى Amesema,

﴿أَمْ هُمْ سُلَّامٌ يَسْتَمِعُونَ فِيهِ﴾

“Au wanazo ngazi za kusikilizia?”

Maana yake: je, wana ngazi za kupanda mbinguni (mpaka mahali walipo Malaika).

¹ Fat’h Al-Bari 2:289, 6:194 na 7:375 na Muslim 3:338 na 339.

فَلْيَأْتِ مُسْتَوْعُهُمْ بِسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ

“Basi msikilizaji wao huyo na alete hoja ilio wazi!”

Maana yake: Hebu msikilizaji wao alete ushahidi wa kuthibitisha ukweli wa matendo na kauli zao. Kamwe hawamudu kufanya hayo na kwa hivyo, hawana lolote na hawana ushahidi katika msimamo wao. Allah تعالیٰ Anawakaripia kuhusu dai lao kuwa Yeye ana watoto wa kike na kuwa Malaika ni wanawake! Wapagani walijichagulia na kuwapendelea watoto wa kiume kuliko watoto wa kike, na pindi mmoja wao anapoletea habari ya kuzaliwa mtoto wa kike, uso wake hugeuka mweusi kutokana na hasira! Lakini, wamefanya kuwa Malaika ni watoto wa kike wa Allah تعالیٰ na wakawaabudu wao badala ya Allah تعالیٰ,

أَمْ لَهُ الْآبِنَاتُ وَلَكُمُ الْآبْنُونَ ﴿٥٦﴾

Au Yeye Mwenyezi Mungu ana wasichana, na nyinyi ndio mna wavulana?

Na hili ni onyo kali na karipio kali.

Allah تعالیٰ Amesema,

أَمْ تَسْأَلُهُمْ أَجْرًا

“Au wewe unawaomba ujira.”

Maana yake: Kama ujira kutokana na ufikishaji wako Ujumbe wa Allah تعالیٰ. Yaani, wewe, usiwaombe chochote juu ya hilo,

فَهُمْ مِّنْ مَّغْرَمٍ مُّتَقَلِّوْنَ

“Na kwa hivyo ndio wanaelemewa na uzito wa gharama?”

Maana yake: Katika hali hii, mmojawapo anaweza kulalamika kwa kitu kidogo cha usumbufu na kuona ugumu na uzito kutokana nacho.

أَمْ عِنْدَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُمُونَ ﴿٥٧﴾

“Au wanayo elimu ya ghaibu, nao wameandika?”

Maana yake: Jambo haliko hivyo, kwani hakuna yeyote mbinguni au ardhini anayejua ghaibu isipokuwa Allah تعالیٰ Peke Yake,

﴿٤٣﴾ أَمْ يُرِيدُونَ كَيْدًا ۖ فَالَّذِينَ كَفَرُوا هُمُ الْمَكِيدُونَ ﴿٤٤﴾

“Au wanataka kufanya vitimbi tu? Lakini hao waliokufuru ndio watakaotegeka.”

Allah تعالى Anauliza, ‘watu hawa wanaotoa kauli hizi kuhusu Mtume na dini Yake, wanatafuta kuwadanganya watu na kupanga njama dhidi ya Mtume ﷺ na Masahaba wake, kama wanaweza kufanya hivyo, basi wajue kuwa njama zao zitawadhuru wao wenyewe. Na kwa hivyo, ubaya utawaangukia wao badala ya hao wanaowakusudia.

﴿٤٥﴾ أَمْ هُمْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ ۗ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٤٦﴾

“Au wanae mungu asiye kuwa Mwenyezi Mungu? Subhanallah! Ametakasika Mwenyezi Mungu na hao wanaowashirikisha naye.”

Hili ni kanusho dhidi ya washirikina kutokana na wao kuyaabudu masanamu na washirika wengine pamoja na Allah تعالى.

Kisha Allah تعالى Anaitakasa Nafsi Yake Tukufu kutokana na wanayosema na kumzulia, na wanayomshirikisha nayo.

سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ

“Ametakasika Mwenyezi Mungu na hao wanaowashirikisha Naye.”

﴿٤٧﴾ وَإِنْ يَرَوْا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ سَاقِطًا يَقُولُوا سَحَابٌ مَّرْكُومٌ ﴿٤٨﴾ فَذَرَهُمْ حَتَّىٰ يُلَاقُوا

﴿٤٩﴾ يَوْمَهُمُ الَّذِي فِيهِ يُصْعَقُونَ ﴿٥٠﴾ يَوْمَ لَا يُغْنِي عَنْهُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٥١﴾

﴿٥٢﴾ وَإِنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا عَذَابًا دُونَ ذَلِكَ وَلَٰكِن أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٣﴾ وَأَصْبَرَ لِحُكْمِ رَبِّكَ

﴿٥٤﴾ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا ۖ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٥٥﴾ وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَإِدْبَرَ النُّجُومِ ﴿٥٦﴾

44. Na hata wangeona pande linatoka mbinguni linaanguka wangesema: Ni mawingu yaliyobebana.

45. Basi waache mpaka wakutane na siku yao watakapohilikishwa.

46. Siku ambayo hila zao hazitawafaa hata kidogo, wala wao hawatanusuriwa.

47. Na hakika waliodhulumu watapata adhabu nyengine isiyokuwa hii, lakini wengi wao hawajui.

48. Na ingojee hukumu ya Mola Wako Mlezi. Kwani wewe hakika uko mbele ya Macho Yetu, na mtakase kwa kumsifu Mola Wako Mlezi unaposimama,

49. Na usiku pia mtakase, na zinapokuchwa nyota.

Ubainifu wa Ukaidi wa Washirikina; na Kwamba Nao Pia Wataadhibiwa

Allah تعالى Anaeleza tena kuhusu ukaidi wa washirikina na kiburi chao kwa vitu vinavyoonekana kwa njia za fahamu za binadamu.

وَإِنْ يَرَوْا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ سَاقِطًا

“Na hata wangeona pande linatoka mbinguni linaanguka...”

Maana yake: Juu yao kama adhabu, wasingeamini kinachowajia, kwani wangesema, haya ni matabaka ya mawingu yaliyopandana. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا مِّنَ السَّمَاءِ فَظَلُّوا فِيهِ يَعْرُجُونَ ﴿١٤﴾ لَقَالُوا إِنَّمَا سُكَّرَتْ أَبْصَارُنَا
بَلْ نَحْنُ قَوْمٌ مَّسْحُورُونَ ﴿١٥﴾

“Na lau Tungaliwafungulia mlango wa mbingu, na wakaanza kupanda humo. Hakika wangalisema: Macho yetu yamelewalewa tu, bali sisi ni watu tuliologwa.” (15:14-15)

Allah تعالى Amesema,

فَذَرَّهُمْ

“Basi waache,”

‘Ewe Muhammad ﷺ,

حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي فِيهِ يُصْعَقُونَ

“Mpaka wakutane na siku yao watakapohilikishwa.”

Siku ya Ufufuo,

يَوْمَ لَا يُغْنِي عَنْهُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا

“Siku ambayo hila zao hazitawafaa hata kidogo.”

Maana yake: Katika Siku ya Ufufuo, hadaa na njama zao walizozipanga humu duniani hazitaweza kuwasaidia wao hata kidogo,

وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ

“Wala wao hawatanusuriwa.”

Allah تعالى Amesema,

وَإِنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا عَذَابًا دُونَ ذَلِكَ

“Na hakika waliodhulumu watapata adhabu nyingine isiyokuwa hii.”

Maana yake Licha ya adhabu hii ya humu duniani. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَلَنُنذِرَنَّهُمْ مِنَ الْعَذَابِ الْأَدْنَىٰ دُونَ الْعَذَابِ الْأَكْبَرِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢١﴾

“Na Tutawaonjesha adhabu khafifu kabla ya adhabu kubwa, huenda labda watarejea.” (32:21)

Allah تعالى Amesema;

وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْمُونَ

“Lakini wengi wao hawajui.”

Maana yake: Tutawaadhibu humu duniani na kuwajaribu kwa kuwapa balaa ili waweze kujirudi na kutubu. Hata hivyo, wao huwa hawaelewi kinachokusudiwa kwao, kwa sababu pindi adhabu ikiondoshwa, wao hurejea kwenye kutenda mabaya waliyokuwa wakiyafanya kabla yake. Na imekuja katika “Hadithi” inayoelezea habari ya Allah تعالى pale mja atakaposema: “Ni

mara ngapi Mola wangu ninakuasi, lakini Huniadhibu?" Allah تعالى Atasema: "Ewe Mja wangu! mara ngapi Nakuadhibu lakini hujui?"

Mtume ﷺ Anaamrisha Kuwa na Subira, na Kumtukuza Allah تعالى

Allah تعالى Amesema,

وَأَصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا

"Na ingojee hukumu ya Mola wako Mlezi. Kwani wewe hakika uko mbele ya Macho Yetu."

Maana yake: 'Kuwa mstahamilivu juu ya maudhi yao na wala usiwajali kwa sababu wewe uko chini ya Uangalizi na Ulinzi Wetu na kwa hakika Tutakulinda dhidi ya watu waovu,'

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ حِينَ تَقُومُ

"Na mtakase kwa kumsifu Mola wako Mlezi unaposimama."

Adh-Dhahhak amesema, maana yake, kusimama kwa ajili ya Sala (na useme): "Utakaso ni Wako ewe Mola; na Sifa Njema ni Zako, Jina lako ni Tukufu, Umetukuka Utukufu Wako, na hapana mola wa haki wa kuabudiwa isipokuwa Wewe."¹ Muslim alinukuu katika Sahih yake kuwa 'Umar رضي الله عنه alikuwa akisoma dua hii wakati wa kuanza kusali.² Ahmad na wakusanyaji wa *Sunan* wamenukuu Hadithi hii kutoka kwa Abu Sa'id na wengine, kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisema hivyo.³ Abu Al-Jawza' amesema;

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ حِينَ تَقُومُ

"Na mtakase kwa kumsifu Mola Wako Mlezi unaposimama,"

"Unapolala na unapoamka."⁴ Hii ni rai iliyochaguliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.⁵ Rai hii inatiliwa nguvu na Hadithi ambayo Imamu Ahmad ameinukuu kuwa 'Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema,

¹ At-Tabari 22:489.

² Muslim 1:299.

³ Ahmad 3:50, Abu Dawud 1:490, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 2:47 na 50, An-Nasai 2:132 na Ibn Majah 1:264 na 265.

⁴ Al-Qurtubi 17:79.

⁵ At-Tabari 22:488.

«مَنْ تَعَارَى مِنَ اللَّيْلِ فَقَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَخَدَّهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ، وَلَا حَزَلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ. ثُمَّ قَالَ: رَبِّ اغْفِرْ لِي - أَوْ قَالَ: ثُمَّ دَعَا - اسْتَجِيبَ لَهُ، فَإِنْ عَزَمَ فَتَوَضَّأَ ثُمَّ صَلَّى، قُبِلَتْ صَلَاتُهُ»

*"Mwenye kuamka usiku na kusema, 'Hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, ni Mpweke Hana mshirika. Ufalme ni Wake na Sifa Njema ni Zake, Yeye ni Muweza wa kila kitu. Kutakasika ni Kwake na Shukurani ni Zake, na hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na Allah ni Mkubwa mno. Wala hapana hila wala nguvu ya kufanya jambo isipokuwa kwa Allah.' Halafu akasema: 'Ewe Mola Wangu Mlezi nighufirie.' Au amesema: 'Akaomba dua, basi atajibiwa, na ikiwa ataazimia na kuchukua udhu akasali, basi Sala yake itapokewa.'"*¹

Ameitoa Al-Bukhari katika Sahih yake na wakusanyaji wa *Sunan* nao wameinukuu Hadithi hii.²

Ibn Abu Najih amesimulia kutoka kwa Mujahid alitoa rai juu ya Aya,

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ حِينَ تَقُومُ

"Na mtakase kwa kumsifu Mola Wako Mlezi unaposimama."

Kwa kusema, "Katika kila mkusanyiko unaokuwemo wewe." Ath-Thawri رحمه الله تعالى amesema kuwa Abu Is-haq رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Abu Al-Ahwas amesema kuwa,

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ حِينَ تَقُومُ

"Na mtakase kwa kumsifu Mola Wako Mlezi unaposimama."

"Pindi mtu anapotaka kusimama katika mkusanyiko. Akasema: 'Utukufu ni Wako, Ewe Allah تعالى, na Sifa Njema ni Zako.'"³ Abu Hurayrah رضي الله عنه amesimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ Ahmad 5:313.

² *Fat'h Al-Bari* 3:47. Abu Dawud 5:305, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:359, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:215 na Ibn Majah 2:1276.

³ Al-Qurtubi 17:78.

«مَنْ جَلَسَ فِي مَجْلِسٍ فَكَثُرَ فِيهِ لَفْظُهُ، فَقَالَ قَبْلَ أَنْ يَقْرَمَ مِنْ مَجْلِسِهِ: سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوبُ إِلَيْكَ، إِلَّا غَفَرَ اللَّهُ لَهُ مَا كَانَ فِي مَجْلِسِهِ ذَلِكَ»

“Mwenye kukaa katika kikao ambamo upuuzi unazungumzwa kwa wingi. Hivyo kabla hajasimama kuondoka katika kikao hicho akasema, ‘Utukufu ni Wako Ewe Allah, na Sifa ni Zako, nashuhudia kwamba hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe, naomba msamaha Wako, natubu Kwako.’ Allah Atamsamehe kushiriki kwake katika yaliyosemwa katika mkusanyiko huo.”

Hadithi hii imenukuliwa na At-Tirmidhi, na haya ni maneno yake, pia imenukuliwa na An-Nasa’i katika ‘Amal Al-Yawm wal-Laylah. At-Tirmidhi alisema, “Hasan Sahih.”¹ Pia imenukuliwa na Al-Hakim katika *Mustadrak* wake, na akasema, “Isnadi yake ina vigezo vya Muslim.”² Allah تعالى Amesema;

وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ

“Na usiku pia mtakase.” Maana yake: Umkumbuke na umuabudu Allah تعالى kwa kusoma Qur’an na kusali usiku.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَكَ عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَحْمُودًا ﴿١٧٩﴾

“Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunna khasa kwako wewe. Huenda Mola Wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinachosifika.”
(17:79)

Allah تعالى Amesema;

وَادْبَرَ الْأُنْجُومِ

“Na zinapokuchwa nyota.”

Inakusudiwa raka mbili kabla ya Sala ya Alfajiri, kwa mujibu wa Hadithi ya Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما. Raka hizi mbili ni Sunnah inayofanywa kabla nyota hazijatua.³

¹ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:392 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:105.

² Al-Hakim 1:536.

³ At-Tabari 22:379.

Imethibitishwa katika Sahihi Mbili kuwa Mama Aisha رضي الله عنها alisema, "Mtume ﷺ hakuna rakaa mbili alizokuwa na umakini nazo kama rakaa mbili za Alfajiri."¹ Katika masimulizi ya Muslim, Mtume ﷺ alisema,

«رَكَعَاتَا الْفَجْرِ خَيْرٌ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا فِيهَا»

*"Rakaa mbili za Al-Fajr ni bora zaidi kuliko dunia hii na vyote vilivyomo ndani yake."*²

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu At-Tur*, Sifa zote njema pamoja na Shukurani zinamstahiki Allah تعالى.

* * *

¹ *Fath Al-Bari* 3:55 na Muslim 1:501

² Muslim 1:501

Tafsiri ya Suratu An-Najm

Sura ya 53

Iliteremshwa Makkah

Sura ya Kwanza Ambamo Aya ya Sijida Iliteremshwa Ndani Yake

Al-Bukhari alinukuu kutoka kwa 'Abdullah (bin Mas'ud رضي الله عنه) alisema; "Suratu An-Najm" ndiyo ya kwanza ambayo sijida ya kisomo iliteremshwa ndani yake. Mtume ﷺ (alisoma akiwa Makkah na) alisujudu. Wale waliokuwa pamoja naye walifanya vivyo hivyo, isipokuwa mzee mmoja alichota mchanga mkononi na akasujudu juu yake. Baadaye, nilimshuhudia akiuawa hali ya kuwa ni kafiri; alikuwa ni Umayyah bin Khalaf."¹

Al-Bukhari aliinukuu Hadithi hii katika sehemu nyingi katika Sahihi yake, kama walivyofanya Muslim, Abu Dawud na An-Nasa'i, kwa isnadi nyingi toka kwa Abu Is-haq kutoka kwa Abdullah.²



¹ Fat'h Al-Bari 8:480.

² Fat'h Al-Bari 6:641 na 243, 7:202 na 348, Muslim 1:405, Abu Dawud 2:122 na An-Nasai 2:160.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

سُورَةُ النَّجْمِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ﴿١﴾ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ﴿٢﴾
 وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٣﴾ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾
 عَمَّهُ شَدِيدُ الْفَوَىٰ ﴿٥﴾ ذُو مِرَّةٍ فَاسْتَوَىٰ ﴿٦﴾ وَهُوَ
 بِالْأُنْفِ الْأَعْلَىٰ ﴿٧﴾ ثُمَّ دَنَا فَتَدَلَّىٰ ﴿٨﴾ فَكَانَ قَابَ
 قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٩﴾ فَأَوْحَىٰ إِلَىٰ عَبْدِهِ مَا أَوْحَىٰ ﴿١٠﴾ مَا
 كَذَّبَ الْفُؤَادُ مَا رَأَىٰ ﴿١١﴾ أَفَتُمْنُونَهُ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ ﴿١٢﴾
 وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ ﴿١٣﴾ عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَىٰ ﴿١٤﴾
 عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَىٰ ﴿١٥﴾ إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَىٰ ﴿١٦﴾
 مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ ﴿١٧﴾ لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ
 الْكُبْرَىٰ ﴿١٨﴾ أَفَرَأَيْتُمْ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ﴿١٩﴾ وَمَتَوَةَ الثَّالِثَةَ
 الْأُخْرَىٰ ﴿٢٠﴾ أَلَكُمُ الذَّكْرُ وَلَهُ الْأُنْثَىٰ ﴿٢١﴾ تِلْكَ إِذًا
 قِسْمَةٌ ضِيزَىٰ ﴿٢٢﴾ إِنْ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءُ سَمِيَتْهُمَا أَنْتُمْ
 وَعَبَاوُكُم مَّا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطَانٍ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ
 وَمَا تَهْوَى الْأَنْفُسُ ۗ وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنْ رَبِّهِمُ الْهُدَىٰ ﴿٢٣﴾
 أَمْ لِلْإِنْسَانِ مَا تَمَنَّىٰ ﴿٢٤﴾ فَلِلَّهِ الْآخِرَةُ وَالْأُولَىٰ ﴿٢٥﴾ *
 وَكَمْ مِنْ مَلَكٍ فِي السَّمَوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِنْ
 بَعْدِ أَنْ يُأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَرْضَىٰ ﴿٢٦﴾

وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ﴿١﴾ مَا ضَلَّ
 صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ﴿٢﴾ وَمَا يَنْطِقُ
 عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٣﴾ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ
 يُوحَىٰ ﴿٤﴾

1. Naapa kwa nyota inapotupwa kwa kushambulia.
2. Mwenzenu huyu hukupotea, wala hakukosea.
3. Wala hatamki kwa matamanio.
4. Hayakuwa haya ila ni Wahyi ulio funuliwa.

Allah تعالیٰ Ameapa kuwa Mjumbe ni Mkweli na Hatamki Isipokuwa kwa Ufunuo

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالیٰ alinukuu kutoka kwa Ash-Sha'bi na wengine walieleza kuwa Muumba Anaapa kwa chochote Anachotaka miongoni mwa viumbe wake, lakini viumbe huapa kwa kumtaja Muumbaji tu. Allah تعالیٰ Amesema,

وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ﴿٥٦﴾

“Naapa kwa nyota inapotua.” Ibn Abu Najih alisimulia kuwa Mujahid alisema, “Nyota ina maana ya Thurea pindi inapotua wakati wa Alfajiri.”¹ Adh-Dhahhak alisema “Pindi Mashetani yanaporushiwa nayo.” Aya hii inafanana na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

فَلَا أُقْسِمُ بِمَوْجِعِ النُّجُومِ ﴿٥٦﴾ وَإِنَّهُ لَقَسَمٌ لَّو تَعْلَمُونَ عَظِيمٌ ﴿٥٧﴾ إِنَّهُ لَقُرْءَانٌ كَرِيمٌ ﴿٥٨﴾
 فِي كِتَابٍ مَّكْنُونٍ ﴿٥٩﴾ لَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ ﴿٦٠﴾ تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦١﴾

“Basi Naapa kwa maanguko ya nyota, na hakika bila ya shaka hichi ni kiapo kikubwa, laiti mngelijua! Hakika hii bila ya shaka ni Qur’ani Tukufu. Katika Kitabu kilichohifadhiwa. Hapana akigusaye ila waliotakaswa. Ni uteremsho unaotoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.” (56:75-80)

Allah تعالى Amesema:

مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ﴿٦٢﴾

“Mwenzenu huyu hakupotea, wala hakukosea.”

Hiki ndicho kinachoapiwa. Ni ushahidi kuwa Mjumbe wa Allah ﷻ ni mwenye akili timamu na anafuata Ukweli. Hakupotea, kama ilivyo kwa wajinga wasioiendea njia yoyote kwa ujuzi, wala yeye hakukosea kama wale wenye ujuzi wanaoujua Ukweli, lakini wanaukwepa kwa makusudi na kuliendea jambo jingine. Kwa hivyo, Allah تعالى Alimsafisha Mjumbe Wake na Ujumbe wake dhidi ya njia za wapotevu wa Kikristo na Kiyahudi, kwa kuujua ukweli na kuuficha, huku wakiendelea kushikamana na upotevu. Kinyume na hivyo, Mtume ﷺ, yuko katika njia sahihi, huku akifuata uongofu na yaliyo sahihi.

Mtume Muhammad ﷺ ni Rehema kwa Viumbe Wote; Hasemi kwa Utashi Wake

Allah تعالى Amesema,

وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٦٣﴾

“Na wala hatamki kwa matamano.” Inaelezwa kuwa Mtume ﷺ hatamki kutokana na matamano na utashi wake,

¹ At-Tabari 22:495.

إِنَّ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ﴿١﴾

“Hayakuwa haya ila ni ufunuo uliofunuliwa.”

Maana yake: Anawafikishia watu kile alicheamrisha akifikisha, kwa ukamilifu bila nyongeza wala upungufu. Imam Ahmad alimnukuu Abu Umamah رضي الله عنه kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«لَيْذُخْلَنَ الْجَنَّةَ بِشَفَاعَةِ رَجُلٍ لَيْسَ بِبَنِيِّ مِثْلُ الْحَيِّينِ - أَوْ مِثْلُ أَحَدِ الْحَيِّينِ - رَيْبَةً
وَمُضْرَةً»

“Hakika wataingia Peponi, kwa uombezi wa mtu asiyekuwa Mtume, mfano wa vijiji viwili au mfano wake, idadi inayolingana na makabila mawili au mojawapo kati ya Rabi’ah na Mudhar.”

Mtu mmoja aliuliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Rabi’ah si kabila dogo ndani ya Mudhar?” Mtume ﷺ akajibu,

«إِنَّمَا أَقُولُ مَا أَقُولُ»

“Kwa hakika ninasema ninachokisema.”¹

Imam Ahmad alinukuu kuwa ‘Abdullah bin ‘Amr رضي الله عنه alisema, “Nilikuwa nikiandika kila kitu nilichokisikia kutoka kwa Mtume ﷺ, kwa lengo la kuhifadhi. Makuraishi walinivunja moyo kuendelea na jambo hili, kwa kuniambia, ‘Wewe unanukuu kila kitu unachokisikia kutoka kwa Mtume ﷺ, ilhali yeye ni mwanaadamu na wakati mwingine huzungumza huku akiwa amekasirika.’ Niliacha kunukuu kutokana na maneno hayo, lakini baadaye nilimuambia Mtume ﷺ walichokisema Makureish, akaniambia,

«اَكْتُبْ، فَوَ الَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! مَا خَرَجَ مِنِّي إِلَّا الْحَقُّ»

“Andika! Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu ipo katika Milki Yake, kila neno litokalo kwangu ni la kweli.”²

Imam Abu Dawud pia aliikusanya Hadithi hii.³

¹ Ahmad 5:257.

² Ahmad 2:162.

³ Abu Dawud 4:60.

عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَى ﴿١﴾ ذُو مِرَّةٍ فَاسْتَوَى ﴿٢﴾ وَهُوَ بِالْأُفُقِ الْأَعْلَى ﴿٣﴾ ثُمَّ دَنَا
 فَتَدَلَّى ﴿٤﴾ فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَى ﴿٥﴾ فَأَوْحَى إِلَى عَبْدِهِ مَا أَوْحَى ﴿٦﴾ مَا كَذَبَ
 الْفُؤَادُ مَا رَأَى ﴿٧﴾ أَفَتُمَدُّونَهُ عَلَىٰ مَا يَرَى ﴿٨﴾ وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَى ﴿٩﴾ عِنْدَ
 سِدْرَةِ الْمُنْتَهَى ﴿١٠﴾ عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَى ﴿١١﴾ إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَى ﴿١٢﴾ مَا زَاغَ
 الْبَصَرُ وَمَا طَغَى ﴿١٣﴾ لَقَدْ رَأَى مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَى ﴿١٤﴾

5. Amemfundisha aliye mwingi wa nguvu,
6. Mwenye nguvu kubwa, akalingana sawa.
7. Naye yuko juu kabisa upeo wa macho.
8. Akakaribia na akateremka.
9. Akawa ni kama baina ya pinde mbili, au karibu zaidi.
10. Akamfunulia mja Wake Alichomfunulia.
11. Moyo haukusema uwongo uliyoyaona.
12. Je! Mnabishana naye kwa aliyoyaona?
13. Na akamuona mara nyingine,
14. Penye Mkunazi wa Mwisho.¹
15. Karibu yake ndiyo ipo Bustani inayokaliwa.
16. Kilipoufunika huo Mkunazi hicho kilichoufunika.
17. Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka.
18. Kwa hakika aliona katika Ishara kubwa kabisa za Mola Wake Mlezi.

¹ Sidrat Al-Muntaha: Mkunazi wa mwishoni kabisa katika mbingu ya saba ambapo hakuna kinachovuka zaidi ya hapo.

Mwalimu wa Mtume Mwaminifu ﷺ ni Roho Mwaminifu (Jibril عليه السلام)

Allah تعالى Anaeleza kuwa ni Yeye Ndiye Aliyemfundisha Mtume Wake Muhammad ﷺ kile ambacho amekuja nacho kwa watu kupitia Malaika,

شَدِيدُ الْقُوَى

“Aliye mwingi wa nguvu.”

Naye ni Jibril عليه السلام, kama alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine,

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿١٩﴾ ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ﴿٢٠﴾ مُطَاعٍ نَمَّ أَمِينٍ ﴿٢١﴾

“Kwamba hakika bila ya shaka hii ni kauli ya Mjumbe mtukufu, Mwenye nguvu na mwenye cheo kwa huyo Mwenye Kiti cha Enzi, Anayetiwa, tena muaminifu.” (81:19-21)

Allah تعالى Amesema hapa,

ذُو مِرَّةٍ

“Mwenye kutua.”

Maana yake: Mwenye nguvu, kwa mujibu wa Mujahid, Al-Hasan na Ibn Zayd.¹ Katika Hadithi sahihi kutoka kwa ‘Abdullah bin ‘Umar na Abu Hurayrah رضي الله عنهم, kuwa Mtume ﷺ alisema;

«لَا تَجِلُّ الصَّدَقَةُ لِعَنِيٍّ وَلَا لِذِي مِرَّةٍ سَوِيٍّ»

“Si halali Sadaka kupewa tajiri wala Dhu Mirrah (mtu mwenye nguvu) katika akili na mwili.”²

Allah تعالى Amesema,

فَأَسْتَوِي

“Akatulia.”

Ina maana ya Malaika Jibril عليه السلام, kwa mujibu wa Al-Hasan, Mujahid, Qatadah na Ar-Rabi’ bin Anas,³

¹ At-Tabari 22:499 na Al-Qurtubi 17:85.

² Abu Dawud 2:286 na An-Nasai 5:99.

³ At-Tabari 22:501.

وَهُوَ بِالْأَفُقِ الْأَعْلَى ﴿٥٣﴾

“Naye yuko juu kabisa upeo wa macho.”

Maana yake: Jibril عليه السلام alipanda mpaka katika sehemu ya upeo wa macho, kwa mujibu wa ‘Ikrimah na wengine; ‘Ikrimah alisema, “sehemu ya juu kabisa ya upeo wa macho ambapo machweo huanza kujitokeza.” Mujahid alisema, “Ni (mahali) jua linapochomoza.”¹

Qatadah alisema, “Mahali ambapo mchana hutokea.”² Ibn Zayd na wengine kadhaa wamesema maneno kama hayo.

Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alimuona Jibril عليه السلام katika umbo lake halisi akiwa na mbawa mia sita, kila ubawa mmoja unajaza upande mmoja wa upeo wa macho, na lulu na marijani zikianguka kutoka kila ubawa mmoja kwa kadiri ambavyo Allah تعالى Pekee Ndiye Ajuaye zaidi.”³ Imamu Ahmad peke yake aliikusanya Hadithi hii.

Imamu Ahmad alinukuu kuwa ‘Abdullah bin ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Mtume ﷺ alimuomba Jibril عليه السلام ajitokeze yeye mwenyewe akiwa katika umbo lake halisi na Jibril عليه السلام akamuambia, ‘Muombe Mola Wako.’ Mtume ﷺ alimuomba Mola Wake Mtukufu, kilidhihiri kiwingu kutoka upande wa mashariki na kuendelea kupanda na kuenea. Wakati Mtume ﷺ alipomuona Jibril عليه السلام katika umbo lake halisi, alipoteza fahamu. Jibril عليه السلام alishuka chini na kumzindua Mtume ﷺ na kumfuta mate kutoka mashavu yake.”⁴ Ahmad peke yake aliandika Hadithi hii.

¹ Al-Qurtubi 17:88.

² At-Tabari 22:501.

³ Ahmad 1:322. Isnadi yake ni dhaifu. (Al-Bukhari na Muslim waliandika sawa na hayo bila ya kutaja lulu na rubi. (Angalia masimulizi yaliyoandikwa na Ahmad 1:450, ambayo ni sawa na hayo).

⁴ Ahmad 1:322. Isnadi yake ni dhaifu, kuna Idrisa bin Munabih ambaye ni dhaifu. Taz. “Al-Taqrīb” (334) asiyezingatiwa maneno yake. Taz. “Mizan Al-Itadali” 1:149.

Maana ya Akawa “Baina ya Pinde Mbili.”

Kauli ya Allah تعالى،

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٥٣﴾

“Akawa ni kama baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi.”

Maana yake, Jibril عليه السلام alisogea karibu na Muhammad ﷺ wakati alipokuwa akimshukia duniani. Kwa wakati huo, umbali kati yao ulikuwa kiasi cha urefu wa ncha mbili za upinde, pindi pinde zinapovutwa kwa nguvu, kwa mujibu wa Mujahid na Qatadah.³ Inasemekana kuwa hii inamaanisha umbali kati ya uzi wa upinde na katikati ya fimbo.

Kauli ya Allah تعالى،

أَوْ أَدْنَىٰ

“au karibu zaidi.”

Inajulisha kuwa umbali ni kama ulivyoelezwa, si zaidi. Namna hii ya maelezo inapatikana katika sehemu nyingi ndani ya Qur’an, kama vile,

ثُمَّ قَسَتْ قُلُوبُكُمْ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَهِيَ كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدُّ قَسْوَةً

“Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo, hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi.” (2:74)

Aya inasema kuwa nyoyo zao hazikuwa laini kuliko mawe, bali ngumu zaidi kuliko mawe, na zaidi. Kuna Aya inayofanana na hiyo,

مُخَشَّوْنَ النَّاسِ كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً

“Wanawaogopa watu kama kumuogopa Mwenyezi Mungu, au kwa khofu kubwa zaidi...” (4:77),

Na Kauli ya Allah تعالى،

وَأَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ مِائَةِ أَلْفٍ أَوْ يَزِيدُونَ ﴿٣٧﴾

“Na Tulimtuma kwa watu laki moja au zaidi.” (37:147),

¹ At-Tabari 22:503 na ‘Abdur-Razzaq 3:250

Inajulisha kuwa hawakuwa chini ya laki moja, bali ni idadi hiyo au zaidi. Kwa hivyo, hii inathibitisha ukweli uliotajwa, bila ya kuacha mashaka au kumaanisha kinyume. Sawa na hivyo, Allah تعالى Amesema,

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٥٣﴾

“Akawa ni kama baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi.”

Tulishaeleza hapo awali kuwa Jibril عليه السلام ndiye aliyeteremka chini karibu na Mtume ﷺ, kwa mujibu wa Mama wa Waumini, ‘A’ishah, ‘Abdullah bin Mas’ud, Abu Dharr na Abu Hurayrah رضي الله عنهم.¹

Tutataja kauli zao kuhusu suala hili huko mbele, Inshaallah. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa ‘Abdullah bin Mas’ud عنه رضي الله عنه alisema kuhusu Aya hii,

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٥٣﴾

“Akawa ni kama baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi.”

Mtume ﷺ amesema,

«رَأَيْتُ جِبْرِيلَ لَهُ سِتْمَاةٌ جَنَاحٍ»

“Nilimuona Jibril; akiwa na mbawa mia sita.”²

Al-Bukhari alinukuu kutoka kwa Talq bin Ghannam kutoka kwa Za’idah kutoka kwa Ash-Shaybani alisema: “Nilimuuliza Zirr kuhusu Aya ifuatayo,

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٥٣﴾ فَأَوْحَىٰ إِلَىٰ عَبْدِهِ مَا أَوْحَىٰ ﴿٥٤﴾

**“Akawa ni kama baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi.
Akamfunulia mja Wake (Mwenyezi Mungu) Alichomfunulia.”**

Zirr alisema, “Abdullah alitusimulia kuwa Mtume Muhammad ﷺ, alimuona Jibril عليه السلام akiwa na mbawa mia sita.”³

¹ At-Tabari 22:504.

² At-Tabari 22:503.

³ Fat’h Al-Bari 8:476.

Kauli ya Allah تعالى,

فَأَوْحَىٰ إِلَىٰ عَبْدِهِ مَا أَوْحَىٰ ﴿١٠﴾

“Akamfunulia mja Wake Alichomfunulia.”

Maana yake: Jibril عليه السلام alifikisha kwa mja wa Allah تعالى, Mtume Muhammad ﷺ, chochote alichotakiwa kukifikisha. Au, hapa inaweza kumaanisha: Allah تعالى Alimteremshia mja Wake Muhammad ﷺ chochote Alichomteremshia kupitia kwa Jibril عليه السلام. Maana zote mbili ni sahihi. Sa’id bin Jubayr alisema juu ya Kauli ya Allah تعالى,

فَأَوْحَىٰ إِلَىٰ عَبْدِهِ مَا أَوْحَىٰ ﴿١٠﴾

“Akamfunulia mja Wake Alichomfunulia.”

Allah تعالى Alimteremshia,

أَلَمْ نَجِدَكَ يَتِيمًا فَفَآوَىٰ ﴿١١﴾

“Kwani hakukukuta yatima akakupa makaazi?” (93:6),

Na Kauli Yake,

وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ﴿١٢﴾

“Na Tukakunyanyulia utajo wako?” (94:4)¹

Mwingine alisema, “Allah تعالى Alimteremshia Mtume ﷺ kuwa hakuna Mtume mwingine atakayeingia Peponi mpaka aingie yeye kwanza, umma wake. Kisha ndio uingine Umma wa Mitume mingine.”

Je Mtume ﷺ Alimuona Mola Wake Mlezi Usiku wa Isra?

Kisha Allah تعالى Akasema,

مَا كَذَّبَ الْفُؤَادُ مَا رَأَىٰ ﴿١٣﴾ أَفَتُؤْمِنُونَهُ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ ﴿١٤﴾

“Moyo haukusema uwongo uliyoyaona. Je! Mnabishana naye kwa aliyoyaona?”

¹ Al-Qurtubi 17:52.

Muslim alinukuu kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuhusu:

مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَأَى ﴿١٠١﴾

“Moyo haukusema uwongo uliyoyaona.” Na

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَى ﴿١٠٢﴾

“Na akamuona mara nyingine.”

“Alimuona Allah تعالى mara mbili moyoni mwake.”¹ Simak alisimulia sawa na hayo kutoka kwa ‘Ikrimah kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما² Abu Swalih, As-Suddi na wengine kadha walisema sawa na hayo kuwa Mtume ﷺ alimuona Allah تعالى mara mbili moyoni mwake.³

Masruq alisema, “Nilikwenda kwa mama A’ishah رضي الله عنها na nilimuuliza, ‘Je, Muhammad ﷺ alimuona Mola Wake Mlezi,’ Akasema, ‘Umesema jambo lisababishalo nywele kusimama!’ Mimi nikasema, ‘Ngoja!’ Na nikasoma Aya hii,

لَقَدْ رَأَى مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَى ﴿١٠٣﴾

“Kwa yakini aliona katika Ishara kubwa kabisa za Mola Wake Mlezi.”

Akasema, ‘Akili yako imekwenda wapi? Alikuwa Jibril عليه السلام. Nani anayekuambia kuwa Muhammad ﷺ alimuona Mola Wake Mlezi, au ameficha sehemu yoyote katika aliyoamrisha, au alijua chochote kati ya mambo matano ambayo Allah تعالى Ameyataja,

إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُنزِّلُ الْغَيْثَ

“Hakika kujua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye Ndiye Anayeiteremsha mvua.” (31:34),

Hakika limekuwa jambo kubwa kumzulia Allah تعالى uongo, Mtume ﷺ alimuona Jibril عليه السلام mara mbili, katika umbo lake halisi, mara moja karibu na *Sidrat*

¹ Muslim 1:158.

² At-Tabari 22:507.

³ At-Tabari 22:508.

Al-Muntaha na mara nyingine katika *Ajyad* (huko Makkah), Jibril عليه السلام alikuwa na mbawa mia sita zilizotanda upeo wa macho.”¹

Muslim alinukuu kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema, “Nilimuuliza Mtume ﷺ, ‘Ulimuona Mola Wako.’ Akasema,

«نُورٌ أَنَّى أَرَاهُ»

“Nuru, nitamuona vipi?”

Katika masimulizi mengine, Mtume ﷺ alisema,

«رَأَيْتُ نُورًا»

“Nimeiona nuru.”²

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَى ۖ عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَى ۖ عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَى ۖ

“Na akamuona mara nyingine. Penye Mkunazi wa mwisho. Karibu yake ndiyo ipo Bustani inayokaliwa.”

Hii ni mara ya pili Mtume ﷺ kumuona Jibril عليه السلام katika umbo aliloubwa na Allah تعالى; ni wakati wa usiku wa Israa. Tumeshataja Hadithi kadha kuhusu Mtume ﷺ kumuona Jibril عليه السلام mwanzoni wa Surat Israa. Hakuna haja ya kuzirudia hapa. Imamu Ahmad aliandika kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه alitoa rai kuhusu Aya,

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَى ۖ عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَى ۖ

“Na akamuona mara nyingine. Penye Mkunazi wa mwisho.”

Mtume ﷺ amesema,

¹*TuhfatAl-Ahwadhi* 9:167. (Masimulizi sahihi yaliyotafsiriwa na Muslim kadhalika yapo kwa Al-Bukhari), na. 174 n1 177 na hayataji jambo la kumuona Jibril katika *Sidrah*, kama yalivyotajwa na Aya, na masimulizi yaliyofuatia ya Ibn Masud kutoka kwa ‘Asim.

²Muslim 1:161

«رَأَيْتُ جِبْرِيلَ وَلَهُ سِتْمَاءَةٌ جَنَاحٌ يَتَّبِعُ مِنْ رِيشِهِ التَّهَاقُوتُ مِنَ الدَّرِّ رَأْيَا قَوْتٍ»

“Nimemuona Jibril akiwa na mbawa mia sita na vazi la rangi ya kijani na lulu na yakuti zinapukutika kutoka kwenye manyoya yake.”¹

Hadithi hii ina isnadi nzuri na yenye nguvu. Ahmad pia alinukuu kuwa ‘Abdullah (Ibn Mas’ud رضي الله عنه) alisema, “Mtume ﷺ alimuona Jibril عليه السلام katika umbo lake halisi huku akiwa na mbawa mia sita, kila ubawa ukifunika upande mmoja wa upeo wa macho. Kutoka katika mbawa zake, mawe ya thamani yalikuwa yakidondoka kwa namna ambayo Allah تعالى Ndiye Anayejua.”²

Hadithi hii ina isnadi nzuri. Imamu Ahmad alinukuu kuwa ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ amesema,

«رَأَيْتُ جِبْرِيلَ عَلَى سِدْرَةِ الْمُنْتَهَى وَلَهُ سِتْمَاءَةٌ جَنَاحٌ»

“Nimemuona Jibril juu ya Sidrat Al-Muntaha akiwa na mbawa mia sita.”

Mmoja katika wasimulizi wa Hadithi alimuuliza ‘Asim kuhusu mbawa za Jibril عليه السلام na ‘Asim akawa anaeleza. Baadhi ya Masahaba wake waliuliza na mmoja wao akasema, “Kila ubawa mmoja ulifunika kilichokuwa baina ya mashariki na magharibi.”³

Hadithi hii ina isnadi nzuri. Imamu Ahmad alinukuu kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَتَانِي جِبْرِيلُ فِي خُضْرٍ مُعَلَّقٍ بِهِ الدَّرُّ»

“Jibril alinijia katika (akiwa amevaa) vazi la kijani huku limening’inizwa lulu”⁴

Hadithi hii ina isnadi nzuri. Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa ‘Amir alisema kuwa Masruq alimuuliza mama Aishah رضي الله عنها, “Ewe Mama wa Waumini? Je Muhammad ﷺ alimuona Mola Wake Mtukufu?” Akajibu: “Utukufu ni wa Allah تعالى! Nywele zangu zinasimama kwa sababu ya ulichokisema. Mambo matatu, ikiwa yeyote anakuambia kuhusu lolote kati ya hayo atakuwa

¹ Ahmad 1:460.

² Ahmad 1:355.

³ Ahmad 1:407.

⁴ Rejeo lililopita.

amedanganya. Anayekuambia kuwa Muhammad ﷺ amemuona Mola Wake Mlezi, atakuwa amedanganya.” Akasoma Aya hizi mbili,

لَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ

“Macho hayamfikilii bali Yeye anayafikilia macho. Naye ni Mjuzi, Mwenye Habari.” (6:103), Pia,

وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُكَلِّمَهُ اللَّهُ إِلَّا وَحْيًا أَوْ مِنْ وَرَآئِ حِجَابٍ

“Na haikuwa kwa mwanaadamu kwamba Mwenyezi Mungu Amsemeze ila kwa Wahyi (Ufunuo), au kwa nyuma ya pazia.” (42:51)

Akaendelea, “Na atakayekuambia kuwa Muhammad ﷺ alijua kesho kitatokea nini, atakuwa amedanganya.” Akasoma,

إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُنزِّلُ الْغَيْثَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ

“Hakika kuijua Saa (ya Kiyama) Kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye Ndiye Anayeiteremsha mvua. Na Anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi.” (31:34)

Mama Aishah رضي الله عنها akasema, “Na atakayekuambia kuwa Muhammad ﷺ ameficha chochote katika Ujumbe atakuwa amedanganya.” Akasoma Aya hii,

يَتَأْتِيهَا الرُّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ

“Ewe Mtume! Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi.” (5:67).

Aliendelea, “Hata hivyo, alimuona Jibril عليه السلام mara mbili katika umbo lake halisi.”¹ Imamu Ahmad pia alinukuu kuwa Masruq رضي الله عنه alisema, “Nilimuuliza mama A’ishah رضي الله عنها, ‘Je Allah تعالى Hakusema,

وَلَقَدْ رَءَاهُ بِالْأُفُقِ الْمُبِينِ

“Na hakika yeye alimuona kwenye upeo wa macho ulio safi.” (81:23), na,

¹Ahmad 6:49.

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَى ﴿٥٣﴾

“Na akamuona mara nyingine” Akasema, ‘Nilikuwa wa kwanza miongoni mwa Umami huu kumuuliza Mtume ﷺ kuhusu jambo hilo. Akasema,

«إِنَّمَا ذَاكَ جِبْرِيلُ»

“Hakika huyo ni Jibril.”

Alimuona mara mbili tu akiwa katika umbo lake halisi. Alimuona Jibril عليه السلام akishuka kutoka mbinguni kuja ardhini na alikuwa mkubwa hivyo alifunika kilichokuwa katika upeo wa macho kati ya mbingu na ardhi.¹ Hadithi hii imeandikwa katika Sahih Mbili kupitia kwa Ash-Sha’bi.²

Malaika, Nuru na Rangi Viliifunika Sidrat Al-Muntaha

Allah تعالى Amesema,

إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَى ﴿٥٤﴾

“Kilipoufunika huo Mkunazi hicho kilichoufunika.”

Tumetaja hapo awali, katika Hadithi kuhusu *Al-Isra’* kuwa Malaika, Nuru ya Allah تعالى, na rangi za kuvutia ziliifunika *Sidrah*. Imamu Ahmad alinukuu kuwa ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Pindi Mtume ﷺ alipochukuliwa katika Safari ya *Isra’*, alipanda juu mpaka katika *Sidrat Al-Muntaha*, ambayo iko katika mbingu ya saba. Hapo huishia kila kinachopanda kutoka ardhini na kuzuiwa hapo, na huzuiwa kila kinachoteremka kutoka juu yake huzuiwa hapo,

إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَى ﴿٥٤﴾

“Kilipoufunika huo Mkunazi hicho kilichoufunika.”

Akasema, “vipepeo wa dhahabu.” Mtume ﷺ alipewa vitu vitatu: alipewa Sala tano, alipewa Aya za mwishoni mwa *Surat Al-Baqarah* (2:284-286), na msamaha wa dhambi kwa watu miongoni mwa umami wake wasiomshirikisha Allah تعالى na chochote.³ Muslim aliikusanya Hadithi hii.

¹ Ahmad 6:241

² *Fat’h Al-Bari* 8:472 na Muslim 1:359

³ Ahmad 1:422

Kauli ya Allah تعالى,¹

مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ

“Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka.”

Inajulisha kuwa jicho la Mtume ﷺ halikugeuka kulia wala kushoto, kwa mujibu wa ‘Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما,²

وَمَا طَغَىٰ

“Wala halikuruka mpaka.”

Bila ya kuzidisha katika alichofaradhishiwa. Hii ni sifa kubwa inayoonesha uimara wa Mtume ﷺ kumuabudu Allah تعالى, kwa sababu yeye alikifanya kile alichoaamrisha, na hakuomba zaidi ya alivyopewa. Kauli ya Allah تعالى,

لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَىٰ

“Kwa yakini aliona katika Ishara kubwa kabisa za Mola Wake Mlezi.”

Inalingana na Aya nyingine,

لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا

“ili Tumuoneshe baadhi ya Ishara Zetu.” (17:1),

Maana yake: Ishara zinazothibitisha Nguvu na Uweza wa Allah تعالى. Wakiegemea juu ya Aya hizi mbili. Baadhi ya wanazuoni wa *Ahlu-Sunnah* walisema kuwa Mtume ﷺ hakumuona Allah تعالى wakati wa Safari ya Isra.’ Kwa sababu Allah تعالى Amesema,

لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَىٰ

“Kwa yakini aliona katika Ishara kubwa kabisa za Mola Wake Mlezi.”

Walisema kuwa, Mtume ﷺ angemuona Mola Wake Mlezi, angewaambia watu.

¹ Muslim 1:157.

² At-Tabari 22:521.

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ﴿١٩﴾ وَمَنْوَةَ الثَّالِثَةَ الْآخَرَىٰ ﴿٢٠﴾ أَلَكُمُ الذَّكْرُ وَلَهُ الْأُنثَىٰ ﴿٢١﴾
 تِلْكَ إِذًا قِسْمَةٌ ضِيزَىٰ ﴿٢٢﴾ إِنَّ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءُ سَمَّيْتُمُوهَا أَنْتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا
 مِنْ سُلْطَانٍ ۚ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْأَنْفُسُ ۗ وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنْ رَبِّهِمْ الْهُدَىٰ
 ﴿٢٣﴾ أَمْ لِلْإِنْسَانِ مَا تَمَنَّىٰ ﴿٢٤﴾ فَلِلَّهِ الْآخِرَةُ وَالْأُولَىٰ ﴿٢٥﴾ * وَكَمْ مِنْ مَلَكٍ فِي
 السَّمَوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِنْ بَعْدِ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَرْضَىٰ ﴿٢٦﴾

19. Je! Mmemuona Lata na Uzza?

20. Na Manata, mwingine wa tatu?

21. Je! Nyinyi mnao wana wanaume na Yeye ndio awe na wanawake?

22. Huo ni mgawanyo wa dhulma!

23. Hayo hayakuwa ila ni majina mliyowapa nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu Hakuleta uthibitisho wowote juu ya hayo. Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi. Na kwa yakini uwongofu ulikwishawafikia kutoka kwa Mola wao Mlezi.

24. Ati mtu anaweza kupata kila anachokitamani?

25. Mwenyezi Mungu tu Ndiye Mwenye dunia na Akhera.

26. Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi Mungu Kutoa idhini kwa Amtakaye na Kumridhia.

Majibu Dhidi ya Washirikina na Ubainifu wa Al-Lat na Al-'Uzza

Allah تعالى Amesema Akiwakemea washirikina katika kuabudu masanamu na kumuekea washindani. Wanayajengea nyumba masanamu yao kwa kuiga Ka'abah iliyojengwa na Nabii Ibrahim عليه السلام, Kipenzi cha Allah تعالى.

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ

“Je! Mmemuona Lata?”

Al-Lat lilikuwa ni jiwe jeupe lililonakishiwa katika mji wa Al-Taif. Na kujengewa nyumba juu yake, yenye mapazia, watumishi na eneo wanalolitukuza na

kuliadhimisha watu wa At-Taif, ambao ni kabila la Thaqif na marafiki zao, walimabudu Al-Lat. Walikuwa wakijigamba kwa Waarabu, isipokuwa Makuraishi, kuwa walikuwa na Al-Lat. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Jina la Al-Lat wamelitohoa kutokana na Jina la Allah تعالى, na kulifanya la kike. Allah تعالى Ametakasika mbali na wanayomnasibisha nayo. Iliripotiwa kuwa Al-Lat hutamkwa Al-Lat kwa sababu, kwa mujibu wa ‘Abdullah bin ‘Abbas, Mujahid, na Ar-Rabi’ bin Anas, Al-Lat alikuwa mtu aliyekuwa akichanganya *Sawiq* (namna ya togwa ya shayiri) na maji kwa ajili ya wenye kuhiji wakati wa Jahiliyyah. Alipofariki, wao walibakia karibu na kaburi lake wakamuabudu yeye.”¹ Al-Bukhari alinukuu kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema juu ya Kauli ya Allah تعالى,

أَلَلَّتْ وَالْعَزَىٰ

“*Lata na Uzza?*”

“Al-Lat alikuwa mtu aliyekuwa akichanganya *Sawiq* kwa ajili ya wenye kuhiji.”² Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “walilitohoa jina la sanamu lao Al-’Uzza kutokana na Jina la Allah Al-’Aziz. Al-’Uzza ulikuwa mti ambao juu yake uliwekwa mnara na mapazia, katika eneo la Nakhlah, kati ya Makkah na At-Ta’if. Makuraishi walimnyenyekea Al-’Uzza.”³ Wakati wa vita vya Uhud, Abu Sufyan alisema, “Sisi tunaye Al-’Uzza, lakini wewe huna Al-’Uzza.” Mtume ﷺ akajibu,

«قُولُوا: اللَّهُ مَوْلَانَا وَلَا مَوْلَىٰ لَكُمْ»

“*Semeni, “Allah ni Mlinzi Wetu, lakini nyinyi hamna mlinzi.”*”⁴

Manat lilikuwa sanamu jingine katika eneo la Mushallal karibu na Qudayd, kati ya Makkah na Al-Madinah. Makabila ya Khuza’ah, Aws na Khazraj yalikuwa yakilinyenyekea wakati wa Jahiliyyah. Walikuwa wakitangaza Hija katika Ka’bah kutokea jirani ya Manat. Al-Bukhari alisimulia kauli ya mama A’ishah yenye maana hii.⁴ Kulikuwa na masanamu mengine katika Rasi ya Uarabuni ambayo Waarabu waliyatukuza kama walivyoyitukuza Ka’bah, licha ya masanamu matatu aliyoyataja Allah تعالى katika Kitabu Chake Kitukufu. Allah

¹ At-Tabari 22:523.

² *Fat’h Al-Bari* 8:478.

³ At-Tabari 22:523.

⁴ *Fat’h Al-Bari* 6:188.

⁵ *Fat’h Al-Bari* 8:479.

تعالى Aliyataja masanamu haya matatu kwa sababu yalikuwa maarufu kuliko mengine. An-Nasa'i alinukuu kuwa Abu At-Tufayl alisema, "Mtume ﷺ alipoikomboa Makkah, alimtuma Khalid bin Al-Walid رضي الله عنه kwenda Nakhlah ambapo sanamu Al-'Uzza lilikuwa limesimamishwa juu ya miti mitatu msituni. Khalid رضي الله عنه alikata miti hiyo mitatu na akaisogelea nyumba iliyojengwa kulizunguka na akaiharibu. Aliporejea kwa Mtume ﷺ na kumjulisha habari hiyo, Mtume ﷺ alimuambia,

«ارْجِعْ فَإِنَّكَ لَمْ تَصْنَعْ شَيْئًا»

"Rudi, kwani wewe hujafanya kitu."

Khalid رضي الله عنه alirudi na pale walinzi waliokuwa watumishi wa Al-'Uzza walipomuona, walianza kuomba kwa kumuita Al-'Uzza!. Khalid رضي الله عنه alipolikaribia lile sanamu alikuta mwanamke akiwa uchi na nywele timtim na alikuwa akijirushia mchanga kichwani mwake. Khalid رضي الله عنه akamuua kwa upanga, akarudi kwa Mtume ﷺ, ambaye alimuambia,

«بَلِّغْ الْعُرَى!»

"Huyo 'Uzza!"¹

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى amesimulia, "Al-Lat lilikuwa sanamu la kabila la Thaqif katika eneo la At-Ta'if. Banu Mu'attib walikuwa walinzi wa Al-Lat na pia watumishi wake."²

Inasemwa kwamba Mtume ﷺ aliwatuma Al-Mughirah bin Shu'bah na Abu Sufyan Sakhr bin Harb kulivunja Al-Lat. Walipokea amri ya Mtume na wakajenga msikiti mahali hapo katika mji wa At-Ta'if. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema kuwa Manat lilikuwa sanamu la makabila ya Aws na Khazraj, na makabila mengine yaliyofuata dini yao katika Yathrib (Al-Madinah). Sanamu Manat lilikuwa karibu na pwani, jirani na eneo la Mushallal katika mji wa Qudayd. Mtume ﷺ alimtuma Abu Sufyan Sakhr bin Harb au 'Ali bin Abu Talib رضي الله عنه kulivunja. Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alisema kuwa Dhul-Khalasah lilikuwa

¹ An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:474. Abu Ya'la na 902. imethibitishwa kuwa Abu At-Tufail alimwona Mtume ﷺ, lakini si kusikia chochote kutoka kwake

² Ibn Hisham 1:87

sanamu la makabila ya Daws, Khath'am na Bajilah, na Waarabu walioishi katika eneo la Tabalah.¹ Inasemwa kuwa Dhul-Khalasah liliitwa Ka'bah ya Kusini, na Ka'bah ya Makkah iliitwa Ka'bah ya Kaskazini. Mtume ﷺ alimtuma Jarir bin 'Abdullah Al-Bajali رضي الله عنه kwa Dhul-Khalasah na akalivunja. Ibn Is-haq alisema kuwa Fals lilikuwa sanamu la Tay' na makabila ya jirani katika Mlima Tay', kama vile Salma na Ajja. Ibn Hisham alisema kuwa baadhi ya wanazuoni walimuambia kuwa Mtume ﷺ alimtuma 'Ali bin Abu Talib رضي الله عنه kwa Fals, naye akalivunja na akakuta mapanga mawili katika hazina yake, ambayo baadaye Mtume ﷺ alimpa 'Ali رضي الله عنه kama ngawira. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى pia alisema kuwa makabila ya Himyar, na watu wa Yemen kwa ujumla wake, walikuwa na nyumba ya ibada huko San'a' iliyoitwa Riyam. Alieleza kulikuwa na mbwa mweusi ndani yake na kuwa watu wa dini waliokwenda na Tubba' walimuondoa, wakamuua na wakavunja ile nyumba. Ibn Is-haq alisema kuwa Rudha' lilikuwa jengo la Bani Rabi'ah bin Ka'b bin Sa'd bin Zayd Manat bin Tamim,² ambalo Al-Mustawghir bin Rabi'ah bin Ka'b bin Sa'd alilivunja baada ya kusilimu. Huko Sandad kulikuwa na Dhul-Ka'bat, sanamu la makabila ya Bakr na Taghlib, wana wa Wa'il, na pia kabila la Iyad.

Kuwakanusha Washirikina Wanaoyapa Masanamu Yao Sifa ya Kiume na Kudai Kuwa Malaika ni Wanawake

Allah تعالى Amesema,

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ﴿١٦﴾ وَمَنْوَةَ الثَّالِثَةَ الْآخَرَیٰ ﴿١٧﴾

Je! Mmemuona Lata na Uzza? Na Manaat, mwingine wa tatu?

Kisha Allah تعالى Amesema,

أَلَكُمُ الذَّكْرُ وَلَهُ الْأُنثَىٰ ﴿١٨﴾

“Je! Nyinyi mnao wana wanaume na Yeye ndio awe na wanawake?”

Allah تعالى Aliwauliza washirikina, 'Mnamchagulia Allah تعالى watoto wa kike nanyi mnapendelea wa kiume, ikiwa kama hivi mnagawana na viumbe wengine mfano wenu, basi huo unakuwa,

¹ Ibn Hisham 1:87.

² Ibn Hisham 1:89.

قِسْمَةٌ ضِيزَىٰ

“Mgawanyo wa dhulma!”

Maana yake: Unakuwa mgawanyo wa upendeleo na dhuluma. ‘Inakuwaje basi mnafanya mgao huu kati yenu na Mola wenu Mlezi ambao lau ungekuwa baina ya viumbe ungekuwa wa kipumbavu na dhuluma.

Kisha Allah تعالى Anakanusha uongo huo uliozushwa, upotovu na ukanaji ukweli uliozushwa kutokana na kuabudu masanamu kwa kuyaita miungu,

إِنَّ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنْتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ

“Hayo hayakuwa ila ni majina mliyowapa nyinyi na baba zenu.”

Kwa utashi wenu.

مَا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطَانٍ

“Mwenyezi Mungu Hakuleta uthibitisho wowote juu ya hayo.”

Maana yake: Ushahidi,

إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْأَنْفُسُ

“Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi.”

Wao hawana ushahidi, isipokuwa kuwaamini mababu zao walioifuata njia hii potofu hapo zamani, halikadhalika, ndoto na tamaa zao za kuwa viongozi, na hapa tena wapate utukufu na heshima kutokana na mababu zao.

وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنْ رَبِّهِمْ الْهُدَىٰ

“Na kwa yakini uwongofu ulikwishawafikia kutoka kwa Mola wao Mlezi.”

Maana yake: Allah تعالى Aliwatuma kwao Mitume wakiwa na ukweli na ushahidi usiopingika.

Hata hivyo, wao hawakuushikilia au kuufuata uongofu uliowajia kupitia kwa Mtume ﷺ.

Mawazo ya Kutamani Hayamfanyi Mtu kuwa Muadilifu

Allah تعالى Amesema,

أَمْ لِلْإِنْسَانِ مَا تَمَنَّى ﴿٥٣﴾

“Ati mtu anakipata kila anachokitamani?”

Aya inaeleza wazi kuwa si kila mtu anapata kila kizuri anachokitamani,

لَيْسَ بِأَمَانِيكُمْ وَلَا أَمَانِي أَهْلُ الْكِتَابِ ۗ

“Si kwa matamano yenu, wala matamano ya Watu wa Kitabu!”

(4:123)

Allah تعالى Anasema, si kila mtu anayedai kaongoka basi ni kweli kaongoka, na si kila mtu anayepata anachokitamani kwa ajili ya nafsi yake.

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا تَمَنَّى أَحَدُكُمْ فَلْيَنْظُرْ مَا يَتَمَنَّى، فَإِنَّهُ لَا يَدْرِي مَا يُكْتَبُ لَهُ مِنْ أَمْرِيهِ»

“Mmoja wenu atakapotamani kitu awe mwangalifu na anachokitamani kwani hajui ataandikiwa nini kutokana na anachokitamani.”¹

Ahmad peke yake aliikusanya Hadithi hii. Kauli ya Allah تعالى,

فَلِلَّهِ الْآخِرَةُ وَالْأُولَى ﴿٥٤﴾

“Mwenyezi Mungu tu Ndiye Mwenye dunia na Akhera.”

Maana yake: Mambo yote ni ya Allah تعالى na Yeye ni Mfalme na Mmiliki wa dunia na Akhera, Ambaye Hufanya Alitakalo kuwa na Asilolitaka kutokuwa.

¹Ahmad 2:357. Isnadi yake ni dhaifu. Sheikh Albani ameidhofisha. Taz. “Adhaifu” (2255).

Hakuna Uombezi Isipokuwa kwa Idhini ya Allah تعالى

Allah تعالى Amesema,

وَكَمْ مِنْ مَلَكٍ فِي السَّمَوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِنْ بَعْدِ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ
وَيَرْضَى ۗ

“Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi Mungu Kutoa idhini kwa Amtakaye na Kumridhia.”

Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine;

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ

**“Ni nani huyo awezaye kuombea mbele Yake bila ya idhini Yake?”
(2:255) Na,**

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ ۗ

“Wala uombezi mbele Yake hautafaa kitu, isipokuwa kwa Aliyempa idhini.” (34:23)

‘Ikiwa hii ndiyo hali ya Malaika walio karibu Naye, mtakuwaje nyinyi, enyi wajinga mnaotumaini Allah تعالى Akukubalieni uombezi wa masanamu na washindani mnaowaabudu na kumshi rikisha Yeye bila ya kupewa idhini Yake au mamlaka ya kuwaabudu hao, bali, Allah تعالى Ameharamisha kuabudu sanamu kupitia ndimi za Mitume Wake na Aliteremsha kuharamisha huko katika vitabu Vyake.

* * *

إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ لَيَسْمُونَ الْمَلَائِكَةَ تَسْمِيَةً
 الْأُنثَى ﴿٤٧﴾ وَمَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ
 وَإِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا ﴿٤٨﴾ فَأَعْرِضْ عَنْ مَنْ
 تَوَلَّىٰ عَنْ ذِكْرِنَا وَلَمْ يُرِدْ إِلَّا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٤٩﴾ ذَلِكَ
 مَبْلَغُهُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ
 سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اهْتَدَىٰ ﴿٥٠﴾ وَلِلَّهِ مَا فِي
 السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَوُوا بِمَا عَمِلُوا
 وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَىٰ ﴿٥١﴾ الَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبِيرَ
 الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ إِلَّا اللَّمَمَ إِنَّ رَبَّكَ وَاسِعُ الْمَغْفِرَةِ هُوَ
 أَعْلَمُ بِكُمْ إِذْ أَنشَأَكُم مِّنَ الْأَرْضِ وَإِذْ أَنتُمْ أَجْنَةٌ فِي
 بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ فَلَا تُرْكُوا أَنفُسَكُمْ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اتَّقَىٰ
 ﴿٥٢﴾ أَفَرَأَيْتَ الَّذِي تَوَلَّىٰ ﴿٥٣﴾ وَأَعْطَىٰ قَلِيلًا وَأَكْدَىٰ
 ﴿٥٤﴾ أَعِنْدَهُ عِلْمُ الْغَيْبِ فَهُوَ يَرَىٰ ﴿٥٥﴾ أَمْ لَمْ يُدَبَّرْ بِمَا
 فِي صُحُفِ مُوسَىٰ ﴿٥٦﴾ وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّىٰ ﴿٥٧﴾ أَلَمْ تَرَ
 وَازِرَةً وَّرَزَّ أُخْرَىٰ ﴿٥٨﴾ وَأَنْ لَّيْسَ لِلْإِنْسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ
 ﴿٥٩﴾ وَأَنْ سَعِيدهُ سَوْفَ يُرَىٰ ﴿٦٠﴾ ثُمَّ يُجْزَاهُ الْجَزَاءَ
 الْأَوْفَىٰ ﴿٦١﴾

إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ
 لَيَسْمُونَ الْمَلَائِكَةَ تَسْمِيَةً
 الْأُنثَى ﴿٤٧﴾ وَمَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ
 إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ
 وَإِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ
 شَيْئًا ﴿٤٨﴾ فَأَعْرِضْ عَنْ مَنْ تَوَلَّىٰ
 عَنْ ذِكْرِنَا وَلَمْ يُرِدْ إِلَّا الْحَيَاةَ
 الدُّنْيَا ﴿٤٩﴾ ذَلِكَ مَبْلَغُهُمْ مِنَ الْعِلْمِ
 إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ
 سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اهْتَدَىٰ ﴿٥٠﴾

27. Hakika wasioamini
 Akhera bila ya shaka wao
 ndio wanawaita Malaika
 kwa majina ya kike.

28. Nao hawana ujuzi
 wowote kwa hayo isipokuwa
 wanafuata dhana tu. Na
 dhana haisaidii chochote
 mbele ya haki.

29. Basi muachilie mbali
 anayeupa kisogo ukumbusho
 wetu, na wala hataki ila
 maisha ya dunia.

30. Huo ndio mwisho wao wa ujuzi. Hakika Mola Wako Mlezi Ndiye
 Anayemjua zaidi mwenye kuipotea njia Yake, na Yeye Ndiye Anayemjua
 zaidi mwenye kuongoka.

Kukanusha Madai ya Washirikina kuwa Malaika ni Watoto wa Kike wa Allah

Allah تعالى Anawawaonya washirikina kutokana na kuwazulia Malaika majina ya kike na kudai kuwa wao ni watoto wa kike wa Allah تعالى. Allah تعالى Ameepukana mbali na wanayomzushia. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَجَعَلُوا الْمَلَائِكَةَ الَّذِينَ هُمْ عِبَادُ الرَّحْمَنِ إِنْتًا أَشْهَدُوا خَلْقَهُمْ ۖ سَتُكْتَبُ شَهَادَتُهُمْ
وَدُسُّوْنَ

“Na wakawafanya Malaika, ambao ni waja wa Mwingi wa Rehema, ni wanawake! Kwani wameshuhudia kuumbwa kwao? Ushahidi wao utaandikwa na wao watahojiwa!” (43:19)

Na kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Amesema;

وَمَا هُمْ بِمِنَ عِلْمٍ

“Nao hawana ujuzi.”

Maana yake: Hawana elimu sahihi ya kuthibitisha kauli zao. Wanachokisema ni uongo mtupu, upotevu, udanganyifu na ukafiri wa kutisha.

إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ ۖ وَإِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا

“Isipokuwa wanafuata dhana tu. Na dhana haisaidii chochote mbele ya haki.”

Maana yake: Dhana haina faida wala haisimami mahali pa ukweli. Na hakika imethibiti Hadithi iliyonukuliwa katika Sahih, Mtume ﷺ amesema,

«إِيَّاكُمْ وَالظَّنَّ، فَإِنَّ الظَّنَّ أَخَذَبُ الْحَدِيثِ»

“Jihadharini na dhana kwani dhana ni uongo zaidi wa mazungumzo.”¹

¹ Fat’h Al-Bari 5:441.

Amri ya Kuwapuuza Watu wa Batili

Kauli ya Allah تعالى،

فَأَعْرَضَ عَنْ مَنْ تَوَلَّىٰ عَنْ ذِكْرِنَا

“Basi muachilie mbali anayeupa kisogo ukumbusho wetu.”

Maana yake: Kaa mbali na wale wanaouacha ukweli na uachane nao.

وَلَمْ يُرِدْ إِلَّا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا

“Na wala hataki ila maisha ya dunia.”

Maana yake: Ambaye shughuli zake nyingi na elimu yake ni dunia; hili ndilo lengo la wale wasio na kheri ndani yao,

ذَٰلِكَ مَبْلَغُهُمْ مِنَ الْعِلْمِ

“Huo ndio mwisho wao wa ujuzi.” Maana yake: Kuyatafuta maisha ya dunia na kufanya bidii katika mambo yake ndio elimu bora waliyoipata. Na kuna dua iliyoripotiwa:

«اللَّهُمَّ لَا تَجْعَلِ الدُّنْيَا أَكْبَرَ هَمِّنَا، وَلَا مَبْلَغَ عِلْمِنَا»

“Ewe Mola! Usijaaalie dunia kuwa ndio lengo letu kubwa wala ukomo wa elimu yetu.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ اهْتَدَىٰ

“Hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Anayemjua zaidi mwenye kuipotea njia Yake, na Yeye Ndiye Anayemjua zaidi mwenye kuongoka.”

Maana yake: Yeye ni Muumba wa viumbe wote na Anajua chenye Kuwanufaisha waja Wake. Allah تعالى ni Mmoja Anayeongoa Amtakaye na kumuacha kupotoka Anayemtaka. Na Aya hii inaashiria Nguvu, Ujuzi, Elimu na Hekima za Allah تعالى. Kwa hakika, Yeye ni Mwadilifu na kamwe Hatoi hukumu au Kupitisha jambo kwa dhuluma.

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 9:476.

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ لِيَجْزِيَ الَّذِيْنَ اَسْتَوٰٓا۟ بِمَا عَمِلُوْا وَيَجْزِيَ الَّذِيْنَ اَحْسَنُوْا بِالْحَسَنٰٓى ﴿٣١﴾ الَّذِيْنَ يَجْتَنِبُوْنَ كَبِيْرَ الْاِثْمِ وَالْفَوٰحِشِ اِلَّا اللَّغْمَ ۗ اِنَّ رَبَّكَ وَسِعُ الْمَغْفِرَةِ ۗ هُوَ اَعْلَمُ بِكُمْ اِذْ اَنْشَأَكُمْ مِّنَ الْاَرْضِ وَاِذْ اَنْتُمْ اَجْنٰةٌ فِى بُطُوْنِ اُمَّهَاتِكُمْ ۗ فَلَا تُزَكُّوْا اَنْفُسَكُمْ ۗ هُوَ اَعْلَمُ بِمَنْ اَتَقٰٓى ﴿٣٢﴾

31. Ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda, na waliotenda mema Awalipe mema.

32. Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vichafu, isipokuwa makosa khafifu. Hakika Mola Wako Mlezi ni Mkunjufu wa maghufira. Naye Anakujueni sana tangu Alipokuumbeni kutoka kwenye ardhi, na mlipokuwa mimba matumboni mwa mama zenu. Basi msijisifu usafi wa nafsi zenu. Yeye Anamjua sana mwenye kujikinga na maovu.

Allah تعالیٰ Anajua Kila Kitu, Kidogo na Kikubwa, na Anamjazi Kila Mmoja kwa Mujibu wa Matendo Yake.

Allah تعالیٰ Anaeleza Yeye ni Mmiliki wa mbingu na ardhi na kuwa Yeye Amejitosheleza. Yeye ni Hakimu kwa viumbe Wake na Anawatawala kwa uadilifu. Ameumba viumbe kwa haki.

لِيَجْزِيَ الَّذِيْنَ اَسْتَوٰٓا۟ بِمَا عَمِلُوْا وَيَجْزِيَ الَّذِيْنَ اَحْسَنُوْا بِالْحَسَنٰٓى

“Ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda, na waliotenda mema Awalipe mema.”

Anamjazi kila mmoja kwa amali zake, ikiwa kheri basi atalipwa wema na kama shari atalipwa kwa adhabu.

Sifa za Waja Wema, na Kusamehewa Makosa Madogo na Sio Makubwa

Kisha Allah تعالیٰ Akafasiri kuwa watenda wema ni wale wanaojiepusha na dhambi kubwa na machafu katika maadili. Wakati mwingine huwa wanafanya makosa madogo lakini wanasamehewa madhambi hayo madogo madogo na wanasitiriwa. Kama Allah تعالیٰ Alivyosema katika Aya nyingine;

إِن تَجْتَبُوا كَبَائِرَ مَا تُهَوِّنَ عَنْهُ نُكْفِرْ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَنُدْخِلْكُمْ مُدْخَلًا كَرِيمًا ﴿٣١﴾

“Mkiyaepuka makubwa mnayokatanzwa. Tutakufutieni makosa yenu madogo, na Tutakingizeni mahali patukufu.” (4:31)

Allah تعالی Amesema katika Aya hii,

الَّذِينَ تَجْتَنِبُونَ كَبَائِرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ إِلَّا اللَّعَمَ ۗ

“Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vichafu, isipokuwa makosa khafifu.”

Al-Lamam maana yake, makosa na dhambi ndogondogo. Imamu Ahmad alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Sijapata kuona kitu chochote kinachofanana na *Al-Lamam* iliyo bora kuliko Hadithi aliyoisimulia Abu Hurayrah رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى كَتَبَ عَلَى ابْنِ آدَمَ حَظَّهُ مِنَ الزَّانَا، أَدْرَكَ ذَلِكَ لَا مَحَالَةَ، فَرَزْنَا الْعَيْنِ النَّظْرُ، وَزَنَا اللِّسَانَ التُّطُقُ، وَالنَّفْسُ تَتَمَنَّى وَتَشْتَهِي، وَالْفَرْجُ يُصَدِّقُ ذَلِكَ أَوْ يُكَذِّبُهُ»

“Hakika Allah Mtukufu Amehukumu juu ya mwanaadamu atapata fungu lake katika zinaa wala hilo halina shaka kabisa. Zina ya jicho ni kuangalia, zina ya ulimi ni kutamka, nafsi inatamani na kuwa na tamaa, na utupu husadikisha hilo au kulikataa.”¹

Hadithi hii imeandikwa katika Sahih Mbili.² Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Macho huzini kwa kuangalia, midomo kwa kubusu, mikono kwa kutenda dhambi, miguu kwa kutembea, na utupu ama kuithibitisha au kukataa. Pindi mtu anapozini, atakuwa ni mtu anayezini, vinginevyo ni *Al-Lamam*.”³ Pia Masruq na Ash-Sha’bi walitoa rai sawa na hii.⁴ ‘Abdur-Rahman bin Nafi’, aliyejulikana kama Ibn Lubabah At-Ta’ifi pia, alisema, nilimuuliza Abu Hurayrah رضي الله عنه kuhusu Kauli ya Allah تعالی,

إِلَّا اللَّعَمَ ۗ

“Isipokuwa makosa khafifu.” Akanijibu, ‘Yanafungamana na kubusu,

¹ Ahmad 2:276

² *Fat’h Al-Bari* 11:28 na Muslim 4:2046

² At-Tabari 22:537

³ At-Tabari 22:537

kukonyeza, kutazama na kukumbatia. Pindi utupu unapokutana na utupu mwingine inapasa kuoga na hiyo ndiyo zinaa.”¹

Kuhamasisha Toba na Kukatazwa Mtu Kujisifu

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ رَبَّكَ وَاسِعُ الْمَغْفِرَةِ

“Hakika Mola Wako Mlezi ni Mkunjufu wa maghufira.”

Anasema kuwa rehema Zake zinaenea kila kitu na msamaha Wake huwezekana kwa kila jambo, ikiwa mtu atatubu,

قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ
جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٥٣﴾

“Sema: Enyi waja Wangu waliojidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na Rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.” (39:53)

Allah تعالى Amesema,

هُوَ أَعْلَمُ بِكُمْ إِذْ أَنشَأَكُم مِّنَ الْأَرْضِ

“Naye Anakujueni sana tangu Alipokuumbeni kutoka kwenye ardhi.”

‘Yeye Anawaona nyinyi, ni Mjuzi wa matendo na maneno yenu na yanayotokana nanyi, tangu Alipomuumba Adam kutoka ardhini na Akawatoa wanawe kutoka katika kiuno chake, wakiwa wadogo kama mchwa. Akawagawanya katika makundi mawili, kundi la Peponi na kundi la Motoni.’

وَإِذْ أَنشَأْتُمُ أَجْنَةً فِي بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ

“Na mlipokuwa mimba matumboni mwa mama zenu.”

Pale Alipompa amri Malaika aandike riziki, umri na matendo ya kila mja kama atakuwa miongoni mwa watu waovu au wema. Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 22:537

فَلَا تُزَكُّوْا اَنْفُسَكُمْ

“Basi msijisifu usafi.” Anakataza mtu kujisifu yeye mwenyewe na kujifikiria kuwa yuko juu kwa amali zake,

هُوَ اَعْلَمُ بِمَنْ اَنْتَقَى

“Yeye Anamjua sana mwenye kujikinga na maovu.” Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ يُزَكُّوْنَ اَنْفُسَهُمْ ۗ بَلِ اللّٰهُ يُزَكِّيْ مَنْ يَّشَاءُ وَلَا يُظْلَمُوْنَ فَتِيْلًا ﴿٤٩﴾

“Jee huwaoni wale wanaodai kuwa ati wametakasika? Bali Mwenyezi Mungu Humtakasa Amtakaye. Na hawatadhulumiwa hata kadiri ya kijiuzi kilichomo ndani ya uwazi wa kokwa ya tende.” (4:49)

Katika Sahih yake, Muslim alinukuu kuwa Muhammad bin ‘Amr bin ‘Ata alisema, “Nilimuita binti yangu, *Barrah* (mwema), na Zaynab bint Abu Salamah akaniambia, ‘Mtume ﷺ amekataza kutumia jina la aina hii. Mwanzoni, mimi niliitwa *Barrah* akaniambia,

«لَا تُزَكُّوْا اَنْفُسَكُمْ، اِنَّ اللّٰهَ اَعْلَمُ بِاَهْلِ الْبَيْرِ مِنْكُمْ»

“Msizitakase Nafsi zenu, Hakika Allah ni Mjuzi zaidi wa mtu mwema miongoni mwenu.”

Wakasema, ‘Tumuite nani,’ Yeye akasema,

«سَمُّوْهَا زَيْنَبُ»

“Muiteni Zaynab.”¹

Imamu Ahmad alinukuu Hadithi kutoka kwa ‘Abdur-Rahman bin Abu Bakrah, kutoka kwa baba yake aliyesema, “Mtu mmoja alimsifu mtu mwingine mbele ya Mtume. Mtume ﷺ akasema,

«رَيْلَكَ قَطَعْتَ عُنُقَ صَاحِبِكَ - مَرَارًا - اِذَا كَانَ اَحَدُكُمْ مَادِحًا صَاحِبَهُ لَا مَحَالَةَ، فَلْيَقُلْ: اَحْسِبْ فَلَانَا وَاللّٰهُ حَسِيْبُهُ، وَلَا اَرْكَبْ عَلٰى اللّٰهِ اَحَدًا، اَحْسِبُهُ كَذَا وَكَذَا، اِنْ كَانَ يَعْلَمُ ذَلِكَ»

¹ Muslim 3:1687

“Ole wako! Umekata shingo ya rafiki yako (akakariri maneno haya) ikiwa mmoja wenu anamsifu rafiki yake, ikiwa ni lazima amsifu, basi aseme, “Nadhani fulani ni hivi na vile; Allah Anajua zaidi kumhusu yeye, wala sitamtakasa yeyote kwa Allah,’ ikiwa anamjua rafiki yake kama alivyoeleza.”¹

Al-Bukhari, Muslim, Abu Dawud na Ibn Majah waliikusanya Hadithi hii.² Imamu Ahmad alinukuu kuwa Hammam bin Al-Harith alisema, “Mtu mmoja alikuja kwa ‘Uthman bin ‘Affan رضي الله عنه na akamsifu. Al-Miqdad bin Al-Aswad akaanza kumrushia mtu yule mchanga usoni, huku akisema, ‘Mtume ﷺ alituumuru tuwarushie mchanga usoni tunapowaona watu wenye kusifia.”³ Muslim na Abu Dawud pia waliikusanya Hadithi hii.⁴

أَفْرَأَيْتَ الَّذِي تَوَلَّى ۖ وَأَعْطَى قَلِيلًا وَأَكْدَى ۚ ۝ أَعِنْدَهُ عِلْمُ الْغَيْبِ فَهُوَ يُرَىٰ ۚ ۝
 ۝ أَمْ لَمْ يُنَبِّأْ بِمَا فِي صُحُفِ مُوسَىٰ ۚ ۝ وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّىٰ ۚ ۝ أَلَّا تَنْزُرُوا بِرِزْقِ
 ۝ وَرَزَقَ آخَرَ ۚ ۝ وَأَنْ لَّمْ يَسْئَلْ لِّلْإِنْسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ۚ ۝ وَأَنَّ سَعْيَهُ سَوْفَ يُرَىٰ ۚ ۝ ثُمَّ
 ۝ يُجْزَاهُ الْجَزَاءَ الْأَوْفَىٰ ۚ ۝

33. Je! Umemuona yule aliyegeuka?

34. Na akatoa kidogo, akajizua?

35. Je! Anayo huyo ilimu ya ghaibu, basi ndio anaona?

36. Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa?

37. Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi?

38. Ya kwamba hakika nafsi iliyobeba madhambi haibebi madhambi ya mwengine?

39. Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyoyafanya mwenyewe?

40. Na kwamba vitendo vyake vitaonekana?

41. Kisha ndio atalipwa malipo yake kwa ukamilifu.

¹ Ahmad 5:46 na 5:41

² Fat'h Al-Bari 5:324 na 10:491 na 507, Muslim 4:22496, Abu Dawud 5:154 na Ibn Majah 2:1232

³ Ahmad 6:5

⁴ Muslim 4:2297 na Abu Dawud 5:153

Ukosoaji Dhidi ya Watu Wanaomuasi Allah تعالى na Wenye Kuzuia Kutoa Sadaka

Allah تعالى Anatoa onyo kwa wale wanaoacha kumtii Yeye,

فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّى ﴿٣١﴾ وَلَٰكِن كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿٣٢﴾

“Kwa sababu hakusadiki, wala hakusali. Bali alikanusha, na akageuka.” (75:31-32),

وَأَعْطَىٰ قَلِيلًا وَأَكْدَىٰ ﴿٣٣﴾

“Na akatoa kidogo, akajizuia?”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Akatoa kidogo, akaacha kutoa.”¹ Sawa na kauli hiyo ilisemwa na Mujahid, Sa’id bin Jubayr, ‘Ikrimah, Qatadah na wengine.² ‘Ikrimah na Sa’id walisema: “Kama suala la watu wanaochimba kisima, wakati wanaendelea hivyo, wakakuta jiwe linalowazuia kumaliza kazi yao. Kwa hivyo wakasema, ‘Tumemaliza,’ na wakaacha kazi.” Kauli ya Allah تعالى,

أَعِنْدَهُ عِلْمُ الْغَيْبِ فَهُوَ يَرَىٰ ﴿٣٤﴾

“Je! Anayo huyo ilimu ya ghaibu, basi ndio anaona?”

Je, mtu huyu aliyeacha kutoa anajua ya ghaibu kwamba mali yake itakwisha ndio maana akajizuilia kufanya wema na kutoa? Uhakika ni kinyume chake; yeye amejizuia kutoa na kutenda wema kwa khofu ya umaskini na ubakhili uliopitiliza. Mtume ﷺ alisema katika Hadithi,

«أَنْفِقْ بِبِلَالٍ، وَلَا تَخْشَ مِنْ ذِي الْعَرْشِ إِفْلَاحًا»

“Ewe Bilal! Toa na usihofie kupungua riziki kutoka kwa Mwenye Arshi.”³

Allah تعالى Amesema,

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِّنْ شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُ ۖ وَهُوَ خَيْرُ الرَّزَاقِينَ ﴿٣٥﴾

“Na chochote mtakacho kitoa Yeye Atakilipa. Naye ni Mbora wa wanaoruzuku.” (34:39)

¹ At-Tabari 22:541.

² At-Tabari 22:542.

³ At-Tabararani 10:191.

Ubainifu wa Sahifa za Musa عليه السلام na Ibrahim عليه السلام

Allah تعالى Amesema,

﴿أَمْ لَمْ يُنَبِّأْ بِمَا فِي صُحُفِ مُوسَىٰ﴾ وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّى ﴿٢٧﴾

“Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa?. Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi?”

Sa’id bin Jubayr na Ath-Thauri walisema, “Inamaanisha kuwa alifikisha yote aliyotakiwa ayafikisha.”¹ Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu,

﴿وَفَّى﴾

“Aliyetimiza ahadi.”

Aliyafikisha yote aliyoamrisha na Allah تعالى kuyafikisha.”² Sa’id bin Jubayr alisema juu ya:

﴿وَفَّى﴾

“Aliyetimiza ahadi.”

“Alichoaamrisha.”³ Qatadah alisema kuhusu:

﴿وَفَّى﴾

“Aliyetimiza ahadi.” “Alimtii Allah تعالى na akaufikisha Ujumbe kwa viumbe Wake.” Rai hii aliikhitari Ibn Jarir رحمه الله تعالى kwa sababu inajumuisha kauli ya kabla yake na inaiunga mkono. Allah تعالى Amesema,

﴿وَإِذِ ابْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۗ قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ۗ﴾

“Na kumbuka Mola Wake Mlezi alipomjaribu Ibrahim kwa kumpa amri fulani, naye akazitimiza, akamuambia: Hakika Mimi Nitakufanya uwe mwongozi wa watu.” (2:124)

Hivyo, Nabii Ibrahim عليه السلام alitimiza amri zote alizoamriwa na Mola Wake Mlezi, na alijiepusha na makatazo yote, na alifikisha Ujumbe wa Allah تعالى kwa ukamilifu wake. Kwa hivyo, Yeye anastahiki kufanywa kiongozi wa wanaadamu katika mambo yake yote, kauli na matendo. Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 22:544.

² At-Tabari 22:543.

³ At-Tabari 22:544.

ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنْ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٦٣﴾

“Kisha Tukakufunulia ya kwamba ufuata mila ya Ibrahim, mwongofu, na wala hakuwa miongoni mwa washirikina.” (16:123)

At-Tirmidhi amepokea katika Jamii yake kutoka kwa Dardai na Abu Dhari kutoka kwa Mtume ﷺ, kutoka kwa Allah تعالى Amesema; “Ewe Mwanadamu, Nisalie Mimi raka nne mwanzoni mwa mchana, Nitakupa wewe ulinzi hadi mwisho wake.”

Hatabeba Yeyote Mzigo wa Mwingine Siku ya Kiyama

Allah تعالى Ameeleza Alichokiteremsha katika maandiko ya Nabii Ibrahim na Nabii Musa عليه السلام,

أَلَّا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ﴿١٨٠﴾

“Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine.”

Maana yake: Kila nafsi itabeba dhuluma zake yenyewe, ikiwa ni ukafiri au dhambi, na hapana mwingine wa kuibebwa mizigo yake ya dhambi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَأَنْ تَدْعُ مُثْقَلَةٌ إِلَىٰ جَمَلِهَا لَا تُحْمَلُ مِنْهُ شَيْءٌ وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ﴿١٨١﴾

“Na aliyetopewa na mzigo wake akiomba uchukuliwe hautachukuliwa hata kidogo, na hata angalimuomba jamaa yake wa karibu.” (35:18)

Allah تعالى Amesema,

وَأَنْ لَّيْسَ لِلْإِنْسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿١٨٢﴾

“Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyoyafanya mwenyewe?”

Kwa hivyo, kama ambavyo hakuna nafsi itakayobeba madhambi ya nafsi nyingine, halikadhalika, nafsi haitanufaika kutokana na yaliyochumwa na nyingine. Ni sawa ilivyoeleza Hadithi iliyonukuliwa na Muslim katika Sahih, kuwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنهما, Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا مَاتَ الْإِنْسَانُ انْقَطَعَ عَمَلُهُ إِلَّا مِنْ ثَلَاثٍ: مِنْ وَلَدٍ صَالِحٍ يَدْعُو لَهُ، أَوْ صَدَقَةٍ جَارِيَةٍ مِنْ بَعْدِهِ، أَوْ عِلْمٍ يُنْتَفَعُ بِهِ»

“Pindi mtu anapofariki, amali zake hukatika isipokuwa (mambo) matatu: mtoto mwema anayemuomba dua, au Sadaka inayoendelea au elimu inayonufaisha.”¹

Mambo haya matatu, kwa kweli, ni matokeo ya matendo, bidii na amali zake mwenyewe. Ni sawa na inavyoeleza Hadithi ifuatayo,

«إِنَّ أَطْيَبَ مَا أَكَلَ الرَّجُلُ مِنْ كَسْبِهِ، وَإِنَّ وَلَدَهُ مِنْ كَسْبِهِ»

“Hakika kitu bora zaidi anachokula mtu ni kinachotokana na chumo lake, na hakika mwanaye ni miongoni mwa chumo lake.”²

Sadaka yenye kuendelea anayoiacha mtu, kama mali ya Wakfu, ni sehemu ya matendo na amali zake mwenyewe. Allah تعالى Amesema,

إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي الْمَوْتَىٰ وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا وَآثَرَهُمْ³

“Hakika Sisi Tunawafufua wafu, na Tunayaandika wanayo yatanguliza.” (36:12)

Elimu ambayo mtu anaieneza kwa watu na inawaongoza, ni sehemu ya matendo na amali zake. Hadithi iliyothibiti katika Sahih inaeleza,

«مَنْ دَعَا إِلَىٰ هُدًى كَانَ لَهُ مِنَ الْأَجْرِ مِثْلُ أُجُورِ مَنْ اتَّبَعَهُ، مِنْ غَيْرِ أَنْ يَنْقُصَ مِنْ أُجُورِهِمْ شَيْئًا»

“Mwenye kulingania kwenye uongofu atakuwa na malipo kama malipo ya wenye kumfuata, (pasi na) kupungua kitu katika malipo yao.”³

Allah تعالى Amesema,

وَأَنَّ سَعْيَهُ سَوْفَ يُرَىٰ ﴿٥٠﴾

“Na kwamba vitendo vyake vitaonekana?”

Maana yake: Siku ile ya ufufuo,

¹ Muslim 3:1255

² An-Nasai 7:241

³ Muslim 4:2060

وَقُلْ أَعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَىٰ عِلِّيِّمِ الْغَيْبِ
وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾

Na sema: Tendeni vitendo. Na Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Waumini wataviona vitendo vyenu. Na mtarudishwa kwa Mwenye Kujua siri na dhahiri; Naye Atakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda. (9:105),

Kisha Allah تعالى Atakukumbusheni amali zenu na Atakulipeni malipo yaliyokamilika kutokana na amali zenu ikiwa ni njema mtalipwa mema na ikiwa ni mbaya, basi mtalipwa hivyo hivyo.

Kauli ya Allah تعالى katika Aya hii,

ثُمَّ يُجْزَاهُ الْجَزَاءَ الْأَوْفَىٰ ﴿١٠٥﴾

“Kisha ndio atalipwa malipo yake kwa ukamilifu.”

* * *

وَأَنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ أَلْمُنْتَهَىٰ ﴿٤٢﴾ وَأَنَّهُ هُوَ أَضْحَكَ وَأَبْكَى ﴿٤٣﴾
 وَأَنَّهُ هُوَ أَمَاتَ وَأَحْيَا ﴿٤٤﴾ وَأَنَّهُ خَلَقَ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ
 وَالْأُنثَىٰ ﴿٤٥﴾ مِن نُّطْفَةٍ إِذَا تُمْنَىٰ ﴿٤٦﴾ وَأَنَّ عَلَيْهِ النَّشْأَةَ
 الْأُخْرَىٰ ﴿٤٧﴾ وَأَنَّهُ هُوَ أَغْنَىٰ وَأَقْنَىٰ ﴿٤٨﴾ وَأَنَّهُ هُوَ
 رَبُّ الشُّعْرَىٰ ﴿٤٩﴾ وَأَنَّهُ أَهْلَكَ عَادًا الْأُولَىٰ ﴿٥٠﴾
 وَثَمُودًا فَمَا أَبْقَىٰ ﴿٥١﴾ وَقَوْمَ نُوحٍ مِّن قَبْلُ إِنَّهُمْ كَانُوا هُمْ
 أَظْلَمَ وَأَطْغَىٰ ﴿٥٢﴾ وَالْمُؤْتَفِكَةَ أَهْوَىٰ ﴿٥٣﴾ فَغَشَّهَا مَا
 غَشَّىٰ ﴿٥٤﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكَ تَتَمَارَىٰ ﴿٥٥﴾ هَذَا نَذِيرٌ
 مِّنَ النَّذْرِ الْأُولَىٰ ﴿٥٦﴾ أَزِفَتِ الْأَرْفَةُ ﴿٥٧﴾ لَيْسَ لَهَا مِن
 دُونِ اللَّهِ كَاشِفَةٌ ﴿٥٨﴾ أَفَمَن هَذَا أَلْحَدِيثُ تَعْجِبُونَ ﴿٥٩﴾
 وَتَضْحَكُونَ وَلَا تَتَّبِعُونَ ﴿٦٠﴾ وَأَنْتُمْ سَمِعْتُمْ ﴿٦١﴾
 فَاسْتَجِدُوا لِلَّهِ وَأَعْبُدُوا ﴿٦٢﴾

وَأَنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ أَلْمُنْتَهَىٰ ﴿٤٢﴾ وَأَنَّهُ هُوَ
 هُوَ أَضْحَكَ وَأَبْكَى ﴿٤٣﴾ وَأَنَّهُ هُوَ
 أَمَاتَ وَأَحْيَا ﴿٤٤﴾ وَأَنَّهُ خَلَقَ
 الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ﴿٤٥﴾ مِن
 نُّطْفَةٍ إِذَا تُمْنَىٰ ﴿٤٦﴾ وَأَنَّ عَلَيْهِ
 النَّشْأَةَ الْأُخْرَىٰ ﴿٤٧﴾ وَأَنَّهُ هُوَ
 أَغْنَىٰ وَأَقْنَىٰ ﴿٤٨﴾ وَأَنَّهُ هُوَ رَبُّ
 الشُّعْرَىٰ ﴿٤٩﴾ وَأَنَّهُ أَهْلَكَ عَادًا
 الْأُولَىٰ ﴿٥٠﴾ وَثَمُودًا فَمَا أَبْقَىٰ ﴿٥١﴾
 وَقَوْمَ نُوحٍ مِّن قَبْلُ إِنَّهُمْ كَانُوا هُمْ
 أَظْلَمَ وَأَطْغَىٰ ﴿٥٢﴾ وَالْمُؤْتَفِكَةَ
 أَهْوَىٰ ﴿٥٣﴾ فَغَشَّهَا مَا غَشَّىٰ ﴿٥٤﴾
 فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكَ تَتَمَارَىٰ ﴿٥٥﴾

42. Na kwa hakika kwa kurejea Mola Wako Mlezi ndio mwisho.

43. Na kwamba Yeye Ndiye Aliyeumba furaha na huzuni.

44. Na kwamba Yeye Ndiye Anayefisha na Kuhuisha.

45. Na kwamba Yeye Ndiye Aliyeumba jozi, dume na jike.

46. Kutokana na mbegu ya uzazi inapomiminwa.

47. Na kwamba ni juu yake ufufuo mwengine.

48. Na kwamba ni Yeye Ndiye Anayetajirisha na Kufakirisha.

49. Na kwamba hakika Yeye Ndiye Mola Mlezi wa nyota ya Shii'ra yenye kunga'aa.

50. Na kwamba Yeye Ndiye Aliyewaangamiza A'di wa kwanza,

51. Na Thamudi hakuwabakisha.

52. Na kabla yao kaumu ya Nuhu. Na hao hakika walikuwa ni madhaalimu zaidi, na waovu zaidi;

53. Na miji iliyopinduliwa, ni Yeye Aliyeipindua.

54. Vikaifunika vilivyofunika.

55. Basi neema gani ya Mola Wako Mlezi unayoifanyia shaka?

Baadhi ya Sifa za Mola Mlezi, na kuwa Yeye Atamrejsha Mtu Kama Alivyomuanzisha, na Kutajwa Baadhi ya Anayowafanyia Waja Wake

Allah تعالى Amesema,

وَأَنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ أَلْمَنَتِ

“Na kwa hakika kwa Mola Wako Mlezi ndio mwisho.”

Maana yake: Marejeo ya kila kitu Siku ya Ufufuo. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa ‘Amr bin Maymun Al-Awd alisema, “Siku moja, Mu’adh bin Jabal رضي الله عنه alisimama miongoni mwetu, akasema, ‘Enyi Wana wa Awd! Mimi ni mjumbe wa Mtume ﷺ kwenu; jueni kuwa marejeo ni kwa Allah تعالى, ima kwenda Peponi au Motoni.”¹ Kauli ya Allah تعالى,

وَأَنَّهُ هُوَ أَضْحَكَ وَأَبْكَىٰ

“Na kwamba Yeye Ndiye Anayeleta kicheko na kilio.”

Maana yake, Aliwaumbia viumbe Wake uwezo wa kucheka au kulia na sababu za mambo hayo mawili yaliyo kinyume.

وَأَنَّهُ هُوَ أَمَاتَ وَأَحْيَا

“Na kwamba Yeye Ndiye Anayefisha na Kuhuisha.”

Katika Kauli nyingine sawa na hii, Allah تعالى Amesema,

¹Al-Hakim 1:83. Sanadi yake ina dosari.

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ

“Ambaye Ameumba mauti na uhai...” (67:2)

Allah تعالى Amesema,

وَأَنَّهُ خَلَقَ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَى ﴿٦٧﴾

“Na kwamba Yeye Ndiye Aliyeumba jozi, dume na jike.”

Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine:

أُحْسِبُ الْإِنْسَانَ أَن يُبْرِكَ سُدَى ﴿٦٨﴾ أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِن مَّيِّ يُمْنَى ﴿٦٩﴾ ثُمَّ كَانَ عَلَقَةً ﴿٧٠﴾ فَخَلَقَ فَسَوَّى ﴿٧١﴾ فَعَجَلَ مِنْهُ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَى ﴿٧٢﴾ أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَيَّ أَن نُّخَيِّقَ الْمَوْتَ ﴿٧٣﴾

“Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure? Kwani hakuwa yeye tone ya manii lililoshushwa? Akawa kidonge cha damu, tena Mwenyezi Mungu Akamuumba na Akamtengeneza vilivyo. Akamfanya namna mbili, mwanamume na mwanamke. Hivi hakuwa Yeye Allah kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu?” (75:36-40)

Allah تعالى Amesema,

وَأَنَّ عَلَيْهِ النِّشْأَةَ الْآخَرَى ﴿٧٤﴾

“Na kwamba ni juu yake ufufuo mwengine.”

Maana yake: Kama Alivyoanzisha uumbaji wa kwanza. Yeye ni Mweza wa Kuurudisha tena uhai, Akiuhuisha kwa ajili ya Siku ya Hukumu,

وَأَنَّهُ هُوَ أَعْنَى وَأَقْنَى ﴿٧٥﴾

“Na kwamba ni Yeye Ndiye Anayetosheleza na kukinaisha.”

Ni Allah تعالى Ndiye Mwenye Kuwapa mali waja wake ambayo Ameifanya ni akiba kwao. Hawahitaji kuiuza. Na huu ndio utimilifu wa neema. Kauli nyingi za wanazuoni wa Tafsiri zinazungukia katika maana hii. Kama rai za Abu Swalih, Ibn Jarir na wengine.¹ Mujahid alisema,

¹ At-Tabari 22:548 - 549.

أَغْنَىٰ

“Anayetosheleza.”

Maana yake: Anampa (mja) mali ya kumtajirisha.

وَأَقْنَىٰ

“Na kukinaisha.”

Inamaanisha: Anawapa waja mali. Maana sawa na hiyo ilitolewa na Qatadah. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na Mujahid walisema;

أَغْنَىٰ

“Anayetosheleza.”

Maana yake: Alimpa mali.

وَأَقْنَىٰ

“Na kukinaisha.”

Maana yake: Na kumfanya kuridhika.

وَأَنذَرَهُ هُوَ رَبُّ الشَّعْرَىٰ ﴿٥١﴾

“Na kwamba hakika Yeye ndiye Mola Mlezi wa nyota ya Shii’ra.”

Ibn ‘Abbas, Mujahid, Qatadah na Ibn Zayd رضي الله عنهم alisema kuhusu *Ash-Shi’ra* kuwa ni nyota ing’aaayo, iitwayo *Mirzam Al-Jawza’* (Sirius), ambayo kikundi cha Waarabu kilikuwa kikiabudu.¹

وَأَنذَرَهُ أَهْلَكَ عَادًا الْأُولَىٰ ﴿٥٢﴾

“Na kwamba Yeye Ndiye Aliyewaangamiza A’di wa kwanza.”

Watu wa Hud عليه السلام. Wao ni uzao wa ‘Ad, mwana wa Iram, bin Sam, bin Nuh عليه السلام. Inalingana na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

¹ At-Tabari 22:551

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦٨﴾ إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٦٩﴾ الَّتِي لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِي الْبِلَادِ ﴿٧٠﴾

“Kwani hukuona jinsi Mola Wako Mlezi Alivyowafanya kina A’di? Wa Iram, wenye majumba marefu? Ambao haukuumbwa mfano wake katika nchi?” (89:6-8)

Watu wa ‘Ad walikuwa wenye nguvu na waasi sana kwa Allah تعالى na Mjumbe Wake. Allah تعالى Akawaangamiza.

بَرِيحٍ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ ﴿٦٦﴾ سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ سَبْعَ لَيَالٍ وَثَمَنِيَةَ أَيَّامٍ حُسُومًا ﴿٦٧﴾

“...Kwa upepo mkali usiozuilika. Aliowapelekea siku saba, na siku nane, mfululizo...” (69:6-7)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَتَمُودًا فَمَا أَبْقَى ﴿٦٥﴾

“Na Thamudi hakuwabakisha.”

Anaeleza kuwa Aliwaangamiza wote na hakumuacha yeyote miongoni mwao.

وَقَوْمِ نُوحٍ مِّن قَبْلُ ﴿٦٤﴾

“Na kabla yao kaumu ya Nuhu.”

Kabla ya ‘Ad na Thamud,

إِنِّيهِمْ كَانُوا هُمْ أَظْلَمَ وَأَطْغَى ﴿٦٣﴾

“Na hao hakika walikuwa ni madhaalimu zaidi, na waovu zaidi.”

Madhalimu zaidi katika kumuasi Allah تعالى kuliko waliokuja baada yao.

وَالْمُؤْتَفِكَةَ أَهْوَى ﴿٦٢﴾

“Na miji iliyopinduliwa, ni Yeye Aliyeipindua.”

Maana yake: Miji (ya Sodoma na Gomorrah) ambapo Mtume Lut عليه السلام alitumwa. Allah تعالى Aliigeuza miji yao juu chini Akawatupia mawe ya **Sijjil**.

Kauli ya Allah تعالى،

فَعَشْنَهَا مَا عَشَىٰ ﴿٥٣﴾

“Vikaifunika vilivyofunika.”

Inafanana na suala la mawe ya *Sijjil* Aliyowapelekea juu yao.

وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا ۖ فَسَاءَ مَطَرُ الْمُنذِرِينَ ﴿٥٤﴾

“Na Tukawanyeshea mvua, basi ni ovu mno mvua ya waliyonywa.” (26:173)

Allah تعالى Amesema,

فَيَأْتِي ۙ آءِ الْآءِ رَبِّكَ تَتَمَارَىٰ ﴿٥٥﴾

“Basi neema gani ya Mola Wako Mlezi unayoifanyia shaka?”

Maana yake: ‘Ni ipi katika neema za Allah تعالى kwa ajili yako ewe mwanaadamu unayoitilia shaka?’ Kwa mujibu wa Qatadah.¹ Ibn Jurayj alisema kuwa Aya ifuatayo,

فَيَأْتِي ۙ آءِ الْآءِ رَبِّكَ تَتَمَارَىٰ ﴿٥٥﴾

“Basi neema gani ya Mola Wako Mlezi unayoifanyia shaka?”

Imeelekezwa kwa Mtume ﷺ kwa kusema: “Ewe Muhammad!” Hata hivyo, maelezo ya kwanza ni bora zaidi, na ndiyo maana Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliyakhitari.

هَذَا نَذِيرٌ مِّنَ النُّذُرِ الْأُولَىٰ ﴿٥٦﴾ أَرْفَتِ الْأَرْفَةَ ﴿٥٧﴾ لَيْسَ لَهَا مِن دُونِ اللَّهِ كَاشِفَةٌ ﴿٥٨﴾
 أَفَمِنَ هَذَا الْحَدِيثِ تَعَجَّبُونَ ﴿٥٩﴾ وَتَضْحَكُونَ وَلَا تَبْكُونَ ﴿٦٠﴾ وَأَنْتُمْ سَمِعْتُمْ ﴿٦١﴾
 فَاسْجُدُوا لِلَّهِ وَاعْبُدُوا ﴿٦٢﴾

56. Huyu ni muonyaji miongoni mwa wale waonyaji wa kale.

57. Kiyama kimekaribia!

58. Hapana wa kukidhihirisha isipokuwa Mwenyezi Mungu.

¹ At-Tabari 22:556.

59. Je! Mnyastaajabia maneno haya?

60. Na mnacheka, wala hamlii?

61. Nanyi mmeghafilika?

62. Basi msujudieni Mwenyezi Mungu, na mumuabudu.

Onyo na Uzinduzi, Amri ya Kusujudu na kuwa Mnyenyekevu

Allah تعالی Amesema,

هَذَا نَذِيرٌ

“Huyu ni muonyaji”.

Akimaanisha Mtume Muhammad ﷺ,

مِنَ النَّذْرِ الْأُولَىٰ

“Miongoni mwa wale waonyaji wa kale”.

Maana yake: Kama wale waonyaji wa kale, alitumwa kuwa mjumbe kama walivyotumwa wao kama wajumbe. Allah تعالی Amesema:

قُلْ مَا كُنْتُ بِدَعَاٍ مِّنَ الرُّسُلِ

“Sema: Mimi si kiroja miongoni mwa Mitume.” (46:9)

Allah تعالی Amesema;

أَزَفَتِ الْأَرْفَةُ ﴿٢٧﴾

“Kiyama kimekaribia!”

Maana yake: Kile kilicho karibu (siku ile ya ufufuo) kimekaribia

لَيْسَ لَهَا مِن دُونِ اللَّهِ كَاشِفَةٌ ﴿٢٨﴾

“Hapana wa kukizuia isipokuwa Mwenyezi Mungu.”

Hapana yeyote isipokuwa Allah تعالی Mwenye Uweza wa kuzuia ujio wake. Wala hapana ajuaye lini kitawadia, isipokuwa Yeye. Mwonyaji mwenye

tahadhari kubwa ya kufikisha ujumbe wake juu ya janga linalokaribia ili lisiwaangukie wale anaowaonya. Kama Allah تعالى Alivyosema katika Aya nyingine;

إِنَّ هُوَ إِلَّا تَنْذِيرٌ لَّكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ ﴿٥٣﴾

“Yeye si vinginevyo ila ni Mwonyaji kwenu kabla ya adhabu kali kabisa isiyomithilika.” (34:46)

Na katika Hadithi:

«أَنَا التَّنْذِيرُ الْعُرْيَانُ»

“Mimi ni mwonyaji niliye bayana.”¹

Akimaanisha, Aliharakisha kuwaonya watu kuhusu ubaya aliouona ukija, na kwamba hakupata nafasi ya kuvaa chochote, bali alikimbilia kuwaonya watu wake na katika hali hiyo. Maana hii inakubaliana na maana ya Aya hii.

أَزِفَتِ الْأَرْفَةُ ﴿٥٤﴾

“Kiyama kimekaribia!”

Kwa kurejea kukaribia Siku ya Kiyama. Allah تعالى Amesema mwanzoni mwa Surah:

أَقْرَبَتِ السَّاعَةُ وَأَنْشَقَّ الْقَمَرُ ﴿٥٤﴾

“Saa imekaribia, na mwezi umepasuka!” (54:1)

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Sahl bin Sa’d عنه رضي الله alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِيَّاكُمْ وَمُحَقَّرَاتِ الذُّنُوبِ، فَإِنَّمَا مَثَلُ مُحَقَّرَاتِ الذُّنُوبِ كَمَثَلِ قَوْمٍ نَزَلُوا بِبَطْنِ وَادٍ، فَجَاءَ ذَا بَعُودٍ وَجَاءَ ذَا بَعُودٍ، حَتَّى أَنْصَجُوا خُبْرَتَهُمْ، وَإِنَّ مُحَقَّرَاتِ الذُّنُوبِ، مَتَى يُرْخَدُ بِهَا صَاجِبُهَا، تُنْهَلِكُهَا»

“Tahadharini na dhambi zinazodharauliwa! Hakika, mfano wa dhambi zinazodharauliwa ni kama watu waliopiga kambi bondeni. Mmoja wao akawaleta kipande cha kuni, mwingine akaleta kingine

¹ Fat’h Al-Bari 11:323.

na mwingine kadhalika, mpaka wakaivisha mkate wao. Hakika dhambi zinazodharauliwa wakati mhusika wake atakapoadhibiwa nazo zitamuangamiza.”¹

Allah تعالیٰ Anawaonya washirikina kwa kusikiliza kwao Qur’an, lakini baadaye huikengeuka na kuipuuza,

تَعْجَبُونَ

“Mnayastaajabia.”

Maana yake: Wakitia shaka kwamba ni kweli.

وَتَضْحَكُونَ

“Na mnacheka.”

Kwa kejeli na dhihaka.

وَلَا تَبْكُونَ

“Wala hamlii.”

Kama wanavyolia wale wanaoamini.

وَيَحْزُونَ لِلأَذْقَانِ يَبْكُونَ وَيَزِيدُهُمْ خُشُوعًا ﴿١٠٩﴾

“Na huanguka kifudifudi na huku wanalia, na inawazidisha unyenyekevu.” (17:109)

Allah تعالیٰ Amesema;

وَأَنْتُمْ سَامِدُونَ

“Nanyi mmeghafilika?”

Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالیٰ alisimulia kuwa baba yake alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu *Saamiduun*, kuwa ni “Kuimba; kwa lahaja za ki-Yemen, *‘Ismud lanaa.’* Yaani, “tuimbieni sisi.’ ‘Ikrimah alitoa maelezo kama hayo.² Katika masimulizi mengine kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kwamba maana yake ni,

¹ Ahmad 5:331

² At-Tabari 22:559

سَلْمِدُونَ

“Mmeghafilika?”

Maana yake: “Kugeuka.”¹ Sawa na haya yalisimuliwa na Mujahid na ‘Ikrimah. Allah تعالى Ametuamrisha waja wake tumsujudie, tumuabudu Yeye kwa mujibu wa njia ya Mjumbe Wake, na kutimiza mahitaji ya Tawhidi na uaminifu.

فَأَسْجُدُوا لِلَّهِ وَأَعْبُدُوا ۝

“Basi msujudieni Mwenyezi Mungu, na mumuabudu.”

(Basi msujudie Allah تعالى na muabudu Yeye). Akimaanisha kwa utii, Ikhlas na Tawhidi. Al-Bukhari alimnukuu Abu Ma’mar kuwa alisema, ‘Abdul-Warith alisema, Ayyub alisema, ‘Ikrimah alisema kuwa, Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mtume ﷺ alisujudu baada tu ya kusoma *An-Najm* na Waislamu, washirikina, majini na wanaadamu waliokuwepo walisujudu pamoja naye.”² Bukhari peke yake alisimulia Hadithi hii bila Muslim. Imamu Ahmad alinukuu kuwa Al-Muttalib bin Abu Wada’ah alisema, “Wakati akiwa bado Makkah, Mtume ﷺ alisoma *Surat An-Najm*, akasujudu pamoja na waliokuwa pamoja naye wakati huo. Hata hivyo, nilinyanyua kichwa changu na nikakataa kusujudu.” Al-Muttalib wakati huo alikuwa bado hajasilimu, lakini tangu wakati huo aliingia katika Uislamu, hakuwahi kumsikia yeyote akiisoma Sura hii mpaka mwisho bila ya kusujudu pamoja na waliokuwa wakisujudu baada ya kuisoma.”³ An-Nasa’i pia aliikusanya Hadithi hii katika Kitabu cha Swala.⁴

Huu ni mwisho wa Tafsiiri ya *Suratu An-Najm*. Sifa zote Njema pamoja na shukrani ni stahiki ya Allah تعالى.

* * *

¹Abdur-Razzaq 3:255.

²*Fat’h Al-Bari* 8:480.

³Ahmad 6:399.

⁴An-Nasai 2:160.

Tafsiri ya Suratu Iqtarabat

As-Sa'ah¹

Sura ya 54

Iliteremshwa Makkah

Hadithi ya Abu Waqid imeshatangulia, kuwa Mtume ﷺ akisoma Surat *Qaf* na *Iqtarabat As-Sa'ah*, wakati wa (Sala ya Idi) *Al-Adhah* na *Al-Fitr*.

Mtume ﷺ alikuwa akizisoma Sura hizi mbili wakati wa mikusanyiko na matukio makubwa kwa sababu Sura hizi zina ahadi na maonyo ya Allah ﷻ, na maelezo kuhusu asili ya Uumbaji, Ufufuo, Tawhid, Uthibitisho wa Utume, na majukumu mengine makubwa.



¹ Pia inaitwa *Surat Al-Qamar*.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

سُورَةُ الْقَمَرِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَقْرَبَتِ السَّاعَةُ وَأَدْنَقَ الْقَمَرُ ﴿١﴾ وَإِن يَرَوْا آيَةً يُعْرَضُوا
وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ ﴿٢﴾ وَكَذَّبُوا وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ
وَكَذَّبُوا أَمْرٍ مُّسْتَقَرٌّ ﴿٣﴾ وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنَ الْأَنْبَاءِ مَا فِيهِ
مُزْدَجَّرٌ ﴿٤﴾ حِكْمَةٌ بَلِغَةٌ ﴿٥﴾ فَمَا تُغْنِ الْأُنذُرُ ﴿٦﴾ فَتَوَلَّ
عَنْهُمْ يَوْمَ يَدْعُ الدَّاعِ إِلَى شَيْءٍ نُّكْرٍ ﴿٧﴾ خُشَعًا
أَبْصَرُهُمْ يَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ كَأَنَّهُمْ جَرَادٌ مُّنتَشِرٌ ﴿٨﴾
مُهْطِعِينَ إِلَى الدَّاعِ ﴿٩﴾ يَقُولُ الْكَافِرُونَ هَذَا يَوْمَ عَسِيرٍ ﴿١٠﴾
* كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ فَكَذَّبُوا عَبْدَنَا وَقَالُوا مَجْنُونٌ
وَأَزْدِجِرَ ﴿١١﴾ فَدَعَا رَبَّهُ أَنِّي مَغْلُوبٌ فَانتَصِرَ ﴿١٢﴾ فَفَتَحْنَا
أَبْوَابَ السَّمَاءِ بِمَاءٍ مُّطَهَّرٍ ﴿١٣﴾ وَفَجَّرْنَا الْأَرْضَ عُيُونًا
فَالْتَقَى الْمَاءُ عَلَى أَمْرٍ قَدْ قُدِرَ ﴿١٤﴾ وَحَمَلْنَاهُ عَلَى ذَاتِ
الْأَوْحِ وَدُسِّرَ ﴿١٥﴾ تَجْرِي بِأَعْيُنِنَا جَزَاءَ لِمَن كَانَ كُفِرَ ﴿١٦﴾
وَلَقَدْ تَرَكْنَاهَا آيَةً فَهَلْ مِن مُّذَكِّرٍ ﴿١٧﴾ فَكَيْفَ كَانَ
عَدْلِي وَنُنذِرِ ﴿١٨﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْءَانَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِن
مُّذَكِّرٍ ﴿١٩﴾

أَقْرَبَتِ السَّاعَةُ وَأَدْنَقَ الْقَمَرُ ﴿١﴾
وَإِن يَرَوْا آيَةً يُعْرَضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ
مُّسْتَمِرٌّ ﴿٢﴾ وَكَذَّبُوا وَاتَّبَعُوا
أَهْوَاءَهُمْ ﴿٣﴾ وَكُلُّ أَمْرٍ مُّسْتَقَرٌّ ﴿٤﴾
وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنَ الْأَنْبَاءِ مَا فِيهِ
مُزْدَجَّرٌ ﴿٥﴾ حِكْمَةٌ بَلِغَةٌ ﴿٦﴾ فَمَا
تُغْنِ الْأُنذُرُ ﴿٧﴾

1. Kiama kimekaribia, na mwezi umepasuka!

2. Na wakiona miujiza hugeuka upande na husema: Huu ni uchawi tu unazidi kuendelea.

3. Na wamekanusha na wamefuata matamania yao. Na kila jambo ni lenye kuthibiti.

4. Na bila ya shaka zimewajia habari zenye makaripio.

5. Hekima kamili; Lakini maonyo hawawafai wao kitu!

Kiyama kimekaribia na Mwezi Umepasuka

Allah تعالیٰ Anajulisha kuhusu kukaribia kwa Saa na mwisho wa dunia na kwisha kwake.

أَتَىٰ أَمْرَ اللَّهِ فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ ۗ

“Amri ya Mwenyezi Mungu itafika tu. Basi msiihimize.” (16:1),

أَقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ مُّعْرِضُونَ ﴿٢١﴾

“Imekaribia watu hisabu yao, nao wamo katika mghafala wanapuuzwa.” (21:1)

Hadithi Kuhusu Saa ya Mwisho

Kuna Hadithi kadhaa zenye maana hii. Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bazzar رحمه الله تعالیٰ alinukuu kuwa Anas رضي الله عنه alisema siku moja, pindi jua likiwa limekaribia kuzama, Mtume ﷺ aliwahutubia kwa kusema,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! مَا بَقِيَ مِنَ الدُّنْيَا فِيمَا مَضَىٰ مِنْهَا إِلَّا كَمَا بَقِيَ مِنْ يَوْمِكُمْ هَذَا فِيمَا مَضَىٰ مِنْهُ»

“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Haujabakia muda wa dunia ukilinganisha na uliopita isipokuwa ni kama muda uliosalia wa siku yenu hii ukilinganisha na uliopita.”¹

Hadithi nyingine inayounga mkono na kuelezea Hadithi hiyo, imeandikwa na Imamu Ahmad, ‘Abdullah bin ‘Umar رضي الله عنهما alisema, “Tulikuwa tumeketi pamoja na Mtume ﷺ wakati jua likiwa linapanda juu ya Qu’ayqa’an,² baada ya’Alasiri. akasema,

«مَا أَعْمَارُكُمْ فِي أَعْمَارٍ مَنْ مَضَىٰ إِلَّا كَمَا بَقِيَ مِنَ النَّهَارِ فِيمَا مَضَىٰ»

“Muda wenu uliosalia ukilinganisha na uliopita ni kama muda uliobakia katika mchana ukilinganisha na uliopita.”³

¹ Majma’ Az-Zawaid 10:311

² Mlima mdogo ulioko Makkah karibu na Hijr ya Ka’bah

³ Ahmad 2:115

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Sahl bin Sa'd رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«بُعِثْتُ أَنَا وَالسَّاعَةُ مُكْذَّابًا»

“Nimetumwa mimi pamoja na Saa (Kiyama) kama hivi (tukiwa sambamba).”

Na akaashiria kwa kidole cha kati na cha shahada.¹ Sahih Mbili nazo zimerikodi Hadithi hii.² Imamu Ahmad alimnukuu Wahb As-Suwa'i رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ, amesema,

«بُعِثْتُ أَنَا وَالسَّاعَةُ كَهَيْدِهِ مِنْ هَذِهِ، إِنْ كَادَتْ لَتَسْبِقُنِي»

“Nimetumwa mimi kabla kidogo na Saa ya Mwisho ni kama umbali kati ya hapa na hapa, cha mwisho kinakaribia kukipita cha kwanza.”

Al-A'mash alikikutanisha kidole chake cha shahada na cha kati wakati akiisimulia Hadithi hii.³

Imamu Ahmad alimnukuu Al-Awza'i kuwa Isma'il bin 'Ubaydullah alisema, “Anas bin Malik رضي الله عنه alikwenda kwa Al-Walid bin 'Abdul-Malik ambaye alimuuliza kuhusu alichosikia kutoka kwa Mtume ﷺ kuhusu Saa ya Mwisho. Anas رضي الله عنه alisema, nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«أَنْتُمْ وَالسَّاعَةُ كَهَاتَيْنِ»

“Ninyi na Saa ya Mwisho ni karibu karibu kama hivi (vidole) viwili.”

Imamu Ahmad peke yake aliikusanya Hadithi hii.⁴ Kuna Hadithi inayoshuhudia Hadithi hizi katika Sahih kuhusu majina ya Mtume ﷺ, Al-Hashir (maana yake ni Mkusanyaji), miongoni mwa majina ya Mtume ﷺ; Yeye ni wa kwanza kukusanywa, na watu wote watakusanyika baada ya hapo (kwa ajili ya Siku ya hesabu).⁵ Kauli ya Allah تعالى,

¹ Ahmad 5:338

² Fat'h Al-Bari 11:355 na Muslim 4:2268

³ Ahmad 4:309

⁴ Ahmad 3:223

⁵ Fat'h Al-Bari 6:641

وَأَنْشَقَّ الْقَمَرُ

“Na mwezi umepasuka!”

Hili lilitokea wakati wa uhai wa Mtume ﷺ, kwa mujibu wa Hadith *Mutawatir* ambazo ni sahihi. Wanazuoni wameafikiana kuwa mwezi ulipasuka vipande viwili wakati wa uhai wa Mtume ﷺ, na tukio hilo lilikuwa miongoni mwa miujiza waziwazi aliyopewa na Allah تعالى. Hadithi zinaeleza wazi kuwa mwezi ulipasuka.

Hadithi Zinazoeleza Kupasuka kwa Mwezi

Simulizi ya Anas Bin Malik رضي الله عنه

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, “Watu wa Makkah walimuomba Mtume ﷺ muujiza. Hivyo basi, mwezi ukapasuliwa sehemu mbili Mtume ﷺ akiwa Makkah. Allah تعالى Amesema,

أَقْرَبَتِ السَّاعَةُ وَأَنْشَقَّ الْقَمَرُ ﴿١﴾

“Kiyama kimekaribia, na mwezi umepasuka!”¹

Imamu Muslim naye pia aliikusanya Hadithi hii.² Al-Bukhari alinukuu kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, “Watu wa Makkah walimuomba Mtume ﷺ awatolee muujiza, akawaonesha mwezi ukigawanyika sehemu mbili, mpaka wakaona (mlima wa) Hira’ baina yao.”³ Hadithi hii imeandikwa katika Sahihi Mbili kwa isnadi tofauti.

Simulizi ya Jubayr Bin Mut'im رضي الله عنه

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Jubayr bin Mut'im رضي الله عنه alisema, “Mwezi ulipasuka vipande viwili wakati wa uhai wa Mtume ﷺ, sehemu moja ya mwezi ilikuwa juu ya mlima na kipande kingine juu ya mlima mwingine. Wakasema, ‘Muhammad ameturoga.’ Baadaye wakasema, ‘Kama angeweza kuturoga, asingeweza kufanya hivyo kwa watu wote.’” Imamu Ahmad peke yake aliinukuu

¹ Ahmad 3:165.

² Muslim 4:2159.

³ *Fat'h Al-Bari* 7:221 na 8:484 na Muslim 4:2159.

Hadithi hii kwa isnadi hii ya usimulizi.¹ Al-Bayhaqi alitumia isnadi nyingine ya usimulizi katika Hadithi inayolingana na hii aliyoikusanya katika *Ad-Dala'il*.²

Simulizi ya Abdullah bin Abbas رضي الله عنه

Al-Bukhari amenukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mwezi ulipasuka wakati wa uhai wa Mtume ﷺ”³ Al-Bukhari na Muslim waliikusanya Hadithi hii.⁴ Ibn Jarir رضي الله عنه aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa rai kuhusu kauli ya Allah تعالى:

أَقْرَبَتْ السَّاعَةُ وَأَذْشَقَ الْقَمَرُ ﴿١﴾ وَإِنْ يَرَوْا آيَةً يُعْرَضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ ﴿٢﴾

“Kiama kimekaribia, na mwezi umepasuka! Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: Huu ni uchawi tu unazidi kuendelea.”

“Hili lilitokea kabla ya Hijrah; mwezi ulipasuka na watu waliuona ukiwa katika vipande viwili.”⁵

Simulizi ya ‘Abdullah Bin Umar رضي الله عنه

Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bayhaqi رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Abdullah bin ‘Umar رضي الله عنه alitoa rai juu ya Kauli ya Allah تعالى:

أَقْرَبَتْ السَّاعَةُ وَأَذْشَقَ الْقَمَرُ ﴿١﴾

“Kiyama kimekaribia, na mwezi umepasuka!”

“Hili lilitokea wakati wa uhai wa Mtume ﷺ; mwezi ulipasuka vipande viwili. Sehemu yake moja ilikuwa chini ya Jabali na nyingine nyuma ya Jabali.” Mtume ﷺ alisema,

«اللَّهُمَّ اشْهَدْ»

“Yaa Allah! Shuhudia.”⁶

¹ Ahmad 4:81.

² *Dalail An-Nubuwwah* 2:268.

³ *Fat’h Al-Bari* 8:484.

⁴ *Fat’h Al-Bari* 7:221 na 8:484 na Muslim 4:2159.

⁵ At-Tabari 22:569.

⁶ *Dalail An-Nubuwwah* 2:267.

Hii ni Simulizi iliyokusanywa na Imam Muslim na Imam Tirmidhi.¹ Imam Tirmidhi akasema, “*Hasan Sahih.*”²

Simulizi ya ‘Abdullah Bin Mas’ud رضي الله عنه

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنهما alisema, “Mwezi ulipasuka vipande viwili wakati wa uhai wa Mtume ﷺ, na wao waliona sehemu zake mbili.” Mtume ﷺ akasema,

«اشْهَدُوا»

“*Shuhudieni.*”³

Al-Bukhari na Muslim⁴ waliikusanya Hadithi hii.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa ‘Abdullah (Ibn Mas’ud رضي الله عنه) alisema, “Niliona mlima kati ya vipande viwili vya mwezi pale ulipopasuka.”⁵ Imamu Ahmad alimnukuu ‘Abdullah kuwa, “Mwezi ulipasuka wakati wa uhai wa Mtume ﷺ na niliona mlima kati ya vipande vyake viwili.”⁶

Ukaidi wa Washirikina na Msimamo wao Mbaya

Allah تعالى Amesema,

وَأَنْ يَرَوْا آيَةً

“*Na wakiona ishara.*”

Wao wanapoona dalili, ushahidi na alama.

يُعْرَضُوا

“*Hugeuka*”

Hawaziamini. Bali wanazikengeuka, wanazipa migongo yao.

¹ Muslim 4:2159.

² Tuhfatul Ahwadhi 9:175.

³ Ahmad 1:377.

⁴ *Fat’h Al-Bari* 8:483 na Muslim 4:2158.

⁵ At-Tabari 22:572.

⁶ Ahmad 1:413.

وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ ﴿٥٤﴾

“Na husema: Huu ni uchawi tu unazidi kuendelea.”

Wanasema, ‘Alama tuliyoiona ulikuwa uchawi, tuliorogezwa.’ Maana ya *Mustamir*, ‘Hivi karibuni utaisha’, kwa mujibu wa Mujahid, Qatadah¹ na wengine. Maana yake: Kuwa kupasuka kwa mwezi kulikuwa batili na hivi karibuni kutafifia na kupotea.

وَكَذَّبُوا وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ﴿٥٥﴾

“Na wamekanusha na wamefuata matamaniao yao.”

Wameukataa ukweli ulipowajia, wakafuata ujinga na upumbavu unaotokana na hadaa na tamaa zao. Kauli ya Allah تعالى،

وَكُلُّ أَمْرٍ مُّسْتَقَرٌّ ﴿٥٦﴾

“Na kila jambo ni lenye kuthibiti.”

Maana yake: Kheri itakuwa kwa watu wa kheri na shari itakuwa kwa watu shari,² ilhali Ibn Jurayj alisema, “Yatawafika wao kulingana na watu wake.”³ Mujahid alitoa rai juu ya maana ya,

وَكُلُّ أَمْرٍ مُّسْتَقَرٌّ ﴿٥٧﴾

“Na kila jambo ni lenye kuthibiti.”

Kwa kusema, “Katika Siku ya Kiama.” Kauli ya Allah تعالى،

وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنَ الْأَنْبَاءِ ﴿٥٨﴾

“Na bila ya shaka zimewajia wao habari.”

Katika hii Qur’an, zimewajia habari za umma zilizopita ambazo zilikadhibisha Mitume wao pamoja na maelezo ya adhabu, mateso na hilaki zilizowaangukia,

¹ At-Tabari 22:570.

² At-Tabari 22:572.

³ Adur - Al-Manthur 7:673.

مَا فِيهِ مُزْدَجَرٌ

“Zenye makaripio.”

Zenye maonyo na mafunzo ya kuwataka waache ushirikina na kuendelea kwao na ukadhibishaji.

حِكْمَةٌ بَلِغَةٌ

“Hekima kamili.”

Katika muongozo wake Allah تعالى, Humuongoa Amtakaye, na Humuacha apotee anayetaka,

فَمَا تُغْنِ النُّذُرُ

“Lakini waonyaji hawawafai wao kitu!”

Maana yake: Lakini hotuba za maonyo haziwasaidii wale ambao Allah تعالى Amewaandikia uovu na kupiga mihuri nyoyo zao.

Ni nani atakayewaongoa watu wa aina hii badala ya Allah? Aya hii inalingana na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

قُلْ فَلِلَّهِ الْحُجَّةُ الْبَلِغَةُ ۗ فَلَوْ شَاءَ لَهَدْنَاكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٤٩﴾

“Sema: Basi Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye hoja ya kukata. Na kama Angelipenda Angekuongezeni nyinyi nyote.” (6:149) Na,

وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ وَالنُّذُرُ عَنْ قَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٥١﴾

“Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasioamini.” (10:101)

فَتَوَلَّ عَنْهُمْ يَوْمَ يَدْعُ الدَّاعِ إِلَىٰ شَيْءٍ نُّكْرٍ ﴿١٥١﴾ خُشْعًا أَبْصَرُهُمْ تَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ كَأَنَّهُمْ جَرَادٌ مُّنتَشِرٌ ﴿١٥٢﴾ مُهْطِعِينَ إِلَى الدَّاعِ ۗ يَقُولُ الْكٰفِرُونَ هٰذَا يَوْمٌ عَسِرٌ ﴿١٥٣﴾

6. Basi jiepushe nao. Siku atakapoita mwitaji kuliendea jambo zito (la kiama);

7. Macho yao yatainama chini; watatoka makaburini kama nzige waliotawanyika.

8. Wanamkimbilia munitaji, na makafiri wanasema: Hii ni siku ngumu.

Mwisho Mbaya wa Makafiiri Siku ya Kiyama

Allah تعالیٰ Anasema, ‘Ewe Muhammad, wape mgongo watu hawa ambao pale, wanapoona muujiza, wao hukadhibisha na kusema huu ni uchawi unaoendelea.’ Wape mgongo na usubiri mpaka,

يَوْمَ يَدْعُ الدَّاعُ إِلَىٰ شَيْءٍ نُّكْرٍ

“Siku atakapoita munitaji kuliendea jambo linalochusha.”

Maana yake: Kwenye kitu kibaya kinachotisha. Nayo ni Hesabu na yaliyo ndani yake miongoni mwa balaa, zilzala na vitisho.

خُشَعًا أَبْصَرُهُمْ

“Macho yao yatainama.”

Macho yao yatadhalilika.

تَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ كَأَنَّهُمْ جَرَادٌ مُّنتَشِرٌ

“Watatoka makaburini kama nzige waliotawanyika.”

Watakusanyika haraka sana katika eneo la Hesabu kwa makundi, kwa kumuitika munitaji kama vile makundi ya nzige wakienea kila mahali. Allah تعالیٰ Amesema,

مُهْطِعِينَ

“Wanamkimbilia.” Maana yake: Upesi upesi.

إِلَىٰ الدَّاعِ ط

“Kwa munitaji.” Bila kusita wala kuchelewa.

يَقُولُ الْكَافِرُونَ هَذَا يَوْمٌ عَسِيرٌ

“Na makafiri wanasema: Hii ni siku ngumu.” Maana yake: ‘Hii ni Siku ngumu, kali, ya kutisha na ya huzuni.’

فَذَلِكَ يَوْمَئِذٍ يَوْمٌ عَسِيرٌ ﴿١٠﴾ عَلَى الْكَافِرِينَ غَيْرُ يَسِيرٍ ﴿١١﴾

“Siku hiyo, itakuwa ngumu. Kwa makafiri haitakuwa nyepesi.”
(74:9-10)

* كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ فَكَذَّبُوا عَبْدَنَا وَقَالُوا مَجْنُونٌ وَازْدَجَرَ ﴿١٠﴾ فَدَعَا رَبَّهُ أَنِّي مَغْلُوبٌ فَانتَصِرْ ﴿١١﴾ فَفَتَحْنَا أَبْوَابَ السَّمَاءِ بِمَاءٍ مُّثَمَرٍ ﴿١٢﴾ وَفَجَّرْنَا الْأَرْضَ عُيُونًا فَالْتَقَى الْمَاءُ عَلَى أَمْرٍ قَدَرٍ ﴿١٣﴾ وَحَمَلْنَاهُ عَلَى ذَاتِ الْأَلْوَحِ وَدُسِرَتْ ﴿١٤﴾ تَجْرِي بِأَعْيُنِنَا جَزَاءً لِمَنْ كَانَ كُفِرَ ﴿١٥﴾ وَلَقَدْ تَرَكْنَاهَا آيَةً فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ﴿١٦﴾ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذْرٍ ﴿١٧﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ﴿١٨﴾

9. Kabla yao kaumu ya Nuhu walikanusha; wakamkanusha mja Wetu, na wakasema ni mwendawazimu, na kumkaripia.

10. Ndipo Basi akamuomba Mola Wake Mlezi akasema: Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi naomba Uninusuru!

11. Mara Tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika.

12. Na Tukazipasua chemchem za maji katika ardhi yakakutana kwa jambo liliokadiriwa.

13. Na Tukamchukua kwenye Jahazi iliyotengenezwa kwa mbao na misumari.

14. Ikawa inakwenda kwa uangalizi Wetu, kama ni malipo kwa aliyekuwa amekanushwa.

15. Na bila ya shaka Tuliacha iwe ni Ishara. Lakini je, yupo anaye kumbuka?

16. Basi ilikuwaje adhabu Yangu, na maonyo Yangu.

17. Na bila ya shaka Sisi Tumeifanya Qur’ani iwe nyepesi kufahamika. Lakini yupo anayekumbuka?

Kisa cha Watu wa Nabii Nuhu عليه السلام na Mafunzo Yake, na Visa vya Kaumu (zingine)

Allah تعالى Amesema,

كَذَّبَتْ

“Walikanusha.”

‘Kabla ya watu wako wewe Ewe Muhammad.’

قَوْمُ نُوحٍ فَكَذَّبُوا عَبْدَنَا

“Kaumu ya Nuhu, wakamkanusha mja Wetu.”

Maana yake: Walimkataa waziwazi kwa kumkadhibisha na kumsingizia kichaa.

وَقَالُوا مَجْنُونٌ وَّازْدَجَرَ

“Na wakasema ni mwendawazimu, na akakaripiwa.”

Mujahid alisema kuhusu *Wazdujir*: “Alifukuzwa kwa madai kuwa alikuwa mwendawazimu.”¹ Kulisemwa pia kuwa maana ya *Wazdujir*, alikaripiwa, alivunjwa moyo, alitishwa na akaonywa na watu wake:

قَالُوا يَا نَحْنُ لَمْ تَنْتَه يَنْوُحُ لَتَكُونَنَّ مِنَ الْمَرْجُومِينَ ﴿١١٦﴾

“Wakasema: Ikiwa huachi, ewe Nuhu, bila ya shaka utapigwa mawe.” (26:116)

Haya yalisemwa na Ibn Zayd,² na ni thabiti.

فَدَعَا رَبَّهُ أَنِّي مَغْلُوبٌ فَأَنْتَصِرْ ﴿١١٧﴾

“Basi akamuomba Mola Wake Mlezi akasema: Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi naomba ninusuru!”

Maana yake: ‘Mimi ni dhaifu na siwezi kuwashinda au kuwazuia watu wangu, hivyo isaidie dini Yako!’ Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 22:576.

² At-Tabari 22:577.

فَفَتَحْنَا أَبْوَابَ السَّمَاءِ بِمَاءٍ مُّهِيبٍ ﴿١٧﴾

“Basi Tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika.”

As-Suddi alisema kuhusu *Munhamir*, Maana yake: “Mengi.”¹

وَفَجَّرْنَا الْأَرْضَ عُيُونًا

“Na Tukazipasua ardhi kwa chemchem.”

Maana yake: Kutoka kila sehemu ya ardhi, na hata katika jiko ambapo moto ulikuwa unawaka — maji na chemchemi zikibubujika.

فَالْتَقَى الْمَاءُ

“Yakakutana maji.”

Maana yake: Kutoka mbinguni na katika ardhi,

عَلَىٰ أَمْرٍ قَدْ قُدِرَ

“Kwa jambo liliokadiriwa.”

Ibn Jurayj alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما:

فَفَتَحْنَا أَبْوَابَ السَّمَاءِ بِمَاءٍ مُّهِيبٍ ﴿١٧﴾

“Basi Tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika.”

Mbingu haijawahi kunyesha kabla ya siku hiyo mvua nyingi, maji pekee yaliyotoka mbinguni kabla ya siku hiyo na tangu wakati huo yakawa yanatoka mawinguni. Lakini milango ya mbingu ilifunguliwa juu yao siku hiyo, na kwa hivyo, maji yaliyokuja hayakutoka mawinguni. Hivyo maji ya sehemu zote mbili (ardhini na mbinguni) yalikutana kwa jambo lilioloamriwa.”² Allah تعالى Amesema,

وَحَمَلْنَاهُ عَلَىٰ ذَاتِ الْأَلْوَحِ وَدُسِّرِ ﴿١٨﴾

“Na Tukamchukua kwenye safina ya mbao na misumari.”

¹ Al-Qurtubi 17:131.

² Ad-Dur Al-Manthur 7:675.

Ibn ‘Abbas , Sa’id bin Jubayr, Al-Quradhi, Qatadah na Ibn Zayd رضي الله عنه walisema kuwa *Dusur* maana yake misumari.¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliikhitari rai hii.² Kauli ya Allah تعالى،

تَجْرِي بِأَعْيُنِنَا

“Ikawa inakwenda kwa nadhari yetu.”

Maana yake: ‘Kwa Amri Yetu chini ya Ulinzi na Uangalizi Wetu,’

جَزَاءَ لِمَنْ كَانَ كُفِرَ

“Kuwa ni malipo kwa alivyo kuwa amekanushwa.”

Maana yake: Kama malipo yao kwa sababu ya wao kumkufuru Allah تعالى na kama zawadi kwa Nuhu عليه السلام. Allah تعالى Amesema،

وَلَقَدْ تَرَكْنَهَا آيَةً

“Na bila ya shaka Tuliacha safina ile ili iwe ni Ishara.”

Qatadah alisema, “Allah تعالى Aliiacha safina ya Nabii Nuhu عليه السلام ikiwa nzima kama ilivyokuwa hata kizazi cha kwanza cha umma huu kimeiona.”³

Hata hivyo, inajionesha hapa kuwa Allah تعالى Aliihifadhi safina hiyo kama alama, kwa ajili ya mfano, Allah تعالى Amesema،

وَأَيُّهُمْ أَنَا حَمَلْنَا ذُرِّيَّتَهُمْ فِي الْفُلِكِ الْمَشْحُونِ ﴿٤١﴾ وَخَلَقْنَا لَهُمْ مِنْ مِثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ ﴿٤٢﴾

“Na ni Ishara kwao kwamba Sisi Tuliwapakia vizazi vyao katika majahazi yaliyosheheni. Na Tukawaumbia vipando mfano wake wa vile wanavyovipanda.” (36:41-42),

إِنَّا لَمَّا طَغَا الْمَاءُ حَمَلْنَاكُمْ فِي الْجَارِيَةِ ﴿١١﴾ لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذْكِرَةً وَنَعْيًا أَدْنَىٰ وَعَيْتٌ ﴿١٢﴾

“Maji yalipofurika Sisi Tulikupandisheni katika safina, Ili Tuyafanye hayo kuwa ni waadhi kwenu na kila sikio linalosikia liyahifadhi.” (69:11-12),

¹ At-Tabari 22:580 na Al-Qurtubi 17:132.

² At-Tabari 22:578.

³ At-Tabari 22:582.

Allah تعالى Amesema; Kauli ya Allah تعالى katika Aya hii,

فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ

“Je, yupo anayekumbuka?”

Maana yake: ‘Kuna yeyote atakayepokea maonyo haya na kukumbuka?’ Imamu Ahmad alimnukuu ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه kuwa alisema, “Mtume ﷺ alinisomea,

فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ

“Je, yupo anayekumbuka?”¹

Al-Bukhari aliikusanya Hadithi sawa na hii kutoka kwa ‘Abdullah رضي الله عنه aliyesema, “Nilimsomea Mtume ﷺ,

(فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ)

“Je, yupo anayekumbuka?”

Naye akasema,²

فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ

“Je, yupo anayekumbuka?”

Kauli ya Allah تعالى,

فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذُرِي ﴿٥٤﴾

“Basi ilikuwaje adhabu Yangu, na maonyo Yangu.”

Maana yake: ‘Namna gani ilivyokuwa ya kutisha adhabu Yangu Niliyowaadhibu wale walionikufuru Mimi na wakawakataa Mitume Wangu, na kudharau Maonyo Yangu. Ulikuwaje Msaada Wangu Niliowapa Mitume na kilikuwaje kisasi Changu kwao?’

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ

“Na bila ya shaka Sisi Tumeifanya Qur’ani iwe nyepesi kufahamika.”

¹ Fat’h Al-Bari 8:485.

² Fat’h Al-Bari 8:484.

Maana yake: ‘Tumeifanya Qur’an kuwa rahisi kuisoma na kuifahamu kwa ajili ya, kumkumbusha mwanaadamu.’ Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

كَيْتَبُ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ مُبَارَكٌ لِيَدَّبَّرُوا آيَاتِهِ وَلِيَتَذَكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٣٨﴾

“Na Kitabu, hiki Tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya zake, na wawaidhike wenye akili.” (38:29),

فَإِنَّمَا يَسَّرْنَاهُ بِلِسَانِكَ لِتُبَشِّرَ بِهِ الْمُتَّقِينَ وَتُنذِرَ بِهِ قَوْمًا لُدًّا ﴿١٩﴾

“Na hakika Tumeifanya nyepesi (Qur’ani) kwa ulimi wako, ili uwabashirie kwayo wachamungu, na uwaonye kwayo watu wabishi.” (19:97)

Allah تعالى Amesema,

فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ

“Je, yupo anayekumbuka?”

Maana yake: ‘Kuna yeyote atakayekumbuka kupitia Qur’an hii, ambayo Tumeifanya rahisi kuikumbuka na kuielewa? ‘ Muhammad bin Ka’b Al-Quradhi alitoa rai juu ya Aya hii akasema, “Je kuna yeyote atakayeji pusha na maovu?”¹

* * *

¹Ad-Dur Al-Manthur 7:676.

كَذَّبَتْ عَادٌ فَكَيْفَ كَانَ عَدَابِي وَنُذِرِ ﴿١٨﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا
 عَلَيْهِمْ رِيحًا صَرْصَرًا فِي يَوْمِ نَحْسٍ مُّسْتَمِرٍّ ﴿١٩﴾ تَنْزِعُ
 النَّاسَ كَأَنَّهُمْ أُعْجَازُ خَلْجٍ مُّنْقَعِرٍ ﴿٢٠﴾ فَكَيْفَ كَانَ عَدَابِي
 وَنُذِرِ ﴿٢١﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْءَانَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُّذَكِّرٍ ﴿٢٢﴾
 كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِالنُّذُرِ ﴿٢٣﴾ فَقَالُوا أَبَشْرًا مِّمَّنَّا وَاحِدًا نَتَّبِعُهُ
 إِنَّا إِذًا لَّيُفِي ضَلَالِي وَسُغُرٍ ﴿٢٤﴾ أَلَيْسَ الذِّكْرُ عَلَيْهِ مِنْ بَيْنِنَا
 بَلْ هُوَ كَذَابٌ أَشْرٌ ﴿٢٥﴾ سَيَعْمُونَ غَدًا مِنَ الْكَذَابِ
 الْأَشْرُ ﴿٢٦﴾ إِنَّا مُرْسَلُونَ أَنْفَاقَهُ فِتْنَةً لَهُمْ فَارْتَبِعِهِمْ وَأَصْطِرِبْ
 وَنَبِّئِهِمْ أَنَّ الْمَاءَ قِسْمَةٌ بَيْنَهُمْ كُلُّ شِرْبٍ مُحْتَضَرٌ ﴿٢٧﴾
 فَتَادُوا صَاحِبَهُمْ فَتَعَاطَى فَعَقَرَ ﴿٢٨﴾ فَكَيْفَ كَانَ
 عَدَابِي وَنُذِرِ ﴿٢٩﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ صَيْحَةً وَاحِدَةً فَكَانُوا
 كَهَشِيمِ الْمُخْتَطِرِ ﴿٣٠﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْءَانَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ
 مِنْ مُّذَكِّرٍ ﴿٣١﴾ كَذَّبَتْ قَوْمُ لُوطٍ بِالنُّذُرِ ﴿٣٢﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا
 عَلَيْهِمْ حَاصِبًا إِلَّا ءَالَ لُوطٍ حَجَّتْهُمْ بِسْحَرٍ ﴿٣٣﴾ نِعْمَةٌ
 مِنْ عِنْدِنَا كَذَلِكَ نَجْزِي مَنْ شَكَرَ ﴿٣٤﴾ وَلَقَدْ أَنْذَرَهُمْ
 بَطْشَتَنَا فَتَمَارَوْا بِالنُّذُرِ ﴿٣٥﴾ وَلَقَدْ رَاوَدُوهُ عَنْ صَيفِيهِ
 فَطَمَسْنَا أَعْيُنَهُمْ فَذُوقُوا عَدَابِي وَنُذِرِ ﴿٣٦﴾ وَلَقَدْ
 صَبَّحَهُمْ بُكْرَةً عَذَابٌ مُّسْتَقِرٌّ ﴿٣٧﴾ فَذُوقُوا عَدَابِي وَنُذِرِ
 ﴿٣٨﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْءَانَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُّذَكِّرٍ ﴿٣٩﴾

كَذَّبَتْ عَادٌ فَكَيْفَ كَانَ عَدَابِي وَنُذِرِ
 ﴿١٨﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا
 صَرْصَرًا فِي يَوْمِ نَحْسٍ مُّسْتَمِرٍّ ﴿١٩﴾
 تَنْزِعُ النَّاسَ كَأَنَّهُمْ أُعْجَازُ خَلْجٍ
 مُّنْقَعِرٍ ﴿٢٠﴾ فَكَيْفَ كَانَ عَدَابِي
 وَنُذِرِ ﴿٢١﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْءَانَ
 لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُّذَكِّرٍ ﴿٢٢﴾

18. Kina A'di walikanusha. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo yangu?

19. Hakika Sisi Tuliwapelekea upepo wenye baridi na sauti kali katika siku ya nuksi mfululizo.

20. Ukiwang'oa watu kama vigogo vya mitende viliong'olewa.

21. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo yangu?

22. Na bila ya shaka Sisi Tumeifanya nyepesi Qur'ani kufahamika; lakini yupo anayekumbuka?

Habari ya 'Ad

Allah تعالى Anaeleza kuwa 'Ad, ni watu wa Hud عليه السلام, walimkana Mtume wao, kama walivyofanya watu wa Nuhu عليه السلام. Kwa hivyo, Allah تعالى Aliwapelekea juu yao,

عَلَيْهِمْ رِيحًا صَرْصَرًا

“Upepo wa kimbunga.”

Maana yake: Baridi kali na upepo wenye nguvu,

فِي يَوْمٍ نَحْسٍ

“Katika siku korofi.”

Dhidi yao, kwa mujibu wa Adh-Dhahhak, Qatadah na As-Suddi,¹

مُسْتَمِرٍّ

“Mfululizo.”

Juu yao kwa sababu ya maafa, adhabu na maangamizi yaliyowasibu humu duniani siku hiyo yanaendelea mpaka Akhera,

تَنَزَّعَ النَّاسَ كَأَنَّهُمْ أَعْجَازُ نَخْلٍ مُنْقَعِرٍ ﴿١٨﴾

“Ukiwang’oa watu kama vigogo vya mitende viliong’olewa”

Upepo ulikuwa ukim’oa mmoja wao na kumnyanyua juu, mpaka akawa haonekani, kisha kwa nguvu sana alirudishwa kichwa chini. Kichwa chake kilipondwa na mwili wake ndio uliosalia, bila ya kichwa.

كَأَنَّهُمْ أَعْجَازُ نَخْلٍ مُنْقَعِرٍ ﴿١٨﴾ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذْرٍ ﴿١٩﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْءَانَ لِلذِّكْرِ
فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ﴿٢٠﴾

“Kama vigogo vya mitende viliong’olewa. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu? Na bila ya shaka Sisi Tumeifanya nyepesi Qur’ani kufahamika; lakini yupo anaye kumbuka?”

¹ At-Tabari 22:587.

كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِالنُّذُرِ ﴿١٨﴾ فَقَالُوا أَبَشَرًا مِثَّنَا وَاحِدًا نَتَّبِعُهُ إِنَّا إِذَا لَفِيَ ضَلَالٍ وَسُعُرٍ ﴿١٩﴾
 أَلَيْسَ الَّذِي آذَىٰ عَلَيْهِ مِن بَيْنِنَا بَلْ هُوَ كَذَّابٌ أَشِرٌّ ﴿٢٠﴾ سَيَعْمُونَ غَدًا مِّنَ الْكَذَّابِ الْأَشِرِّ
 ﴿٢١﴾ إِنَّا مُرْسَلُونَ النَّاقَةَ فِتْنَةً هُمْ فَآزَنَتِمْ وَأَصْطَبِرُ ﴿٢٢﴾ وَتَبِعْتُمْ أَنَّ الْمَاءَ قِسْمَةٌ بَيْنَهُمْ
 كُلُّ شَرِبٍ مُحْتَضِرٌ ﴿٢٣﴾ فَتَنَادَوْا صَاحِبُهُمْ فَتَعَاطَىٰ فَعَقَرَ ﴿٢٤﴾ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذُرِ
 ﴿٢٥﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ صَيْحَةً وَاحِدَةً فَكَانُوا كَهَشِيمِ الْحَتِّظِرِ ﴿٢٦﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا
 الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِن مُّدَكِّرٍ ﴿٢٧﴾

23. *Thamudi waliwakanusha Waonyaji.*

24. *Wakasema: Ati tumfuate binaadamu mmoja katika sisi? Basi hivyo sisi tutakuwa katika upotofu na ukichaa!*

25. *Ni yeye tu aliyeteremshiwa huo ukumbusho kati yetu sote? Bali huyu ni mwongo mwenye kiburi!*

26. *Kesho watajua ni nani huyo mwongo mwenye kiburi.*

27. *Hakika Sisi Tutawapelekea ngamia jike ili kuwajaribu, basi watazame tu na ustahamili.*

28. *Na waambie kwamba maji yatagawanywa baina yao; kila sehemu ya maji itahudhuriwa na aliyekhusika.*

29. *Basi wakamuita mtu wao akaja akamchinja.*

30. *Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!*

31. *Hakika Sisi Tuliwapelekea ukelele mmoja tu, wakawa kama mabuwa ya kujengea uwa.*

32. *Na bila ya shaka Sisi Tumeifanya Qur'ani iwe nyepesi kwa kukumbuka, lakini yupo akumbukaye?*

Kisa cha Thamud

Allah تعالی Anaeleza hapa kuwa watu wa Thamud walimkataa Mtume wao Salih عليه السلام,

فَقَالُوا أَبَشَرًا مِّنَّا وَاحِدًا نَّتَّبِعُهُمْ إِنَّا إِذَا لَفِئَ صُلَّيْ وَسُعُرٍ ﴿١٧﴾

“Wakasema: Ati tumfuata binaadamu mmoja katika sisi? Basi hivyo sisi tutakuwa katika upotofu na ukichaa!”

Na wao walisema, ‘Tutakuwa tumefeli na tumepata hasara kama sisi sote tutajisalimisha kwa mtu mmoja miongoni mwetu.’ Walishangazwa kuwa mkumbushaji alitumwa kwao yeye peke yake tu, na kwa hivyo, wakamshutumu kuwa ni mwongo,

بَلْ هُوَ كَذَّابٌ أَشِرُّ

“Bali huyu ni mwongo mwenye kiburi!”

Maana yake: Anevuka mipaka katika uongo wake. Allah تعالی Alijibu,

سَيَعْلَمُونَ غَدًا مِّنَ الْكَذَّابِ الْأَشِرِّ ﴿١٨﴾

“Kesho watajua ni nani huyo mwongo mwenye kiburi.”

Na kwa hivyo kuwaonya na kuwatisha wao na kuwapa ahadi ya kweli.

إِنَّا مُرْسَلُونَ لِنَأْفِقَ فِتْنَةَ هُمْ

“Hakika Sisi Tutawapelekea ngamia jike ili kuwajaribu.”

Kwa kuwapa jaribio kaumu ya Thamud, Allah تعالی Aliwapelekea ngamia jike bora, mwenye mimba aliyetoka katika mwamba mgumu, kwa mujibu wa maombi yao, kama ushahidi kutoka kwa Allah تعالی. Baadaye, walitakiwa kuyaamini waliyoletewa na Nabii Salih عليه السلام. Allah تعالی Alimuamuru Mja na Mjumbe Wake عليه السلام,

فَأَرْتَقِبْهُمْ وَأَصْطَبِرْ

“Basi watazame tu na ustahamili.” Allah تعالی Aliamuru, ‘Subiri, Ewe Salih, na uangalie kitakachowafika, nawe uwe mstahamilivu; kwa hakika, mwisho bora utakuwa kwako, nawe utapata mafanikio humu duniani na Akhera.’

وَنُنْفِثُهُمْ أَنْ الْمَاءَ قِسْمَةٌ بَيْنَهُمْ^ط

“Na waambie kwamba maji yatagawanywa baina yao.”

Siku moja kwa ajili ya ngamia anywe na siku moja kwa ajili yao wao wanywe.

قَالَ هَذِهِ نَاقَةٌ هَاهَا شَرِبَتْ وَلَكُمْ شَرِبَ يَوْمٍ مَعْلُومٍ ﴿١٥٥﴾

“Akasema: ngamia huyu jike; awe na zamu yake ya kunywa, na nyinyi muwe na zamu yenu ya kunywa katika siku maalumu.”
(26:155)

Kauli ya Allah تعالى،

كُلُّ شَرِبٍ مُّحْتَضِرٌ

“Kila sehemu ya maji itahudhuriwa.”

Mujahid alisema, “Siku Ngamia huyo hanywi, wao waliweza kunywa maji, na wakati ambapo hawakuyanywa, basi walikunywa maziwa yake.”¹

Allah تعالى Amesema;

فَتَادُوا صَاحِبِهِمْ فَتَعَاطَىٰ فَعَقَرَ ﴿١٥٦﴾

“Basi wakamuita mtu wao akaja akamchinja.”

Kwa mujibu wa Wanazuoni wa Tafsiri, alikuwa akiitwa Qudar bin Salif; yeye ndiye alikuwa muovu zaidi kati yao,

إِذْ أَنْبَعَتْ أَشَقْنَهَا ﴿١٥٧﴾

“Aliposimama mwovu wao mkubwa.” (91:12)

Allah تعالى Amesema hapa,

فَتَعَاطَىٰ

“Akaja.”

Maana yake: Kudhuru,

¹ At-Tabari 22:592.

فَعَقَّرَ ﴿١٨﴾ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذْرِ ﴿١٩﴾

“Akamchinja. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!”

‘Niliwaadhibu, basi ilikuwaje adhabu Niliyowapa kwa sababu ya kutoniamini na kumkana Mjumbe Wangu.’

إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ صَيْحَةً وَاحِدَةً فَكَانُوا كَهَشِيمِ الْحَتِّظِرِ ﴿٢٠﴾

“Hakika Sisi Tuliwapelekea ukelele mmoja tu, wakawa kama mabuwa ya kujengea uwa.”

Waliisha wote mpaka wa mwisho wao na hakuna yeyote katika wao aliyesalia. Wakafa wote, kama mimea na majani yanavyokauka na kufa. As-Suddi alisema, “kuwa wao walikuwa kama nyasi kavu jangwani pindi zinapounguzwa na upepo unazitawanya zote.” Ibn Zayd alisema, “Waarabu walikuwa wakijenga uzio (*Hizar*, neno lililotoholewa kutokana na, *Al-Muhtazir*) uliofanywa kwa vichaka vikavu, kuzunguka ngamia na mifugo yao, kwa hivyo Allah تعالى Amesema,

كَهَشِيمِ الْحَتِّظِرِ

“Kama mabuwa ya kujengea uwa.”

كَذَّبَتْ قَوْمُ لُوطٍ بِالنُّذْرِ ﴿٢١﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ حَاصِبًا إِلَّا آءَالَ لُوطٍ حُجَيْنَهُمْ بِسَحْرِ ﴿٢٢﴾ نِعْمَةً مِّنْ عِنْدِنَا كَذَلِكَ نَجْزِي مَنْ شَكَرَ ﴿٢٣﴾ وَلَقَدْ أَنْذَرَهُمْ بَطْشَتَنَا فَتَمَارَوْا ﴿٢٤﴾ بِالنُّذْرِ ﴿٢٥﴾ وَلَقَدْ رَاوَدُوهُ عَن ضَيْفِيهِ فَطَمَسْنَا أَعْيُنَهُمْ فَذُوقُوا عَذَابِي وَنُذْرِ ﴿٢٦﴾ وَلَقَدْ صَبَّحَهُمْ بُكْرَةً عَذَابٌ مُّسْتَقَرٌّ ﴿٢٧﴾ فَذُوقُوا عَذَابِي وَنُذْرِ ﴿٢٨﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْءَانَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِن مُّذَكِّرٍ ﴿٢٩﴾

33. Kaumu Lut'i nao waliwakadhibisha Waonyaji.

34. Hakika Sisi Tukawapelekea kimbunga cha vijiwe, isipokuwa wafuasi wa Lut'i. Hao Tuliwaokoa karibu na alfajiri.

35. Kwa neema inayotoka Kwetu. Hivyo ndivyo Tumlipavyo anaye shukuru.

36. Na hakika yeye aliwaonya na Adhabu Yetu; lakini wao waliyatilia shaka hayo maonyo.

37. Na walimtaka awape wageni wake. Tukayapofua macho yao, na Tukawaambia: Onjeni basi adhabu na maonyo Yangu!

38. Na iliwafikia wakati wa asubuhi adhabu ya kuendelea.

39. Basi onjeni adhabu na maonyo Yangu!

40. Na hakika Tumeifanya nyepesi Qur’ani kuikumbuka. Lakini yupo anaye kumbuka?

Kisa cha Watu wa Nabii Lut عليه السلام

Allah تعالی Anaeleza kuwa watu wa Lut عليه السلام waliasi na wakamkataa Mjumbe wao na wakafanya maovu ya liwati, nao ni uchafu mbaya kabisa ambao hakuna watu wa kabla yao waliopata kuwatangulia kutenda dhambi hiyo. Hii ndiyo sababu Allah تعالی Aliwahilikisha kwa namna ya adhabu ambayo Hakuuhilikisha umati wowote kabla yao. Allah تعالی Alimuamuru Jibril عليه السلام, ainyanyue miji juu angani na kisha kuipindua juu chini ikifuatiwa na mawe yaliyofanywa kwa Sijji.¹ Kwa hivyo hapa Akasema:

إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ حَاصِبًا إِلَّا آلَ لُوطٍ لَّوَطٍ مُّجْتَبَيْنَهُمْ بِسِحْرِ

“Hakika Sisi Tukawapelekea kimbunga cha vijiwe, isipokuwa wafuasi wa Lut’i. Hao Tuliwaokoa karibu na alfajiri.”

Waliuacha mji wao katika sehemu ya mwisho ya usiku na wakanusuriwa kutokana na adhabu iliyowapata watu wao. Hakuna yeyote katika wao aliyemuamini Lut عليه السلام, hata mkewe alipatwa na adhabu iliyowakumba watu wake. Mtume Lut عليه السلام aliondoka Sodomakiwa pamoja na mabinti zake kwa usalama, pasi na kudhurika. Allah تعالی Amesema,

كَذَلِكَ نَجْزِي مَنْ شَكَرَ ﴿١٥﴾ وَلَقَدْ أَنْذَرَهُمْ بَطْشَتَنَا

“Hivyo ndivyo Tumlipavyo anayeshukuru. Na hakika yeye aliwaonya adhabu Yetu.”

¹ Angalia Tafsiri ya Surat Hud.

Maana yake: Kabla ya adhabu kuwafika watu wake, aliwaonya juu ya adhabu na mateso ya Allah تعالى. Wao hawakulijali onyo, wala hawakumsikiliza Lut عليه السلام, bali walitia shaka na wakafanya kiburi.

وَلَقَدْ رَاوَدُوهُ عَن صَيِّفِهِ

“Na walimtaka awape wageni wake.”

Maana yake: Usiku malaika Jibril عليه السلام, Mika'il عليه السلام na Israfil عليه السلام walimjia wakiwa katika umbo la vijana wazuri, kama mtihani kutoka kwa Allah تعالى kwa ajili ya kaumu ya Nabii Lut عليه السلام. Lut عليه السلام aliwakaribisha wageni wake, na mke wake mwovu, akatuma ujumbe kwa watu wake kuwajulisha juu ya wageni wa Lut عليه السلام. Wakamjia mbio kutoka kila upande, naye Lut عليه السلام alilazimika kuwafungia mlango. Wakaja wakati wa usiku na wakajaribu kuvunja mlango. Lut عليه السلام akajaribu kuwaondosha na kuwakinga wageni dhidi yao kwa kusema,

هَتُّوْلَاءِ بَنَاتِي إِن كُنتُمْ فَعٰلِيْنَ ﴿٧١﴾

“Hawa hapa mabinti zangu, ikiwa nyinyi ni wenye kutenda.”
(15:71),

Inakusudia wanawake wao,

قَالُوْا لَقَدْ عَلِمْتَمَا لَنَا فِيْ بَنَاتِكَ مِنْ حَقِّ

“Wakasema: Bila shaka umekwishajua hatuna haki juu ya mabinti zako.”

Maana yake: ‘Hatuna haja na wanawake,’

وَإِنَّكَ لَتَعْلَمُ مَا تُرِيْدُ ﴿٧٩﴾

“Na unayajua tunayoyataka.” (11:79)

Hali ilipozidi na wao wakasisitiza juu ya kuingia, Jibril عليه السلام aliwatokea na akawapiga macho yao kwa ncha ya ubawa na kuwasababishia kukosa kuona. Wakarejea kupapasa ukutani huku wakitoa vitisho kwa Lut عليه السلام juu ya nini kitampata wakati wa asubuhi.

Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ صَبَّحَهُم بُكْرَةً عَذَابٌ مُسْتَقِرٌّ ﴿٢٨﴾

“Na iliwafikia wakati wa asubuhi adhabu Yangu ya kuendelea.”

Maana yake: Adhabu ambayo hawakuwa na namna ya kuikwepa wala kuiepuka.

فَذُوقُوا عَذَابِي وَتُذِرِ ﴿٢٩﴾ وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ﴿٣٠﴾

“Basi onjeni adhabu na maonyo Yangu! Na hakika Tumeisahilisha Qur’ani kuikumbuka. Lakini yupo anaye kumbuka?”

* * *

وَلَقَدْ جَاءَ ءَالَ فِرْعَوْنَ النَّذِيرُ ﴿٤١﴾ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كُلِّهَا
 فَأَخَذْنَاهُمْ أَخَذَ عَزِيزٍ مُّقْتَدِرٍ ﴿٤٢﴾ أَكْفَارُكُمْ خَيْرٌ مِّنْ
 أَوْلِيَّتِكُمْ أَمْ لَكُمْ بَرَاءَةٌ فِي الزُّبُرِ ﴿٤٣﴾ أَمْ يَقُولُونَ نَحْنُ جَمِيعٌ
 مُّنتَصِرُونَ ﴿٤٤﴾ سَيُزَمُّ الْجَمْعُ وَيُوَلُّونَ الدُّبُرَ ﴿٤٥﴾ بَلِ
 السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَدْهَىٰ وَأَمَرٌ ﴿٤٦﴾ إِنَّ
 الْمُجْرِمِينَ فِي ضَلَالٍ وَسُعُرٍ ﴿٤٧﴾ يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ
 عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ ﴿٤٨﴾ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ
 بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾ وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ﴿٥٠﴾
 وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا أَشْيَاعَكُمْ فَهَلْ مِنْ مُّذَكِّرٍ ﴿٥١﴾ وَكُلُّ شَيْءٍ
 فَعَلُوهُ فِي الزُّبُرِ ﴿٥٢﴾ وَكُلُّ صَغِيرٍ وَكَبِيرٍ مُّسْتَطَرٌّ ﴿٥٣﴾ إِنَّ
 التَّقِيْنَ فِي جَنَّتٍ وَبِهَرٍ ﴿٥٤﴾ فِي مَقْعَدِ صِدْقٍ عِنْدَ مَلِيكٍ
 مُّقْتَدِرٍ ﴿٥٥﴾

وَلَقَدْ جَاءَ ءَالَ فِرْعَوْنَ النَّذِيرُ ﴿٤١﴾
 كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كُلِّهَا فَأَخَذْنَاهُمْ أَخَذَ
 عَزِيزٍ مُّقْتَدِرٍ ﴿٤٢﴾ أَكْفَارُكُمْ خَيْرٌ مِّنْ
 أَوْلِيَّتِكُمْ أَمْ لَكُمْ بَرَاءَةٌ فِي الزُّبُرِ ﴿٤٣﴾
 أَمْ يَقُولُونَ نَحْنُ جَمِيعٌ مُّنتَصِرُونَ ﴿٤٤﴾
 سَيُزَمُّ الْجَمْعُ وَيُوَلُّونَ الدُّبُرَ ﴿٤٥﴾ بَلِ
 السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَدْهَىٰ
 وَأَمَرٌ ﴿٤٦﴾

41. Na Waonyaji waliwafikia watu wa Firauni.

42. Walizikadhibisha Ishara Zetu zote. Nasi Tukawashika kama Anavyoshika Mwenye Nguvu Mwenye Uweza.

43. Je! Makafiri wenu ni bora kuliko hao, au yameandikwa vitabuni kuwa nyinyi hamtiwi makosani?

44. Au ndio wanasema: Sisi ni wengi tutashinda tu.

45. Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma.

46. Bali Saa ya Kiyama ndio miadi yao, na Saa hiyo ni nzito zaidi na chungu zaidi.

Kisa cha Firauni na Watu Wake

Allah تعالی Anatueleza kisa cha Firauni na watu wake. Mjumbe aliwajia kutoka kwa Allah تعالی, huyo ni Musa عليه السلام akisaidiwa na nduguye, Harun عليه السلام. Mitume wao waliwabashiria ikiwa wataamini, na kuwapa onyo ikiwa watakataa. Allah تعالی Aliwatia nguvu kwa miujiza na dalili kubwa, lakini Firauni na watu wake walikataa. Basi Allah تعالی Aliwaadhibu kwa namna ya adhabu ya mwenye nguvu mwenye kuweza; Aliwaangamiza wote bila kuacha yeyote wa kueleza kilichowasibu wala athari yoyote.

Nasaha kwa Makuraishi na Kupewa Onyo

Allah تعالی Amesema,

أَكْفَارُكُمْ

“Je! Makafiri wenu.”

Maana yake: ‘Enyi washirikina wa Kikuraishi.’

حَيْرٌ مِّنْ أَوْلِيَّكُمْ

“Ni bora kuliko hao.”

Maana yake: Bora kuliko umati uliotajwa hapa, ambao uliangamizwa kwa sababu ya wao kuwakana Mitume na kukataa Maandiko. ‘Nyinyi ni bora kuliko hao.’

أَمْ لَكُمْ بَرَاءَةٌ فِي الزُّبُرِ

“Au yameandikwa vitabuni kuwa nyinyi hamtiwi makosani?”

‘Je nyinyi mna kinga kwa Allah تعالی kuwa adhabu na mateso hayatakupateni.’ Allah تعالی Amesema kuhusu Makuraishi,

أَمْ يَقُولُونَ نَحْنُ جَمِيعٌ مُّنتَصِرُونَ ﴿٥٤﴾

“Au ndio wanasema: Sisi ni wengi tutashinda tu.”

Wanaamini kuwa wao wanasaidiana wao kwa wao au mkusanyiko wao mkubwa utawaepusha wao dhidi ya wenye kutaka kuwadhuru.

Allah تعالی Akasema,

سَيِّزِمُ الْجَمْعُ وَيُولُونَ الدُّبُرَ ﴿٤٥﴾

“Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma.”

Maana yake: Watatengana na watashindwa. Al-Bukhari alinukuu kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mtume ﷺ, akiwa katika hema lililokuwa katika umbo la kuba katika Siku ya vita ya Badr, alisema,

«أَتَشُدُّكَ عَيْدَكَ وَوَعْدَكَ، اللَّهُمَّ إِنْ شِئْتَ لَمْ نُعْبَدْ بَعْدَ الْيَوْمِ فِي الْأَرْضِ أَبَدًا»

“Ya Allah! Nakuomba Utimize ahadi na agano Lako. Ya Allah! Ikiwa Unataka (kuwaangamiza waumini) basi Hutaabudiwa ardhini baada ya leo abadani.”

Abubakr رضي الله عنه akamshika mkono na kusema, ‘Inatosha, Ewe Mjumbe wa Allah! Umeshamsisitiza Mola Wako tayari.’ Wakati huo Mtume ﷺ alikuwa amevaa dereya yake na akatoka huku akisoma,

سَيِّزِمُ الْجَمْعُ وَيُولُونَ الدُّبُرَ ﴿٤٥﴾ بَلِ السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَدْهَىٰ وَأَمَرٌ ﴿٤٦﴾

“Wingi wao utatimuliwa mbio na watageuza migongo yao. Bali Kiyama ndio muda wao uliopangwa, na itakuwa ya huzuni mno na chungu zaidi.”¹

Al-Bukhari pia alimnukuu Yusuf bin Mahak kuwa alisema, “Nilikuwa pamoja na Mama wa Waumini, ‘A’ishah, akasema, ‘Wakati nilipokuwa binti mdogo katika mji wa Makkah, Mtume Muhammad ﷺ aliteremshiwa Aya hii,

بَلِ السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَدْهَىٰ وَأَمَرٌ ﴿٤٦﴾

“Bali Saa ya Kiyama ndio miadi yao, na Saa hiyo ni nzito zaidi na chungu zaidi”²

Hivi ndivyo Al-Bukhari alivyoandika kwa ufupi, lakini alikusanya pia Simulizi kwa urefu katika Kitabu cha Fadhila za Qur’an.³ Muslim hakuandika Hadithi hii.

¹ Fat’h Al-Bari 8:485-486.

² Fat’h Al-Bari 8:485 na 486.

³ Fat’h Al-Bari 8:655.

إِنَّ الْمَجْرِمِينَ فِي ضَلَالٍ وَسُعُرٍ ﴿٤٧﴾ يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ ذُقُوا مَسَّ
 سَقَرٍ ﴿٤٨﴾ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾ وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ﴿٥٠﴾
 وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا أَشْيَاعَكُمْ فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ﴿٥١﴾ وَكُلُّ شَيْءٍ فَعَلُوهُ فِي الزُّبُرِ ﴿٥٢﴾ وَكُلُّ
 صَغِيرٍ وَكَبِيرٍ مُسْتَطَرٌّ ﴿٥٣﴾ إِنَّ الْأَتْقِينَ فِي جَنَّتِمْ وَنَهْرٍ ﴿٥٤﴾ فِي مَقْعَدِ صِدْقٍ عِنْدَ مَلِيكٍ
 مُّقْتَدِرٍ ﴿٥٥﴾

47. Hakika waovu wamo katika upotofu na wazimu.

48. Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu!

49. Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo.

50. Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.

51. Na bila ya shaka Tumekwishawaangamiza wenzenu. Lakini yupo anayekumbuka?

52. Na kila jambo walilolifanya limo vitabuni.

53. Na kila kidogo na kikubwa kimeandikwa.

54. Hakika wachamungu watakuwa katika bustani na mito.

55. Katika makao mazuri na yakuridhiria ya Mfalme Mwenye Uweza.

Mwisho wa Watu Waovu

Allah تعالیٰ Anaeleza kuwa waovu wamepotoka mbali na ukweli na wamemezwa ndani ya hali ya kuchanganyikiwa, kwa sababu ya shaka na wasiwasi waliomo. Maelezo haya yanaendana na kila kafiri na mzushaji wa madhehebu ya kila aina na namna. Allah تعالیٰ Anasema,

يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ

“Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe.”

Maana yake: Kama walivyomezwa katika shaka, wasiwasi na kusitasita, wameishia Motoni. Na kama walivyopotea, wataishia katika kuburuzwa juu

ya nyuso zao, hawajui watapelekwa wapi. Wataambiwa kwa kukemewa na kufedheheshwa,

ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ

“Nyinyi onjeni mguso wa Jahannamu!”

Kila Kitu Kiliumbwa na Makadirio Yake (Kadari)

Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥٤﴾

“Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo.”

Ni Kauli Yake Allah تعالى,

وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَرَهُ تَقْدِيرًا ﴿٥٥﴾

“...na Akaumba kila kitu na Akakikadiria kwa kipimo.” (25:2) na,

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿٥٦﴾ الَّذِي خَلَقَ فَسَوَّى ﴿٥٧﴾ وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَى ﴿٥٨﴾

“Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa, Aliyeumba, na Akaweka sawa. Na Ambaye Amekadiria na Akakiongoza.”(87:1-3),

Maana yake: Alikawekea kipimo kila kitu Akawaongoza viumbe katika kukiendea. Maimamu wa Sunnah wanathibitisha kupitia Aya hii tukufu kama ushahidi kuwa Allah تعالى Ameumba viumbe pamoja na kadari zao, kabla hawajaumbwa. Allah تعالى Anakijua kila kitakachotukia kabla ya kutukia na Aliandika kila kitu kitakachotokea kabla ya kufanyika. Wametumia Aya hii na zinazofanana nayo pamoja na Hadithi kupinga mtazamo wa madhehebu ya *Qadariyyah*, ambayo yaliibuka wakati wa zama za mwisho za Masahaba. Mada hii nimeieleza kwa kirefu katika maelezo juu ya mlango wa Imani katika Sahih Al-Bukhari. Hapa nitataja baadhi ya Hadithi zinazofungamana na Aya hii tukufu.

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Washirikina wa Kikuraishi walikuja kwa Mtume ﷺ kubishana naye huku wakipuuza suala la *Qadar*. Aya ifuatayo ikateremshwa,

يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ ذُقُوا مَسَّ سَقَرٍ ﴿٤١﴾ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٢﴾

“Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu! Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo.”¹

Muslim, At-Tirmidhi na Ibn Majah walikusanya Hadithi hii.² Al-Bazzar alinukuu kutoka kwa ‘Amr bin Shu’ayb kutoka kwa baba yake alisimulia kuwa babu yake alisema, “Aya hizi ziliteremshwa kuhusu wanaokanusha *Al-Qadar*,

إِنَّ الْمَجْرِمِينَ فِي ضَلَالٍ وَسُعْرٍ ﴿٤٣﴾ يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ ذُقُوا مَسَّ سَقَرٍ ﴿٤٤﴾ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٥﴾

“Hakika wakosefu wamo katika upotofu na wazimu. Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu! Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo.”³

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى pia alinukuu kuwa Zurarah alisema kuwa baba yake alisema kuwa Mtume ﷺ alisoma Aya hii,

ذُقُوا مَسَّ سَقَرٍ ﴿٤٦﴾ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٧﴾

“Onjeni mguso wa Jahannamu! Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo.”

Na akasema,

«نَزَلَتْ فِي أَنَاسٍ مِنْ أُمَّتِي يَكُونُونَ فِي آخِرِ الزَّمَانِ يُكذَّبُونَ بِقَدْرِ اللَّهِ»

“Aya hizi ziliteremka kuhusu baadhi ya watu wa umati wangu watakaokuja zama za mwisho watakaokuwa wanakadhibisha *Al-Qadar*.”⁴

¹ Ahmad 1:444.

² Muslim 4:2046. *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:176 na Ibn Majah 1:32.

³ *Kashf Al-Astar* 3:72, kuna udhaifu kidogo katika isnadi ya wasimulizi.

⁴ At-Tabarani 5:276.

Ata' bin Abu Rabah alisema, "Nilikwenda kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na nikamkuta akichota maji kutoka kisima cha Zamzam. Chini ya nguo zake kulikuwa kumelowa maji ya Zamzam, nami nikamuambia, 'Pamezungumziwa juu ya Al-Qadar.' Akauliza, 'Wamefanya hivyo?' Nikajibu, 'Ndiyo.' Akasema, 'Naapa kwa Jina la Allah تعالیٰ! Aya hii iliteremka mahususi kwa ajili yao.

ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ ﴿٥٤﴾ إِنَّا كُلُّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥٥﴾

"Onjeni mguso wa Jahannamu! Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo."

Hao ni watu waovu wa umati huu. Usiwazuru wagonjwa wao wala kusalia maiti wao. Ikiwa nitamuona mmoja wao, ninaweza kumng'oa macho yake kwa vidole vyangu hivi viwili."¹

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Nafi' alisema, "'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنه alikuwa na rafiki katika Miji ya Ash-Sham ambaye wakiandikiana barua. 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنه alimuandikia, 'Niliambiwa kuwa umeanza kuzungumzia kuhusu Al-Qadar. Kwa hivyo, usithubutu kuniandikia kitu chochote tena. Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«سَبَّكُونُ فِي أُمَّتِي أَفْرَامٌ يُكَذِّبُونَ بِالْقَدَرِ»

*"Kutakuwa katika umati wangu watu watakaokataa Al-Qadar."*²

Abu Dawud alikusanya Hadithi hii kutoka kwa Ahmad bin Hanbal.³ Imamu Ahmad alimnukuu 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema,

«كُلُّ شَيْءٍ بِقَدَرٍ حَتَّى الْعَجْزُ وَالْكَبِيرُ»

*"Kila kitu kimekadiriwa, hata kushindwa na akili."*⁴

Muslim aliiikusanya Hadithi hii kwa kutumia isnadi ya simulizi ya Imamu Malik.⁵ Pia kuna Hadithi sahihi ambapo Mtume ﷺ amesema;

¹ Juz Al-Hassan bin 'Arafah 46 Sanadi yake ina dosari.

² Ahmad 2:90.

³ Abu Dawud 5:20.

⁴ Ahmad 2:110.

⁵ Muslim 4:2045.

«اسْتَعِينِ بِاللَّهِ وَلَا تَعْجِزْ، فَإِنْ أَصَابَكَ أَمْرٌ فَقُلْ: قَدَّرَ اللَّهُ وَمَا شَاءَ فَعَلْ، وَلَا تَقُلْ:
لَوْ أَنِّي فَعَلْتُ كَذَا لَكَانَ كَذَا، فَإِنْ لَوْ تَفْتَحْ عَمَلَ الشَّيْطَانِ»

“Muombe Allah msaada, wala usishindwe. Na ukipatwa na jambo, sema’ Allah Amelikadiria, na Yeye Hufanya Atakavyo.’ Wala usiseme, ‘Lau ningefanya hivi au vile, basi ingelikuwa kadha, kwani ‘lau...ninge...inge...’ hufungua Mlango wa amali ya Shetani”¹

Katika Hadithi ya ‘Abbas رضي الله عنه، Mtume ﷺ alimuambia,

«وَأَعْلَمُ أَنَّ الْأُمَّةَ لَوِ اجْتَمَعُوا عَلَى أَنْ يَنْفَعُوا بَشِيئَةً، لَمْ يَكْتُبْهُ اللَّهُ لَكَ لَمْ يَنْفَعُوا،
وَلَوْ اجْتَمَعُوا عَلَى أَنْ يَضُرُّوكَ بَشِيئَةً، لَمْ يَكْتُبْهُ اللَّهُ عَلَيْكَ لَمْ يَضُرُّوكَ، جَمَعَتْ
الْأَقْلَامُ وَطُوبِيَتِ الصُّحُفُ»

“Na ujue kuwa, lau umati utakusanyika juu ya kukunufaisha kwa jambo ambalo Allah Hakukuandikia hawatakunufaisha, na lau watakusanyika ili wakudhuru kwa jambo ambalo Hajakuandikia hawatakudhuru. Kalamu zimekauka na Vitabu vimefungwa.”²

Imamu Ahmad alimnukuu Ubadah bin Al-Walid bin Ubadah kuwa baba yake alimuambia, “Nilikwenda kwa ‘Ubadah alipokuwa mgonjwa, na nikadhani kuwa alikuwa amekaribia kufariki. Hivyo nikasema, ‘Ewe baba yangu, nipe nasaha na ufanye vyema katika jambo hili.’ Akasema, ‘Nisaidie nikae kitako,’ na baada ya kuketi, alisema, ‘Ewe mwanangu! Tambua kuwa hutaonja furaha ya Imani au kupata elimu ya kweli juu ya Allah تعالى mpaka uamini Al-Qadar, kheri yake na shari yake.’ Nikauliza, ‘Ewe baba yangu! Nitaijuaje kheri yake na shari yake?’ Akajibu, ‘Pindi utakapojua kuwa kila kilichokukosa hakikuwa cha kukupata na kilichokupata hakikuwa cha kukukosa. Ewe mwanangu! Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنَّ أَوَّلَ مَا خَلَقَ اللَّهُ الْقَلَمَ، ثُمَّ قَالَ لَهُ: اكْتُبْ، فَجَرَى فِي تِلْكَ السَّاعَةِ بِمَا هُوَ
كَائِنٌ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Hakika! Cha kwanza Alichokiumba Allah ni kalamu, akaiambia: ‘Andika,’ kwa hiyo nayo ikaandika katika saa hiyo kila chenye kuwa mpaka Siku ya Kiyama.”

¹Muslim 4:2052.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 7:219.

“Ewe mwanangu! kama hutakuwa na imani hii, utaingia Jahanamu.”¹ At-Tirmidhi pia aliinukuu na akasema: “*Hasan Sahih Gharib.*”²

Imethibiti katika Sahih Muslim kutoka kwa ‘Abdullah bin ‘Amr رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ اللَّهَ كَتَبَ مَقَادِيرَ الْخَلْقِ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِخَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ»

“*Hakika Allah Ameandika makadirio ya viumbe kabla Hajaumba mbingu na ardhi kwa miaka elfu khamsini.*”

Ibn Wahb aliongeza,

وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ

“***Na Kiti chake cha Enzi kilikuwa juu ya maji...***” (11:7)³

At-Tirmidhi pia aliinukuu, na akasema: “*Hasan, Sahih Gharib.*”⁴

Onyo la Kujihadhari na Makamio ya Allah تعالى

Allah تعالى amesema,

وَمَا أَمْرًا إِلَّا وَاحِدَةً كَلِمَةً بِلَبْسٍ

“***Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.***”

Haya ni maelezo kuhusu kutekelezwa kwa Utashi Wake kwa viumbe Wake, kama Alivyotueleza Kutekelezwa kwa Hukumu Yake kwao,

وَمَا أَمْرًا إِلَّا وَاحِدَةً

“***Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu.***”

Maana yake: ‘Tunakiamrisha kitu mara moja, pasi na haja ya kurudia amri tena; na kila Tunachokiamuru kinatii kwa haraka kuliko kupepesa jicho bila ya uchelewaji wowote, hata kidogo.’ Allah تعالى Amesema,

¹ Ahmad 5:317.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:368.

³ Muslim 4:2044.

⁴ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 5:370.

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا أَشْيَاعَكُمْ

“Na bila ya shaka Tumekwisha waangamiza wenzenu.”

Maana yake: Umati wa hapo kabla ambao uliwakataa Mitume wao,

فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ

“Lakini yupo anayekumbuka?”

Maana yake: Kuna yeyote atakayepokea maonyo kwa kukumbuka hilaki na adhabu aliyowahukumia Allah تعالى? Kama Allah تعالى Anavyosema,

وَحِيلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ كَمَا فُعِلَ بِأَشْيَاعِهِمْ مِّن قَبْلُ إِنَّهُمْ كَانُوا فِي شَكٍّ مُّرِيبٍ ﴿٥٤﴾

“Na watatiliwa kizuizi baina yao na hayo wanayoyatamani, kama walivyofanyiwa wenzao zamani. Hakika hao walikuwa na shaka ya kutia wasiwasi.” (34:54)

Kauli ya Allah تعالى,

وَكُلُّ شَيْءٍ فَعَلُوهُ فِي الزُّبُرِ ﴿٥٥﴾

“Na kila jambo walilolifanya limo vitabuni.”

Maana yake: Kila walichotenda kimeandikwa katika Vitabu walivyokabidhiwa Malaika,

وَكُلُّ صَغِيرٍ وَكَبِيرٍ

“Na kila kidogo na kikubwa.”

Maana yake: Matendo yao yote.

مُسْتَطَرًّا

“Kimeandikwa.”

Kila kitu walichokifanya na kuhifadhiwa katika daftari la amali zao, ambalo haliachi kitu, kikubwa au kidogo, bali kimo na kuhesabiwa.

Imamu Ahmad alinukuu kuwa mama A'ishah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«يَا عَائِشَةُ إِنَّا لِكُفَّاتِ الذُّنُوبِ، فَإِنَّ لَهَا مِنَ اللَّهِ طَالِيًا»

“Ewe ‘Aishah! Jihadhari na (kufanya) madhambi yanayodharauliwa (madogo madogo) kwani kuna aliyepewa jukumu na Allah la kuyaandika.”¹

An-Nasa’i na Ibn Majah pia aliikusanya Hadithi hii.²

Mwisho Mwema ni wa Wachamungu

Allah تعالى Amesema,

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَنَهْرٍ

“**Hakika wachamngu watakuwa katika bustani na mito.**”

Maana yake: Tofauti na mwisho unaowakabili waovu, pamoja na hasara, kuchanganyikiwa na kuburuzwa Motoni juu ya nyuso zao, kadhalika na kufedheheshwa, kuadhibiwa na kutishwa. Allah تعالى Amesema,

فِي مَقْعَدٍ صِدْقٍ

“**Katika makalio ya haki.**”

Katika Makazi matukufu ya Allah تعالى, yenye kuzungukwa na Radhi, Fadhila, Ukarimu na Rehema Zake.

عِنْدَ مَلِكٍ مُّقْتَدِرٍ

“**Kwa Mfalme Mwenye Uweza.**”

Maana yake: Kwa Mfalme Mkubwa Aliyeumba kila kitu na Kukikadiria kipimo chake; Yeye ni Muweza wa Kuwapa chochote wanachokitamani na kukiomba. Imamu Ahmad alimnukuu ‘Abdullah bin ‘Amr رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْمُضْطُوبُونَ عِنْدَ اللَّهِ عَلَى مَنَابِرٍ مِنْ نُورٍ عَنِ يَمِينِ الرَّحْمَنِ وَكِلْتَا يَدَيْهِ يَمِينٌ، الَّذِينَ يَنْغَدِلُونَ فِي حُكْمِهِمْ وَأَهْلِيهِمْ وَمَا وَلَوْ»

¹ Ahmad 6:151.

² Tuhfat Ashraf 12:250 na Ibn Majah 2:1417.

“Hakika, waadilifu watakuwa kwa Allah juu ya mimbari za nuru kulia kwa Ar-Rahman, na Mikono Yake yote Miwili ni kulia. Wao ni wale wanaofanya uadilifu katika hukumu zao katika familia zao na wale wanaowasimamia.”¹

Muslim na An-Nasa’i pia aliinukuu Hadithi hii.²

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Surah Iqtarabat* (Al-Qamar). Sifa zote Njema pamoja na Shukurani Anastahiki Allah تعالى, na mafanikio na kuwezesha na kuhifadhika dhidi ya makosa ni Kwake.



¹ Ahmad 2:60.

² Muslim 3:1458 na An-Nasai 8:221.

Tafsiri ya Suratu Ar-Rahman

Sura ya 55

Iliteremshwa Makkah

Utangulizi wa Suratu Ar-Rahman

Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Zirr alisema kuwa mtu mmoja alipata kumuambia Ibn Mas'ud رضي الله عنه¹ "Hii husomwa:² *"Maa-in Ghayri Aasin au Asin."* Alimuuliza, "Wewe una ujuzi huo wa usomaji Qur'an?" Akamjibu, "Mimi husoma sehemu ya sura *Mufasswal* katika Rakaa moja." *"Al-Mufasswal"* ni sura fupi za Qur'an ambazo *Bismillah* katika sura hizo hazikuachana sana. Na wanazuoni wametofautiana katika uainishaji wa mwanzo wake, kuna waliosema zinaanza na sura *"Qaf"* na wengine wamesema *"Al-Hujuraat"*

Akasema, "Ole wako! Unasoma Qur'an upesi upesi, kama mashairi. Najua kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisoma Sura mbili kutoka mwanzoni mwa Sehemu ya *Mufasswal* (katika Rakaa moja)." Ibn Mas'ud رضي الله عنه aliichukulia *Surat Ar-Rahman* kuwa ndio mwanzoni mwa Sehemu ya *Mufasswal*.³ Abu 'Isa At-Tirmidhi alinukuu kuwa Jabir رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alikwenda kwa Masahaba wake na akawasomea *Surat Ar-Rahman* kutoka mwanzo mpaka mwisho lakini hawakusema chochote. Mtume ﷺ akasema,

لَقَدْ قَرَأْتُهَا عَلَى الْجِنِّ لَيْلَةَ الْجِنِّ فَكَانُوا أَحْسَنَ مَرْدُودًا مِنْكُمْ، كُنْتُ كُلَّمَا أَتَيْتُ
عَلَى قَوْلِهِ: ﴿يَا أَيُّهَا آيَاتُ رَبِّكَمَا تَكْذِبَانِ﴾ قَالُوا: لَا يَسْبِيءُ مِنْ نِعْمِكَ رَبَّنَا نَكْذِبُ
فَلَكَ الْحَمْدُ

"Niliwasomea Majini, katika usiku wa Majini na jibu lao lilikuwa bora kuliko lenu! Niliposoma Kauli ya Allah: 'Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayoikanusha. 'Wao walijibu, 'Hapana neema yako yoyote tunayoikanusha, ewe Mola wetu Mlezi! Sifa zote Njema pamoja na Shukurani Unastahiki Wewe."

¹ Kama ilivyo katika simulizi ya Imamu Ahmad, simulizi sawa na hiyo ilinukuliwa na Ibn Mas'ud katika Muslim na. 822.

² Hiyo ni *Surat Muhammad* 47:15.

³ Ahmad 1:412.

At-Tirmidhi aliinukuu na akasema, “Hadithi hii ni *Gharib*.”¹ Al-Hafidh Abu bakr Al-Bazzar رحمه الله تعالى pia aliikusanya Hadithi hii.² Abu Ja’far Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa ‘Abdullah bin ‘Umar رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisoma *Surat Ar-Rahman*, au ilisomwa mbele yake, akasema,

«مَا لِي أَسْمَعُ الْجِنَّ أَحْسَنَ جَوَابًا لِرَبِّهَا مِنْكُمْ؟»

“Kwa nini mimi niliwasikia majini wakitoa jibu bora kwa Mola wao Mlezi kuliko nyinyi?”

Wakauliza, “Kwa nini, Ewe Mjumbe wa Allah” Yeye akawajibu,

«مَا أَتَيْتُ عَلَى قَوْلِ اللَّهِ تَعَالَى: ﴿فِي آيَاتِنَا كَذِبًا﴾ إِلَّا قَالَتِ الْجِنَّ: لَا بِشَيْءٍ مِنْ نَعْمِ رَبِّنَا نُكَذِّبُ»

“Niliposoma Kauli ya Allah Mtukufu, **“Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayoikanusha?”** Majini walijibu kwa kusema, ‘Hapana neema Yako yoyote tunayoikanusha.’³

Al-Hafidh Al-Bazzar رحمه الله تعالى pia aliikusanya Hadithi hii.⁴

* * *

¹ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:177.

² Al-Hakim 2:473.

³ At-Tabari 23:23.

⁴ *Kash Al-Astar* 3:74.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu

سُورَةُ الرَّحْمَنِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّحْمَنُ ۝ عَلَّمَ الْقُرْآنَ ۝ خَلَقَ الْإِنْسَانَ ۝
 عَلَّمَهُ الْبَيَانَ ۝ الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ بِحُسْبَانٍ ۝ وَالنَّجْمُ
 وَالشَّجَرُ يَسْجُدَانِ ۝ وَالسَّمَاءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ
 الْمِيزَانَ ۝ أَلَّا تَطْغَوْا فِي الْمِيزَانِ ۝ وَأَقِيمُوا
 الْوِزْنَ بِالْقِسْطِ وَلَا تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ ۝ وَالْأَرْضَ
 وَضَعَهَا لِلْأَنَامِ ۝ فِيهَا فَاكِهَةٌ وَالنَّخْلُ ذَاتُ
 الْأَكْمَامِ ۝ وَالْحَبُّ ذُو الْعَصْفِ وَالرَّيْحَانُ ۝ فَبِأَيِّ
 آيَاتِنَا نُنَكِّدُ بَانَ ۝ خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ صَلْصَلٍ
 كَالْفَخَّارِ ۝ وَخَلَقَ الْجَانَّ مِنْ مَّارِجٍ مِنْ نَارٍ ۝
 فَبِأَيِّ آيَاتِنَا نُنَكِّدُ بَانَ ۝ رَبُّ الشَّرْقَيْنِ وَرَبُّ
 الْمَغْرِبَيْنِ ۝ فَبِأَيِّ آيَاتِنَا نُنَكِّدُ بَانَ ۝ مَرْجَ
 الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيَانِ ۝ بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَا يَبْغِيَانِ ۝
 فَبِأَيِّ آيَاتِنَا نُنَكِّدُ بَانَ ۝ نَخْرُجُ مِنْهَا
 الْوَلُودَ ۝ وَالْمَرْجَاتُ ۝ فَبِأَيِّ آيَاتِنَا نُنَكِّدُ بَانَ ۝ وَهَ
 الْجَوَارِ الْمُشَفَّاتُ فِي الْبَحْرِ كَالْأَعْلَامِ ۝ فَبِأَيِّ آيَاتِنَا
 نُنَكِّدُ بَانَ ۝

الرَّحْمَنُ ۝ عَلَّمَ الْقُرْآنَ ۝
 خَلَقَ الْإِنْسَانَ ۝ عَلَّمَهُ الْبَيَانَ ۝
 الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ بِحُسْبَانٍ ۝
 وَالنَّجْمُ وَالشَّجَرُ يَسْجُدَانِ ۝
 وَالسَّمَاءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ
 الْمِيزَانَ ۝ أَلَّا تَطْغَوْا فِي الْمِيزَانِ ۝
 وَأَقِيمُوا الْوِزْنَ بِالْقِسْطِ وَلَا
 تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ ۝ وَالْأَرْضَ
 وَضَعَهَا لِلْأَنَامِ ۝ فِيهَا فَاكِهَةٌ
 وَالنَّخْلُ ذَاتُ الْأَكْمَامِ ۝ وَالْحَبُّ
 ذُو الْعَصْفِ وَالرَّيْحَانُ ۝ فَبِأَيِّ
 آيَاتِنَا نُنَكِّدُ بَانَ ۝

1. Arrah'man, Mwingi wa Rehema.

2. Amefundisha Qur'ani.

3. Amemuumba mwana-adamu.

4. Akamfundisha kusema.

5. Jua na mwezi huenda kwa hisabu.

6. *Na nyota na miti, inanyenyekea.*
7. *Na mbingu Ameziinua, na Ameweka uadilifu,*
8. *Ili msidhulumu katika kipimo.*
9. *Basi pimeni bidhaa kwa haki, wala msipunje katika mizani.*
10. *Na ardhi ameiweka kwa ajili ya viumbe.*
11. *Humo yamo matunda na mitende yenye mafumba.*
12. *Na nafaka zenye makapi, na mimea yenye harufu nzuri.*
13. *Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayoikanusha*

Ar-Rahman Ameteremsha Qur'an na Kuifundisha

Allah تعالی Anaeleza Fadhila na Rehema Zake kwa viumbe Wake, kutokana na Kuwateremshia Qur'an waja Wake, Alifanya jambo la kuhifadhi na kuelewa kuwa rahisi kwa Aliowaneemesha, Allah تعالی Akasema;

الرَّحْمَنُ ۝ عَلَّمَ الْقُرْآنَ ۝ خَلَقَ الْإِنْسَانَ ۝ عَلَّمَهُ الْبَيَانَ ۝

***“Arrah’man, Mwingi wa Rehema, Amefundisha Qur’ani.
Amemuumba mwanaadamu, Akamfundisha kusema.”***

Al-Hasan alisema: “Ni umbuji katika mazungumzo.” Inamaanisha kuwa Allah تعالی Anafundisha Qur’an, yaani, kuwafundisha waja namna ya kuisoma na kuwarahisishia kutamka na kutaja herufi kutoka sehemu mbalimbali za mdomo, koo, ulimi na midomo.

Miongoni mwa Dalili za Allah تعالی, Jua, Mwezi, Mbingu na Ardhi

Allah تعالی Amesema,

الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ بِحُسْبَانٍ ۝

“Jua na mwezi huenda kwa hisabu.” Huenda katika njia zao kwa mfuatano kamili, kwa kufuata mahesabu yaliyoratibiwa. Maana yake: Kamwe hakuna kuchelewa wala kuwahi.

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي هَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٥٥﴾

“Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao.” (36:40),

Na Allah تعالى Amesema;

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٦٦﴾

“Ndiye Anayepambazua mwangaza wa asubuhi; na Ameufanya usiku kwa mapumziko na utulivu, na jua na mwezi kwenda kwa hisabu. Hayo ndiyo makadirio ya Aliyetukuka Mwenye Nguvu, Mwenye Ujuzi.” (6:96),

Allah تعالى Amesema,

وَالنَّجْمِ وَالشَّجَرِ يَسْجُدَانِ ﴿٥٦﴾

“Na nyota, na miti, inanyenyekea.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema, “Wanazuoni wa Tafsiri wana rai tofauti juu ya maana ya Kauli ya Allah تعالى, ‘Wan-Najm.’ Hata hivyo, wamekubaliana kuwa miti iliyotajwa hapa ni ile yenye mashina (vigogo).”¹

Ali bin Abu Talhah alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “An-Najm ina maana ya mimea ambayo huota ardhini.”²

Rai kama hiyo ilisemwa na Sa’id bin Jubayr, As-Suddi na Sufyan Ath-Thawri.³ Hii ndiyo rai aliyoikhitari Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Mujahid alisema, “An-Najm (nyota); moja, yaani anga.”⁴ Al-Hasan na Qatadah walisema sawa na hayo.⁵ Hii ni sawa na kusema kuwa inamaanisha kuwa ni dhahiri, na Allah تعالى Anajua zaidi, kwani Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 23:11.

² At-Tabari 23:11.

³ At-Tabari 23:11.

⁴ At-Tabari 23:12.

⁵ At-Tabari 23:12.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ
وَالنُّجُومُ وَالْجِبَالُ وَالشَّجَرُ وَالْدَّوَابُّ وَكَثِيرٌ مِنَ النَّاسِ ۗ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ ۗ وَمَنْ
يُنِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُكْرِمٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ۝

“Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu Hutenda Atakavyo.” (22:18)

Kauli ya Allah تعالى،

وَالسَّمَاءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ الْمِيزَانَ ۝

“Na mbingu Ameziinua, na Ameweka mizani.”

Maana yake: Uadilifu. Sawa na Alivyosema katika Aya nyingine,

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ ۝

“Kwa hakika Tuliwatuma Mitume Wetu kwa dalili waziwazi, na Tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu...” (57:25)

Allah تعالى Amesema katika Aya hii,

أَلَّا تَطْغَوْا فِي الْمِيزَانِ ۝

“Ili msidhulumu katika kupima mizani.”

Maana yake: Ameumba mbingu na ardhi kwa uadilifu na ukweli, uliojengwa kwa kila kitu, na kuchunga, uadilifu na ukweli. Kauli ya Allah تعالى،

وَأَقِيمُوا الْوَزْنَ بِالْقِسْطِ وَلَا تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ ۝

“Na wekeni mizani kwa haki, wala msipunje katika mizani.”

Maana yake: Msilaghai katika uzito na vipimo, bali chungeni uadilifu na usawa.

وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ﴿١٨٦﴾

“Na pimeni kwa haki iliyonyooka.” (26:182)

Allah تعالى Amesema,

وَالْأَرْضَ وَضَعَهَا لِلْأَنَامِ ﴿١٨٧﴾

“Na ardhi Ameiweka kwa ajili ya viumbe.”

Allah تعالى Aliinyanyua mbingu na Akaiweka ardhi chini na Kuisawazisha kwa milima madhubuti, ili iwe imara kwa ajili ya wanaoishi juu ya ardhi hiyo. Yaani, namna na jinsi mbalimbali za viumbe, katika umbo, rangi na lugha zao.

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Mujahid, Qatadah na Ibn Zayd walisema kuwa *Al-An’am* maana yake viumbe.¹

فِيهَا فَكَّهَةٌ ﴿١٨٨﴾

“Humo yamo matunda.”

Ya rangi, ladha na harufu mbalimbali.

وَالنَّخْلُ ذَاتُ الْأَكْمَامِ ﴿١٨٩﴾

“Matunda na mitende yenye mafumba.”

Allah تعالى Ameutaja mtende peke yake kutokana na utukufu na manufaa yake ukiwa mbichi au mkavu.

Ibn Jurayj alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa *Al-Akmam*, inamaanisha vikonyo vya matunda.²

Rai sawa na hiyo ilisemwa na wanazuoni wa Tafsiri zaidi ya mmoja. Inamaanisha vikonyo ambavyo mbegu huota na kuwa mkungu wa tende mbivu ambazo baadae huiva.

Allah تعالى Amesema,

وَالْحَبُّ ذُو الْعَصْفِ وَالرَّحْمَانُ ﴿١٩٠﴾

“Na nafaka zenye makapi, na rehani.”

¹ At-Tabari 23:15-16.

² *Ad-Dur Al-Manthur* 7:693.

‘Ali bin Abu Talhah alisema kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَالْحُبُّ ذُو الْعَصْفِ

“Na nafaka zenye makapi.”

‘Maana ya *Asf* ni majani makavu.’¹ Al-‘Awfi alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, “*Asf* ni majani ya kijani yaliyokatwa kutoka katika kikonyo, huitwa ‘*Asf* pindi yanapokauka.’”² Kadhalika, Qatadah, Adh-Dhahhak na Abu Malik walisema kuwa ‘*Asf* maana yake majani makavu.

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na wengine walisema kuwa *Rayhan* maana yake majani,³ ilhali Al-Hasan alisema inamaanisha mimea yenu hii yenye kunukia vizuri.⁴ ‘Ali bin Abu Talhah alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa *Rayhan* maana yake majani ya kijani (mabichi).⁵

Hapa inamaanisha, na Allah تعالى Anajua zaidi, kuna namna kadha wa kadha za mazao yenye kutoa majani makavu, kama vile ngano, shayiri, na *Rayhan* ni majani yanayotoka katika vikonyo.

Mwanaadamu Amezungukwa na Neema za Allah تعالى

Allah تعالى Amesema,

فَبِأَيِّ آءِ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٠﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha.”

Maana yake: “Enyi wanaadamu na majini, ni fadhila na neema ipi ya Allah تعالى Aliyokupeni nyinyi mnayoikanusha?’ Mujahid na wengine walisema vivyo hivyo, na ziko dhahiri pindi mtu atakaposoma Aya zinazofuata, yaani neema zilizo dhahiri kwenu ambazo hamuwezi kuzikanusha wala kuzipinga. Kwa hiyo, tunasema, kama ambavyo Waumini miongoni mwa majini walivyosema, “Ya Allah! Hatukanushi yoyote katika neema Zako. Sifa zote njema pamoja na

¹ At-Tabari 23:18. Isnadi yake ni dhaifu.

² At-Tabari 23:18.

³ At-Tabari 23:19.

⁴ Al-Baghawi 4:268.

⁵ At-Tabari 23:21.

shukurani zinakustahiki Wewe.” Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alikuwa akisema, “Hapana, ewe Mola Wetu Mlezi!” Yaani, “Hatukanushi neema Yako yoyote.”¹

خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ صَلْصَلٍ كَالْفَخَّارِ ﴿١٤﴾ وَخَلَقَ الْجَانَّ مِنْ مَّارِجٍ مِنْ نَارٍ ﴿١٥﴾ فَبِأَيِّ
 ءَالَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿١٦﴾ رَبُّ الْمَشْرِقَيْنِ وَرَبُّ الْمَغْرِبَيْنِ ﴿١٧﴾ فَبِأَيِّ ءَالَاءِ رَبِّكُمَا
 تُكَذِّبَانِ ﴿١٨﴾ مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيَانِ ﴿١٩﴾ بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَا يَبْغِيَانِ ﴿٢٠﴾ فَبِأَيِّ ءَالَاءِ
 رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢١﴾ نَخْرُجُ مِنْهَا اللُّؤْلُؤَ وَالْمَرْجَانَ ﴿٢٢﴾ فَبِأَيِّ ءَالَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ
 ﴿٢٣﴾ وَلَهُ الْجَوَارِ الْمُنشَآتُ فِي الْبَحْرِ كَالْأَعْلَمِ ﴿٢٤﴾ فَبِأَيِّ ءَالَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢٥﴾

14. Amemuumba mtu kwa udongo wa kinamo (mfinyanzi) kama vyombo vya udongo.

15. Na Akawaumba majini kwa ulimi wa moto.

16. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

17. Mola Mlezi wa mashariki mbili na wa magharibi mbili.

18. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

19. Anaziendesha bahari mbili zikutane.

20. Baina yao kipo kizuizi, zisiingiliane.

21. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

22. Katika bahari hizo mbili zinatoka lulu na marijani.

23. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

24. Na ni Vyake Yeye hivi viendavyo baharini vilivyoundwa kama vile milima.

25. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

¹ At-Tabari 23:23.

Ubainifu wa Kuumbwa kwa Wanaadamu na Majini

Allah تعالی Anataja kuwa Amemuumba mwanaadamu kutokana na udongo wa mfinyanzi, kama unaotumika katika kufinyanga vyungu, na Ameumba majini kutokana na ncha ya mwale wa moto usio na moshi.

Haya yalisemwa na Adh-Dhahhak kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما.¹ Pia yalisemwa na ‘Ikrimah, Mujahid, Al-Hasan na Ibn Zayd.²

Al-‘Awfi alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, “Kutokana na sehemu bora kabisa kwenye moto, kutokana na mwale usio na moshi.”³

Imamu Ahmad alimnukuu Mama A’ishah رضي الله عنها kuwa Mtume ﷺ amesema,

«خُلِقَتِ الْمَلَائِكَةُ مِنْ نُورٍ، وَخُلِقَ الْجَانُّ مِنْ مَارِجٍ مِنْ نَارٍ، وَخُلِقَ آدَمُ مِنْ مِمَّا وُصِفَ
لَكُمْ»

*“Malaika wameumbwa kutokana na nuru, Majini kutokana na mwale wa moto usio na moshi, na ‘Adam kutokana na mlichoelezwa.”*⁴

Muslim pia aliikusanya Hadithi hii.⁵

Kauli ya Allah تعالی:

فَبِأَيِّ آءَاءِ رَبِّكُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٥٥﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha.”

Maelezo yake yameshatangulia.

¹ At-Tabari 23:26.

² At-Tabari 23:27. Isnadi yake ni dhaifu, Adh-Dhahaak hakumsimulia kutoka kwa Ibn Abbasi.

³ At-Tabari 23:26.

⁴ Ahmad 6:168.

⁵ Muslim 4:2294.

Allah تعالیٰ ni Mola Mlezi wa Mashariki Mbili na Magharibi Mbili

Allah تعالیٰ Amesema,

رَبُّ الْمَشْرِقَيْنِ وَرَبُّ الْمَغْرِبَيْنِ ﴿٥٥﴾

“Mola Mlezi wa mashariki mbili na wa magharibi mbili.”

Inamaanisha mawio ya majira ya kiangazi na kusi na machweo ya majira ya kiangazi na kusi.

Allah تعالیٰ Amesema katika Aya nyingine,

فَلَا أُقْسِمُ بِرَبِّ الْمَشَارِقِ وَالْمَغْرِبِ إِنَّا لَعَنِدُونَ ﴿٥٦﴾

“Basi Naapa kwa Mola Mlezi wa mashariki zote na magharibi zote kwamba Sisi Tunaweza.” (70:40),

Ikirejea sehemu tofauti tofauti ambapo jua huchomoza na kisha kuzama kila siku.

Allah تعالیٰ Amesema katika Aya nyingine,

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٥٧﴾

“Mola Mlezi wa mashariki na magharibi, hapana mungu isipokuwa Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa wako.” (73:9),

Ikikusudiwa mahali tofauti pa mawio na machweo ya Jua na manufaa ya mabadiliko hayo kwa viumbe, wanaadamu na majini.

Allah تعالیٰ Amesema;

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٨﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayoikanusha.”

Allah تعالی Ameumba Aina Mbalimbali za Maji

Allah تعالی Amesema,

مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيَانِ ﴿٥٥﴾

“Anaziendesha bahari mbili zikutane.”

Kuziachilia huru, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما¹. Kauli ya Allah تعالی,

يَلْتَقِيَانِ

“Zikutane.”

Ibn Zayd alisema, “Anazizuia zisikutane kwa kutumia kizuizi cha kuzitenganisha Alichokiweka katikati yake kwa ajili ya Kutenganisha baina ya maji yasiyo na chumvi na yenye chumvi.”² Huku yasiyo na chumvi yakitokea kwenye mito inayotembea. Tulishaeleza jambo hili katika *Suratu Al-Furqan* wakati wa kuitafsiri Kauli ya Allah تعالی;

وَهُوَ الَّذِي مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ هَذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ وَجَعَلَ بَيْنَهُمَا بَرْزَخًا
وَحِجْرًا مَحْجُورًا ﴿٥٥﴾

“Naye Ndiye Aliyepileka bahari mbili, hii tamu mno, na hii ya chumvi chungu. Na Akaweka baina yao kinga na kizuizi kizuiacho.”
(25:53)

Allah تعالی Amesema,

بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَّا يَبْغِيَانِ ﴿٥٦﴾

“Baina yao kipo kizuizi, zisiingiliane.”

Maana yake: Ameweka kizuizi kati kati ya aina hizi mbili za maji, ili yasiingiliane ama sivyo, zinaweza kubadilisha sifa zilizoumbwa nazo.

¹ Ahmad 6:168.

² Muslim 4:2294.

سَخَّرَ مِنْهَا أَلْوَانًا وَمَرْجَانًا

“Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani.”

Lulu ni maarufu. Kuhusu marijani, wanasema inamaanisha lulu ndogondogo. Mujahid, Qatadah, Abu Ruzayn, Adh-Dhahaak waliyasema hayo, na pia ilisimuliwa kutoka kwa ‘Ali رضي الله عنه¹. Pia ilisemekana kuwa inamaanisha lulu kubwa na nzuri, haya yalitajwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa baadhi ya Salaf.² Ibn Abu Hatim alinukuu kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Pindi mvua inaponyesha, Chaza wa bahari hufungua vinywa vyao, matone yanayodondokea ndani yake hugeuka na kuwa lulu.”³ Isnadi ya simulizi ni Sahih. Kwa kuwa namna hii ya mapambo ni neema kutoka kwa Allah تعالى kwenda kwa watu wa ardhini, Allah تعالى Anawakumbusha kuihusu,

فَبِأَيِّ آيَاتٍ نُّكَذِّبُكَ

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?”

Allah تعالى Amesema,

وَلَهُ الْجَوَارِ الْمُنشَآتُ

“Na ni Vyake Yeye hivi viendavyo.”

Maana yake: Meli zinazoelea,

فِي الْبَحْرِ

“Baharini.”

Mujahid alisema, “Meli yoyote inayotweka tanga, ni katika *Munsha’at*, na ikiwa haitweki tanga, si katika *Munsha’at*.⁴

Qatadah alisema, “*Al-Munsha’at* maana yake vimeumbwa.” Wengine walisema, ni *Al-Munshi’at* maana yake, “kuzinduliwa.”

¹ At-Tabari 23:33 na Al-Qurtubi 17:163.

² At-Tabari 23:34.

³ At-Tabari 23:35.

⁴ At-Tabari 23:37.

كَالَّذِينَ

“Kama vilima.”

Maana yake: Ni kama milima kwa ukubwa wake, pia ina maana ya biashara na huduma za kibiashara zinazoziwesha, kwa kusafirisha kutoka eneo moja kwenda jingine na kutoka jimbo moja hadi jingine. Meli huwapa watu manufaa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kusafirisha aina mbalimbali za bidhaa wanazozihitaji. Kwa hivyo, Allah تعالى Amesema:

فَأَيُّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٥﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayo ikanusha?”

* * *

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهَ رَبِّكَ ذُو الْجَلَلِ
 وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢٨﴾ يَسْأَلُهُ
 مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلَّ يَوْمٍ هُوَ فِي شَأْنٍ ﴿٢٩﴾
 فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٠﴾ سَنَفَعُ لَكُمْ أَيُّهُ
 الثَّقَلَانِ ﴿٣١﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٢﴾ يَمَعْتُرُ
 آلِينَ وَالْإِنْسِ إِنْ أَسْتَطَعْتُمْ أَنْ تَتَفَدُّوا مِنْ أَقْطَارِ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ فَانْفُدُوا لَا تَتَفَدُّوْنَ إِلَّا بِسُلْطَنِ
 ﴿٣٣﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٤﴾ يُرْسَلُ عَلَيْكُمَا
 شُوَاظٌ مِّن نَّارٍ وَنُحَاسٌ فَلَا تَنْتَصِرَانِ ﴿٣٥﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ
 رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٦﴾ فَلِذَا أَنْشَقَّتِ السَّمَاءُ فَكَانَتْ وَرْدَةً
 كَالِدِهَانِ ﴿٣٧﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٨﴾
 فَيَوْمَئِذٍ لَا يُسْأَلُ عَنْ ذَنْبِهِ إِنْسٌ وَلَا جَانٌّ ﴿٣٩﴾ فَبِأَيِّ
 آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٤٠﴾ يُعْرِفُ الْمُجْرِمُونَ بِسِيْمَتِهِمْ
 فَيُؤْخَذُ بِالنُّوَصِيِّ وَالْأَقْدَامِ ﴿٤١﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا
 تُكَذِّبَانِ ﴿٤٢﴾ هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي يُكَذِّبُ بِهَا الْمُجْرِمُونَ
 ﴿٤٣﴾ يَطُوفُونَ فِيهَا وَبَيْنَ حَمِيمٍ ءَانٍ ﴿٤٤﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ
 رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٤٥﴾

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهَ
 رَبِّكَ ذُو الْجَلَلِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾
 فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢٨﴾
 يَسْأَلُهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
 كُلَّ يَوْمٍ هُوَ فِي شَأْنٍ ﴿٢٩﴾ فَبِأَيِّ
 آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٠﴾

26. Kila kilichoko juu yake kitatoweka.

27. Na Atabakia Mwenyewe Mola Wako Mlezi Mwenye Utukufu na Ukarimu.

28. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

29. Vinamuomba Yeye vilivyomo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye yumo katika mambo.

30. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

Allah تعالى ni Mwenye Uhai wa Milele, Mkwasi Asiyehitajia Chohote

Allah تعالى Anaeleza kuwa wakazi wote wa dunia wataisha na kufa, walio mbinguni watakufa, isipokuwa Anayemtaka Allah تعالى. Dhati ya Allah تعالى Peke Yake ndiyo itakayobakia, kwa sababu Mola Wetu Mlezi, Mtukufu, ni wa Milele, na Hafi. Qatadah alisema, “Kwanza, Allah تعالى Amewataja viumbe Wake na Akasema watakufa.” Na katika dua iiyopokewa: ‘Ewe wa Milele

Unayewaruzuku viumbe wote! Ewe Uliyeumba mbingu na ardhi bila ya aliyekutangulia. Ewe Mwenye Utukufu na Heshima, hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Wewe. Tunajikinga katika Rehema Zako. Tujaalie mafanikio katika mambo yetu. Usituache tujitegemee sisi wenyewe hata kama kwa jambo la papo kwa papo na wala kumtegemea yeyote katika viumbe Wako.” Ash-Sha’b alisema, “Pale unaposema,

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾

“Kila kilioko juu yake kitatoweka.” Usisimame, endelea kusoma,

وَيَبْقَىٰ وَجْهَ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾

“Na Atabakia Mwenyewe Mola Wako Mlezi Mwenye Utukufu na Ukairimu.”¹

Aya hii inalingana na Kauli ya Allah تعالى،

كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ ﴿٢٨﴾

“...Kila kitu kitaangamia isipokuwa Yeye...” (28:88)

Katika Aya hii, Allah تعالى Anaisifu Dhati Yake Tukufu kuwa ni *Dhul-Jalal wal-Ikram*, inajulisha kuwa Yeye Ndiye Anayestahiki kunyenyekewa, na kwa hivyo, kamwe Asidharauliwe; na Atiwe na hakuna kumuasi. Kama ilivyo katika Kauli Yake Allah تعالى

وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدْوَةِ وَالْعِشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ ﴿٢٩﴾

“Na isubirisha nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola Wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka Radhi Yake.” (18:28),

Ni sawa na Alivyosema katika Aya nyingine kuhusu wenye kutoa sadaka:

إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ ﴿٧٠﴾

“Hakika Sisi Tunakulisheni kwa ajili ya kutafuta Radhi za Allah.” (76:9)

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alitoa rai juu ya maana ya *Dhul-Jalal wal-Ikram*, kwa kusema, “Mwenye Ukuu na Fakhari.”² Baada ya kueleza kuwa wakazi wa

¹Ad-Dur Al-Manthur 7:698.

²At-Tabari 23:86.

ardhini watakufa na kwenda akhera, ilhali Yeye, *Dhul-Jalal wal-Ikram*, Atawahukumu kwa uadilifu. Allah تعالى Akasema,

فَبِأَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٥﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?”

Allah تعالى Amesema,

يَسْأَلُهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلَّ يَوْمٍ هُوَ فِي شَأْنٍ ﴿٥٦﴾

“Vinamuomba Yeye vilivyomo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye Yumo katika mambo.”

Katika Aya hii, Allah تعالى Anathibitisha kuwa Yeye ni Mkwasi, Hana haja na chochote bali viumbe ndio wenye kumhitajia, katika hali na namna zote. Wao wote wanahitaji msaada Wake kwa hiyari na kwa nguvu. Kila siku, Yeye Yuko katika mambo. Al-A'mash alisimulia kutoka kwa Mujahid, kuwa 'Ubayd bin 'Umayr alisema,

كُلَّ يَوْمٍ هُوَ فِي شَأْنٍ

“Kila siku Yeye Yumo katika mambo.”

Akasema, “Kati ya mambo Yake ni kuwa Yeye Hujibu dua, au Kumpa mwenye haja Kwake, au Kumuondolea dhiki, au Kumponya mgonjwa.”¹

سَنَفْرُغُ لَكُمْ أَيُّهَ الثَّقَلَانِ ﴿٥٧﴾ فَبِأَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٨﴾ يَمَعَشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ
 إِنَّ أَسْتَطَعْتُمْ أَنْ تَفْعَلُوا مِنْ أَقْطَارِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ فَانْفَعُوا ۚ لَا تَفْعَلُونَ إِلَّا
 بِسُلْطَنِ ﴿٥٩﴾ فَبِأَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٠﴾ يُرْسَلُ عَلَيْكُمَا شُوَاظٌ مِّنْ نَّارٍ وَنُحَاسٌ
 فَلَا تَنْتَصِرَانِ ﴿٦١﴾ فَبِأَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٢﴾

31. Tutakuhisabuni enyi makundi mawili.

32. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

33. Enyi makundi ya majini na watu! Mkiweza kupenya kwenye mbingu na ardhi, basi penyeni! Hamtapenya ila kwa Nguvu (Zangu).

¹ At-Tabari 23:39.

34. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

35. Mtapelekewa muwako wa moto na shaba; wala hamtopata wa kuwanusuru (wala kuwaokoa).

36. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

Onyo kwa Wanaadamu na Majini na Ubainifu wa Vitisho Vitakavyowasibu

Ibn Jurayj alisema kuwa Aya,

سَنَفِّرُكُمْ لَكُمْ

“Tutakushughulikieni.” Maana yake: ‘Tutakuhukumuni,’ wakati Imamu Al-Bukhari alisema, inamaanisha, “Tutakupeni jaza yenu. Hakika, hakuna jambo litakalomshughulisha Allah تعالی dhidi ya kufanya jambo jingine.”¹ Namna hii ya mazungumzo ni kawaida katika lugha ya Kiarabu. Kwa mfano, mtu anaweza kusema, “Nitakushughulikia,” hata wakati akiwa hashughulishwi na kitu kingine chochote. Kauli nyingine ya Allah تعالی;

أَيُّهُ التَّقْلَانِ

“Enyi makundi mawili.”

Ina maana ya wanaadamu na majini, kama katika Hadithi;

«يَسْمَعُهَا كُلُّ شَيْءٍ إِلَّا التَّقْلَيْنِ»

“Kila kitu kitasikia, isipokuwa Thaqalayn.”²

Katika simulizi nyingine inayoeleza jambo hilo, Mtume ﷺ alisema,

«إِلَّا الْإِنْسَ وَالْجِنَّ»

“...isipokuwa wanaadamu na majini.”

Allah تعالی Amesema,

فَبِأَيِّ آءِآلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٥﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?”

¹ Fat’h Al-Bari 8:487.

² Fat’h Al-Bari 3:244. (Hii ni namba 1338 ya Al-Bukhari, kuhusu kafiri na mnafiki kupigwa na malaika baada ya kuingizwa kaburini).

Kisha, Allah تعالى Akasema;

يَمَعَشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ إِنَّ أَسْتَطَعْتُمْ أَنْ تَنْفُدُوا مِنْ أَقْطَارِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ فَانْفُدُوا
لَا تَنْفُدُونَ إِلَّا بِسُلْطَانٍ ﴿٣٧﴾

“Enyi makundi ya majini na watu! Mkiweza kupenya kwenye mbingu na ardhi, basi penyeni! Hamtapenya ila kwa kupewa madaraka (nguvu).”

Maana yake: “Kamwe hamtamudu kutoroka Amri na Hukumu za Allah تعالى, kwa sababu Amekuzungukeni. Hamtaweza kukwepa au kuzuia kanuni na hukumu Yake juu yenu, nyinyi mmezingirwa nayo popote mlipo.’ Pia inazungumzia mkusanyiko pale Malaika, watakaokuwa katika mistari saba katika kila upande, watakapotuzingira. Hakuna kiumbe yeyote atakayeweza kutoroka siku hiyo.

إِلَّا بِسُلْطَانٍ

“ila kwa kupewa madaraka.”¹

Maana yake: Isipokuwa kwa Amri ya Allah تعالى,

يَقُولُ الْإِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ أَيْنَ الْمَفْرُوجُ ﴿٧٥﴾ كَلَّا لَا وَزَرَ ﴿٧٦﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمُسْتَقَرُّ ﴿٧٧﴾

“Siku hiyo mtu atasema: Yako wapi makimbilio? La! Hapana pa kukimbilia! Siku hiyo pa kutua ni kwa Mola Wako Mlezi tu.” (75:10-12),

Na Allah تعالى Amesema;

وَالَّذِينَ كَسَبُوا السَّيِّئَاتِ جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا وَتَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ مَّا هُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ عَاصِمٍ طَّ كَانَمَا
أَغْشَيْتَ وُجُوهُهُمْ فِطْعًا مِّنَ اللَّيْلِ مُظْلِمًا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٧﴾

“Na wale waliochuma maovu, malipo ya uovu ni mfano wake vile vile, na yatawafika madhila. Hawatakuwa na wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu. Nyuso zao kama kwamba zimefunikwa na vipande vya usiku wa giza. Hao ndio watu wa Motoni, wao humo watadumu.” (10:27)

¹ Neno la Kiarabu, *Sultan* linamaanisha madaraka au mamlaka.

Kauli ya Allah تعالى،

يُرْسَلُ عَلَيْكُمَا شُوَاظٌ مِّن نَّارٍ وَنُحَاسٌ فَلَا تَنْتَصِرَانِ ﴿٢٦﴾

“Mtapelekewa muwako wa moto na shaba; wala hamtashinda.”

‘Ali bin Abu Talhah alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: *Shuwadh* ni mwale wa moto.¹ Abu Swalih alisema, “Ni mwale ambao haujafikia kiwango cha moto ni zaidi ya moshi.” Adh-Dhahhak alisema,

شُوَاظٌ مِّن نَّارٍ

“Muwako wa moto.” “Mafuriko ya moto.” Allah تعالى Amesema;

وَنُحَاسٌ

“Na shaba” ‘Ali bin Abu Talhah alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, “Ni moshi wa moto.”² Simulizi sawa na hiyo ilisimuliwa na Abu Swalih, Sa’id bin Jubayr na Abu Sinan.³

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa Waarabu walikuwa wakiuita moshi wa moto, *Nuhas* na *Nihas*. Lakini akasema kuwa wanazuoni wa usomaji Qur’an walisema kuwa katika Aya hii, neno linalosomwa ni *Nuhas*.⁴

Mujahid alisema, “Shaba iliyoyeyuka ikamwagwa juu ya vichwa vyao.”⁵ Qatadah alitoa rai sawa na hiyo.⁶ Adh-Dhahhak alisema, “*Nuhas* shaba iliyo majimaji.” Aya inamaanisha, ‘Ikiwa nyinyi, wanaadamu na majini, mtajaribu kutoroka katika Siku ya Kiyama, kisha Malaika, wakiwemo wale ambao miongoni mwao ni walinzi wa Jahanamu, watakurudisheni kwa kukuelekezeeni moshi wa moto na shaba iliyo majimaji juu yenu.’ Kauli ya Allah تعالى،

فَلَا تَنْتَصِرَانِ ﴿٢٦﴾ فَيَأْتِيءَ الْآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢٧﴾

“Wala hamtashinda. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayo ikanusha.”

¹ At-Tabari 23:45.

² At-Tabari 23:47.

³ At-Tabari 23:47.

⁴ At-Tabari 23:48.

⁵ At-Tabari 23:48.

⁶ At-Tabari 23:48.

فَإِذَا أَنْشَقَّتِ السَّمَاءُ فَكَانَتْ وَرْدَةً كَالدِّهَانِ ﴿٢٧﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢٨﴾
 فَيَوْمَئِذٍ لَا يُسْأَلُ عَنْ ذَنْبِهِ إِنْسٌ وَلَا جَانٌّ ﴿٢٩﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٠﴾
 يُعْرِفُ الْمُجْرِمُونَ بِسِيمَاهُمْ فَيُؤْخَذُ بِالنَّوَصِي وَالْأَقْدَامِ ﴿٣١﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٢﴾
 هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي يُكَذِّبُ بِهَا الْمُجْرِمُونَ ﴿٣٣﴾ يَطُوفُونَ فِيهَا بَيْنَ حَمِيمٍ ءَانِ ﴿٣٤﴾
 فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٥﴾

37. Itakapopasuka mbingu ikawa nyekundu kama rangi ya ngozi nyekundu ya wekundu wa mafuta ya zaituni.

38. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

39. Siku hiyo hataulizwa dhambi zake mtu wala jini.

40. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

41. Watajulikana waovu kwa alama zao, basi watashikwa kwa nywele zao za utosini na kwa miguu.

42. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

43. Hii ndiyo Jahannamu ambayo wakosefu wakiikanusha.

44. Watakuwa wakizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayochemka sana.

45. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

Vitisho vya Kiyama

Allah تعالى Amesema,

فَإِذَا أَنْشَقَّتِ السَّمَاءُ

“Itakapopasuka mbingu...” Katika Siku ya Kiyama. Maana ya Aya hii iko wazi, na inalingana na Aya nyingine kama vile,

وَأَنْشَقَّتِ السَّمَاءُ فَهِيَ يَوْمَئِذٍ وَاهِيَةٌ ﴿١٦﴾

“Na mbingu zitapasuka, kwani siku hiyo zitakuwa dhaifu kabisa.”
 (69:16),

وَيَوْمَ تَشْقَى السَّمَاءُ بِالْغَمِّمِ وَتُزَلَّ الْمَلَائِكَةُ تَزِيلًا ﴿٢٥﴾

“Na siku zitapopasuka mbingu kwa mawingu, na wateremshwe Malaika kwa wingi.” (25:25)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

إِذَا السَّمَاءُ أَنْشَقَّتْ ﴿١﴾ وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ﴿٢﴾

“Itapochanika mbingu, na ikamsikiliza Mola Wake Mlezi, na ikapasiwa kumsikiliza.” (84:1-2)

Kauli ya Allah تعالى،

فَكَانَتْ وَرْدَةً كَالدِّهَانِ

“ikawa nyekundu kama rangi ya ngozi nyekundu ya wekundu wa mafuta ya zaituni.”

Maana yake: Itayeyuka kama mashapo na fedha zinavyoyeyuka baada ya kutiwa joto, na zitatiwa rangi kama rangi inavyotiwa katika kitu, nyekundu, manjano, bluu, au kijani. Hii inaonesha ukubwa wa vitisho vya Siku ya Kiyama. As-Suddi alisema: “Itakuwa kama ilivyo rangi na kama mafuta machafu.” Mujahid alisema:

كَالدِّهَانِ ﴿١٥﴾

“kama rangi ya ngozi nyekundu ya wekundu wa mafuta ya zaituni.”

“Kama rangi ya mafuta.”¹ Allah تعالى Amesema;

فَيَوْمَئِذٍ لَا يُسْأَلُ عَنْ ذَنْبِهِ إِنْسٌ وَلَا جَانٌّ ﴿١٦﴾

“Siku hiyo hataulizwa dhambi zake mtu wala jini.”

Hii inalingana na kauli Yake nyingine;

هَذَا يَوْمٌ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٣٥﴾ وَلَا يُؤْدِنُ هُمْ فَيَعْتَذِرُونَ ﴿٣٦﴾

“Hii ni siku ambayo hawatatamka kitu, wala hawataruhusiwa kutoa udhuru.” (77:35-36)

Hali ndiyo hii katika wakati huo, kisha viumbe wote wataulizwa kuhusu amali zao. Allah تعالى Amesema;

¹ At-Tabari 23:50.

﴿٢٦﴾ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾ فَوَرَبِّكَ لَنَسْأَلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ

“Hivyo basi, Naapa kwa Mola Wako Mlezi (ewe Muhammad)! Kwa hakika, Tutawasaili wao wote. Kuhusu yote waliyokuwa wakiyatenda.” (15:92-93)

Qatadah alisema, “Wataulizwa juu ya hilo, kisha midomo yao itatiwa muhuri na mikono na miguu yao itaeleza waliyoyafanya.”¹ Allah تعالی Amesema,

يُعَرَّفُ الْمَجْرُمُونَ بِسِيمَتِهِمْ

“Watajulikana wakosefu kwa alama zao.”

Maana yake: Kwa alama maalumu zenye kuwatambulisha. Al-Hasan na Qatadah walisema, “Watajulikana kwa nyuso zao nyeusi na macho ya bluu.”²

Mimi nasema kuwa alama hizi ni tofauti na alama zitakazowatambulisha Waumini, kama vile nuru itakayojitokeza sehemu ya miili yao waliokuwa wakiosha wakati wakitawadha. Allah تعالی Anasema,

فَيُؤْخَذُ بِالنَّوَاصِي وَالْأَقْدَامِ

“Na watashikwa (Yaani hao makafiri) kwa nywele zao za utosini na kwa miguu.”

Maana yake: Malaika wa adhabu watawainamisha vichwa vyao mpaka miguuni mwao na watawatupa kama hivi Motoni. Al-A’ mash alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Atashikwa utosini mwake na miguu yake na kuvunjwa kama fimbo inavyovunjwa na kutupiwa jikoni.”³ Allah تعالی Amesema;

﴿٢٨﴾ هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي يُكَذِّبُ بِهَا الْمَجْرُمُونَ ﴿٢٩﴾

“Hii ndiyo Jahannamu ambayo wakosefu wakiikanusha.”

Maana yake: ‘Moto huu ndio mliokuwa mkiukana kuwepo kwake, sasa uoneni uko mbele ya macho yenu!’ Wataambiwa hivyo kwa kufedheheshwa na kudharauliwa.

¹ At-Tabari 23:52.

² At-Tabari 23:52.

³ Ad-Dur Al-Manthur 7:704.

يَطُوفُونَ بَيْنَهَا وَبَيْنَ حَمِيمٍ ءَانٍ ﴿٧١﴾

“Watakuwa wakizunguka baina ya huo moto na maji ya moto yanayochemka sana.”

Maana yake: Wakati mwingine wataadhibiwa kwa moto wakati mwingine watapewa *Hamim* ambacho ni kinywaji kama shaba iliyoyeyuka ikikatakata matumbo yao na viungo vya ndani. Hii ni kama Kauli Yake Allah تعالى;

إِذِ الْأَغْلَالُ فِي أَعْنَاقِهِمْ وَالسَّلْسِلُ يُسْحَبُونَ ﴿٧٢﴾ فِي الْحَمِيمِ ثُمَّ فِي النَّارِ يُسْجَرُونَ ﴿٧٣﴾

“Zitakapokuwa pingu shingoni mwao na minyororo, huku wanaburuzwa. Katika maji ya moto, kisha wanaunguzwa Motoni.”
(40:71-72)

Allah تعالى Amesema,

حَمِيمٍ ءَانٍ

“Yanayochemka sana.”

Maana yake: Ya moto kutokana na joto kubwa na kali sana. Yaani haiwezekani kuhimili. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema;

يَطُوفُونَ بَيْنَهَا وَبَيْنَ حَمِيمٍ ءَانٍ ﴿٧١﴾

“Watakuwa wakizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayochemka sana.”

“Yaliyofikia halijoto ya juu kabisa na kuchemka kwa ukali.”¹ Sawa na haya yalisemwa na Mujahid, Sa’id bin Jubayr, Adh-Dhahhak, Al-Hasan, Ath-Thawri na As-Suddi.² Qatadah pia alitoa rai, “Kuchemka kwake kulianza pale Allah تعالى Alipoumba mbingu na ardhi!”³ Muhammad bin Ka’b Al-Quradhi alisema, “Mja aliyeasi atashikwa utosini atakorogwa katika maji hayo yanayochemka mpaka nyama yake inayeyuka na inasalia mifupa na macho yake kichwani mwake tu.” Hii ndiyo maana ya Kauli ya Allah تعالى,

¹ At-Tabari 23:54.

² At-Tabari 23:54-55 na Al-Qurtubi 17:175.

³ At-Tabari 23:54.

﴿٧٢﴾ فِي الْحَمِيمِ نُورٌ فِي النَّارِ يُسْجَرُونَ ﴿٧٢﴾

“Katika maji ya moto, kisha wanaunguzwa Motoni.” (40:72)

Na *Al-Hamim* inamaanisha “moto.” Kuna maelezo mengine kutoka kwa *Al-Quradhi*;

حَمِيمٍ ءَانٍ

“Na maji ya moto yanayochemka sana.”

Kuwa maana yake, “Yameandaliwa.” Hii pia ni rai ya Ibn Zayd.¹ Na inaposemwa kuwa inamaanisha “Yameandaliwa.” Yasihitilafiane na taarifa ya kwanza kutoka kwa *Al-Quradhi* ambayo inasema kuwa inamaanisha ya moto. Kwani Allah تعالی Amesema:

﴿٥٨﴾ تُسْقَىٰ مِنْ عَيْنٍ ءَانِيَةٍ ﴿٥٨﴾

“Zikinyweshwa kutoka chemchem inayochemka.” (88:5)

Ambayo maana yake ni joto kali lisilomithilika. Na kauli Yake nyingine;

غَيْرَ نَظِيرِينَ إِنَّهُ

“Sio kungojea kiwive...” (33:53)

Ambayo inamaanisha yamepikwa vyema na kuandaliwa. Kwa hivyo Kauli Yake;

حَمِيمٍ ءَانٍ

“Na maji ya moto yanayochemka sana.”

Hamim, Maana yake: Ya moto sana kwa hakika. Kuwaadhibu waasi na wakati huo huo Kuwaneemesha wachamungu, ni katika neema, rehema, uadilifu, huruma na ukarimu wa Allah تعالی kwa viumbe Wake. Maonyo dhidi ya adhabu Yake, kama ilivyotajwa katika Aya hizi ni ili Kuwatia moyo viumbe wote waache ushirikina na uasi waliojiingiza. Na hii ndiyo sababu Allah تعالی Anawakumbusha juu ya neema hii;

﴿١٠٠﴾ فَبِأَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿١٠٠﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha.”

* * *

¹ At-Tabari 23:55.

وَلَمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ جَنَّاتٍ ﴿٤٦﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا
 تُكذِّبَانِ ﴿٤٧﴾ ذَوَاتَا أَفْنَانٍ ﴿٤٨﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا
 تُكذِّبَانِ ﴿٤٩﴾ فِيهِنَّ عَيْنَانِ تَجْرِيَانِ ﴿٥٠﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ
 رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٥١﴾ فِيهِنَّ مِنْ كُلِّ فَيْكِهِمُ رَوْحَانِ ﴿٥٢﴾
 فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٥٣﴾ مُتَّكِئِينَ عَلَى فُرُشٍ
 بَطَّائِنُهَا مِنْ إِسْتَبْرَقٍ وَجَنَى الْجَنَّتَيْنِ دَانٍ ﴿٥٤﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ
 رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٥٥﴾ فِيهِنَّ قَصِيرَاتُ الْإِطْرَفِ لَمْ يَطْمِئِنَّ
 إِنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌّ ﴿٥٦﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ
 ﴿٥٧﴾ كَأَنَّهُنَّ الْيَاقُوتُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٥٨﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا
 تُكذِّبَانِ ﴿٥٩﴾ هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَنِ إِلَّا الْإِحْسَنُ ﴿٦٠﴾
 فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٦١﴾ وَمِنْ دُونِهِمَا جَنَّتَانِ ﴿٦٢﴾
 فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٦٣﴾ مُدْهَمَمَتَانِ ﴿٦٤﴾ فَبِأَيِّ
 آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٦٥﴾ فِيهِنَّ عَيْنَانِ تَضَاحَتَانِ ﴿٦٦﴾
 فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٦٧﴾ فِيهِنَّ فَيْكِهِمُ وَخَلٌّ وَرُمَانٌ ﴿٦٨﴾
 فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٦٩﴾ فِيهِنَّ حَمْرَاتُ
 حِسَانٍ ﴿٧٠﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٧١﴾ حُورٌ
 مَّقْصُورَاتٌ فِي الْخِيَامِ ﴿٧٢﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ
 ﴿٧٣﴾ لَمْ يَطْمِئِنَّ إِنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌّ ﴿٧٤﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ
 رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٧٥﴾ مُتَّكِئِينَ عَلَى رَفْرَفٍ خُضْرٍ وَعَبْقَرِيٍّ
 حِسَانٍ ﴿٧٦﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٧٧﴾ تَبْرَكَ أَسْمُ
 رَبِّكَ ذِي الْجَلَلِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٧٨﴾

وَلَمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ جَنَّاتٍ ﴿٤٦﴾
 فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٤٧﴾
 ذَوَاتَا أَفْنَانٍ ﴿٤٨﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ
 رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٤٩﴾ فِيهِنَّ عَيْنَانِ
 تَجْرِيَانِ ﴿٥٠﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا
 تُكذِّبَانِ ﴿٥١﴾ فِيهِنَّ مِنْ كُلِّ فَيْكِهِمُ
 رَوْحَانِ ﴿٥٢﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا
 تُكذِّبَانِ ﴿٥٣﴾

46. Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola Wake Mlezi atapata Bustani mbili.

47. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

48. Bustani zenye matawi yaliyotanda.

49. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

50. Ndani yake zimo chemchem mbili zinazopita.

51. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

52. Humo katika kila matunda zimo namna mbili.

53. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

Hali za Wachamungu na Starehe Zao Peponi

Allah تعالى Amesema,

وَلِمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ

“Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola Wake Mlezi”

Katika Siku ya Ufufuo.

وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٤٠﴾

“Na akajizuilia nafsi yake na matamano.” (79:40),

Na asiyeendekeza wala kupendelea maisha ya duniani. Anayejua kuwa Akhera ni bora na ya milele, hivyo anatekeleza alichuamrisha Mola Wake Mlezi na anajiepusha na makatazo Yake, atapata bustani mbili kutoka kwa Mola Wake Mlezi katika Siku ya Kiama. Al-Bukhari alimnukuu ‘Abdullah bin Qays رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«جَنَّاتٍ مِنْ فِضَّةٍ أُنْتَهَمَا وَمَا فِيهِمَا، وَجَنَّاتٍ مِنْ ذَهَبٍ أُنْتَهَمَا وَمَا فِيهِمَا، وَمَا بَيْنَ
الْقُرْمِ وَبَيْنَ أَنْ يَنْظُرُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ عَزَّ وَجَلَّ إِلَّا رِذَاءَ الْكِبْرِيَاءِ عَلَىٰ وَجْهِ فِي جَنَّةِ
عَدْنٍ»

“Bustani mbili za fedha – vyombo vyake na vilivyomo, na bustani mbili za dhahabu – vyombo vyake na vilivyomo. Na hakuna kizuizi baina yao na kumuona Mola Wao Mlezi, Mtukufu, isipokuwa vazi la kiburi juu ya Uso Wake katika Pepo ya Adni.”¹

Kundi zima, isipokuwa Abu Dawud, waliikusanya Hadithi hii kupitia ‘Abdul-‘Aziz.² Aya hii ni ya ujumla na inatumika kwa wote wawili, wanadamu na majini, ikitoa ushahidi kuwa miongoni mwa majini wapo wanaoamini na wachamungu

¹ Fat’h Al-Bari 8:491.

² Muslim 1:163, Tuhfat Al-Ahwadhi 7:232, An-Nasai katika Al-Kubra 4:419 na Ibn Majah 1:66

na wataingia Peponi. Kwa hivyo Allah تعالی Anawakumbusha *Thaqalayn* (majini na watu) kuhusu neema hii kwa kusema;

وَلَمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ جَنَّاتٍ ۖ فِيهَا ۖ آلاءٌ رَّبِّكُمْ يُكذِّبَانِ ﴿٥٧﴾

“Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola Wake Mlezi atapata Bustani mbili. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?”

Kisha Anazielezea bustani hizo mbili kwa kusema,

ذَوَاتَا أَفْنَانٍ ﴿٥٨﴾

“Bustani zenye matawi yaliyosongamana.”

Miti yake ina matawi mazuri yanayoshikilia na kuzaa kila aina ya matunda mazuri yaliyoiva.

فِيهَا ۖ آلاءٌ رَّبِّكُمْ يُكذِّبَانِ ﴿٥٩﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?”

‘Ata’ Al-Khurasani na wengine kadha walisema kuwa *Afnan* maana yake matawi yenye kuenea ambayo yanayafikia matawi ya miti mingine.

فِيهَا عَيْنَانِ تَجْرِيَانِ ﴿٦٠﴾

“Ndani yake zimo chemchem mbili zinazopita.”

Zikiwa huru kumwagilia miti na matawi haya yanayozaa matunda ya aina zote.

فِيهَا ۖ آلاءٌ رَّبِّكُمْ يُكذِّبَانِ ﴿٦١﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?”

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالی alisema kuwa mojawapo kati ya chemchemi hizi inaitwa *Tasnim*, na nyingine inaitwa *As-Salsabil*.¹ ‘Atiyah alisema kuwa maji ya mojawapo kati ya chemchemi hizi yanatoka katika maji yasiyotuama na nyingine kutokana na pombe yenye kuwafurahisha wenye kuinywa.² Kauli ya Allah تعالی

¹ Al-Qurtubi 17:178. (Angalia Surat Al-Mutaffifin 83:27-28, na Surat Al-Insan 76:17-18).

² Al-Qurtubi 17:178.

فِيهِمَا مِنْ كُلِّ فَنَكِهِمَ زَوْجَانِ ﴿٥٤﴾

“Humo katika kila matunda zimo namna mbili”

Aina mbalimbali za matunda ambayo walikuwa wakiyajua hapo kabla na yaliyo bora, na yale ambayo hawakuyajua kabla. Ndani yake kuna furaha ambayo hakuna jicho lililopata kuiona, wala sikio lililosikia, wala kupita katika akili ya yeyote,

فِي أَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٥٥﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayo ikanusha?”

Ibrahim bin Al-Hakam bin Aban alisema kuwa baba yake amesimulia kutoka kwa ‘Ikrimah kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Hakuna tunda linalopatikana duniani, tamu au chungu, bali linapatikana Peponi, hata handhali.”¹ Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema tena, “Hakuna cha duniani kilicho Akhera isipokuwa jina.” Maana yake kuna tafauti kubwa kati ya matunda ya duniani na akhera na ufananaji ni katika majina tu.

مُتَكِّينَ عَلَىٰ فُرُشٍ بَطَآئِنُهَا مِنْ إِسْتَبْرَقٍ ۗ وَجَنَىٰ الْجَنَّتَيْنِ دَانٍ ﴿٥٤﴾ فِي أَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا
تُكذِّبَانِ ﴿٥٥﴾ فِيهِنَّ قَصِيرَاتُ الْغُرُبَاتِ لَمْ يَطْمِئِنَّ أَنْسُ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌّ ﴿٥٦﴾ فِي أَيِّ ءَالَآءِ
رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٥٧﴾ كَأَنَّهُنَّ الْيَاقُوتُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٥٨﴾ فِي أَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٥٩﴾
هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَنِ إِلَّا الْإِحْسَنُ ﴿٦٠﴾ فِي أَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكذِّبَانِ ﴿٦١﴾

54. Wawe wameegemea matandiko yenye bit’ana ya hariri nzito (vitambaa vya ndani); na matunda ya Bustani hizo yapo karibu.

55. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

56. Humo watakuwamo wanawake watulizao macho yao; hajawagusa mtu kabla yao (waume zao) wala jini.

57. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

58. Kama kwamba wao ni yakuti na marijani.

¹Al-Qurtubi 17:179.

59. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha.

60. Hayakuwa malipo ya ihsani ila ihsani?

61. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

Allah تعالیٰ Amesema,

مُتَكِينٍ

“Wawe wameegemea.”

Inakusudiwa watu wa Peponi, ambao wataegemea au wataketi kimarufaa katika starehe zao;

عَلَىٰ فُرْشٍ بَطَّالِيهَا مِنۢ إِسْتَبْرَقٍ

“Wawe wameegemea matandiko yenye bit’ana ya hariri nzito.”

Ambayo ni hariri nzito, kwa mujibu wa ‘Ikrimah, Adh-Dhahhak na Qatadah.¹ Abu ‘Imran Al-Jawni alisema, “Ni hariri nzito iliyodariziwa kwa dhahabu.” Kwa namna hii, heshima ya nje imetajwa kijuujuu kwa kutajwa heshima ya ndani.

Abu Is-haq رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Hubayrah bin Yarim alisema kuwa ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Hii ni kwa ndani yake, hivyo itakuwaje ukiiona kwa nje.”²

Allah تعالیٰ Amesema,

وَجَنَىٰ الْجَنَّتَيْنِ دَانٍ

“Na matunda ya Bustani hizo yapo karibu.”

Karibu na Waumini ambao wataweza kuchukua lolote walitakalo kwa namna yoyote ile waitakayo. Kama Allah تعالیٰ Alivyosema;

قُطُوفُهَا دَانِيَةٌ

“Matunda yake yakaribu.” (69:23),

Na amesema tena;

¹ At-Tabari 23:61 na Al-Qurtubi 17:179.

² At-Tabari 23:62. Isnadi yake ni dhaifu.

وَدَانِيَةً عَلَيْهِمْ ظِلُّهَا وَذُلَّتْ قُطُوفُهَا تَذَلِيلًا ﴿١٤﴾

“Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao, na mashada ya matunda yataning’inia mpaka chini.” (76:14),

Maana yake: Matunda haya yanashuka katika matawi yao kwa wale wenye kuyataka kwa sababu yako karibu na mikono yao,

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿١٥﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayoikanusha?”

Baada ya Allah تعالى kutaja makochi, baadaye Alisema,

فِيهِنَّ

“Humo.”

Maana yake: Juu ya makochi na vitanda hivi,

قَصِيرَاتُ الْإِطْرَافِ

“Watulizao macho yao.”

Wanawake bikira, wake wanaohifadhi macho yao, hawamtamani yeyote isipokuwa waume zao, ambao watawaona kuwa ni wanaume wazuri sana Peponi. Haya yalisemwa na Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Qatadah, ‘Ata’ Al-Khurasani na Ibn Zayd.¹ Iliripotiwa kuwa mmojawapo kati ya wake hawa atamuambia mumewe, “Naapa kwa Jina la Allah تعالى! Sioni kitu chochote Peponi kizuri zaidi ya wewe wala ninachokipenda kuliko wewe. Kwa hivyo, namshukuru Allah تعالى Aliyekufanya wewe uwe kwa ajili yangu nami kwa ajili yako.” Allah تعالى Amesema,

لَمْ يَطْمِئِنِّيَنَّ إِنَّسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌّ

“Hajawagusa mtu kabla yao wala jini.”

Maana yake: Wao ni bikira wa kufurahisha wa umri wa kulingana ambao hawajapata kuingiliwa na yeyote, mwanaadamu au jini, kabla ya waume zao. Huu ni ushahidi kuwa Waumini miongoni mwa majini nao pia wataingia Peponi.

¹ At-Tabari 23:63 na 21:41.

Artat bin Al-Mundhir alisema, “Damrah bin Habib aliulizwa kama majini wataingia Peponi, akajibu, ‘Ndiyo, na wao wataoa. Majini wa kiume watakuwa na wanawake wa kijini wa kike na wanaume wa kibinaadamu watakuwa na wanawake wa kibinaadamu.”¹ Kauli ya Allah تعالى،

لَمْ يَطْعَمْنَ إِنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌّ ﴿٥٦﴾ فَبِأَيِّ آءِالَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٧﴾

“Hajawagusa mtu kabla yao wala jini. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?”

Kisha Allah تعالى Anaeleza sifa za wanawake hawa kwa ajili ya watakaowao:

كَأَنَّهُنَّ الْيَاقُوتُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٥٨﴾

“Kama kwamba wao ni yakuti na marijani.”

Mujahid, Al-Hasan, Ibn Zayd na wengine walisema, “Wao ni safi kabisa kama rubi na weupe kama Marijaani.” Kwa hivyo hapa ameleza Marijaani kama lulu.² Imamu Muslim alinukuu kuwa Muhammad bin Sirin رحمه الله تعالى alisema, “Baadhi ya watu walijigamba au walishangaa kuwa ni nani walio wengi Peponi, wanaume au wanawake.” Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, ‘Kwani Abu Al-Qasim, Yaani, Mtume Muhammad ﷺ hakusema.

«إِنَّ أَوَّلَ زُمْرَةٍ تَدْخُلُ الْجَنَّةَ عَلَى صُورَةِ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ، وَالَّتِي تَلِيهَا عَلَى [أَضْوَاءِ] كَزَوْكِبِ دُرِّيٍّ فِي السَّمَاءِ، لِكُلِّ امْرِيءٍ مِنْهُمْ زَوْجَتَانِ اثْنَتَانِ، يُرَى مَخَّ سُوْقَيْهِمَا مِنْ وَرَاءِ اللَّحْمِ، وَمَا فِي الْجَنَّةِ أَغْرَبُ»

“Hakika, kundi la kwanza litakaloingia Peponi litakuwa katika sura ya mwezi usiku wa Mbalamwezi, na kundi linalofatia ni katika sura ya nyota mbinguni. Kila mmoja wao ataoa wake wawili. Uboho wa mifupa ya miundi yao utaonekana nyuma ya nyama. Na katika Pepo hakuna msela (bachela).”³

Hadithi hii ilinukuliwa katika Sahih Mbili.⁴ Imamu Ahmad alinukuu kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ At-Tabari 23:65.

² At-Tabari 23:66-67.

³ Muslim 4:2178.

⁴ Fat’h Al-Bari 6:367 na 417 na Muslim 4:2179-2180.

«لَعَدْوَةٌ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ رَوْحَةٌ خَيْرٌ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا فِيهَا، وَلَقَابٌ قَوْسٍ أُخِدْتُمْ، أَوْ مَوْضِعٌ قَدِّهِ - يَغْنِي سَوْطَهُ - مِنَ الْجَنَّةِ خَيْرٌ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا فِيهَا، وَلَوْ اطَّلَعَتِ امْرَأَةٌ مِنْ نِسَاءِ أَهْلِ الْجَنَّةِ إِلَى الْأَرْضِ لَمَلَأَتْ مَا بَيْنَهُمَا رِيحًا، وَلَطَابَ مَا بَيْنَهُمَا، وَلَتَصِيفُهَا عَلَى رَأْسِهَا خَيْرٌ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا فِيهَا»

“Kuondoka asubuhi au jioni katika njia ya Allah ni bora kuliko dunia na vilivyomo; na mahali padogo Peponi kama eneo la upinde wa mmoja wenu na kamba yake ni bora kuliko dunia na vilivyomo. Lau angejitokeza duniani mmoja wa wanawake wa Peponi basi angejaza dunia harufu nzuri, na ingejaa furaha. Hakika, ushungi wa kichwani mwake, ni bora kuliko dunia na vilivyomo.”¹

Al-Bukhari pia alikusanya simulizi sawa na hii.²

Allah تعالى Amesema,

هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَنِ إِلَّا الْإِحْسَانُ ﴿٥٦﴾

“Ati yaweza kuwa malipo ya ihsani ila ihsani?”

Allah تعالى Anatangaza kuwa Akhera, wote, yaani, wema na wachamungu wanastahiki malipo kwa amali njema walizofanya duniani,

لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ﴿٥٧﴾

“Kwa wafanyao wema ni wema na zaidi.” (10:26)

Maana yake: Hizi ni neema kubwa ambazo haziwezi kupatikana kwa amali njema tu, bali Fadhila na Rehema za Allah تعالى, baada ya yote haya Allah تعالى Anasema;

فَبِأَيِّ ءَالَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٨﴾

“Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?”

¹ Ahmad 3:141.

² Fat'h Al-Bari 6:19.

وَمِنْ دُونِهِمَا جَنَّتَانِ ﴿٦٢﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٣﴾ مُدْهَمَمَتَانِ ﴿٦٤﴾ فَبِأَيِّ
 آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٥﴾ فِيهِمَا عَيْنَانِ نَضَّخَتَاَنِ ﴿٦٦﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ
 ﴿٦٧﴾ فِيهِمَا فَنَكِهَةٌ وَنَخْلٌ وَرُؤْمَانٌ ﴿٦٨﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٩﴾ فِيهِنَّ حَيْرَاتٌ
 حِسَانٌ ﴿٧٠﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٧١﴾ حُورٌ مَّقْصُورَاتٌ فِي الْخِيَامِ ﴿٧٢﴾ فَبِأَيِّ
 آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٧٣﴾ لَمْ يَطْمِئِنَّ أَنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌ ﴿٧٤﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا
 تُكَذِّبَانِ ﴿٧٥﴾ مُتَكَبِّرِينَ عَلَى رَفْرَفٍ خُضِرٍ وَعَبَقَرِيٍّ حِسَانٍ ﴿٧٦﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا
 تُكَذِّبَانِ ﴿٧٧﴾ تَبْرَكَ اسْمُ رَبِّكَ ذِي الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٧٨﴾

62. Na zaidi ya hizo Bustani nyingine mbili.

63. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

64. Za kijani kibivu.

65. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

66. Humo kuna chemchem mbili zenye kufurika.

67. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

68. Imo humo miti ya matunda, na mitende na mikomamanga.

69. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

70. Humo wamo wanawake wema wazuri.

71. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

72. Wanawake wazuri wanaotawishwa katika mahema.

73. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

74. Hajawagusa mtu wala jini kabla yao (yaani waume zao).

75. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

76. Wameegemea juu ya matakia ya kijani na mazulia mazuri.

77. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?

78. Limetukuka Jina la Mola Wako Mlezi Mwenye Utukufu na Ukarimu.

Bustani hizi mbili ni za hadhi ya chini na daraja, kuliko zile mbili za kabla yake, kama zilivyoenezwa katika Qur'an. Allah تعالى Amesema:

وَمِنْ دُونِهِمَا جَنَّتَانِ ﴿٧٧﴾

“Na zaidi ya hizo zipo Bustani nyingine mbili.”

Hapo nyuma tumetaja Hadithi inayoeleza kuwa kuna bustani mbili zilizotengenezwa kwa dhahabu, vyombo vyake na vilivyomo, na kuna bustani mbili zilizotengenezwa kwa fedha, vyombo vyake na vilivyomo. Mbili za kwanza ni kwa wale Waumini wa karibu (*Muqarribin*) na mbili zilizofuatia ni kwa wale wa kuumeni (*As'hab Al-Yamin*).¹ Abu Musa alisema, “Kuna bustani mbili zilizotengenezwa kwa dhahabu kwa ajili ya *Muqarribin* na bustani mbili zilizotengenezwa kwa fedha kwa ajili ya *As'hab Al-Yamin*.” Kuna ushahidi mwingi unaoonesha kuwa bustani mbili za awali Peponi ni bora kwa daraja kuliko zilizofuatia. Allah تعالى Ametaja bustani mbili za awali kabla ya zilizofuatia, na kwa hivyo, inajulisha ubora wao. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَمِنْ دُونِهِمَا جَنَّتَانِ ﴿٧٨﴾

“Na zaidi ya hizo zipo Bustani nyingine mbili.”

Na hii ni namna iliyo dhahiri katika kuzipa utukufu bustani mbili za kwanza kuliko mbili zinazofuatia. Allah تعالى Ameerza bustani mbili za awali:

ذَوَاتَا أَفْنَانٍ ﴿٧٩﴾

“Bustani zenye miti ambazo zina matawi mengi.”

Ambayo ni matawi yaliyojitandaza, kama tulivyoeleza, au furaha za namna kwa namna. Na Akasema kuhusu bustani mbili ziizofuatia,

¹ *Fat'h Al-Bari* 8:491.

مُدَّهَامَتَانِ

“Za kijani kibivu.”

Kuwa rangi yake imekoza, kwa sababu ya kupata maji kwa wingi. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “*Mud-hammatan’* Maana yake, zimekolea rangi ya kijani kibivu iliyokoza kutokana na kupata maji kwa wingi.”¹ Muhammad bin Ka’b alisema:

مُدَّهَامَتَانِ

“Za kijani kibivu.”

“Rangi ya kijani kibivu iliyokoza sana.” Hakuna shaka kuwa bustani mbili za awali ndio bora zaidi, matawi yake ni mapya, machanga na yamechanganyikana. Allah تعالى Amesema kuhusu bustani mbili za awali,

فِيهِمَا عَيْنَانِ تَجْرِيَانِ

“Humo kuna mbili zenye kufurika.”

Ambapo Alisema kuhusu chemchemi za bustani mbili za baadaye,

نَضَّاحَتَانِ

“Mbili zenye kufurika.”

‘Ali bin Abu Talhah alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: “Inamaanisha zikibubujika. Kutiririka kwa uhuru kuna nguvu kuliko kububujika.”²

Adh-Dhahaak alisema kuwa,

نَضَّاحَتَانِ

“Mbili zenye kufurika”

Maana yake: Zina maji ya kutosha na kwa muda wote yanatiririka.³ Allah تعالى Amesema kuhusu bustani mbili za awali,

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:715.

² Ad-Dur Al-Manthur 7:716.

³ At-Tabari 23:357.

فِيهِمَا مِنْ كُلِّ فَنِكَهَةٍ زَوْجَانِ ﴿٥٦﴾

“Humo katika kila matunda zimo namna mbili.”

Lakini Akasema kuhusu bustani za baadaye,

فِيهَا فَنِكَهَةٌ وَنَخْلٌ وَرُمَّانٌ ﴿٥٧﴾

“Imo humo miti ya matunda, na mitende na mikomamanga.”

Hakuna shaka kuwa maelezo ya kwanza ni bora zaidi na inamaanisha kuwemo namna na aina nyingi za matunda kuliko maelezo ya pili. Kisha Allah تعالى Akasema;

فِيهِنَّ خَيْرَاتٌ حِسَانٌ ﴿٥٨﴾

“Humo wamo wanawake wema wazuri.”

Imesemwa, imekusudiwa kheri nyingi Peponi, kwa mujibu wa Qatadah. Imesemwa pia kuwa *Khayrat* ni wingi wa neno *Khayrah* na maana yake ni mwanamke mwema, mwenye maadili mazuri, kwa mujibu wa wanazuoni wengi. Pia ilisimuliwa kutoka kwa Umm Salaman رضي الله عنها Hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ.¹ Kuna Hadithi nyingine kuwa hao *Al-Hur Al-Ayn* wataimba,

«نَحْنُ الْخَيْرَاتُ الْحِسَانُ، خُلِقْنَا لِأَزْوَاجِ كِرَامٍ»

“Sisi ni Al-Khayrat Al-Hisan (wanawake wema), tumeumbwa kwa ajili ya waume wenye heshima.”²

Allah تعالى Amesema:

حُورٌ مَّقْصُورَاتٌ فِي الْحِيَامِ ﴿٥٩﴾

“Wanawake wazuri wanaotawishwa katika mahema.”

Lakini Akasema kuhusu bustani mbili za kwanza,

فِيهِنَّ قَنَصِرَاتُ الْطَّرْفِ ﴿٦٠﴾

“Humo watakuwemo wanawake watulizao macho.”

¹ At-Tabari 23:75.

² At-Tabarani katika *Al-Awsat* 7:257.

Hakuna shaka kuwa wake safi wanaoyahifadhi macho yao ni bora kuliko waliolindwa katika mahema ingawa wote hao wamehifadhika. Kuhusu Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فِي الْحَيَامِ

“Katika mahema.”

Al-Bukhari alinukuu kuwa ‘Abdullah bin Qays رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ خَيْمَةً مِنْ لَوْلُؤَةٍ مُجَوَّفَةٍ، عَرْضُهَا سِتُونَ مِيلاً، فِي كُلِّ زَاوِيَةٍ مِنْهَا أَهْلٌ، مَا يَرَوْنَ الْآخَرِينَ يَطُوفُ عَلَيْهِمُ الْمُؤْمِنُونَ»

“Hakika, Peponi, Kuna hema la lulu lenye uwazi, upana wake ni maili sitini, katika kila kona kuna wake, Muumini anawazungukia bila ya wengine kuona.”¹

Katika simulizi nyingine Mtume ﷺ alisema kuwa hema hili lina upana wa maili thelathini.² Muslim aliinukuu Hadithi hii. Katika simulizi nyingine, Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ لِلْمُؤْمِنِ فِي الْجَنَّةِ لَخَيْمَةً مِنْ لَوْلُؤَةٍ وَاحِدَةٍ مُجَوَّفَةٍ، طُولُهَا سِتُونَ مِيلاً، لِلْمُؤْمِنِ فِيهَا أَهْلٌ يَطُوفُ عَلَيْهِمُ الْمُؤْمِنُونَ فَلَا يَرَى بَعْضُهُمْ بَعْضًا»

“Hakika Peponi Muumini atakuwa na hema moja la lulu lenye uwazi urefu wake ni maili sitini ndani yake. Muumini atakuwa na wake, Muumini atawatembelea wote bila ya wao kuonana.”³

Allah تعالى Amesema,

لَمْ يَطْمِئِنِّيَنَّ إِنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌّ ﴿٧٦﴾

“Hajawagusa mtu wala jini kabla yao.”

Tulishaeleza Aya hii hapo awali. Allah تعالى Aliongeza katika maelezo ya kundi la kwanza la wake wa Waumini,

¹ Fat’h Al-Bari 8:491.

² Fat’h Al-Bari 6:366.

³ Muslim 4:2182.

كَأَنَّهُنَّ الْيَاقُوتُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٥٥﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٦﴾

“Kama kwamba wao ni yakuti na marijani. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha.”

Allah تعالى Amesema,

مُتَكِبِينَ عَلَى رَفْرَفٍ خُضِرٍ وَعَبْقَرِيٍّ حِسَانٍ ﴿٥٧﴾

“Wameegemea juu ya matakia ya kijani na mazulia mazuri.”

‘Ali bin Abu Talhah alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: “*Rafraf* maana yake mito.”¹

Mujahid, ‘Ikrimah, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahhak na wengine pia walisema kuwa *Rafraf* maana yake mito.² Al-‘Ala’ bin Badr alisema: “*Rafraf* ni namna ya mavazi yanayoning’inia katika makochi.” Kauli ya Allah تعالى,

وَعَبْقَرِيٍّ حِسَانٍ

“Na mazulia mazuri.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Qatadah, Adh-Dhahhak na As-Sudd walisema kuwa ‘*Abqariy* maana yake mazulia ya thamani kubwa.³ Allah تعالى Amesema,

تَبَرَّكَ اسْمُ رَبِّكَ ذِي الْجَلَلِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٥٨﴾

“Limetukuka Jina la Mola Wako Mlezi Mwenye Utukufu na Ukarimu.”

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye Ana haki zaidi ya Kunyenyekewa na wala Haasiwi, na siku zote Kutiwa, Kutukuzwa na Kuabudiwa, Mwenye Kushukuriwa na wala Hakanushwi Neema Zake, Mwenye kukumbukwa na wala haifai kumsahau. ‘Abdullah bin ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

¹ At-Tabari 23:83.

² At-Tabari 23:84.

³ At-Tabari 23:85.

ذِي الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

“Mwenye Utukufu na Ukarimu.” Maana yake: Mwenye Utukufu na Kiburi.⁴ Katika Hadithi, Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ مِنْ إِجْلَالِ اللَّهِ إِكْرَامُ ذِي الشَّيْبَةِ الْمُسْلِمِ، وَذِي السُّلْطَانِ، وَحَامِلِ الْقُرْآنِ غَيْرِ
الْغَالِي فِيهِ، وَلَا الْجَافِي عَنْهُ»

“Hakika, miongoni mwa amali za kumtukuza Allah, ni kumheshimu mzee Muislamu, mwenye mamlaka, na mwenye kuhifadhi Qur’an, asiyepetuka mpaka katika kufuata kanuni zake, wala anayeisoma haraka bila kuzingatia maana yake, wala asiyejitenga nayo.”²

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Rabi’ah bin ‘Amir رضي الله عنه alisema: “Nimemsikia Mtume ﷺ akisema,

«أَلِظُوا بِذِي الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ»

“Mdumu (katika kumuomba Allah) kwa kusema, “Ya Dhal-Jalal wal-Ikram (Ewe Mwenye Utukufu na Ukarimu).”¹

An-Nasa’i pia aliikusanya Hadithi hii.² Muslim na wakusanyaji wanne wa Sunan walinukuu kuwa mama A’ishah رضي الله عنها alisema, “Pale Mtume ﷺ alipofika katika kutoa Salam (ya kukamilisha Sala), alikaa kiasi kwa ajili ya kusema,

«اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَمِنْكَ السَّلَامُ، تَبَارَكْتَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ»

“Mola Wangu! Wewe ni As-Salaam na amani inatoka Kwako, Umetukuka Yaa Dhal-Jalaal Wal-Ikraam (Ewe Mwenye Utukufu na Ukarimu).”³

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Ar-Rahman*, Sifa zote njema pamoja na Shukurani ni za Allah تعالى na Fadhila hutoka Kwake.



¹ At-Tabari 23:86.

² Abu Dawud 5:174. Isnadi yake ni dhaifu, Abu Kinana hafahamiki katika Isnadi yake hii. Taz. “At-Takrib” (2899).

³ Ahmad 4:177.

⁴ An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:479.

⁵ Muslim 414. Abu Dawud 2:179, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 2:192 na An-Nasai 3:69 na Ibn Majah 1:298.

Tafsiri ya Suratul Waqi'ah

Sura ya 56

Iliteremshwa Makkah

Fadhila za Suratu *Al-Waqi'ah*

Abu Is'haq رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa 'Ikrimah kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa Abubakr رضي الله عنه alisema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Umepatwa na mvi." Mtume ﷺ alimjibu,

«شَيْتَنِي هُوَ وَالْوَاقِعَةُ وَالْمُرْسَلَاتُ وَعَمَّ يَتَسَاءَلُونَ وَإِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ»

"Sura Hud" ya 11, "Al-Waqi'ah" ya 56, "Al-Mursalat" ya 77, "Amma Yatasa'alun" ya 78, na "Idha Ash-Shamsu Kuwwirat" ya 81" zimefanya mimi nipate mvi.'

At-Tirmidhi alikusanya Hadithi hii na kusema, "*Hasan Gharib*."¹

* * *

¹ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:184.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْوَاقِعَاتِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِذَا وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ❶ لَيْسَ لَوْقَعَتِهَا كَاذِبَةٌ ❷ حَافِضَةٌ ❸ رَافِعَةٌ ❹ إِذَا رُجَّتِ الْأَرْضُ رَجًا ❺ وَبُسَّتِ الْجِبَالُ بَسًا ❻ فَكَانَتْ هَبَاءً مُنْبَثًا ❼ وَكُنْتُمْ أَزْوَاجًا ثَلَاثَةً ❽ فَأَصْحَابُ الْمَيْمَنَةِ مَا أَصْحَابُ الْمَيْمَنَةِ ❾ وَأَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ مَا أَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ ❿ وَالسَّيِّقُونَ وَالسَّيِّقُونَ ⓫ أُولَئِكَ الْمُقَرَّبُونَ ⓬ فِي جَنَّتِ النَّعِيمِ ⓭ ثَلَاثَةٌ ⓮ مِنَ الْأُولَى ⓯ وَقَلِيلٌ مِنَ الْآخِرِينَ ⓰ عَلَى سُرُرٍ مَوْضُونَةٍ ⓱ مُتَّكِينَ عَلَيَّهَا مُتَقَابِلِينَ ⓲ يَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُخَلَّدُونَ ⓳ بِأَكْوَابٍ وَأَبَارِيقٍ وَكَأْسٍ مِنْ مَعِينٍ ⓴ لَا يُصَدَّعُونَ عَنْهَا وَلَا يُنْفَوْنَ ⓵ وَفَكَهْرُهُ مِمَّا يَتَخَيَّرُونَ ⓶ وَلَحْمٍ طَيْرٍ مِمَّا يَشْتَبُونَ ⓷ وَخَوْرُ عَيْنٍ ⓸ كَأَمْثَلِ اللَّوْلِيِّ الْمَكُونِ ⓹ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ⓺ لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْثِيمًا ⓻ إِلَّا قِيلًا سَلَامًا سَلَامًا ⓼

إِذَا وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ❶ لَيْسَ لَوْقَعَتِهَا كَاذِبَةٌ ❷ حَافِضَةٌ ❸ رَافِعَةٌ ❹ إِذَا رُجَّتِ الْأَرْضُ رَجًا ❺ وَبُسَّتِ الْجِبَالُ بَسًا ❻ فَكَانَتْ هَبَاءً مُنْبَثًا ❼ وَكُنْتُمْ أَزْوَاجًا ثَلَاثَةً ❽ فَأَصْحَابُ الْمَيْمَنَةِ مَا أَصْحَابُ الْمَيْمَنَةِ ❾ وَأَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ مَا أَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ ❿ وَالسَّيِّقُونَ وَالسَّيِّقُونَ ⓫ أُولَئِكَ الْمُقَرَّبُونَ ⓬ فِي جَنَّتِ النَّعِيمِ ⓭

1. Litakapotukia hilo Tukio.
2. Hapana wa kukanusha kutukia kwake.
3. Literemshalo linyanyualo.
4. Itakapotikiswa ardhi kwa mtikiso.
5. Na milima itaposagwasagwa.
6. Iwe mavumbi yanayopeperushwa.

7. Na nyinyi mtakuwa namna tatu:-

8. Basi watakuwepo wa kuliani; je, ni wepi wa kuliani?

9. Na wa kushotoni; je, ni wepi wa kushotoni?

10. Na wa mbele watakuwa mbele.

11. Hao ndio watakaokaribishwa.

12. Katika Bustani zenye neema.

Utajo wa Vitisho vya Siku ya Kiyama

Al-Waqi'ah (tukio), ni jina mojawapo la Siku ya Kiyama, kwa sababu ya uhakika wa kutukia kwake. Sawa na Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine ,

فَيَوْمَئِذٍ وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ﴿٥٦﴾

“Siku hiyo ndio Tukio litatukia.” (69:15)

Kauli ya Allah تعالى,

لَيْسَ لَوْقَعَتِهَا كَاذِبَةٌ ﴿٥٧﴾

“Hapana cha kukanusha kutukia kwake.”

Inamaanisha kuwa Atakapoamuru Siku ya Kiyama kuanza, hakuna wa kuzuia au kuiondoa. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

أَسْتَجِيبُوا لِلرَّبِّكُمْ مِّن قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدَّ لَهُ مِنَ اللَّهِ ﴿٤٢﴾

“Muitikieni Mola Wenu Mlezi kabla haijafika siku isiyoepekika itokayo kwa Mwenyezi Mungu.” (42:47).

Na Allah تعالى Amesema;

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ ﴿٧٠﴾ لِّلْكَافِرِينَ لَيْسَ لَهُمْ دَافِعٌ ﴿٧١﴾

“Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea, kwa makafiri - ambayo hapana awezaye kuizuia.” (70:1-2).

Na Allah تعالى Amesema;

وَيَوْمَ يَقُولُ كُن فَيَكُونُ قَوْلَهُ الْحَقُّ وَلَهُ الْمَلَكُ يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ عَلِيمُ الْغَيْبِ
وَالشَّهَادَةِ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ ﴿٧٣﴾

“Na Anaposema: Kuwa! Basi huwa. Kauli Yake ni Haki. Na Ufalme wote ni Wake Siku litapopulizwa baragumu, Mjuzi wa yaliyo fichikana na yanayoonekana. Naye Ndiye Mwenye Hekima na Mwenye Khabari.” (6:73)

Ama kuhusu maana ya:

كَاذِبَةٌ

“Kadhibah.” Muhammad bin Ka'b amesema: “Kwa hakika itakuja.” Qatadah amesema, “Haitasimamishwa, kurudishwa au kuahirishwa.”¹ Kauli ya Allah

تعالى،

خَافِضَةٌ رَّافِعَةٌ ﴿٧٤﴾

“...Literemshalo linyanyualo...”

Inaashiria kuwa *Al-Waqi'ah* inawashusha baadhi ya watu hadi katika sehemu za chini kabisa katika Moto, hata kama walikuwa wenye nguvu duniani. Pia inawainua wengine hadi daraja za juu kabisa kwenye neema ya milele, hata kama walikuwa wanyonge duniani. Hayo yalisemwa na Al-Hasan, Qatadah na wengine.² Al-'Awfi amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما:

خَافِضَةٌ رَّافِعَةٌ ﴿٧٥﴾

“...Literemshalo linyanyualo...” “Litawafanya wa mbali na wa karibu kulisikia.” 'Ikrimah amesema, “Litawashusha, na kuwafanya walio karibu kulisikia, na litanyanyuka hadi walio mbali walisikie.” Adh-Dhahhak na Qatadah wamesema sawa na hivyo. Kauli ya Allah تعالى،

إِذَا رُجَّتِ الْأَرْضُ رَجًا ﴿٧٦﴾

“Itakapotikiswa ardhi kwa mtikiso.”

Inamaanisha, itatikiswa kwa nguvu na itatetemeka kwa mapana na marefu yake. Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, Mujahid, Qatadah na wengine wamesema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 23:89.

² At-Tabari 23:90.

إِذَا رُجَّتِ الْأَرْضُ رَجًا ﴿١﴾

"Itakapotikiswa ardhi kwa mtikiso."

Inamaanisha, "Itatikiswa kwa nguvu."¹ Ar-Rabi` bin Anas amesema, "Dunia itatikiswa pamoja na vyote vilivyo ndani yake, kama chekeche kutikiswa pamoja na vilivyomo." Hayo ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ﴿٢﴾

"Itakapotetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wake!" (99:1) Na,

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ آتِفًاؤًا رِيكُمُ ءَ إِنَّا زَلْزَلْنَا السَّاعَةَ شَيْءٌ عَظِيمٌ ﴿٣﴾

"Enyi watu! Mcheni Mola Wenu Mlezi. Hakika tetemeko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu." (22:1).

Kauli ya Allah تعالى:

وَأُتْسِتِ الْجِبَالُ بَسًا ﴿٤﴾

"Na milima itaposagwasagwa."

Inamaanisha, kupondwapondwa bila ya kutulia. Hayo yalisemwa na Ibn 'Abbas, Mujahid, 'Ikrimah na Qatadah na wengine رضي الله عنهم.² Ibn Zayd amesema: "Milima itakuwa kama Allah تعالى Alivyoielezea,

كُتِبْنَا مَهِيلاً ﴿٥﴾

"...kama tifutifu la mchanga!" (73:14)."³

Kauli ya Allah تعالى:

فَكَانَتْ هَبَاءً مُنْبِتًا ﴿٦﴾

"Iwe mavumbi yanayopeperushwa."

Abu Is'haq رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Al-Harith, kutoka kwa 'Ali رضي الله عنه: "Itakuwa kama dhoruba la mavumbi kutimka na baada ya muda kupotea bila ya kuacha alama zake nyuma." Al-'Awfi amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 23:91.

² At-Tabari 23:92, 93.

³ At-Tabari 23:93.

فَكَانَتْ هَبَاءً مُنْبِتًا

“Iwe mavumbi yanayopeperushwa.”

“Inaelezwa ni kama cheche kupanda juu kutoka katika moto unapowashwa, lakini cheche hizo zinapoanguka chini, huzimika haraka.”¹ ‘Ikrimah amesema, “Chembe za cheche zenye kupulizwa na upepo.” Ilhali Qatadah amesema,

هَبَاءً مُنْبِتًا

“...mavumbi yanayopeperushwa.” “Ni kama majani makavu ya miti yanayotawanywa na upepo kila mahali.” Aya hii inafanana na Aya zingine zenye kujulisha kuwa milima itaondolewa kutoka mahali pake, ikiwa imesagwasagwa na kupeperushwa kutoka katika mihimili yake, na kuwa kama pamba iliyochambuliwa katika Siku ya Kiyama.

Makundi Matatu ya Watu Siku ya Kiyama

Kauli ya Allah تعالى،

وَكُنْتُمْ أَزْوَاجًا ثَلَاثَةً

“Na nyinyi mtakuwa namna tatu.”

Inamaanisha kuwa watu siku ya Kiyama watagawanyika katika makundi matatu. Watu watakaokuwa katika upande wa kulia wa Arshi, na hao ni wale waliotokea katika upande wa kulia wa Adam عليه السلام.² Kundi hili litapewa Vitabu vyao vya kumbukumbu kwa mkono wa kulia na watapelekwa katika upande wa kulia. As-Suddi amesema kwamba watakuwa watu wa Peponi. Wengine watakuwa katika upande wa kushoto wa Arshi, na wao ni wale waliotokea katika upande wa kushoto wa Adam عليه السلام. Hawa watapewa Vitabu vyao vya kumbukumbu kwa mikono yao ya kushoto na watapelekwa katika upande wa kushoto. Wao watakuwa watu wa Motoni, Allah تعالى Atuokoe dhidi ya vitendo vyao. Kundi la tatu litakuwa la wale ambao wako mbele zaidi na wako karibu zaidi na Allah تعالى. Watakuwa bora zaidi kwa daraja na heshima na karibu zaidi na Allah تعالى kuliko wale wa upande wa kulia. Wao ni viongozi wa wale wa upande wa kulia, kwa sababu wao ni pamoja na Mitume, Manabii,

¹ At-Tabari 23:94.

² Angalia masimulizi ya Abu Dharr, na. 349 ya Al-Bukhari, na yametajwa katika juzu ya tano, mwanzoni mwa Tafsiri ya Surat Al-Isra’.

waumini wa kweli na watu waliokufa shahidi. Wao ni wachache zaidi kuliko wale wa upande wa kulia; kwa ajili hiyo, Kauli ya Allah تعالى،

وَأَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ مَا أَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ ﴿٣١﴾ وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ ﴿٣٢﴾

“Basi watakuwepo wa kuliani; je, ni wepi wa kuliani? Na wa kushotoni; je, ni wepi wa kushotoni? Na wa mbele watakuwa mbele.”

Allah تعالى Amewagawa watu katika makundi matatu baada ya kufa kwao, kama ilivyojulishwa mwishoni mwa Surah hii. Allah تعالى Amewataja katika Kauli yake،

ثُمَّ أَوْرَثْنَا الْكِتَابَ الَّذِينَ اصْطَفَيْنَا مِنْ عِبَادِنَا فَمِنْهُمْ ظَالِمٌ لِنَفْسِهِ وَمِنْهُمْ مُقْتَصِدٌ وَمِنْهُمْ سَابِقٌ بِالْخَيْرَاتِ بإِذْنِ اللَّهِ ﴿٣٣﴾

“Kisha Tumewarithisha Kitabu hao ambao Tuliwateua miongoni mwa waja Wetu. Kati yao yupo aliyejidhulumu nafsi yake, na yupo wa katikati, na yupo aliyetangulia katika mambo ya kheri, kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu.” (35:32)

Muhammad bin Ka'b, Abu Hazra Ya'qub bin Mujahid wamesema،

وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ ﴿٣٤﴾

“Na wa mbele watakuwa mbele.”

Ni kuhusu Mitume, amani iwafikie wao wote, wakati As-Suddi amesema kuwa wao ni watu wa mahali pa juu (*Ahl Al-'Illiyin*, Peponi). Kama Allah تعالى Alivyosema; Maana ya 'wa mbele' ni kuwa walikuwa mbele katika kufanya matendo mema kama Allah تعالى Alivyowaamuru،

وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ

“Na yakimbilieni maghufira ya Mola Wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi.” (3:133)

Na Allah تعالى Amesema;

¹ Al-Qurtubi 17:199.

سَابِقُونَ إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكَمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

'Kimbilieni msamaha wa Mola Wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi.' (57:21)

Kwa hiyo, wanaoharakisha kumtii Allah تعالى duniani na wa mbele katika kufanya matendo mema, watakuwa miongoni mwa waumini wa mbele kupewa utukufu huko Akhera. Kwa hakika, malipo ni kwa mujibu wa aina ya amali, na kadiri mtu anavyotenda, ndivyo atakavyohukumiwa. Kwa hivyo, Kauli ya Allah:

أُولَئِكَ الْمُقَرَّبُونَ ﴿١٣﴾ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿١٤﴾

"Hao ndio watakaokaribishwa. Katika Bustani zenye neema."

ثَلَاثَةٌ مِّنَ الْأُولَىٰ ﴿١٥﴾ وَقَلِيلٌ مِّنَ الْآخِرِينَ ﴿١٦﴾ عَلَىٰ سُرُرٍ مَّوْضُونَةٍ ﴿١٧﴾ مُتَّكِنِينَ عَلَيْهَا ﴿١٨﴾ مُتَقَابِلِينَ ﴿١٩﴾ يَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُونَ ﴿٢٠﴾ بِأَكْوَابٍ وَأَبَارِيقٍ وَكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿٢١﴾ لَا يُصَدَّعُونَ عَنْهَا وَلَا يُنزِفُونَ ﴿٢٢﴾ وَفِيكِهِمْ مِمَّا يَتَخَبَّروْنَ ﴿٢٣﴾ وَحَمْرٍ طَيْرٍ مِّمَّا يَشْتَبُونَ ﴿٢٤﴾ وَحُورٌ عِينٌ ﴿٢٥﴾ كَأَمْثَلِ اللَّوْلُؤِ الْمَكْنُونِ ﴿٢٦﴾ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾ لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْتِيهَا ﴿٢٨﴾ إِلَّا قِيْلًا سَلَامًا سَلَامًا ﴿٢٩﴾

13. Kundi kubwa ni katika watu wa mwanzo.

14. Na wachache ni katika watu wa mwisho.

15. Watakuwa juu ya viti vya fakhari vilivyotonewa (mapambo).

16. Wakiviegemea wakielekeana.

17. Wakitumikiwa na wavulana wa ujana wa milele.

18. Kwa vikombe na mabirika na bilauri za vinywaji kutoka chemchem safi zenye kupita.

19. Hawataumwa kichwa kwa vinywaji hivyo wala hawatoleweshwa.

20. Na matunda wayapendayo.

21. Na nyama za ndege kama wanavyotamani.

22. Na Mahurulaini.

23. Walio kama mfano wa wanawake wenye macho mazuri, makubwa.

24. Ni malipo kwa waliyokuwa wakiyatenda.

25. Humo hawatasikia porojo wala maneno ya dhambi.

26. Isipokuwa maneno ya Salama na amani.

Malipo ya Watu wa Mbele katika Imani

Allah تعالی Anaeleza kuwa waumini wa mwanzo ni kundi kubwa katika vizazi vilivyotangulia na wachache kutoka katika vizazi vya mwisho. Wafasiri wametofautiana katika maana ya vizazi vya mwanzo na vya mwisho. Baadhi wamesema kuwa wa mwanzo inamaanisha nyumati (zilizoamini) mwanzoni, wakati wa mwisho ni Umati huu. Hayo yalisimuliwa kutoka kwa Mujahid na Al-Hasan Al-Basri, na amekusanya Ibn Abi Hatim, na rai hii ndiyo aliyochagua Ibn Jarir رحمه الله تعالى.¹ Aliichukulia kuwa iliungwa mkono na kauli ya Mtume ﷺ:

«نَحْنُ الْأَخِرُونَ السَّابِقُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

"Sisi ni umati wa mwisho, wenye kutangulia Siku ya Kiyama."²

Ibn Jarir رحمه الله تعالى hakutaja maelezo yoyote wala kuinasibisha rai hii kwa yeyote mwingine. Hadithi yenye kuunga mkono rai hiyo ni aliyopokea Imamu Abu Muhammad bin Abi Hatim رحمه الله تعالى kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: Ziliposhuka Aya zifuatazo,

ثُلَّةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٤﴾ وَقَلِيلٌ مِنَ الْآخِرِينَ ﴿٢٥﴾

"Fungu kubwa katika wa mwanzo, na wachache katika wa mwisho."

Habari hizi zikawa nzito kwa Masahaba wa Mtume ﷺ. Ikateremshwa Aya ifuatayo,

ثُلَّةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٤﴾ وَقَلِيلٌ مِنَ الْآخِرِينَ ﴿٢٥﴾

"Fungu kubwa katika wa mwanzo. Na wachache katika wa mwisho."

Mtume ﷺ akasema,

«إِنِّي لَأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا رُبْعَ أَهْلِ الْجَنَّةِ، ثَلَاثُ أَهْلِ الْجَنَّةِ، بَلْ أَنْتُمْ نِصْفُ أَهْلِ الْجَنَّةِ - أَوْ: سَطْرُ أَهْلِ الْجَنَّةِ - وَتَقَاسِمُونَهُمُ النِّصْفَ الثَّانِي»

¹ At-Tabari 23:98.

² Fat'h Al-Bari 11:526.

"Mimi natarajja kuwa mtakuwa robo ya watu wa Peponi, theluthi moja ya watu wa Peponi. Bali, nyinyi ni nusu ya watu wa Peponi, na mtagawana nao nusu ya pili."

Imamu Ahmad pia ameinukuu hadithi hii.¹ Hata hivyo, rai hii aliyoichagua Ibn Jarir رحمه الله تعالى ina walakini, bali ni kauli dhaifu. Hayo ni kwa sababu Umati huu ni bora zaidi kuliko umma zote, kwa mujibu wa Qur'an. Kwa hiyo, haiwezekani kwamba waumini wa mbele kutoka katika nyumati zilizotangulia wawe wengi zaidi kuliko wa Umati huu; kinyume chake ndio sahihi. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Kwamba,

ثَلَاثَةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ ﴿٣٩﴾

"Fungu kubwa ni katika watu wa mwanzo..."

Inarejea katika vizazi vilivyotangulia vya Umati huu, wakati Aya,

وَقَلِيلٌ مِنَ الْآخِرِينَ ﴿٤٠﴾

"...Na wachache katika wa mwisho."

Inarejea katika watu wa mwisho katika umati huu.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kuwa As-Sari bin Yahya amesema kuwa Al-Hasan alisoma Aya hii,

وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ ﴿٤١﴾ أُولَئِكَ الْمُقَرَّبُونَ ﴿٤٢﴾ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٤٣﴾ ثَلَاثَةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ ﴿٤٤﴾

"Na wa mbele watakuwa mbele. Hao ndio watakaokaribishwa Katika Bustani zenye neema. Fungu kubwa ni katika watu wa mwanzo."

Akatoa rai, "Kundi kutoka katika kizazi cha mwanzo cha Umati huu." Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى pia amenukuu kuwa Muhammad bin Sirin رحمه الله تعالى amesema kuhusu Aya hii:

ثَلَاثَةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ ﴿٤٤﴾ وَقَلِيلٌ مِنَ الْآخِرِينَ ﴿٤٥﴾

"Fungu kubwa katika watu wa mwanzo. Na wachache katika watu wa mwisho."

"Walikuwa wakisema au kutumaini kuwa wote watakuwa kutoka katika Umati

¹ Ahmad 2:391. Isnadi yake ni dhaifu, kuna Sharik bin Abdillah hifdhi yake sio nzuri.

huu." Basi, hizo ni kauli za Al-Hasan na Ibn Sirin kwamba wale wa mwanzo katika imani, wote ni kutoka katika Umati huu.

Hakuna shaka kuwa vizazi vya mwanzo vya kila umati vilikuwa bora zaidi kuliko vya mwisho. Katika muktadha huu, Aya hii inaweza kujumuisha umma wote wa waumini waliotangulia. Kwa ajili hii, imethibiti katika vitabu vya Hadithi sahihi na vyenginevyo, kutoka katika njia zaidi ya moja, kwamba Mtume ﷺ amesema;

«خَيْرُ الْقُرُونِ قَرْنِي، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ»

"Watu bora ni katika zama zangu, kisha zama ifuatayo, kisha zama inayofuata hao..."¹

Pia amesema:

«لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي ظَاهِرِينَ عَلَى الْحَقِّ، لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَدَلَهُمْ وَلَا مَنْ خَالَفَهُمْ، إِلَى قِيَامِ السَّاعَةِ»

"Kundi katika Umti wangu litaendelea kushindania haki, bila ya kudhuriwa na wenye kuwatelekeza, wala wenye kuwakhaliifu, mpaka Siku ya Kiyama."

Katika Simulizi nyingine:

«حَتَّى يَأْتِيَ أَمْرُ اللَّهِ تَعَالَى وَهُمْ كَذَلِكَ»

"Mpaka Amri ya Allah ifike ilhali wao wakiwa katika hali hiyo."²

Umati huu una utukufu zaidi kuliko umma zote zingine. Waumini wa mwanzo wa Ummah huu ni wengi zaidi na wana daraja ya juu kuliko wa umma zingine, kwa sababu ya nafasi ya dini yao na Mtume wao. Katika Hadithi iliyopokewa na idadi kubwa ya watu "Mutawatir" Mtume ﷺ anataja kuwa watu sabini elfu wa Umati huu wataingia Peponi bila ya hesabu. Katika Simulizi nyingine ya Hadithi hii, Mtume ﷺ ameongeza,

«مَعَ كُلِّ أَلْفٍ سَبْعُونَ أَلْفًا»

"Pamoja na kila elfu moja, kuna elfu sabini nyingine."

¹ Al-Bukhari na. 3651.

² Al-Bukhari na. 71, 3116, 3640, 3641, 7311, 7312, 7459, 7460 na zingine.

Katika simulizi nyingine, amesema,

«مَعَ كُلِّ وَاحِدٍ سَبْعُونَ أَلْفًا»

“Kwa kila mmoja wao kuna wengine elfu sabini.”

Kauli ya Allah تعالى،

عَلَىٰ سُرُرٍ مَّوْضُونَةٍ ﴿٥٦﴾

“**Watakuwa juu ya viti vya fakhari vilivyotonewa.**” Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema, “Vilivyofumwa kwa dhahabu.”¹ Sawa na hayo yamesimuliwa kutoka kwa Mujahidi, ‘Ikrimah, Sa’idi bin Jubayr, Zayd bin Aslam, Qatadah, Adh-Dhahhak na wengine.² Kauli ya Allah تعالى،

مُتَّكِنِينَ عَلَيْهَا مُتَّقِلِينَ ﴿٥٧﴾

“**Wakiviegemea wakielekeana.**” Kwa kuashiria kuwa wataelekeana, na hakuna yeyote katika wao atakayekuwa nyuma,

يَطُوفُ عَلَيْهِمْ وَاْدَانٌ مُّخَلَّدُونَ ﴿٥٨﴾

“**Wakitumikiwa na wavulana wa ujana wa milele,**” Yaani: Watakaodumu katika sifa (hiyo ya ujana) tu, hawatakuwa, hawatazeeka wala kubadilika umbo.

بِأَكْوَابٍ وَأَبَارِيقَ وَكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿٥٩﴾

“**Kwa vikombe na mabirika na bilauri za vinywaji kutoka chemchem safi.**”

Vikombe hivyo havina vishikio au milizamu, wakati mwingine majagi huwa na vishikio na wakati mwingine hayana. Vyote, hata glasi, vitajazwa pombe kutoka katika chemchem itiririkayo, si kutoka katika vyombo vinyoweza kumalizika unapokunywa. Bali, chemchem hiyo ya pombe ni yenye kutiririka tu.

لَّا يُصَدَّعُونَ عَنْهَا وَلَا يُنزِفُونَ ﴿٦٠﴾

“**Hawataumwa kichwa kwa vinywaji hivyo wala hawatoleweshwa.**”

Inamaanisha, kamwe hawataumwa na kichwa kutokana na pombe hiyo wala kulewa. Bali, pombe hiyo haitaathiri akili zao, ingawa itakuwa yenye nguvu

¹ At-Tabari 23:99.

² At-Tabari 23:99, 100.

na ladha tamu sana. Adh-Dhahhak amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema: "Pombe (ya duniani) ina athari nne, inaleweshwa, huleta maumivu ya kichwa, huchochea kutapika na husababisha kukojoa sana. Kwa hivyo Allah تعالى Ametaja pombe ya Peponi kutokuwa na sifa hizi."¹ Mujahid, 'Ikrimah, Sa'id bin Jubayr, 'At iyah Al-'Awfi, Qatadah na As-Suddi wamesema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

لَا يُصَدَّعُونَ عَنْهَا

"Hawataumwa kichwa kwa vinywaji hivyo..." Inamaanisha "Haiwasababishi maumivu ya kichwa."² Wamesema kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا يُزْفُونَ

"...Wala hawatoleweshwa." Inamaanisha kuwa "Haiwaondolei akili."³ Kauli ya Allah تعالى،

وَفَنَكِهِمْ مِمَّا يَتَخِفُّونَ ۚ وَلَحْمٍ طَيْرٍ مِّمَّا يَشْتَبُونَ

"Na matunda wayapendayo, na nyama za ndege kama wanavyo tamani."

Inamaanisha, matunda yoyote wanayotamani watapewa. Aya hii ni ushahidi kuwa tunaruhusiwa kuchagua matunda tunayoyapenda na kuyatamani kula. Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Thabit رضي الله عنه kuwa Anas رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ alikuwa akipenda ndoto. Mtu alipoota ndoto, basi alimuuliza kuhusu ndoto hiyo kama alikuwa mtu haifahamu, na alipenda zaidi kusikiliza ndoto za mtu aliyekuwa akitajwa kwa wema. Mwanamke mmoja alipata kuja kwake na kusema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Niliota kuwa nimepelekwa nje ya Madina na kuingizwa Peponi. Nilisikia kelele iliyoifanya Pepo ilie. Nikaangalia na kumuona fulani na fulani,' na akataja majina ya watu kumi na mbili ambao Mtume ﷺ alikuwa amewatuma katika safari ya kijeshi. Baadaye waliletwa (Peponi, katika ndoto) huku majeraha yao yakivuja damu. Kukasemwa, 'Wapeleke katika mto Baydakh au — Baydhakh.'

Wakapelekwa na kutumbukizwa humo na nyuso zao zikang'aa kama mwezi kamili. Wakaletewa sahani ya dhahabu, iliyokuwa na tende za kijani. Walikula tende nyingi kadiri walivyotaka na kila walipogeuzwa sahani, walikula kila tunda

¹ Al-Qurtubi 17:203. Isnadi yake ina dosari.

² At-Tabari 23:103, 104.

³ At-Tabari 23:104,105.

lililokuwemo, kadiri walivyotaka, na mimi (mwanamke huyo alisema) nilikula pamoja nao." Baadaye, jeshi hilo lilituma mjumbe kufikisha habari (za vita) na kusema kuwa fulani na fulani wameuliwa vitani, huku akitaja majina ya watu kumi na mbili waliotajwa katika ndoto ya mwanamke yule. Kwa hivyo, Mtume ﷺ alimuita tena mwanamke huyo na akamuomba: Asimulie tena ndoto yake. Na yeye akafanya hivyo.

Hii ni simulizi iliyokusanywa na Abu Ya'la¹ na Al-Hafidh Adhi-ya' رحمه الله تعالى amesema, "Hadith hii inafikia vigezo vya Muslim." Kauli ya Allah تعالى,

وَلَحْمٍ طَيْرٍ مِّمَّا يَشْتَبُونَ ﴿٥٦﴾

"Na nyama za ndege kama wanavyotamani."

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Anas رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ طَيْرَ الْجَنَّةِ كَأَمْثَالِ الْبُنْحَبِ، يَرْعَى فِي شَجَرِ الْجَنَّةِ»

"Ndege wa Peponi ni kama "ngamia" aina ya Bukht² walio malishoni katika miti ya Peponi."

Abubakr رضي الله عنه amesema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Kwa hakika, ndege hao lazima watakuwa laini sana." Mtume ﷺ akasema,

«أَكَلَهَا أَنْعَمُ مِنْهَا»

"Wenye kuwala ni laini zaidi."

Alikariri Kauli yake mara tatu. Mtume ﷺ aliendelea,

«وَإِنِّي لَأَرْجُو أَنْ تَكُونَ مِمَّنْ يَأْكُلُ مِنْهَا»

"Na Ninatumaini kuwa utakuwa miongoni mwa watakaowala."³

Imamu Ahmad peke yake ndiye aliikusanya Hadithi hii kwa kutumia isnadi hii. Allah تعالى Amesema;

كَأَمْثَالِ اللَّؤْلُؤِ الْمَكْنُونِ ﴿٥٧﴾

"Walio kama mfano wa lulu ziliohifadhiwa."

¹ Ahmad 3:135, na Musnad Abu Ya'la 6:44.

² Aina ya ngamia wenye shingo ndefu sana. Angalia An-Nihayah.

³ Ahmad 3:221.

Kwa kuashiria kuwa wao ni kama lulu halisi nyeupe. Kauli ya Allah تعالیٰ,

كَأَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَّكْنُونٌ ﴿١٤﴾

“Hao wanawake kama mayai yaliyohifadhika.” (37:49),

Na pia maelezo yao katika Surat Ar-Rahman (sura ya 55). Kwa ajili hiyo, Allah تعالیٰ Amesema baada ya hapo,

جَزَاءٌ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

“Ni malipo kwa waliyokuwa wakiyatenda.”

Inamaanisha, ‘furaha hizo ni malipo ya amali njema walizofanya (duniani). ‘Allah تعالیٰ Amesema,

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْتِيَمًا ﴿١٦﴾ إِلَّا قِيلًا سَلَامًا سَلَامًا ﴿١٧﴾

“Humo hawatasikia porojo wala maneno ya dhambi. Isipokuwa maneno ya Salama na amani.”

Inamaanisha hawatasikia neno la kuchukiza au maneno ya kipuuzi Peponi.

لَا تَسْمَعُ فِيهَا لَغِيَةً ﴿١٨﴾

“Hawatasikia humo upuuzi.” (88:11),

Inamaanisha, hakutasemwa maneno ya kuchukiza humo. Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَلَا تَأْتِيَمًا

“...wala maneno ya dhambi...” Inamaanisha, wala maneno ya kipuuzi,

إِلَّا قِيلًا سَلَامًا سَلَامًا ﴿١٩﴾

“Isipo kuwa maneno ya Salama na amani.”

Watasalimiana kwa Salam, kama Allah تعالیٰ Alivyosema katika Aya nyingine,

تَحِيَّاتُهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ﴿٢٠﴾

“Maamkio yao humo yatakuwa: Salaam! (amani)” (14:23)

Na, kama tulivyotaja, maneno yao yatakuwa mbali na maneno machafu na yale ya kipuuzi.

وَأَصْحَابُ الْيَمِينِ مَا أَصْحَابُ الْيَمِينِ ﴿٧٧﴾ فِي سِدْرٍ مَّخْضُودٍ ﴿٧٨﴾
 وَمَاءٍ مَّنْضُودٍ ﴿٧٩﴾ وَظِلِّ مَمْدُودٍ ﴿٨٠﴾ وَمَاءٍ مَّسْكُوبٍ ﴿٨١﴾
 وَفِكَهَةٍ كَثِيرَةٍ ﴿٨٢﴾ لَا مَقْطُوعَةٍ وَلَا مَمْنُوعَةٍ ﴿٨٣﴾
 وَفُرْشٍ مَّرْفُوعَةٍ ﴿٨٤﴾ إِنَّا أَنْشَأْنَهُمْ إِنْشَاءً ﴿٨٥﴾
 جَعَلْنَهُمْ أَنْبَارًا ﴿٨٦﴾ عُرُبًا أَتْرَابًا ﴿٨٧﴾ لِأَصْحَابِ
 الْيَمِينِ ﴿٨٨﴾ ثَلَاثَةٌ مِنَ الْأُولَىٰ ﴿٨٩﴾ وَثَلَاثَةٌ مِنَ الْآخِرِينَ ﴿٩٠﴾
 وَأَصْحَابُ الشِّمَالِ مَا أَصْحَابُ الشِّمَالِ ﴿٩١﴾ فِي سَمُومٍ ﴿٩٢﴾
 وَخَيْمٍ ﴿٩٣﴾ وَظِلِّ مِّنْ تَحْمُومٍ ﴿٩٤﴾ لَا بَارِدٍ وَلَا كَرِيمٍ ﴿٩٥﴾
 إِنَّهُمْ كَانُوا قَبْلَ ذَلِكَ مُتْرَفِينَ ﴿٩٦﴾ وَكَانُوا يُصِرُّونَ عَلَىٰ
 الْحِنْدِ الْعَظِيمِ ﴿٩٧﴾ وَكَانُوا يَقُولُونَ أَهَذَا مِثْنَا وَكُنَّا
 تُرَابًا وَعِظْمًا أَهْنَا لَمَبْعُوثُونَ ﴿٩٨﴾ أَوْءَابَاؤُنَا الْأُولَىٰ ﴿٩٩﴾
 قُلْ إِنَّ الْأُولَىٰ وَالْآخِرِينَ ﴿١٠٠﴾ لَمَجْبُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ
 يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿١٠١﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ أَيْمَانُ الضَّالِّينَ الْمَكْذِبُونَ ﴿١٠٢﴾
 لَا يَكُلُونَ مِن شَجَرٍ مِّن رَّقُومٍ ﴿١٠٣﴾ فَمَا لِقَوْمِهَا الْبُطُونُ ﴿١٠٤﴾
 فَشَرِبُوا عَلَيْهِ مِنَ الْحَمِيمِ ﴿١٠٥﴾ فَشَرِبُوا شُرْبَ
 أَهْلِيمٍ ﴿١٠٦﴾ هَذَا نُزُّهُمْ يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٠٧﴾

وَأَصْحَابُ الْيَمِينِ مَا أَصْحَابُ الْيَمِينِ
 ﴿٧٧﴾ فِي سِدْرٍ مَّخْضُودٍ ﴿٧٨﴾ وَظِلِّ مَمْدُودٍ ﴿٧٩﴾
 وَمَاءٍ مَّنْضُودٍ ﴿٨٠﴾ وَظِلِّ مَمْدُودٍ ﴿٨١﴾
 وَمَاءٍ مَّسْكُوبٍ ﴿٨٢﴾ وَفِكَهَةٍ كَثِيرَةٍ ﴿٨٣﴾
 لَا مَقْطُوعَةٍ وَلَا مَمْنُوعَةٍ ﴿٨٤﴾
 وَفُرْشٍ مَّرْفُوعَةٍ ﴿٨٥﴾ إِنَّا أَنْشَأْنَهُمْ
 إِنْشَاءً ﴿٨٦﴾ جَعَلْنَهُمْ أَنْبَارًا ﴿٨٧﴾
 لِأَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٨٨﴾ ثَلَاثَةٌ مِنَ
 الْأُولَىٰ ﴿٨٩﴾ وَثَلَاثَةٌ مِنَ
 الْآخِرِينَ ﴿٩٠﴾

27. Na wale wa mkono wa kulia, ni wepi watakuwa wa kuliani?

28. Katika mikunazi isiyo na miba.

29. Na migomba iliyo pangiliwa.

30. Na kivuli cha kudumu kilichotanda.

31. Na maji yanayomiminika.

32. Na matunda mengi.

33. Yasiyokatika wala hayakatazwi.

34. Na matandiko yaliyonyanyuliwa.

35. Hakika Sisi Tumewaumba (Mahurulaini) upya.

36. Na Tutawafanya wanawake bikira.

37. Wanapendana na waume zao, hirimu moja.

38. Kwa ajili ya watu wa kuliani.

39. Fungu kubwa ni katika wa mwanzo.

40. Na fungu kubwa ni katika wa mwisho.

Watu wa Kuliani na Malipo Yao

Allah تعالى Ametaja marejeo ya mwisho kwa walio mbele kwa imani, watu ambao walio karibu Naye zaidi. Akataja mwisho wa watu wa upande wa kulia, miongoni mwa waumini wema. Maymun bin Mihran amesema kuwa wale wa upande wa kulia wana daraja ya chini kuliko wale walio mbele kwa Imani walio karibu zaidi na Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى

وَأَصْحَابُ الْيَمِينِ مَا أَصْحَابُ الْيَمِينِ ﴿٧٧﴾

“Na wale wa mkono wa kulia, ni yepi yatakuwa ya wa kuliani?”

Ni kina nani watu wa upande wa kulia, watakuwa na hali gani na makazi yao yatakuwa yapi. Allah تعالى Anayajibu maswali hayo kwa kusema,

فِي سِدْرٍ مَّخْضُودٍ ﴿٧٨﴾

“Katika mikunazi isiyo na miba.” Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, ‘Ikrimah, Mujahid, Ibn Al-Ahwas, Qasamah bin Zuhayr, As-Safr bin Nusayr, Al-Hasan, Qatadah, ‘Abdullah bin Kathir, As-Suddi, Abu Hazrah na wengine wamesema, “Ni ambayo haina miba.”¹ Na kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: “Ni yenye matunda.” Hayo pia yamesimuliwa kutoka kwa ‘Ikrimah na Mujahid. Ndivyo pia alivyosema Qatadah kama tulivyotaja. Kwa hivyo patakuwa pamejaa matunda yasiyo na miba. Kwa hivyo inaonekana kuwa maana zote zinatumiwa hapa. Mikunazi, ya duniani ina miba na matunda machache sana. Huko Akhera, ni kinyume; haina miba na ina matunda mengi, uzito wake unavuta shina lake. ‘Utbah bin ‘Abd As-Sulami رضي الله عنه amesema, “Nilikuwa nimekaa pamoja na Mtume ﷺ, alipokuja bedui na kusema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Nimekusikia ukitaja mti wa Peponi ambao mimi sijui mti mwingine wenye miba kuliko huo, yaani mti unaoitwa *Talh*.” Mtume ﷺ akasema:

¹ At-Tabari 23:110.

«إِنَّ اللَّهَ يَجْعَلُ مَكَانَ كُلِّ شَوْكَةٍ مِنْهَا تَمْرَةً، مِثْلَ خُصْوَةِ النَّيْسِ الْمَلْبُودِ، فِيهَا سَبْعُونَ لَوْنًا مِنَ الطَّعَامِ، لَا يُشْبِهُ لَوْنًا آخَرَ»

*"Allah Atajaalia tunda kwa kila mahali pa mwiba, mithili ya kondoo dume aliyehasiwa, humo kutakuwa na rangi sabini za chakula, kila moja ikitafautiana na nyingine."*¹

Allah تعالیٰ Amesema,

وَطَلَحٍ مَّنْضُودٍ ﴿٥٦﴾

"Na migomba iliyopangiliwa." Inarejea katika mti mkubwa wenye miba uliokuwepo katika sehemu ya Hijaz (Magharibi mwa Uarabuni). Mujahidi amesema kuwa:

مَّنْضُودٍ

"...iliyopangiliwa." Inamaanisha: "Matunda yake yamebevana juu ya mengine. Allah تعالیٰ Anawakumbusha Makuraishi kuhusu miti ya aina hiyo, kwa kuwa waliitumia kwa kivuli walichokipata kutokana na miti ya aina ya *Talh* na *Sidr*."² Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالیٰ amenukuu kutoka kwa Abu Sa'idi رضي الله عنه amesema kuwa

وَطَلَحٍ مَّنْضُودٍ ﴿٥٦﴾

'Talh Mandhud.' Inamaanisha migomba. Na (Ibn Abi Hatim) amesema, "Simulizi sawa na hii Imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbas, Abu Hurayrah, Al-Hasan, 'Ikrimah, Qasamah bin Zuhayr, Qatadah na Abu Hazrah رضي الله عنهم."³

Mujahid na Ibn Zayd wamesema kadhalika, Ibn Zayd ameongeza, "Watu wa Yemen huuita mgomba kwa jina la *Talh*."⁴

Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ hakutaja maelezo mengine ya neno *Talh*. Kauli ya Allah

تعالیٰ,

وَوَطْلٍ مَّمْدُودٍ ﴿٥٧﴾

"Na kivuli kilichotanda."

¹ *Al-Ba'ith* cha Abi Dawud, Taz. "As-Suhbat" cha Al-Bani:2734, At-Tabarani katika *Al-Awsat* na. 402. Masimulizi sawa na hayo yaliandikwa na Ahmad 4:183 na yanafuata hivi punde, na Ibn Abi 'Asim katika *As-Sunnah* na. 716. Pia angalia *Al-Majma'* na. 18727.

² At-Tabari 23:114.

³ At-Tabari 23:112, 113.

⁴ At-Tabari 23:113.

Al-Bukhari amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ شَجْرَةً يَسِيرُ الرَّابِئُ فِي ظِلِّهَا مِائَةَ عَامٍ لَا يَنْقُطُهَا، أَقْرُوا إِنَّ شَيْئًا: ﴿وَيُظِلُّ تَمْدُورٌ﴾»

*"Peponi, kuna mti ambao mpanda mnyama anaweza kusafiri kwa miaka mia moja chini ya kivuli chake bila ya kukimaliza. Mkitaka, someni: 'Na kivuli kilichotanda.'"*¹

Muslim pia aliikusanya Hadithi hii.² Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ شَجْرَةً يَسِيرُ الرَّابِئُ فِي ظِلِّهَا مِائَةَ عَامٍ، أَقْرُوا إِنَّ شَيْئًا: ﴿وَيُظِلُّ تَمْدُورٌ﴾»

*"Peponi kuna mti wenye kivuli ambacho mpanda mnyama anaweza kusafiri kwa miaka mia moja. Someni mkitaka: "Na kivuli kilicho tanda.""*³

Muslim,⁴ Al-Bukhari⁵ na 'Abdur-Razzaq⁶ waliikusanya Hadithi hii. Kauli ya Allah تعالى،

وَفِيكَهٖ كَثِيرٌ ۖ لَا مَقْطُوعَةٍ وَلَا مَمْنُوعَةٍ ۗ

"Na matunda mengi. Hayatindiki wala hayakatazwi."

Kwa kuashiria kuwa watakuwa na matunda mengi ya aina mbalimbali, ambayo hakuna jicho lililopata kuyaona, hakuna sikio lililopata kusikia na hakuna fikra iliyopata kufikirika, sawa na Kauli ya Allah تعالى،

كُلَّمَا رُزِقُوا مِنْهَا مِنْ ثَمَرَةٍ رِّزْقًا قَالُوا هَذَا الَّذِي رُزِقْنَا مِنْ قَبْلُ وَأُتُوا بِهِ مُتَشَابِهًا

"Kila watapopewa matunda humo, watasema: Haya ndiyo kama tuliyoopewa mbele. Na wataletewa matunda yaliyofanana." (2:25)

¹ Fat'h Al-Bari 8:495.

² Muslim 4:2175.

³ Ahmad 2:482.

⁴ Muslim 4:2175.

⁵ Fat'h Al-Bari 6:368.

⁶ Abdur-Razzaq 11:417.

Umbo litafanana, lakini ladha itakuwa tofauti. Katika Sahihi Mbili, *Sidrat Al-Muntaha* (mti katika mbingu ya saba) umeelezwa hivi:

«فَإِذَا وَرَقُهَا كَأَذَانِ الْفَيْلَةِ، وَنَبْطُهَا مِثْلُ قِلَالِ حَجْرٍ»

“... Tahamaki majani yake yalikuwa kama masikio ya ndovu na mikungu yake ilishabihiana na majagi ya udongo wa Hajar.”¹

Sahihi Mbili pia zilikusanya Hadithi kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, ambaye alisema, “Jua lilipatwa na Mjumbe wa Allah ﷺ akawaongoza watu katika Sala ya kupatwa kwa jua. Wakauliza, ‘Ewe Mjumbe wa Allah, tumekuona ukikifikia kitu wakati wa kusimama (katika Sala), halafu ukasogea nyuma. Akasema:

«إِنِّي رَأَيْتُ الْجَنَّةَ فَتَنَاوَلْتُ مِنْهَا عُقُودًا، وَلَوْ أَخَذْتُهُ لَأَكَلْتُمْ مِنْهُ مَا بَقِيََتِ الدُّنْيَا»

“Niliona Pepo na nikafikia mkungu wa matunda. Kama ningeuchukua, na kula, basi mngekuwa mnakula kutokana na mkungu huo kwa muda wote uliobakia duniani.”²

Imamu Ahmad amenukuu kuwa ‘Utbah bin ‘Abd As-Sulami رضي الله عنه amesema, “Bedui mmoja alikuja kwa Mtume ﷺ na akamuuliza kuhusu *Hawdh*³ na Pepo. Bedui huyo aliuliza, ‘Je Peponi kuna matunda’ Mtume ﷺ akasema,

«نَعَمْ، وَفِيهَا شَجَرَةٌ تُدْعَى طُوبَى»

“Ndiyo, na ndani yake kuna mti unaoitwa *Tuba*.” Akataja kitu ambacho sikikumbuki. Akauliza, ‘Je, unafanana na mti gani wa huku kwetu?’ Mtume ﷺ akasema,

«لَيْسَتْ تُشْبِهُ شَيْئًا مِنْ شَجَرِ أَرْضِكَ»

“Hafanani na mti wowote ulio katika ardhi yako.”

Mtume ﷺ akamuuliza,

«أَتَيْتَ الشَّامَ؟»

“Je, ulishafika Shamu.”

Bedui huyo akajibu: ‘Hapana.’ Mtume ﷺ akasema,

¹ *Fat’h Al-Bari* 6:349, *Muslim* 1:146.

² *Fat’h Al-Bari* 2:627, *Muslim* 2:626.

³ Hodhi ya Mtume ambapo wafuasi wake watakunywa huko Akhera.

«تُشْبِهُ شَجَرَةً بِالشَّامِ تُدْعَى الْجَوْزَةَ، تَنْبُتُ عَلَى سَاقٍ وَاحِدَةٍ، وَيَنْفَرِسُ أَغْلَاهَا»

"Unashabihiana na mti unaomea katika ardhi ya Shamu unaoitwa Al-Jawzah, unaokuwa na shina moja na juu yake kuenea matawi kila mahali."

Bedui huyo aliuliza, 'Mkungu wa matunda yake una ukubwa gani?' Mtume ﷺ akasema,

«مَسِيرَةُ شَهْرِ الْغُرَابِ الْأَبْيَعِ وَلَا يَفْتُرُ»

"Umbali wa kuruka kunguru kwa mwezi mmoja bila ya kupumzika."

Bedui huyo aliuliza, 'Shina lake ni la ukubwa gani?' Mtume ﷺ akasema,

«لَوْ اِرْتَحَلْتُ جَذَعَةً مِنْ اِبِلِ اَهْلِكَ مَا اَحَاطْتُ بِاَطْلِبِهَا، حَتَّى تَنْكَبِرَ تَرْقُوتُهَا هَرَمًا»

"Kama umbali anaoweza kusafiri ngamia jike wa umri wa miaka minne, hataweza kumaliza shina lake isipokuwa mpaka mabega yake yavunjike kwa sababu ya uzee."

Akauliza, 'Je, kuna zabibu?' Mtume ﷺ akaitikia ndiyo. Bedui huyo akauliza, 'Zabibu zina ukubwa gani?' Mtume ﷺ akasema,

«هَلْ ذَبَحَ اَبُوكَ تَيْسًا مِنْ غَنَمِهِ قَطُّ عَظِيمًا؟»

"Je, baba yako amepata kuchinja kondoo dume?"

Bedui akajibu, 'Ndiyo, ' na Mtume ﷺ akamuuliza,

«فَسَلِّحْ اِهَابُهُ فَاَعْطَاهُ اُمُّكَ فَقَالَ: اَتَّخِذِي لَنَا مِنْهُ دَلْوًا؟»

"Akamchuna ngozi yake na ngozi hiyo kumpa mama yako na kumtaka atengenezee ndoo ya maji."

Bedui huyo tena akajibu ndiyo na kusema, 'Zabibu hiyo ingenitosha mimi na familia yangu!.' Mtume ﷺ alikubali na kusema,

«نَعَمْ، وَعَامَّةَ عَشِيرَتِكَ»

"Ndiyo, na pia kwa ukoo wako wote."¹

¹ Ahmad 4:183.

Kauli ya Allah تعالى،

لَا مَقْطُوعَةَ وَلَا مَمْنُوعَةَ ﴿٢٧﴾

“Yasiyokatika wala hayakatazwi,”

Hayakosekani, wakati wa kusi wala kiangazi. Bali, mara zote yapo kwa wenye kutaka kula, daima. Muda wowote matunda hayo yanapohitajika, yanapatikana na kunakuwepo wepesi wa kuyapata kwa uwezo wa Allah تعالى. Qatadah amesema, “Hakuna kitakachowazuia kupata matunda hayo, kwa matawi, miba au umbali.”¹ Tumeshataja Hadithi hapo mwanzo iliyoeleza kuwa mtu akichukua tunda la Peponi, jingine huota mahali pale. Kauli ya Allah تعالى،

وَقُرْشٍ مَّرْفُوعَةٍ ﴿٢٨﴾

“Na matandiko yaliyonyanyuliwa.” Inamaanisha, juu, laini na mazuri. Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّا أَدْنَأْنَهُنَّ إِذْشَاءً ﴿٢٩﴾ فَجَعَلْنَهُنَّ أَبْكَارًا ﴿٣٠﴾ عُرُبًا أَتْرَابًا ﴿٣١﴾ لِأَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٣٢﴾

“Hakika Sisi Tutawaumba (Mahurulaini) upya, na Tutawafanya vijana, Wanapendana na waume zao, hirimu moja. Kwa ajili ya watu wa kuliani.”

Aya hiyo inaeleza kuhusu wanawake watakaokuwa katika vitanda na viti, lakini kwa kuwa vitanda vinaashiria hilo, si kwa kutajwa waziwazi. Ni kama ilivyokuja katika, Kauli ya Allah تعالى kuhusu Sulayman عليه السلام:

إِذْ عُرِضَ عَلَيْهِ بِالْعَشِيِّ الصَّافِرَاتُ الْجِيَادُ ﴿٣٣﴾ فَقَالَ إِنِّي أَحْبَبْتُ حُبَّ الْخَيْرِ عَنْ ذِكْرِ رَبِّي حَتَّى تَوَارَتْ بِالْحِجَابِ ﴿٣٤﴾

“Alipopelekewa jioni farasi wasimamao kidete, tayari kutoka shoti; Basi akasema: Navipenda vitu vizuri kwa kumkumbuka Mola Wangu Mlezi. Kisha wakafichikana nyuma ya boma.” (38:31-32),

Neno “Tawarat” lililo katika Aya hizo linamaanisha kuchwa kwa jua, kwa mujibu wa wanazuoni wengi wa Tafsir. Al-Akhfash amesema kuwa Aya،

إِنَّا أَدْنَأْنَهُنَّ

“Hakika Sisi Tutawaumba...”

¹ At-Tabari 23:118.

Imeashiria wanawali wa Peponi ingawa haikuwataja waziwazi.¹ Abu 'Ubaydah amesema kuwa walishatajwa hapo mwanzo katika Kauli ya Allah تعالى،

وَحُورٌ عِينٌ ﴿٢٧﴾ كَأَمْثَلِ اللَّوْلُؤِ الْمَكْنُونِ ﴿٢٨﴾

“Na Mahurulaini. Walio kama mfano wa lulu ziliohifadhiwa.”²

Kwa hiyo, Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّا أَنْشَأْنَاهُنَّ إِنْشَاءً ﴿٢٩﴾

“Hakika Sisi Tumewaumba...” Inamaanisha, katika maisha mengine, hawa ni wanawake wa duniani watakaolingia peponi, watarudishwa wakiwa vijana wanawari, wakiwa wenye hamu kwa waume zao kwa furaha na bashasha. Abu Dawud At-Tayalisi amenukuu kutoka kwa Anas رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema،

«يُعْطَى الْمُؤْمِنُ فِي الْجَنَّةِ قُوَّةً كَذَا وَكَذَا فِي النِّسَاءِ»

“Peponi, muumini atapewa nguvu kadhaa kwa ajili ya wanawake.”

Anas رضي الله عنه amesema، “Nikauliza، ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Mtu ataweza kufanya hivyo?’ Akasema،

«يُعْطَى قُرَّةَ مَاءَةٍ»

“Atapewa nguvu za “watu” mia moja.”³

At-Tirmidhi pia ameinukuu na kusema، **“Sahih Gharib.”⁴** Abu Al-Qasim At - Tabarani amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ aliulizwa، “Ewe Mtume! Je، tutajamiiana na wake zetu Peponi?” Yeye akasema؛

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيَبْصَلُ فِي الْيَوْمِ إِلَى مِائَةِ عَذْرَاءٍ»

“Mtu ataweza kujamiiana na wanawari mia moja kwa siku moja.”⁵

Al-Hafidh Abu 'Abdullah Al-Maqdisi رحمه الله تعالى amesema، “Kwa maoni yangu، Hadithi hii inafikia vigezo vya Sahih، na Allah تعالى Anajua zaidi.” Kauli ya Allah تعالى،

¹ At-Tabari 23:118.

² At-Tabari 23:118.

³ Musnad At-Tayalis 269.

⁴ Tuhfat Al-Ahwadhi 7:241.

⁵ At-Tabarani katika As-Saghir 2:68.

عُرُبًا

“**Urub**” Sa'id bin Jubayr amesimulia kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما amesema, “Watakuwa katika hali ya kuwapenda waume zao, je, hamkupata kumuona ngamia jike anapokuwa katika joto la kutaka dume?” Basi watakuwa kama hivyo hivyo. Adh-Dhahhak amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما ambaye alisema, “*Urub* ni wenye hamu na waume wao, na waume wao ni wenye kuwapenda.”¹ Maneno sawa na hayo yamesemwa na 'Abdullah bin Sarj, Mujahid, 'Ikrimah, Abu Al-'Aliyah, Yahya bin Abi Kathir, 'Atiyah, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahhak na wengine.² Adh-Dhahhak amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما;

أَتْرَابًا

“**Atrab**.” Inamaanisha “Watakuwa na umri mmoja, miaka thelathini na tatu.”³ Mujahid alisema, “(Umri) sawa...”⁴

Na katika simulizi nyingine, “(Umri wa) kulingana.” 'Atiyah amesema, “Kiulinganifu.” Kauli ya Allah تعالى,

لِّأَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٢٧﴾

“**Kwa ajili ya watu wa kuliani.**” Inamaanisha, wanawake hao waliumbwa, kuhifadhiwa au kuoreshwa kwa wale wa upande wa kulia. Inaonekana kwamba kinachomaanishwa hapa ni kuwa waliumbwa kwa ajili ya wale wa upande wa kulia. Dhahiri ni kwamba itafungamana na Kauli Yake Aliyetukuka,

إِنَّا أَنْشَأْنَهُمْ إِنْشَاءً ﴿٢٦﴾ فَجَعَلْنَهُمْ أُنْكَارًا ﴿٢٧﴾ عُرُبًا أَتْرَابًا ﴿٢٨﴾ لِأَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٢٩﴾

“Hakika Sisi Tutawaumba (Mahurul-aini) upya. Na Tutawafanya vijana. Wanapendana na waume zao, hirimu moja. Kwa ajili ya watu wa kuliani.”

Hii ni rai ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى.⁵ Inawezekana kuwa Kauli ya Allah تعالى,

لِّأَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٢٨﴾

“**Kwa ajili ya watu wa kuliani.**” Inarejea katika maelezo ya kabla yake ambayo ni,

¹ Ad-Dur Al-Manthur 8:16.

² At-Tabari 23:121, 122, 123.

³ Ad-Dur Al-Manthur 8:16.

⁴ At-Tabari 23:24.

⁵ At-Tabari 23:125.

﴿٢٧﴾ لِأَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٢٨﴾

“...hirimu moja. Kwa ajili ya watu wa kuliani.” Inamaanisha, katika umri wao. Al-Bukhari na Muslim wamenukuu kuwa Abu Hurayrah رضى الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«أَوَّلُ زُمْرَةٍ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ عَلَى صُورَةِ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ، وَالَّذِينَ يَلُونَهُمْ عَلَى صُورِهِ أَشَدُّ كَوْنًا دُرِّيًّا فِي السَّمَاءِ إِضَاءَةً، لَا يُبُولُونَ، وَلَا يَتَخَوَّطُونَ، وَلَا يَتَقَلَّبُونَ، وَلَا يَتَمَخَّطُونَ، أَمْشَاطُهُمُ الذَّهَبُ، وَرَشْحُهُمُ الْمِسْكُ، وَمَجَامِرُهُمُ الْأَلْوَةُ، وَأَرْوَاجُهُمُ الْحُورُ الْعَيْنُ، أَخْلَافُهُمْ عَلَى خُلُقِ رَجُلٍ وَاحِدٍ، عَلَى صُورَةِ أَبِيهِمْ آدَمَ، سِتُونَ ذِرَاعًا فِي السَّمَاءِ»

“Kundi la kwanza kuingia Peponi litakuwa liking’aa kama mbalamwezi ya mwezi kamili. Watakaowafuatia watakuwa kama sayari yenye kung’aa sana angani. Hawatajaisaidia haja ndogo, wala kubwa, kutema mate wala kupenga kamasi. Vitana vyao vitakuwa vya dhahabu na majasho yao yatakuwa ya miski; na vitezo vyao vya mshubiri vitatumika. Wake zao watakuwa katika Al-Hur Al- Ayn. Maumbo yao yatafanana na umbo la baba yao ‘Adam, dhira sitini kwenda juu.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

﴿٢٩﴾ ثَلَاثَةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ ﴿٣٠﴾ وَثَلَاثَةٌ مِنَ الْآخِرِينَ ﴿٣١﴾

“Fungu kubwa ni katika wa mwanzo, na fungu kubwa ni katika wa mwisho.”

Inamaanisha kundi la wale wa upande wa kulia litatokana na vizazi vyao vilivyotangulia na kundi kutokana na vizazi vya mwisho litatokana na vizazi vyao. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Abdullah bin Mas`ud رضى الله عنه amesema, “Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ katika usiku mmoja na katika asubuhi iliyofuatia tulimuendea na akasema,

«عُرِضَتْ عَلَيَّ الْأَنْبِيَاءُ وَأَتْبَاعُهَا بِأُمَّمِهَا، فَيَمُرُّ عَلَيَّ النَّبِيُّ، وَالنَّبِيُّ فِي الْعِصَابَةِ، وَالنَّبِيُّ فِي الثَّلَاثَةِ، وَالنَّبِيُّ وَلَيْسَ مَعَهُ أَحَدٌ»

¹ Fath Al-Bari 6:417, Muslim 4:2179

"Baadhi ya Manabii na umma wao walioneshwa kwangu. Kuna Mtume alipita mbele yangu akiwa na kundi la watu, mwingine alikuwa na watu watatu, na mwingine hakuwa na mtu yeyote."

Qatadah, mmoja wa wasimulizi wa Hadithi, akasoma Aya hii,

أَلَيْسَ مِنْكُمْ رَجُلٌ رَشِيدٌ ﴿٥٦﴾

'Hivyo, hamna hata mtu mmoja miongoni mwenu aliyeongoka?'
(11:78)

«حَتَّىٰ مَرَّ عَلَيَّ مُوسَىٰ بْنُ عِمْرَانَ فِي كَنَابَةِ بْنِ إِسْرَائِيلَ»

"Mpaka Musa, mwana wa 'Imran akanipita, akiwa na kundi kubwa katika Wana wa Israel."

Mtume ﷺ akasema;

«قُلْتُ: رَبِّي مَنْ هَذَا؟ قَالَ: هَذَا أَخْرَكَ مُوسَىٰ بْنُ عِمْرَانَ وَمَنْ تَبِعَهُ مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ» قَالَ: «قُلْتُ: رَبُّ قَائِنِ أُمَّتِي؟ قَالَ: انظُرْ عَنْ يَمِينِكَ فِي الطَّرَافِ» قَالَ: «فَإِذَا وُجُوهُ الرِّجَالِ» قَالَ: «قَالَ: أَرْضَيْتَ؟» قَالَ: «قُلْتُ: قَدْ رَضِيتُ رَبًّا». قَالَ: «انظُرْ إِلَى الْأُفُقِ عَنْ يَسَارِكَ، فَإِذَا وُجُوهُ الرِّجَالِ» قَالَ: «أَرْضَيْتَ؟ قُلْتُ: قَدْ رَضِيتُ رَبًّا» قَالَ: «فَإِنَّ مَعَ هَؤُلَاءِ سَبْعِينَ أَلْفًا يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ بِغَيْرِ حِسَابٍ»

"Nikamuuliza Mola Wangu Mlezi, "Huyu ni nani?" Yeye Akasema, "Huyu ni ndugu yako Musa, Mwana wa 'Imran, na waliofuatana naye ni miongoni mwa Wana wa Israel." Nikasema, "Ewe Mola Wangu Mlezi! Uko wapi Umati wangu?" Allah Akasema, "Angalia upande wako wa kulia juu ya kilima." Na nilipoangalia niliona nyuso za watu. Allah Akasema, "Umeridhika?" Nikasema, "Nimeridhika, Ewe Mola Wangu Mlezi." Allah Akasema, "Angalia katika upeo wa macho upande wako wa kushoto." Na nikaona nyuso za watu. Akauliza tena, "Umeridhika?" Nikasema, "Nimeridhika, Ewe Mola Wangu Mlezi" Akasema, "Na pamoja nao watakuwepo wengine sabini elfu watakaingia Peponi bila ya hesabu."

'Ukkashah bin Mihsan رضي الله عنه kutoka kwa Bani Asad, miongoni mwa

walioshiriki katika vita vya Badr, alisema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Niombe kwa Allah تعالى niwe miongoni mwao.' Mtume ﷺ akasema,

«اللَّهُمَّ اجْعَلْهُ مِنْهُمْ»

"Yaa Allah, mjaalie yeye awe miongoni mwao."

Mtu mwingine akasema, 'Ewe Mjumbe wa Allah ﷺ, niombe kwa Allah تعالى na mimi niwe miongoni mwao.' Mtume ﷺ akasema,

«سَبَقَكَ بِهَا عُكَّاشَةُ»

"Ameshakutangulia wewe Ukkashah."

Mtume ﷺ amesema,

«فَإِنْ اسْتَطَعْتُمْ - فِدَاكُمْ أَبِي وَأُمِّي - أَنْ تَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّبْعِينَ فَأَفْعَلُوا، وَإِلَّا فَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ الظَّرَابِ، وَإِلَّا فَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ الْأَفْوَى، فَإِنِّي قَدْ رَأَيْتُ نَاسًا كَثِيرًا قَدْ تَأَسَّبُوا حَوْلَهُ»

"Mkiweza – baba na mama yangu wawe kafara kwa ajili yenu! Jitahidini muwe katika watu hao sabini elfu, au katika makundi ya upande wa kulia, au katika makundi yaliyo katika upeo wa macho, kwa sababu niliona makundi makubwa yaliyokusanyika katika upande huo."

Akaendelea: «إِنِّي لِأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا رُبْعَ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

"Ninatumaini kuwa mtakuwa robo ya watu wa Peponi."

Tukasema, 'Allahu Akbar.' Akasema,

«إِنِّي لِأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا ثُلُثَ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

"Ninatumaini kuwa mtakuwa theluthi ya watu wa Peponi."

Tukasema, 'Allahu Akbar.' Mtume ﷺ akasema,

«إِنِّي لِأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا نِصْفَ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

"Ninatumaini kuwa mtakuwa nusu ya watu wa Peponi, "

Tukasema 'Allahu Akbar.' Mtume ﷻ akasoma Aya hii:

ثَلَاثَةٌ مِنَ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٧﴾ وَثَلَاثَةٌ مِنَ الْآخِرِينَ ﴿٢٨﴾

"Kundi kubwa katika wa mwanzo, na kundi kubwa katika wa mwisho."

Tukaambizana, 'Ni kina nani hao sabini elfu?' Tukasema, 'Ni waliozaliwa katika Uislamu na hawakumshirikisha Allah تعالی na chochote.' Habari hiyo ikamfikia Mtume ﷻ, akasema,

«بَلْ هُمْ الَّذِينَ لَا يَكْتُمُونَ، وَلَا يَسْتَرْفُونَ وَلَا يَتَطَيَّرُونَ، وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ»

"Hao ni watu wasiojitibu kwa kuchoma moto mwilini, wala hawafanyi zinguo, wala hawatizamii kwa mishale, wao ni wenye kumtegemea Mola Wao Mlezi tu."¹

Hadith hii ina isnadi nyingi za simulizi zilizokusanywa katika Sahih na vitabu vingine vya Hadith.²

وَأَصْحَابُ الشِّمَالِ مَا أَصْحَابُ الشِّمَالِ ﴿٢٩﴾ فِي سُمُومٍ وَحَمِيمٍ ﴿٣٠﴾ وَظِلٍّ مِّنْ تَحْتُمُومٍ ﴿٣١﴾ لَا بَارِدٍ وَلَا كَرِيمٍ ﴿٣٢﴾ إِنَّهُمْ كَانُوا قَبْلَ ذَلِكَ مُتْرَفِينَ ﴿٣٣﴾ وَكَانُوا يُصِرُّونَ عَلَىٰ الْحِنثِ الْعَظِيمِ ﴿٣٤﴾ وَكَانُوا يَقُولُونَ أَهَذَا مِثْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظْنَا أَيْنَا لَمَجْعُوثُونَ ﴿٣٥﴾ أَوْءَابَاؤُنَا الْأَوْلُونَ ﴿٣٦﴾ قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ﴿٣٧﴾ لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٣٨﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ أَيْهَا الضَّالُّونَ الْمَكْذِبُونَ ﴿٣٩﴾ لَأَكْلُونَ مِنْ شَجَرٍ مِّنْ زُقُومٍ ﴿٤٠﴾ فَمَا لُونُ مِنهَا الْبَطُونُ ﴿٤١﴾ فَشَرِبُوا عَلَيْهِ مِنَ الْحَمِيمِ ﴿٤٢﴾ فَشَرِبُوا شَرِبَ أَهْلِيمٍ ﴿٤٣﴾ هَذَا نُزُّهُم يَوْمَ الدِّينِ ﴿٤٤﴾

41. Na watu wa kushotoni; je ni yepi ya wa kushotoni?

42. Katika upepo wa moto, na maji yanayochemka.

43. Na kivuli cha moshi mweusi.

¹ Al-Hakim 4:577.

² Fat'h Al-Bari 10:164, 224, 11:312, 413, na Muslim 1:198, 199, Tuhfat Al-Ahwadhi 7:139, na Ahmad 1:401.

44. *Si cha kuburudisha wala kustarehesha.*
45. *Hakika hao walikuwa kabla ya haya wakiishi maisha ya anasa.*
46. *Na walikuwa wakishikilia kufanya madhambi makubwa.*
47. *Na walikuwa wakisema: Tutakapokufa na tukawa udongo na mifupa, ati ndio tutafufuliwa?*
48. *Au baba zetu wa zamani?*
49. *Sema: Hakika wa kwanza na wa mwisho*
50. *Bila ya shaka watakusanywa kwa wakati wa siku maalumu.*
51. *Kisha nyinyi, mliopotea, mnaokanusha,*
52. *Kwa yakini mtakula mti wa Zaqqumu.*
53. *Na kwa mti huo mtajaza matumbo.*
54. *Na juu yake mtakunywa maji yanayochemka.*
55. *Tena mtakunywa kama wanavyokunywa ngamia wenye kiu.*
56. *Hiyo ndiyo karamu yao Siku ya Malipo.*

Hali za Watu wa Upande wa Kushoto na Malipo Yao

Baada ya Allah تعالى kutaja hali za watu wa upande wa kulia, akafuatisha kutaja hali za watu wa upande wa kushoto,

وَأَصْحَابُ الشِّمَالِ مَا أَصْحَابُ الشِّمَالِ ﴿٥٦﴾

“Na watu wa kushotoni; Vipi hali ya watu wa kushotoni?”

Inamaanisha, ‘Ni ipi hali ya walio upande wa kushoto.’ Kisha Anaeleza Kauli Yake, kwa Kusema,

فِي سَمُومٍ

“Katika upepo wa moto...” Inamaanisha upepo mkali mno wa moto.

وَحَمِيمٍ

“...na maji yanayochemka...” Maana yake: Ya moto vikali mno.

وْظِلِّ مِّنْ تَحْمُومٍ ﴿٢٧﴾

“Na kivuli cha moshi mweusi.” Kivuli cha moshi, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas ,¹ Mujahid, `Ikrimah, Abu Salih, Qatadah, As-Suddi na wengine رضي الله عنهم.² Katika kauli inayofanana, Allah تعالى Amesema,

أَنْطَلِقُوا إِلَىٰ مَا كُنْتُمْ بِهِ تَكْدِبُونَ ﴿٢٧﴾ أَنْطَلِقُوا إِلَىٰ ظِلِّ ذِي ثَلَاثِ شُعَبٍ ﴿٢٨﴾ لَا ظَلِيلٍ وَلَا يُغْنِي مِنَ الْآلِهَبِ ﴿٢٩﴾ إِنَّهَا تَرْمِي بِشَرِّ كَالْقَاصِرِ ﴿٣٠﴾ كَأَنَّهُ جَمَلٌ صُفْرٌ ﴿٣١﴾ وَبَلْ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٢﴾

“Nendeni kwenye adhabu mliyokuwa mkiikanusha! Nendeni kwenye kivuli chenye mapande matatu! Hakikingi moto, wala hakiwaepushi na mwako. Hakika Moto huo unatoa cheche kama majumba! Kama kwamba ni ngamia wa rangi ya manjano! Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!” (77:29-34).

Kauli ya Allah تعالى katika Aya hii,

وْظِلِّ مِّنْ تَحْمُومٍ ﴿٢٧﴾

“Na kivuli cha yahmum (moshi mweusi).” Inamaanisha, moshi mweusi,

لَا بَارِدٍ وَلَا كَرِيمٍ ﴿٣٢﴾

“Si cha kuburudisha wala kustarehesha.”

Inamaanisha hakina hewa nzuri wala mwonekano mzuri. Al-Hasan na Qatadah wameeleza juu ya Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا كَرِيمٍ

“...wala kustarehesha.” “Hauna mandhari mazuri.”³ Adh-Dhahhak amesema, “Kila kinywaji kisicho cha kukata kiu, si Karimu (yaani si kizuri).”⁴

Kisha, Allah تعالى Alisema kuwa wanastahiki mwisho huo.

¹ At-Tabari 23:129.

² At-Tabari 23:129, 130.

³ At-Tabari 23:131.

⁴ At-Tabari 23:131.

إِنِّهْمْ كَانُوا قَبْلَ ذَلِكَ مُتْرَفِينَ ﴿٥٦﴾

“Hakika hao walikuwa kabla ya haya wakiishi maisha ya anasa.” Inamaanisha, duniani, walikuwa wakifurahia anasa za kidunia na kupuuza waliyoletewa na Mitume.

وَكَانُوا يُصْرُونَ

“Na walikuwa wakishikilia...” Inamaanisha waling'ang'ania na hawakutaka kutubu.

عَلَىٰ الْحِنْتِ الْعَظِيمِ

“...kufanya madhambi makubwa.” Katika kumkufuru Allah تعالى na kuyafanya masanamu na washindani kuwa miungu badala ya Allah تعالى.

Inamaanisha ushirikina, kwa mujibu wa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما. Hayo yamesemwa pia na Mujahid, 'Ikrimah, Adh-Dhahhak, Qatadah, As-Suddi na wengine.¹ Kauli ya Allah تعالى

وَكَانُوا يَقُولُونَ ﴿٥٧﴾ أَيُّدَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظْمًا أَيُّنَا لَمَبْعُوثُونَ ﴿٥٨﴾ أَوْءَابَاؤُنَا الْآوَّلُونَ ﴿٥٩﴾

‘Na walikuwa wakisema: Tutakapokufa na tukawa udongo na mifupa, ati ndio tutafufuliwa? Au baba zetu wa zamani?’

Walisema hayo huku wakikanusha fikra kuwa ufufuo huo utatokea. Allah تعالى Amesema,

قُلْ إِنَّ الْآوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ﴿٦٠﴾ لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٦١﴾

“Sema: Hakika wa zamani na wa mwisho bila ya shaka watakusanywa kwa wakati na siku maalumu.”

Inamaanisha, ‘Sema, Ewe Muhammad, vizazi vya mwanzo na vilivyokuja baada yao vya wana wa Adam vitakusanywa katika Siku ya Kiyama na hakuna katika wao atakayeachwa.” Allah تعالى Amesema:

ذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّجْمُوعٌ لَّهُ النَّاسُ وَذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّشْهُودٌ ﴿٦٢﴾ وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مَّعْدُودٍ ﴿٦٣﴾

يَوْمَ يَأْتِ لَا تَكَلِّمُ نَفْسٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ فَمِنْهُمْ شَقِيٌّ وَسَعِيدٌ ﴿٦٤﴾

¹ At-Tabari 23:132.

“Hiyo ndiyo Siku itakayokusanyiwa watu, na hiyo ndiyo Siku itakayoshuhudiwa. Na Sisi Hatuiakhirishi ila kwa muda unao hisabiwa. Siku hiyo itakapofika, hatosema hata mtu yeyote ila kwa idhini Yake Mwenyezi Mungu. Kati yao watakuwamo waliomo mashakani na wenye furaha.” (11:103-105)

Kwa kuzingatia hilo Amesema hapa,

لَمَجْبُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿١٠٣﴾

“Bila ya shaka watakusanywa kwa wakati na siku maalumu.”

Kwa sababu wakati huo umeshapangwa na hautawahi wala kuchelewa, wala kuongezeka wala kupungua. Kauli ya Allah تعالى ,

ثُمَّ إِنَّكُمْ أَيُّهَا الضَّالُّونَ الْمُكَذِّبُونَ ﴿١٠٤﴾ لَأَكِلُونَ مِن شَجَرٍ مِّن زُقُومٍ ﴿١٠٥﴾ فَمَا لِعُونَ مِثْمَا
الْبُطُونِ ﴿١٠٦﴾

“Kisha nyinyi, mliopotea, mnaokanusha, kwa yakini mtakula mti wa Zaqqumu. Na kwa mti huo mtajaza matumbo.”

Kwa kuashiria kuwa watakamatwa na watalazimishwa wanywe kutokana na mti unaoitwa Zaqqum mpaka matumbo yao yajae,

فَشَرِبُونَ شُرْبَ الْهَيْمِرِ ﴿١٠٧﴾ هَذَا نُزُّهُم يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٠٨﴾

“Tena mtakunywa kama wanavyokunywa ngamia wenye kiu. Hiyo ndiyo karamu yao Siku ya Malipo.”

Hamim ni maji yanayochemka, wakati *Al-Him* inamaanisha kiu cha ngamia, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهم, Mujahid, Sa’id bin Jubayr na ‘Ikrimah.¹ As-Suddi amesema “*Al-Him* ni ugonjwa unaowapata ngamia, kwa kuwasababishia kupata kiu, na wanakunywa maji bila ya kiu kukatika mpaka wanakufa.” Kwa hiyo, amesema, watu wa Jahanamu, kamwe kiu chao hakitakatika kwa kunywa *Hamim*. Allah تعالى Amesema,

هَذَا نُزُّهُم يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٠٩﴾

“Hiyo ndiyo karamu yao Siku ya Malipo.”

¹ At-Tabari 23:136.

'Haya ndiyo tuliyoeleza, ndivyo watakavyokaribishwa kwa Mola Wao Mlezi Siku ya Hesabu yao.' Allah تعالى Amesema kuhusu waumini,

﴿١٧﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَانَتْ لَهُمْ جَنَّاتُ الْفِرْدَوْسِ نُزُلًا

“Hakika wale walioamini na wakatenda mema mashukio yao yatakuwa kwenye Pepo za Firdausi.” (18:107),

Maana yake: Watakirimiwa na kutukuzwa.

* * *

حٰنْ خَلَقْنٰكُمْ فَلَوْلَا تُصَدِّقُونَ ﴿٥٧﴾ اَفَرءَيْتُمْ مَا تُمْنُونَ
 حٰنْ قَدَرْنَا مَحْلُوقَهُۥٓ اَمْ نَحْنُ الْخٰلِقُونَ ﴿٥٨﴾ حٰنْ قَدَرْنَا
 بَيْنَكُمْ الْمَوْتَ وَمَا حٰنْ بِمَسْبُوقِينَ ﴿٥٩﴾ عَلٰٓى اَنْ يُبَدَّلَ
 اَمْثَلَكُمْ وُنُسِيفِكُمْ فِى مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٠﴾ وَّلَقَدْ عَلِمْتُمْ
 الْنَّشَاةَ الْاٰوَلٰى فَلَوْلَا تَذْكُرُونَ ﴿٦١﴾ اَفَرءَيْتُمْ مَا تَحْرُثُونَ
 ﴿٦٢﴾ اَفَاَنْتُمْ تَزْرَعُونَهُۥٓ اَمْ حٰنْ الْزَّارِعُونَ ﴿٦٣﴾ لَوْ نَشَاءُ
 لَجَعَلْنٰهُ حُطْبًا فَظَلْتُمْ تَفَكِّهُونَ ﴿٦٤﴾ اِنَّا لَمُغْرَمُونَ ﴿٦٥﴾
 بَلْ حٰنْ مَحْرُومُونَ ﴿٦٦﴾ اَفَرءَيْتُمُ الْمَآءَ الَّذِى تَشْرَبُونَ ﴿٦٧﴾
 اَفَاَنْتُمْ اَنْزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمَزْنِ اَمْ حٰنْ الْمُنزِلُونَ ﴿٦٨﴾ لَوْ نَشَاءُ
 جَعَلْنٰهُ اُجَاجًا فَلَوْلَا تَشْكُرُونَ ﴿٦٩﴾ اَفَرءَيْتُمُ النَّارَ الَّتِى
 تُورُونَ ﴿٧٠﴾ اَفَاَنْتُمْ اَنْشَأْتُمْ شَجَرَتَهَا اَمْ حٰنُ الْمُنشِئُونَ
 ﴿٧١﴾ حٰنْ جَعَلْنٰهَا تَذْكِرَةً وَمَتَعًا لِّلْمُقْوِينَ ﴿٧٢﴾ فَسَبِّحْ
 بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٧٣﴾

حٰنْ خَلَقْنٰكُمْ فَلَوْلَا تُصَدِّقُونَ ﴿٥٧﴾
 اَفَرءَيْتُمْ مَا تُمْنُونَ ﴿٥٨﴾ اَفَاَنْتُمْ
 مَحْلُوقَهُۥٓ اَمْ نَحْنُ الْخٰلِقُونَ ﴿٥٩﴾
 حٰنْ قَدَرْنَا بَيْنَكُمْ الْمَوْتَ وَمَا حٰنْ
 بِمَسْبُوقِينَ ﴿٦٠﴾ عَلٰٓى اَنْ يُبَدَّلَ
 اَمْثَلَكُمْ وُنُسِيفِكُمْ فِى مَا لَا تَعْلَمُونَ
 ﴿٦١﴾ وَّلَقَدْ عَلِمْتُمْ الْنَّشَاةَ الْاٰوَلٰى
 فَلَوْلَا تَذْكُرُونَ ﴿٦٢﴾

57. Sisi Tumekuumbeni;
basi hamsadiki?

58. Je! Mnaiona mbegu ya
uzazi mnayomimina?

59. Je! Mnaiumba nyinyi,
au ni Sisi ndio Waumbaji?

60. Sisi Tumekuwekeeni
mauti; na wala Sisi
Hatushindwi

61. Kuwaleta wengine badala yenu na Kukuumbeni nyinyi kwa umbo msilolijua.

62. Na bila ya shaka mlikwishajua umbo la kwanza, basi kwa nini hamkumbuki?

Ushahidi kwamba Kiyama Kitatokea na Hoja za Kuwepo Ufufuo

Allah تعالى Anasema kuwa Ufufuo utakuwepo na Anawakanusha wapotofu wampingao wale wanaosema,

أَيُّدَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظْمًا أَءِنَّا لَمَبْعُوثُونَ

“Tutakapokufa na tukawa udongo na mifupa, ati ndio tutafufuliwa?” 56:47

Kauli yao katika kukataa na kukadhibisha Ufufuo ni kuona kwao kuwa jambo hilo haliwezekani. Allah تعالى Amesema,

نَحْنُ خَلَقْنَاكُمْ

“Sisi Tumekuumbeni...” Inamaanisha, ‘Tumekuumbeni baada ya kutokuwepo kwenu. Kwa hiyo, je, Aliyeanzisha Uumbaji, si Ndiye Mwenye Uweza zaidi wa Kuurudishia.’ Kauli ya Allah تعالى,

فَلَوْلَا تُصَدِّقُونَ

“...basi hamsadiki?” ‘Kwa nini basi hamuamini Ufufuo?’ Kisha Allah تعالى Akasema, ilhali Akiwapa ushahidi kuwa Ufufuo upo,

أَفَرَأَيْتُمْ مَا تُمْنُونَ ﴿٥٦﴾ ءَأَنْتُمْ تَخْلُقُونَهُ أَمْ نَحْنُ الْخَالِقُونَ ﴿٥٧﴾

“Je! Mnaiona mbegu ya uzazi mnayoimimina? Je! Mnaiumba nyinyi, au ni Sisi ndio Waumbaji?”

Inamaanisha, ‘Je, nyinyi ndio mnaobakisha mbegu za uzazi matumboni na kuumba uhai kutokea humo, hatua baada ya hatua au ni Allah تعالى Ndiye Mwenye Kuyafanya hayo.’ Kauli ya Allah تعالى ,

نَحْنُ قَدَّرْنَا بَيْنَكُمُ الْمَوْتَ

“Sisi Tumekuwekeeni mauti...” Inamaanisha, ‘Tumefanya kuwe na kifo kati yenu.’ Adh-Dhahhak ametoa rai, “Allah تعالى Aliwafanya watu wa mbinguni na ardhini wawe sawa kuhusu kifo.”¹ Kauli ya Allah تعالى ,

¹ Al-Qurtubi 17:216.

وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوبِينَ

"...na wala Sisi hatushindwi." Inamaanisha, 'Kamwe Hatushindwi,'

عَلَىٰ أَنْ نُبَدِّلَ أَمْثَلَكُمْ

'**Kuwaleta wengine badala yenu...**' Inamaanisha, 'kubadili umbo lenu la sasa, Siku ya Kiyama.'

وَنُشِئَكُمْ فِي مَا لَا تَعْلَمُونَ

"...na Kukuumbeni nyinyi kwa umbo msilolijua." Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ النَّشْأَةَ الْأُولَىٰ فَلَوْلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٥٧﴾

"**Na bila ya shaka mlilwisha jua umbo la kwanza, basi kwa nini hamkumbuki?"**

Inamaanisha, 'mnajua kuwa Allah تعالى Amekuumbeni baada ya kutokuwepo kwenu. Amekuumbeni na Kukupeni masikio, macho na nyoyo. Basi hamkumbuki na kuzingatia kuwa Mwenye Kuweza Kukuumbeni tangu mwanzoni ni mwenye uwezo mkubwa wa Kukurejesheni na Kukufufueni katika uhai mpya.' Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ﴿٥٨﴾

"**Na Yeye Ndiye Anayeanzisha uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake.**" (30:27), Na,

أَوَلَا يَذْكُرُ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ قَبْلُ وَلَمْ يَكُ شَيْئًا ﴿٥٩﴾

"**Je! Hakumbuki mwanaadamu ya kwamba Tulimuumba kabla, na hali hakuwa chochote?"** (19:67),

أَوَلَمْ يَرِ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُّبِينٌ ﴿٦٠﴾ وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٦١﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ وَهُوَ

بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٦٢﴾

"**Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi Tumemuumba yeye kutokana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa ndiye mgomvi wa dhaahiri! na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa**

kwake, akasema: Ni nani huyo atakayeihisha mifupa nayo imekwishamung'unyika? Sema: Ataihuisha huyo huyo Aliyeiumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila Uumbaji.”(36:77-79), Kadhalika Allah تعالى Amesema;

أَحْسَبُ الْإِنْسَانَ أَنْ يُتْرَكَ سُدًى ﴿٦٦﴾ أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِنْ مَنِيِّ يَمِينِي ﴿٦٧﴾ ثُمَّ كَانَ عَلَقَةً
فَخَلَقَ فَسَوَّى ﴿٦٨﴾ فَعَمَلَ مِنْهُ الذَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَى ﴿٦٩﴾ أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَى أَنْ
تُحْيِيَ الْمَوْتَى ﴿٧٠﴾

“Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure? Kwani hakuwa yeye tone la manii lilioshushwa? Akawa kidonge cha damu, tena Mwenyezi Mungu Akamuumba na Akamtengeneza vilivyo. Akamfanya namna mbili, mwanamume na mwanamke. Je! Huyo hakuwa ni Muweza wa Kufufua wafu?” (75:36-40)

أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَحْرُثُونَ ﴿٦١﴾ ءَأَنْتُمْ تَزْرَعُونَهُ أَمْ نَحْنُ الذَّارِعُونَ ﴿٦٢﴾ لَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَاهُ
حُطْبًا فَظَلْتُمْ تَفَكَّهُونَ ﴿٦٣﴾ إِنَّا لَمُعْرِمُونَ ﴿٦٤﴾ بَلْ نَحْنُ مُحْرِمُونَ ﴿٦٥﴾ أَفَرَأَيْتُمْ الْمَاءَ
الَّذِي تَشْرَبُونَ ﴿٦٦﴾ ءَأَنْتُمْ أَنْزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمُزْنِ أَمْ نَحْنُ الْمُنزِلُونَ ﴿٦٧﴾ لَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَاهُ
أُجَاجًا فَلَوْلَا تَشْكُرُونَ ﴿٦٨﴾ أَفَرَأَيْتُمْ النَّارَ الَّتِي تُورُونَ ﴿٦٩﴾ ءَأَنْتُمْ أَنْشَأْتُمْ شَجَرَتَهَا أَمْ
نَحْنُ الْمَنْشُؤُونَ ﴿٧٠﴾ نَحْنُ جَعَلْنَاهَا تَذَكُّرًا وَرَمْتَنَا لِلْمُقَوِّينَ ﴿٧١﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ
الْعَظِيمِ ﴿٧٢﴾

63. Je! Mnaona mbegu mnayopanda?

64. Je! Ni nyinyi mnayoiotesha au ni Sisi ndio wenye kuotesha?

65. Tungelitaka Tungeliiyafanya kuwa mapepe, mkabaki mnastaajabu,

66. Mkisema: Hakika sisi tumegharimika.

67. Bali sisi tumenyimwa.

68. Je! Mnayaona maji mnayoyanywa?

69. Je! Ni nyinyi mnayoyateremsha kutoka mawinguni au ni Sisi Ndio Wenye Kuyateremsha?

70. Tungelipenda Tungeliyafanya ya chumvi. Basi mbona hamshukuru?

71. Je! Mnaona moto mnaouwasha?

72. Ni nyinyi mliouumba mti wake au Sisi ndio Waumbaji?

73. Sisi Tumeufanya uwe ni ukumbusho na manufaa kwa walioko nyikani.

74. Basi litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye Mkuu.

Utanabahishwaji wa Upweke wa Allah تعالى Unadhihirishwa na Yeye Kuotesha Mimea, Kuteremsha Mvua na Kuumba Moto ambao Mwanadamu Anauhitaji

Allah تعالى Amesema,

أَفْرَأَيْتُمْ مَا تَحْرُثُونَ ﴿٥٧﴾

“Je! Mnaona mbegu mnayoipanda?” Inakusudiwa kulima na kupanda mbegu ardhini.

ءَأَنْتُمْ تَزْرَعُونَهُۥٓ

“Je! Ni nyinyi mnaoioatesha...” “Je nyinyi ndio mnaosababisha mbegu iote ardhini.

أَمْ نَحْنُ الَّذِينَ نَزْرَعُونَ

“...Au ni Sisi ndio wenye kuotesha?” Allah تعالى Anasema, ‘Bali ni Sisi ndio tunaosababisha mbegu ibakie nzima na kumea ardhini.’

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا تَقُولَنَّ: زَرَعْتُ وَلَكِن قُلْ: حَرَثْتُ»

“Msiseme, “Zara’tu (nimeotesha), bali semeni, “Harathtu, (nimepanda).”

Abu Hurayrah رضي الله عنه akaongeza, “Je, hujasikia Kauli ya Allah تعالى,

أَفْرَأَيْتُمْ مَا تَحْرُثُونَ ﴿٥٧﴾ ءَأَنْتُمْ تَزْرَعُونَهُۥٓ أَمْ نَحْنُ الَّذِينَ نَزْرَعُونَ ﴿٥٨﴾

“Je! Mnaona mbegu mnayoipanda? Je! Ni nyinyi mnaoioatesha au ni Sisi ndio wenye Kuotesha?”¹

¹ At-Tabari 23:139.

Allah تعالیٰ Amesema,

لَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَاهُ حُطْبًا

“Tungelitaka Tungeliifanya ikawa mapepe.”

Inamaanisha, ‘Tumeotesha mbegu kwa Rehema Zetu na Kuiacha ardhini kwa ajili ya rehema kwenu. Tukitaka, Tutazigeuza ziwe kavu kabla ya kukomaa na kuwa tayari kuvunwa,’

فَظَلُّنَا تَفَكَّهُونَ

“...mkabaki mnastaajabu,”

Allah تعالیٰ Ameerleza Kauli Yake kwa Kusema,

إِنَّا لَمُعْرَمُونَ ﴿٦٦﴾ بَلْ نَحْنُ مَحْرُومُونَ ﴿٦٧﴾

“Mkisema: Hakika sisi tumegharimika; Bali sisi tumenyimwa.”

Allah تعالیٰ Anasema, ‘kama Tutameng’enya mimea ikawa mabua makavu, mtakuwa mnastaajabia kilichotokea, wakati mwingine kwa kusema: Sisi kwa hakika ni *Mughramun*, yaani, tumegharimika. ‘Mujahid na ‘Ikrimah wamesema kuwa *Mughramun* maana yake tumelipiziwa kisasi.¹ Qatadah amesema, “Mngesema, `Tumeadhibiwa, ‘wakati mwingine, na, `Tumenyimwa,’ kwa nyakati zingine.”² ‘Ikrimah amesema kuwa ‘Mtakuwa *Tafakkahun*’ Inamaanisha ‘Mtalaumiana (wenyewe).”³ au, kusikitika, kwa mujibu wa Al-Hasan, Qatadah na As-Suddi.⁴ Watakuwa wakihuzunikia walichotumia au madhambi waliyoyatenda siku za nyuma yaliyosababisha kuangamiza mimea yao.

Al-Kisa’i amesema, “*Tafakkaha*” Ni neno lenye maana mbili zinazokinzana.” Waarabu husema *Tafakkahtu* wanapomaanisha kuwa wameneemeka na jambo au wamepata huzuni. Kisha Allah تعالیٰ Akasema tena,

أَفَرَأَيْتُمُ الْمَاءَ الَّذِي تَشْرَبُونَ ﴿٦٨﴾ ءَأَنْتُمْ أَنْزَلْتُمُوهُ مِنَ السَّمَاءِ

“Je! Hamyaoni maji mnayokunywa? Je! Ni nyinyi mnayoyateremsha kutoka mawinguni...”

¹ At-Tabari 23:141.

² At-Tabari 23:141.

³ At-Tabari 23:140.

⁴ At-Tabari 23:140.

Inamaanisha, mawingu, kwa mujibu wa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na wengine.¹ Kauli ya Allah تعالى،

أَمْ نَحْنُ الْمُنزِلُونَ

"...au ni Sisi ndio wenye kuyateremsha?"

Allah تعالى Anaeleza kuwa kwa hakika Yeye Ndiye Mwenye Kuleta mvua.

لَوْ نَشَاءُ جَعَلْنَاهُ أُجَاجًا

"Tungelipenda Tungeliyafanya ya chumvi." Inamaanisha ya chumvi, machungu, yasiyonyweka na yasiyofaa kwa ajili ya mimea,

فَلَوْلَا تَشْكُرُونَ

"Basi mbona hamshukuru?"

Kwa nini hamshukuru neema za Allah تعالى Alizokupeni kwa Kuwaletea mvua nzuri, yenye maji yaliyo tayari kutumika.

لَكُمْ مِنْهُ شَرَابٌ وَمِنْهُ شَجَرٌ فِيهِ تُسِيمُونَ ﴿١٠﴾ يُنْبِتُ لَكُمْ بِهِ الزَّرْعَ وَالزَّيْتُونَ
وَالنَّخِيلَ وَالْأَعْنَبَ وَمِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١١﴾

"...Katika hayo nyinyi mnapata ya kunywa, na miti ya kulishia. Kwa hayo Yeye Anaizalisha kwa ajili yenu mimea, na mizaituni, na mitende, na mizabibu, na kila namna ya matunda. Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanaofikiri." (16:10-11)

Kisha Allah تعالى Akasema;

أَفَرَأَيْتُمُ النَّارَ الَّتِي تُؤْتُونَ

"Je! Hamuoni moto mnaouwasha?"

'Maana yake: Mnaowasha kwa kutumia mti.

ءَأَنْتُمْ أَنْشَأْتُمْ شَجَرَتَهَا أَمْ نَحْنُ الْمُنشِئُونَ ﴿١٧﴾

"Ni nyinyi mliouumba mti wake au Sisi ndio Waumbaji?"

¹ At-Tabari 23:143.

Maana yake: 'Tumejalia uwashaji moto uwezekane.' Waarabu walikuwa na aina mbili za miti iliyoitwa *Al-Markh* na *Al-Afar* (waliyoitumia kuwashia moto). Walipokuwa wakipikicha tawi la kijani katika jingine la miti hiyo miwili, cheche zilikuwa zikitoka humo. Kauli ya Allah تعالى ,

لَحْنٌ جَعَلْنَاهَا تَذْكَرَةً

"Sisi Tumeufanya uwe ni ukumbusho..." Yaani wa ule Moto wa Jahanmu, kwa mujibu wa Mujahid na Qatadah.¹ Qatadah amesema, "Tuliambiwa kuwa Mtume ﷺ amesema,

«يَا قَوْمِ نَارُكُمْ هَذِهِ الَّتِي تُوقَدُونَ، جُزْءٌ مِنْ سَبْعِينَ جُزْءًا مِنْ نَارِ جَهَنَّمَ»

"Enyi watu, moto wenu huu ambao mnaouwasha, ni sehemu moja tu kati ya sehemu sabini za moto wa Jahanamu."

Wakasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Moto huu peke yake una joto kali la kutosha." Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّهَا قَدْ ضُرِبَتْ [بِالْمَاءِ] - أَوْ مَرَّتَيْنِ - حَتَّى يَسْتَنْفَعَ بِهَا بَنُو آدَمَ وَيَذْنُوا مِنْهَا»

*"Ulizamishwa katika maji mara mbili ili wana wa 'Adam wanufaika nao na kuusogelea."*²

Simulizi hii ni kutoka kwa Qatadah ambayo ni *Mursal*, ilinukuliwa na Imamu Ahmad رضي الله عنه katika Musnad wake kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ;

«إِنَّ نَارَكُمْ هَذِهِ جُزْءٌ مِنْ سَبْعِينَ جُزْءًا مِنْ نَارِ جَهَنَّمَ، وَضُرِبَتْ بِالْبَحْرِ مَرَّتَيْنِ، وَلَوْلَا ذَلِكَ مَا جَعَلَ اللَّهُ فِيهَا مَتَفَعَةً لِأَحَدٍ»

*"Kwa hakika, moto wenu huu ni sehemu moja kati ya sabini ya moto wa Jahanamu. Na Umetoswa mara mbili baharini, isingekuwa hivyo, Allah Asingefanya uwe na manufaa kwa yeyote."*³

Imamu Malik رحمه الله تعالى pia amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ At-Tabari 23:144.

² At-Tabari 23:144.

³ Ahmad 2:244.

«نَارُ بَيْبِ آدَمَ الَّتِي يُوقَدُونَ، جُزْءٌ مِنْ سَبْعِينَ جُزْءًا مِنْ نَارِ جَهَنَّمَ»

“Moto wa wana wa ‘Adam wanaoukoka ni sehemu moja kati ya sabini za moto wa Jahanamu.”

Wakasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Moto huu pekee una joto la kutosha kabisa.” Yeye akasema,

«إِنَّهَا قَدْ فَضَلَتْ عَلَيْهَا بِتِسْعَةِ وَسِتِّينَ جُزْءًا»

“Moto wa Jahanamu ulizidishwa joto mara sitini na tisa zaidi.”¹

Al-Bukhari aliikusanya Hadithi hii kutoka kwa Imamu Malik na Muslim kutoka kwa Abu Az-Zinad.² Kauli ya Allah تعالى،

وَمَتَّعًا لِّلْمُقْوِينَ

“...na manufaa kwa wale wasafiri.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما، Mujahid, Qatadah, Adh-Dhahhak na An-Nadr bin ‘Arabi amesema, “Maana ya *Al-Muqwin* ni wasafiri.”³ Hii pia aliichagua Ibn Jarir رحمه الله تعالى na kusema, “Kutokea humo imekuja kauli *Aqwat Ad-Dar* (nyumba imekuwa tupu), pindi watu wake wanaposafiri.”⁴ ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam amesema kuwa hapa *Al-Muqwi* inamaanisha njaa. Layth bin Abi Sulaym amesimulia kuwa Mujahid amesema kuhusu Ayah hiyo,

وَمَتَّعًا لِّلْمُقْوِينَ

“...na manufaa kwa wasafiri.”

“Kwa walio majumbani mwao na wale wasafiri, kwa ajili ya kila aina ya chakula kinachohitajika kupikwa kwa moto.” Ibn Abi Najih pia amesimulia kuwa Mujahid amesema, “kwa ajili ya *Muqwin*, inamaanisha watu wote wanaofurahia kula chakula kilichoivishwa kwa moto.”⁵ Sawa na hayo yametajwa kutoka kwa

¹ *Al-Mu’awana* 2:994.

² *Fat’h Al-Bari* 6:380, Muslim 4:2184.

³ At-Tabari 23:145.

⁴ At-Tabari 23:146.

⁵ At-Tabari 23:145.

'Ikrimah, na maelezo haya ni ya ujumla zaidi kuliko yaliyotangulia, kwa kuwa wale walio katika maeneo yao na wanaosafiri, ima tajiri au maskini, wote wana haja ya moto kwa ajili ya kupika, kupata joto na kupata mwanagaza. Kisha ni katika ukarimu wa Allah تعالی kuwa Amefanya sifa ya kuwasha moto katika baadhi ya vitu, kama mawe, wanayoweza kutumia watu kuchukua katika mizigo katika safari zao. Msafiri anapohitaji moto kambini mwake ili kupika au kupata joto, anatoa vitu hivyo na kuvitumia katika kuwashia moto. Anafarijika karibu na moto na anaweza kuutumia kwa haja mbalimbali alizo nazo. Allah تعالی Anataja neema hii mahususi katika hali ya wasafiri, ingawa kila mmoja ananufaika na moto. Kauli ya Allah تعالی,

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٥٧﴾

“Basi litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye Mkuu.”

Inamaanisha, Yule Ambaye kwa Uwezo Wake Ameumba vitu hivyo. Ameumba maji mazuri yaondoayo kiu, na Angetaka, Angeyaumba yawe na chumvi kama ya baharini. Pia Ameumba moto unaounguza, na Amejaalia manufaa kutokana nao kwa ajili ya waja wake na Akaufanya moto kuwa ni wenye kufaa kwa ajili ya maisha yao ya duniani na kama onyo la adhabu kwao huko Akhera.

* * *

* فَلَا أُقْسِمُ بِمَوَاقِعِ النُّجُومِ ﴿٧٥﴾ وَإِنَّهُ لَقَسَمٌ لَوْ
تَعْلَمُونَ عَظِيمٌ ﴿٧٦﴾ إِنَّهُ لَقُرْءَانٌ كَرِيمٌ ﴿٧٧﴾ فِي كِتَابٍ
مَكْنُونٍ ﴿٧٨﴾ لَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ ﴿٧٩﴾ تَنْزِيلٌ مِّنْ
رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٨٠﴾ أَفَبِعَذَابِنَا أَسْفَهْتُمْ أَأَنْتُمْ مَّدْهُونُونَ ﴿٨١﴾
وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَنْتُمْ تُكذِّبُونَ ﴿٨٢﴾ فَلَوْلَا إِذَا بَلَغَتِ
الْحُلُقُومَ ﴿٨٣﴾ وَأَنْتُمْ حِينِيذٍ تَنْظُرُونَ ﴿٨٤﴾ وَحَنْ أَقْرَبُ
إِلَيْهِ مِنْكُمْ وَلَيْكِن لَّا تُبْصِرُونَ ﴿٨٥﴾ فَلَوْلَا إِنْ كُنْتُمْ غَيْرَ
مَدِينِينَ ﴿٨٦﴾ تَرْجِعُونَهَا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٨٧﴾ فَأَمَّا إِنْ
كَانَ مِنَ الْمُقْرَبِينَ ﴿٨٨﴾ فَرُوحٌ وَرِيحَانٌ وَجَنَّتْ نَعِيمٍ ﴿٨٩﴾
وَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنَ أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٩٠﴾ فَسَلَامٌ لَّكَ مِنَ
أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٩١﴾ وَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنَ الْمُكذِّبِينَ الضَّالِّينَ ﴿٩٢﴾
﴿٩٣﴾ فَتُزَلُّ مِنْ حَمِيمٍ ﴿٩٤﴾ وَتَصْلِيَةٌ حَمِيمٍ ﴿٩٥﴾ إِنْ هَذَا
هُوَ حَقُّ الْيَقِينِ ﴿٩٦﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٩٧﴾

* فَلَا أُقْسِمُ بِمَوَاقِعِ النُّجُومِ ﴿٧٥﴾
وَإِنَّهُ لَقَسَمٌ لَوْ تَعْلَمُونَ عَظِيمٌ ﴿٧٦﴾
إِنَّهُ لَقُرْءَانٌ كَرِيمٌ ﴿٧٧﴾ فِي كِتَابٍ
مَكْنُونٍ ﴿٧٨﴾ لَا يَمَسُّهُ إِلَّا
الْمُطَهَّرُونَ ﴿٧٩﴾ تَنْزِيلٌ مِّنْ رَّبِّ
الْعَالَمِينَ ﴿٨٠﴾ أَفَبِعَذَابِنَا أَسْفَهْتُمْ
أَنْتُمْ مَّدْهُونُونَ ﴿٨١﴾ وَتَجْعَلُونَ
رِزْقَكُمْ ﴿٨٢﴾ وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ
أَنْتُمْ تُكذِّبُونَ ﴿٨٣﴾

75. Basi naapa kwa kuchwa kwa nyota.

76. Na hakika bila ya shaka hiki ni kiapo kikubwa, laiti mngeli jua!

77. Hakika hii bila ya shaka ni Qur'ani Tukufu.

78. Katika Kitabu kilichohifadhiwa.

79. Hapana akigusaye ila waliotakaswa.

80. Ni uteremsho unaotoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.

81. Je, ni hii Qur'an mnayoipinga na kuikanusha?

82. Na mnafanya shukrani ya riziki zenu ndio kumkadhibisha Aliye Kuumbeni na Kukuruzukuni?

Kuapa kwa Allah تعالى juu ya Utukufu wa Qur'an

Matumizi ya *La* (katika *Fala*) si herufi ya ziada isiyo na maana, kama baadhi ya wanazuoni wa *Tafsir* wanavyosema. Bali hutumika mwanzoni mwa kiapo kinapokuwa cha kukanusha. Hayo ni sawa na wakati mama A'ishah رضي الله عنها aliposema, "La naapa kwa Allah تعالى! Mkono wa Mtume ﷺ hakupata kumgusa mwanamke yeyote hata kidogo."¹

Kwa hivyo kwa msemu huu, maana yake ni, "Hapana! Naapa kwa maanguko ya nyota. Jambo hilo haliko kama mnavyodai - kuhusu Qur'an – kuwa ni matokeo ya uchawi au ulozi, bali ni Qur'an Tukufu." Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema, "Baadhi ya wanazuoni wa lugha ya Kiarabu wamesema kuwa maana ya:

فَلَا أُقْسِمُ

"Basi naapa..."

Na, 'Jambo hilo haliko kama mnavyodai.' Halafu, anasisitiza kiapo kwa kusema, 'Ninaapa.'²

فَلَا أُقْسِمُ بِمَوَاقِعِ النُّجُومِ ﴿٧٥﴾

"Basi naapa kwa maanguko ya nyota."

Mujahd amesema, "Mahali pa machweo ya nyota mbinguni," Na amesema kuwa inarejea katika sehemu za kuchomoza na kuchwa.³ Hayo yalisemwa na Al-Hasan, Qatadah na yamechaguliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.⁴ Qatadah pia amesema kuwa inamaanisha sehemu zao.⁵ Kauli ya Allah تعالى,

وَإِنَّهُمْ لَقَسِمٌ لَوْ تَعْلَمُونَ عَظِيمٌ ﴿٧٦﴾

"Na hakika bila ya shaka hiki ni kiapo kikubwa, laiti mngelijua!"

Kwa maana, 'hiki ni kiapo kikubwa kwa mimi kuapa - kama nyinyi mnaujua ukubwa wa kiapo hiki, mtaujua ukubwa wa lililoapiwa."

¹ *Fat'h Al-bari* 8:504.

² At-Tabari 23:147.

³ At-Tabari 23:148.

⁴ At-Tabari 23:148.

⁵ At-Tabari 23:148.

إِنَّهُ لَقُرْآنٌ كَرِيمٌ ﴿٧٦﴾

“Hakika hii bila ya shaka ni Qur’ani Tukufu.”

Maana yake: Qur’an hii aliyoteremshiwa Muhammad ﷺ ni Kitabu Kitukufu,

فِي كِتَابٍ مَّكْنُونٍ ﴿٧٧﴾

“Katika Kitabu kilichohifadhiwa.”

Kwa maana kitukufu; kutoka Kitabu Kitukufu, Kilichohifadhiwa vyema. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Isma’il bin Musa amesema kuwa Sharik amesimulia kutoka kwa Hakim, ambaye ni Ibn Jubayr, kutoka kwa Sa’id bin Jubayr, kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuhusu:

لَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْأَمْطَهُرُونَ ﴿٧٨﴾

“Hapana akigusaye ila waliotakaswa.”

Amesema, “Ni kile Kitabu kilichopo mbinguni.”¹ Al-`Awfi amesimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuhusu:

لَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْأَمْطَهُرُونَ ﴿٧٩﴾

“Hapana akigusaye ila waliotakaswa.”

Kwamba maana ya ‘waliotakaswa’ ni “Malaika.”² Sawa na hayo yalisemwa na Anas, Mujahid, ‘Ikrimah, Sa’id bin Jubayr, Adh-Dhahhak, Abu Ash-Sha` tha’, Jabir bin Zayd, Abu Nahik, As-Suddi, ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam na wengine.³

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Ibn ‘Abdul-A’la amesema kuwa Ibn Thawr amesema kuwa Ma’mar amesema kutoka kwa Qatadah kuhusu:

لَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْأَمْطَهُرُونَ ﴿٨٠﴾

“Hapana akigusaye ila waliotakaswa.”

¹ At-Tabari 23:149.

² At-Tabari 23:150.

³ At-Tabari 23:150, 151, na Al-Qurtubi 17:235.

Kwamba, "Hakuna anayeweza kukigusa, kwa Allah تعالی, isipokuwa waliotakasika. Hata hivyo, duniani, Majusi na wanafiki wasiotakasika hukigusa." Na amesema, "Katika usomaji wa Ibn Mas'ud رضي الله عنه ni: "Hapana akigusaye ila waliotakaswa."¹ Abu Al-'Aliyah amesema:

(مَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ)

"Hawakigusi ila waliotakaswa."

"Haijakukusudieni nyinyi, kwa sababu nyinyi ni watenda dhambi!"² Ibn Zayd amesema, "Makafiri wa Kikuraishi walidai kuwa mashetani waliteremsha Qur'an. Allah تعالی Alisema kuwa waliotakasika tu ndio wenye kugusa Qur'an, kama ilivyosemwa:

وَمَا تَزَلَتْ بِهِ الشَّيْطَانُ ﴿٦٦﴾ وَمَا يُبَغِي هُمْ وَمَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٦٧﴾ إِنَّهُمْ عَنِ السَّمْعِ
لَمَعَزُولُونَ ﴿٦٨﴾

"Wala Mashet'ani hawakuteremka nayo, wala haitakiwi kwao, na wala hawawezi. Hakika hao wametengwa na kusikia." (26:210-212)"³

Kauli hii ni nzuri, na haikinzani na yale ya kabla yake. Kauli ya Allah تعالی,

تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٩﴾

"Ni uteremsho unaotoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote."

Inamaanisha hii Qur'an ni ufunuo kutoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote na vyote vilivyomo. Si kama wanavyosema kuwa ni uchawi, ulozi au ushairi, bali ni ukweli, bila ya shaka hakuna ukweli unaoizidi. Kauli ya Allah تعالی,

أَفَبِعَذَابِنَا أَتَىٰكُمُ الْمُرْسَلُونَ ﴿٧٠﴾

"Je, ni hii Qur'an mnayoipinga na kuikanusha?"

¹ At-Tabari 23:152.

² At-Tabari 23:151.

³ At-Tabari 23:149 kutoka kwa Adh-Dhahhak.

Al-Awf amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa neno *Mud'hinun* linamaanisha "Hamuiamini na mnaikataa."¹

Mithili ya hayo yalisemwa na Adh-Dhahhak, Abu Hazrah na As-Suddi.² Mujahid amesema,

مُدْهِنُونَ

"...mnayoipinga na kuikanusha?"

Inamaanisha "Mnataka kujijaza kwayo na kuitegemea."³

وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَنْتُمْ تُكذِّبُونَ

"Na mnafanya shukrani ya riziki zenu ndio kumkadhibisha Aliye Kuumbeni na Kukuruzukuni?"

Baadhi yao wamesema kuwa riziki hapa maana yake ni shukrani, yaani: mnakanusha bila ya shukrani. 'Ali bin Abi Talhah amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa aliisoma Aya hiyo kama ifuatavyo:-

(وَتَجْعَلُونَ شُكْرَكُمْ أَنْتُمْ تُكذِّبُونَ)

"Halafu badala ya kushukuru, nyinyi mnakadhibisha!"⁴

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Muhammad bin Bashshar, ambaye alisimulia kutoka kwa Muhammad bin Ja'far, ambaye alisimulia kutoka kwa Shu'bah, kutoka kwa Abu Bishr, kutoka kwa Sa'id bin Jubayr ambaye alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما amesema, "Kamwe watu hawakupelekewa mvua isipokuwa baadhi yao walikufuru na kusema, 'Nafasi fulani ya nyota imeleta mvua!'" Na Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisoma:

(وَتَجْعَلُونَ شُكْرَكُمْ أَنْتُمْ تُكذِّبُونَ)

"Halafu badala ya kushukuru, nyinyi mnakadhibisha!"⁵

¹ At-Tabari 23:153.

² At-Tabari 23:153.

³ At-Tabari 23:153.

⁴ At-Tabari 23:154, 155.

⁵ At-Tabari 23:154.

Isnadi hii ni Sahih kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما. Katika Muwatta' yake, Malik amesimulia kutoka kwa Salih bin Kaysan, kutoka kwa 'Ubaydullah bin 'Abdullah bin 'Utbah bin Mas'ud, kutoka kwa Zayd bin Khalid Al-Juhani ambaye alisema, "Mtume ﷺ alituingoza katika Sala ya Subh huko Al-Hudaybiyah baada ya usiku uliokuwa wenye mvua. Baada ya kukamilisha Sala hiyo, aliwageukia watu na kusema:

«هَلْ تَذُرُونَ مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ؟»

"Je, mnajua alichokisema Mola Wenu Mlezi."

Waliokuwepo wakajibu, 'Allah na Mjumbe Wake wanajua zaidi.' Yeye Akasema,

«قَالَ: أَصْبَحَ مِنْ عِبَادِي مُؤْمِنٌ بِي وَكَافِرٌ، فَأَمَّا مَنْ قَالَ: مُطِرْنَا بِمُضَلِّ اللَّهِ وَرَحْمَتِهِ، فَذَلِكَ مُؤْمِنٌ بِي، كَافِرٌ بِالْكَوْثَبِ، وَأَمَّا مَنْ قَالَ: مُطِرْنَا بِنَوْءِ كَذَا وَكَذَا، فَذَلِكَ كَافِرٌ بِي وَمُؤْمِنٌ بِالْكَوْثَبِ»

"Allah Amesema, "Waja wamepambazuka wakiwa kuna mwenye Kuniadini na mwenye Kunikufukuru. Yeyote aliyesema kuwa mvua imenysha kwa sababu ya baraka na Rehema za Allah, ameniadini, na amekataa nyota; na yeyote aliyesema kuwa mvua imenysha kwa sababu ya nyota fulani, Hakuniadini, bali anaamini nyota."¹

Hadith hii imenukuliwa katika Sahihi Mbili, Abu Daud na An-Nasa'i, wote kwa kutumia isnadi ya simulizi ya Imamu Malik رحمه الله تعالى.²

Qatadah amesema, "Al-Hasan alikuwa akisema, 'Baadhi ya watu wamejiletea shari kubwa wao wenyewe, kwa kukikanusha Kitabu cha Allah تعالى" Kauli ya Al-Hasan inamaanisha kuwa watu wa aina hiyo hawajanufaika na Kitabu cha Allah تعالى kwa sababu wamekikanusha, kama Alivyosema Allah تعالى:

أَفِيهِذَا الْحَدِيثِ أَنْتُمْ مُدْهِنُونَ ﴿٥٦﴾ وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَنْكُمْ تَكْتَدِبُونَ ﴿٥٧﴾

"Je, ni hii Qur'an mnayoipinga na kuikanusha? Na mnafanya shukrani ya riziki zenu ndio kumkadhibisha Aliye Kuumbeni na Kukuruzukuni?"

¹ Al-Muwatta' 192.

² Fat'h Al-Bari 2:388, Muslim 1:83, Abu Dawud 4:227, An-Nasai 3:165.

فَلَوْلَا إِذَا بَلَغَتِ الْحُلُقُومَ ﴿٥٦﴾ وَأَنْتُمْ حِينِيذٍ تَنْظُرُونَ ﴿٥٧﴾ وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْكُمْ وَلَكِنْ
لَّا تُبْصِرُونَ ﴿٥٨﴾ فَلَوْلَا إِنْ كُنْتُمْ غَيْرَ مَدِينِينَ ﴿٥٩﴾ تَرْجِعُونَهَا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٦٠﴾

83. Basi ni pale roho inapofika Kooni.

84. Na nyinyi wakati huo mnatazama!

85. Na Sisi Tuko karibu zaidi naye kuliko nyinyi lakini hamuoni.

86. Na lau kuwa nyinyi hamumo katika mamlaka Yangu.

87. Kwanini hamuirudishi hiyo roho, ikiwa nyinyi mnasema kweli?

Hakuna Awezaye Kuizuiya Roho Pindi Inapotolewa, na Huu ni Uthibitisho Kuwa Hesabu Itakuwepo

Allah تعالی Amesema,

فَلَوْلَا إِذَا بَلَغَتِ

"Basi si pale Roho inapofika..." Maana yake: Katika kuizungumzia roho wakati mtu anapokufa.

الْحُلُقُومِ

"...Kooni." Maana yake: Wakati mtu anapokufa. Allah تعالی Amesema katika Aya nyingine,

كَلَّا إِذَا بَلَغَتِ التَّرَاقِيَ ﴿٦١﴾ وَقِيلَ مَنْ رَاقٍ ﴿٦٢﴾ وَظَنَّ أَنَّهُ الْفِرَاقُ ﴿٦٣﴾ وَالْتَفَتِ إِلَى أُولَئِكَ بِالرِّسَاقِ ﴿٦٤﴾ إِلَى رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمَسَاقِيُّ ﴿٦٥﴾

"La, hashu! (Roho) itakapofikia kwenye mifupa ya koo, Na pakasemwa: Nani wa kumganga? Na mwenyewe akajua kwa hakika kuwa huko ndiko kufariki; Na utapoambatishwa muundi kwa muundi, siku hiyo ndiyo kuchungwa kupelekwa kwa Mola Wako Mlezi!" (75:26-30)

Kauli ya Allah تعالی hapa,

وَأَنْتُمْ حِينِيذٍ تَنْظُرُونَ ﴿٦٦﴾

"Na nyinyi wakati huo mnatazama!" Maana yake: Mtu anayefariki na kushuhudia mzubao wa mauti unaompata.

وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْكُمْ

“Na Sisi Tuko karibu zaidi naye kuliko nyinyi.” Kwa maana ya Malaika.

وَلَيْكِن لَّا تُبْصِرُونَ

“...lakini hamuoni...”. Hamuezi kuwaona Malaika. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَهُوَ الْغَافِرُ فَوقَ عِبَادِهِ ۗ وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ حَفَظَةً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَكُمْ الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ
رُسُلُنَا وَهُمْ لَا يُفَرِّطُونَ ﴿٦١﴾ ثُمَّ رُدُّوْا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقِّ ۗ أَلَا لَهُ الْحُكْمُ وَهُوَ أَسْرَعُ
الْحَسْبِ ۗ ﴿٦٢﴾

“Naye Ndiye Mwenye Nguvu za Kushinda, Aliye juu ya waja Wake. Na Hukupelekeeni waangalizi, mpaka mmoja wenu yakimjia mauti wajumbe Wetu humfisha, nao hawafanyi taksiri. Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola Wao wa Haki. Hakika, Hukumu ni Yake. Naye ni Mwepesi kuliko wote wanaohisabu.”
(6:61-62)

Kauli ya Allah تعالى,

فَلَوْلَا إِنْ كُنْتُمْ غَيْرَ مَدِينِينَ ﴿٦١﴾ تَرْجِعُونَهَا

“Na lau kuwa nyinyi hamumo katika Mamlaka Yangu, kwa nini hamuirudishi hiyo roho.”

Kwa maana ‘Hamuirudishi roho iliyofika Kooni, irudi mwilini mwake ili asife, kama nyinyi hamtapata hesabu na malipo.’ Sa’id bin Jubayr na Al-Hasan Al-Basri wamesema:

فَلَوْلَا إِنْ كُنْتُمْ غَيْرَ مَدِينِينَ ﴿٦١﴾

“Na lau kuwa nyinyi hamumo katika Mamlaka Yangu.”

“Maana yake: Kama hamuamini kuwa mtahesabiwa, kulipwa, kufufuliwa na kuadhibiwa, basi kwa nini hamuirudishi roho hiyo mwilini mwake.” Mujahid amesema kuwa,

غَيْرَ مَدِينِينَ

“...hamumo katika Mamlaka Yangu...” Maana yake: “Kama nyinyi mna hakika kwamba hamtafufuliwa.”

فَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنَ الْمُقْرَبِينَ ﴿٨٨﴾ فَرَوْحٌ وَرَيْحَانٌ وَجَنَّتْ نَعِيمٍ ﴿٨٩﴾ وَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنْ أَصْحَابِ
 الْيَمِينِ ﴿٩٠﴾ فَسَلَامٌ لَكَ مِنْ أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٩١﴾ وَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنَ الْمُكْذِبِينَ الضَّالِّينَ ﴿٩٢﴾
 فَتُزَلُّ مِنْ حَمِيمٍ ﴿٩٣﴾ وَتَصْلِيَةٌ حَمِيمٍ ﴿٩٤﴾ إِنَّ هَذَا هُوَ حَقُّ الْيَقِينِ ﴿٩٥﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ
 الْعَظِيمِ ﴿٩٦﴾

88. Basi akiwa miongoni mwa waliokaribishwa.

89. Basi ni raha, na manukato, na Bustani zenye neema.

90. Na akiwa katika watu wa upande wa kulia.

91. Basi ni Salamu kwako uliye miongoni mwa watu wa upande wa kulia.

92. Na ama akiwa katika waliokadhibisha wapotovu.

93. Basi karamu yake ni maji yanayochemka.

94. Na kutiwa Motoni.

95. Hakika hii ndiyo haki yenye yakini.

96. Basi litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye Mkubwa.

Hali za Watu Wakati wa Kufa Kwao

Kuna hali za aina tatu ambazo watu hukabiliana nazo wakati wa kufa kwao. Ama wewe ni miongoni mwa waumini wa karibu au wa chini ya daraja hilo katika upande wa kulia, au waliokataa ukweli na wapakotea mbali uongofu na hawakumjua Allah تعالی. Kauli ya Allah تعالی,

فَأَمَّا إِنْ كَانَ

“Basi akiwa...” Maana yake: Mtu anayekaribia kufa,

مِنَ الْمُقْرَبِينَ

“...miongoni mwa waliokaribishwa.” Aliyetimiza majukumu na matendo yaliyopendekezwa ya ibada na akaepuka yaliyokatazwa na kuchukia mambo, hata baadhi ya yaliyoruhusiwa.

﴿٥٦﴾ فَرَّوْحٌ وَرَيْحَانٌ وَجَنَّتْ نَعِيمٌ

“Basi Kwake ni raha, na manukato, na Bustani zenye neema.”

Watakuwa na *Rawh* na *Rayhan*; na habari njema za sifa hizo watafikishiwa na Malaika wakati wa kifo. Tulishatangulia kutaja Hadithi ya Mtume ﷺ iliyosimuliwa kutoka kwa Al-Bara' ambamo malaika wa rehema husema (kumuambia anayefariki),

«أَبْتَهَا الرُّوحُ الطَّيِّبُ فِي الْجَسَدِ الطَّيِّبِ كُنْتَ تَعْمُرِيتهُ، أَخْرَجِي إِلَى رَوْحٍ وَرَيْحَانٍ
وَرَبُّ غَيْرِ غَضْبَانَ»

“Ewe roho nzuri katika mwili mzuri ulimokuwemo, njoo katika Raha na Manukato na Mola Mlezi Ambaye Hajaghadhibika.”¹

‘Ali bin Abi Talhah amesimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, “*Rawh* inamaanisha kupumzika,² na *Rayhan* inamaanisha mahali pa kupumzikia.” Mujahid amesema sawa na hivyo kuwa *Rawh* inamaanisha kupumzika.³ Abu Hazrah amesema kuwa *Rawh* inamaanisha: “Kupumzika kusikokuwa duniani.” Sa’id bin Jubayr na As-Suddi amesema kuwa inamaanisha kufurahi. Na kutoka kwa Mujahid:

فَرَّوْحٌ وَرَيْحَانٌ

“...Basi kwako ni raha, na manukato...” Maana yake ni: “Pepo na furaha.” Qatadah amesema kuwa *Rawh* inamaanisha rehema. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na Sa’id ibin Jubayr amesema kuwa *Rayhan* inamaanisha riziki. Maana zote hizo ni sahihi na zinakubalika katika maana. Waumini wa karibu wanaofariki watayapata yote hayo; rehema, kupumzika, riziki, furaha, na starehe.

وَجَنَّتْ نَعِيمٌ

“...na Bustani zenye neema.” Abu Al-‘Aliyah amesema, “Hakuna katika waumini wa karibu atakayeondoka (duniani) mpaka kwanza aletewe tawi la *Rayhan* kutoka Peponi na roho yake kukamatwa humo.”⁴ Muhammad bin Ka’b amesema, “Kila mtu anayekufa atajua wakati wa kifo chake kama yeye ni

¹ At-*Tiwal* na. 238. Masimulizi sawa na hayo yamenukuliwa na Abu Dawud na wengine.

² At-Tabari 23:159.

³ At-Tabari 23:160.

⁴ At-Tabari 23:160.

katika watu wa Peponi au wa Motoni." Katika Sahih, kumenukuliwa kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ أَرْوَاحَ الشَّهَدَاءِ فِي حَوَاصِلِ طُيُورِ خُضْرٍ، تَشْرَحُ فِي رِيَاضِ الْجَنَّةِ حَيْثُ شَاءَتْ، ثُمَّ تَأْوِي إِلَى قَنَادِيلَ مُعَلَّقَةٍ بِالْعَرْشِ»

"Roho za waliokufa shahidi zinaishi katika viwiliwili vya ndege wa kijani wanaruka popote wanapotaka katika bustani za Peponi, halafu wanapumzika katika viota vyao katika mashada ya mataa yenye kuning'inia katika Kiti cha Enzi."¹ Isome hadi mwisho.

Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'Ata' bin as-Sa'ib amesema, "Siku ya kwanza nilipomuona 'Abdur-Rahman bin Abi Layla, nilimuona mzee aliyekuwa na nywele zilizogeuka mvi kichwani na kidevuni. Alikuwa akiendesha punda nyuma ya jeneza. Nilimsikia akisema, 'Fulani alinisinulia kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«مَنْ أَحَبَّ لِقَاءَ اللَّهِ أَحَبَّ اللَّهُ لِقَاءَهُ، وَمَنْ كَرِهَ لِقَاءَ اللَّهِ كَرِهَ اللَّهُ لِقَاءَهُ»

"Mwenye kupenda kukutana na Allah, Allah Anapenda Kukutana naye, na anayechukia Kukutana na Allah, Allah Anachukia Kukutana naye."

Watu waliokuwa karibu yake walianza kulia, na akawauliza kwa nini walikuwa wanalia. Wakasema, 'Sote hatupendi kufa.' Yeye akasema,

«لَيْسَ ذَلِكَ، وَلَكِنَّهُ إِذَا اخْتَضِرَ ﴿فَلَمَّا إِنْ كَانَ مِنَ الْمُقْرَبِينَ ﴿٨٨﴾ فَرُوحٌ وَرِيحَانٌ وَحَنَّتْ نَعِيرٌ ﴿فَإِذَا بُشِّرَ بِذَلِكَ أَحَبَّ لِقَاءَ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ، وَاللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ لِلِقَائِهِ أَحَبُّ ﴿وَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنَ الْمُكَذِّبِينَ الضَّالِّينَ ﴿٩٢﴾ فَزُلَّ مِنْ حِمِيرٍ ﴿٩٢﴾ وَتَصَلِيَةُ حِمِيرٍ ﴿فَإِذَا بُشِّرَ بِذَلِكَ كَرِهَ لِقَاءَ اللَّهِ، وَاللَّهُ تَعَالَى لِلِقَائِهِ أَكْرَهُ»

*"Hiyo si maana yake. Bali ni pale mtu anapofikiwa na kifo: **Basi ni raha, na manukato, na Bustani zenye neema.**" Na habari hizi njema zinafikishwa kwake, atapenda kukutana na Allah Mtukufu. Naye Allah Mtukufu Anapenda zaidi Kukutana naye, **'Na ama akiwa katika waliokadhibisha wapotovu, Basi karamu yake ni maji yanayochemka. Na kutiwa Motoni.'** Akifikishiwa habari hizo, atachukia kukutana na Allah na Allah Naye pia Anachukia zaidi Kukutana naye."²*

¹ Muslim 3:1502.

² Ahmad 4:259.

Hii ni simulizi aliyokusanya Imam Ahmad; na katika Sahih, kuna Hadithi yenye kushuhudia maana yake. Imenukuliwa kutoka kwa mama A'ishah رضي الله عنها.¹ Kauli ya Allah تعالى،

وَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنْ أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٧٦﴾

“Na akiwa katika watu wa upande wa kulia.”

Maana yake: Kama huyo anayekufa ni miongoni mwa watu wa upande wa kulia.

فَسَلِّمْ لَكَ مِنْ أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٧٧﴾

“Basi ni Salamu kwako uliye miongoni mwa watu wa upande wa kulia.”

Inamaanisha, malaika watawafikishia habari njema kwa kuwaambia, “Amani iwe juu yenu,” Yaani, muwe watulivu, mtapelekwa katika mahali salama, nyinyi ni miongoni mwa walio katika upande wa kulia, ‘Ikrimah amesema, “Malaika watawasalimia kwa Salam na kuwafikishia habari kuwa yeye ni miongoni mwa walio katika upande wa kulia.” Maana hii ni nzuri, na inaendana na Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا
وَأَبْشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٧٨﴾ نَحْنُ أَوْلِيَاؤُكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ
وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَشْتَهُونَ أَنْفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدْعُونَ ﴿٧٩﴾ نُزُلًا مِنْ غَفُورٍ رَحِيمٍ ﴿٨٠﴾

“Hakika waliosema: Mola Wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa. Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata kinachotamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyovitaka. Ni takrima itokayo kwa Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.” (41:30-32).

¹ Fat'h Al-Bari 11:364, Muslim 4:2065.

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَمَّا إِنْ كَانَ مِنَ الْمُكَذِّبِينَ الضَّالِّينَ ﴿٧٦﴾ فَتُزَلُّ مِنْ حَمِيمٍ ﴿٧٧﴾

“Na ama akiwa katika waliokadhibisha wapotovu. Basi karamu yake ni maji yanayochemka, na kutiwa Motoni.”

Inamaanisha, kama mtu anayekaribia kufa ni katika waliokataa ukweli, walipotea mbali na uongofu,

فَتُزَلُّ

“Basi karamu yake...” Maana yake: Kama mgeni.

مِنْ حَمِيمٍ

“...ni maji yanayochemka.”

Yenye kuyeyusha matumbo na ngozi.

وَتَصْلِيَةٌ حَمِيمٍ ﴿٧٨﴾

“Na kutiwa Motoni.”

Maana yake: Katika moto wa Jahanamu, utakaomzingira kutoka pande zote. Allah تعالى Amesema, baada ya hapo,

إِنَّ هَذَا هُوَ حَقُّ الْيَقِينِ ﴿٧٩﴾

“Hakika hii ndiyo haki yenye yakini.”

Maana yake: Habari hizi ni kweli; hazina shaka, wala hakuna atakayekwepa,

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٨٠﴾

“Basi litakase Jina la Mola Wako Mlezi aliye Mkubwa.”

Jabir رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ قَالَ: سُبْحَانَ اللَّهِ الْعَظِيمِ وَبِحَمْدِهِ، غُرِسَتْ لَهُ نَخْلَةٌ فِي الْجَنَّةِ»

“Mwenye kusema, “Ametakasika Allah Mtukufu na Sifa njema ni Zake!” Basi utaoteshwa mtende kwa ajli yake Peponi.”

Hadith hii ilikusanywa na At -Tirmidhi na An-Nasa'i; At -Tirmidhi amesema, "Hasan Gharib."¹ Al-Bukhari amenukuu katika kitabu chake (*Sahih yake*) kutoka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«كَلِمَتَانِ خَفِيفَتَانِ عَلَى اللِّسَانِ، ثَقِيلَتَانِ فِي الْمِيزَانِ، حَبِيبَتَانِ إِلَى الرَّحْمَنِ:
سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ، سُبْحَانَ اللَّهِ الْعَظِيمِ»

"Matamko mawili mepesi kwenye ulimi, mazito katika Mizani, yanayopendwa sana na Ar-Rahman: "Ametakasika Allah pamoja na Sifa Zake, Ametakasika Allah Mtukufu."

Kundi la Maulamaa wa Hadithi wameikusanya Hadithi hiyo isipokuwa Imamu Abu Dawud.²

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Al-Waqi'ah*, sifa zote njema pamoja na shukrani ni za Allah تعالى na fadhila zote zinatoka Kwake.

* * *

¹ Muslim 4:2072, Tuhfatul - Ahwadh 9:434, An-Nasai katika Al-Kubra 6:207, Ibn Majah 2:1251.

² Tuhfat Al-Ahwadh 9:434, An-Nasai katika Al-Kubra 6:207.

Tafsir ya Suratul Hadid Sura ya 57 Iliteremshwa Madinah

Fadhila za *Surat Al-Hadid*

Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'Irbadh bin Sariyah amesema kuwa Mtume wa Allah ﷺ alikuwa akisoma *Al-Musabbihat*¹ kabla ya kulala, kwa kusema,

«إِنَّ فِيهَا آيَةً أَفْضَلُ مِنْ أَلْفِ آيَةٍ»

*"Humo mna Aya iliyo bora zaidi ya Aya elfu moja."*²

Abu Dawud, At -Tirmidhi na An-Nasa'i waliikusanya Hadithi hii; At -Tirmidhi akasema, *"Hasan Gharib."*³

Aya iliyoashiriwa katika Hadithi hii - na Allah تعالى Anajua zaidi, ni

هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ ۗ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٨﴾

***"Yeye Ndiye wa Mwanzo na Ndiye wa Mwisho, Naye Ndiye wa Dhaahiri na wa Siri, Naye Ndiye Mjuzi wa kila kitu."* (57:3)**

Allah تعالى Akitaka, tutalitaja tena jambo hili. Tunamtumaini Allah تعالى na tunamtegemea Yeye, na Anatutosha kwa Kutusaidia.

* * *

¹ Sura za Qur'an zinazoanza kwa *Tasbih* (Kumtukuza Allah); angalia *Surah* ya 57, 59.61, 62, 64

² Ahmad 4:128, angalia tanbihi inayofuata.

³ Abu Dawud 5:304, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:238, 9:351. Kuna udhaifu katika masimulizi hayo. Inawezekana kuwa kwamba masimulizi sahihi zaidi ni ya Ad-Darimi na. 3424, na An-Nasai katika *Al-Kubra* na. 10551, ambayo ni *Mursal*.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

“Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.”

سُورَةُ الْحَدِيدِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١﴾
 لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَسِعَتْ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢﴾
 هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ ۗ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣﴾
 هُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ۖ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۗ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا ۗ وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٤﴾
 لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٥﴾
 يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ ۗ وَهُوَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٦﴾

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ
 وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١﴾ لَهُ مُلْكُ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَسِعَتْ ۖ وَيُحِيطُ ۗ
 وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢﴾ هُوَ
 الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ ۗ
 وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣﴾

1. Kinamsabih na Kumtakasa Mwenyezi Mungu kila kiliomo ndani ya mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hekima.

2. Yeye Ndiye Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi. Anahuisha na Anafisha. Na Yeye ni Mwenye Uweza wa kila kitu.

3. Yeye ndiye wa Mwanzo na Ndiye wa Mwisho. Naye Ndiye wa Dhaahiri na wa Siri, Naye Ndiye Mjuzi wa kila kitu.

Kila kitu kilichopo Kinamtukuza Allah تعالى na Kutaja baadhi ya Sifa Zake

Katika Aya hii, Allah تعالى Anaeleza kuwa kila kitu kilichomo mbinguni na ardhini Humsifu na Kumtukuza Yeye, wakiwemo wanyama na mimea sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine,

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَكِنْ لَا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٤٤﴾

“Zinamtakasa mbingu zote saba na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa sifa Zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye Maghufira.” (17:44)

Na Kauli Yake:

وَهُوَ الْعَزِيزُ

“Na Yeye Ndiye Mwenye Nguvu.”

Maana yake: Ambaye vitu vyote Humnyenyekea,

الْحَكِيمُ

“Mwenye Hekima.”

Katika Uumbaji Wake, Uimarishaji na Uwekaji wa sheria.

لَهُ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ مَتَّحِيٍّ وَيُؤْتِي

“Yeye Ndiye Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi. Anahuisha na Anafisha.”

Yeye ni Mmiliki wa Pekee wa viumbe Wake, Huhuisha, Kufisha na Kumpa Akitakacho kwa Amtakaye.

وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“Na Yeye ni Mwenye Uweza wa kila kitu.”

Chochote Atakacho, huwa, na Asichokitaka hakiwi. Amesema,

هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ^ط

“Yeye Ndiye wa Mwanzo na Ndiye wa Mwisho, Naye Ndiye wa Dhaahiri na wa Siri.”

Hii ni Aya iliyoashiriwa katika Hadithi ya ‘Irbadh bin Sariyah kwamba ni bora zaidi kuliko Aya elfu moja. Abu Dawud amenukuu kutoka kwa Abu Zamil amesema, “Nilimuambia Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa kuna kitu nilikuwa nakihisi moyoni mwangu.” Akasema, ‘Shaka’ Akacheka. Kisha, amesema, ‘Hakuna anayeweza kuepuka hilo.” Allah تعالى Amesema,

فَإِنْ كُنْتَ فِي شَكٍّ مِمَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ فَسْأَلِ الَّذِينَ يَقرءُونَ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكَ لَقَدْ جَاءَكَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٩٤﴾

“Na ikiwa unayo shaka katika Tuliyo kuteremshia, basi waulize wasomao Kitabu kabla yako. Kwa yakini imekwisha kujia Haki kutoka kwa Mola Wako Mlezi.” (10:94)

Akaniambia, ‘Unapojisikia namna hivyo moyoni, soma,

هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٩٤﴾

“Yeye Ndiye wa Mwanzo na Ndiye wa Mwisho. Naye Ndiye wa Dhaahiri na wa Siri, Naye Ndiye Mjuzi wa kila kitu.”¹

Kuna kauli tofauti takribani zaidi ya kumi za wanazuoni wa Tafsir kuhusu maelezo ya Aya hii. Al-Bukhari amesema, “Yahya amesema, ‘Adh-Dhahir: Maana yake: ‘Kujua vitu vyote.’ Kadhalika, Al-Batin: ‘Kujua vitu vyote.’²

“Shaykh wetu Al-Hafidh Al-Mizzi amesema, “Yahya ni Ibn Ziyad Al-Farra’, aliyeandika kitabu kiitwacho *Ma`ani Al-Qur’an*.” Kuna Hadithi zilizoeleza suala hilo. Miongoni mwazo, Imamu Ahmad amenukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisoma dua hii alipokuwa akienda kulala,

¹ Abu Dawud 5:335.

² Fat’h Al-Bari 13:374.

«اللَّهُمَّ رَبَّ السَّمَوَاتِ السَّبْعِ، وَرَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ، رَبَّنَا وَرَبَّ كُلِّ شَيْءٍ، مُنْزِلَ التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْفُرْقَانِ، فَالِقَ الْحَبِّ وَالنَّوَى، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ كُلِّ شَيْءٍ أَنْتَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهِ، أَنْتَ الْأَوَّلُ لَيْسَ قَبْلَكَ شَيْءٌ، وَأَنْتَ الْآخِرُ لَيْسَ بَعْدَكَ شَيْءٌ، وَأَنْتَ الظَّاهِرُ لَيْسَ فَوْقَكَ شَيْءٌ، وَأَنْتَ الْبَاطِنُ لَيْسَ دُونَكَ شَيْءٌ. اقْضِ عَنَّا الدَّيْنَ، وَأَغْنِنَا مِنَ الْفَقْرِ»

“Yaa Allah, Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa Arshi Tukufu! Mola Wetu Mlezi, na Mola Mlezi wa kila kitu, Aliyeteremsha Taurati, Injili na Furqan, Mwenye Kupasua punje na kokwa! Najikinga Kwako kutokana na shari ya kila kitu ambacho utosi wake unauhibiti Wewe. Ewe Allah! Wewe ni wa Mwanzo (Al-Awwal), hakuna kabla Yako chochote. Wewe ni wa Mwisho, hakuna baada Yako. Wewe ni wa Dhahiri (Adh-Dhahir) hakuna kilicho juu Yako. Na wewe ni wa Siri (Al-Batin), hakuna kilicho chini Yako. Utuondolee madeni na Utuondolee ufukara.”¹

Muslim amenukuu Hadithi hii kupitia kwa Sahl, ambaye alisema, “Abu Salih alikuwa akituamrisha tulalie ubavu wa kulia tunapoenda kulala, halafu tusome,

«اللَّهُمَّ رَبَّ السَّمَوَاتِ وَرَبَّ الْأَرْضِ وَرَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ، رَبَّنَا وَرَبَّ كُلِّ شَيْءٍ، فَالِقَ الْحَبِّ وَالنَّوَى، وَمُنْزِلَ التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْفُرْقَانِ، أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ كُلِّ ذِي شَرٍّ أَنْتَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهِ، اللَّهُمَّ أَنْتَ الْأَوَّلُ فَلَيْسَ قَبْلَكَ شَيْءٌ، وَأَنْتَ الْآخِرُ فَلَيْسَ بَعْدَكَ شَيْءٌ، وَأَنْتَ الظَّاهِرُ فَلَيْسَ فَوْقَكَ شَيْءٌ، وَأَنْتَ الْبَاطِنُ فَلَيْسَ دُونَكَ شَيْءٌ، اقْضِ عَنَّا الدَّيْنَ، وَأَغْنِنَا مِنَ الْفَقْرِ»

“Yaa Allah, Mola Mlezi wa mbingu na Mola Mlezi wa Arshi Tukufu! Mola Wetu Mlezi, na Mola Mlezi wa kila kitu. Na Wewe ni Mwenye Kupasua Punje na Kokwa, Aliyeteremsha Taurati, Injili na Furqan, Najikinga Kwako kutokana na shari ya kila kitu ambacho utosi wake Unauhibiti. Ewe Allah! Wewe ni Al-Awwal, hakuna cha kabla yako; Na wewe ni Al-Akhir, hakuna cha baada Yako; Na wewe ni Adh-Dhahir, hakuna cha juu Yako; Na wewe ni Al-Batin, hakuna cha chini Yako. Tulipie madeni na Ututosheleze dhidi ya ufukara.”

¹ Ahmad 2:404.

na alikuwa akisimulia simulizi hii kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ.¹

هُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۚ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ
فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا ۗ وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ
وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٦﴾ لَهُ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٧﴾
يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُؤَلِّجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ ۗ وَهُوَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٨﴾

4. Yeye Ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita; Akakaa vyema juu ya Kiti cha Enzi. Anayajua yanayoingia katika ardhi na yanayo toka humo, na yanayoteremka kutoka mbinguni, na yanayopanda humo. Naye Yu pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona mnayoyatenda.

5. Ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake. Na mambo yote yanarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.

6. Anaingiza usiku katika mchana, na Anaingiza mchana katika usiku. Na Yeye ni Mwenye Kuyajua yaliomo vifuni.

Ujuzi, wa Allah تعالى Uwezo na Ufalme Wake, Havina Ukomo

Allah تعالى Anaeleza kuwa Ameumba mbingu na ardhi, na vyote vilivyo baina yake, katika Siku sita Akawa katika Arshi Yake baada ya Kuziumba. Tulishayaeleza hayo katika maelezo ya Surat Al-A'raf.²

Kauli ya Allah تعالى،

يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْأَرْضِ

“Anayajua yanayoingia katika ardhi.” Maana yake: Anajua kiasi cha mbegu na matone ya maji yanayoingia ardhini.

وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا

“Na yanayotoka humo.” Katika mimea na matunda. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine.

¹ Muslim 4:2084

² Angalia juzu ya nne, Tafsir ya Surat Al-A'raf (7:54)

وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَمَا تَسْقُطُ مِنَ
وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٧﴾

“Na Ziko Kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye Anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinachobainisha.” (6:59)

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ

“...na yanayoteremka kutoka mbinguni...” Ikiwemo mvua, theluji na barafu na chochote Anachoamua Allah تعالى kiteremke kutoka mbinguni baada ya maamuzi na amri zinazoletwa na malaika watukufu. Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا يَعْزُجُ فِيهَا

“...na yanayopanda humo.” Miongoni mwa Malaika na matendo ya watu. Katika Sahih, kuna Hadithi ambayo Mtume ﷺ amesema،

«يُرْفَعُ إِلَيْهِ عَمَلُ اللَّيْلِ قَبْلَ النَّهَارِ، وَعَمَلُ النَّهَارِ قَبْلَ اللَّيْلِ»

“Kwake Yeye Hupanda amali za usiku kabla ya mchana na amali za mchana kabla ya usiku.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

‘Naye Yu pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona mnayoyatenda.’

Inamaanisha, Anakuangalieni na Kushuhudia amali zenu popote mtakapokuwa, nchi kavu au baharini, wakati wa usiku au mchana, nyumbani au katika maeneo ya wazi au jangwani.

Vyote hivyo Kwake Yeye ni sawa katika Ujuzi Wake na vyote vilivyo katika Uoni Wake na Usikiaji Wake. Anasikia maneno yenu na Anakuoneni mahali mlipo. Anajua siri zenu na mnayoyadhihirisha. Kama Allah تعالى Alivyosema،

¹Muslim 1:162

أَلَا إِنَّهُمْ يَنْتُونُ صُدُورَهُمْ لِيَسْتَخْفُوا مِنْهُ أَلَا حِينَ يَسْتَغْشُونَ ثِيَابَهُمْ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ
وَمَا يُعْلِنُونَ إِنَّهُمْ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٥٧﴾

“Jueni kuwa wanapojigubika nguo zao Yeye Anajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona mnayoyatenda.” (11:5)

Allah تعالى Amesema,

سَوَاءٌ مِنْكُمْ مَنْ أَسْرَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿١٠﴾
“Ni sawa (Kwake Allah) anayeficha kauli yake kati yenu na anayeidhirisha, na anayejificha usiku na anayetembea kweupe mchana (Wote Anawajua).” (13:10)

Kwa hakika, hakuna Mola wa Kuabudiwa kwa haki, isipokuwa Allah تعالى.

Katika Sahih, kuna Hadithi ambayo Mtume ﷺ alimjibu Jibril عليه السلام, alipomuuliza kuhusu *Ihsan*:

«أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ تَأْتِكَ تَرَاهُ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ»

“Kumuabudu Allah kama vile unamuona. Kama wewe humuoni, basi Yeye Anakuona.”¹

Kauli ya Allah تعالى,

لَهُدُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿١٠٠﴾

“Ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake. Na mambo yote yanarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, Allah تعالى ni Mfalme na Mmiliki wa dunia na Akhera. Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine,

وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَىٰ ﴿٩٢﴾

‘Na hakika ni Yetu Sisi Akhera na dunia.’ (92:13)

Kwa hakika, Allah تعالى Anasifika kwa sifa hiyo, kama Alivyosema katika Aya nyingine,

¹ Fat’h Al-Bari 1:140.

وَهُوَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ لَهُ الْحَمْدُ فِي الْأُولَى وَالْآخِرَةِ ۗ

“Naye ni Mwenyezi Mungu Ambaye hapana Mungu isipokuwa Yeye. Sifa zote njema pamoja na shukurani ni Zake Yeye, Mwanzo na Mwisho.” (28:70), Na Kauli ya Allah تعالى،

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَلَهُ الْحَمْدُ فِي الْآخِرَةِ ۗ وَهُوَ الْحَكِيمُ

الْخَبِيرُ ﴿٣٤﴾

“Sifa njema zote pamoja na shukurani ni za Mwenyezi Mungu, ambaye ni Vyake vyote vilivyomo mbinguni na katika ardhi. Na Sifa ni Zake Yeye katika Akhera. Naye ni Mwenye Hekima, Mwenye Khabari.” (34:1)

Allah تعالى Anamiliki kila kitu cha mbinguni na ardhini, na wote waliomo humo ni waja Wake na humnyenyekea Yeye, kama Alivyosema,

إِنْ كُلُّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتَى الرَّحْمَنِ عَبْدًا ﴿٣٥﴾ لَقَدْ أَحْصَيْنَاهُمْ وَعَدَّهُمْ

عَدًّا ﴿٣٦﴾ وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ﴿٣٧﴾

“Hapana yeyote aliyomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Arrahmani Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa Wake. Yeye hakika Amewadhibiti na Amewahesabu sawa sawa. Na kila mmoja katika wao atamfikia Siku ya Kiyama peke yake.” (19:93-95)

Ndio sababu ya Kauli ya Allah تعالى hapa,

وَالِلَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ

“Na mambo yote yanarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.”

Inamaanisha kuwa mambo yote yatarejea Kwake katika Siku ya Kiyama na Atawahukumu viumbe Wake Anavyotaka. Kwa hakika, Yeye ni Muadilifu kuliko wote, Ambaye kamwe Hadhulumu, hata kwa uzito wa chembe ya vumbi; ikiwa mtu atafanya hata amali moja njema, Allah تعالى Ataizidisha mara kumi zaidi,

وَيُؤْتِي مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾

“...na Hutoa kutoka Kwake malipo makubwa.” (4:40), Na,

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَإِنْ كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ
مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا وَكَفَىٰ بِنَا حَاسِبِينَ ﴿٥٧﴾

“Nasi Tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali Tutaiteta. Nasi Tunatosha kuwa washika hesabu.”(21:47)

Kauli ya Allah ﷻ،

يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُؤَلِّجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ ۚ وَهُوَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٥٨﴾

“Anaingiza usiku katika mchana, na Anaingiza mchana katika usiku.”

Maana yake: Huwafanyia viumbe Atakavyo. Huingiza usiku katika mchana na kinyume chake na Kuvikadiria hivyo kwa Hekima Yake, Atakavyo. Wakati mwingine, Huurefusha usiku zaidi ya mchana na kinyume chake. Wakati mwingine, Huufanya sawa usiku na mchana. Wakati mwingine, Huleta majira ya baridi, halafu vuli, kiangazi na kipupwe. Yote hayo Huyafanya kwa Hekima Yake na kipimo Chake kwa kila kitu katika viumbe Wake,

وَهُوَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ

“Na Yeye ni Mwenye Kuyajua yaliomo vifuani.”

Anajua siri, na haijalishi zimefichikana kwa kiasi gani.

* * *

ءَامِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَأَنْفِقُوا مِمَّا جَعَلَكُمْ مُسْتَحْلِفِينَ فِيهِ ۖ
فَالَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَأَنْفَقُوا هُمْ أَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿٧﴾ وَمَا لَكُمْ
لَا تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ ۗ وَالرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ لِتُؤْمِنُوا بِرَبِّكُمْ وَقَدْ
أَخَذَ مِنْكُمْ مِيثَاقَكُمْ إِذْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾ هُوَ الَّذِي يُزِيلُ عَلَى
عِبَادِهِ ءَايَاتٍ يَبْنَطُ لِيُخْرِجَكُمْ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۗ
وَإِنَّ اللَّهَ بِكُمْ لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٩﴾ وَمَا لَكُمْ أَلَّا تُنْفِقُوا فِي
سَبِيلِ اللَّهِ وَلِلَّهِ مِيرَاثُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ لَا يَسْتَوِي
مِنْكُمْ مَن أَنْفَقَ مِنْ قَبْلِ الْفَتْحِ وَقَتْلَ ۗ أُولَئِكَ أَعْظَمُ
دَرَجَةً مِنَ الَّذِينَ أَنْفَقُوا مِنْ بَعْدُ وَقَتَلُوا ۗ وَكُلًّا وَعَدَ اللَّهُ
الْحَسَنَى ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١٠﴾ مَن ذَا الَّذِي
يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضِعِفَهُ لَهُ ۗ وَلَهُ أَجْرٌ كَرِيمٌ ﴿١١﴾
يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَى نُورُهُمْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ
وَبِأَيْمَانِهِمْ بُشْرَانُكُمْ الْيَوْمَ جَنَّتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ
خَالِدِينَ فِيهَا ۗ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٢﴾ يَوْمَ يَقُولُ
الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَاتُ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا انظُرُونَا نَقْتِسَبْ
مِنْ نُورِكُمْ قِيلَ ارْجِعُوا وَرَاءَكُمْ فَالْتَمِسُوا نُورًا فَضُرِبَ
بَيْنَهُمْ بِسُورٍ لَهُدٍ بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ مِنْ قِبَلِهِ
الْعَذَابُ ﴿١٣﴾ يُنَادُوا بِهِمْ أَلَمْ نَكُنْ مَعَكُمْ ۗ قَالُوا بَلَى
وَلَكِنَّا كُنَّا فِتْنَةً أَنْفُسَكُمْ وَتَرَضْتُمْ وَأَرْتَبْتُمْ وَغَرَّتْكُمُ
الْأُمَانِي حَتَّىٰ جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ وَعَرَّيْكُمْ بِاللَّهِ الْغُرُورُ ﴿١٤﴾ فَالْيَوْمَ
لَا يُؤَخِّدُكُمْ مِنْكُمْ فَدْيَةٌ وَلَا مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ مَأْوَانُكُمْ النَّارُ
هِيَ مَوْلَانُكُمْ ۗ وَيَسَّ الْمَصِيرُ ﴿١٥﴾

ءَامِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَأَنْفِقُوا مِمَّا
جَعَلَكُمْ مُسْتَحْلِفِينَ فِيهِ ۖ فَالَّذِينَ
ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَأَنْفَقُوا هُمْ أَجْرٌ كَبِيرٌ
﴿٧﴾ وَمَا لَكُمْ لَا تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ ۗ
وَالرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ لِتُؤْمِنُوا بِرَبِّكُمْ
وَقَدْ أَخَذَ مِنْكُمْ مِيثَاقَكُمْ إِذْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ
﴿٨﴾ هُوَ الَّذِي يُزِيلُ عَلَى
ءَايَاتٍ يَبْنَطُ لِيُخْرِجَكُمْ مِنَ
الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ بِكُمْ
لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٩﴾ وَمَا لَكُمْ أَلَّا
تُنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلِلَّهِ مِيرَاثُ
السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ لَا يَسْتَوِي
مِنْكُمْ مَن أَنْفَقَ مِنْ قَبْلِ الْفَتْحِ
وَقَتْلَ ۗ أُولَئِكَ أَعْظَمُ دَرَجَةً مِنَ
الَّذِينَ أَنْفَقُوا مِنْ بَعْدُ وَقَتَلُوا ۗ وَكُلًّا
وَعَدَ اللَّهُ الْحَسَنَى ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ
خَبِيرٌ ﴿١٠﴾ مَن ذَا الَّذِي يُقْرِضُ
اللَّهُ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضِعِفَهُ لَهُ ۗ وَلَهُ
أَجْرٌ كَرِيمٌ ﴿١١﴾

7. Muaminini Mwenyezi
Mungu na Mtume Wake; na
toeni katika mali ambayo

Amekufanyeni nyinyi kuwa ni viongozi wake. Basi walioamini miongoni mwenu, na wakatoa, wana malipo makubwa.

8. Na mna nini hata hamumuamini Mwenyezi Mungu na hali Mtume anakuiteni mumuamini Mola Wenu Mlezi? Naye Amekwishachukua ahadi yenu, ikiwa nyinyi ni Waumini.

9. Yeye Ndiye Anayemteremshia mja Wake Aya zinazobainisha wazi ili Akutoeni gizani muingie kwenye nuru. Na hakika Mwenyezi Mungu kwenu ni Mpole, Mwenye Kurehemu.

10. Na mna nini hata hamtoi katika njia ya Mwenyezi Mungu, na hali urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya ushindi na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao waliotoa baadae na wakapigana. Na wote hao Mwenyezi Mungu Amewaahidia wema. Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda.

11. Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, ili Amzidishie maradufu, na apate malipo makubwa.

Kuamrisha Imani na Kuhamasisha Kutoa

Allah تعالی Anaamuru kumuamini Yeye na Mjumbe Wake, na kwamba mtu anapaswa kudumu katika njia na kushikamana nayo. Allah تعالی Anahimiza kuhusu kutumia kutokana na Alichompa amana mwanadamu-Alivyokukopesheni. Mali hiyo ilikuwa mikononi mwa wale wa kabla yenu na baadaye ikahamishiwa kwenu. Kwa hiyo, enyi wanadamu, mali Aliyokupeni amana itumieni kulingana na Alivyokuamrisheni Allah تعالی katika kumtii. Vinginevyo, Atakuulizeni na Kukupeni adhabu kutokana na kupuuzia Aliyokufaradhisieni katika hilo. Kauli ya Allah تعالی,

مِمَّا جَعَلَكُمْ مُسْتَخْلَفِينَ فِيهِ

“...katika Alivyokufanyeni nyinyi kuwa ni waangalizi wake.”

Inaashiria kuwa nyinyi - wanadamu – mali mlizonazo mtawaachia wengine. Katika hali hii, watakaorithi kutoka kwenu wanaweza kumtii Allah تعالی kwa

mali zao, na kwa hivyo wakawa wema zaidi kuliko nyinyi kutokana na Alichowapa Allah تعالى. Pia wanaweza kumuasi Allah تعالى, na katika hali hii mtakuwa mmewasaidia kutenda dhambi na kuruka mipaka. Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'Abdullah bin Ash-Shikhir amesema, "Nilikwenda kwa Mtume ﷺ na nikamkuta akisoma,

«أَلَيْسَ الْكَافِرُ يَقُولُ ابْنُ آدَمَ: مَالِي مَالِي، وَهَلْ لَكَ مِنْ مَالِكَ إِلَّا مَا أَكَلْتَ فَأَفْتَيْتَ، أَوْ لَبَسْتَ فَأَبْلَيْتَ، أَوْ تَصَدَّقْتَ فَأَمْضَيْتَ؟»

“Kumekushughulisheni kutafuta wingi wa mali, Mwana wa 'Adam anadai, "Mali yangu, mali yangu." Lakini huna chako, isipokuwa ulichokula, ukakimaliza, au ulichokivaa kikachakaa au ulichotoa sadaka na ukakitanguliza.”¹

Imamu Muslim pia alikusanya Hadithi hii pamoja na nyongeza:

«وَمَا سِوَى ذَلِكَ، فَذَاهِبٌ وَتَارِكُهُ لِلنَّاسِ»

“Na Kisichokuwa hicho, utaondoka na kuwaachia watu.”²

Kauli ya Allah تعالى,

فَالَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَأَنفَقُوا هُمْ أَجْرٌ كَبِيرٌ

“Basi walioamini miongoni mwenu, na wakatoa, wana malipo makubwa.”

Inahimizwa kuwa na imani na kutumia mali katika vitendo vya utii wa amri za Allah تعالى. Yeye Amesema,

وَمَا لَكُمْ لَا تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالرَّسُولِ يَدْعُوكُمْ لِتُؤْمِنُوا بِهِ كَرِهُوا

“Na mna nini hata hamumuamini Mwenyezi Mungu na hali Mtume anakuiteni mumuamini Mola Wenu Mlezi?”

¹ Ahmad 4:24.

² Muslim 4:2273.

Inamaanisha, “nini kinachokuzieni nyinyi kuamini, ilhali Mtume ni miongoni mwenu akikulinganieni imani na kukuleteeni dalili na shuhuda zenye kuthibitisha ukweli wa alichokuleteeni.” Na tumeeleza Hadithi kupitia njia tofauti mwanzoni mwa maelezo juu ya mlango wa Imani katika Sahih Al-Bukhari, ambapo siku moja Mtume ﷺ aliwaambia Masahaba wake رضي الله عنهم,

«أَيُّ الْمُؤْمِنِينَ أَعْجَبُ إِلَيْكُمْ إِيْمَانًا؟»

“Ni nani nyinyi mnamchukulia kuwa na Imani thabiti miongoni mwa waumini?”

Wao wakasema, “Malaika.” Yeye akasema,

«وَمَا لَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ وَهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ؟»

“Na nini kitawazuia wao kuamini ilhali wako kwa Mola Wao Mlezi?”

Wao wakasema, “Basi ni Manabii.” Yeye akasema,

«وَمَا لَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ وَالْوَحْيَ يَنْزِلُ عَلَيْهِمْ؟»

“Nini kitawazuia wao kuamini ihali ufunuo huwateremkia wao?”

Wao wakasema, “Basi, sisi.” Yeye akawaambia,

«وَمَا لَكُمْ لَا تُؤْمِنُونَ وَأَنَا بَيِّنٌ أَظْهَرُكُمْ؟ وَلَكِنْ أَعْجَبُ الْمُؤْمِنِينَ إِيْمَانًا، قَوْمٌ يَجِئُونَ
بِعُدُوكُمْ، يَجِدُونَ صُحُفًا يُؤْمِنُونَ بِمَا فِيهَا»

“Nini kitakuzieni nyinyi kuamini, ilhali mimi niko miongoni mwenu? Kwa hakika, waumini watakaokuwa na imani ya kustaajabisha ni watu watakaokuja baada yenu; wao watakuta vitabu na wataamini yaliyomo ndani yake.”¹

Tumeshataja sehemu ya Hadithi hii katika *Surat Al-Baqarah*, katika kueleza Kauli ya Allah تعالى,

¹ Al-Majma' 10:65.

الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ

“Ambao huyaamini ya ghaibu.” (2:3)

Kauli ya Allah تعالى،

وَقَدْ أَخَذَ مِيثَاقَكُمْ

“Naye amekwishachukua ahadi yenu.”

Inafanana na Kauli Yake nyingine،

وَأَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَمِيثَاقَهُ الَّذِي وَاثَقَكُمْ بِهِ إِذْ قُلْتُمْ سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا

‘Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, na ahadi Yake Aliyofungamana nanyi mlipo sema: Tumesikia tukat’ii.’ (5:7),

Inamaanisha kumpa Mtume ﷺ ahadi ya utii. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema kuwa agano lililotajwa hapa, ni la kutoka kwa wanadamu, walipokuwa bado katika mgongo wa Adam عليه السلام. Hii pia ni rai ya Mujahidi, na Allah تعالى Anajua zaidi.² Kauli ya Allah تعالى،

هُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ عَلَىٰ عَبْدِهِ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ

‘Yeye Ndiye Anayemteremshia mja Wake Aya zinazobainisha wazi.’

Dalili dhahiri, shuhuda zisizopingika na uthibitisho wa wazi kabisa،

يُخْرِجُكُمْ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ

“...ili Akutoeni gizani muingie kwenye nuru.”

Kutoka katika giza la ujinga, ukafiri na kauli kinzani kuelekea kwenye nuru ya uongofu, uhakika na imani،

وَإِنَّ اللَّهَ بِكُمْ لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ

“Na hakika Mwenyezi Mungu kwenu ni Mpole, Mwenye Kurehemu.”

² At-Tabari 23:172.

Kwa kuteremsha Vitabu vya Kiungu na kutuma Mitume wa kuwaongoza wanaadamu, kuondoa shaka na kuondoa desturi potofu. Baada ya Allah تعالى Kuwaamuru wanadamu kwanza kuamini na kutumia Alichowaruzuku Amewahimiza kuwa na imani na Amesema kuwa Ameondoa vikwazo vyote kati yao na upatikanaji wa imani. Allah تعالى tena Amewahimiza kutoa,

وَمَا لَكُمْ أَلَّا تُنْفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلِلَّهِ مِيرَاثُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ^ع

“Na mna nini hata hamtoi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu?”

Maana yake: Toeni na msihofie umaskini au uhaba. Kwa hakika, Yeye mnayetoa mali katika njia Yake ni Mfalme na Mmiliki wa mbingu na ardhi na Anadhibiti kila jambo. Zikiwemo hazina za mali. Yeye ni Mmiliki wa Arshi, pamoja na nguvu zote zilizomo, na Yeye Ndiye Aliyesema,

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُ^ط وَهُوَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ^ب

“Na chochote mtakachokitoa Yeye Atakilipa. Naye ni Mbora wa wanaoruzuku.” (34:39), Aidha amesema,

مَا عِنْدَكُمْ يَنْفَدُ^ط وَمَا عِنْدَ اللَّهِ بَاقٍ^ط

“Mlivyonavyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ndivyo vitakavyobakia.” (16:96)

Kwa hiyo, wanaomtumaini na kumtegemea Allah تعالى watatoa na hawatahofu umaskini au ufakiri kuwajia kutoka kwa Mmiliki wa Arshi. Wanajua kuwa Allah تعالى kwa hakika Atawalipa mbadala kwa chochote wanachotoa.

Fadhila za Kutoa Mali na Kupigana Kabla ya Ukombozi wa Makkah

Kauli ya Allah تعالى,

لَا يَسْتَوِي مِنْكُمْ مَنْ أَنْفَقَ مِنْ قَبْلِ الْفَتْحِ وَقَتْلَ^ع

‘Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya Ushindi na wakapigana vita.’

Inamaanisha wale ambao hawakupigana na kutoa mali kabla ya ukombozi wa Makka hawalingani na waliotoa sadaka na wakapigana.

Kabla ya Makka kukombolewa, mambo yalikuwa magumu kwa Waislamu na watu wema tu ndio waliosilimu. Baada ya Makkah kukombolewa, Uislamu ulienea sana duniani kote na watu waliingia katika dini ya Allah تعالى makundi makundi. Kwa ajili hiyo, Amesema:

أُولَئِكَ أَكْثَرُ دَرَجَةٍ مِّنَ الَّذِينَ أَنْفَقُوا مِنْ بَعْدِ وَقْتِنَا وَكُلًّا وَعَدَ اللَّهُ الْحَسَنَىٰ

“Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao waliotoa baadae na wakapigana. Na wote hao Mwenyezi Mungu Amewaahidia wema.”

Wengi huchukulia kuwa kusudio la ukombozi hapa kuwa ni wa Makka. Ash-Sha’bi na wengine kadhaa wamesema kuwa Aya inarejea katika Mkataba wa Al-Hudaybiyyah.¹

Kuna ushahidi juu ya rai hii unaopatikana katika Hadithi kutoka kwa Anas, Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Anas amesema, “Khalid bin al-Walid na ‘Abdur-Rahman bin ‘Awf رضي الله عنه waligombana. Khalid akamwambia ‘Abdur-Rahman, ‘mnajifaharisha kwetu kuhusu siku (vita) mlivyoshiriki kabla yetu.’ Habari hizo zilipomfikia Mtume ﷺ, alisema,

«دَعُوا لِي أَصْحَابِي، فَوَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَوْ أَنْفَقْتُمْ مِثْلَ أُحُدٍ - أَوْ مِثْلَ الْجَبَالِ -
ذَهَبًا، مَا بَلَّغْتُمْ أَعْمَالَهُمْ»

“Niachieni Masahaba wangu, Waacheni, kwani ninaapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake Lau mtatoa sadaka inayolingana na Mlima Uhud, - au sawa na milima - dhahabu, hamtafikia amali zao.”²

Inajulikana wazi kuwa Khalid bin Al-Walid رضي الله عنه, ambaye Mtume ﷺ alikusudia kumwambia yeye, alisilimu wakati wa kipindi cha baina ya Mkataba wa Al-Hudaybiyyah na kukombolewa Makka. Ugomvi baina ya Khalid na Abdur-Rahman ulitokea kwa sababu ya vita vya Bani Jadhimah. Mtume ﷺ alimtuma Khalid bin Al-Walid رضي الله عنه kwao baada ya ukombozi wa Makkah, na wakasema, “Saba’na,”³ badala ya kusema, “Aslamna” (tumesilimu). Kwa hivyo

¹ At-Tabari 23:175.

² Ahmad 3:266.

³ Maana yake: “Wasabai.” Ilikuwa hivyo kwa sababu hawakujua jina la dini ya Mtume ﷺ

Khalid aliamuru wauliwe na kuuliwa mateka wao (wa kivita); 'Abdur-Rahman bin 'Awf na 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما walimpinga. Hiyo ndiyo sababu ya ugomvi uliotokea baina ya Khalid na 'Abdur-Rahman رضي الله عنهما. Lakini katika Sahihi, Mtume ﷺ amesema,

«لَا تَسُبُّوا أَصْحَابِي، فَوَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَوْ أَتَّفَقَ أَحَدُكُمْ بِمِثْلِ أُحُدٍ ذَهَبًا، مَا بَلَغَ مَدِّي أَحَدِهِمْ وَلَا نَصِيفُهُ»

"Msiwatukane Maswahaba wangu, kwani ninaapa kwa Ambaye nafsi yangu imo Mkononi Mwake! Kama mmoja wenu angetoa (sadaka) ya dhahabu mfano wa Uhud, isingefikia kibaba'cha mmoja wao au nusu yake."²

Kauli ya Allah تعالى،

وَكُلًّا وَعَدَ اللَّهُ الْحُسَيْنِيَّ

"Na wote hao Mwenyezi Mungu Amewaahidia wema."

Inamaanisha, waliotoa katika mali zao kabla na baada ya ukombozi wa Makka; wote watapata malipo ya amali zao njema, ingawa baadhi yao wanatofautiana kwa daraja na kupata malipo zaidi ya wengine. Ni sawa na kauli ya Allah تعالى،

لَا يَسْتَوِي الْقَاعِدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ غَيْرُ أُولِي الضَّرَرِ وَالْمُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَاهِدِينَ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ عَلَى الْقَاعِدِينَ دَرَجَةً وَكُلًّا وَعَدَ اللَّهُ الْحُسَيْنِيَّ وَفَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَاهِدِينَ عَلَى الْقَاعِدِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٥٧﴾

"Hawawi sawa Waumini wanaokaa tu wala hawana dharura, na wale wanaopigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Mwenyezi Mungu Amewatukuza cheo wale wanaopigana kwa mali yao na nafsi zao kuliko wale wanaokaa tu. Ingawa Mwenyezi Mungu Amewaahidi wote mashukio mema, lakini Mwenyezi Mungu Amewaboresha wanaopigana kwa ujira mkubwa kuliko wanaokaa tu." (4:95)

Kuna Hadithi katika Sahih inayoeleza,

¹ Kibaba.

² Muslim 4:25.

«الْمُؤْمِنُ الْقَوِيُّ خَيْرٌ وَأَحَبُّ إِلَى اللَّهِ مِنَ الْمُؤْمِنِ الضَّعِيفِ، وَفِي كُلِّ خَيْرٍ»

“Muumini mwenye nguvu ni bora na mwenye kupendwa zaidi na Allah kuliko muumini dhaifu; na kila mmoja ana heri.”¹

Ametuzindua Mtume ili asije akadharauliwa yule aliye dhaifu kwa kuangalia sifa za mwenye nguvu, ndio maana akamsifu huyu wa pili ijapokuwa yule wa mwanzo ni bora zaidi. Kauli ya Allah تعالى:

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ

“Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayo yatenda.”

Inamaanisha, kwa kuwa Allah تعالى ni Mjuzi wa yote kikamilifu, Ametofautisha baina ya malipo ya waumini waliotoa mali zao na wakapigana kabla ya ukombozi na waliotoa mali zao na kupigana baada ya hapo. Kwa hakika, Allah تعالى Ameyafanya hayo kwa Ujuzi Wake juu ya nia ya wale wa aina ya kwanza na unyoofu wao Kwake, wakati huo huo kutoa mali katika nyakati za taabu, umaskini na dhiki kubwa. Hayo yapo katika Hadithi,

«سَبَقَ دِرْهَمٌ مِائَةَ أَلْفٍ»

“Dirham moja iliyotolewa mwanzo imezishinda laki moja.”²

Hakuna shaka kuwa waumini humchukulia Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه kuwa ni mwenye fungu kubwa kulingana na maana ya Aya hii. Alikuwa kiongozi wa waliotekeleza hilo, kati ya wafuasi wa Manabii wote. Alitoa mali yake yote ili kutafuta radhi za Allah تعالى. Alifanya hivyo kwa hiari, si kulipa deni au kupata fadhila ya yeyote katika wanadamu. Allah تعالى Awe Radhi naye.

Kuhimizwa Kutoa katika Njia ya Allah تعالى

Kauli ya Allah تعالى,

مَنْ دَا أَلَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا

“Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema.”

Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه amesema kuwa Aya hii inarejea katika kutoa mali katika njia ya Allah تعالى. Pia ilielezwa kuwa inahusu kutumia mali juu ya

¹ Muslim 4:2052.

² An-Nasai 5:59.

watoto. Lililo sahihi ni kuwa, maana yake ni pana zaidi ya hayo. Hivyo wenye kutoa mali katika njia ya Allah تعالى kwa nia njema na nyoyo nyoofu, basi wanakuwa ndani ya maana pana ya Aya hii. Allah تعالى Akasema katika Aya nyingine:

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضِعِفَهُ لَهُ

“Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, ili Amrudishie maradufu, na apate malipo ya ukarimu.”

Na katika Aya nyingine,

أَضْعَافًا كَثِيرَةً

‘Mzidisho mwingi.’ (2:245),

Inamaanisha, malipo mema na riziki nyingi: Peponi katika Siku ya Kiyama. Ibn Abi Hatim amenukuu kuwa ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه, “Aya hii,

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضِعِفَهُ لَهُ

“Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, ili Amrudishie maradufu, na apate malipo ya ukarimu.”

Ilipoteremshwa, Abu Ad-Dahdah Al-Ansari رضي الله عنه alisema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Allah تعالى Anatuomba mkopo?’ Mtume ﷺ akasema,

«نَعَمْ، يَا أَبَا الدَّحْدَاحِ»

“Ndiyo, Ewe Abu Ad-Dahdah.”

Akasema, ‘Nipe mkono wako, Ewe Mjumbe wa Allah. “Mtume ﷺ akaushika mkono wake. Abu Ad-Dahdah رضي الله عنه akasema, ‘Kwa hakika, nimetoa shamba langu kumkopesha Mola Wangu Mlezi.’ Alikuwa ana shamba lililokuwa na mitende mia sita; maisha yake na wanawe yalikuwa katika shamba hilo pia. Abu Ad-Dahdah رضي الله عنه alimuendea mkewe na kumuita, ‘Umm Ad-Dahdah! ‘ Akaitikia, ‘Naam.’ akamuambia, ‘Ondoka katika shamba, kwa sababu nimemkopesha Mola Wangu Mlezi, Mtukufu.’ Akasema, ‘Hiyo ni biashara yenye faida kubwa, Ewe Abu Ad-Dahdah! ‘Kisha mkewe akaondoa vitu vyake na watoto.” Mtume ﷺ akasema,

«كَمْ مِنْ عَذْقٍ رَدَّاحٍ فِي الْجَنَّةِ لِأَبِي الدَّحْدَاحِ»

“Ni mikungu yenye tende tamu sana atakayokuwa nayo Abu Ad-Dahdah huko Peponi!”

Katika simulizi nyingine, Mtume ﷺ alisema,

«رُبَّ نَخْلَةٍ مَدَلَّوْا، عُرُوْفَهَا دُرٌّ وَيَأْتُوْتُ، لِأَبِي الدَّحْدَاحِ فِي الْجَنَّةِ»

"Huenda Mitende mingi imeinamisha chini mikungu yake, iliyojaa lulu na yakuti Peponi kwa ajili ya Abu Ad-Dahdah!"¹

يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَى نُورُهُمْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِمْ بُشْرَانِكُمُ الْيَوْمَ جَنَّاتٌ تَجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٢﴾ يَوْمَ يَقُولُ الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَاتُ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا انظُرُونَا نَقْتِسِسْ مِنْ نُورِكُمْ قِيلَ ارْجِعُوا وَرَاءَكُمْ فَالْتَمِسُوا نُورًا فَضُرِبَ بَيْنَهُم بِسُورٍ لَهُدٍ بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ مِنْ قِبَلِهِ الْعَذَابُ ﴿١٣﴾ يُنَادُوهُمْ أَلَمْ نَكُنْ مَعَكُمْ قَالُوا بَلَىٰ وَلَكِنَّكُمْ فَتَنْتُمْ أَنْفُسَكُمْ وَتَرَبَّصْتُمْ وَارْتَبْتُمْ وَغَرَّتْكُمُ الْأَمَانِيُّ حَتَّىٰ جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ وَغَرَّكُمْ بِاللَّهِ الْغُرُورُ ﴿١٤﴾ فَالْيَوْمَ لَا يُؤْخَذُ مِنْكُمْ فِدْيَةٌ وَلَا مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا مَأْوَانِكُمُ النَّارُ هِيَ مَوْلَانِكُمْ وَبئسَ الْمَصِيرُ ﴿١٥﴾

12. Siku utakapowaona Waumini wanaume na Waumini wanawake, nuru yao iko mbele yao, na kuliani kwao: Furaha yenu leo - Bustani zipitazo mito kati yake mtakaa humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

13. Siku wanafiki wanaume na wanafiki wanawake watapo waambia walioamini: Tungojeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu. Waambiwe: Rejeeni nyuma yenu mkaitafute nuru! Utiwe baina yao ukuta wenye mlango - ndani yake mna rehema, na nje upande wake wa mbele kuna adhabu.

14. Watawaita wawaambie: Kwani vile hatukuwa pamoja nanyi? Watawaambia: Ndiyo, lakini mlifitini wenyewe, na mkasitasita, na mkatia shaka, na matamania ya nafsi zenu yakakudanganyeni. mpaka ilipokuja Amri ya Mwenyezi Mungu, na mdanganyifu akakudanganyeni msimfuate Mwenyezi Mungu.

¹ Juzuu ya Al-Hasan bin Arafah 92 ni sahihi kwa ushahidi mwingi, na ina ushahidi wa Hadithi ya Anas kwa Ibn Hibbaar (7159).

15. Basi leo haitapokelewa kwenu kikomboleo, wala kwa wale walio kufuru. Makaazi yenu ni Motoni, ndio bora kwenu; na ni marejeo maovu yalioje!

Siku ya Kiyama Waumini Watapewa Nuru, Kulingana na Amali zao Njema

Allah تعالی Anaeleza kuwa waumini waliotoa sadaka watakuja katika Siku ya Kiyama huku nuru ikiwatangulia mbele katika eneo la kukusanywa watu kulingana na daraja ya amali zao njema. Kama ilivyosimuliwa kutoka kwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه:

يَسْعَى نُورُهُمْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ

"...**nuru yao iko mbele yao...**" Amesema, "Watapita juu ya *Sirat* kulingana na amali zao. Baadhi yao watakuwa na nuru kubwa kama mlima, wengine kama mtende, wengine kama ukubwa wa mtu akiwa amesimama. Nuru ndogo kati ya hizo itakuwa sawa na ukubwa wa kidole cha shahada, inayowaka wakati mwingine na kuzimika wakati mwingine." Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى waliikusanya Hadithi hii.¹

Adh-Dhahhak ametoa rai juu ya Aya, "Kila mmoja atapewa nuru katika Siku ya Kiama. Watakapofika katika *Sirat*, nuru zao wanafiki zitazimika. Waumini watakapoona hilo, watadhania kuwa nuru zao pia zitazimika, kama nuru za wanafiki. Hapo ndipo waumini watakapomuomba Allah تعالی, '**Ewe Mola Wetu Mlezi! Tutimizie nuru yetu.**'" Kauli ya Allah تعالی,

وَأَيَّمَنِ

"...**na kuliani kwao...**" Adh-Dhahhak amesema: "Vitabu vyao vya kumbukumbu."² Kama Kauli ya Allah تعالی:

فَمَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ

"...basi atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia..."
(17:71)

Kauli ya Allah تعالی,

¹ At-Tabari 23:179.

² At-Tabari 23:179.

بُشِّرْكُمْ الْيَوْمَ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Furaha yenu leo - Bustani zipitazo mito kati yake...”

Inamaanisha, wataambiwa, “Pokeeni habari njema Leo, kuhusu bustani zipitazo mito chini yake.”

خَالِدِينَ فِيهَا

“...mtakaa humo milele.” Maana yake: Mtaishi humo milele.

ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

“Huko ndiko kufuzu kukubwa.”

Hali za Wanafiki Siku ya Kufufuliwa (Kiyama)

Kauli ya Allah تعالى،

يَوْمَ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالْمُنَافِقَاتُ لِلَّذِينَ آمَنُوا انظُرُونَا نَقْتَبِسْ مِنْ نُورِكُمْ

“Siku wanafiki wanaume na wanafiki wanawake watapowaambia walioamini: Tungojeni ili tupate mwangaza kutoka katika nuru yenu.’

Allah تعالى Anatuambia katika Aya hii kuhusu matukio ya kutisha, na matetemeko makubwa yakiwa ni baadhi ya mambo makubwa yatakayotokea Siku ya Kiyama katika Eneo la Mkusanyiko wa watu. Hakuna atakayenusurika katika Siku hiyo, isipokuwa waliomuamini Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ, wakatii amri za Allah تعالى na wakaepuka makatazo Yake. Al-’Awfi, Adh-Dhahhak na wengine wamesimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: “Watu watakapokuwa wamekusanyika gizani, Allah تعالى Atapeleka nuru, na waumini watakapoona nuru wataiendea. Nuru hiyo itawaongoza kutoka kwa Allah تعالى kwenda Peponi. Wanafiki watakapowaona waumini wakifuata nuru, watawafuata. Hata hivyo, Allah تعالى Atawazimishia nuru wanafiki na watasema (kuwaambia waumini),

انظُرُونَا نَقْتَبِسْ مِنْ نُورِكُمْ

“Tungojeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu.”

Waumini watawajibu kwa kusema,

أَرْجِعُوا وَرَاءَكُمْ

“Rejeeni nyuma yenu...”¹ Gizani mlipokuwa, na muingojee nuru huko!” Kauli ya Allah تعالى،

فَضْرِبَ بَيْنَهُمْ سُورَ لَهْدٍ بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ مِنْ قِبَلِهِ الْعَذَابُ

‘Utiwe baina yao ukuta wenye mlango - ndani yake mna Rehema, na nje upande wake wa mbele kuna Adhabu.’

Al-Hasan na Qatadah wamesema kuwa ukuta uliotajwa hapa upo baina ya Peponi na Jahanamu.² ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin aslam amesema kuwa ukuta uliotajwa katika Aya hii ni ukuta Alioueleza Allah تعالى katika Kauli Yake،

وَبَيْنَهُمَا حِجَابٌ

“Na baina ya makundi mawili hayo patakuwapo pazia.” (7:46)³

Maelezo sawa na hayo yamesimuliwa kutoka kwa Mujahid na wengine⁴ na ni sahihi. Kauli ya Allah تعالى،

بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ

“...ndani yake mna Rehema...” Inamaanisha, Pepo na vyote vilivyomo humo.

وَظَاهِرُهُ مِنْ قِبَلِهِ الْعَذَابُ

“...na nje upande wake wa mbele kuna Adhabu.” Inamaanisha, Jahanamu, kwa mujibu wa Qatadah, Ibn Zayd na wengine.⁵ Kauli ya Allah تعالى،

يُنَادُوهُمْ أَلَمْ نَكُنْ مَعَكُمْ

“Watawaita wawaambie: Kwani vile hatukuwa pamoja nanyi?”

Yaani, wanafiki watawaita waumini kwa kusema, “Je, hatukuwa pamoja nanyi katika maisha ya duniani, tukihudhuria Sala za Ijumaa na za Jamaa. Je,

¹ At-Tabari 23:182.

² At-Tabari 23:182, na Ibn Abi Shaybah 13:175.

³ At-Tabari 23:183.

⁴ At-Tabari 23:182.

⁵ At-Tabari 23:184.

hatukusimama pamoja nanyi katika Mlima 'Arafah (wakati wa Hajj), kushiriki vitani katika upande wenu na kufanya vitendo vyote vya ibada pamoja nanyi?"

قَالُوا بَلَىٰ

“Watawaambia: Ndiyo...”

Waumini watawajibu wanafiki kwa kusema, “Ndiyo, mlikuwa pamoja nasi,

وَلَكِنَّكُمْ فَتَنْتُمْ أَنْفُسَكُمْ وَتَرَبَّصْتُمْ وَارْتَبْتُمْ وَغَرَّتْكُمُ الْأَمَانِيُّ

“...lakini mlifitini wenyewe, na mkasitasita, na mkatia shaka, na matamania ya nafsi zenu yakakudanganyeni...”

Qatadah amesema,

وَتَرَبَّصْتُمْ

“...na mkasitasita...” “Juu ya ukweli na watu wake.”

وَارْتَبْتُمْ

“...na mkatia shaka...” Kuwa kuna kufufuliwa baada ya mauti.

وَعَرَّتْكُمْ الْأَمَانِيُّ

“Na matamania ya nafsi zenu yakakudanganyeni.”

Inamaanisha: Mlisema kuwa mtasamehewa madhambi yenu; au, watasema: dunia imekuhadaeni.

حَتَّىٰ جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ

“Mpaka ilipokuja Amri ya Mwenyezi Mungu.”

Inamaanisha: mkaendelea hivyo mpaka mauti yakakufikieni.

وَعَرَّكُمْ بِاللَّهِ الْغُرُورُ

“Na mdanganyifu akakudanganyeni msimfuate Mwenyezi Mungu.”

Shetani 'Ighai.¹ Qatadah amesema, “Walidanganywa na Shetani Wallahi! Waliendelea kudanganywa mpaka Allah تعالی Akawatupia Motoni.”²

¹ At-Tabari 23:185.

² At-Tabari 23:185.

Maana ya maneno hayo ni kuwa waumini watawajibu wanafiki kwamba, “Mlikuwa pamoja nasi kimwili bila ya nia, wala nyoyo. Mlikuwa na shaka. Mlikuwa mkijionesha kwa watu na kumtaja Allah تعالی kidogo sana.”

Mujahid alitoa rai, “Wanafiki walikuwa pamoja na waumini duniani, wakioana baina yao, lakini wakiwasaliti hata walipokuwa wakishirikiana nao. Walikuwa wafu. Makundi mawili hayo yatapewa nuru katika Siku ya Kiama, lakini nuru ya wanafiki itazimwa watakapoufikia ukuta; hayo ni pindi kambi mbili hizo zitakapotenganishwa!”¹

Kauli ya Allah تعالی،

مَأْوَانِكُمُ النَّارُ ط

“Makaazi yenu ni Motoni.”

Inamaanisha Motoni ndio kituo chenu cha mwisho na humo ndipo mtakapokwenda kuishi.

هِيَ مَوْلَانِكُمْ ط

“...ndio bora kwenu.”

Inamaanisha, ni mahali panapokustahikini zaidi kuliko makazi mengine yoyote, kwa sababu ya ukafiri wenu na shaka, na Moto ni mbaya mno kuwa Makazi ya mwisho.

* * *

¹ At-Tabari 23:184.

* أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ وَلَا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ ۗ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَيَسْقُوتَ ۖ
 ۞ أَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمْ
 الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ۞ ۞ إِنَّ الْمُضْطَرِّقِينَ وَالْمُضْطَرِّقَاتِ
 وَأَقْرَضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا يُضَعَّفُ لَهُمْ ۗ وَلَهُمْ أَجْرٌ كَرِيمٌ
 ۞ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ ۗ
 وَالشُّهَدَاءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ لَهُمْ أَجْرُهُمْ وَنُورُهُمْ ۗ وَالَّذِينَ
 كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ۞
 أَعْلَمُوا أَنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ ۗ وَهُوَ زِينَةٌ وَتَفَاخُرٌ
 بَيْنَكُمْ وَتَكَاثُرٌ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ ۗ كَمَثَلِ غَيْثٍ أَعْجَبَ
 الْكُفَّارَ نَبَاتُهُ ثُمَّ يَهِيجُ فَتَرَاهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَكُونُ حُطَمًا ۗ
 وَفِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۗ وَمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٌ ۗ وَمَا
 الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ۞ ۞ سَابِقُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ
 مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أُعِدَّتْ
 لِلَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۗ ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن
 يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ۞

* أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ تَخْشَعَ
 قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ
 وَلَا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ
 قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْأَمَدُ فَقَسَتْ
 قُلُوبُهُمْ ۗ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَيَسْقُوتَ ۖ
 ۞ أَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ
 مَوْتِهَا ۗ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ
 تَعْقِلُونَ ۞

16. Je! Wakati haujafika bado kwa walioamini zikanyenyeka nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyo teremka? Wala wasiwe kama waliopewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa waovu.

17. Jueni kwamba Mwenyezi Mungu Huifufua ardhi baada ya kufa kwake.

Tumekubainishieni Ishara ili mpate kuzingatia.

Kuhimizwa Unyenyekevu na Katazo la Kuwaiga Watu wa Kitabu

Allah تعالی Anauliza, 'Je, haujafika wakati kwa nyoyo za waumini kulainika kwa kumtaja Allah تعالی na kusikiliza Qur'an, ili waifahamu, washikamane nayo, na kuifuata. Imamu Muslim amenukuu kuwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه amesema, "Miaka minne tu ilipita baina ya kusilimu kwetu na kuteremshwa Aya hii, ambamo Allah تعالی Ametukaripia,

أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ

"Je! Wakati haujafika bado kwa walioamini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu..."

Imamu Muslim aliikusanya karibu na mwisho wa kitabu chake.¹ An-Nasa'i pia aliikusanya Hadithi hii katika Tafsir ya Aya hii.² Kauli ya Allah تعالی,

وَلَا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ

"Wala wasiwe kama waliopewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu..."

Allah تعالی Anawakataza waumini kutokuwaiga wale waliopewa Kitabu kabla yao, Wayahudi na Manaswara. Kadiri muda ulivyokwenda, walibadili Kitabu cha Allah تعالی walichokuwa nacho, na wakakiuza kwa thamani ndogo kabisa. Pia walikiacha Kitabu cha Allah تعالی nyuma yao wakafuata rai za kubuni pamoja na itikadi potofu. Wakawaiga watu katika dini ya Allah تعالی, na kuwafanya mapadri na watawa wao kuwa miungu badala ya Allah تعالی. Wakati huo huo, nyoyo zao zikawa ngumu na hawakukubali mawaidha; nyoyo zao hazikulainikia kwa ahadi wala kwa vitisho vya Allah تعالی

وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَنَسِقُونَ

"...na wengi wao wakawa wapotovu."

Maana yake: Kwa vitendo; kwa hiyo, nyoyo zao zikaharibika na amali zao kubatilika. Kama Allah تعالی Alivyosema:

¹ Muslim 4:2319.

² An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:481.

فِيمَا نَقَضِهِمْ مِيثَاقَهُمْ لَعَنَّاهُمْ وَجَعَلْنَا قُلُوبَهُمْ قَاسِيَةً يُخَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَن مَّوَاضِعِهِ
وَنَسُوا حَظًّا مِمَّا ذُكِّرُوا بِهِ ۗ

“Basi kwa sababu ya kuvunja ahadi yao Tuliwalaani, na Tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu. Wanayabadilisha maneno kutoka pahala pake, na wamesahau sehemu ya yale waliyokumbushwa.” (5:13)

Inamaanisha: Nyoyo zao ziliharibika na kuwa ngumu, na tabia yao ikawa kupotosha Maneno ya Allah تعالی mbali na maana yake halisi. Wakaacha ibada walizoamrisha na wakafanya waliyoharamishiwa. Ndio sababu Allah تعالی Aliwakataza waumini kuwaiga kwa namna yoyote, kwa mambo ya kimsingi au ya tanzu.

Allah تعالی Amesema,

اعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ سَمِيُّ الْأَرْضِ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٥٧﴾

“Jueni kwamba Mwenyezi Mungu Huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Tumekubainishieni Ishara ili mpate kuzingatia.”

Aya hii inaashiria kuwa Yeye Hulainisha nyoyo baada ya kuwa ngumu. Huwaongoza waliotatizika baada ya kupotoka, na Huondoa tabu baada ya kuzidi. Basi, kama Allah تعالی Anavyofufua wafu na ardhi kavu kwa Kupeleka mvua nyingi iliyohitajika, pia Huzipa uongofu nyoyo ngumu kwa dalili na hoja za Qur’an. Pia Huzipa nuru (ya imani) baada ya kughafilika, na kutokuweza kufikiwa na uongofu. Sifa zote njema pamoja na shukurani ni Zake Mwenye Kumpa uongofu Amtakaye baada ya kupotoka, Anayemuacha apotee yule ambaye kabla ya hapo alikuwa ameongoka. Kwa hakika, ni Yeye Hufanya Atakacho na Yeye ni Mwingi wa Hekima, Muadilifu katika yote Ayafanyayo, Mpole Kuliko Wote, Mjuzi Kuliko Wote, Mkubwa Kuliko Wote, Aliye Juu kabisa Kuliko Wote.

إِنَّ الْمُصَدِّقِينَ وَالْمُصَدِّقَاتِ وَأَقْرَضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا يَضَعْفُ لَهُمْ وَلَهُمْ أَجْرٌ كَرِيمٌ
﴿٥٨﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ ۗ وَالشُّهَدَاءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ لَهُمْ
أَجْرُهُمْ وَتُورَهُمْ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿٥٩﴾

18. Kwa hakika wanaume wanaotoa sadaka, na wanawake wanaotoa sadaka, na wakamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, watazidishiwa maradufu na watapata malipo makubwa.

19. Na waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, hao ndio Masidiqi na Mashahidi mbele ya Mola Wao Mlezi. Wao watapata malipo na nuru yao. Na waliokufuru na wakakadhibisha Aya Zetu, hao ndio watu wa Motoni.

Malipo ya Watoa Sadaka, Waumini wa Kweli na waliokufa Shahidi, na Makazi ya Makafiri

Allah تعالى Anaeleza malipo Atakayowapa wale waliotoa mali zao, ima awe mwanamume au mwanamke, kuwapa wenye haja, mafakiri na maskini,

وَأَقْرَضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا

“Na wakamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema...”

Maana yake: Wanatoa sadaka kwa moyo mkunjiufu ili kutafuta radhi za Allah تعالى. Hawatafuti kulipwa wala kushukuriwa na waliowapa. Kauli ya Allah تعالى.

يُضَعَفُ لَهُمْ

“Watazidishiwa maradufu...”

Kwa maana kwamba Yeye Atawazidishia mpaka mara kumi ya mfano wake mpaka mara mia saba na hata zaidi.

وَلَهُمْ أَجْرٌ كَرِيمٌ

“...na watapata malipo makubwa.”

Maana yake: Malipo mema, mazuri, na marejeo mema na makazi matukufu. Kauli ya Allah تعالى,

وَالَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّٰدِقُونَ^ط

“Na waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, hao ndio Masidiqi...”

Ibara hii inakamilisha maelezo kuhusu waliomuamini Yeye na Mitume Wake, kwa kuwagawa katika makundi ya *as-Siddiqun*, waumini wa kweli. Al-'Awf amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuhusu,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۖ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّٰدِقُونَ^ط

“Na walio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, hao ndio Masidiqi...”

Kwamba maana yake haiendelei katika Aya inayofuatia,

وَالشُّهَدَاءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ لَهُمْ أَجْرُهُمْ وَنُورُهُمْ^ط

“...na Mashahidi mbele ya Mola Wao Mlezi. Wao watapata malipo yao na nuru yao.”¹

Abu Adh-Dhuha alisoma,

أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّٰدِقُونَ^ط

“...hao ndio Masidiqi...” Akatulia kidogo, akaendelea kusoma:

وَالشُّهَدَاءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ

“...na Mashahidi mbele ya Mola Wao Mlezi.”²

Masruq, Adh-Dhahhak, Muqatil bin Hayyan na wengine wamesema sawa na hivyo. Al-A'mash amesimulia kutoka kwa Abu Adh-Dhuha kutoka kwa Masruq kutoka kwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه aliyetoa rai juu ya Kauli ya Allah تعالى،

أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّٰدِقُونَ^ط وَالشُّهَدَاءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ

“...hao ndio Masidiqi na Mashahidi mbele ya Mola Wao Mlezi.”

“Wao ni makundi matatu.” Inamaanisha kuna wanaotoa sadaka, *Siddiqun* na waliokufa shahidi. Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَٰئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصَّٰدِقِينَ

وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّٰلِحِينَ^ع

¹ At-Tabari 23:191.

² At-Tabari 23:191.

“Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wako pamoja na wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema.” (4:69)

Kwa hiyo, Allah تعالى Ametofautisha kati ya *Siddiqin* na waliokufa shahidi, kwa kumaanisha kuwa wao ni makundi mawili tofauti, kwa hivyo hakuna shaka kuwa *Siddiq* wana daraja ya juu zaidi kuliko waliokufa shahidi. Imamu Malik bin Anas رحمه الله تعالى amenukuu katika *Muwatta'* yake kutoka kwa Abu Sa'id Al-Khudri رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ أَهْلَ الْجَنَّةِ لَيَتَرَاءُونَ أَهْلَ الْعَرْفِ مِنْ قَوْمِهِمْ، كَمَا تَتَرَاءُونَ الْكُؤُكَبَ الدَّرِّيَّ الْغَائِبَ فِي الْأَفْقِ مِنَ الْمَشْرِقِ أَوْ الْمَغْرِبِ، لِتَفَاضِلِ مَا بَيْنَهُمْ»

“Hakika watu wa Peponi watatazamana na wakazi walioko katika majengo ya juu miongoni mwa watu wao, kama mtu anavyotazama nyota ing'aayo kwa mbali upande wa mashariki au magharibi katika upeo wa macho, kwa sababu ya ubora wao baina yao.”

Kwa hayo, watu wakauliza, “Ewe Mjumbe wa Allah! Je, Majengo hayo marefu ni kwa ajili ya Mitume ambao hakuna wa kuwafikia?” Mtume ﷺ akajibu,

«بَلَى، وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، رِجَالٌ آمَنُوا بِاللَّهِ وَصَدَّقُوا الْمُرْسَلِينَ»

“Hapana! Naapa kwa Ambaye nafsi yangu imo Mkononi Mwake! Hayo ni kwa ajili ya watu wanaomuamini Allah na wakawaamini Mitume.”

Al-Bukhari na Muslim pia waliikusanya Hadithi hii.¹ Kauli ya Allah تعالى،

وَالشُّهَدَاءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ

“...na Mashahidi mbele ya Mola Wao Mlezi.”

Yaani, watakuwa katika bustani za Peponi, kama ilivyonukuliwa katika Sahih:

«إِنَّ أَرْوَاحَ الشُّهَدَاءِ فِي حَوَاصِلِ طَيْرٍ خَضِرٍ تَسْرَحُ فِي الْجَنَّةِ حَيْثُ شَاءَتْ، ثُمَّ تَأْوِي إِلَى تِلْكَ الْقَنَادِيلِ فَاطَّلَعَ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ اطَّلَاعَةً فَقَالَ: مَاذَا تُرِيدُونَ؟ فَقَالُوا: نُحِبُّ أَنْ

¹ *Fat'h Al-Bari* 6:368, *Muslim* 4:2177.

تَرَدُّنَا إِلَى الدَّارِ الدُّنْيَا فَتَقَاتِلَ فِيكَ فَتُقْتَلَ، كَمَا قُتِلْنَا أَوَّلَ مَرَّةٍ، فَقَالَ: إِنِّي قَدْ قَضَيْتُ
أَنَّهُمْ إِلَيْهَا لَا يَرْجِعُونَ»

*'Roho za waliokufa shahidi zinaishi katika miili ya ndege wa kijani, wanaoruka popote wanapotaka Peponi, halafu wanarejea katika viota vyao katika mashada. Mola Wako Mlezi Atakapowatazama mtazamo na Kuwauliza, 'Kuna chochote mnachotaka.' Watasema, "Tunatamani kuwa Uturejeshe duniani, ili tukapigane kwa ajili Yako na kuuliwa kama tulivyouliwa hapo awali." Allah Atawaambia: Nimeshapitisha Uamuzi kuwa hamtarejeshwa huko.'*¹

Kauli ya Allah تعالى،

لَهُمْ أَجْرُهُمْ وَنُورُهُمْ^ط

“Wao watapata malipo yao na nuru yao.” Yaani, kuwa Allah تعالى Atawapa wao malipo mazuri na nuru kubwa itakayowatangulia mbele yao. Katika hili, waumini wanatofautiana kuhusu kiwango cha malipo watakatayopata, kulingana na amali zao njema duniani. Imamu Ahmad amenukuu kuwa ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه amesema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«الشَّهَدَاءُ أَرْبَعَةٌ: رَجُلٌ مُؤْمِنٌ جَيِّدُ الْإِيمَانِ، لَقِيَ الْعَدُوَّ فَصَدَّقَ اللَّهَ فَقُتِلَ، فَذَلِكَ
الَّذِي يَنْظُرُ النَّاسُ إِلَيْهِ هَكَذَا»

“Mashahidi wapo wa aina nne, kuna Muumini mkweli katika imani yake, anayekabiliana na adui (vitani), anatimiza wajibu wake kwa Allah na akauliwa. Huyu ni ambaye watu watamuona hivyo.”

Mtume ﷺ akainua kichwa chake mpaka kofia yake ikaanguka kutoka kichwani kwake, na ya ‘Umar pia ikaanguka. Mtume ﷺ aliendelea kusema,

«وَالثَّانِي مُؤْمِنٌ لَقِيَ الْعَدُوَّ فَكَأَنَّمَا يُضْرَبُ ظَهْرُهُ بِسَوْكِ الطَّلْحِ، جَاءَهُ سَهْمٌ غَرِبَ
فَقَتَلَهُ، فَذَلِكَ فِي الدَّرَجَةِ الثَّانِيَةِ. وَالثَّالِثُ رَجُلٌ مُؤْمِنٌ خَلَطَ عَمَلًا صَالِحًا وَآخَرَ
سَيِّئًا، لَقِيَ الْعَدُوَّ فَصَدَّقَ اللَّهَ حَتَّى قُتِلَ، فَذَلِكَ فِي الدَّرَجَةِ الثَّالِثَةِ. وَالرَّابِعُ رَجُلٌ
مُؤْمِنٌ أَشْرَفَ عَلَى نَفْسِهِ إِسْرَافًا كَثِيرًا، لَقِيَ الْعَدُوَّ فَصَدَّقَ اللَّهَ حَتَّى قُتِلَ، فَذَلِكَ فِي
الدَّرَجَةِ الرَّابِعَةِ»

¹Muslim 3:1502

“(Wa pili) ni muumini anayekabiliana na adui na anachomwa na mkuki uliopoteza shabaha na anakufa. Muumini huyo ni wa daraja la pili. Wa tatu ni muumini aliyechanganya amali njema na mbaya; anakabiliana na adui kwa ukweli katika wajibu wake kwa Allah mpaka anauliwa. Hili ni daraja la tatu. La nne ni muumini aliyefanya dhambi nyingi, huyo anakabiliana na adui na huku akiwa mkweli katika wajibu wake kwa Allah, na anauliwa. Hili ni daraja la nne.”¹

‘Ali bin Al-Madini pia alisimulia Hadithi hii na kusema, “Isnadi hii ya Kimisri inayofaa.”² At -Tirmidhi amesema, “*Hasan Gharib*.”³ Kauli ya Allah تعالى,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ

“Na waliokufuru na wakakadhibisha Ishara Zetu, hao ndio watu wa Motoni.”

Allah تعالى Alipotaja makazi na hali za watu wema, amefuatisha kutaja hali na malipo ya watu waovu.

أَعْلَمُوا أَنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَهُوَ زِينَةٌ وَتَفَاخُرٌ بَيْنَكُمْ وَتَكَاثُرٌ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ كَمَثَلِ غَيْثٍ أَعْجَبَ الْكُفَّارَ نَبَاتُهُ ثُمَّ يَهِيجُ فَتَرَاهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَكُونُ حُطَمًا وَفِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٌ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿١٦﴾ سَابِقُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أُعِدَّتْ لِلَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ؕ ذَٰلِكُمْ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ؕ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿١٧﴾

20. Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na pumbao, na pambo, na kujifakhirisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake, kisha hunyauka ukayaona yamepiga manjano kisha yakawa mabua. Na akhera kuna adhabu kali na maghufira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu.

¹ Ahmad 1:23.

² 'Ilal Al-Hadith 1:349.

³ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 5:274. Kauli ya 'Ali bin Al-Madini inazingatia isnadi ipi imepitia. Wanazuoni wengi huichukulia Hadithi hiyo kuwa ni dhaifu.

21. Kimbilieni msamaha wa Mola Wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi, iliyowekewa waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake. Hiyo ndiyo Fadhila ya Mwenyezi Mungu, Humpa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kuu.

Maisha ya Dunia Hii ni Starehe Yenye Kupita

Allah تعالى Anaidhalilisha dunia na Kuiponda,

أَنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَهَوٌّ وَزِينَةٌ وَتَفَاخُرٌ بَيْنَكُمْ وَتَكَاثُرٌ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ

“...kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na pumbao, na pambo, na kujifakhirisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto.”

Yaani si vingine umuhimu wa dunia kwa watu wake upo katika taswira hiyo, kama Alivyosema katika Aya nyingine,

زُيِّنَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ وَالْقَنَاطِيرِ الْمُقَنْطَرَةِ مِنَ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ وَالْأَنْعَامِ وَالْحَرْثِ ۗ ذَلِكَ مَتَعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْبُ الْمَوْتَابِ ﴿١٤﴾

“Watu wamepambiwa matamania ya kupenda wanawake, na wana, na mirundiko ya dhahabu na fedha, na farasi asili, na mifugo, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema.” (3:14)

Allah تعالى Anapiga pia mfano wa dunia, si chochote isipokuwa ni kama ua lenye kunyauka na furaha zake huisha na neema zake kuondoka, kwa kusema ni,

كَمَثَلِ غَيْثٍ

“...kama mvua...” Ambayo huwanyeshea watu, baada ya wao kukata tamaa. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَهُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ الْغَيْثَ مِنْ بَعْدِ مَا قَنَطُوا وَيَنْشُرُ رَحْمَتَهُ ۗ وَهُوَ الْوَلِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٢٨﴾

“Naye Ndiye Anayeiteremsha mvua baada ya wao kuishakata tamaa, na Hueneza Rehema Yake. Naye Ndiye Mlinzi Mwenye Kushukuriwa.” (42:28)

Kauli ya Allah تعالى،

أَعْجَبَ الْكُفَّارَ نَبَاتُهُ

“...huwafurahisha wakulima mimea yake...”

Yaani wakulima kufurahia mimea inayoota baada ya ujio wa mvua. Na kama wakulima wanavyofurahia mimea, makafiri wanafurahia dunia. Kwa kuwa wao ni wenye pupa nayo na wenye kuipenda mno.

ثُمَّ يَهْجِعُ فَتْرَتَهُ مُضْفَرًا ثُمَّ يَكُونُ حُطَمًا

“...kisha hunyauka ukayaona yamepiga manjano kisha yakawa mabua.”

Inamaanisha, mara mimea hiyo hubadilika na kuwa rangi ya manjano, baada ya kuwa kijani kibichi. Baada ya hapo, rangi ya kijani inaondoka na kubaki mkavu wote. Huu ni mfano wa maisha ya duniani, huanza kwa ujana, halafu ukomavu na kisha uzee na udhaifu. Huu ndio mfano wa wanadamu duniani. Katika hatua ya mwanzo ya maisha, wanaonekana wakiwa vijana na wazuri. Taratibu, wanaanza kuzeeka, mwendo unabadilika na nguvu kuisha. Kisha wanazeeka. Kutembea kunashindikana kwao, huku wakishindwa kufanya mambo mepesi.

Allah تعالى Amesema,

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفًا وَشَيْبَةً يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ وَهُوَ الْعَلِيمُ الْقَدِيرُ ﴿٥٤﴾

“Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni kutokana na udhaifu Akajaalia nguvu baada ya unyonge, Akajaalia baada ya nguvu unyonge tena na ukongwe. Anaumba Atakavyo. Naye Ndiye Mjuzi, Mwenye uweza.” (30:54)

Mfano huu unajulisha kukaribia kuondoka dunia na mwisho wake, wakati ni kinyume chake, Akhera kwa hakika ipo.

Hivyo Ametahadharisha kuipenda sana dunia na Akahimiza kufanya mambo yale ya heri.

وَفِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٌ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ

“Na akhera kuna adhabu kali na maghufira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu.”

Yaani, kwa hakika, Akhera ambayo kwa hakika ipo, ina vitu viwili tu, ama adhabu kali au msamaha kutoka kwa Allah تعالى na radhi Zake. Allah تعالى Amesema,

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ

“Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu.”

Inamaanisha, dunia ni furaha yenye kuhadaa wenye kuipenda. Kwa hakika, wenye kuipenda sana dunia huifurahia na kudhania kuwa inawapenda, mpaka wanadhania kuwa hakuna maisha mengine isipokuwa hayo. Wakati dunia ni dhalili sana ikilinganishwa na Akhera. Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa ‘Abdullah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَللَّحْنَةِ أَقْرَبُ إِلَيَّ أَحَدِكُمْ مِنْ شِرَاكِ نَعْلِي، وَالنَّارُ مِثْلُ ذَلِكَ»

“Pepo iko karibu zaidi na mmoja wenu kuliko kamba za kiatu chake, na ndivyo pia ulivyo Moto.”¹

Al-Bukhari aliikusanya Hadithi hii kupitia simulizi ya Ath-Thawri.² Hadithi hii inaashiria ukaribu wa heri na shari kwa mwanadamu. Kwa ajili hiyo, Allah Mtukufu Amewahimiza wanadamu kukimbilia katika kufanya matendo mema na utii na kuepuka makatazo. Kwa kufanya hivyo, dhambi na makosa yao yatasamehewa na watapata malipo na utukufu. Allah تعالى Amesema,

سَابِقُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

“Kimbilieni msamaha wa Mola Wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi.”

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

¹ Ahmad 1:387.

² Fat'h Al-Bari 11:328.

وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٦﴾

“Na yakimbilieni maghufira ya Mola Wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyowekwa tayari kwa wachamungu.” (3:133)

Kauli ya Allah تعالى hapa,

أُعِدَّتْ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۗ ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ

الْعَظِيمِ ﴿١٧﴾

“...iliyowekwa waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake. Hiyo ndiyo Fadhila ya Mwenyezi Mungu, Humpa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kuu.”

Inamaanisha, “Sifa Alizowapambia Allah تعالى, ni katika Fadhila Zake, na neema na hisani kwao.” Tumetaja Hadithi iliyokusanywa katika Sahih ambamo wahamiaji maskini walimuambia Mtume ﷺ, “Ewe Mjumbe wa Allah! Matajiri watapata daraja za juu na furaha ya kudumu.” Yeye akawauliza,

«وَمَا ذَاكَ؟»

“Kwa nini hivyo?”

Wakasema, “Wao Wanasali kama sisi na wanafunga saumu kama sisi. Hata hivyo, wanatoa sadaka, ilhali sisi hatuwezi kufanya hivyo, na wanaacha huru watumwa, na sisi hatufanyi hivyo.” Mtume ﷺ akasema,

«أَفَلَا أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ إِذَا فَعَلْتُمْوَهُ سَبَقْتُمْ مِّن بَعْدِكُمْ، وَلَا يَكُونُ أَحَدٌ أَفْضَلَ مِنْكُمْ إِلَّا مَن صَنَعَ مِثْلَ مَا صَنَعْتُمْ: تُسَبِّحُونَ وَتُكَبِّرُونَ وَتُحَمِّدُونَ ذَبْرًا كُلَّ صَلَاةٍ ثَلَاثًا وَثَلَاثِينَ.»

“Je nikuambieni kuhusu amali njema ambayo, mkiifanya mtalingana na waliokutangulieni na hakuna wa kukupiteni na kuwa bora zaidi yenu, isipokuwa watakaofanya kama hivyo. Semeni, “Utukufu ni wa Allah,” “Allah ni Mkubwa Zaidi,” na “Kila sifa njema pamoja na shukurani Anastahiki Allah,” Mara thelathini na tatu baada ya kila Sala.”

Baadaye walirejea na kusema, "Ndugu zetu matajiri wamesikia tunachofanya na wao sasa wanafanya hivyo hivyo." Mtume ﷺ akasema,

«ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ»

*"Hizo ni fadhila za Allah ambazo Humpa Amtakaye."*¹

* * *

¹Muslim 1:416.

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِنْ قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا ۗ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾
 لِكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٢٣﴾ الَّذِينَ يَتَخَلَّوْنَ
 وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ ۗ وَمَنْ يَتَوَلَّ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَنِيُّ
 الْحَمِيدُ ﴿٢٤﴾ لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ
 الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيُقِيمُوا النَّاسَ بِالْقِسْطِ ۗ وَأَنْزَلْنَا
 الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ
 يَنْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ ۗ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٥﴾ وَلَقَدْ
 أَرْسَلْنَا نُوحًا وَإِبْرَاهِيمَ وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِمَا النُّبُوَّةَ
 وَالْكِتَابَ فَمِثْمُ مِثْمُتِهِمْ ۗ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَاسِقُونَ ﴿٢٦﴾ ثُمَّ
 قَفَّيْنَا عَلَىٰ آثَرِهِمْ بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ
 وَآتَيْنَاهُ الْإِنجِيلَ وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ رَأْفَةً
 وَرَحْمَةً وَرَهَابِيَّةً ابْتَدَعُوهَا مَا كَتَبْنَاهَا عَلَيْهِمْ إِلَّا ابْتِغَاءَ
 رِضْوَانِ اللَّهِ فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا ۗ فَآتَيْنَا الَّذِينَ آمَنُوا
 مِنْهُمْ أَجْرَهُمْ ۗ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَاسِقُونَ ﴿٢٧﴾ يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ
 آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَآمِنُوا بِرُسُلِهِ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِنْ
 رَحْمَتِهِ وَيَجْعَلْ لَكُمْ نُورًا تَمْشُونَ بِهِ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ
 وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٨﴾ لَقَلَّ يَعْلَمُ أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا
 يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَيْءٍ مِنَ فَضْلِ اللَّهِ ۗ وَأَنَّ الْفَضْلَ بِيَدِ اللَّهِ
 يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِنْ قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا ۗ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾
 لِكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٢٣﴾ الَّذِينَ يَتَخَلَّوْنَ
 وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ ۗ وَمَنْ يَتَوَلَّ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَنِيُّ
 الْحَمِيدُ ﴿٢٤﴾

22. Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla Hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.

23. Ili msihuzunike kwa kilichokupoteeni, wala msijitape kwa Alichokupeni. Na Mwenyezi Mungu Hampendi kila anayejivuna akajifakhi-risha.

24. Ambao wanafanya ubakhili, na wanaamrisha watu wafanye ubakhili. Na anayegeuka, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuji-tosha, Mwenye Kusifiwa.

Kila Kinachomfika Mwanadamu Kimeshakadiriwa na Allah تعالى

Allah تعالى Anakumbushia Kudura Yake na Uamuzi juu ya vitu vyote kabla Kuumbwa viumbe,

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ

“Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu...”

Maana yake: ‘Hakuna kinachokufika au kutokea,’

إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا

“...ila umekwishaandikwa katika Kitabu kabla hatujauumba.”

Maana yake: ‘Kabla Hatujawaumba viumbe na kuanza maisha yao.’ Qatadah ametoa rai juu ya Aya hii,

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ

“Hautokei msiba katika ardhi...” Kwa maana ya njaa.

وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ

“...wala katika nafsi zenu...” Inakusudia, “taabu na maradhi.” Pia amesema, “Tuliambiwa kuwa kila anayechomwa na mwiba, kutenguka kifundo, au kuvuja damu, kutokana na dhambi zake. Anachosamehe Allah تعالى ni kikubwa zaidi.”¹

Ayah hiyo tukufu inaleta ushahidi waziwazi wa kupotoka kwa madhehebu ya *Qadariyyah*, wanaokanusha Kudura ya Allah تعالى na Ujuzi Wake juu ya kila kitu kabla havijatokea. Imamu Ahmad amenukuu kuwa ‘Abdullah bin ‘Amr bin Al-‘As amesema, “Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«قَدَّرَ اللَّهُ الْمَقَادِيرَ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِخَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ»

“Allah Amekadiria vipimo (vya kila kitu) kwa miaka khamsini kabla ya Kuumba mbingu na dunia.”²

Imamu Muslim aliikusanya Hadithi hii katika Sahih yake pamoja na nyongeza:

¹ At-Tabari 23:196.

² Ahmad 2:169.

«وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ»

“Na Arshi Yake ilikuwa juu ya maji.”

At -Tirmidhi pia aliihusanya na kusema, “Hasan Sahih.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

“Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.”

Inamaanisha kuwa Yeye Anajua vitu vyote kabla havijatokea, na Anaviandika sawasawa kabisa kwa namna vinavyotokea wakati wa kutokea, na hilo ni jepesi Kwake. Kwa hakika, Allah تعالى Anajua kilichotokea, kitakachotokea na ambacho hakikutokea, na umbo litakalotokea kama litatokea.

Kuamrisha kuwa na Subira na Shukrani

Kauli ya Allah تعالى،

لِكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ

“Ili msihuzunike kwa kilichokupoteeni, wala msijitape kwa Alichokupeni.”

Inamaanisha, ‘Tulikujulisheni kuhusu Elimu Yetu yenye kuenea, Kuandika vitu vyote kabla ya kutokea na Kuumba vitu vyote kwa kipimo Tunachokijua Sisi, ili mtambue kuwa kilichokusibuni kisingekukoseni. Kwa hiyo, msihuzunike mlichokikosa, kwa sababu kama mngekuwa mmeandikiwa, mngekipata.’ (Pia husomwa);

(وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ)

“...wala msijitape kwa Alichokupeni...”

Inamaanisha, kilichokufikieni. Kwa mujibu wa usomaji huo, inamaanisha

ءَاتَاكُمْ

“...kwa Alichokupeni.” Maana yake: Zote mbili ni sawa.

¹ Muslim 4:2044, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:370.

Allah تعالیٰ hapa Anasema, 'Msijifaharisha mbele za watu kuhusu Alichoku neemesheni Allah تعالیٰ, kwa sababu si nyinyi mlikipata kwa juhudi zenu. Bali, yote hayo yalikuja kwasababu Allah تعالیٰ Amejaalia kwenu na Amekupeni kama riziki. Kwa hiyo, msitumie Alichokupeni Allah تعالیٰ kama sababu ya kujifaharisha na kuwafanyia wengine ujeuri.' Kwa kuzingatia hilo Allah تعالیٰ Amesema,

وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ

“Na Mwenyezi Mungu Hampendi kila anayejivuna akajifakhirisha.”

Inamaanisha, wanaowafanyia watu ujeuri.

'Ikrimah ametoa rai kwa kusema, “Kila mmoja wetu hupata furaha na huzuni. Hata hivyo, furaha yako ifanye kwa kushukuru na unapopatwa na huzuni uwe na subira.”¹

Kukatazwa kwa Ubakhili

Allah تعالیٰ Akasema,

الَّذِينَ يَبْخُلُونَ وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ

“Ambao wanafanya ubakhili, na wanaamrisha watu wafanye ubakhili.”

Inamaanisha wenye kufanya uovu na kuwashajiisha watu kuufanya,

وَمَنْ يَتَوَلَّ

“Na anayegeuka...” Dhidi ya kushikamana na amri za Allah تعالیٰ na kuzitekeleza,

فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ

“...basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujitosha, Msifiwa.” Kama Nabii Musa عليه السلام alivyosema,

إِنْ تَكْفُرُوا أَنْتُمْ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَأِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ

“Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitosha, Msifiwa.” (14:8)

¹ At-Tabari 23:1.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيُقِيمُوا النَّاسَ بِالْقِسْطِ
 وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَن يَنْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ
 إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٥٧﴾

25. Kwa hakika Tuliwatuma Mitume Wetu kwa dalili waziwazi, na Tukateremsha Kitabu pamoja nao na mzani, ili watu wasimamie uadilifu, na Tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu, na ili Mwenyezi Mungu Amjue anayemnusuru Yeye na Mitume Wake kwa ghaibu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu Mwenye Kushinda.

Mitume Walipewa Miujiza na Walitumwa na Ukweli na Haki

Allah تعالیٰ Amesema tena,

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ

“Kwa hakika Tuliwatuma Mitume Wetu kwa dalili waziwazi...”

Kuhusu miujiza, dalili zisizopingika na shuhuda za wazi,

وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ

“...na Tukateremsha Kitabu pamoja nao...” Nacho ni maandiko ya kweli,

وَالْمِيزَانَ

“...na Mizani...”

Huo ni uadilifu, kwa mujibu wa Mujahid, Qatadah na wengine.¹ Aya hii inarejea katika ukweli uliohibitishwa na akili sahihi zilizonyooka zenye kupingana na rai zilizopotoka. Kama Alivyosema Allah تعالیٰ katika Aya nyingine,

أَفَمَنْ كَانَ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّهِ

**“Basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola Wake Mlezi,...”
(11:17),**

¹ At-Tabari 23:200.

Allah تعالى Amesema;

فَطَرَتَ اللَّهُ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا

“...umbile la Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu.” (30:30) Na,

وَالسَّمَاءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ الْمِيزَانَ

“Na mbingu Ameziinua, na Ameweka mizani.” (55:7)

Ndio sababu Allah تعالى Amesema hapa,

لِيُقِيمَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ

“...ili watu wasimamie uadilifu...”,

Ukweli na uadilifu ulio katika kuwatii Mitume, katika yote waliyofikisha kutoka kwa Mola Wao Mlezi, na kufuata yote waliyoamrisha. Kwa hakika, walicholeta Mitume ni kweli, ambayo zaidi yake hakuna kweli nyingine.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى,

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

“Na yametimia Maneno ya Mola Mlezi Wako kwa kweli na uadilifu.” (6:115),

Neno Lake ni kweli katika yote wanayofikisha Mitume Wake, na Muadilifu katika Amri na Makatazo Yake yote. Ndio sababu waumini, watakapochukua nafasi zao Peponi na vyumba vya juu na viti vilivyopangwa safu, watasema,

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي هَدَانَا لِهَذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَنْ هَدَانَا اللَّهُ لَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ

“Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, Ambaye Ametuongoza kufikia haya. Wala hatukuwa wenye kuongoka wenyewe ingelikuwa Mwenyezi Mungu Hakutuongoza. Hakika Mitume wa Mola Wetu Mlezi walileta haki.” (7:43)

Faida za Chuma

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ

“...na Tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi...”

Inamaanisha, ‘Tumekifanya chuma cha kuwazuia wenye kukataa ukweli na kuupinga baada ya kuletwa ushahidi.’ Na kwa kuzingatia hilo, Mtume ﷺ aliishi Makka kwa miaka kumi na tatu baada ya kupewa Utume. Katika wakati huo, ufunuo uliendelea kumteremkia na hoja nyingi dhidi ya washirikina na kueleza Tawhid kwa kina na ushahidi. Ushahidi ulipowekwa dhidi ya waliomkataa Mtume, Allah تعالى Alijaalia Hijrah. Akawaamuru waumini kuwapiga makafiri kwa kutumia panga, kwa kuwatuma kukata shingo za waliopinga, kukataa na kukadhibisha Qur’an. Imamu Ahmad na Abu Dawud wamenukuu kuwa ‘Abdullah bin ‘Umar رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«بُعِثْتُ بِالسِّنْفِ بَيْنَ يَدَيْ السَّاعَةِ حَتَّى يُعْبَدَ اللَّهُ وَخَذَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَجُعِلَ رِزْقِي
تَحْتَ ظِلِّ رُمْحِي، وَجُعِلَ الذَّلَّةُ وَالصَّغَارُ عَلَى مَنْ خَالَفَ أَمْرِي، وَمَنْ تَشَبَهَ بِقَوْمٍ
فَهُوَ مِنْهُمْ»

“Nimetumwa na upanga kabla ya ile Saa, ili Allah Aabudiwe Peke Yake bila ya mshirika. Riziki yangu imewekwa chini ya kivuli cha mkuki wangu, na udhalili na unyonge umefanywa kwa mwenye kukataa amri yangu na mwenye kujishabihisha na watu ni mmoja wao.”¹

Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ

“...chenye nguvu...”

Maana yake: Kwa kutengeneza silaha, kama panga, visu, mishale, ngao na silaha nyingine mbalimbali.

¹ Ahmad 2:50, Abu Dawud 4:314.

وَمَنْفَعُ لِلنَّاسِ

“...na manufaa kwa watu...”

Maana yake: Katika maisha yao, kwa kukitumia kutengenezea sarafu, nyundo, shoka, chezo misumeno, sepetu na vitu vingine vya matumizi kwa kulimia, kupandia mbegu, kupikia, kuokea na vitu vingine vya lazima maishani mwao. Kauli ya Allah تعالى،

وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ

“...ili Mwenyezi Mungu Amjue Anayemnusuru Yeye na Mitume Wake kwa ghaibu.”

Inamaanisha, wenye nia ya kushika silaha kwa ajili ya kunusuru (Dini ya) Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ،

إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٦﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu Mwenye Kushinda.”

Maana yake: Kwa hakika, Allah تعالى ni Mwenye Nguvu, Mwenye Uweza, na Huwapa ushindi wenye Kumpa ushindi na Kumnusuru (kwa maana ya Dini yake). Hata hivyo, Allah تعالى Hahitaji msaada wa wanadamu, bali Aliamrisha Jihad ili Kuwajaribu watu wao kwa wao.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا وَإِبْرَاهِيمَ وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِمَا النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ فَمِمْهُمْ مُهْتَدٍ
وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَسَقُونَ ﴿٢٧﴾ ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلَىٰ آثَارِهِم بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ
وَأَتَيْنَاهُ الْإِنجِيلَ وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ رَأْفَةً وَرَحْمَةً وَرَهَابِيَّةً ابْتَدَعُوهَا مَا
كَتَبْنَاهَا عَلَيْهِمْ إِلَّا ابْتِغَاءَ رِضْوَانِ اللَّهِ فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا فَفَاتِنَا الَّذِينَ آمَنُوا
مِنْهُمْ أَجْرَهُمْ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَسَقُونَ ﴿٢٨﴾

26. Na bila ya shaka Tulimtuma Nuhu na Ibrahim, na Tukaweka katika kizazi chao Unabii na Kitabu. Basi wapo miongoni mwao walioongoka, na wengi katika wao ni wapotovu.

27. Tena Tukafuatisha nyuma yao Mitume wengine, na Tukamfuatisha Isa bin Mariamu, na Tukampa Injili. Na Tukajaalia katika nyoyo za waliomfuata upole na rehema. Na uruhubani (utawa wa mapadri) wameuzua wao. Sisi Hatukuwaandikia hayo, ila kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuufuata inavyotakiwa kuufuata. Basi wale walioamini katika wao Tuliwapa ujira wao. Na wengi wao ni wapotovu.

Wengi katika Umati wa Mitume Walikuwa Waasi

Allah تعالى Anaeleza kwamba tangu Alipomtuma Nuh عليه السلام, Mitume wote Aliowatuma baada ya hapo walitoka katika uzao wake. Vitabu vyote vilivyoshuka na Mitume wote waliopata ufunuo baada ya Ibrahim, Khalil wa Allah عليه السلام, walikuwa wa uzao wa Ibrahim عليه السلام.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine:

وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

“Na Tukajaalia katika dhuria Yake Unabii na Kitabu...” (29:27)

Wa mwisho katika Mitume wa Wana wa Israil alikuwa 'Isa, mwana wa Mariam عليه السلام, alieleza habari njema za kuja Muhammad ﷺ. Allah تعالى Amesema,

ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلَىٰ آثَارِهِم بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَآتَيْنَاهُ الْإِنْجِيلَ

‘Tena Tukafuatisha nyuma yao Mitume wengine, na Tukamfuatisha Isa bin Mariamu, na Tukampa Injili.’

Akimaanisha Injili Aliyomteremshia,

وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ

“Na Tukajaalia katika nyoyo za waliomfuata...”

Maana yake: Wanafunzi wake,

رَأْفَةً

“...upole...” Na huruma.

وَرَحْمَةً

“...*na rehema...*” Kwa wanyama. Kauli ya Allah تعالى,

وَرَهْبَانِيَّةً أُتِّدَعُوهَا

“*Na umonaki (utawa wa mapadri) wameuzua wao.*”

Inarejea kwenye utawa uliozushwa na Wakristo,

مَا كَتَبْنَا عَلَيْهَا

“*Sisi Hatukuwaandikia hayo...*”

Allah تعالى Hakuwafaradhisia, bali walijichagulia wao wenyewe.’ Kuna rai mbili kuhusu maana ya,

إِلَّا أُتْبِعَاءَ رِضْوَانِ اللَّهِ

“...*ila kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.*”

Ya kwanza ni kuwa, walitaka kumridhisha Allah تعالى kwa kuzusha umonaki. Sa’id bin Jubayr na Qatadah wamesema hayo.¹ Maana ya pili ni: “Hatujawafaradhisia kufanya hilo, bali, Tumewafaradhisia kutafuta Radhi ya Allah تعالى.” Kauli ya Allah تعالى,

فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا

“...*Lakini hawakuufuata inavyotakiwa kuufuata.*”

Inamaanisha, hawakuyafanya yale waliyoamrisha kuyafanya. Aya hii inawakosoa kwa namna mbili: Mosi, walizusha mambo katika dini ya Allah, ambayo Allah تعالى Hakuwapangia. Pili ni kuwa hawakutimiza matakwa ya waliyoyazusha wenyewe na ambayo walidai kuwa ilikuwa namna ya kujiweka karibu na Allah تعالى. Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Abu ‘Abdur-Rahman An-Nasa’i رضي الله عنهما — na haya ni maneno yake - amenukuu kuwa Ibn ‘Abbas عليه السلام waliobadili Taurati na Injili, na miongoni mwao walikuwepo waumini waliosoma Taurati na Injili. Wafalme wao waliambiwa, ‘Hatukukabiliwa na ukosoaji na matusi makubwa kama ya watu hawa.’ - wanasoma Aya,

¹ At-Tabari 23:203.

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٥٤﴾

“Na wasiohukumu kwa Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.” (5:44)

Aya hizi zinatutia dosari katika amali zetu, waite na wasome Aya hizi kwa namna yetu na waamini njia yetu. ‘Mfalme aliwaita na kuwakusanya na kuwatishia kifo kama hawataachana na Taurati na Injili halisi na kufuata Taurati na Injili iliyopotoshwa. Wakasema, ‘Kwa nini mnayataka hayo, tuacheni.’ Baadhi yao wakasema, ‘Jengeni mnara mwembamba ulioinuka juu na mtuweke huko na mtupandishie vyakula na vinywaji. Kwa njia hii, hamtatusikia.’ Kundi jingine miongoni mwao likasema, ‘Tuacheni twende ardhini na tule na tunywe kama wanyama wafanyavyo, na ikiwa mtatukuta katika ardhi yenu, basi Mtuue.’ Kundi jingine miongoni mwao likasema, ‘Tujengeeni majumba (ya utawa) jangwani na maeneo yaliyotengwa, ambapo tutachimba visima na kulima mboga. Hapo hatutakanusheni na hata hatutapita kwenu.’ Makundi hayo yalisema hayo, ingawa wote walikuwa ni sehemu katika makabila yao. Na kuhusu jambo hili ndipo Allah تعالى Aliteremsha Aya hii,

وَرَهْبَانِيَّةً ابْتَدَعُوهَا مَا كَتَبْنَا عَلَيْهَا إِلَّا ابْتِغَاءَ رِضْوَانِ اللَّهِ فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا

“Na umonaki (utawa wa mapadri) wameuzua wao. Sisi Hatukuwaandikia hayo, ila kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuufuata inavyotakiwa kuufuata.”¹

Imamu Ahmad amemnukuu Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لِكُلِّ نَبِيٍّ رَهْبَانِيَّةٌ، وَرَهْبَانِيَّةٌ هَذِهِ الْأُمَّةِ الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Kila Mtume ana Rahbaniyyah (umonaki); Jihad katika njia ya Allah, Mtukufu, ndio Rahbaniyyah ya Umati huu.”

Al-Hafidh Abu Yaa’la aliiikusanya Hadithi hii na katika simulizi hii, Mtume ﷺ amesema,

¹ At-Tabari 23:203. An-Nasai 8:231.

«لِكُلِّ أُمَّةٍ رَهْبَانِيَّةٌ، وَرَهْبَانِيَّتُهُ هَذِهِ الْأُمَّةُ الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

“Kila Umati una utawa “Rahbaniyyah”; utawa katika umma huu ni kufanya Jihad katika njia ya Allah.”¹

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Sa’id Al-Khudri رضي الله عنه amesema kuwa mtu mmoja alikuja kwake na kumuomba nasaha, na Abu Sa’id رضي الله عنه akamuambia kuwa na yeye alipata kumuuliza jambo kama hilo Mtume ﷺ. Abu Sa’id رضي الله عنه akasema, “Kwa hivyo, ninakupa nasaha ya kumcha Allah تعالى, kwa sababu ndio jambo kuu kuliko yote. Lazimiana na Jihad kwa sababu ni Utawa “Rahbaniyyah” wa Kiislamu. Lazimiana kumtaja Allah تعالى kwa kusoma Qur’an, kwasababu itakuwa ndio roho yako mbinguni na utajo wako duniani.” Imamu Ahmad peke yake aliikusanya Hadithi hii.²

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَءَامِنُوا بِرَسُولِهِ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِن رَّحْمَتِهِ وَيَجْعَل لَكُمْ نُورًا تَمْشُونَ بِهِ وَيَغْفِرَ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٨﴾ لَعَلَّ يَعْلَمَ أَهْلَ الْكِتَابِ ءَلَّا يَقْدِرُونَ عَلَى شَيْءٍ مِّن فَضْلِ اللَّهِ ۗ وَأَنَّ الْفَضْلَ بِيَدِ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾

28. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na muaminini Mtume Wake, Atakupeni sehemu mbili katika Rehema Yake, na Atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo. Na Atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

29. Ili watu wa Kitabu wajue kwamba wao hawana uweza wowote juu ya Fadhila za Mwenyezi Mungu. Na Fadhila zote zimo Mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Humpa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Fadhila kuu.

¹Ahmad 3:266, Isnadi yake ni dhaifu.

²Ahmad 3:82. simulizi hii ni dhaifu. Al-Albani ameipa simulizi ya Abu Sa’id daraja la Hasan kwa kuunga mkono maana. Hadithi hizo hapo juu zipo katika *As-Sahihah* na. 555.

Waumini Miongoni mwa Watu wa Kitabu Watapewa Malipo Maradufu

Tumetangulia kutaja Hadithi kuwa An-Nasa'i aliandika kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa Aya hii ni kuhusu watu waliopewa Kitabu walioamini Uislamu, na kwamba watapata malipo mara mbili kama watafanya hivyo. Kuna Aya katika Surat Al-Qasas inayounga mkono maana hiyo.¹ Pia, kuna Hadithi kutoka kwa Ash-Sha'bi kutoka kwa Abu Burdah kutoka kwa baba yake kutoka kwa Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema,

«ثَلَاثَةٌ يُؤْتَوْنَ أَجْرَهُمْ مَرَّتَيْنِ: رَجُلٌ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ آمَنَ بِنَبِيِّهِ وَآمَنَ بِي فَلَهُ أَجْرَانِ، وَعَبْدٌ مَمْلُوكٌ أَدَّى حَقَّ اللَّهِ وَحَقَّ مَوْلَاهُ فَلَهُ أَجْرَانِ، وَرَجُلٌ آدَبَ أُمَّتَهُ فَأَحْسَنَ نَادِيَّهَا، ثُمَّ أَغْتَقَهَا وَتَزَوَّجَهَا فَلَهُ أَجْرَانِ»

“Watu watatu watapa malipo mara mbili. Muumini kutoka kwa watu waliopewa Kitabu aliyemuamini kikweli Mtume wake na kuniamini mimi, atapata malipo mara mbili. Mtumwa anayetimiza haki za Allah na haki za bwana wake, atapata malipo mara mbili. Mtu mwenye kijakazi na akamuelimisha vyema na kumfundisha maadili mema vyema. Kisha akamuacha huru na akamuoa atapata malipo mara mbili.”

Hadith hii imenukuliwa katika Sahihi Mbili.² Adh-Dhahhak, 'Utbah bin Abu Hakim na wengine walikubaliana na Ibn 'Abbas رضي الله عنهما katika hilo, na Ibn Jarir رضي الله عنه amefika tafsiri hiyo.³ Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنْ تَتَّقُوا اللَّهَ يَجْعَلْ لَكُمْ فُرْقَانًا وَيُكَفِّرْ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾

“Enyi mlioamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu Atakupeni kipambanuo, na Atakufutieni makosa, na Atakusameheni, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kubwa. (8:29)

¹ Angalia Surat Al-Qasas 28:52-54.

² Fath Al-Bari 1:229, Muslim 1:134.

³ At-Tabari 23:208, 210.

Sa'id bin 'Abdul-'Aziz amesema, 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alimuuliza mwanazuoni wa Kiyahudi, 'Ni yapi malipo ya juu mnayoweza kuongezewa?' Yeye Akamjibu, 'Kifl' Yaani, 'sehemu ambayo ni kadiri ya mema mia tatu na hamsini.' 'Umar رضي الله عنه akasema, 'Sifa njema pamoja na shukurani ni za Allah تعالى Anayetupatia Kifl mbili.' Sa'id akataja Kauli ya Allah تعالى:

يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِنْ رَحْمَتِهِ

"...Atakupeni sehemu mbili katika Rehema Yake."

Sa'id akasema, "Na Kifl. Yaani, sehemu mbili katika siku ya Ijumaa ni mithili ya hivyo." Haya yamenukuliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.¹ Rai hii inaungwa mkono na Hadithi ambayo Imam Ahmad aliinukuu kutoka kwa 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَلَئَكُمْ وَمَثَلُ الْيَهُودِ وَالنَّصَارَى كَمَثَلِ رَجُلٍ اسْتَعْمَلَ عَمَلًا فَقَالَ: مَنْ يَعْمَلُ لِي مِنْ صَلَاةِ الصُّبْحِ إِلَى بَضْفِ النَّهَارِ عَلَى قِرَاطٍ قِرَاطٍ؟ أَلَا فَعَمِلْتَ الْيَهُودُ، ثُمَّ قَالَ: مَنْ يَعْمَلُ لِي مِنْ صَلَاةِ الظُّهْرِ إِلَى صَلَاةِ الْعَصْرِ عَلَى قِرَاطٍ قِرَاطٍ؟ أَلَا فَعَمِلْتَ النَّصَارَى، ثُمَّ قَالَ: مَنْ يَعْمَلُ لِي مِنْ صَلَاةِ الْعَصْرِ إِلَى غُرُوبِ الشَّمْسِ عَلَى قِرَاطَيْنِ قِرَاطَيْنِ؟ أَلَا فَأَنْتُمْ الَّذِينَ عَمِلْتُمْ، فَغَضِبَ النَّصَارَى وَالْيَهُودُ وَقَالُوا: نَحْنُ أَكْثَرُ عَمَلًا وَأَقْلُ عَطَاءً، قَالَ: هَلْ ظَلَمْتُمْ مِنْ أَجْرِكُمْ شَيْئًا؟ قَالُوا: لَا، قَالَ: فَإِنَّمَا هُوَ فَضْلِي أُوتِيهِ مَنْ أَسَاءَ»

"Mfano wenu na Wayahudi na Wakristo ni kama mtu aliyeajiri wafanyakazi na kuwauliza, 'Nani atakayenifanyia kazi tangu Sala ya Alfajiri mpaka mchana kwa malipo ya Qirat (kipimo cha dhahabu) moja?' Basi Wayahudi wakafanya kazi hiyo. Mtu huyo akauliza tena, na 'Nani atakayenifanyia kazi kuanzia Sala ya Adhuhuri mpaka wakati wa Sala ya Alasiri kwa malipo ya Qirat moja', Basi Wakristo wakafanya kazi hiyo. Kisha mtu huyo akauliza, 'Nani atakayenifanyia kazi kuanzia wakati wa Sala ya Alasiri mpaka kuchwa kwa jua kwa malipo ya Qirat mbili.' Nyinyi ndio mnaofanya kazi hiyo. Wayahudi na Wakristo wakakasirika na kusema, "Sisi tumefanya kazi zaidi na

¹ At-Tabari 23:210.

*kupata malipo kidogo,' Allah Akawauliza wao: 'Je, nyinyi nimewadhulumu chochote katika malipo yenu?' Wao wakasema, 'Hapana.' Akasema Allah, 'Basi hiyo ni Rehema Yangu Ninayompa yeyote Nimtakaye.'*¹ Al-Bukhari alilikusanya Hadithi hii.²

Imamu Al-Bukhari amenukuu kwamba Abu Musa رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَثَلُ الْمُسْلِمِينَ وَالْيَهُودِ وَالنَّصَارَى كَمَثَلِ رَجُلٍ اسْتَعْمَلَ قَوْمًا يَعْمَلُونَ لَهُ عَمَلًا يَوْمًا إِلَى اللَّيْلِ عَلَى أَجْرٍ مَعْلُومٍ، فَعَمِلُوا إِلَى نِصْفِ النَّهَارِ فَقَالُوا: لَا حَاجَةَ لَنَا فِي أَجْرِكَ الَّذِي شَرَطْتَ لَنَا، وَمَا عَمِلْنَا بِاطِلٍ، فَقَالَ لَهُمْ: لَا تَفْعَلُوا، أَكْمِلُوا بَيْتَهُ عَمَلِكُمْ، وَخُذُوا أَجْرَكُمْ كَامِلًا، فَأَبَوْا وَتَرَكَوْا وَاسْتَأْجَرَ آخَرِينَ بَعْدَهُمْ فَقَالَ: أَكْمِلُوا بَيْتَهُ يَوْمِكُمْ وَلَكُمْ الَّذِي شَرَطْتُ لَهُمْ مِنَ الْأَجْرِ، فَعَمِلُوا حَتَّى إِذَا كَانَ جِوْنٌ صَلُّوا النَّمْصَرَ قَالُوا: مَا عَمِلْنَا بِاطِلٍ، وَتِلْكَ الْأَجْرُ الَّذِي جَعَلْتَ لَنَا فِيهِ. فَقَالَ: أَكْمِلُوا بَيْتَهُ عَمَلِكُمْ، فَإِنَّمَا بَقِيَ مِنَ النَّهَارِ شَيْءٌ يَسِيرٌ، فَأَبَوْا. فَاسْتَأْجَرَ قَوْمًا أَنْ يَعْمَلُوا لَهُ بَيْتَهُ يَوْمِهِمْ فَعَمِلُوا لَهُ بَيْتَهُ يَوْمِهِمْ حَتَّى غَابَتِ الشَّمْسُ، فَاسْتَكْمَلُوا أُجْرَةَ الْفَرِيقَيْنِ كِلَيْهِمَا، فَذَلِكَ مَثَلُهُمْ وَمَثَلُ مَا قَبِلُوا مِنْ هَذَا النَّوْرِ»

"Mfano wa Waislamu, Wayahudi na Wakristo ni kama wa mtu aliyejiri wafanyakazi wa kumfanyia kazi kutoka asubuhi mpaka usiku kwa mshahara maalumu. Wakafanya kazi mpaka katikati ya mchana na kusema, 'Hatuhitaji mshahara ulioahidi na kazi yetu ilikuwa ya hasara.' Akawaambia, 'Msifanye hivyo, kamilisheni kazi iliyobakia na mtapata mshahara kamili nilioupanga.' Hata hivyo, walikataa na kuacha, na akawaajiri wafanyakazi wengine. Akawaambia, 'Kamilisheni kazi katika muda uliobakia wa mchana na nitakupeni mshahara sawa na niliowaahidi wale wa mwanzo.' Wakafanya kazi mpaka wakati wa Sala ya Alasiri na kusema, 'Yote tuliyoafanya ni kazi bure tu nasi tunaacha mshahara uliotuahidi.' Akawaambia, 'Kamilisheni kazi yenu, kwani umebakia muda mchache tu.' Hata hivyo, walikataa, na akawaajiri wengine kwa

¹ Ahmad 2:6, 111.

² Fat'h Al-Bari 4:521 na 6:571.

muda uliosalia, na wakafanya kazi mpaka machweo ya jua na wakapata mishahara ya yale makundi mawili ya mwanzo. Huo ni mfano wao (Wayahudi na Wakristo) na wale waliopokea nuru hii (yaani, Uislamu)." Al-Bukhari ndiye pekee aliyeinukuu Hadithi hii.¹

Allah تعالی Amesema;

لَعَلَّ يَعْلَمَ أَهْلُ الْكِتَابِ أَلَّا يَقْدِرُونَ عَلَى شَيْءٍ مِّنْ فَضْلِ اللَّهِ وَأَنَّ الْفَضْلَ بِيَدِ اللَّهِ

"Ili watu wa Kitabu wajue kwamba wao hawana uweza wowote juu ya Fadhila za Mwenyezi Mungu."

Maana yake: ili wawe na hakika kuwa hawataweza kuzuia Allah تعالی Anachowapa watu au kutoa Anachozuia Allah تعالی,

وَأَنَّ الْفَضْلَ بِيَدِ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ

"Na Fadhila zote zimo Mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Humpa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Fadhila kuu."

Huu ndio mwisho wa *Tafsiri ya Suratu Al-Hadid*, Sifa zote njema pamoja na Shukrani ni za Allah تعالی na Fadhila zote zinatoka Kwake.

* * *

¹ Fat'h Al-Bari 4:523.

Tafsiri ya Suratul Mujadilah

Sura ya 58

Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمُجَادِلَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿١﴾

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿١﴾ الَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْكُمْ مِمَّن نَسَأَهُمْ مَا هُمْ عَنْ أُمَّهَاتِهِمْ إِنْ أُمَّهَاتُهُمْ إِلَّا الَّتِي وَلَدْنَهُمْ وَإِنَّهُمْ لَيَقُولُونَ مُنْكَرًا مِنَ الْقَوْلِ وَزُورًا وَإِنَّ اللَّهَ لَعَفُوفٌ غَفُورٌ ﴿٢﴾ وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْ نِسَائِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَتَمَاسَا ذَلِكَ تَوْعَلُوتٌ بِهِ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٣﴾ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَتَمَاسَا فَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فإِطْعَامُ سِتِّينَ مِسْكِينًا ذَلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتَلْكَ حُدُودَ اللَّهِ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤﴾

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿١﴾

1. Mwenyezi Mungu Amekwisha sikia usemi wa mwanamke anayejadiliana nawe juu ya mumewe, na anamshitakia Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anayasikia maji-bizano yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona.

Sababu za Kushuka Surah hii

Imamu Ahmad amenukuu kuwa رضي الله عنها 'A'ishah amesema, "Kila sifa njema Anastahiki Allah تعالى,

Mwenye Kusikia sauti. "Mwanamke aliyejadiliana" alikuja kwa Mtume ﷺ na

kujadiliana naye ilhali nikiwa katika upande mwingine wa chumba, bila ya kuweza kusikia kilichozungumzwa.

Allah تعالى Akashusha Aya hii,

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا

“Mwenyezi Mungu Amekwisha sikia usemi wa mwanamke anayejadiliana nawe juu ya mumewe...”

Mpaka mwisho wa Aya hii.¹

Al-Bukhari aliiandika Hadithi hii katika Sahhi yake katika kitabu cha *Tawhid* bila ya isnadi ya msimulizi.²

An-Nasa’i, Ibn Majah, Ibn Abi Hatim na Ibn Jarir pia waliikusanya Hadithi hii.³

Katika Hadithi aliyokusanya Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى, ‘A’ishah رضي الله عنها alisema, “Ametukuka Yule Ambaye Kusikia Kwake kumekienea kila kitu. Nilisikia baadhi ya aliyoyasema Khuwaylah bint Tha`labah رضي الله عنها. Alikuwa akimshitaki mumewe kwa Mtume ﷺ. Akasema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Ametumia mali yangu, ameumaliza ujana wangu na tumbo langu limemzalia sana. Nilipozeeka, na kutokuzaa, amenitamkia *Dhihaar!*’⁴ Ewe Allah تعالى! Ninakuletea mashitaka.’

Mara, Jibril عليه السلام akashuka na Aya,

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا

“Mwenyezi Mungu Amekwishasikia usemi wa mwanamke anayejadiliana nawe juu ya mumewe...”

Akaongeza, “Mumewe alikuwa ‘Aws bin as-Samit رضي الله عنه.⁵

¹ Ahmad 6:46.

² *Fat’h Al-Bari* 13:384.

³ An-Nasai 6:168, Ibn Majah 1:67, na At-Tabari 23:225.

⁴ Maana ya *Adh-Dhihar* ni mtu kumuambia mkewe, “Wewe ni haramu kwangu kukuingilia wewe kama alivyo mama yangu.”

⁵ At-Tabari 23:226

الَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْكُمْ مِمَّا هِيَ أُمَّهَاتُهُمْ إِلَّا الَّتِي وَلَدْتَهُمْ
 وَإِنَّهُمْ لَيَقُولُونَ مُنْكَرًا مِنَ الْقَوْلِ وَزُورًا وَإِنَّ اللَّهَ لَعَفُوفٌ غَفُورٌ ﴿١﴾ وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ
 مِنْ نِسَائِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَتَمَاسَّ ذَلِكُمْ تَوْعُظُونَ
 بِهِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢﴾ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامَ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ
 يَتَمَاسَّ ۗ فَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فإِطْعَامَ سِتِّينَ مِسْكِينًا ۗ ذَلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۗ وَتِلْكَ
 حُدُودُ اللَّهِ ۗ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٣﴾

2. Wale miongoni mwenu wanaowatenga wake zao, hao si mama zao. Hawakuwa mama zao ila wale waliowazaa. Na hakika hao wanasema neno linalokanusha, na la uwongo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Msamaha, Mwingi wa Kusamehe.

3. Na wale wanaowaharamisha wake zao, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema, basi wamkomboe mtumwa kabla hawajagusana. Mnapewa maonyo kwa hayo. Na Mwenyezi Mungu Anayajua yote mnayoyatenda.

4. Na asiyepata mtumwa wa kumkomboa, basi afunge miezi miwili mfululizo kabla hawajagusana. Na asiyeweza hayo basi awalishe masikini sitini. Hayo ni hivyo ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na kwa makafiri iko adhabu chungu.

Adh-Dhihar na Kafara Yake

Imam Ahmad amenukuu kuwa Khuwaylah bint Tha'labah رضي الله عنها amesema, "Wallahi! Allah تعالي Alishusha mwanzo wa Surat Al-Mujadilah kunihusu mimi na 'Aws bin as-Samit رضي الله عنه. Nilikuwa kwake na alikuwa mzee sana na tabia zake zikabadilika. Siku moja, alikuja kwangu na nilijadiliana naye kuhusu jambo, na akasema kwa hasira, 'Wewe ni kama mgongo wa mama yangu.'

Alitoka na kukaa na baadhi ya watu wake. Akarudi na kutaka kujamiiana nami. Nikasema, 'Hapana, Naapa kwa Ambaye Mkononi Mwake upo uhai wa Khuwaylah! Huna nafasi kwangu baada ya yale uliyoyasema, mpaka Allah تعالى na Mjumbe Wake wahukumu jambo hili.' Alitaka awe na namna yake pasi na kujali hiyari yangu na nikamsukuma; alikuwa amezeeka.' Nikamuendea jirani yangu mmoja na kuazima nguo kutoka kwake na nikamuendea Mtume ﷺ. Nikamueleza kilichotokea na nikamlalamikia tabia mbaya aliyonifanyia 'Aws. Akasema,

«يَا خُوَيْلَةَ، ابْنُ عَمِّكَ شَيْخٌ كَبِيرٌ، فَاتَّقِي اللَّهَ فِيهِ»

"Ewe Khuwaylah! Binamu yako ni mzee, kwa hivyo uwe na Taqwa ya Allah ndani yake."

Wallah! Kabla sijaondoka, baadhi ya Aya za Qur'an zilishuka kunihusu. Mtume ﷺ alijisikia uzito wakati alipokuwa akipokea wahyi kama kawaida yake kisha akarudia hali ya kawaida, akaniambia,

«يَا خُوَيْلَةَ، قَدْ أَنْزَلَ اللَّهُ فِيكَ وَفِي صَاحِبِكَ قُرْآنًا»

"Ewe Khuwaylah! Allah Amenishushia jambo kuhusu wewe na mumeo."

Alinisomea,

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿١﴾

"Mwenyezi Mungu Amekwishasikia usemi wa mwanamke anayejadiliana nawe juu ya mumewe, na anamshitakia Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anayasikia majibizano yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona...", mpaka,

وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢﴾

"Na kwa makafiri iko adhabu chungu."

Akaniambia,

«مُرِيهِ فَلْيَعْبِتْ رَقَبَةً»

“Muamuru amuache huru mtumwa.”

Nikasema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Hana mtumwa wa kumuacha huru.’ Akasema,

«فَلْيَضْمُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ»

“Afunge saumu kwa miezi miwili mfululizo.”

Nikasema, ‘Wallahi! Yeye ni mzee na hawezi kufunga.’ Akasema,

«فَلْيُطْعِمِ سِتِّينَ يَسْكِينًا وَنَسَقًا مِنْ تَمْرٍ»

“Awalishe maskini sitini kwa kuwapa Wasq¹ ya tende.”

Nikasema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Wallahi, hana vitu hivyo.’ Akasema,

«فَإِنَّا سَنُؤْتِيهِ بِعَرَقٍ مِنْ تَمْرٍ»

“Tutamsaidia kwa kumpa kapu² la tende.”

Nikasema, ‘Nami, Ewe Mjumbe wa Allah! Nitampa jingine.’ Akasema,

«فَقَدْ أَصَبْتُ وَأَخْسَنْتِ فَأُدْهِمِي فَتَصَدَّقِي بِهِ عَنْهُ، ثُمَّ اسْتَوْصِي بِإِبْنِ عَمَلِكٍ خَيْرًا»

“Umefanya jambo jema. Kwa hivyo nenda na utoe tende kwa niaba yake na umtunze binamu yako.”

“Niliyafanya hayo.”³ Abu Dawud pia aliikusanya Hadithi hii katika kitabu cha Talaka katika *Sunan* yake,⁴ kwa mujibu wa ambaye jina lake ni Khawlah bint Tha`labah رضي الله عنها. Pia alijulikana kama Khawlah bint Malik bin Tha`labah, na Khuwaylah. Yote hayo yanakaribiana, na Allah تعالى Anajua zaidi. Huu ndio usahihi kuhusu sababu za kushuka *Surah* hii. Kwa hiyo, Kauli ya Allah تعالى,

¹ Wasq moja inalingana na Sa' 60 au kadiri ya lita 165.

² Ambayo ilikuwa kadiri ya Sa' kumi na tano.

³ Ahmad 6:410.

⁴ Abu Dawud 2:662, 664.

الَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْكُمْ مِنْ نِسَائِهِمْ

“Na wale wanaojitenga na wake zao...”

Inarejea katika *Dhihar*, neno lililochukuliwa kutoka katika neno “*Adh-Dhahr*” linalomaanisha, mgongo. Katika enzi za *Jahiliyyah*, mtu alipotaka kumtamkia *Dhihar* mkewe, alikuwa akisema, “Kwangu mimi, wewe ni kama mgongo wa mama yangu.” Hiyo ilikuwa njia moja ya kutoa talaka kwa wakati huo. Allah تعالی aliuruhusu Ummah huu kulipa kafara kwa ajili ya kauli hiyo na hakuichukulia kuwa talaka, tofauti na ilivyokuwa katika wakati wa *Jahiliyyah*. Kauli ya Allah تعالی,

مَا هُنَّ أُمَّهَاتِهِمْ إِنْ أُمَّهُتُّهُنَّ إِلَّا الَّتِي وَلَدْنَهُمْ

“Hawakuwa mama zao ila wale waliowaza.”

Inamaanisha, mume anapomuambia mkewe kuwa yeye ni kama mama yake, au mgongo wa mama yake na mengine kama hayo, hawi mama yake. Bali mama yake ni aliyemzaa. Kwa ajili hiyo, Allah تعالی Amesema,

وَأَيْتُهُمْ لَيَقُولُنَّ مُنْكَرًا مِنَ الْقَوْلِ وَزُورًا

“Na hakika hao wanasema neno linalochusha, na la uwongo.”

Inamaanisha, maneno ya uwongo na dhambi,

وَإِنَّ اللَّهَ لَعَفُوفٌ غَفُورٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kughufiria, Mwenye Kusamehe.”

Inamaanisha, mliyokuwa mkiyafanya katika wakati wa *Jahiliyyah*, na maneno mnayotamka kwa bahati mbaya, bila ya kukusudia. Kauli ya Allah تعالی,

وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْ نِسَائِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا

“Na wale wanaojitenga na wake zao, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema.”

Ash-Shafi’ رحمه الله تعالی amesema, “Inamaanisha kuwa naye kwa muda fulani baada ya *Dhihar*, bila ya kumuacha, ingawa anaweza kufanya hivyo.” Ahmad bin Hanbal رحمه الله تعالی amesema, “Ni kurudia kujamiiana naye au kukusudia tu

kufanya hivyo, inakuwa si halali kwake adhabu ya kulipa kafara iliyotajwa katika Aya hiyo.” Imenukuliwa kutoka kwa Malik رضي الله عنه kuwa ni kutia nia ya kujamiiana naye au kuendelea kuishi naye. Na imenukuliwa kutoka kwake kuwa amesema: ‘Ni kujamiana.’ Sa’id bin Jubayr amesema kuwa Aya hii,

ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا

“...*kisha wakarudia katika yale waliyoyasema.*”

Maana yake: Ikiwa watataka kurejea kujamiiana ambako kulikatazwa baina yao. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى amesema: kuwa ni kutumia kiungo chake cha kujamiiana, na hakuona ubaya wowote wa kufanya yasiyofikia hilo kabla ya kulipa kafara. ‘Ali bin Abi Talhah amesimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما:

مِن قَبْلِ أَنْ يَتَمَّاسًا

“...*kabla hawajagusana...*”

“Kugusana’ hapa kunamaanisha kujamiiana.”¹ Sawa na hayo, yalisemwa na ‘Ata’, Az-Zuhri, Qatadah na Muqatil bin Hayyan. Az-Zuhri ameongeza, “Asimbusu au kumgusa isipokuwa mpaka alipe kafara.” Wakusanyaji maarufu wa Hadithi wamenukuu kutoka kwa ‘Ikrimah, kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa mtu mmoja alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Nimemtamkia *Dhihar* mke wangu, lakini kisha nikajamiiana naye kabla sijalipa kafara.” Mtume ﷺ akasema,

«مَا حَمَلَكَ عَلَىٰ ذَٰلِكَ بِرَحْمَتِكَ اللَّهُ»

“Allah Akurehemu, kwanini umefanya hivyo.”

Akasema, “Niliona mapambo yake yaking’aa katika mbalamwezi.” Mtume ﷺ akasema,

«فَلَا تَقْرُبْنَهَا حَتَّىٰ تَفْعَلَ مَا أَمَرَكَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ»

“Basi usimguse mpaka ufanye Alichokuamrisha Allah Mtukuka kufanya.”

¹ At-Tabari 23:231.

At -Tirmidhi amesema, Hadithi ina daraja ya "Hasan Gharib Sahih." Abu Dawud na An-Nasa'i pia wameinukuu. Kauli ya Allah تعالى،

فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ

"...basi wamkomboe mtumwa..."

Inamaanisha ulazima wa kumpa uhuru mtumwa kabla hawajagusana. Ayah hii inataja mtumwa yeyote, si watumwa waumini tu kama katika suala la kafara ya kuua (bila kukusudia).

ذَلِكَمُ تَوْعُظُونَ بِهِ

"Mnapewa maonyo kwa hayo."

Maana yake: Onyo la kukuhofisheni katika hali hiyo.

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ

"Na Mwenyezi Mungu Anayajua yote mnayoyatenda."

Maana yake: Yeye ni Mwenye Kujua Yote katika yenye manufa kwenu. Kauli ya Allah تعالى،

فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَتَمَاسَا^ط فَمَنْ لَّمْ يَسْتَطِعْ فَاِطْعَامُ
سِتِّينَ مِسْكِينًا

"Na asiyepata mtumwa kumkomboa, basi na afunge miezi miwili mfululizo kabla hawajagusana. Na asiyeweza hayo basi awalisha masikini sitini."

Imeelezwa katika Hadithi zenye kuweka adhabu hizo katika mpangilio huo, kama katika Hadithi iliyoandikwa katika Sahihi Mbili kuhusu mtu aliyejamiiana na mkewe katika mchana wa mwezi wa Ramadhani.¹ Kauli ya Allah تعالى،

¹ Abu Dawud 2:666, Tuhfat Al-Ahwadhi 4:380, An-Nasai 6:167 na Ibn Majah 1:666.

ذَٰلِكَ لِمُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۚ

“Hayo ni hivyo ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake..”

Maana yake: ‘Tumeiweka adhabu hii ili mpate ubainifu huu.’

وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ

“Na hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Mambo aliyokataza, basi msiikiuke,

وَاللَّكَفِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٠﴾

“Na kwa makafiri iko adhabu chungu.”

Maana yake: Wasioamini na kutokushikamana na sheria za Kiislamu wasidhanie kamwe kuwa watanusurika na adhabu. Bali wataadhibiwa vikali duniani na Akhera.

* * *

إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ كُبِتُوا كَمَا كُبِتَ الَّذِينَ مِنْ
 قَبْلِهِمْ ۗ وَقَدْ أَنْزَلْنَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ مُهِينٌ
 ﴿٥﴾ يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوا أَحْصَاهُ
 اللَّهُ وَسُوهُ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٦﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ
 يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ مَا يَكُونُ مِنْ
 نَجْوَىٰ ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا
 آدَىٰ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا ۗ ثُمَّ
 يُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٧﴾
 أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ جَاءُوا عَنِ النَّجْوَىٰ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا جَاءُوا
 عَنْهُ وَيَتَنَجَّجُونَ بِالْإِثْرِ وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَتِ الرَّسُولِ
 وَإِذَا جَاءُوكَ حَيَّوْكَ بِمَا لَمْ يُحَيِّكَ بِهِ اللَّهُ وَيَقُولُونَ فِي
 أَنْفُسِهِمْ لَوْلَا يُعَذِّبُنَا اللَّهُ بِمَا نَقُولُ ۗ حَسْبُكُمْ جَهَنَّمُ
 يَصْلَوْنَهَا ۗ فَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿٨﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا
 تَنَجَّيْتُمْ فَلَا تَتَنَجَّجُوا بِالْإِثْرِ وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَتِ الرَّسُولِ
 وَتَتَنَجَّجُوا بِالْبَرِّ وَالْأَقْوَامِ ۗ وَأَتَقُوا اللَّهَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ
 ﴿٩﴾ إِنَّمَا النَّجْوَىٰ مِنَ الشَّيْطَانِ لِيَحْزُرَ الَّذِينَ آمَنُوا
 وَلَيْسَ بِضَارِهِمْ شَيْئًا إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَعَلَى اللَّهِ فَايَتَوَكَّلِ
 الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٠﴾

إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ كُبِتُوا
 كَمَا كُبِتَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۗ وَقَدْ
 أَنْزَلْنَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ وَلِلْكَافِرِينَ
 عَذَابٌ مُهِينٌ ﴿٥﴾ يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ
 جَمِيعًا فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوا أَحْصَاهُ
 اللَّهُ وَسُوهُ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ
 ﴿٦﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي
 السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ مَا
 يَكُونُ مِنْ نَجْوَىٰ ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ
 رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ
 وَلَا آدَىٰ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا
 هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا ۗ ثُمَّ
 يُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ
 شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٧﴾

5. Hakika wanaopinzana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, watadhakilishwa kama walivyodhakilishwa wale waliokuwa kabla yao. Na Tulikwishateremsha Aya zilizowazi.

Na makafiri watapata adhabu ya kufedhehesha.

6. Siku Atapowafufua wote Mwenyezi Mungu, na Awaambie yale waliyoyatenda. Allah Ameyadhibiti, na wao wameyasahau! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushuhudia kila kitu.

7. Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu Anajua vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi? Hauwi mnong'ono wa watu watatu ila Yeye huwa ni wane wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao. Wala wa wachache kuliko hao, wala walio wengi zaidi, ila Yeye Yu pamoja nao popote pale walipo. Kisha Siku ya Kiyama Atawaambia waliyoyatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

Maelezo ya Adhabu kwa Maadui wa Dini

Allah تعالى Anaeleza kuwa wanaomkataa Yeye na Mjumbe Wake na Kupinga Amri Zake,

كُتِبُوا كَمَا كُتِبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“...watadhalilishwa kama walivyodhalilishwa wale waliokuwa kabla yao.”

Inamaanisha, watadhalilishwa, watalaaniwa na kufedheheshwa, kama yalivyowakuta wa kabla yao,

وَقَدْ أَنْزَلْنَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ

“Na Tulikwisha teremsha Ishara zilizo wazi.”

Inamaanisha, hakuna wa kuzipinga au kuzikataa, isipokuwa kafiri, muasi, mtenda dhambi,

وَاللَّكْفِيرِينَ عَذَابٌ مُهِينٌ

“Na makafiri watapata adhabu ya kufedhehesha.”

Maana yake: Kama malipo ya haki kwa kukaidi kwao kiujeuri juu ya kufuata, kutii na kufuata Dini ya Allah تعالى. Allah تعالى Amesema,

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا

“Siku Atapowafufua Mwenyezi Mungu...” Ambayo ni Siku ya Ufufuo Atakusanya vizazi vya mwanzo na vya mwisho katika sehemu moja,

فَيُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا

“Kisha Siku ya Kiyama Atawaambia waliyoyatenda.”

Atawaambia kwa kina yote waliyoyafanya, ima wema au uovu.

أَحْصَنَهُ اللَّهُ وَنَسُوهُ

“Mwenyezi Mungu Ameyadhibiti, na wao wameyasahau!”

Inamaanisha, Allah تعالى Ameandika na kutunza matendo yote, ingawa wamesahau waliyoyafanya,

وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushuhudia kila kitu.”

Maana yake: Hapotezi kitu, wala Hakifichiki wala Hasahau.

Elimu ya Allah تعالى Inawaenea Viumbe

Kisha Allah تعالى Anaeleza kuhusu elimu Yake Kuvienea viumbe wote, Kutambua, Kusikia maneno yao na Kuwaona, popote wanapokuwepo na katika hali yoyote wanayokuwemo.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَا يَكُونُ مِنْ نَجْوَى ثَلَاثَةٍ

“Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu Anajua vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi? Hauwi mning’ono wa watu watatu...”

Maana yake: Siri ya watu watatu,

إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةَ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا أَدْنَىٰ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ
أَيَّنَ مَا كَانُوا

“...ila Yeye huwa ni wanne wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao. Wala wa wachache kuliko hao, wala walio wengi zaidi, ila Yeye Yu pamoja nao popote pale walipo.”

Inamaanisha, Anawaangalia, Anayasikia vyema maneno yao, ima yawe yametamkwa hadharani au faragha. Malaika Wake wanayaandika yote

wanayoyasema, ingawa Yeye Anajua zaidi na Anawasikia vyema. Sawa na kauli nyingine ya Allah تعالى:

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ وَأَنَّ اللَّهَ عَلَّمَهُ الْغُيُوبَ ﴿٧٨﴾

“Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu Anajua siri zao na minong’ono yao, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyajua sana ya ghaibu?” (9:78),

أَمْ حَسِبُونَ أَنَّا لَا نَسْمَعُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ بَلَىٰ وَرُسُلْنَا لَدَيْهِمْ يَكْتُبُونَ ﴿٨٠﴾

“Au wanadhani kwamba hatusikii siri zao na minong’ono yao? Wapi! Na wajumbe wetu wapo karibu nao, wanayaandika.” (43:80)

Kwa sababu hii, wengi wamesema kuwa kuna muwafaka miongoni mwa wanazuoni kuwa neno “pamoja” linarejea katika Elimu ya Allah تعالى. Bila ya shaka, maana yake ni sahihi, hususani ikiwa tutaongezea humo uhakika kuwa Kusikia Kwake Kunaenea vitu vyote, pia kama kulivyo Kuona Kwake. Yeye, Mtukuka, Hakosi Kujua mambo yao yote,

ثُمَّ يُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“Kisha Siku ya Kiyama Atawaambia waliyoyatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

Imamu Ahmad amesema: “Allah تعالى Alianza Aya ya (58:7) kwa Kutaja Ujuzi Wake na Kumalizia kwa Kutaja Ujuzi Wake.”

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ هُجُوا عَنِ النَّجْوَىٰ ثُمَّ يُعُودُونَ لِمَا هُجُوا عَنْهُ وَيَتَنَجَّجُونَ بِالْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَةِ الرَّسُولِ وَإِذَا جَاءُوكَ حَيَّوْكَ بِمَا لَمْ يُحَيِّكَ بِهِ اللَّهُ وَيَقُولُونَ فِي أَنفُسِهِمْ لَوْلَا يُعَذِّبُنَا اللَّهُ بِمَا نَقُولُ حَسِبُهُمْ جَهَنَّمُ يَصَلُّونَهَا فَيَنسَ الْمَصِيرُ ﴿٧٩﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا تَنَجَّيْتُمْ فَلَا تَتَنَجَّجُوا بِالْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَةِ الرَّسُولِ وَتَتَنَجَّجُوا بِالْبَرِّ وَالْتَّقْوَىٰ ؕ وَأَتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٨٠﴾ إِنَّمَا النَّجْوَىٰ مِنَ الشَّيْطَانِ لِيَحْزُرَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَيْسَ بِضَارِّهِمْ شَيْئًا إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٨١﴾

8. Kwani huwaoni wale waliokatazwa kunong'onezana kisha wakayarudia yale yale waliyokatazwa, na wakanong'ona juu ya mambo ya dhambi, na ya uadui, na ya kumuasi Mtume? Na wakikujia hukuamkia maamkio asiyoamrisha Mwenyezi Mungu. Na husema katika nafsi zao: Mbona Mwenyezi Hatuadhibu kwa haya tuyasemayo? Basi Jahannamu itawatoshia; wataingia humo! Na hayo ndiyo marejeo maovu yaliyoje!

9. Enyi mlioamini! Mnaponong'ona msinong'one kwa sababu ya mambo ya madhambi, na uadui, na kumuasi Mtume. Bali mnong'onezane kwa kutenda mema na kuacha maovu. Na mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye Kwake mtakusanywa nyote.

10. Kwa hakika minong'ono inatokana na Shetani ili awahuzunisha walioamini, na wala haitawadhuru chochote ila kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Na kwa Mwenyezi Mungu tu ndio wategemee Waumini.

Uovu wa Wayahudi

Ibn Abi Najih amesimulia kutoka kwa Mujahid,

أَلَمْ تَرِ إِلَى الَّذِينَ جَاءُوا عَنِ النَّجْوَى ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا جَاءُوا عَنْهُ

“Kwani huwaoni wale waliokatazwa kunong'onezana kisha wakayarudia yale yale waliyokatazwa.”

Amesema, ni “Wayahudi.”¹ Maneno sawa na hayo yalisemwa na Muqatil bin Hayyan, ambaye aliongeza, “Mtume ﷺ alikuwa na mkataba wa amani na Wayahudi. Swahaba mmoja wa Mtume ﷺ alipokuwa akipita katika mkutano wa Wayahudi walikuwa wakiambizana siri ili kuwashawishi waumini wadhania kuwa walikuwa wakipanga njama za kumuua au kumdhuru. Muumini alipoona hivyo, alihofia usalama wake na kubadili njia aliyokuwa akipita. Mtume ﷺ aliwakataza waache mazungumzo yao maovu ya kisiri, lakini hawakusikia na wakaendeleza minong'ono yao. Allah تعالی Akashusha Ayah hii kuhusu jambo lao,

¹ At-Tabari 23:236.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ جَاءُوا عَنِ النَّجْوَى ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا جَاءُوا عَنْهُ

“Kwani huwaoni wale waliokatazwa kunong’onezana kisha wakayarudia yale yale waliyokatazwa.”

Kauli ya Allah تعالى،

وَيَتَنَجَّوْنَ بِالْأَثْمِرِ وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَتِ الرَّسُولِ

“...na wakanong’ona juu ya mambo ya dhambi, na ya uadui, na ya kumuasi Mtume?”

Inamaanisha, walikuwa wakiambizana,

بِالْأَثْمِرِ

“...dhambi...”

Iliyowahusu wao wenyewe,

وَالْعُدْوَانِ

“...na ya uadui...”

Yanayowaathiri wengine. Wanazungumzia kumuasi na kumkataa Mtume ﷺ, kwa kuchagiza na kumuambia kila mtu afuate njia yao,

وَإِذَا جَاءُوكَ حَيَّوْكَ بِمَا لَمْ يُحَيِّكَ بِهِ اللَّهُ

“Na wakikujia hukuamkia maamkio asiyoamrisha Mwenyezi Mungu.”

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kuwa ‘A’ishah رضي الله عنها amesema, “Baadhi ya Wayahudi walikuja kwa Mtume ﷺ na kumsalimia kwa kumuambia, ‘As-Sam ‘Alayka.’¹ ‘Mauti yawe juu yako, Ewe Abul-Qasim.’ Nikasema, ‘wa ‘Alaykum As-Sam (pia mauti yakufikieni).’ Mtume ﷺ akasema,

¹ Ad-Dur Al-Manthur 8:80. Hii ni Hadithi Mursal. Angalia sehemu inayozungumzia Hadithi mwanzoni mwa kitabu hiki.

«يَا عَائِشَةُ! إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْفَحْشَ وَلَا التَّمَشُّشَ»

“Ewe ‘A’ishah, Allah Hapendi ukosefu wa adabu wala maneno mabaya.”

Nikasema, ‘Hukuwasikia wakisema, ‘As-Sam Alayka.’” Akasema,

«أَوْ مَا سَمِعْتِ أَقُولُ: وَعَلَيْكُمْ»

“Hukunisikia nikiwaitikia kwa kusema, ‘Wa ‘Alaykum (Nanyi pia).’”

Allah تعالی Akateremsha Aya hii,

وَإِذَا جَاءُوكَ حَيَّوْكَ بِمَا لَمْ يُحَيِّكَ بِهِ اللَّهُ

“Na wakikujia hukuamkia maamkio asiyoamrisha Mwenyezi Mungu.”²

Masimulizi hayo yaliyokusanywa katika Sahih yanaeleza kuwa ‘A’ishah رضي الله عنها alisema, “Nanyi mfikwe na mauti, fedheha na laana.” Mtume ﷺ akamuambia,

«إِنَّهُ يُسْتَجَابُ لَنَا فِيهِمْ، وَلَا يُسْتَجَابُ لَهُمْ فِيْنَا»

“Allah Hupokea dua zetu dhidi yao, lakini sio yao dhidi yetu.”³

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه amesema, “Myahudi alipita karibu na Mtume ﷺ, aliyekuwa amekaa pamoja na Masahaba wake, akawasalimia na wakamuitikia.

Mtume ﷺ akawaambia Masahaba wake رضي الله عنهم,

«هَلْ تَذَرُونَ مَا قَالَ؟»

“Mnajua alivyosema?”

Wakasema, ‘Amesema: As-Salam, Ewe Mjumbe wa Allah.’ Mtume ﷺ akasema,

¹ Angalia hapa chini.

² At-Tabari 23:236, 237.

³ Fat’h Al-Bari 10:466.

«بَلْ قَالَ: سَامٌ عَلَيْكُمْ»

“Bali amesema, Sam ‘Alaykum.” Inamaanisha, ‘mauti yawe juu yenu.’ Mjumbe wa Allah ﷻ akasema,

«رُدُّوهُ»

“Mrudisheni hapa.” Na aliporudishwa, Mtume ﷻ alimuuliza,

«أَقُلْتُ: سَامٌ عَلَيْكُمْ؟»

“Ulisema: Sam ‘Alaykum?”

Akaitikia, ‘Ndiyo.’ Mtume ﷻ akasema,

«إِذَا سَلَّمَ عَلَيْكُمْ أَحَدٌ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ فَقُولُوا: عَلَيْكَ»

“Watu wa Kitabu wanapokusalimieni, semeni, ‘Wa‘Alaykum.”

Inamaanisha, ‘na kwenu nyinyi pia.’¹ Msingi wa Hadithi ya Anas رضي الله عنه ni katika Sahih na Hadithi hii ya ‘A’ishah رضي الله عنها ipo katika Sahih.² Kauli ya Allah تعالى,

وَيَقُولُونَ فِي أَنْفُسِهِمْ لَوْلَا يُعَذِّبُنَا اللَّهُ بِمَا نَقُولُ

“Na husema katika nafsi zao: Mbona Mwenyezi Mungu Hatuadhibu kwa haya tuyasemayo?”

Inamaanisha Wayahudi hutamka maneno hayo, kwa kubadilisha maana ya maamkizi ya Kiislamu, na kuwa kauli ya kutukana, basi wanasema katika nafsi zao, ‘Kama angekuwa Mtume, Allah تعالى Angetuadhibu kwa tuliyoyasema. Allah تعالى Anajua wanayoyaficha. Kwa hiyo, ikiwa Muhammad ﷺ alikuwa Mtume, Allah تعالى Angeleta adhabu upesi, duniani.’ Allah تعالى Alijibu,

حَسْبُهُمْ جَهَنَّمُ

“Basi Jahannamu itawatosha...” Jahanamu itawatosha huko Akhera,

يَصْلَوْنَهَا فَيَنْسَأَلُ الْمَصِيرُ

“...wataingia humo! Na hayo ndiyo marejeo maovu yaliyoje!”

¹ At-Tabari 23:240.

² Fat’h Al-Bari 10:463.

Imamu Ahmad amenukuu kuwa ' Abdullah bin 'Amr رضي الله عنه amesema kuwa Wayahudi walikuwa wakisema, "Sam 'Alayka," kwa maana mauti yawe juu yako, kumuambia Mtume ﷺ. Halafu wakawa wanaambizana, "Kwa nini Allah تعالى Hatuadhibu kwa tunayoyasema?" Aya hii ikashuka,

وَإِذَا جَاءُوكَ حَيَّوكَ بِمَا لَمْ يُحَيِّكَ بِهِ اللَّهُ وَيَقُولُونَ فِي أَنْفُسِهِمْ لَوْلَا يُعَذِّبُنَا اللَّهُ بِمَا نَقُولُ
حَسْبُهُمْ جَهَنَّمُ يَصَلُّونَهَا فَیَسْتَأْذِنُ الْمَصِيرُ

"Na wakikujia hukuamkia maamkio asiyoamrisha Mwenyezi Mungu. Na husema katika nafsi zao: Mbona Mwenyezi Hatuadhibu kwa haya tuyasemayo? Basi Jahannamu itawatosha; wataingia humo! Na hayo ndiyo marejeo maovu yaliyoje!"¹

Isnadi yake ni Hasan, lakini wao Al-Bukhari na Muslim hawakuiandika.

Adabu za Najwa, (Mazungumzo ya Siri)

Allah تعالى Anawafundisha waja Wake waumini kuepuka njia za makafiri na wanafiki,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا تَنَجَّيْتُمْ فَلَا تَتَنَجَّوْا بِالْأَيْمِ وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَتِ الرَّسُولِ

"Enyi mlioamini! Mnaponong'ona msinong'one kwa sababu ya mambo ya madhambi, na uadui, na kumuasi Mtume."

Yaani, msifanye mazungumzo ya siri kama makafiri wajinga miongoni mwa Watu waliopewa Kitabu na washirika wao miongoni mwa wanafiki, wanaoiga njia zao,

وَتَتَنَجَّوْا بِالْيَمِينِ وَالْتَّقْوَىٰ ۗ وَأَتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ

"Bali mnong'onezane kwa kutenda mema na kuacha maovu. Na mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye Kwake mtakusanywa nyote."

Na kisha Atakuambieni amali zenu na maneno yenu yote; ambayo Ameyahifadhi na Atakulipeni kwa hayo.

Allah تعالى Amesema,

¹ Ahmad 2:170.

إِنَّمَا النَّجْوَى مِنَ الشَّيْطَانِ لِيَحْزُبَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَيْسَ بِضَارِّهِمْ شَيْئًا إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ
وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٥٨﴾

“Kwa hakika minong’ono inatokana na Shetani ili awahuzunisha walioamini, na wala haitawadhuru chochote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na juu ya Mwenyezi Mungu tu ndio wategemee Waumini.”

Allah تعالى Anaeleza kuwa minong’ono, ya uovu kwa waumini ni,

مِنَ الشَّيْطَانِ لِيَحْزُبَ الَّذِينَ ءَامَنُوا

“...inatokana na Shetani ili awahuzunisha walioamini...”

Maana yake: Wenye kufanya siri hizo, hufanya hivyo kwasababu ya udanganyifu wa shetani,

لِيَحْزُبَ الَّذِينَ ءَامَنُوا

“...ili awahuzunisha walioamini...”

Shetani hutafuta kuwaharibia waumini, ingawa hila zake hazitawadhuru waumini, isipokuwa Allah تعالى Akitaka. Wenye kupatwa na shari yao hiyo, basi ajikinge kwa Allah تعالى na amtumaini Yeye, kwani hakuna kitakachomdhuru, Allah تعالى Akitaka.

Sunnah pia inakataza minong’ono hiyo ya kishari ili kusiwe na Muislamu wa kusumbuliwa nayo. Imamu Ahmad amenukuu kuwa ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا كُنتُمْ ثَلَاثَةً فَلَا يَتَنَاجَى اِثْنَانٍ دُونَ صَاحِبَيْهِمَا، فَإِنَّ ذَلِكَ يُحْزِنُهُ»

“Mkiwa watatu, basi wawili kati yenu wasinong’one na kumuacha mwenzao, kwasababu hilo litamhuzunisha.”¹

Hadith hii ilikusanywa katika Sahihi Mbili kwa kutumia isnadi ya masimulizi ya Al-A’mash.² ‘Abdur-Razzaq amesimulia kuwa ‘Abdullah bin ‘Umar رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ Ahmad 1:425, 431.

² *Fat’h Al-Bari* 11:58, Muslim 4:1718.

«إِذَا كُنتُمْ ثَلَاثَةً فَلَا يَتَنَاجَىٰ اِثْنَانِ دُونَ صَاحِبِهِمَا ، فَإِنَّ ذَٰلِكَ يُخْزِنُهُ»

“Kama mtakuwa watu watatu, basi wawili kati yenu wasinong’one bila ya mtu wa tatu, isipokuwa kwa idhini yake, kwasababu hilo litamhuzunisha.”¹ Muslim aliikusanya Hadithi hii.²

* * *

¹Abdur-Razzaq 11:26.

²Muslim 4:1717.

فَأَفْسَحُوا يَفْسَحِ اللَّهُ لَكُمْ^ط

“Basi fanyeni nafasi, Na Mwenyezi Mungu Atakufanyieni nyinyi nafasi..”

Kwa hakika, malipo ni jinsi ya kitendo. Katika Hadith, Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ بَنَى لِلَّهِ مَسْجِدًا بَنَى اللَّهُ لَهُ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ»

“Mwenye kujenga Masjid kwa ajili ya Allah, Allah Humjengea nyumba Peponi.”¹

Katika hadithi nyingine, Mtume ﷺ amesema,

«وَمَنْ يَسَّرَ عَلَى مُعْسِرٍ يَسَّرَ اللَّهُ عَلَيْهِ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، وَاللَّهُ فِي عَوْنِ الْعَبْدِ مَا كَانَ الْعَبْدُ فِي عَوْنِ أَخِيهِ»

“Mwenye kumuondolea shida mtu, basi Allah Atamuondolea shida za duniani na Akhera. Kwa hakika, Allah Humsaidia mja madamu mja anamsaidia nduguye.”²

Kuna Hadithi nyingi zinazoelezea maudhui haya, Allah تعالى Amesema,

فَأَفْسَحُوا يَفْسَحِ اللَّهُ لَكُمْ^ط

“...basi fanyeni nafasi. Na Mwenyezi Mungu Atakufanyieni nyinyi nafasi...”

Qatadah amesema, “Aya hii ilishuka kuhusu mikusanyiko katika sehemu ambazo Allah تعالى Hutajwa. Mtu alipokuja kujiunga katika mkutano kujiunga pamoja na Mtume ﷺ, watu walikuwa wakisita kumuachia nafasi ili wasipoteze nafasi zao. Allah تعالى Akawaamuru wasogee na kuachiana nafasi.”³

¹ Fath Al-Bari 1:648.

² Muslim 4:2074.

³ At-Tabari 23:244.

Imamu Ahmad na Imamu Ash-Shafi' wamenukuu kuwa 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا يُقِمُّ الرَّجُلُ الرَّجُلَ مِنْ مَجْلِسِهِ فَيَجْلِسَ فِيهِ، وَلَكِنْ تَفَسَّحُوا وَتَوَسَّعُوا»

*"Mmoja wenu asimuondoe mwingine kutoka mahali pake na kukaa hapo, bali asogee na kuacha nafasi."*¹

Hadithi hii imenukuliwa katika Sahihi Mbili.² Imamu Ahmad amenukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا يُقِمُّ الرَّجُلُ الرَّجُلَ مِنْ مَجْلِسِهِ ثُمَّ يَجْلِسُ فِيهِ، وَلَكِنْ اِفْسَحُوا يَفْسَحِ اللَّهُ لَكُمْ»

*"Mtu asimuondoe mwingine kwenye kikao kisha yeye akakaa hapo. Bali asogee na kuacha nafasi na Allah Atakupeni nafasi."*³

Imamu Ahmad pia amenukuu Hadithi hii kwa maneno haya:

*"Mtu asiondoke ili kumuachia nafasi mtu mwingine, bali asogee na kuacha nafasi, na Allah Atakuwekea nafasi."*⁴

Imesimuliwa kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى na wengine wamesema kuwa:

إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُوا فِي الْمَجْلِسِ فَأَفْسَحُوا يَفْسَحِ اللَّهُ لَكُمْ^ط

"Mkiambiwa: Fanyeni nafasi katika mabaraza, basi fanyeni nafasi. Na Mwenyezi Mungu Atakufanyieni nyinyi nafasi."

Inamaanisha mabaraza ya vita, na kwamba,

وَإِذَا قِيلَ أَدْنُوا فَأَدْنُوا

"Na mkiambiwa: Ondokeni, basi ondokeni."

¹ Ahmad 2:126, na *Tartib Ash-Shafii'* 2:186.

² *Fath Al-Bari* 1:64, Muslim 4:1714.

³ Ahmad 2:523.

⁴ Ahmad 2:238

Inamaanisha, "Nendeni mkapigane."¹ Oatadah amesema,

وَإِذَا قِيلَ أَنْشُرُوا فَأَنْشُرُوا

"Na mkiambiwa: Ondokeni, basi ondokeni."

Inamaanisha, "Mkiitwa kwenye jema lolote, basi nendeni."²

Fadhila za Elimu na Watu wa Elimu

Kauli ya Allah تعالى,

يَرْفَعُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَالَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ دَرَجَاتٍ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ

"Mwenyezi Mungu Atawainua walioamini miongoni mwenu, na waliopewa ilimu daraja za juu. Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayo yatenda."

Maana yake: Msidhanie kuwa ikiwa mmoja wenu atamuachia nafasi ndugu yake, au kuinuka anapoamriwa kufanya hivyo, kwamba hilo litapunguza haki au heshima yake. Bali, hilo litazidisha ubora na daraja yake kwa Allah تعالى, na Allah تعالى Hatapoteza jema lake. Kinyume chake, Atamlipa duniani na Akhera. Kwa hakika, anayenyenyeka Amri ya Mola Wake Mlezi, basi Allah تعالى Atainua daraja yake na Kumfanya atambulike kwa tabia yake njema.

Kauli ya Allah تعالى,

يَرْفَعُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَالَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ دَرَجَاتٍ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ

"Mwenyezi Mungu Atawainua walioamini miongoni mwenu, na waliopewa ilimu daraja za juu. Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda."

Maana yake: Kwa hakika, Allah تعالى Anawajua wanaostahiki malipo hayo na wasiostahiki.

¹ At-Tabari 23:244, Al-Qurtubi 17:299, na Ad-Dur Al-Manthur 8:82.

² At-Tabari 23:245.

Ahmad amenukuu kuwa Abu At-Tufayl 'Amir bin Wathilah amesema kuwa Nafi' bin 'Abdul-Harith alikutana na 'Umar bin al-Khattab رضي الله عنه katika sehemu iliyoitwa 'Usfan. 'Umar رضي الله عنه alimteua Abu At-Tufayl kuwa kadhi wa Makkah. 'Umar رضي الله عنه akamuuliza, "Nani unamteua kuwa naibu wako kwa ajili ya watu wa bondeni (yaani, Makkah)." 'Amir akasema, "Nimemteua Ibn Abza, mtumwa aliyepata uhuru, awe naibu wangu." 'Umar رضي الله عنه akasema, "Umefanya mtumwa aliyepata uhuru awe kadhi wo wakati usipokuwepo?" Akasema, "Ewe Amiri wa Waumini! Amehifadhi Kitabu cha Allah تعالى na ana elimu ya taratibu za mirathi, pamoja na kuwa hakimu hodari." 'Umar رضي الله عنه akasema, "Kwa hakika, Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ اللَّهَ يَرْفَعُ بِهَذَا الْكِتَابِ قَوْمًا وَيَضَعُ بِهِ الْآخَرِينَ»

*"Kwa hakika, Allah Huwatukuza watu kwa kitabu hiki na Kuwadhalilisha wengine."*¹ Muslim aliiandika Hadithi hii.²

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نَجَّيْتُمُ الرُّسُولَ فَقَدِمُوا بَيْنَ يَدَيْ جَوْنِكُمْ صَدَقَةٌ ذَٰلِكَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَأَطْهَرُ ؕ فَإِن لَّمْ تَجِدُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾ ؕ أَشْفَقْتُمْ أَن تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيْ جَوْنِكُمْ صَدَقْتُمْ ؕ فَإِذْ لَمْ تَفْعَلُوا وَتَابَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَءَاتُوا الزَّكَاةَ وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ ؕ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٣﴾

12. Enyi mlioamini! Mnaposema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu. Hiyo ni kheri kwenu na usafi zaidi. Na ikiwa hamkupata cha kutoa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

13. Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu? Ikiwa hamkufanya hayo, na Mwenyezi Mungu Akapokea toba yenu, basi shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda.

¹ Ahmad 1:35.

² Muslim 1:552.

Amri ya Kutoa Sadaka kabla Mtu Hajazungumza Faragha na Mtume ﷺ

Allah تعالى Amewaamuru waumini, mmoja wao anapotaka kuzungumza na Mtume ﷺ faragha, atangulize kutoa sadaka ili sadaka yake imtakase na kumfanya astahiki kuongea na Mtume ﷺ kwa faragha. Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

ذَلِكَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَأَطْهَرٌ

“Hiyo ni kheri kwenu na usafi zaidi.”

Kisha Amesema,

فَإِنْ لَّمْ تَجِدُوا

“Na ikiwa hamkupata...”

Inamaanisha, ikiwa hawezi kufanya hivyo kwa sababu ya umaskini,

فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“...basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Amewaamrisha wale ambao kifedha, wanaweza kutoa sadaka ya aina hii. Allah تعالى Amesema,

ءَأَشْفَقْتُمْ أَنْ تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيْ نَجْوَانِكُمْ صَدَقْتُمْ

“Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu?”

Inamaanisha, kwani mnaogopa amri ya kutoa sadaka kabla ya kuzungumza faragha na Mtume ﷺ kuwa itadumu milele.

فَإِذْ لَمْ تَفْعَلُوا وَتَابَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ

وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ

“Ikiwa hamkufanya hayo, na Mwenyezi Mungu Akapokea toba yenu, basi shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt’iini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayo yatenda.”

Allah تعالی Akafuta wajibu wa kutoa sadaka hii. Ilisemekana kuwa ndiye pekee aliyeitekeleza amri hiyo kabla ya kufutwa, 'Ali bin Abi Talib رضي الله عنه. 'Ali bin Abi Talhah amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما:

فَقَدَّمُوا بَيْنَ يَدَيَّ نَجْوَانَكُمْ صَدَقَةً

“...tangulizani sadaka kabla ya kusemezana kwenu?”

“Waislamu waliendelea kumuuliza Mtume ﷺ maswali mpaka yakamletea dhiki. Allah تعالی Alitaka kumpunguzia dhiki Mtume Wake ﷺ. Kwa hivyo Aliposema hayo, Waislamu wengi walichelea kulipa sadaka hiyo na wao wakaacha kumuuliza. Baadaye, Allah تعالی Aliteremsha Ayah hii,

ءَأَشْفَقْتُمْ أَنْ تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيَّ نَجْوَانَكُمْ صَدَقْتُمْ ۖ فَإِذَا لَمْ تَفْعَلُوا وَتَابَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ
فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ

“Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu? Ikiwa hamkufanya hayo, na Mwenyezi Mungu Akapokea toba yenu, basi shikeni Sala, na toeni Zaka...”

Kwa hivyo Allah تعالی Aliwarahisishia.”¹

‘Ikrimah na Al-Hasan Al-Basri ametoa rai juu ya Kauli ya Allah تعالی:

فَقَدَّمُوا بَيْنَ يَدَيَّ نَجْوَانَكُمْ صَدَقَةً

“...tangulizani sadaka kabla ya kusemezana kwenu?”

Hayo yalifutwa na Ayah ifuatayo:

ءَأَشْفَقْتُمْ أَنْ تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيَّ نَجْوَانَكُمْ صَدَقْتُمْ ۖ

“Mnachelea kutanguliza hiyo sadaka kabla ya kusemezana kwenu?”²

¹ At-Tabari 23:249. Angalia sehemu inayohusu Hadithi mwanzoni mwa kitabu hiki.

² At-Tabari 23:250.

“Sa’id bin Abi`Arubah amesimulia kutoka kwa Qatadah na Muqatil bin Hayyan kwamba, “Watu waliendelea kumuuliza Mtume ﷺ mpaka wakasababisha akawa katika hali ngumu. Allah تعالى Akampa nafasi ya kuzuia tabia yao hiyo kwa kutumia Aya hiyo. Baada ya hapo, mtu aliyetaka kuzungumza na Mtume ﷺ kuhusu jambo mahususi, alitakiwa kutoa sadaka. Hilo likawa zito kwa watu na Allah تعالى Akateremsha baadaye Aya nyingine iliyowapa unafuu,

فَإِنْ لَّمْ تَجِدُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Na ikiwa hamkupata cha kutoa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”¹

Ma’mar amesimulia kutoka kwa Qatadah kuwa Aya,

إِذَا نَجَّيْتُمُ الرُّسُولَ فَقَدِمُوا بَيْنَ يَدَيْ نَجْوَانِكُمْ صَدَقَةٌ

“Mnapo sema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu.”

Ilifutwa baada ya kutumika kwa saa moja tu ya mchana.² ‘Abdur-Razzaq amenukuu kuwa Mujahid amesema kuwa ‘Ali رضي الله عنه alisema, “Si mwingine, bali mimi peke yangu nilitekeleza Aya hiyo, mpaka ilipofutwa,” na ninadhani kuwa alisema, “ilidumu kwa saa moja tu.”³

أَلَمْ نَرِ إِلَى الَّذِينَ تَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مَا هُمْ مِنْكُمْ وَلَا مِنْهُمْ وَيَخْلِفُونَ عَلَى
 الْكَذِبِ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١١﴾ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢﴾
 أَخَذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ فَلَهُمْ عَذَابٌ مُهِينٌ ﴿١٣﴾ لَنْ تَغْنِي عَنْهُمْ
 أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ؕ أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١٤﴾ يَوْمَ
 يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيَخْلِفُونَ لَهُ كَمَا يَخْلِفُونَ لَكُمْ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ ؕ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ
 الْكَاذِبُونَ ﴿١٥﴾ اسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ الشَّيْطَانُ فَأَنسَلَهُمْ ذِكْرَ اللَّهِ ؕ أُولَئِكَ حِزْبُ الشَّيْطَانِ
 ؕ أَلَا إِنَّ حِزْبَ الشَّيْطَانِ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٦﴾

¹ At-Tabari 23:248.

² At-Tabari 23:249.

³ ‘Abdur-Razzaq 3:280.

14. Huwaoni wale waliofanya urafiki na watu ambao Mwenyezi Mungu Amewakasirikia? Hao si katika nyinyi, wala si katika wao. Na huapa kwa uwongo, na hali kuwa wanajua.

15. Mwenyezi Mungu Amewaandalia adhabu kali. Kwa hakika waliyokuwa wakiyatenda ni maovu kabisa.

16. Wamefanya viapo vyao ni ngao, na wakaipinga Njia ya Mwenyezi Mungu. Basi hao watapata adhabu ya kufedhehesha.

17. Hayatawafaa kitu mali yao wala watoto wao mbele ya Mwenyezi Mungu. Hao ndio watu wa Motoni. Humo watadumu milele.

18. Siku Atakayowafufua Mwenyezi Mungu wote, wamuwapie kama wanavyokuwapieni nyinyi. Na watadhani kuwa wamepata kitu! Kwa hakika hao ndio waongo.

19. Shetani amewatawala na akawasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hao ndio kundi la Shetani. Kweli hakika kundi la Shetani ndilo lenye kukhasirika.

Kuwarudi Wanafiki

Allah تعالیٰ Anawarudi wanafiki kwa kitendo chao cha kuwasaidia na kuwaunga mkono makafiri kisiri ingawa, kiukweli, hawakuwa pamoja na makafiri wala Waislamu. Allah تعالیٰ Amesema katika Aya nyingine,

مُدَبِّدِينَ بَيْنَ ذَلِكَ لَا إِلَىٰ هَٰؤُلَاءِ وَلَا إِلَىٰ هَٰؤُلَاءِ ۚ وَمَن يُضْلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهٗ سَبِيلًا ﴿١٤٣﴾

“Wanayumbayumba baina ya huku na huko. Huku hawako na huko hawako. Na ambaye Mwenyezi Mungu Amemuacha apotee, kabisa hutompatia njia.” (4:143)

Kauli ya Allah تعالیٰ hapa,

أَلَمْ تَرَ إِلَىٰ الَّذِينَ تَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ

“Huwaoni wale waliofanya urafiki na watu ambao Mwenyezi Mungu Amewakasirikia?”

Maana yake: Wayahudi ambao wanafiki walikuwa washirika wao kisiri. Kauli ya Allah تعالى،

مَا هُمْ مِنْكُمْ وَلَا مِنْهُمْ

“Hao si katika nyinyi, wala si katika wao.”

Wanafiki hao hawako pamoja na waumini, wala washirika wao, Wayahudi.

وَيَحْلِفُونَ عَلَى الْكُذِبِ وَهُمْ يَعْلَمُونَ

“Na huapa kwa uwongo, na hali kuwa wanajua.”

Inamaanisha, wanafiki hudanganya wanapoapa, huku wanajua kuwa wanadanganya, na hicho kinaitwa kiapo cha *Al-Ghamus*. Tunajikinga kwa Allah تعالى dhidi ya njia zao. Wanafiki wanapokutana na waumini husema kuwa wanaamini na wanapokwenda kwa Mtume ﷺ, humuapia kwa Allah تعالى kuwa walikuwa waumini. Walijua kuwa walikuwa wakiongopa katika kiapo chao, na walijua kuwa hawakutamka itikadi yao ya kweli. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Ameshuhudia hapa kuwa wanadanganya katika viapo vyao na Anajua kuwa wanaongopa, ingawa kauli yao kwa Mtume ﷺ ni kweli kimsingi. Allah تعالى Amesema,

أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٥٨﴾

“Mwenyezi Mungu Amewaandalia adhabu kali. Kwa hakika waliyo kuwa wakiyatenda ni maovu kabisa.”

Maana yake: Allah تعالى Amewaandalia wanafiki adhabu iumizayo kutokana na maovu yao, kuwasaidia kwao makafiri na uongo wao na usaliti kwa waumini. Kauli ya Allah تعالى،

اتَّخَذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

“Wamefanya viapo vyao ni ngao, na wakaipinga Njia ya Mwenyezi Mungu.”

Inamaanisha, wanafiki walisingizia kuwa waumini na wakaficha ukafiri kwa kinga ya viapo vyao vya uongo. Wengi hawakuwa wakiujua msimamo wao wa kweli na kwa hivyo wakadanganyika kwa viapo vyao. Kwa sababu ya hilo, baadhi ya watu walizuilika dhidi ya Njia ya Allah تعالى،

فَلَهُمْ عَذَابٌ مُّهِينٌ

“Basi hao watapata adhabu ya kufedhehesha.”

Inamaanisha, kama jaza kwa kudharau umuhimu wa kuapa kwa Jina la Allah تعالى, ilhali wakidanganya na kusaliti. Allah تعالى Amesema,

لَنْ تُغْنِيَ عَنْهُمْ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا

“Hayatawafaa kitu mali yao wala watoto wao mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Mali yao yoyote haitaweza kuwaepushia janga litakapotumwa kwao.

أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

“Hao ndio watu wa Motoni. Humo watadumu milele.”

Allah تعالى Amesema,

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا

“Siku Atakayowafufua Mwenyezi Mungu wote.”

Inamaanisha Siku ya Ufufuo ambapo Atawakusanya wote kwa pamoja na hatamuacha yeyote katika wao,

فَيَخْلِفُونَ لَهُمْ كَمَا يَخْلِفُونَ لَكُمْ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ

“...wamuapie kama wanavyokuapieni nyinyi. Na watadhani kuwa wamepata kitu!”

Inamaanisha, wataapa kwa Allah تعالى kuwa walikuwa wakifuata uongofu na njia sahihi, kama walivyokuwa wakiwaapia waumini duniani. Kwa hakika, wanaoishi kwa kufuata desturi fulani wanaweza kufa wakiwa katika hali hiyo. Kwa hivyo, watafufuliwa katika njia yao. Wanafiki watadhani kuwa viapo vyao vitawasaidia kwa Allah تعالى, kama vilivyowasaidia kwa watu, kwa jinsi walivyojisingizia. Kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema,

وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ ۚ

“Na watadhani kuwa wamepata kitu!”

Inamaanisha, kwa kumuapia Mola Wao Mlezi (kuwa walikuwa waumini). Allah تعالى Anakemea fikra yao hiyo;

أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْكَاذِبُونَ

“Kwa hakika hao ndio waongo.”

Inasisitiza kuwa wanadanganya, Allah تعالى Alisema;

أَسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ الشَّيْطَانُ فَأَنسَهُمْ ذِكْرَ اللَّهِ ۚ

“Shetani amewatawala na akawasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu.”

Inamaanisha, Shaytan amezifikisha nyoyo zao kwa kiasi ambacho amewafanya wamsahau Allah تعالى. Hayo ndiyo ambayo Shetani huwafanyia. Abu Dawud amenukuu kuwa Abu Ad-Darda رضي الله عنه amesema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«مَا مِنْ ثَلَاثَةٍ فِي قَرْيَةٍ وَلَا بَدْوٍ، لَا تُقَامُ فِيهِمُ الصَّلَاةُ إِلَّا قَدِ اسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ الشَّيْطَانُ، فَعَلَيْكَ بِالْجَمَاعَةِ، فَإِنَّمَا يَأْكُلُ الذُّبُّ الْقَاصِيَةَ»

“Watu watatu katika kijiji au jangwa hawaachi kusimamsha Sala, isipokuwa Shaytan amewadhibiti. Kwa hivyo, shikamana na Jama`ah, kwani mbwa mwitu humla kondoo aliyepotea.”

Za'idah ameongeza kuwa As-Sa'ib amesema kuwa Jama`ah, inamaanisha, “Kusali katika jamaa.”¹ Allah تعالى Amesema,

أُولَئِكَ حِزْبُ الشَّيْطَانِ ۚ

“Hao ndio kundi la Shetani.”

¹ Abu Dawud 1:371.

Inamaanisha wenye kudhibitiwa na shetani na matokeo yake, ni kusahau kumtaja Allah تعالى,

أَلَا إِنَّ حِزْبَ الشَّيْطَانِ هُمُ الْخٰسِرُونَ

“Kweli hakika kundi la Shetani ndilo lenye kukhasirika.”

* * *

إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۗ أُولَئِكَ فِي الْأَذَلِّينَ ﴿٢٠﴾
 كَتَبَ اللَّهُ لَأَعْلَيْنَ أَنَا وَرُسُلِي ۗ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ
 ﴿٢١﴾ لَا يَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
 يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ
 أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ ۗ أُولَئِكَ كَتَبَ فِي
 قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ ۖ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ
 تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ
 وَرَضُوا عَنْهُ ۗ أُولَئِكَ حِزْبُ اللَّهِ ۗ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ
 الْمُفْلِحُونَ ﴿٢٢﴾

إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۗ
 أُولَئِكَ فِي الْأَذَلِّينَ ﴿٢٠﴾ كَتَبَ اللَّهُ
 لَأَعْلَيْنَ أَنَا وَرُسُلِي ۗ إِنَّ اللَّهَ
 قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢١﴾ لَا يَجِدُ قَوْمًا
 يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
 يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ
 كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ
 إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ ۗ أُولَئِكَ
 كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُمْ
 بِرُوحٍ مِّنْهُ ۖ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي

مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ۗ أُولَئِكَ حِزْبُ اللَّهِ ۗ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ
 هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٢٢﴾

20. Hakika wanaopinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hao ndio miongoni mwa madhalili wa mwisho.

21. Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.

22. Huwakuti watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanaopinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao Ameandika katika nyoyo zao Imani, na Amewapa nguvu kwa Roho itokayo Kwake. Na Atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu Awe radhi nao, na wao wawe radhi Naye. Hao ndio Hizbullahi, Kundi la Mwenyezi Mungu. Hakika Kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufanikiwa.

Wapinzani wa Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ ni Washindwa na Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ ni Washinda;

Allah تعالی Anasema kuwa waasi na makafiri wakaidi wenye kumkataa Yeye na Mjumbe Wake, wasioingia katika dini na wanajiweka mbali na Ukweli, wako katika upande mwingine, ilhali uongofu nao uko katika upande mwingine,

أُولَئِكَ فِي الْأَذْدَانِ

“...hao ndio miongoni mwa madhalili wa mwisho.”

Waovu, wenye kuwekwa mbali na heri; watadhalilishwa duniani na Akhera. Kauli ya Allah تعالی,

كَتَبَ اللَّهُ لَأَعْلَبَنَ أَنَا وَرُسُلِي

“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda.”

Inamaanisha, Ametoa hukumu, iliyoandikwa katika Kitabu cha Kwanza, na Ameamua katika hukumu kama Alivyotaka – ambayo kamwe haiwezi kupingwa, kubadilishwa au kuzuiwa — kuwa ushindi wa mwisho ni wao, Kitabu Chake, Mtume Wake na waja Wake waumini, duniani na Akhera:

إِنَّ الْعَاقِبَةَ لِلْمُتَّقِينَ

“Hakika Mwisho ni wa wachamngu.” (11:49),

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾ يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ ۖ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٥٢﴾

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi, Siku ambayo hautawafaa madhaalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata makaazi mabaya kabisa.” (40:51-52).

Kauli ya Allah تعالی hapa,

كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ۗ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٠﴾

“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.”

Inamaanisha, Allah تعالى Amepitisha Amri kuwa Atawashinda maadui Zake. Kwa hakika, hii ni hukumu ya mwisho na jambo lililopangwa tayari; ushindi wa mwisho ni kwa waumini duniani na Akhera.

Waumini Hawafanyi Urafiki na Makafiri

Allah تعالى Amesema,

لَا يَتَّخِذُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ ۗ

“Huwakuti watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao.”

Inamaanisha: Msiwe marafiki wakadhibishaji, hata kama wao ni katika jamaa wa karibu kabisa.

Kauli ya Allah تعالى,

لَا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ۗ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ اللَّهِ فِي شَيْءٍ إِلَّا أَنْ تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقَنَّةً وَيُحَذِّرْكُمْ اللَّهُ نَفْسَهُ ۗ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٢١﴾

“Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa na chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.” (3:28), na,

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا
وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنْ رَبِّ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي
سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّى يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرٍ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٠﴾

“Sema: Ikiwa baba zenu, na wenenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyoyachuma, na biashara mnazoogopa kuharibika, na majumba mnayoyapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Jihadi katika Njia Yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu Alete Amri Yake. Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wapotovu.” (9:24)

Sa'id bin 'Abdul-'Aziz na wengine wamesema kuwa Ayah hii,

لَا يَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

“Huwakuti watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho...”

Aya hii ilishuka kumhusu Abu 'Ubaydah 'Amir bin 'Abdullah bin al-Jarrah رضي الله عنه alipomuua baba yake aliyekuwa kafiri, wakati wa vita vya Badr.¹ Kwa ajili hiyo, 'Umar bin al-Khattab رضي الله عنه aliliweka jambo la Khilafah katika mashauriano ya watu sita mbele yake, akasema; “Kama Abu 'Ubaydah angekuwa hai, ningemteua awe Khalifah.” Pia ilisemwa katika Kauli ya Allah تعالى،

وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ

“...hata wakiwa ni baba zao...” Ilishuka kumhusu Abu 'Ubaydah رضي الله عنه, alipomuua baba yake katika vita vya Badr, ilhali Aya،

أَوْ أَبْنَاءَهُمْ

“...au watoto wao...” Ilishuka kumhusu Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه alipokusudia kumuua mwanaye (aliyekuwa kafiri), 'Abdur-Rahman, (katika Vita vya Badr), ilhali Aya،

¹ Angalia *Al-Isabah* chini ya wasifu wa 'Amir bin 'Abdullah bin Al-Jarrah. Hapo imesimuliwa na 'Abdullah bin Shawdhab, bin Hajar amesema kuwa At-Tabarani alikuwa na isnadi nzuri kuihusu. Hata hivyo, Hadithi hizo ni *Mursal*.

أَوْ إِخْوَانَهُمْ

“...*au ndugu zao...*” ilishuka kumhusu Mus’ ab bin ‘Umayr رضي الله عنه, aliyemuua ndugu yake, ‘Ubayd bin ‘Umayr, katika Vita vya Badr, na kuwa Aya,

أَوْ عَشِيرَتِهِمْ

“...*au jamaa zao.*” ilishuka kumhusu ‘Umar رضي الله عنه, aliyemuua mmoja katika jamaa zake katika Vita vya Badr, na pia kuwa Aya hii ilishuka kumhusu Hamzah, ‘Ali na Ubaydah bin al-Harith رضي الله عنهم. Waliwaua jamaa zao wa karibu, ‘Utbah, Shaybah na Al-Walid bin ‘Utbah katika Vita hivyo. Allah تعالى Anajua zaidi. Jambo kama hilo ni wakati Mtume ﷺ aliposhauriana na Masahaba wake رضي الله عنهم kuhusu jambo la kuwafanyia mateka wa vita vya Badr. Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه alitoa wazo kuwa wapokee fidia yao ili Waislamu waweze kuzitumia katika kujiimarisha zaidi.

Alieleza ukweli kuwa mateka walikuwa mabinamu na wanaukoo, na kuwa huenda wangesilimu baadaye, kwa msaada wa Allah تعالى. ‘Umar رضي الله عنه akasema, “Lakini mimi nina rai tofauti, Ewe Mjumbe wa Allah! Acha mimi nimuue fulani, jamaa yangu, na ‘Ali amuue ‘Aqil (kaka yake ‘Ali), na fulani amuue fulani. Hebu ijulikane wazi kwa Allah تعالى kuwa hatuwahurumii hawa washirikina.” Kauli ya Allah تعالى,

أُولَئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ

“Hao Ameandika katika nyoyo zao Imani, na Amewapa nguvu kwa Roho itokayo Kwake.”

Maana: Waliokuwa na sifa ya kutokufanya urafiki na wenye kumhalifu Allah na Mjumbe Wake, hata kama wao ni wazazi wao au ndugu, ni wale ambao Allah تعالى Amewajaalia imani. Yaani, furaha, katika nyoyo zao na huipenda zaidi imani nyoyoni mwao na furaha inakaa humo. As-Suddi amesema kuwa Aya,

كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ

“Hao Ameandika katika nyoyo zao Imani...”

Inamaanisha “Ametia imani nyoyoni mwao.” Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa,

وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ

“...na Amewapa nguvu kwa Roho itokayo kwake...” Inamaanisha “Amewapa nguvu.” Kauli ya Allah تعالى،

وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا رَضُوا بِاللَّهِ عَنِيبًا وَرَضُوا عَنْهُ

“Na Atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu Awe radhi nao, na wao wawe radhi Naye.”

Imeelezwa mara kadhaa hapo kabla. Kauli ya Allah تعالى،

رَضُوا بِاللَّهِ عَنِيبًا وَرَضُوا عَنْهُ

“Mwenyezi Mungu Awe radhi nao, na wao wawe radhi Naye.”

Hapa pana siri ya ajabu. Waumini watakapokasirishwa dhidi ya ndugu na jamaa zao kwa ajili ya njia ya Allah تعالى، Aliwalipa kwa kuwa radhi nao na Kuwafanya wawe radhi Kwake kwa kuwapa furaha ya milele, ushindi wa mwisho na neema yenye kuenea. Kauli ya Allah تعالى،

أُولَئِكَ حِزْبُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

“Hao ndio Hizbullahi, Kundi la Mwenyezi Mungu. Hakika Kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufanikiwa.”

Inaashiria kuwa wao kundi la Allah تعالى، yaani, Waja Wake wenye kustahiki kupata heshima Yake. Kauli ya Allah تعالى،

أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٦١﴾

“Hakika Kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufanikiwa.” Inaeleza kufaulu kwao, furaha na ushindi duniani na Akhera, kinyume cha wale ambao ni kundi la Shetani.

أَلَا إِنَّ حِزْبَ الشَّيْطَانِ هُمُ الْخَاسِرُونَ

“Kweli hakika kundi la shetani ndilo lenye kukhasirika.”

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya Surat Al-Mujadilah. Sifa zote njema na shukrani ni za Allah تعالى.

Tafsiri ya Suratul Hashr

Sura ya 59

Iliteremshwa Madinah

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alikuwa akiita sura hii, 'Surah Bani An-Nadhir.'¹ Sa'id bin Mansur amenukuu kuwa Sa'id bin Jubayr amesema, "Nilimuuliza Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuhusu Surat Al-Hashr na akasema, 'Ilishuka kuhusu Bani An-Nadhir.'" Al-Bukhari na Muslim wameinukuu kwa isnadi nyingine kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما.²

Al-Bukhari pia ameinukuu kutoka kwa Abu 'Awanah, kutoka kwa Abu Bishr kutoka kwa Sa'id bin Jubayr, ambaye alisema, "Nilimuuliza Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuhusu 'Surat Al -Hashr' akasema, 'Surah Bani An-Nadhir.'³



¹ *Fath Al-Bari* 8:497.

² *Fath Al-Bari* 8:497, *Muslim* 4:2322.

³ *Fath Al-Bari* 8:497.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْحَشْرِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ
 الْحَكِيمُ ﴿١﴾ هُوَ الَّذِي أَخْرَجَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ
 الْكِنَابِ مِنْ دِيَارِهِمْ لِأَوَّلِ الْحَشْرِ ۗ مَا ظَنَنْتُمْ أَنْ يَخْرُجُوا ۗ
 وَظَنُوا أَنَّهُمْ مَابِعْثُهُمْ حُصُوبُهُمْ مِنَ اللَّهِ فَأَتَتْهُمْ
 اللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا ۗ وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ ۗ يُخْرِبُونَ
 بُيُوتَهُمْ بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ فَاعْتَبِرُوا يَا أُولِيَ
 الْأَبْصَارِ ﴿٢﴾ وَلَوْلَا أَنْ كَتَبَ اللَّهُ عَلَيْهِمُ الْجَلَآءَ لَعَذَّبَهُمْ
 فِي الدُّنْيَا ۗ وَهُمْ فِي الْأَخِرَةِ عَذَابِ النَّارِ ﴿٣﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُوا اللَّهَ
 وَرَسُولَهُ ۗ وَمَنْ يُشَاقِقِ اللَّهَ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٤﴾ مَا
 قَطَعْتُمْ مِنْ لَيْتَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوهَا قَائِمَةً عَلَى أُصُولِهَا
 فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيُخْرِىَ الْفَاسِقِينَ ﴿٥﴾

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي
 الْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١﴾
 هُوَ الَّذِي أَخْرَجَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ
 أَهْلِ الْكِنَابِ مِنْ دِيَارِهِمْ لِأَوَّلِ
 الْحَشْرِ ۗ مَا ظَنَنْتُمْ أَنْ يَخْرُجُوا
 وَظَنُوا أَنَّهُمْ مَابِعْثُهُمْ حُصُوبُهُمْ مِنَ اللَّهِ
 فَأَتَتْهُمْ اللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا ۗ
 وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ ۗ يُخْرِبُونَ
 بُيُوتَهُمْ بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ
 فَاعْتَبِرُوا يَا أُولِيَ الْأَبْصَارِ ﴿٢﴾
 وَلَوْلَا أَنْ كَتَبَ اللَّهُ عَلَيْهِمُ الْجَلَآءَ لَعَذَّبَهُمْ
 فِي الدُّنْيَا ۗ وَهُمْ فِي الْأَخِرَةِ عَذَابِ
 النَّارِ ﴿٣﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُوا اللَّهَ
 وَرَسُولَهُ ۗ وَمَنْ يُشَاقِقِ اللَّهَ فَإِنَّ اللَّهَ

شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٤﴾ مَا قَطَعْتُمْ مِنْ لَيْتَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوهَا قَائِمَةً عَلَى أُصُولِهَا فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيُخْرِىَ

الْفَاسِقِينَ ﴿٥﴾

1. Vinamsabihi, Vinamtakasa Mwenyezi Mungu viliomo katika mbingu na viliomo katika ardhi. Naye ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.

2. Yeye Ndiye Aliyewatoa waliokufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu katika nyumba zao wakati wa uhamisho wa kwanza. Hamkudhani kuwa watatoka, nao walidhani kuwa ngome zao zitawalinda na Mwenyezi Mungu. Lakini Mwenyezi Mungu Aliwafikia kwa mahali wasipopatazamia, na Akatia woga katika nyoyo zao. Wakawa wanazibomoa nyumba zao kwa mikono yao na mikono ya Waumini. Basi zingatieni enyi wenye macho!

3. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Asingeliwaandikia kutoka, Angeliwaadhibu katika dunia. Na katika Akhera watapata adhabu ya Moto.

4. Hayo ni kwa sababu walimpinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na mwenye kumpinga Mwenyezi Mungu, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu.

5. Mtende wowote mlioukata au mliouacha unasimama vile vile juu ya mashina yake, basi ni kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu, na kwa Kuwadhalilisha wapotovu.

Kila kitu Kinamtukuza Allah تعالیٰ kwa Namna Yake

Allah تعالیٰ Anaeleza kuwa kila kitu mbinguni na ardhini kinamsifu, kumtukuza, kumnyenyekeka na kumuomba Yeye na kushuhudia Tauhidi Yake. Kauli ya Allah تعالیٰ katika Aya nyingine,

كُسِّحُ لَهُ السَّمَوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسْحَبُ حَمْدِهِ وَلَكِنْ لَا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٥٩﴾

“Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa Sifa Zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa Kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye Msamaha.” (17:44) Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَهُوَ الْعَزِيزُ

“Naye ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Maana yake: Utukufu Wake usiozidiwa,

الْحَكِيمُ

“Mwenye Hikima.” Katika Anachoamua na Kuhukumu.

Mambo Yaliyowakuta Bani An-Nadhir

Kauli ya Allah تعالى،

هُوَ الَّذِي أَخْرَجَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ

“Yeye Ndiye Aliyewatoa waliokufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu...”

Inamaanisha kabila la Kiyahudi la Bani An-Nadhir, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas, Mujahd, Az-Zuhri na wengine kadhaa رضي الله عنهم¹.

Mtume ﷺ alipohamia Al-Madinah, aliwekeana mkataba wa amani na Wayahudi uliokuwa na masharti kuwa asiwapige na wao wasimpige. Mara wakakiuka mkataba huo. Kwa hiyo, Allah تعالى Akawateremshia adhabu; isiyozuilika, na Kudura Yake Aliyoipanga ili wafikia; kamwe haikingiki. Mtume ﷺ aliwalazimisha kuacha ngome yao na kuondoka ambapo Waislamu hawakudhania kuwa wangeweza kudhibiti. Wayahudi walidhania kuwa ngome zingewasaidia dhidi ya adhabu ya Allah تعالى, lakini hazikuwasaidia hata kidogo dhidi ya Allah تعالى. Tena, hawakutarajia kuwajia adhabu kutoka kwa Allah تعالى, na Mjumbe wa Allah ﷻ akawalazimisha kuondoka Al-Madinah. Baadhi yao walikwenda Adhri‘at huko Ash-Sham, ambayo ni ardhi ya Mkusanyiko na Ufufuo, ilhali wengine walikwenda Khaybar. Mtume ﷺ aliwaruhusu waondoke katika ngome zao na wachukue chochote ambacho ngamia wao wangeweza kubeba. Waliharibu mali walizoshindwa kuzibeba. Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

مُخْرَبُونَ يُؤْتِمُّونَ بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ فَاعْتَبِرُوا يَا أُولِيَ الْأَبْصَارِ

“Wakawa wanazibomoa nyumba zao kwa mikono yao na mikono ya Waumini. Basi zingatieni enyi wenye macho!”

Inamaanisha, “Tafakarini mwisho wa waliopinga Amri ya Allah تعالى, wakamkana Mjumbe Wake na kukataa Kitabu Chake. Angalieni jinsi adhabu ifedheheshayo ya Allah تعالى ilivyowasibu wao duniani, pia kama, adhabu iumizayo ambayo Allah تعالى Amewawekea huko Akhera.” Abu Dawud amenukuu

¹ At-Tabari 23:262

kuwa 'Abdur-Rahman bin Ka`b bin Malik amesema kuwa Swahaba mmoja wa Mtume ﷺ amesema, "Washirikina wa Kikuraishi walimuandikia 'Abdullah bin Ubayy na wale waliokuwa bado wakiabudu masanamu katika makabila ya Al-Aws na Al-Khazraj. Mtume ﷺ alikuwepo Al-Madinah kwa wakati huo, kabla ya kuzuka vita vya Badr. Waliandika: 'Mmewapa hifadhi watu wetu. Wallahi, mnapaswa kuwapiga, au tutakufukuzeni au kukusanya majeshi yetu yote, mpaka tuwae askari wenu na kuwateka wanawake wenu."

Habari hizo za vitisho zilipomfikia 'Abdullah bin Ubayy na washirikina wa Al-Aws na Al-Khazraj, walijiandaa kumpiga vita Mtume ﷺ. Habari hizo zilipomfikia Mtume ﷺ aliwaendea na kuwaambia,

«لَقَدْ بَلَغَ وَعِيدُ فُرَيْشٍ مِنْكُمْ الْمَبَالِغَ، مَا كَانَتْ تَكِيدُكُمْ بِأَكْثَرِ مِمَّا تُرِيدُ أَنْ تَكِيدُوا بِهِ
أَنْفُسَكُمْ، تُرِيدُونَ أَنْ تُقَاتِلُوا أَبْنَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ»

"Kitisho cha Makuraishi kimekupeni wasiwasi mkubwa! Makuraishi hawawezi kukupeni madhara kuliko mtakavyojiletea madhara wenyewe kwa vitendo vyenu. Je, mnataka kuwapiga vita watoto wenu na ndugu zenu!"

Waliposikia maneno hayo kutoka kwa Mtume ﷺ walitawanyika na habari za yaliyojiri ziliwafikia washirikina wa Kikuraishi. Baada ya vita vya Badr, Washirikina wa Kikuraishi waliwaandikia Wayahudi wa Al-Madinah, 'Mna deraya na ngome! Wapigeni watu wetu au tutakufanyieni hili na lile, na hakuna atakayetuzuia kuwachukua wanawake wenu." Habari za barua hii pia ilimfikia Mtume ﷺ na Bani An-Nadhir walitaka kusaliti mkataba. Bani An-Nadhir wakatuma ujumbe kwa Mtume ﷺ kumuomba aende na Masahaba wake thelathini رضي الله عنهم ili kukutana na wajuzi wao thelathini katikati ya njia, kutoka kila upande. Wakasema kuwa wajuzi na waledi wao nao kama wangemsikiliza Mtume ﷺ na kumuamni, basi Bani An-Nadhir waliosalia wangeamini. Walitaka kumuua Mtume ﷺ, na Allah تعالى Akamjulisha Mtume Wake kuhusu njama hizo za kutaka kumdhuru. Siku iliyofuata, Mtume ﷺ alikusanya majeshi yake na kuzingira eneo hilo, na akawaambia,

«إِنَّكُمْ وَاللَّهِ لَا تَأْمُنُونَ عِنْدِي إِلَّا بِعَهْدِ نَعَاهِدُونَنِي عَلَيْهِ»

"Wallah! Hamtasalimika isipokuwa mpaka muweke upya mkataba wa amani pamoja nami."

Walikataa kufanya hivyo, na Mtume ﷺ akawapiga katika siku nzima iliyofuatia. Asubuhi iliyofuatia, Mtume ﷺ aliliwekea kizuizi kabila la Bani Quraydhwah na kuliacha kabila la Bani An-Nadhir pekee yao kwa siku nzima. Mtume ﷺ aliwaamuru Bani Quraydhwah wasaini mkataba mpya wa amani, na wakakubali. Mtume ﷺ akawaacha Bani Quraydhwah na kurejea kwa Bani An-Nadhir pamoja na majeshi yake na akawapiga mpaka wakakubali kujisalimisha kwa lengo la kuruhusiwa kupata njia salama ya kundoka Al-Madinah. Bani An-Nadhir wakaondoka Al-Madinah na wakachukua kila kilichoweza kubebwa na ngamia wao na wakachukua samani zao, ikiwemo miti na milango ya nyumba zao. Allah تعالى Alimpa Mtume ﷺ mitende ya Bani An-Nadhir, aliposema,

وَمَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ مِنْهُمْ فَمَا أَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ

“Na mali Aliyoleta Mwenyezi Mungu kwa Mtume Wake kutoka kwao hamkuikimbilia mbio kwa farasi wala ngamia.”

Maana: “Mlichopata bila ya kupigana. Mtume ﷺ aliigawa mali hiyo kuwapa Muhajirin na aliwapa watu wawili tu katika Al-Ansar waliokuwa maskini. Hakuwapa Ansar chochote katika mitende hiyo, isipokuwa watu hao wawili. Mtume ﷺ aliendelea kugawa sehemu ya ngawira kwa ajili yake mwenyewe na ikabaki kuwa sehemu ya sadaka ya Mtume ﷺ iliyohamishwa kwenda kuwakirimu watoto wa binti yake, yaani, watoto wa Fatimah.”¹ Hata hivyo, hebu hapa tueleze vita vya Bani An-Nadhir kwa muhtasari. Tunamuomba Allah تعالى Pekee Atusaidie.

Sababu za Vita vya Bani An-Nadhir

Baada ya kuuawa Masahaba sabini رضي الله عنهم ambao Mtume ﷺ aliwatuma kwenda kufundisha Qur’an katika eneo la Bi’r Ma’unah, isipokuwa ‘Amr bin Umayyah Ad-Damri, ambaye aliua watu wawili wa kabila la Bani ‘Amir akiwa njiani kurejea Al-Madinah. Hakujuu kuwa watu hao wawili walikuwa na mkataba wa amani kutoka kwa Mtume ﷺ. Alipofika Al-Madinah, alimueleza Mtume ﷺ yaliyotokea na Mtume ﷺ akamuambia,

«لَقَدْ قَتَلْتَ رَجُلَيْنِ لِأَدِيَّتِهِمَا»

“Umeua watu wawili, nitalipa fidia yao.”

¹ Abu Dawud 3:404.

Bani An-Nadhir na Bani 'Amir walikuwa washirika na walikuwa na mikataba. Mtume ﷺ aliwaomba Bani An-Nadhir wasaidie kulipa fidia ya watu hao wawili waliouliwa. Eneo la Bani An-Nadhir lilikuwa katika viunga vya Al-Madinah, masafa machache kwa upande wa mashariki.¹

Katika kitabu chake cha Sirah, Muhammad bin Ishaq bin Yasar alisema; "Kisha Mtume ﷺ akawaenda Bani An-Nadhir kuwaomba msaada wa kifedha ili kulipa fidia ya watu wawili wa Bani 'Amir, waliouliwa na 'Amr bin Umayyah Ad-Damri. Walikuwa na ahadi ya kupata amani kutoka kwa Mtume ﷺ kwa mujibu wa (msimulizi wa kati) Yazid bin Ruman. Bani An-Nadhir na Bani 'Amir walikuwa na mkataba wa amani. Mtume ﷺ alipowaenda Bani An-Nadhir ili kuwaomba msaada wa kulipa fidia ya watu wawili hao, wakasema, 'Ndiyo, Ewe Abu Al-Qasim! Tutakusaida kwa kuwa umetuomba msaada.' Lakini wakakutana wao wenyewe kisiri, wakaambizana, 'Hamtapata fursa bora kwa mtu huyu kuliko hii." Mtume ﷺ alipokuwa amekaa jirani na ukuta wa nyumba yao mojawapo. Walisema, 'Nani atakayekwea juu ya ukuta huu na kumuangushia jiwe mtu huyu na tuondokane na taabu zake.' 'Amr bin Jihash bin Ka'b alijitolea na kukwea juu ya ukuta wa nyumba hiyo ili kumuangushia jiwe Mtume. Mtume ﷺ alikuwa ameketi pamoja na Masahaba wake رضي الله عنهم, kama vile Abubakr, 'Umar na 'Ali رضي الله عنهم. Habari za njama hizo zilimfikia Mtume ﷺ kutoka mbinguni, na akasimama na kurejea Al-Madina. Masahaba walipoona kuwa Mtume ﷺ hakuonekana kwa muda mrefu, walikwenda kuangalia mahali alipokuwepo na wakamuona mtu akitokea Al-Madina. Wakamuuliza, na akawajibu kuwa alimuona Mtume ﷺ akiingia Al-Madina. Masahaba wa Mtume ﷺ wakamuenda, na akawaeleza habari za njama za usaliti waliopanga Wayahudi dhidi yake. Akawaamrisha wajitayarisha kwa ajili ya vita na kuwaenda Bani An-Nadhir. Mtume ﷺ alikusanya majeshi yake na kwenda mpaka katika eneo la Bani An-Nadhir, waliokuwa wamejificha katika ngome zao. Mtume ﷺ akaamuru mitende yao ikatwe na kuchomwa moto. Wayahudi wakapaza sauti kwa Mtume ﷺ, 'Ewe Muhammad! Ulikuwa ukikataza uovu duniani na kuwashutumu walioutenda. Kwa nini umeamuru mitende ikatwe na kuchomwa moto?' Wakati huo huo, kundi moja la Banu Awf bin Khazraj akiwemo 'Abdullah bin Ubayy bin Salul, Wadi'ah, Malik bin Abi Qawqal,

¹ *Ad-Durar fi Ikhtisar Al-Maghazi was-Siyar* 180, 181 na Ibn Hisham 3:195. Masimulizi hayo ni *Mursal*.

Suwayd, Daisi na watu wengine walituma ujumbe kwa Bani An-Nadhir kwa kusema, 'Kuweni imara na wenye nguvu. Kamwe hatutakuacheni. Kama mtapigana, tutapigana katika upande wenu na ikiwa mtalazimishwa kuondoka Al-Madinah, tutafuatana nanyi.' Wayahudi wakasubiri msaada huo, lakini wanafiki hawakutimiza. Allah تعالی Alitia hofu katika nyoyo za Wayahudi. Wakamuomba Mtume ﷺ kuwaruhusu kuondoka salama Al-Madinah na asiwaue. Kwa upande wao, waliruhusiwa kuchukua kile ambacho ngamia wao waliweza kuchukua, isipokuwa silaha. Mtume ﷺ alikubali.

Wayahudi walikusanya mali zao zote ambazo ngamia wao walimudu kuzibeba. Wayahudi walikuwa wakivunja nyumba zao na kuibeba milango kwa kutumia ngamia wao. Bani An-Nadhir walihamia Khaybar, na baadhi yao walikwenda Ash-Sham. Vyote walivyoviacha vikawa vya Mtume ﷺ, ambaye alivigawa. Mtume ﷺ aliwagawia *Muhajirin* na hakuna *Al-Ansar* waliopata mgao huo, isipokuwa Sahl bin Hunayf na Abu Dujanah Simaki bin Kharashah. Walisema kuwa walikuwa maskini na Mtume ﷺ aliwapa fungu lao. Watu wawili tu katika Bani An-Nadhir walisilimu, Yamin bin Umayr bin Ka'b bin 'Amr bin Jihash na Abu Sa'id d bin Wahb na waliokoa mali zao kwa sababu ya kusilimu kwao." Ibn Ishaq رحمه الله تعالی aliendelea kusema, "Baadhi ya watoto wa Yamin walinisimulia kuwa Mtume ﷺ alimuambia Yamin,

«أَلَمْ تَرَ مَا لَقِيتُ مِنْ ابْنِ عَمِّكَ وَمَا هَمَّ بِهِ مِنْ شَأْنِي؟»

"Je, hujasikia njama alizozipanga binamu yako dhidi yangu?"

Yamin bin 'Umayr aliahidi zawadi kwa mtu iwapo atamuua binamu yake 'Amr bin Jihash, hivyo basi mtu huyo akamuua, kulingana na ahadi yake."¹ Ibn Ishaq رحمه الله تعالی akasema, "Sura yote ya *Al-Hashr* ilishuka kuhusu Bani An-Nadhir." Habari sawa na hiyo ilinukuliwa na Yunus bin Bukayr kutoka kwa Ibn Ishaq رحمه الله تعالی.² Kauli ya Allah تعالی,

هُوَ الَّذِي أَخْرَجَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ

"Yeye Ndiye Aliyewatoa waliokufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu..."

Inarejea kwa Bani An-Nadhir,

¹ Isnadi hii si sahihi.

² Ibn Hisham 3:199-202.

مِن دِينِهِمْ لِأَوَّلِ الْحَشْرِ^٥

“...katika nyumba zao wakati wa uhamisho wa kwanza.”

Kauli ya Allah تعالى،

مَا ظَنَنْتُمْ أَنْ نَخْرُجُوهَا^٥

“Hamkudhani kuwa watatoka...” Maana yake: Katika siku chache uliwawekea kizuizi. Masahaba walizingira ngome zao kwa siku sita tu, na ngome zao zilikuwa imara. Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

وَلَقَدْ ظَنَنَّا أَنَّهَمْ مَا نَعْتَهُمْ حُصُوبُهُمْ مِّنَ اللَّهِ فَآتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا^٥

“...nao walidhani kuwa ngome zao zitawalinda na Mwenyezi Mungu. Lakini Mwenyezi Mungu Aliwafikia kwa mahali wasipopatazamia.”

Inamaanisha, liliwafikia kutoka kwa Allah تعالى jambo ambalo hawakulitarajia. Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine,

قَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَأَتَى اللَّهُ بُنْيَانَهُمْ مِنَ الْقَوَاعِدِ فَخَرَّ عَلَيْهِمُ السَّقْفُ
مِنْ فَوْقِهِمْ وَأَتَنَّهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٦﴾

“Walipanga vitimbi waliokuwa kabla yao, Mwenyezi Mungu Akayasukua majengo yao kwenye misingi, dari zikawaporomokea juu yao, na adhabu ikawajia kutoka wasipokujua.” (16:26)

Kauli ya Allah تعالى،

وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ^٥

“...na Akatia woga katika nyoyo zao.”

Inamaanisha Allah تعالى Aliwatia hofu, kitisho na woga katika nyoyo zao, na kwa nini yasiwatokee hayo wamezingirwa na Mtume ﷺ aliyepewa ushindi kwa njia ya Allah تعالى kuwatia hofu maadui zake katika umbali wa mwezi mmoja. Kuna maelezo ya Ibn Ishaq رحمه الله تعالى – yaliyotangulia kuelezwa kuhusu jambo hilo;

تُخْرِبُونَ بُيُوتَهُمْ بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ

“Wakawa wanazibomoa nyumba zao kwa mikono yao na mikono ya Waumini.”

Wayahudi walishusha vitu walivyotaka kuvisafirisha katika mapaa na milango yao, ili wavibebe juu ya ngamia wao. Maelezo sawa na hayo yalisemwa na 'Urwah bin az-Zubayr, 'Abdur-Rahman bin Zayd bin aslam na wengine kadhaa رضي الله عنهم¹. Kauli ya Allah تعالى،

وَلَوْلَا أَنْ كَتَبَ اللَّهُ عَلَيْهِمُ الْجَلَاءَ لَعَذَّبْتَهُمْ فِي الدُّنْيَا

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Asingeliwaandikia kutoka, Angeliwaadhibu katika dunia.”

Maana yake: Kama isingekuwa kutokana na ukweli kuwa Allah تعالى tayari Alishajaalia kuwa waondoke Al-Madinah, na kuyaacha makazi yao na mali yao, Angetaka, Angewapelekea aina nyingine ya adhabu, kama vile kuuawa na kukamatwa mateka. Hayo yalisemwa na Az-Zuhri. 'Urwah, As-Suddi na Ibn Zayd amesema kuwa Allah تعالى Alishajaalia kuwa Wayahudi waadhibiwe humu duniani na kupata adhabu ya moto wa Jahanamu Aliowaandalia huko Akhera.² Kauli ya Allah تعالى:

وَهُمْ فِي الآخِرَةِ عَذَابُ النَّارِ

“Na katika Akhera watapata adhabu ya Moto.”

Inamaanisha, ni jambo la majaaliwa kuwa lingewafikia kwa hakika.

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“Hayo ni kwa sababu walimpinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.”

Inamaanisha Allah تعالى Alishatayarisha adhabu hii mahsusi na Alimtuma Mjumbe Wake na Masahaba Wake رضي الله عنهم dhidi yao, kwa sababu walimkadhibisha Allah تعالى na Mjumbe Wake na walikataa habari njema. Alizotanguliza Allah تعالى katika vitabu vya Mitume waliotangulia kuhusu ujio wa Muhammad ﷺ. Wayahudi walijua habari hizo za hakika kuhusu Muhammad ﷺ kama walivyowajua watoto wao wenyewe. Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ يُشَاقِقِ اللَّهَ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

“Na mwenye kumpinga Mwenyezi Mungu, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu.”

¹ Al-Qurtubi 18:4.

² Ar-Razi 29:245.

Mitende ya Wayahudi Ilikatwa kwa Idhini ya Allah تعالی

Kauli ya Allah تعالی,

مَا قَطَعْتُمْ مِنْ لَيْنَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوهَا قَائِمَةً عَلَىٰ أُصُولِهَا فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيُخْزِيَ

الْفٰسِقِينَ ﴿٥٩﴾

“Mtende wowote mlioukata au mliouacha unasimama vile vile juu ya mashina yake, basi ni kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu, na kwa kuwahizi wapotovu.”

Linah ni aina mahsusi ya mitende mizuri. Abu ‘Ubaydah amesema kuwa *Linah* ni namna tofauti ya tende isiyokuwa ‘*Ajwah* na *Barni*.¹

Wengine kadhaa wamesema kuwa *neni Linah* linakusudia kila aina ya tende, isipokuwa ‘*Ajwah* (tende mbivu), ilhali Ibn Jarir رحمه الله تعالی amesema kuwa inakusudia kila aina ya mitende.² Ibn Jarir رحمه الله تعالی alimnukuu Mujahid kwa kusema kuwa pia inajumuisha aina ya *Buwayrah*. Mtume ﷺ alipowawekea kizuizi Bani An-Nadhir, ili kuwafedhehesha na kutia hofu nyoyoni mwao, aliamuru mitende yao ikatwe. Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالی amesimulia kuwa Yazid bin Ruman, Qatadah na Muqatil bin Hayyan wamesema, “Bani An-Nadhir walituma ujumbe kwa Mtume ﷺ, kwa kusema kuwa Muhammad ﷺ alikuwa akitenda uovu katika dunia, kwa sababu aliamrisha mitende ikatwe. Allah تعالی Akateremsha Aya hiyo tukufu ikieleza kuwa *Linah* yoyote iliyoangushwa au kuachwa na Waislamu, ni kwa Ruhusa Yake, Utashi, Idhini na ili Kuwafedhehesha, Kuwadhalilisha maadui na Kuwashusha.”³

Mujahid amesema, “Baadhi ya Muhajirin waliwakataza wengine kukata miti ya Wayahudi, kwa kusema kuwa zilikuwa ngawira kwa ajili ya Waislamu. Qur’an iliwasadikisha waliokataza na kuwatoa makosani waliokata miti hiyo, kwa kueleza kuwa walioikata na wasioikata, walifanya hayo kwa Idhini ya Allah تعالی.” Pia kuna Hadithi iliyosimuliwa kutoka kwa Mtume ﷺ ikiwa na maana

¹ Ar-Razi 29:246.

² At-Tabari 23:268.

³ At-Tabari 23:271.

hiyo hiyo.¹ An-Nasa'i amenukuu kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما amesema kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

مَا قَطَعْتُمْ مِنْ لَيْمَةٍ أَوْ نَزَعْتُمْهَا فَأَيْمَةٌ عَلَىٰ أَصُولِهَا فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيُخْزِيَ الْفَاسِقِينَ ﴿٥٩﴾

“Mtende wowote mlioukata au mliouacha unasimama vile vile juu ya mashina yake, basi ni kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu, na kwa kuwahizi wapotovu.”

“Waliwashurutisha washuke chini kutoka katika ngome zao na wakaamrisha kuikata miti yao. Waislamu wakasita, na baadhi yao wakasema, ‘Tutaikata baadhi na kuiacha mingine. Lazima tumuulize Mtume ﷺ kama tutapata malipo kama tutaikata na kama tutapata madhambi kwa kuiacha.’ Allah تعالى Akateremsha Aya hii,

مَا قَطَعْتُمْ مِنْ لَيْمَةٍ أَوْ نَزَعْتُمْهَا فَأَيْمَةٌ عَلَىٰ أَصُولِهَا فَبِإِذْنِ اللَّهِ

“Mtende wowote mlioukata au mliouacha unasimama vile vile juu ya mashina yake, basi ni kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu.”²

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما amesema kuwa Mtume ﷺ aliamrisha kuwa mitende ya Bani An-Nadhir ikatwe na kuchomwa moto.³ Sahihi Mbili zilikusanya masimulizi sawa na hayo.⁴

Al-Bukhari amenukuu kutoka kwa 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنه kuwa, “Bani An-Nadhir na Bani Quraydhah walipigana (dhidi ya Mtume ﷺ), na Mtume ﷺ akawafukuza Bani An-Nadhir na kuwaruhusu Bani Quraydhah wabakie katika eneo lao mpaka baadaye, Mtume ﷺ alipopigana dhidi ya Quraydhah. Wanaume wao waliuliwa, wanawake na watoto wao kutekwa na mali zao zilitaifishwa na kugawiwa Waislamu. Baadhi yao, hata hivyo, walinusurika kwa sababu walirejea upande wa Mtume ﷺ, naye akawapa hifadhi, na wakashilimu. Wayahudi wote wa Al-Madinah, Bani Qaynuqa', kabila la 'Abdullah bin Salam, Bani Harithah na makabila mengine ya Kiyahudi walifukuzwa Al-Madinah.”⁵

¹ At-Tabari 23:271.

² An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:485. Masimulizi kama hayo yaliandikwa na At-Tirmidhi chini ya *Tafsir* ya Aya hii.

³ Ahmad 2:7.

⁴ Muslim 3:1365.

⁵ *Fat'h Al-Bari* 7:383.

Sahihi Mbili pia zimenukuu kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ aliichoma moto mitende ya Bani An-Nadhir na kuamuru kukatwa mitende ya Al-Buwayrah.

Allah تعالى Alishusha Aya hii,

مَا قَطَعْتُمْ مِّن لِّبْتَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوهَا قَائِمَةً عَلَىٰ أُصُولِهَا فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيُخْرِىَ الْفٰسِقِينَ ﴿٥٩﴾

“Mtende wowote mlioukata au mliouacha unasimama vile vile juu ya mashina yake, basi ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na kwa kuwahizi wapotovu.”¹

Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى amesimulia kuwa vita vya Bani An-Nadhir vilitokea baada ya vita vya Uhud na Bi'r Ma'unah.

* * *

¹ Fat'h Al-Bari 7:383, Muslim 3:1365.

na mayatima, na masikini, na msafiri, ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu. Na Anachokupeni Mtume chukueni, na Anachokukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu.

Matumizi ya Mali Iliyopatikana bila ya Vita - Fai'

Allah تعالی Anaeleza taratibu za *Fai'*, ngawira wanazopata Waislamu kutoka kwa makafiri, bila ya kupigana au kutuma kikosi cha farasi na kikosi cha ngamia katika vita dhidi yao. Mathalani, ngawira zilizokusanywa kutoka kwa Bani An-Nadhir hazikupatikana kwa sababu ya kuwapiga kwa kutuma farasi na ngamia. Waislamu hawakuwapiga Bani An-Nadhir katika vita, bali Allah تعالی Aliwalizimisha watoke nje ya ngome zao, kutokana na hofu Aliyotia nyoyoni mwao kumuogopa Mtume ﷺ. Kwa hiyo, iikuwa *Fai'* ambayo Allah تعالی Alimzawadia Mjumbe Wake, na kwa kuzingatia hilo, alitumia mali hiyo kwa namna ya kufaa. Katika njia njema na kwa ajili ya manufaa ya Waislamu, katika maeneo Aliyotaja Allah تعالی katika Aya hii,

وَمَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْهُمْ

“Na mali Aliyoleta Mwenyezi Mungu kwa Mtume Wake kutoka kwao...”

Inamaanisha, kutoka kwa Bani An-Nadhir,

فَمَا أُوجِفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ

“...hamkuikimbilia mbio kwa farasi wala ngamia.”

Maana yake kutuma ngamia,

وَلَيْكِنَ اللَّهُ يُسَلِّطُ رَسُولَهُ عَلَى مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Lakini Mwenyezi Mungu Huwapa mamlaka Mitume Wake juu ya wowote awatakao. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.”

Inamaanisha, Allah تعالى ni Muweza wa Yote na Hapingwi wala kuzuiwa; Yeye ni Mwenye Kulazimisha juu ya vitu vyote. Allah تعالى Amesema,

مَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ

“...Mali aliyoleta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa hivi vijiji...”

Maana yake: Kutoka katika vijiji na maeneo yaliyokombolewa kwa namna hii. Ngawira zilizokusanywa kutoka kwao zinaangukia katika hukumu hiyo ya ngawira zilizopatikana kutoka kwa Bani An-Nadhir. Ndipo Allah تعالى Amesema,

فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ

“...na kwa ajili ya Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na msafiri...”

Mpaka mwisho wake na Ayah inayofuatia. Hizi ndizo namna za kutumia mali ya *Fai*. Imamu Ahmad amenukuu kuwa ‘Umar رضي الله عنه amesema, “Mali ya Bani An-Nadhir ilikuwa aina ya *Fai*’ ambayo Allah تعالى Alimzawadia Mjumbe Wake ﷺ na ambayo Waislamu hawakutumia kikosi cha farasi au ngamia. Kwa hiyo, ilikuwa mahsusu kwa Mtume ﷺ, na aliitumia kwa ajili ya haja za familia yake kwa mwaka, na iliyosalia ilikuwa ikinunulia deraya na silaha zilizotumika katika njia ya Allah تعالى.”¹ Ahmad alikusanya muhtasari wa habari hiyo. Kundi, isipokuwa Ibn Majah, waliikusanya Hadithi hii.²

Abu Dawud amenukuu kuwa Malik bin ‘Aws amesema, “Nilipokuwa nyumbani, jua lilipanda juu na kuleta joto kali. Ghafila Mjumbe wa ‘Umar bin al-Khattab رضي الله عنه alikuja na nikatoka naye na kwenda mahali alipokuwepo ‘Umar رضي الله عنه akiwa amekalia tendegu la kitanda lilotengenezwa kutokana na matawi ya mtende na bila ya godoro. Akaniambia nilipoingia ndani, ‘Ewe Malik! Baadhi ya watu wa familia yako walinijia kwa sababu ya njaa yao, na niimetoa amri kuwa wapewe msaada, basi chukua ukawagawie.’ Nikasema, ‘Natamani kuwa ungemuamuru mwingine kufanya hilo.’ Akasema, ‘Chukua.’ Kisha Yarfa

¹ Ahmad 1:25.

² *Fat’h Al-Bari* 8:498, *Muslim* 3:1376, *Abu Dawud* 3:371, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 5:381, na *An-Nasai* 7:132.

(mtumishi wa 'Umar رضي الله عنه) akaja na kusema, 'Ewe Amiri wa waumini! Niwaruhusu 'Uthman bin 'Affan, 'Abdur-Rahman bin 'Awf, Az-Zubayr bin al-'Awwam na Sa'id bin Abi Waqqas waingie?' 'Umar رضي الله عنه akasema, 'Ndiyo, ' na wakaingia.

Baada ya kitambo kidogo, Yarfa alikuja tena na kusema, 'Ewe Amiri wa waumini! Nimruhusu Al-'Abbas na 'Ali 'Umar?' Akasema, 'Ndiyo.' Kwa hivyo, waliruhusiwa kungia na Al-'Abbas رضي الله عنه akasema, 'Ewe Amiri wa waumini! Hukumu baina yangu na huyu (yaani, 'Ali).' Kundi (la 'Uthman na wenzake) wakasema, 'Ewe Amiri wa waumini! Hukumu baina yao na uwapumzishe.' Mimi (Malik bin aws) nilidhani kuwa wangetangulia kuwauliza watu hao wanne waje kabla yao kwa ajili ya jambo hilo. 'Umar رضي الله عنه akasema, 'Subirini!' Akauliza kundi ('Uthman na wenzake), 'Ninakuulizeni kwa Allah تعالى Ambaye Idhini Yake imekuwepo mbingu na ardhi, mnajua kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا نُورُثُ، مَا تَرَكَتْنَا صَدَقَةً»

"(Mitume) haturithiwi, na tunachokiacha ni sadaka."

Kundi likajibu, 'Alisema hivyo.' 'Umar رضي الله عنه akamgeukia 'Ali رضي الله عنه na Al-'Abbas رضي الله عنه kuwaambia, 'Ninakuombeni kwa Jina la Allah تعالى Ambaye kwa Idhini Yake, zimekuwepo mbingu na ardhi, nyote wawili mnajua Mtume ﷺ alisema,

«لَا نُورُثُ، مَا تَرَكَتْنَا صَدَقَةً»

"(Mitume) haturithiwi, na chochote tunachokiacha ni sadaka."

Wakajibu, 'Alisema hivyo.' 'Umar رضي الله عنه akasema, 'Allah تعالى Alimpa Mjumbe Wake ﷺ upendeleo maalumu tofauti na Alichowapa watu wote wengine. Allah تعالى Amesema,

وَمَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْهُمْ فَمَا أَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ وَلَكِنَّ اللَّهَ يُسَلِّطُ

رُسُلَهُ عَلَى مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٦﴾

"Na mali Aliyoleta Mwenyezi Mungu kwa Mtume Wake kutoka kwao hamkuikimbilia mbio kwa farasi wala ngamia. Lakini Mwenyezi Mungu Huwapa mamlaka Mitume Wake juu ya wowote awatakao. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu."

Hivyo, mali hii, ngawira aliyokusanya kutoka kwa Bani An-Nadhir, ilikuwa mahsusi kwa ajili ya Mtume ﷺ. Hata hivyo, Wallah! Hakuichukua yote peke yake na kukuacheni, wala hakujipendelea na kukuacheni nyinyi. Mtume ﷺ alichukua matumizi ya kila mwaka kutokana nayo kwa ajili yake na familia yake na iliyobakia aliacha katika Hazina ya Waislamu.' Akaliuliza kundi, 'Ninakuulizeni kwa Jina la Allah تعالی ambaye kwa idhini Yake, zipo mbingu na ardhi, mnalijua hilo?' Walijibu, 'Ndiyo.' 'Umar رضي الله عنه akamuambia 'Ali na Al-'Abbas رضي الله عنهما, 'Ninakuulizeni kwa Jina la Allah تعالی Ambaye kwa Idhini Yake, zipo mbingu na ardhi, mnalijua hilo?' Walijibu, 'Ndiyo.' 'Umar رضي الله عنه akaongeza, 'Allah تعالی Alipomchukua Mtume ﷺ Kwake, Abubakr رضي الله عنه alisema: Mimi ni msimamizi wa Mtume ﷺ, halafu mkamuendea Abubakr رضي الله عنه kumuuliza mirathi ya binamu yako (Al-'Abbas'), na wewe (Ali) kumuuliza mirathi ya mkeo kutoka kwa baba yake.'" Abubakar رضي الله عنه akasema: Mtume ﷺ amesema,

«لَا نُورَثُ، مَا تَرَكْنَا صَدَقَةً»

"(Mtume) haturithiwi, na chochote tunachokiacha ni sadaka."

Allah تعالی Anajua kuwa Abubakr رضي الله عنه alikuwa mkweli, mchamungu, mwongofu na mwenye kufuata haki. Kwa hivyo, Abubakr رضي الله عنه alisimamia majukumu ya mali hiyo. Abubakr رضي الله عنه alipofariki, nilisema: Mimi ni msimamizi wa Mtume ﷺ, kwa hivyo, nikaisimamia kadiri ya alivyoniijaalia Allah تعالی. Halafu nyinyi ('Ali na Al-'Abbas) mkaja kuzungumza nami, mkiwa na madai yale yale na mkanifikishia, kuniomba mali hiyo. Nikakuambieni: Niko tayari kukukabidhini mali hiyo mkitaka. Nitafanya hivyo kwa sharti kuwa mtaweka ahadi kwa Allah تعالی kuwa mtaisimamia kama vilevile alivyofanya Mtume ﷺ. Nyote wawili mkakubali na kwa sharti nililokupeni. Sasa mnakuja kwangu kuleta hukumu tofauti juu ya mali hiyo. Wallahi, sitatoa uamuzi tofauti na ule niliokupeni, mpaka Saa ya Mwisho isimame. Kama hamuezi kuisimamia, basi irejesheni kwangu, na nitafanya kazi hiyo kwa niaba yenu."¹ Waliyanukuu maneno haya kutokana na Hadithi ya Az-Zuhri.² Kauli ya Allah تعالی,

كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ^٤

"...ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu."

¹ Abu Dawud 3:365.

² Fat'h Al-Bari 13:290, Muslim 3:1377, Tuhfat Al-Ahwadhi 5:33 na An-Nasai.

Yaani: 'Tulifanya matumizi ya *Fai'* kama hivyo, ili mali hiyo isibakie kwa matajiri, ambao wangeitumia kulingana na matakwa yao na kuwanyima maskini.'

Amri ya Kumtii Mtume ﷺ kwa Kila Alichomrisha na Alichokatiza

Allah تعالى Amesema,

وَمَا آتَاكُمْ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا

***“Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni
jiejpusheni nacho.”***

Yaani: 'Chochote anachokuamrisheni Mtume ﷺ, kifanyeni na anachokukatazeni kiacheni. Hakika, huwa anaamrisha mema tu na kukataza uovu.'

Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه amesema, "Allah تعالى Anawalaani wanawake wenye kujiweka chale na wenye kuwekewa chale, na wanawake wenye kuondoa nyusi na nywele za usoni na wenye kuweka mwanya bandia baina ya meno yao ili waonekane wazuri zaidi, kwa kubadili umbo Aliloumba Allah تعالى." Kauli yake ilimfikia mwanamke katika Bani Asad aliyelitwa Umm Ya`qub رضي الله عنها, aliyekuja kwa 'Abdallah na kumuambia, "Nimepata habari kuwa umesema kadha wa kadha." Akamjibu, "Kwa nini nisimlaani mtu aliyelaaniwa na Mtume ﷺ na amelaaniwa katika Kitabu cha Allah تعالى!" Umm Ya`qub رضي الله عنها akasema, "Nimesoma Qur'an yote, lakini sikukuta humo hicho unachokisema." Akasema, "Kwa hakika, kama umesoma Qur'an, utakuwa umekuta mahali kunaposomeka hivi,

وَمَا آتَاكُمْ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا

***“Na anachokupeni Mtume chukueni, na anachokukatazeni
jiejpusheni nacho.”***

'Akamjibu, "Ndiyo, nimepakuta." Amesema, "Kwa hakika, Mjumbe wa Allah ﷺ amekataza mambo hayo." Akasema, "Lakini nadhani kuwa mkeo huwa anafanya mambo hayo." Akamuambia, "Nenda kamuangalie." Alikwenda kumuangalia, lakini hakuona chochote katika madai yake. Akarejea kwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه na kumuambia kuwa hakuona chochote kwa mkewe. Akasema, "Kama angekuwa kama ulivyodhania nisingekuwa naye."¹

¹ Ahmad 1:433.

Sahihi Mbili zimeinukuu kutokana na Hadithi ya Sufyan Ath-Thawri ¹رحمة الله تعالى. Pia kama Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه, ambaye alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا أَمَرْتُكُمْ بِأَمْرٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ، وَمَا نَهَيْتُكُمْ عَنْهُ فَاجْتَنِبُوهُ»

“Ninapokuamrishi ni jambo, lifanyeni kadiri ya mnavyoweza. Nikikutazeni, liacheni.”²

Kauli ya Allah تعالى،

وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu.”

Inamaanisha Kumuogopa Allah تعالى kwa kutii Amri Zake na kuacha Makatazo Yake. Kwa hakika, Allah تعالى ni Mkali wa Kuwaadhibu wenye Kumkadhibisha na wenye kuasi Amri Zake pia, na wenye kufanya Aiyoyakemea na Kuyakataza.

لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ ﴿٥﴾ وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٦﴾ وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٧﴾

8. Wapewe mafakiri Wahajiri waliotolewa majumbani mwao na mali yao kwa ajili ya kutafuta Fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Radhi Zake, na wanainusuru Dini ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hao ndio wa kweli.

9. Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda waliohamia kwao, wala hawaoni chuki katika vifua vyao kwa walivyopewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa na ubakhili mkubwa wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa.

¹ Fat'h Al-Bari 8:498, Muslim 3:1678.

² Fat'h Al-Bari 8:498, Muslim 2:975.

10. Na waliokuja baada yao wanasema: Mola Wetu Mlezi! Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani, wala Usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walioamini. Mola Wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole mno na Mwingi wa Mwenye Kurehemu.

Ubainifu wa Watu wanaostahiki Mali ya “Fai”; na ndani Yake Kuna Fadhila za Muhajirin na Al-Ansar

Allah تعالی Anaeleza makundi ya mafakiri na wenye kustahiki mali ya Fai’,

الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا

“...waliotolewa majumbani mwao na mali yao kwa ajili ya kutafuta Fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Radhi Zake.”

Wameacha nyumba zao na wakawahalifu watu wao ili kutafuta Radhi za Allah

تعالى،

وَيَنْصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

“...na wanamsaidia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hao ndio wa kweli.”

Inamaanisha, ‘Hao ni waliokuwa na ukweli kwa kauli na amali, na wao ndio watukufu wa Muhajirin.’ Allah تعالی baada ya hapo Aliwasifu Ansar kwa Kueleza ubora wao, daraja na utukufu wao juu ya wengine, ingawa walikuwa katika haja, na kutokuwa na husuda. Allah تعالی Amesema,

وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao.”

Inakusudia waliokuwa wakazi wa mji uliohamiwa, kabla ya kufika Muhajirin, na walioamini kabla ya Muhajirin wengi. ‘Umar رضي الله عنه alisema, “Ninapendekeza Khalifah wa baada yangu, ajue haki na ubora wa Muhajirin na kutunza heshima yao. Pia ninampendekeza awe mwema kwa Ansar, walioishi katika mji wa Hijrah na wakaamini kwanza, akubali mema yao na awasamehe wenye kukosea miongoni mwao.” Al-Bukhari aliiikusanya Hadithi hii.¹

¹ Fath Al-Bari 8:499, masimulizi sawa na hayo yameandikwa na Tirmidhi na. 2487.

Kauli ya Allah تعالى،

تُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ

“...wanawapenda walio hamia kwao,”

Inaashiria kuwa wao, kutokana na ukarimu wao na tabia yao tukufu, waliwapenda muhajirina na waliwaliwaza kwa mali zao.

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Anas رضي الله عنه amesema, “*Muhajirin* walisema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Hatujapata kukutana na watu kama hawa tuliohamia kwao; wanatuliwaza katika nyakati za uhaba na wanatupa moyo katika nyakati za ukunjufu. Wametupa vingi na wamegawana nasi mali zao nyingi kiasi ambacho, tunahofia kuwa wanaweza kupata malipo yote badala ya sisi.’ Akawaambia,

﴿لَا، مَا أَتَيْتُمْ عَلَيْهِمْ وَدَعَوْتُمْ اللَّهَ لَهُمْ﴾

“Hapana, madam mnawasifu kwa waliyoyafanya na mnawaombea kwa Allah.”¹

Sikuiona katika vitabu, kwa njia hiyo. Al-Bukhari amenukuu kuwa Yahya bin Sa’id alimsikia Anas bin Malik رضي الله عنه, alipofuatana naye kwenda kwa Al-Walid, akamuambia, “Mtume ﷺ aliwaita Ansar ili awagawie Al-Bahrayn. Ansar wakasema, ‘Hapana, mpaka uwape ndugu zetu Muhajrin fungu kama hilo.’ Akasema,

﴿إِنَّمَا لَا، فَاصْبِرُوا حَتَّى تُلْفَوْنِي، فَإِنَّهُ سَيُصِيبُكُمْ بَعْدِي أُنْرَةٌ﴾

“Labda, hapana; lakini hivi karibuni mtawaona watu wakiwatanguliza wengine, kwa hivyo subirini mpaka mtakapokutana nami (katika Siku ya Kiama).”²

Al-Bukhari alikuwa pekee yake katika toleo hilo. Pia amenukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, “*Ansar* walisema (kumuambia Mtume ﷺ, ‘Tugawie mitende yetu baina yetu na ndugu zetu *Muhajirin*.’ Akawajibu, ‘Hapana.’ *Ansar* wakasema (kuwaambia *Muhajirin*), ‘Angalieni tende katika miti na mgawane nasi.’ *Muhajirin* wakasema, ‘Tumesikia na tumetii.’”³ Al-Bukhari peke yake aliinukuu, Muslim hakuinukuu.

¹ Ahmad 3:200.

² *Fat’h Al-Bari* 7:146.

³ *Fat’h Al-Bari* 5:11.

Ansar Hawakuwafanyia Husda Muhajirin

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِّمَّا أُوتُوا

“...wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyopewa...”

Inamaanisha, Ansar hawakuwafanyia husda Muhajirin kwasababu ya daraja bora zaidi, hadhi au utukufu waliopewa na Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى،

مِمَّا أُوتُوا

“...walivyopewa...” Maana yake: Walichoneemeshwa Muhajirin, kwa mujibu wa Qatadah na Ibn Zayd.

Ukarimu wa Ansar

Kauli ya Allah تعالى،

وَيُؤْتُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ

“...bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji.”

Inamaanisha, walipendelea kuwapa maskini badala ya kukidhi haja zao wenyewe, na wakawa wanawapa watu kabla yao wenyewe, ingawa wao pia walikuwa na haja. Hadithi sahihi inasema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«أَفْضَلُ الصَّدَقَةِ جُهْدُ الْمُفِئِلِ»

“Sadaka bora ni ya mwenye tabu, mwenye kichache.”¹

Na Daraja hii ni tukufu kuliko daraja ya wale Aliowaeleza Allah تعالى katika Kauli Zake،

وَيُطْعَمُونَ الطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٨﴾

“Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa.” (76:8), na,

وَأَتَىٰ الْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِ

“Na anawapa mali, kwa kupenda kwake.” (2:177)

¹ Abu Dawud 2:146.

Hao wanatoa sadaka ingawa wanaipenda mali wanayotoa, na huenda wasiwe na haja nayo wala kuwa na dharura nayo. Wanawapendelea wengine zaidi kuliko wao, ingawa wao wana haja na wana ulazima katika walichokitoa sadaka. Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه alitoa sadaka ya mali yake yote na Mtume ﷺ akamuuliza,

«مَا أَتَيْتَ لِأَمْلِكَ؟»

“Umeibakishia nini familia yako?”

Akajibu, “Nimewabakishia Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ.”¹

‘Ikrimah (bin Abu Jahl) na wapiganaji wengine wawili walipewa maji walipojeruhiwa katika vita vya Al-Yarmuk, na kila mmoja wao alisema kuwa tama la maji apewe mwingine miongoni mwa watu hao watatu waliojeruhiwa. Wakafanya hivyo ingawa walikuwa wamejeruhiwa vibaya na wakiwa na kiu kali. Maji yalipomfikia mtu wa tatu, alikutwa amefariki na wengine wawili walifariki na hakuna yeyote kati yao aliyekunywa maji hayo! Allah تعالى Awe radhi nao na wao wawe radhi Naye.

Al-Bukhari amenukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, “Kuna mtu alikuja kwa Mtume ﷺ na kumuambia, ‘Ewe Mtume! Umaskini umenishika.’ Mtume ﷺ alimtuma mjumbe kwa wakeze (wamletee mtu huyo chakula) lakini wakasema kuwa hakikuwepo. Mtume ﷺ akasema,

«أَلَا رَجُلٌ يُضَيِّفُ هَذَا، اللَّيْلَةَ، رَحِمَهُ اللهُ»

“Nani atakayemualika mtu huyu au kumfanyia ukarimu kama mgeni wake usiku wa leo; Allah Ampe Rehema Zake.”

Mtu mmoja katika Ansari alisema, ‘Mimi, Ewe Mjumbe wa Allah!’ Akamchukua nyumbani kwake na kumuambia mkewe, ‘Mfanyie ukarimu mgeni wa Mtume ﷺ.’ Akasema, ‘Wallah! Hakuna zaidi ya mlo wa watoto wangu.’ Akasema, ‘Watoto wakitaka chakula, wapeleke kulala. Halafu zima taa na uende kulala usiku wa leo huku hujala.’ Alifanya alivyoelekezwa. Asubuhi yule Ansari alimuendea Mtume ﷺ ambaye alimuambia,

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 10:161.

لَقَدْ عَجَبَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ - أَوْ صَحَّكَ - مِنْ فُلَانٍ وَفُلَانَةٍ

"Allah Amependezewa au amefurahia kitendo cha fulani na mkewe."

Allah تعالى Akateremsha,

وَيُؤْتِرُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ

"...bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji."

Al-Bukhari ameinukuu Hadithi hii katika sehemu nyingine ya Sahihi yake. Muslim, At-Tirmidhi, An-Nasa'i waliikusanya Hadithi hii. Katika masimulizi mengine ya Hadithi hii, jina la Swahaba lilitajwa, kuwa ni Abu Talhah Al-Ansari, Allah تعالى Awe Radhi Naye.² Kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

"Na wenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa."

Yaani walioondolewa uchoyo, basi wamefaulu na kufanikiwa. Imamu Ahmad amenukuu kuwa Jabir bin 'Abdullah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِيَّاكُمْ وَالظُّلْمَ، فَإِنَّ الظُّلْمَ ظَلَمَاتٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَاتَّقُوا الشُّحَّ، فَإِنَّ الشُّحَّ أَهْلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ، حَمَلَهُمْ عَلَىٰ أَنْ سَفَكُوا دِمَاءَهُمْ وَاسْتَحَلُّوا مَحَارِمَهُمْ»

"Nakutahadharisheni dhidi ya dhuluma, kwani dhuluma ni giza katika Siku ya Kiama. Nakutahadharisheni dhidi ya uchoyo, kwani uchoyo umewaangamiza wale wa kabla yenu. Yaliwafanya wamwage damu na kuhalalisha haramu."³

Muslim aliikusanya Hadithi hii.⁴ Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Al-Aswad bin Hilal amesema kuwa mtu mmoja alimuambia 'Abdullah (bin Mas'ud رضي الله عنه), "Ewe Abu 'Abdur-Rahman! Nahofia kuwa nimejiangamiza." 'Abdullah رضي الله عنه akamuuliza kulikuwa na nini na akasema, "Nilisikia Kauli ya Allah تعالى,

¹ Fat'h Al-Bari 8:500.

² Fat'h Al-Bari 7:149, Muslim 3:1624, 1625, Tuhfatul Al-Ahwadhi 9:197, An-Nasai katika Al-Kubra 6:486.

³ Ahmad 3:323.

⁴ Muslim 4:1996.

وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

“Na wenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa.”

Nami kwa kiasi fulani ni mchoyo ambaye ni nadra kutoa kitu.” ‘Abdullah عنه رضي الله عنه akasema, “Huo si uchoyo Aliotaja Allah تعالى katika Qur’an, unaohusu kutumia mali ya nduguyo bila ya haki. Wewe una ubahili, na jambo baya kwa hakika, ni kuwa mbahili.”¹ Kauli ya Allah تعالى,

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿١٠﴾

“Na waliokuja baada yao wanasema: Mola Wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani, wala Usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walioamini. Mola Wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye Kurehemu.”

Hii ni aina ya tatu ya waumini ambapo walio maskini zaidi wanastahili kupewa sehemu ya *Fai’*. Hao ni *Muhajirin*, *Ansar* na waliowafuata kwa wema. Kauli ya Allah تعالى katika Ayah nyingine,

وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ

“Na wale waliotangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na waliowafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu Ameridhika nao, na wao wameridhika naye.” (9:100)

Na waliowafuata *Muhajirin* na *Ansar* katika kazi zao njema, Sifa nzuri na wenye kuwaombea kwa Allah تعالى hadharani na faraghani. Ndio sababu Allah تعالى Amesema katika Aya hii tukufu,

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ

“Na waliokuja baada yao wanasema...”

¹ At-Tabari 28:29.

Maana yake: Kauli kuwa wanasema,

رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا

“Mola Wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala Usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani...”

Maana yake: Hasira au husuda,

لِلَّذِينَ ءَامَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

“...kwa walioamini. Mola Wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye Kurehemu.”

Kwa hakika, ametumia Imamu Malik رحمه الله تعالى katika Ayah hii tukufu maelezo mazuri kuwa *Rafidhah*¹ wanaowatukana Masahaba hawana fungu katika mali ya *Fai'*, kwa sababu wanashindwa kufanya uadilifu wa wale aliowasifia hapa Allah تعالى kuwa wanasema,

رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

“Mola Wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani, wala Usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walioamini. Mola Wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye Kurehemu.”

Ibn Abi Hatim رضي الله عنها amenukuu kuwa Aishah رضي الله تعالى عنها amesema, “Waliamrisha kumuomba Allah تعالى Awasamehe, badala yake, waliwatukana!”² (‘Aishah رضي الله عنها) Akasoma Aya hii,

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ

“Na waliokuja baada yao wanasema: Mola Wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani”

¹ Kikundi cha Shia.

² Muslim ameandika masimulizi sawa na hayo, 4:2317.

* أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَئِنْ أُخْرِجْتُمْ لَنَخْرُجَنَّ مَعَكُمْ وَلَا نُطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا وَإِنْ قُوتِلْتُمْ لَنَنْصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿١١﴾ لَئِنْ أُخْرِجُوا لَا تَخْرُجُونَ مَعَهُمْ وَلَئِنْ قُوتِلُوا لَا يَنْصُرُونَهُمْ وَلَئِنْ نَصَرُوهُمْ لَيُولِيَنَّ الْأُذُنُ نُمْرًا لَا يَنْصُرُونَ ﴿١٢﴾ لَأَنْتُمْ أَشَدُّ رَهَبَةً فِي صُدُورِهِمْ مِنَ اللَّهِ ۗ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ ﴿١٣﴾ لَا يُقْتَلُونَكُمْ جَمِيعًا إِلَّا فِي قُرَى مُحَصَّنَةٍ أَوْ مِنْ وَرَاءِ جُدُرٍ بَأْسُهُمْ بَيْنَهُمْ شَدِيدٌ ۗ خَسِبُكُمْ جَمِيعًا وَقُلُوبُهُمْ شَتَّىٰ ۗ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٤﴾ كَمَثَلِ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ قَرِيبًا ۗ ذَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٥﴾ كَمَثَلِ الشَّيْطَانِ إِذْ قَالَ لِلْإِنْسَانِ اكْفُرْ فَلَمَّا كَفَرَ قَالَ إِنِّي بَرِيءٌ مِنْكَ إِنِّي الْعَلَمَانِ ﴿١٦﴾ فَكَانَ عَاقِبَتَهُمَا أَنَّهُمَا فِي النَّارِ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ وَذَلِكَ جَزَاءُ الظَّالِمِينَ ﴿١٧﴾

* أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَئِنْ أُخْرِجْتُمْ لَنَخْرُجَنَّ مَعَكُمْ وَلَا نُطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا وَإِنْ قُوتِلْتُمْ لَنَنْصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿١١﴾ لَئِنْ أُخْرِجُوا لَا تَخْرُجُونَ مَعَهُمْ وَلَئِنْ قُوتِلُوا لَا يَنْصُرُونَهُمْ وَلَئِنْ نَصَرُوهُمْ لَيُولِيَنَّ الْأُذُنُ نُمْرًا لَا يَنْصُرُونَ ﴿١٢﴾ لَأَنْتُمْ أَشَدُّ رَهَبَةً فِي صُدُورِهِمْ مِنَ اللَّهِ ۗ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ ﴿١٣﴾ لَا يُقْتَلُونَكُمْ جَمِيعًا إِلَّا فِي قُرَى مُحَصَّنَةٍ أَوْ مِنْ وَرَاءِ جُدُرٍ ۗ بَأْسُهُمْ بَيْنَهُمْ شَدِيدٌ ۗ خَسِبُكُمْ جَمِيعًا وَقُلُوبُهُمْ شَتَّىٰ ۗ ذَلِكَ

بَأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٤﴾ كَمَثَلِ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ قَرِيبًا ۗ ذَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٥﴾ كَمَثَلِ الشَّيْطَانِ إِذْ قَالَ لِلْإِنْسَانِ اكْفُرْ فَلَمَّا كَفَرَ قَالَ إِنِّي بَرِيءٌ مِنْكَ إِنِّي الْعَلَمَانِ ﴿١٦﴾ فَكَانَ عَاقِبَتَهُمَا أَنَّهُمَا فِي النَّارِ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ وَذَلِكَ جَزَاءُ الظَّالِمِينَ ﴿١٧﴾

11. Huwaoni wanao fanya unaafiki wanawaambia ndugu zao walio kufuru katika Watu wa Kitabu: Mkitolewa na sisi lazima tutatoka pamoja nanyi, wala hatutam'tii yeyote kabisa dhidi yenu. Na mkipigwa vita lazima

tutakusaidieni. Na Mwenyezi Mungu Anashuhudia kuwa hao hakika bila ya shaka ni waongo.

12. Pindi wakitolewa hawatatoka pamoja nao, na wakipigwa vita hawatawasaidia. Na kama wakiwasaidia basi watageuza migongo; kisha hawatanusuriwa.

13. Hakika nyinyi mnawakhofia zaidi katika vifua vyao kuliko Mwenyezi Mungu. Hayo ni kwa kuwa hao ni watu wasiofahamu kitu.

14. Hawatapigana nanyi kwa mkusanyiko isipo kuwa katika vijiji vilivyozatitiwa kwa ngome, au nyuma ya kuta. Wao kwa wao vita vyao ni vikali. Utawadhania kuwa wako pamoja, kumbe nyoyo zao ni mbali mbali. Hayo ni kwa kuwa wao ni watu wasio na akili.

15. Ni kama mfano wa waliokuwa kabla yao hivi karibuni. Walionja uovu wa mambo yao. Nao watapata adhabu iliyo chungu.

16. Ni kama mfano wa Shetani anapomuambia mtu: Kufuru. Na akikufuru humuambia: Mimi si pamoja nawe. Hakika mimi namuogopa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.

17. Basi ikawa mwisho wa wote wawili hao ni kuingia Motoni, wadumu humo daima; na hiyo ndiyo jaza ya madhaalimu.

Ahadi ya Uongo ya Wanafiki kwa Bani An-Nadhir (Wayahudi)

Allah تعالى Anaeleza kuwa wanafiki, 'Abdullah bin Ubayy na wengine kama yeye, walimtuma mjumbe kwa Bani An-Nadhir ili kuwaahidi kuwasaidia. Allah تعالى Amesema,

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَإِن أُخْرِجْتُمْ

لنُخْرِجَنَّ بِكُمْ مَعَكُمْ وَلَا نَطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا وَإِن قُوتِلْتُمْ لَنَنصُرَنَّكُمْ

“Huwaoni wanaofanya unaafiki wanawaambia ndugu zao waliokufuru katika Watu wa Kitabu: Mkitolewa na sisi lazima tutatoka pamoja nanyi, wala hatutamt’ii yeyote kabisa dhidi yenu. Na mkipigwa vita lazima tutakusaidieni.”

Allah تعالى Akasema,

وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ

“Na Mwenyezi Mungu Anashuhudia kuwa hao hakika bila ya shaka ni waongo.”

Inamaanisha, wanafiki walidanganya walipotoa ahadi hiyo, kwasababu yalikuwa maneno tu lakini hawakukusudia kuyatimiza. Pia, walichosema kuwa wangekifanya, wasingeweza kamwe kuwatimizia, na kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema,

وَلَيْنَ قُوتُلَا لَا يَنْصُرُوهُمْ

“...na wakipigwa vita hawatawasaidia.”

Inamaanisha, wanafiki hawatashirikiana na Wayahudi katika mapigano.

وَلَيْنَ نَّصْرُوهُمْ

“Na kama wakiwasaidia...”

Hata kama wanafiki wangepigana upande wao.

لِيُؤْتِيَ الْأَدْبَرَ ثُمَّ لَا يُنصَرُونَ

“...basi watageuza migongo; kisha hawatanusuriwa.”

Aya hii ina habari njema, kama habari njema inayoletwa na Ayah inayofuata,

لَأَنْتُمْ أَشَدُّ رَهْبَةً فِي صُدُورِهِمْ مِنَ اللَّهِ

“Hakika nyinyi ni kitisho zaidi katika vifua vyao kuliko Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Wanafiki wanakuogopeni zaidi ya wanavyomuogopa. Kama Alivyosema;

إِذَا فَرِيقٌ مِّنْهُمْ تَخَشَّوْنَ النَّاسَ كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً

“...kundi moja kati yao liliwaogopa watu kama kumuogopa Mwenyezi Mungu, au kwa khofu kubwa zaidi.” (4:77)

Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ

“Hayo ni kwa kuwa wao ni watu wasio na akili.”

Allah تعالى Akasema,

لَا يُفْتَلُونَكُمْ جَمِيعًا إِلَّا فِي قُرَىٰ مُّحَصَّنَةٍ أَوْ مِنْ وَرَاءِ جُدُرٍ

“Hawatapigana nanyi kwa mkusanyiko isipokuwa katika vijiji vilivyozatitiwa kwa ngome, au nyuma ya kuta.”

Inamaanisha, hawatawapiga Waislamu isipokuwa kutokea nyuma ya ngome zilizingirwa, kwasababu ya kuwaogopa Waislamu. Watapigana tu watakapolazimika kujilinda (ingawa wanawaogopa Waislamu kulipiza kisasi).

Allah تعالى Amesema,

بِأَسْهُمٍ بَيْنَهُمْ شَدِيدٌ

“Wao kwa wao vita vyao ni vikali.”

Maana yake: Uadui uliopo baina yao ni mkubwa.

وَيُذِيقُ بَعْضَكُمْ بَأْسَ بَعْضٍ

“...au kukuleteeni fujo la mfarakano.” (6:65)

Kauli ya Allah تعالى katika Aya,

تَحْسَبُهُمْ جَمِيعًا وَقُلُوبُهُمْ شَتَّىٰ

“Utawadhania kuwa wako pamoja, kumbe nyoyo zao ni mbali mbali.”

Maana yake: Ingawa mtu anaweza kuwaona wakiunganisha majeshi na kudhania kuwa majeshi hayo yana mshikamano, bado kiukweli, wamegawanyika sana. Ibrahim An-Nakha' alisema kuwa Aya hii inarejea kwa wanafiki na watu waliopewa Kitabu,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ

“Hayo ni kwa kuwa wao ni watu wasio na akili.”

Kauli ya Allah تعالى،

كَمَثَلِ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ قَرِيبًا ذَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٥٩﴾

“Ni kama mfano wa waliokuwa kabla yao hivi karibuni. Walionja uovu wa mambo yao. Nao watapata adhabu iliyochungu.”

Inamaanisha kabila la Kiyahudi la Bani Qaynuqa¹, kwa mujibu wa Ibn’ Abbas, Qatadah na Muhammad bin Ishaq رضي الله عنهم.²

Mfano wa Wanafiki na Wayahudi

Kauli ya Allah تعالى،

كَمَثَلِ الشَّيْطَانِ إِذْ قَالَ لِلْإِنْسَانِ اكْفُرْ فَلَمَّا كَفَرَ قَالَ إِنِّي بَرِيءٌ مِّنْكَ

“Ni kama mfano wa Shetani anapomuambia mtu: Kufuru. Na akikufuru humuambia: Mimi si pamoja nawe.”

Maana yake: Mfano wa Wayahudi kudanganywa na ahadi za wanafiki, waliosema kuwa wangewasaidia kama Waislamu wangewapiga, ni shetani. Mambo yalipokuwa magumu na Wayahudi kuwekewa kizuizi, wanafiki waliwasaliti na kuwaacha wakipata kipigo kikubwa. Kadhalika, shetani huwahadaa wanadamu waingie kwenye ukafiri na watakapomtii, yeye huwakana na kujitenga na matendo yao, kwa kusema,

إِنِّي - أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ

“Hakika mimi namuogopa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

¹ At-Tabari 23:293.

² At-Tabari 23:293.

Kauli ya Allah تعالى،

فَكَانَ عَنَقِبَيْهِمَا آتُهُمَا فِي النَّارِ خَالِدِينَ فِيهَا

“Basi ikawa mwisho wa wote wawili hao ni kuingia Motoni, wadumu humo daima.”

Inamaanisha, mwisho wa wote, yeye, Shaytan, aliyewaamuru kukufuru na walioitikia wito wake, watakuwa katika Moto wa Jahanamu milele.

وَذَلِكَ جَزَاءُ الظَّالِمِينَ

“...na hiyo ndiyo jaza ya madhaalimu.”

Inamaanisha haya ni malipo ya mtu dhalimu.

* * *

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ
لِغَيْرِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٨﴾ وَلَا
تَكُونُوا كَالَّذِينَ نَسُوا اللَّهَ فَأَنْسَاهُمْ أَنفُسَهُمْ ؕ أُولَٰئِكَ هُم
الْفٰسِقُونَ ﴿١٩﴾ لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ
الْجَنَّةِ ۗ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفٰلِقُونَ ﴿٢٠﴾ لَوْ أَنزَلْنَا
هٰذَا الْقُرْءَانَ عَلَىٰ جَبَلٍ لَّرَأَيْتَهُ خٰشِعًا مُّتَصَدِّعًا مِّنْ
خٰشِيَةِ اللَّهِ ۗ وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ
يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾ هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ عَلِيمٌ
الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ۗ هُوَ الرَّحْمٰنُ الرَّحِيمُ ﴿٢٢﴾ هُوَ اللَّهُ
الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ أَلَمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ
الْمُهَيَّبُ الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ۗ سُبْحٰنَ اللَّهِ عَمَّا
يُشْرِكُونَ ﴿٢٣﴾ هُوَ اللَّهُ الْخَلِيقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ ۗ لَهُ
الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۗ يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ

وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٤﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ
وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَيْرِ ۗ وَاتَّقُوا
اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٨﴾
وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ نَسُوا اللَّهَ
فَأَنْسَاهُمْ أَنفُسَهُمْ ؕ أُولَٰئِكَ هُم
الْفٰسِقُونَ ﴿١٩﴾ لَا يَسْتَوِي
أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۗ
أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفٰلِقُونَ ﴿٢٠﴾

18. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayoyatangualiza kwa ajili ya Kesho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari ya mnyoyatenda.

19. Wala msuwe kama wale waliomsahau Mwenyezi Mungu, na Yeye Akawa-

sahaulisha nafsi zao. Hao ndio wapotovu.

20. Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.

Amri ya kuwa na Taqwa na Kujiandaa kwa ajili ya Siku ya Kiama

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Al-Mundhir bin Jarir amesimulia kuwa baba yake amesema, “Wakati tukiwa pamoja na Mtume ﷺ mwanzoni mwa mchana, baadhi ya watu ambao hawakuvaa viatu walikuja, wakiwa uchi, wamevaa nguo au majoho ya sufu yaliyokuwa na michirizi, wakiwa wameangika mapanga (shingoni mwao). Wote walikuwa wa kabila la Mudhar. Rangi ya Uso wa Mtume ﷺ ilibadilika alipowaona katika umaskini. Akaingia (nyumbani kwake) na kutoka na kumuamuru Bilal رضي الله عنه atoe *Adhan*. Bilal رضي الله عنه akatoa *Adhan* na *Iqamah*, na Mtume ﷺ akaongoza Sala. Akawahutubia, kwanza alisoma,

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ

“Enyi watu! Mcheni Mola Wenu Mlezi Aliye Kuumbeni kutokana na nafsi moja...” (4:1),

Mpaka mwisho wa Aya. Akaisoma Aya iliyo katika *Surat Al-Hashr*:

وَلَتَنْظُرَنَّهُ نَفْسٌ مَّا قَدَّامَتْ لِغَدٍ

“...na kila nafsi iangalie inayoyatanguliza kwa ajili ya Kesho.”

Akasema, “Kila mtu akawa anatoa Dinari yake, Dirhamu yake, nguo zake, Sa¹ Pishi yake ya ngano, Pishi Sa’i ya tende” — mpaka akasema — “hata kama ilikuwa nusu ya tende.” Kisha mtu mmoja katika *Ansar* alikuja hapo na mfuko wa hela, ambao alipata taabu kuubeba; kiukweli, mikono yake haikuweza kuubeba. Watu wakaendelea mpaka nikaona lundo la vyakula na nguo. Niliuona Uso wa Mtume ﷺ uking’aa kama dhahabu, kwa furaha. Mtume ﷺ akasema,

«مَنْ سَنَّ فِي الْإِسْلَامِ سُنَّةً حَسَنَةً فَلَهُ أَجْرُهَا وَأَجْرُ مَنْ عَمِلَ بِهَا بَعْدَهُ، مِنْ غَيْرِ أَنْ يُنْقَصَ مِنْ أَجْرِهِمْ شَيْءٌ، وَمَنْ سَنَّ فِي الْإِسْلَامِ سُنَّةً سَيِّئَةً كَانَ عَلَيْهِ وِزْرُهَا وَوِزْرُ مَنْ عَمِلَ بِهَا، مِنْ غَيْرِ أَنْ يُنْقَصَ مِنْ أَوْزَارِهِمْ شَيْءٌ»

“Mwenye kuanzisha mwendo mwema katika Uislamu, atapata malipo yake na malipo ya wenye kuufanya bila ya malipo yao

¹ Kipimo cha uzito, makofi manne ya mikono miwili kwa pamoja.

*kupungua chochote, na mwenye kuanzisha mwendo mbaya atabeba madhambi yake na madhambi ya mwenye kuufanya bila ya kuwapunguzia madhambi yao chochote.*¹

Muslim amenukuu Hadithi hii kupitia isnadi ya Shu'bah.² Kauli ya Allah تعالى

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اتَّقُوا اللّٰهَ

“Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu,”

Ameamrisha Taqwa ya Allah تعالى yenye kujumuisha kutii Amri Zake na kuepuka Anachokataza. Kauli ya Allah تعالى,

وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ^ط

“...na kila nafsi iangalie inayoyatanguliza kwa ajili ya Kesho.”

Maana yake: Jihesabuni kabla hamjalipwa, na mtafakari amali zenu njema mlizozitanguliza kwa ajili ya Siku ya kurejea kwenu na kukusanywa mbele ya Mola Wenu Mlezi,

وَآتَّقُوا اللّٰهَ^ع

“Mcheni Mwenyezi Mungu.”

Msisitizo wa pili,

إِنَّ اللّٰهَ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari ya mnayo yatenda.”

Allah تعالى Anaelezea kuwa kwa hakika, Anajua amali na hali zenu zote. Hakifichiki Kwake chochote, wala Hakosi Kuliona jambo lenu lolote, kubwa au dogo,

وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ نَسُوْا اللّٰهَ فَاَنْسَلَهُمْ اَنْفُسَهُمْ^ع

“Wala msiwe kama wale waliomsahau Mwenyezi Mungu, na Yeye Akawasahaulisha nafsi zao.”

¹ Ahmad 4:358.

² Muslim 2:704.

Maana yake: Msisahau kumtaja Allah تعالى, vinginevyo, Atakusahaulisheni kufanya amali njema kwa ajili ya kukunufaisheni wakati wa kurejea kwenu, kwa sababu jaza ni kwa jinsi ya amali.

Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

أُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

“Hao ndio wapotovu.”

Inamaanisha wenye kuacha kumtii Allah تعالى watakaoangamia katika Siku ya Kiama na kufeli wakati wa kurejea kwao.

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُمْ ءَمْوَالِكُمْ وَلَا ءَوْلَادُكُمْ عَن ذِكْرِ اللَّهِ ؕ وَمَن يَفْعَلْ ذَٰلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٩﴾

“Enyi mlioamini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio waliopata khasara.” (63:9)

Watu wa Peponi na Watu wa Jahanamu Hawalingani

Kauli ya Allah تعالى,

لَا يَسْتَوِي ءَصْحَابُ النَّارِ ؕ ءَصْحَابُ الْجَنَّةِ

“Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi.”

Inamaanisha, hao hawalingani katika hukumu ya Allah تعالى, katika Siku ya Kiama. Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine,

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ ءَجْرَحُوا السَّيِّئَاتِ أَن نَّجْعَلَهُم كَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّٰلِحٰتِ سَوَآءٌ مَّحْيَاهُمْ وَمَمَاتِهِم ۗ سَآءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿٢١﴾

“Je! Wanadhani wanaotenda maovu kuwa Tutawafanya kama walioamini, na wakatenda mema, sawa sawa uhai wao na kufa kwao? Ni hukumu mbaya wanayoihukumu!” (45:21),

وَمَا يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَلَا الْأُمِّيُّ ۗ قَلِيلًا مَّا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٥٨﴾

“Na kipofu na mwenye kuona hawalingani; na walio amini na watendao mema hawalingani na muovu. Ni machache mnayo yakumbuka.” (40:58), na,

أَمْ نَجْعَلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّقِينَ كَالْفُجَّارِ ﴿٥٩﴾

“Je! Tuwafanye walioamini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au Tuwafanye wachamungu kama waovu?” (38:28)

Kwa hiyo, Allah تعالى Anasema kuwa Atawatukuza wema na Kuwafedhehesha waovu. Na ndio sababu Akasema hapa,

أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفَائِزُونَ

“Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.”

Maana yake: Wao watakuwa salama na hawatapata adhabu ya Allah تعالى.

لَوْ أَنزَلْنَا هَذَا الْقُرْآنَ عَلَىٰ جَبَلٍ لَّرَأَيْتَهُ خَاشِعًا مُّتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ اللَّهِ ۗ وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٦٠﴾ هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَلَيْهِ السُّلْطَانُ ۗ وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٦١﴾ هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ۗ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٦٢﴾ هُوَ اللَّهُ الْخَلِيقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ ۗ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۗ يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٣﴾

21. Lau kuwa Tumeiteremsha hii Qur’ani juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeluona ukinyenyekea, ukipasuka kwa khofu ya Mwenyezi Mungu. Na hiyo mifano Tunawapigia watu ili wafikiri.

22. Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu, Ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mwenye Kuyajua yaliyofichikana na yanayoonekana. Yeye Ndiye Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

23. Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu Ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye Salama, Mtoaji wa Amani, Mwenye Kuyaendesha Mwenyewe mambo Yake, Mwenye Nguvu, Anayefanya Analolitaka, Mkubwa, Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayomshirikisha nayo.

24. Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu, Muumbaji, Mtengenezaji, Mtia Sura, Mwenye Majina mazuri kabisa. Kila kilioko katika mbingu na ardhi kinamtakasa, Naye ni Mwenye Kushinda, Mwenye Hikima.

Kubainisha Ukubwa na Utukufu wa Qur'an

Allah تعالى Anasisitiza utukufu wa Qur'an, na daraja yake ya juu. Na kwamba inastahiki nyoyo zinyenyekee na kuwa laini baada ya kuisikia, kwa sababu ya ahadi na vitisho vyake vya kweli.

لَوْ أَنْزَلْنَا هَذَا الْقُرْآنَ عَلَى جَبَلٍ لَرَأَيْنَاهُ خَسِيعًا مُتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ اللَّهِ

“Lau kuwa Tumeiteremsha hii Qur'ani juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeluona ukinyenyekea, ukipasuka kwa khofu ya Mwenyezi Mungu.”

Kama hivi ndivyo ilivyokuwa kwa milima migumu na mikubwa, kuwa kama ingefahamu Qur'an hii, ingenyenyekea na kuvunjika kwa kumuogopa Allah تعالى, vipi basi kuhusu nyinyi — Enyi wanadamu kwa nini nyoyo hazilainiki na kunyenyekea kwa Kumuogopa Allah تعالى, ilhali mnafahamu Amri ya Allah تعالى na kuzingatia Kitabu Chake. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema,

وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ

“Na hiyo mifano Tunawapigia watu ili wafikiri.”

Imethibiti katika Hadithi ya daraja ya *Mutawatir* inayoeleza kuwa Mtume ﷺ alimtuma mtu amtengenezee Minbar. Kabla ya hapo, alikuwa akisimama karibu na gogo la mti Msikitini wakati wa kuhutubia. Kwa hivyo, Minbar ilipotengenezwa na kuwekwa Msikitini, Mtume ﷺ alikuja kuhutubu na akakipita kigogo hicho cha mti, akaenda katika Minbar, kigogo cha mti kikaanza kulia, kama mtoto mchanga. Kigogo cha mti kilizoea kusikia Allah تعالى Akitajwa na wahyi ukisomwa karibu yake. Katika riwaya nyingine ya Hadithi hii, Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema baada ya kusimulia Hadithi hiyo, “Nyinyi - wanadamu - mnastahiki zaidi kuwa na hamu ya Mtume ﷺ kuliko kigogo cha mti!”¹

Kadhalika, Aya hii tukufu inauliza kuwa ikiwa milima migumu ingenyenyekea na kuvunjika kwa kumhofu Allah تعالى, kama ingesikia Kauli ya Allah تعالى na kuifahamu, vipi kuhusu nyinyi - Enyi wanadamu — mnaoisikia Qur'an na kuifahamu? Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَلَوْ أَنَّ قُرْءَانًا سُيِّرَتْ بِهِ الْجِبَالُ أَوْ قُطِعَتْ بِهِ الْأَرْضُ أَوْ كُفِّرَتْ بِهِ أَلْمُوتَىٰ

“Na kama ingelikuwako Qur’ani ndiyo inayoendeshe milima, na kupasuliwa ardhi, na kusemeshewa wafu.” (13:31)

Tumeshaeleza maana ya Aya hii kuwa, ingekuwa hivyo. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَأَنَّ مِنَ الْجِبَارَةِ لَمَا يَتَفَجَّرُ مِنْهُ الْأَنْهَارُ وَأَنَّ مِنْهَا لَمَّا يَشْقُقُ فَيَخْرُجُ مِنْهُ الْمَاءُ وَأَنَّ مِنْهَا لَمَّا يَهْبِطُ مِنَ خَشْيَةِ اللَّهِ

“...kwani kuna mawe yanayotimbuka mito, na kuna mengine yanayopasuka yakatoka maji ndani yake, na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu.” (2:74)

¹ *Fat’h Al-Bari* 6:696, A-Darimi 1:34, 35.

Kumtukuza Allah تعالى kwa Kutaja Majina na Sifa Zake

Allah تعالى Amesema,

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ۗ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿٥٩﴾

“Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu, Ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye tu. Mwenye Kuyajua yaliyofichikana na yanayoonekana. Yeye Ndiye Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.”

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye Pekee Ndiye Anayestahiki Kuabudiwa, hakuna mola ghairi Yake, wala hakuna mola wa viumbe, isipokuwa Yeye. Kila chenye kuabudiwa kisichokuwa Yeye ni batili. Allah تعالى Anajua Yote, ya ghaibu na ya kuonekana, Anajua yote yanayowahusu viumbe tunaowaona na tusiowaona. Hakuna cha mbinguni au ardhini Asichokijua, haijalishi kitukufu au dhalili, kikubwa au kidogo, hata sisimizi gizani. Kauli ya Allah تعالى,

هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ

“...Ndiye Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.”

Tumeshaelezea hayo mwanzoni mwa *Tafsir* hii, kwa hivyo si lazima kuyarudia hapa, na kusudio ni kuwa Allah تعالى ni Mwenye rehema pana yenye kuenea kwa Viumbe Vyake vyote. Yeye ni *Ar-Rahman* na *Ar-Rahim* wa dunia na Akhera. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ

‘Na Rehema Yangu imeenea kila kitu.’ (7:156),

كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ۗ

“Mola Wenu Mlezi Amejilazimisha Rehema...” (6:54), na,

قُلْ بِفَضْلِ اللَّهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُوا هُوَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ ﴿٥٨﴾

“Sema: Kwa Fadhila ya Mwenyezi Mungu na Rehema Yake! Basi nawafurahi kwa hayo. Haya ni bora kuliko hayo wanayoyakusanya.” (10:58)

Allah تعالى Amesema,

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ أَمْلِكُ

“Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu Ambaye hapana mola isipokuwa Yeye tu. Mfalme.”

Maana ya *Al-Malik* ni “Mmiliki na Mfalme wa vitu vyote,” Mwenye Uweza wote juu yao bila ya kizuizi wala upinzani. Kauli ya Allah تعالى,

الْقُدُّوسُ

“Al-Quddus.”

Inamaanisha “Mtakatifu,” kwa mujibu wa Wahb bin Munabbih, ilhali Mujahid na Qatadah wamesema kuwa *Al-Quddus* ni “Mbarikiwa.”¹ Ibn Jurayji amesema kuwa *Al-Quddus* ni, “Anayetukuzwa na malaika watukufu.”²

الْسَّلَامُ

“As-Salam.”

Inamaanisha, “Asiye na ila yoyote au upungufu na aibu zenye kupunguza sifa na vitendo Vyake kamilifu.” Kauli ya Allah تعالى,

الْمُؤْمِنُ

“Al-Mu'min.”

Maana yake: “Aliyewapa salama waja Wake kwa Kuahidi kuwa Hatawadhulumu,” kwa mujibu wa Adh-Dhahhak aliyeisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما.³ Qatadah amesema, *Al-Mu'min* inamaanisha kuwa “Allah تعالى Anathibitisha kuwa Kauli Zake ni kweli,”⁴ ilhali Ibn Zayd amesema kuwa inamaanisha, “Amewathibitishia waumini Wake wenye kumuamini.”⁵

¹ At-Tabari 23:203.

² *Ad-Dur Al-Manthur* 8:123.

³ *Ad-Dur Al-Manthur* 8:123.

⁴ At-Tabari 23:303.

⁵ At-Tabari 23:303.

Kauli ya Allah تعالى،

الْمُهَيَّمِينَ

“Al-Muhaymin.”

Inamaanisha, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na wengine, “Shahidi kwa amali zote za waja Wake,” kuwa Yeye ni, Mwenye Kuwaangalia.¹

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika aya zingine,

وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushuhudia kila kitu.” (58:6),

ثُمَّ اللَّهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَا يَفْعَلُونَ ﴿٤٦﴾

“Kisha Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa wanayoyafanya.” (10:46),

na,

أَفَمَنْ هُوَ قَائِمٌ عَلَىٰ كُلِّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ ﴿٣٣﴾

“Je! Anayeisimamia kila nafsi kwa yale iliyoyachuma...?” (13:33)

Kauli ya Allah تعالى،

الْعَزِيزُ

“Al-‘Aziz.”

Inamaanisha kuwa “Yeye ni Mwenye Uweza, Mwenye Kukitenza nguvu kila kitu.” Kwa hiyo, Utukufu Wake haukiukwi, kwa sababu ya Uweza Wake, Utukufu, Nguvu za Kiburi Chake.

Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema;

الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ﴿٥٠﴾

“Al-Jabbar, Al-Mutakabbir.”

Maana yake: “Pekee Mwenye Kustahiki kuwa Mshurutishaji na Mkuu.” Ni kama ilivyoielezwa katika Sahih ambapo Allah تعالى Amesema,

¹ Al-Baghawi 4:326.

«الْعَظْمَةُ إِزَارِي، وَالْكِبْرِيَاءُ رِدَائِي، فَمَنْ نَارَعَنِي وَاحِدًا مِنْهُمَا عَذَّبْتُهُ»

“Utukufu ni Shuka Yangu na Kiburi ni Mtandio Wangu; kama yeyote atakayenivua moja kati ya mawili hayo, basi Nitamuadhibu.”¹

Allah تعالی Amesema,

سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ

“Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayo mshirikishanayo.”

Akasema,

هُوَ اللَّهُ الْخَلِيقُ الْبَارِيُّ الْمَصَوِّرُ

“Yeye ni Allah, Al-Khaliq, Al-Bari, Al-Musawwir.”

Al-Khaliq inarejea katika Kupima na Kuweka uwiano, *Al-Bari* inarejea katika Kuanzisha na Kufanya kiwepo kitu Alichokiumba na Kukipima. Kwa hakika, hakuna isipokuwa Allah تعالی Ndiye Mwenye uwezo wa Kupima, Kuleta na Kuumba chochote Anachotaka kiwepo. Kauli ya Allah تعالی,

الْخَلِيقُ الْبَارِيُّ الْمَصَوِّرُ

“Al-Khaliq, Al-Bari, Al-Musawwir.”

Inamaanisha kama Allah تعالی Anataka jambo, Huliambia tu “Kuwa” nalo linakuwa katika umbo Analotaka na namna Anayochagua,

فِي أَيِّ صُورَةٍ مَا شَاءَ رَكَّبَكَ

“Katika sura yoyote Aliyoipenda Akakujenga.” (82:8)

Allah تعالی Anaelezea kuwa Yeye ni *Al-Musawwir*, Anayekifanya kitu chochote Anachotaka kiwepo katika umbo na namna Anayotaka.

¹ Muslim 4:2023.

Al-Asma' Al-Husna

Allah تعالى Amesema,

لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ

“Mwenye Majina mazuri kabisa.”

Tumeeleza maana ya Ayah hii katika Tafsir ya *Surat Al-A'raf*.¹ Sahihi Mbili zimemnukuu Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ لِلَّهِ تَعَالَى تِسْعَةَ وَتِسْعِينَ اسْمًا، مِائَةٌ إِلَّا وَاحِدًا، مَنْ أَحْصَاهَا دَخَلَ الْجَنَّةَ، وَهُوَ
وِثْرٌ يُجِبُّ الْوِثْرَ»

*“Allah Mtukuka Ana Majina tisini na tisa, mia moja kasoro moja; mwenye kuyahifadhi, ataingia Peponi, na Yeye ni Witr (Mmoja) na Anapenda Witr.”*²

Kila Kitu Kinamsifu na Kumtukuza Allah تعالى

Kauli ya Allah تعالى,

يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ

“Kila kilioko katika mbingu na ardhi kinamtakasa.”

Ni sawa na Kauli Yake nyingine,

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمٰوٰتُ السَّبْعُ وَالْاَرْضُ وَمَنْ فِيْهِنَّ وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلٰكِنْ لَا
تَفْقَهُونَ تَسْبِيْحَهُمْ اِنَّهٗ كَانَ حَلِيْمًا غَفُوْرًا ﴿١٧﴾

‘Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa Sifa Zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye Maghfira.’ (17:44)

¹ Angalia juzu ya nne, *Tafsir ya Surat Al-A'raf*.

² Inamaanisha vitu vya witali, *Fat'h Al-Bari* 11:218, *Muslim* 4:2063.

Kauli ya Allah تعالى،

وَهُوَ الْعَزِيزُ

“Na Yeye ni Al-‘Aziz.”

Al-‘Aziz, Yaani, Utukufu Wake hauna ila.

الْحَكِيمُ

“Al-Hakim.”

Mwenye Hekima zote, katika Sheria na Amri Zake.

Huu ni mwisho wa *Tafsir* ya *Suratu Al-Hashr*. Kila Sifa Njema Anastahiki Allah

تعالى.

* * *

Tafsiri ya Suratul Mumtahanah

Sura ya 60

Iliteremshwa Madinah

سُورَةُ الْمُطَهَّنَاتِ

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوِّكُمْ ءَوْلِيَاءَ
تَلْقَوْتُمْ اِلَيْهِمْ بِالْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوا بِمَا جَاءَكُمْ مِنَ الْحَقِّ
تُخْرِجُونَ الرَّسُولَ وَإِيَّاكُمْ ۚ اَنْ تُؤْمِنُوا بِاللّٰهِ رَبِّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ
حَرَجْتُمْ جِهَدًا فِي سَبِيْلِ وَاَبِيغَاةٍ مَّرَضَاتِي ۚ تُسِرُّونَ اِلَيْهِمْ
بِالْمَوَدَّةِ وَاَنَا اَعْلَمُ بِمَا اَخْفَيْتُمْ وَمَا اَعْلَنْتُمْ ۚ وَمَنْ يَفْعَلْهُ
مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيْلِ ۝۱۰ اِنْ يَتَّقِفُوكُمْ يَكُوْنُوا
لَكُمْ اَعْدَاءً وَيَبْسُطُوْا اِلَيْكُمْ اَيْدِيَهُمْ وَاَلْسِنَتَهُمْ بِالسُّوْءِ
وَوَدُّوْا لَوْ تَكْفُرُوْنَ ۝۱۱ لَنْ تَنْفَعَكُمْ اَرْحَامُكُمْ وَلَا اَوْلَادُكُمْ
ۚ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ يَفْصِلُ بَيْنَكُمْ ۚ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ۝۱۲
قَدْ كَانَتْ لَكُمْ اُسُوْةٌ حَسَنَةٌ فِيْ اِبْرٰهِيْمَ وَاَلَّذِيْنَ مَعَهُۥ اِذْ
قَالُوْا لِقَوْمِهِمْ اِنَّا بُرَءُؤْا مِنْكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ
كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ اَلْعَدَاوَةُ وَاَلْبَغْضَاءُ اَبَدًا حَتّٰى
تُؤْمِنُوْا بِاللّٰهِ وَحَدَهٗ ۚ اِلَّا قَوْلَ اِبْرٰهِيْمَ لِاَبِيْهِ لَاسْتَغْفِرَنَّ لَكَ
وَمَا اَمْلِكُ لَكَ مِنَ اللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ ۗ رَبَّنَا عَلَيكَ تَوَكَّلْنَا وَاِلَيْكَ
اَتَيْنَا وَاِلَيْكَ الْمَصِيْرُ ۝۱۳ رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوْا
وَاعْفُزْ لَنَا رَبَّنَا ۗ اِنَّكَ اَنْتَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ۝۱۴ لَقَدْ كَانَ
لَكُمْ فِيْهِمْ اُسُوْةٌ حَسَنَةٌ لِّمَنْ كَانَ يَرْجُوْا اللّٰهَ وَاَلْيَوْمَ الْآخِرَ
وَمَنْ يَتَوَلَّ فَاِنَّ اللّٰهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيْدُ ۝۱۵

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Allah, Mwingi
wa Rehema, Mwenye
Kurehemu.

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا
عَدُوِّي وَعَدُوِّكُمْ ءَوْلِيَاءَ تَلْقَوْتُمْ
اِلَيْهِمْ بِالْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوا بِمَا
جَاءَكُمْ مِنَ الْحَقِّ تُخْرِجُونَ الرَّسُولَ
وَإِيَّاكُمْ ۚ اَنْ تُؤْمِنُوا بِاللّٰهِ رَبِّكُمْ
اِنْ كُنْتُمْ حَرَجْتُمْ جِهَدًا فِي سَبِيْلِ
وَاَبِيغَاةٍ مَّرَضَاتِي ۚ تُسِرُّونَ اِلَيْهِمْ
بِالْمَوَدَّةِ وَاَنَا اَعْلَمُ بِمَا اَخْفَيْتُمْ
وَمَا اَعْلَنْتُمْ ۚ وَمَنْ يَفْعَلْهُ مِنْكُمْ
فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيْلِ ۝۱۰ اِنْ
يَتَّقِفُوكُمْ يَكُوْنُوا لَكُمْ اَعْدَاءً
وَيَبْسُطُوْا اِلَيْكُمْ اَيْدِيَهُمْ
وَاَلْسِنَتَهُمْ بِالسُّوْءِ وَوَدُّوْا لَوْ
تَكْفُرُوْنَ ۝۱۱ لَنْ تَنْفَعَكُمْ اَرْحَامُكُمْ
وَلَا اَوْلَادُكُمْ ۚ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ
يَفْصِلُ بَيْنَكُمْ ۚ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ
بَصِيْرٌ ۝۱۲

1. Enyi mlioamini! Msiwafanye adui Zangu na adui zenu kuwa marafiki, mkiwapa mapenzi, na hali wao wamekwishaikataa haki iliyokujieni, wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi Wenu. Mnapotoka kwa ajili ya Jihadi katika Njia Yangu na kutafuta Radhi Yangu, mnafanya urafiki nao kwa siri, na Mimi Nayajua mnayoyaficha na mnayodhihirisha. Na mwenye kufanya hayo kati yenu basi ameipotea njia ya sawa.

2. Wakikushindeneni wanakuwa maadui zenu, na wanakukunjulieni mikono yao na ndimi zao kwa uovu. Na wanapenda muwe makafiri.

3. Hawatakufaeni jamaa zenu, wala watoto wenu Siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu Atapambanua baina yenu, na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyatenda.

Sababu za kushuka Surat Al-Mumtahanah

Habari ya Hatib bin Abi Balta'ah رضي الله عنه ndiyo sababu ya kushuka mwanzo wa Surah hii tukufu. Alikuwa katika Muhajirin wa Mwanzo na alishiriki katika vita vya Badr. Hatib رضي الله عنه alikuwa na watoto na mali huko Makkah, lakini kabila lake halikuwa Quraysh. Bali, alikuwa rafiki wa 'Uthman رضي الله عنه.

Mtume ﷺ alipoamua kuikomboa Makkah, baada ya watu wake kuvunja mkataba wa amani baina yao, aliamuru Waislamu waunde majeshi ili kuivamia Makkah, na akasema,

«اللَّهُمَّ عَمَّ عَلَيْهِمْ خَيْرَنَا»

"Ewe Allah! Zifiche habari zetu dhidi yao."

Hatib رضي الله عنه aliandika barua kwenda kwa watu wa Makkah, na mwanamke wa kabila la Quraysh akawajulisha nia ya Mtume ﷺ ya kuwavamia. Aliwataka kuwapa jukumu la kuipa usalama familia yake huko Makkah.

Allah تعالى Akamfahamisha hilo Mjumbe Wake, kwa sababu aliitikia dua ya Mtume ﷺ ya kuficha habari za uvamizi. Mtume ﷺ aliwatumia watu kumuendea mwanamke huyo na wakachukua barua. Kisa hiki kimeandikwa katika Sahihi Mbili.

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Hasan bin Muhammad bin 'Ali amesema kuwa 'Abdullah bin Abu Rafi` - au Ubaydullah bin Abu Rafi` - amesema kuwa alimsikia 'Ali رضي الله عنه akisema, "Mtume ﷺ alinituma mimi, Zubayr na Al-Miqdad na kutuambia,

«انظِرُوا حَتَّى تَأْتُوا رَوْضَةَ خَاخٍ فَإِنَّ بِهَا طَعِينَةً مَعَهَا كِتَابٌ فَخُذُوهُ مِنْهَا»

"Nendeni mpaka Rawdat Khakh,¹ ambapo mtamkuta mwanamke mwenye barua. Muichukue barua aliyo nayo."

Tukaelekea huko, huku farasi wetu wakienda mbio, mpaka tukafika Rawdah. Tukamkuta mwanamke na tukamuambia, 'Lete barua uliyo nayo.' Akasema, 'Sina barua.' Tukamuambia, 'Lete barua, vinginevyo, tutakuvua nguo.' Akaitoa kutoka katika misuko ya nywele zake na tukamletea Mtume ﷺ. Barua hiyo iliandikwa na Hatib bin Abu Balta`ah رضي الله عنه kwenda kwa wapagani wa Makkah, akiwaeleza kusudio la Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akamuuliza,

«يَا حَاطِبُ، مَا هَذَا؟»

"Ewe Hatib! Ni nini hiki?"

Hatib رضي الله عنه akamjibu, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Usiharakishe maamuzi juu yangu. Mimi sikuwa Mkuraishi, bali nilikuwa rafiki yao. Muhajirin wote waliokuwa pamoja nawe wana ndugu zao (huko Makkah) wenye kutetea familia zao. Kwa hivyo nilitaka kuwafanyia wema, ili kwamba huenda wangewahifadhi jamaa zangu, kwa kuwa sina undugu nao. Sikufanya hivyo kwa sababu ya ukafiri au kuritadi dini, wala sikufanya hivyo ili kuuhami ukafiri baada ya Kusilimu.' Mtume ﷺ akawaambia Masahaba wake,

«إِنَّهُ صَدَقَكُمْ»

"Kuhusu yeye, amekuambieni kweli."

'Umar رضي الله عنه akasema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Nipe ruhusa nikate kichwa cha mnafiki huyu!" Mtume ﷺ akasema,

¹ Mahali baina ya Makkah na Al-Madinah, kadiri ya maili kumi na mbili kutoka Al-Madinah

«إِنَّهُ قَدْ شَهِدَ بَدْرًا، وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ اللَّهَ أَطَّلَعَ إِلَى أَهْلِ بَدْرٍ فَقَالَ: اغْمَلُوا مَا شِئْتُمْ
فَقَدْ عَفَرْتُ لَكُمْ»

“Yeye alishiriki Vita vya Badr. huenda Allah Aliwaangalia walioshiriki Badr na kusema, “Enyi watu wa Badr, fanyeni mnavyotaka, kwani Nimeshakusameheni.”

Wote isipokuwa Ibn Majah, waliandika Hadithi hii kwa kutumia isnadi kadhaa za masimulizi ambamo yumo Sufyan bin ‘Uyaynah. Al-Bukhari ameongeza katika masimulizi yake katika mlango unaoeleza vita alivyoshiriki Mtume ﷺ, “Allah تعالی Akateremsha Aya,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوِّكُمْ أَوْلِيَاءَ

“Enyi mlioamini! Msiwafanye adui Zangu na adui zenu kuwa marafiki...”

Al-Bukhari amesema katika sehemu nyingine ya Sahihi yake, ‘Amr (msimulizi mmojawapo wa Hadithi) amesema, “Aya hii,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوِّكُمْ أَوْلِيَاءَ

“Enyi mlioamini! Msiwafanye adui Zangu na adui zenu kuwa marafiki...”

Ilishuka kumhusu Hatib رضي الله عنه, lakini sijui kama Ayah ilitajwa katika Hadithi (au ni maelezo ya msimuliaji mmojawapo).” Al-Bukhari pia amesema kuwa ‘Ali bin al-Madini amesema kuwa Sufyan bin ‘Uyaynah aliulizwa, “Je, hii ndiyo sababu ya kushuka Ayah hii,

لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوِّكُمْ أَوْلِيَاءَ

“Msiwafanye adui Zangu na adui zenu kuwa marafiki...”

Akajibu, “Haya ni masimulizi niliyokusanya kutoka kwa ‘Amr, sikuacha hata herufi moja. Sijui kama yupo mwingine aliyehifadhi maneno yake kama hivyo.”¹

¹ Fat’h Al-Bari 6:166, 7:592, 8:502, Muslim 4:1941, Abu Dawud 3:108, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:198, na An-Nasai katika Al-Kubra 6:487.

Amri ya Kuwafanya Makafiri Kuwa Maadui na Kuacha Kuwasadia

Kauli ya Allah تعالى،

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوَّكُمْ ءَوْلِيَاءَ تُلْقُونَ إِلَيْهِم بِالْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوا
بِمَا جَاءَكُمْ مِنَ الْحَقِّ

“Enyi mlio amini! Msiwafanye adui Zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi, na hali wao wamekwisha ikataa haki iliyo kujieni.”

Inarejea kwa washirikina na makafiri waliokuwa wakipigana dhidi ya Allah تعالى، Mjumbe Wake na waumini. Ni wao ndio ambao Allah تعالى Alioamua kuwa wawe maadui zetu na wapigwe vita. Allah تعالى Amewakataza waumini kuwafanya marafiki, wasaidizi au wenza.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine،

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصْرَىٰ ءَوْلِيَاءَ ۚ بَعْضُهُمْ ءَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَمَنْ
يَتَوَلَّهُمْ مِنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ

“Enyi mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao.” (5:51)

Ayah hii ina onyo kali na kitisho cha hakika. Allah تعالى Alisema،

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ أَخَذُوا دِينَكُمْ هُزُوًا وَلَعِبًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ
مِن قَبْلِكُمْ وَالْكَفَّارَ ءَوْلِيَاءَ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ كُنتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾

“Enyi mlioamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia kejeli na mchezo Dini yenu miongoni mwa waliopewa Kitabu kabla yenu, na makafiri wengine. Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni wenye kuamini.” (5:57)

يَتَّيِبُهُمُ اللَّهُ لِيَأْمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ۗ أُرِيدُونَ أَنْ تَجْعَلُوا لِلَّهِ
عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا مُبِينًا ﴿٤٤﴾

“Enyi mlioamini! Msiwafanye makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je, mnataka Mwenyezi Mungu Awe na hoja iliyowazi juu yenu?” (4:144) na,

لَا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ۗ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ
اللَّهِ فِي شَيْءٍ إِلَّا أَنْ تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقَنَّةً وَيُحَذِّرْكُمْ اللَّهُ نَفْسَهُ ۗ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٣٨﴾

“Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.” (3:28)

Ndio sababu Mtume ﷺ alikubali udhuru wa Hatib رضي الله عنه pale aliposema kuwa alitaka tu kuwafanyia wema Makuraishi, kwasababu ya mali na wanafamilia aliowaacha Makkah. Kauli ya Allah تعالى,

تُخْرِجُونَ الرَّسُولَ وَإِيَّاكُمْ

“...wakamfukuza Mtume na nyinyi...”

Inafuata himizo Lake la Kuwapiga na Kuepuka kuwa wasaidizi wao. Hayo ni kwa sababu walimfukuza Mtume ﷺ na Masahaba wake رضي الله عنهم kutokana na kuchukia kwao Tawhid na kukataa kumuabudu Allah تعالى Pekee. Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

أَنْ تُوْمِنُوا بِاللَّهِ رَبِّكُمْ

“...kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi Wenu.”

Inamaanisha, ‘kosa lenu pekee ni kuwa mmemuamini Allah تعالى, Mola Mlezi wa vyote vilivyomo.’ Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَنْ يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٦٠﴾

“Nao hawakuona baya lolote kwao ila kuwa wakimuamini Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Msifiwa,” (85:8) na,

الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِينِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ ۗ

“Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila kwa kuwa wanasema: Mola Wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu!” (22:40)

Kauli ya Allah تعالى،

إِنْ كُنْتُمْ خَرَجْتُمْ جِهَادًا فِي سَبِيلِي وَابْتِغَاءَ مَرْضَاتِي

“Mnapotoka kwa ajili ya Jihadi katika Njia Yangu na kutafuta Radhi Yangu...”

Allah تعالى Anasema, ‘kama nyinyi ni sawa na mlivyosifiwa hapa, basi makafiri msiwasaidie. Kama mmehamia katika Jihad Yangu na kwa ajili ya kutafuta Radhi Zangu, basi msiwafanye marafiki maadui Zangu na maadui wenu, baada ya wao kukufukuzeni kutoka majumbani mwenu, kupora mali zenu na kukataa dini yenu.’ Kauli ya Allah تعالى،

تُسِرُونَ إِلَيْهِمْ بِالْمُؤَدَّةِ وَأَنَا أَعْلَمُ بِمَا أَخْفَيْتُمْ وَمَا أَعْلَنْتُمْ

“...mnafanya urafiki nao kwa siri, na Mimi Nayajua mnayoyaficha na mnayodhihirisha.”

Allah تعالى Anauliza, ‘je, mnafanya hivyo ilhali Ninajua siri za nyoyoni, nia na yote ya dhahiri.”

وَمَنْ يَفْعَلْهُ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿٦١﴾ إِنْ يَتَّقِفُواكُمْ يَكُونُوا لَكُمْ أَعْدَاءً وَيَبْسُطُوا
إِلَيْكُمْ أَيْدِيَهُمْ وَأَلْسِنَتَهُم بِالسُّوْءِ

“Na mwenye kufanya hayo kati yenu basi ameipotea njia ya sawa. Wakikuwezeni wanakuwa maadui zenu, na wanakukunjulieni mikono yao na ndimi zao kwa uovu.”

Inamaanisha, ‘wakikushindeni, watatumia kila aina ya ubaya ili kukuumizeni kwa maneno na vitendo.’

وَوُدُّوْا لَوْ تَكْفُرُوْنَ

“Na wanapenda muwe makafiri.”

Inamaanisha, ‘wana hamu kubwa kuwa msipate jema lolote. Kwa hiyo, uadui wao kwenu ni wa dhahiri na siri, kwa hivyo mnawezaje kuwasaidia watu wa aina hii.’ Hii pia inahimiza uadui. Kauli ya Allah تعالى،

لَنْ نَنْفَعَكُمْ أَرْحَامَكُمْ وَلَا أَوْلَادَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَفْصِلُ بَيْنَكُمْ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٦٠﴾

“Hawatakufaeni jamaa zenu, wala watoto wenu Siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu Atapambanua baina yenu, na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyatenda.”

Inamaanisha ‘mahusiano ya familia zenu hayatakunufaisheni kwa Allah تعالى kama Allah تعالى Ataamua Kukudhuruni kwa namna yoyote. Mahusiano yenu hayatakunufaisheni kama mtawapendezesha kwa Anachochukia Allah تعالى.’ Wenye kuafikiana na familia zao kuwa makafiri ili kuwaridhisha watapata hasara na kufeli na amali zao zitakuwa batili. Mahusiano yao hayatawanufaisha mbele ya Allah تعالى، hata kama uhusiano wao ulikuwa pamoja na Mtume ﷺ. Imamu Ahmad amenukuu kuwa Anas رضي الله عنه amesema kuwa mtu mmoja alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Yuko wapi baba yangu.” Akamuambia,

«فِي النَّارِ»

“Motoni.”

Mtu huyo alipoondoka, Mtume ﷺ alimuita na kumuambia:

«إِنَّ أَبِي وَأَبَاكَ فِي النَّارِ»

“Kwa hakika, baba yangu na baba yako wako Motoni.”¹

Muslim na Abu Dawud² pia waliikusanya Hadithi hii.

¹ Ahmad 3:268.

² Muslim 1:191, Abu Dawud 5:90.

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَّاءُ مِنْكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَاءُ أَبَدًا حَتَّى تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَحَدَهُ إِلَّا قَوْلَ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ لَأَسْتَغْفِرَنَّ لَكَ وَمَا أَمْلِكُ لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ رَبَّنَا عَلَيْكَ تَوَكَّلْنَا وَإِلَيْكَ أَنْتَبْنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ ﴿٦٠﴾ رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا وَآغْفِرْ لَنَا رَبَّنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦١﴾ لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِيهِمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَنْ كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَمَنْ يَتَوَلَّ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٦٢﴾

4. Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale waliokuwa pamoja naye, walipowaambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni; na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka mtakapomuamini Mwenyezi Mungu Peke Yake. Isipo kuwa kauli ya Ibrahim kumuambia baba yake: Hakika nitakuomba msamaha, wala similiki chochote kwa ajili yako mbele ya Mwenyezi Mungu. Mola Wetu Mlezi! Juu Yako tumetegemea, na Kwako tumeelekea, na Kwako ndio marejeo.

5. Mola Wetu Mlezi! Usitufanyie mtihani kwa waliokufuru. Na tusamehe, Mola Wetu Mlezi. Hakika Wewe Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.

6. Kwa yakini umekuwa mfano mzuri kwenu katika mwendo wao, kwa anayemtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na mwenye kugeuka basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujitoshia, Msifiwa.

Waislamu wana Kigezo Kizuri kwa Ibrahim عليه السلام na Wafuasi wake, Watakapowakana Watu wao Walio Makafiri

Allah تعالى Anawaambia wenye kumuamini, Aliowaamuru kupambana na makafiri na uadui wao, na kujiepusha nao na kujitenga nao:

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ

“Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale waliokuwa pamoja naye.”

Maana yake: Wafuasi wake waliomuamini,

إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرءُؤُا مِنْكُمْ

“...walipowaambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi...”

Inamaanisha, ‘tunakukataeni.’

وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ

“...na hayo mnayoyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni...”

Maana yake: ‘Hatuiamini dini na njia yenu.’

وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَاءُ أَبَدًا

“...na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi...”

‘Uhasama na uadui vimekuwepo baina ya sisi na nyinyi tokea sasa na kipindi chote mtakapokuwa katika ukafiri; mara zote tutakukataeni na kukuchukieni.’

حَتَّىٰ تُوْمِنُوا بِاللَّهِ وَحَدَهُ

“...mpaka mtakapomuamini Mwenyezi Mungu Peke Yake.”

Maana yake: ‘Isipokuwa mpaka mumuabudu Allah تعالى Pekee asiye na mshirika, msiamini masanamu na washindani mnaowaabudu badala Yake.’

Kauli ya Allah تعالى,

إِلَّا قَوْلَ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ لَأَسْتَغْفِرَنَّ لَكَ

“Isipokuwa kauli ya Ibrahim kumuambia baba Yake: Hakika nitakuombea msamaha.”

Inamaanisha ‘mna mfano mzuri kutoka kwa Ibrahim عليه السلام na watu wake; ama kuhusu dua ya Ibrahim عليه السلام kumuombea baba yake, ilikuwa ahadi aliyoiweka kwa ajili ya baba yake.’ Ibrahim عليه السلام alipokuwa na hakika kuwa baba yake alikuwa adui wa Allah تعالى, alijitangaza kuwa yuko mbali naye. Baadhi ya waumini walikuwa wakiwaombea dua wazazi wao waliokufa katika ukafiri, na kuwaombea maghufira kwa Allah تعالى. Walifanya hivyo, kwa kudai

kuwa Ibrahim عليه السلام alimuomba dua ya maghufira baba yake. Allah تعالى Amesema katika Kuwajibu,

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولَىٰ قُرْبَىٰ مِنْ
بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿١١٣﴾ وَمَا كَانَ أَسْتِغْفَارُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا
عَنْ مَوْعِدَةٍ وَعَدَهَا إِيَّاهُ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ أَنَّهُ عَدُوٌّ لِلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ ۚ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ

“Haimpasii Nabii na wale walioamini kuwatakia msamaha washirikina, ijapokuwa ni jamaa zao, baada ya kwisha bainika kuwa hao ni watu wa Motoni. Wala haikuwa Ibrahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye. Lakini ilipombainikia kwamba yeye ni adui ya Mwenyezi Mungu, alijjepusha naye. Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, mnyenyekevu,¹ mvumilivu.” (9:113-114)

Kauli ya Allah تعالى hapa,

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرءُؤُا مِنْكُمْ

“Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale waliokuwa pamoja naye, walipowaambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi...” mpaka,

إِلَّا قَوْلَ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ لَأَسْتَغْفِرَنَّ لَكَ وَمَا أَمْلِكُ لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ ^ط

“...Isipokuwa kauli ya Ibrahim kumuambia baba yake: Hakika nitakuomba msamaha, wala similiki chochote kwa ajili yako mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Inamaanisha, ‘Hamtaweza kufuata mfano wa Ibrahim عليه السلام kama ushahidi katika jambo lililotajwa hapa, kama kuwa aliruhusu kumuomba Allah تعالى Awasamehe waliokufa katika Shirk.’ Hii ni kauli ya Ibn ‘Abbas, Mujahid, Qatadah, Muqatil bin Hayyan, Adh-Dhahhak na wengine kadhaa رضي الله عنهم ¹.

¹ Angalia Tafsir ya Surat At-Tawbah (9:114).

² At-Tabari 23:318.

Allah تعالى Amesema kuwa Ibrahim عليه السلام na Masahaba wake, waliondoka pamoja na watu wao na kukataa njia yao, amesema baadaye, huku akimuomba Allah تعالى kwa unyenyekevu,

رَبَّنَا عَلَيْكَ تَوَكَّلْنَا وَإِلَيْكَ أَنبَأْنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ

“Mola Wetu Mlezi! Juu Yako tumetegemea, na Kwako tumeelekea, na Kwako ndio marejeo.”

Tunajisamilisha Kwako, na Kwako ndio Marejeo ya Mwisho, Akhera.”

رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا

“Mola Wetu Mlezi! Usitufanyie mtihani kwa waliokufuru.”

Mujahid amesema, “Inamaanisha, ‘Usituadhibu kwa mikono yao, wala kwa adhabu kutoka Kwako.’ Au watasema, ‘Kama watu hawa wangukuwa wenye kufuata ukweli, adhabu isingewafikia.”¹ Adh-Dhahhak amesema sawa na hayo. Qatadah amesema, “Usiwape makafiri ushindi juu yetu, na Kutuweka katika majaribu mikononi mwao. Kwa hakika, kama Utafanya hivyo, basi watadhani kuwa wamepewa ushindi juu yetu kwa sababu wao wako katika ukweli.” Maana hiyo ndiyo aliyoichagua Ibn Jarir رحمه الله تعالى. ‘Ali bin Abi Talhah amesimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: “Usiwape utawala juu yetu, tusije pata majaribu kwa mikono yao.” Kauli ya Allah تعالى,

وَأَغْفِرْ لَنَا رَبَّنَا إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Na tusamehe, Mola Wetu Mlezi. Hakika Wewe Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Inamaanisha, ‘Usiyadhihirishe makosa yetu kwa wengine wasiokuwa Wewe, na Utusamehe kwa yaliyo kati ya sisi na Wewe.’

إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Hakika Wewe Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Na wenye kutafuta hifadhi katika Utukufu Wako kamwe hawatadhulumiwa.’

¹ At-Tabari 23:319.

الْحَكِيمُ

“Mwenye Hikima.”

‘Katika Maneno, Matendo, Sheria na Amri Zako.’ Allah تعالى Amesema,

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِيهِمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ

“Kwa yakini umekuwa mfano mzuri kwenu katika mwendo wao, kwa anayemtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”

Kwa kurudia kusema alichokisema hapo kabla bila ya kukitaja, yaani, mfano mwema Alioutaja Allah تعالى hapo kabla,

لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ

“...kwa anayemtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”

Kwa hivyo Anawahimiza waumini wanaomuamini Allah na Kurejea Kwake. Kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ يَتَوَلَّ

“Na mwenye kugeuka...”

Maana yake: Mbali na Alichomrisha Allah تعالى,

فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ

“Basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujitosha, Msifiwa.”

Kauli ya Allah تعالى: Katika Aya nyingine,

إِن تَكْفُرُوا أَنْتُمْ وَمَن فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَأِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ

“Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitosha, Msifiwa.” (14:8)

‘Ali bin Talhah amesimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما,

لَغَنِيٌّ

“Ghani”

Ni "Aliye Tajiri kikamilifu." Ambaye ni Allah تعالی. Hii ni Sifa ya Allah تعالی Anayostahiki Yeye Pekee; kwa hakika, Hana wa kulingana, hakuna kama Yeye. Kila Sifa Njema ni za Allah تعالی, Mmoja, Mkamilifu.

حميد

"Hamid"

Inamaanisha Anayestahiki Kusifiwa, katika Kauli Zake na Matendo Yake yote, hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye Peke Yake.

* * *

* عَسَىٰ اللَّهُ أَنْ يَجْعَلَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ
 الَّذِينَ عَادَيْتُمْ مِنْهُمْ مَوَدَّةً
 ۚ وَاللَّهُ قَدِيرٌ ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٦٠﴾ لَا يَنْهٰكُمُ اللَّهُ عَنِ
 الَّذِينَ لَمْ يُقْتِلُوْكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوْكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ اَنْ
 تَبْرُوْهُمْ وَتُقْسِطُوْا اِلَيْهِمْ ۚ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ اَلْمُقْسِطِيْنَ ﴿٦١﴾
 اِنَّمَا يَنْهٰكُمُ اللّٰهُ عَنِ الَّذِيْنَ قَتَلُوْكُمْ فِي الدِّينِ
 وَاَخْرَجُوْكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ وَظَنُّوْهُمُ عَلَىٰ اِخْرَاجِكُمْ اَنْ
 تَوَلَّوْهُمْ ۚ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الظَّالِمُوْنَ ﴿٦٢﴾

* عَسَىٰ اللَّهُ أَنْ يَجْعَلَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ
 الَّذِينَ عَادَيْتُمْ مِنْهُمْ مَوَدَّةً ۚ وَاللَّهُ قَدِيرٌ
 ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٦٠﴾ لَا يَنْهٰكُمُ
 اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقْتِلُوْكُمْ فِي الدِّينِ
 وَلَمْ يُخْرِجُوْكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ اَنْ تَبْرُوْهُمْ
 وَتُقْسِطُوْا اِلَيْهِمْ ۚ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ
 اَلْمُقْسِطِيْنَ ﴿٦١﴾ اِنَّمَا يَنْهٰكُمُ اللّٰهُ
 عَنِ الَّذِيْنَ قَتَلُوْكُمْ فِي الدِّينِ

وَأَخْرَجُوكُمْ مِّن دِيَارِكُمْ وَظَنُّوْهُمُ عَلَىٰ إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوْهُمْ ۚ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٦٢﴾

7. Asaa Mwenyezi Mungu Akatia mapenzi baina yenu na hao maadui zenu, na Mwenyezi Mungu ni Muweza, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

8. Mwenyezi Mungu Hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao uadilifu.

9. Hakika Mwenyezi Mungu Anakukatazeni kufanya urafiki na wale waliokupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanaowafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu.

Huenda Allah تعالیٰ Ataweka Urafiki Baina Yenu na Maadui Zenu

Kauli ya Allah تعالیٰ kwa waumini, baada ya Kuwaamrisha wawe maadui kwa makafiri,

عَسَىٰ اللَّهُ أَنْ يَجْعَلَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ الَّذِينَ عَادَيْتُمْ مِنْهُمْ مَوَدَّةً

“Asaa Mwenyezi Mungu Akatia mapenzi baina yenu na hao maadui zenu.”

Maana yake: Mapenzi baada ya uadui, ulaini baada ya ubaridi na kuwa pamoja baada ya kutengana.

وَاللَّهُ قَدِيرٌ

“...na Mwenyezi Mungu ni Muweza,”

Allah تعالى Ana Uweza wa Kuwakusanya wenye kutofautiana na Kuziweka nyoyo pamoja, baada ya kuwa na uhasama na ugumu. Katika hali hii, nyoyo zitapatana, kama Alivyosema Allah تعالى Alipotaja Fadhila Zake kwa Ansar,

وَأَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءَ فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا
وَكُنْتُمْ عَلَىٰ شَفَا حُفْرَةٍ مِّنَ النَّارِ فَأَنْقَذَكُم مِّنْهَا

“Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile mlivyo kuwa nyinyi kwa nyinyi maadui Naye Akaziunganisha nyoyo zenu; kwa Neema Yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto, Naye Akakuokoeni nalo.” (3:103)

Pia Mtume ﷺ aliwaaambia,

«أَلَمْ أَجِدْكُمْ ضَالًّا فَهَدَاكُمْ اللَّهُ بِِي، وَكُنْتُمْ مُتَفَرِّقِينَ فَأَلَّفَكُمُ اللَّهُ بِِي؟»

“Je, sijakukuteni mliopotea, na Allah Akakuongoeni kupitia kwangu; na mligawanyika katika makundi, na Allah Akaunganisha nyoyo zenu kupitia kwangu.”¹

Allah تعالى Amesema,

هُوَ الَّذِي أُيِّدَكَ بِنَصْرِهِ وَبِالْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٠﴾ وَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ لَوْ أَنْفَقْتَ مَا فِي
الْأَرْضِ جَمِيعًا مَا أَلَّفْتَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ أَلَّفَ بَيْنَهُمْ إِنَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦١﴾

“Kwani Yeye Ndiye Aliyekuunga mkono kwa nusura Yake na kwa Waumini. Na Akaziunga nyoyo zao. Na lau wewe ungelitoa vyote viliomo duniani usingeliweza kuziunga nyoyo zao, lakini Mwenyezi

¹ Fath Al-Bari 7:644.

Mungu Ndiye Aliyewaunganisha. Hakika Yeye Ndiye Mtukufu Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.” (8:62,63)

Na katika Hadithi:

«أَحِبِّ حَبِيبَكَ هَذَا مَا، فَعَسَى أَنْ يَكُونَ بَعِيضَكَ يَوْمًا مَا، وَأَبْغِضْ بَعِيضَكَ هَذَا مَا، فَعَسَى أَنْ يَكُونَ حَبِيبَكَ يَوْمًا مَا»

“Mpende mpendwa wako kwa wastani, Asaa siku moja, anaweza kuwa adui yako. Mchukie kwa wastani anayekuchukia, kwasababu siku moja, anaweza kuwa mpendwa wako.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“...na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Inamaanisha Allah تعالى Anasamehe ukafiri wa makafiri kama watatubia Kwake, kurejea kwa Mola Wao Mlezi na kujisalimisha Kwake katika Uislamu. Kwa hakika, Yeye ni Mwingi wa Msamaha, Mwingi wa Rehema kwa wenye kutubia Kwake dhidi ya madhambi yao, na haijalishi aina ya dhambi.

Ruhusa ya Kuwafanyia Ukirimu Makafiri Wasiopigana Dhidi ya Dini

Kauli ya Allah تعالى؛

لَا يَنْهَى اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقْتَلُوا فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ

“Mwenyezi Mungu Hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu.”

Inamaanisha ambao hawakujihusisha na kufukuzwa kwenu.

Kwa hiyo, Allah تعالى Hajakukatazeni kuwafanyia wema makafiri wasiopigana nanyi kwasababu ya dini, kama vile makafiri wanawake na wanyonge,

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 6:133

أَنْ تَبْرُوهُمْ

“...kuwafanyia wema...” Uwe laini kwao,

وَتُقْسَطُوا إِلَيْهِمْ

“...na uadilifu...” Kuwafanyia uadilifu.

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسَطِينَ

“...Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao uadilifu.”

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Asma' bint Abubakr رضي الله عنها amesema, “Mama yangu, alikuwa mshirikina, alikuja kwangu katika wakati wa Mkataba wa Amani, Mtume ﷺ alipowekeana na Makuraishi. Nikaenda kwa Mtume ﷺ na kumuambia, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Mama yangu amekuja kuniangalia, na kutaka kitu kutoka kwangu, je, nimfanyie wema?’ Mtume ﷺ akamuambia,

«نَعَمْ صِلِي أُمَّكَ»

*“Ndiyo. Muunge mama yako.”*¹

Sahihi Mbili zimenukuu Hadithi hii.² Imamu Ahmad amenukuu kuwa ‘Abdullah bin Zubayr رضي الله عنه amesema, “Qutaylah alikuja kumtembelea binti yake, Asma' bint Abubakr رضي الله عنها, akiwa na zawadi, kama Samli, Jibini na siagi na vyakula lakini alikuwa mshirikina wakati huo. Asma' رضي الله عنها hakuzipokea na hakumruhusu kuingia nyumbani kwake.” ‘A’ishah رضي الله عنها akamuuliza Mtume ﷺ hukumu hiyo. Allah تعالى Akateremsha Aya,

لَا يَنْهَكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُفْتِنُوكُمْ فِي الدِّينِ

“Mwenyezi Mungu Hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita.”

Mpaka mwisho wa Aya. Mtume ﷺ alimuamuru Asma' رضي الله عنها apokee zawadi za mama yake na kumruhusu aingie nyumbani kwake.³ Kauli ya Allah تعالى,

¹ Ahmad 6:344

² Fat'h Al-Bari 5:275, na Muslim 2:696

³ Ahmad 4:4. Isnadi yake ina udhaifu, lakini maana yake inauungwa mkono na masimulizi yaliyotangulia. Na *Dibab* katika chakula kilichotayarishwa kwa tende na siagi liyochujwa.

إِنَّ اللَّهَ تُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao uadilifu.”

Imeelezwa vyema katika *Tafsir ya Surat Al-Hujurat*.¹ Pia tumetaja Hadithi sahihi,

«الْمُقْسِطُونَ عَلَى مَنَابِرَ مِنْ نُورٍ عَنِ يَمِينِ الْعَرْشِ، الَّذِينَ يَنْدِلُونَ فِي حُكْمِهِمْ وَأَهَالِيهِمْ وَمَا وَلَّوْا»

“Waadilifu, watakuwa juu ya majukwaa ya nuru, upande wa kulia wa Arshi, (sababu kubwa ni) kufanya uadilifu katika kuhukumu kwao na kufanya uadiifu kwa jamaa zao na katika usimamizi wao (katika majukumu yaliyo chini yao).”²

Kukatazwa Kuwafanya Marafiki Makafiri na Washirikina Wenye Kupigana Vita

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّمَا يَنْهَكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قَتَلُواكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِنْ دِينِكُمْ وَظَهَرُوا عَلَىٰ إِخْرَاجِكُمْ أَنْ تَوَلَّوهُمْ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anakukatazeni kufanya urafiki na wale waliokupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu.” (60:9)

Inamaanisha, ‘Allah تعالى Anakukatazeni kuwafanyia wema na kuwafanyia urafiki makafiri wenye uhasama wa wazi kwenu, wenye kukupigeni vita, waliokufukuzeni na waliosaidia kufukuzwa kwenu. Allah تعالى Anakukatazeni dhidi ya kuwafanyia urafiki Anakuamrisheni muwe adui Kwao.’ kisha Allah تعالى Anasisitizia kitisho Chake dhidi ya kuwafanyia urafiki, kwa kusema,

وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

“Na wanao wafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu.”

¹ Angalia juzuu ya tisa, *Tafsir ya Surat Al-Hujurat* (49:9).

² Muslim 3:1458.

Kama Alivyosema;

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ ۚ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنكُمْ فَإِنَّهُ مِنَّهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٥١﴾

“...Enyi mliaoamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wenye kudhulumu.” (5:51)

* * *

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا جَاءَكُمْ الْمُؤْمِنَاتُ مُهَاجِرَاتٍ
فَأَمْتَحِنُوهُنَّ ۗ اللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِهِنَّ ۗ فَإِنْ عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ
فَلَا تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ ۗ لَا هُنَّ حِلٌّ لَهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ
لَهُنَّ ۗ وَءَاتُوهُنَّ مَّا أَنفَقُوا ۗ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ أَنْ تَنكِحُوهُنَّ
إِذَا ءَاتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ ۗ وَلَا تُمْسِكُوا بِعِصَمِ الْكَوَافِرِ
وَسَئَلُوا مَّا أَنفَقْتُمْ وَلَيْسَ لَكُم مَّا أَنفَقُوا ۗ ذَٰلِكُمْ حُكْمُ اللَّهِ
فِي حُكْمِ بَيْنِكُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾ وَإِنْ فَاتَكُمْ شَيْءٌ مِّنْ
أَزْوَاجِكُمْ إِلَى الْكُفَّارِ فَعَاقِبْتُمْ فَاتُوا الَّذِينَ ۗ ذَهَبَتْ
أَزْوَاجُهُمْ مِّثْلَ مَّا أَنفَقُوا ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَنْتُمْ بِهِ
مُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾ يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعُكَ
عَلَىٰ أَنْ لَا يُفْرِكْنَ بِاللَّهِ شَيْئًا وَلَا يَسْرِقْنَ وَلَا يَزْنِينَ وَلَا
يَقْتُلْنَ أَوْلَادَهُنَّ وَلَا يَأْتِينَ بِبُهْتَانٍ يَفْتَرِينَهُ بَيْنَ أَيْدِيهِنَّ
وَأَرْجُلِهِنَّ ۗ وَلَا يَعْصِيَنَّكَ فِي مَعْرُوفٍ فَبَايِعْنَهُنَّ وَأَسْتَغْفِرْ
لَهُنَّ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا
تَتَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ قَدْ يَسُؤُوا مِنَ الْآخِرَةِ كَمَا
يَسِئَ الْكُفَّارُ مِنَ أَصْحَابِ الْقُبُورِ ﴿١٣﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا جَاءَكُمْ
الْمُؤْمِنَاتُ مُهَاجِرَاتٍ فَأَمْتَحِنُوهُنَّ
اللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِهِنَّ ۗ فَإِنْ
عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ فَلَا
تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ ۗ لَا هُنَّ
حِلٌّ لَهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ
وَوَاتُوهُنَّ مَّا أَنفَقُوا ۗ وَلَا جُنَاحَ
عَلَيْكُمْ أَنْ تَنكِحُوهُنَّ إِذَا
ءَاتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ ۗ وَلَا
تُمْسِكُوا بِعِصَمِ الْكَوَافِرِ وَسَئَلُوا مَّا
أَنفَقْتُمْ وَلَيْسَ لَكُم مَّا أَنفَقُوا ۗ ذَٰلِكُمْ
حُكْمُ اللَّهِ ۗ حُكْمُ بَيْنِكُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ
حَكِيمٌ ﴿١٠﴾ وَإِنْ فَاتَكُمْ شَيْءٌ مِّنْ
أَزْوَاجِكُمْ إِلَى الْكُفَّارِ فَعَاقِبْتُمْ
فَاتُوا الَّذِينَ ۗ ذَهَبَتْ
أَزْوَاجُهُمْ مِّثْلَ مَّا أَنفَقُوا ۗ وَاتَّقُوا
اللَّهَ الَّذِي أَنْتُمْ بِهِ
مُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾ يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا
جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعُكَ
عَلَىٰ أَنْ لَا يُفْرِكْنَ بِاللَّهِ شَيْئًا وَلَا
يَسْرِقْنَ وَلَا يَزْنِينَ وَلَا يَقْتُلْنَ
أَوْلَادَهُنَّ وَلَا يَأْتِينَ بِبُهْتَانٍ
يَفْتَرِينَهُ بَيْنَ أَيْدِيهِنَّ
وَأَرْجُلِهِنَّ ۗ وَلَا يَعْصِيَنَّكَ فِي
مَعْرُوفٍ فَبَايِعْنَهُنَّ وَأَسْتَغْفِرْ
لَهُنَّ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾
يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا
تَتَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ
قَدْ يَسُؤُوا مِنَ الْآخِرَةِ كَمَا
يَسِئَ الْكُفَّارُ مِنَ أَصْحَابِ الْقُبُورِ ﴿١٣﴾

10. Enyi mliaoamini! Wakikujilieni wanawake Waumini waliohama, basi wafanyieni mtihani - Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujua zaidi Imani yao. Mkiwa mnawajua kuwa ni Waumini basi msiwarudishe kwa makafiri.

Wanawake hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalalikii wanawake Waumini. Na wapeni hao wanaume mahari waliotoa. Wala hapana makosa kwenu kuwaoa mkiwapa mahari yao. Wala msiwaweke wanawake makafiri katika kifungo cha ndoa zenu. Na takeni mlichokitoa, na wao watake walichokitoa. Hiyo ndiyo hukumu ya Mwenyezi Mungu Anayokuhukumuni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Hikima.

11. Na akitoroka yeyote katika wake zenu kwenda kwa makafiri, tena ikatokea mkapata ngawira, basi wapeni waliokimbiwa na wake zao kiasi cha mahari waliyoyatoa. Na mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye mnamuamini.

Baada ya Al-Hudaybiyyah, Wanawake Muhajirina Wasirejeshwe kwa Makafiri

Suratu *Al-Fat-h*,¹ tumesimulia kisa cha mkataba wa Al-Hudaybiyah baina ya Mtume ﷺ na makafiri wa Kikuraishi. Katika mkataba huo, kulikuwa na kipengele hiki: “Yeyote katika Waislamu anayehama kutoka kwetu Makkah na kuja kwenu Madina, arudishwe kwetu, hata kama ni mfuasi wa dini yako.” Hayo yalisemwa na ‘Urwah, Adh-Dhahhak, ‘Abdur-Rahman bin Zayd, Az-Zuhri, Muqatil bin Hayyan na As-Suddi. Hivyo kwa mujibu wa masimulizi haya, Ayah hii inaainisha hukumu iliyoenezwa kwa ujumla katika *Sunnah*. Huu ni ufafanuzi mzuri na kwa mujibu wa rai nyingine ya baadhi ya *Salaf*, inaifuta hukumu iliyokuja katika Hadithi. Allah Mtukuka Aliwaamuru waumini waipime imani ya wanawake waliohamia kwao. Walipohakikisha imani yao, hawakupaswa kuwarejesha kwa makafiri, kwani makafiri hawakuwa halali kwao, wala wao hawakuwa halali kwa makafiri. Katika wasifu wa ‘Abdullah bin Abi Ahmad bin Jahsh katika Al-Musnad Al-Kabir, pia kumetajwa kuwa ‘Abdullah bin Abi Ahmad amesema, “Umm Kulthum bint ‘Uqbah bin Abi Mu`ayt alifanya hijira pamoja na nduguze, ‘Umarah na Al-Walid, walimfuata. Akamuendea Mtume ﷺ na

¹ Angalia mwanzoni mwa *Surat Al-Fath* (48) katika juzu ya tisa.

kumueleza kuhusu Umm Kulthum na kumuomba amrudishe kwao. Allah تعالی Alifuta sehemu ya mkataba huo baina ya Mtume ﷺ na washirikina kuhusu suala la wanawake. Kwa hivyo Alikataza wanawake Waislamu wasirejeshwe kwenda kwa washirikina na Akateremsha Ayah kuhusu kuwapima.”¹ Al-'Awfi amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, kuhusu Kauli ya Allah تعالی:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا جَاءَكُمْ الْمُؤْمِنَاتُ مُهَجِرَاتٍ فَامْتَحِنُوهُنَّ^ط

“Enyi mlioamini! Wakikujilieni wanawake Waumini waliohama, basi wafanyieni mtihani.”

“Kuwatchini kwao kulikuwa kuwataka watoe shahada ya *La ilaha illallah*, na kuwa Muhammad ﷺ ni mja wa Allah na Mjumbe Wake.” Mujahid ameeleza Aya,

فَامْتَحِنُوهُنَّ^ط

“...basi wafanyieni mtihani...”

Kwa kusema, “Waulizeni kwa nini wamehama. Kama wamekuja kwa sababu walikuwa na hasira kwa waume wao, au kwa sababu nyingine yoyote, na mkagundua kuwa hawakuwa na imani, basi warudisheni kwa waume wao.”²

Kauli ya Allah تعالی,

فَإِنْ عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ فَلَا تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ^ط

“Mkiwa mnawajua kuwa ni Waumini basi msiwarudishe kwa makafiri.”

Aya hii inaashiria kuwa imani inaweza kutambulika na kuthibitishwa.

¹ *Jamu' Al-Masanid* 7:243. Masimulizi haya ni *Mursal* na sehemu yake kubwa ipo katika Al-Bukhari, na 4180-1.

² At-Tabari 23:326.

Mwanamke Muumini Amekatazwa Kuolewa na Mshirikina, na Mwanaume Muumini Anakatazwa Kumuoia Mwanamke Mshirikina

Kauli ya Allah تعالى،

لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهَا

“Wanawake hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalaliki...”

Aya hii inawakataza wanawake Waislamu kuolewa na washirikina, ambapo ilikuwa ndoa halali mwanzoni mwa Uislamu. Abu Al-’As bin ar-Rabi’ alimuoa Zaynab رضي الله عنها، binti wa Mtume ﷺ ambaye alikuwa Muislamu, ilhali Abu Al-’As alikuwa bado mshirikina kama watu wake. Alipokamatwa mateka katika vita vya Badr, mkewe, Zaynab رضي الله عنها، alipeleka kitu cha kumkombolea, kidani kilichokuwa cha mama yake, mke wa Mtume ﷺ, Khadijah رضي الله عنها. Mtume ﷺ alishtuka alipokiona kidani hicho na akawaambia Masahaba،

«إِنْ رَأَيْتُمْ أَنْ تُوَلِّتُوا لَهَا أُسْبِرَ مَا فَافَعَلُوا»

“Kama mtaamua kumuachilia huru mateka wake, fanyeni hivyo.”

Wakafanya hivyo, na Mtume ﷺ akamuachilia huru. Kwa masharti ya kumpeleka binti yake kwa Mtume. Abu Al-’As alitekeleza ahadi yake na akamtuma Zaynab رضي الله عنها kwa Mjumbe wa Allah ﷻ pamoja na Zayd bin Harithah رضي الله عنه.¹ Zaynab رضي الله عنها alibakia Al-Madinah baada ya vita vya Badr, vilivyofanyika katika mwaka wa pili wa Hijrah, mpaka mumewe Abu Al-’As bin ar-Rahi’ aliposilimu katika mwaka wa nane baada ya Hijrah.² Wakarejea katika ndoa yao bila ya kutolewa mahari nyingine. Kauli ya Allah تعالى،

وَأَتَوْهُم مَّا أَنْفَقُوا

“...Na wapeni hao wanaume mahari waliotoa.”

Inamaanisha, waume wa wanawake waliohama kutoka kwa washirikina, warejesheeni mahari waliyowapa wake zao. Hayo yalisemwa na Ibn ‘Abbas, Mujahid, Qatadah, Az-Zuhri na wengine kadhaa رضي الله عنهم.³

¹ Abu Dawud 3:140

² Kilicho sahihi ni kuwa, ilikuwa miaka sita kabla ya Al-Hudaybiyyah, kabla Aya hii haijashuka.

³ At-Tabari 23:329

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ أَنْ تَنْكِحُوهُنَّ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ

“Wala hapana makosa kwenu kuwaoa mkiwapa mahari yao.”

Inamaanisha mnaotaka kuwaoa, basi wapeni mahari yao. yaani, kuwaoa sharti ya kwisha eda. Na awepo msimamizi wa ndoa (walii) n.k. kisheria kuhusu ndoa zao n.k. Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا تُمْسِكُوا بِعَصَمِ الْكُوفِرِ

“Wala msiwaweke wanawake makafiri katika kifungo cha ndoa zenu.”

Haya ni makatazo ya Allah تعالى kwa waumini kuwaoa wanawake washirikina au kuwabakisha kwenye ndoa. Katika Sahih, kumenukuliwa kutoka kwa Al-Miswar na Marwan bin al-Hakam walisema kuwa baada ya Mtume ﷺ kuwekeana mkataba na Washirikina wa Kikuraishi huko Al-Hudaybiyyah, baadhi ya wanawake Waislamu walihamia kwake na Allah تعالى Akateremsha Aya hii juu yao،

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا جَاءَكُمْ الْمُؤْمِنَاتُ مَهْجِرَاتٍ

“Enyi mlioamini! Wakikujilieni wanawake Waumini waliohama.”
mpaka،

وَلَا تُمْسِكُوا بِعَصَمِ الْكُوفِرِ

“Wala msiwaweke wanawake makafiri katika kifungo cha ndoa zenu...”

‘Umar bin al-Khattab رضي الله عنه akawapa talaka wakeze wawili, waliokuwa washirikina, na mmoja wao aliolewa na Mu`awiyah bin Abi Sufyan, ilhali mwingine aliolewa na Safwan bin Umayyah.¹

¹ Fat’h Al-Bari 5:391.

Ibn Thawr amesimulia kuwa Ma'mar amesema kuwa Az-Zuhri amesema, "Aya hii ilishuka kwa Mtume ﷺ alipokuwa katika eneo la Al-Hudaybiyyah, baada ya kuwekeana mkataba wa amani. Alikubali kuwa aliyekuja kutoka kwa Makuraishi kwenda upande wake, arejeshwe Makkah. Baadhi ya wanawake walipokuja, Aya hii ilishuka. Allah تعالى Aliamuru kuwa mahari waliyolipwa wanawake hao irejeshwe kwa waume wao. Allah تعالى pia Aliamrisha kuwa ikiwa baadhi ya wanawake wa Kislamu walikimbilia upande wa washirikina, basi washirikina warejeshe mahari kwa waume zao Waislamu.

Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تُمْسِكُوا بِعِصَمِ الْكُوفِرِ

"Wala msiwaweke wanawake makafiri katika kifungo cha ndoa zenu..."

Kauli ya Allah تعالى,

وَسْأَلُوا مَا أَنْفَقْتُمْ وَلَيْسَ لَكُمْ مَا أَنْفَقُوا

"Na takeni mlichio kitoa, na wao watake walicho kitoa."

Maana yake: Waulizeni mlichowalipa wake zenu waliokimbilia kwa washirikina, na wao wanapaswa kurejesha mahari waliyolipwa wake zao waliohamia kwa Waislamu. Kauli ya Allah تعالى,

ذَلِكَمُ حُكْمُ اللَّهِ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ

"Hiyo ndiyo hukumu ya Mwenyezi Mungu Anayo kuhukumuni."

Maana yake: Hukumu hii kuhusu mkataba na kutowajumuisha wanawake katika vipengele vya mkataba, ni uamuzi Alioufanya Allah تعالى kwa ajili ya viumbe Wake,

وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

"Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Hikima."

Maana yake: Anajua chenye Kuwanufaisha Waja Wake naye ni Mwingi wa Hekima kuhusu hilo. Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 23:329, angalia sehemu inayohusu masimulizi mwanzoni mwa kitabu hiki.

وَإِنْ فَاتَكُمْ شَيْءٌ مِّنْ أَزْوَاجِكُمْ إِلَى الْكُفَّارِ فَعَاقِبْتُمْ فَاتُوا الَّذِينَ ذَهَبَتْ أَزْوَاجُهُمْ مِّثْلَ مَا أَنْفَقُوا^١

“Na akitoroka yeyote katika wake zenu kwenda kwa makafiri, tena ikatokea mkapata ngawira, basi wapeni waliokimbiwa na wake zao kiasi cha mahari waliyoyatoa...”

Mujahid na Qatadah wameeleza kuhusu Aya hii, kwa kusema, “Inawahusu makafiri ambao hawakuwa na mkataba wa amani. Ikiwa mwanamke atakimbilia kwa makafiri na wasirejeshe alichomlipa mumewe, basi kama mwanamke anakuja kwao (Waislamu) wasimrejeshee mumewe chochote mpaka kwanza wamlipe Muislamu ambaye mkewe amekwenda upande wao kiasi kilicho sawa na alichotoa.”¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Az-Zuhri amesema, “Waumini walifuata amri ya Allah تعالى na kulipa walichodaiwa na washirikina ili kufidia mahari waliyotoa washirikina kuwapa wanawake (waliohama). Hata hivyo, washirikina hawakukubali hukumu ya Allah تعالى kutoa mahari ya Waislamu. Kauli ya Allah تعالى kwa waumini,

وَإِنْ فَاتَكُمْ شَيْءٌ مِّنْ أَزْوَاجِكُمْ إِلَى الْكُفَّارِ فَعَاقِبْتُمْ فَاتُوا الَّذِينَ ذَهَبَتْ أَزْوَاجُهُمْ مِّثْلَ مَا أَنْفَقُوا^١ وَأَتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَنْتُمْ بِهِ مُؤْمِنُونَ ﴿١٠﴾

“Na akitoroka yeyote katika wake zenu kwenda kwa makafiri, tena ikatokea mkapata ngawira, basi wapeni waliokimbiwa na wake zao kiasi cha mahari waliyoyatoa. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye mnamuamini.”

Kwa hivyo, baada ya kushuka aya hii, ikiwa mwanamke Muislamu atakimbilia kwa washirikina, waumini watapaswa warudishe mahari ya mumewe Muislamu aliyomlipa, kutokana na mali waliyoipata ambayo waliamrishwa kuwarejeshea waume wa washirikina. Katika mali yao waliyoitoa kuwapa wanawake hawa walioamini na kuhama, na kisha watawarudishia wanaume washirikina

¹ At-Tabari 23:338.

kilichobaki kama wanacho katika mahari ya wanawake makafiri pale walipoamini na kumfuata Mtume ﷺ Madina.”¹

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعُنَكَ عَلَىٰ أَنْ لَا يُنْفِرْنَ بِإِلَهِ شَيْعًا وَلَا يَسْرِقْنَ وَلَا
يَزْنِينَ وَلَا يَقْتُلْنَ أَوْلَادَهُنَّ وَلَا يَأْتِينَ بِبُهْتَانٍ يَفْتَرِينَهُ بَيْنَ أَيْدِيهِنَّ وَأَرْجُلِهِنَّ وَلَا
يَعْصِيَنَّكَ فِي مَعْرُوفٍ فَبَايِعُهُنَّ وَاسْتَعْفِفْنَ هُنَّ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٠﴾

12. Ewe Nabii! Watakapokujia wanawake Waumini wanakuahidi ya kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawaua watoto wao, wala hawataleta uzushi wanaouzua tu wenyewe baina ya mikono yao na miguu yao, wala hawatakuasi katika jambo jema, basi peana nao ahadi, na uwatakie maghfira kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira, Mwenye Kurehemu.

Mambo Ambayo Wanawake Waliyawekea Ahadi ya Utii

Al-Bukhari amenukuu kuwa ‘A’ishah رضي الله عنها. mke wa Mtume ﷺ amesema, “Mtume ﷺ alikuwa akiwachunguza wanawake waliohamia upande wake kwa mujibu wa Aya hii,

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعُنَكَ

“Ewe Nabii! Watakapo kujia wanawake Waumini wanakuahidi...”

mpaka,

إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira, Mwenye Kurehemu.”

‘Urwah amesema, “ A’ishah رضي الله عنها amesema, “Mwanamke yeyote muumini alipokubali masharti hayo, Mtume ﷺ alikuwa akimuambia,

¹ At-Tabari 23:337.

«قَدْ بَايَعْتُكَ»

“Nimepokea ahadi yako ya utii.”

Lakini, Wallahi, kamwe hakugusa mkono wa mwanamke yeyote wakati alipokuwa akichukua ahadi zao za utii. Alipokea ahadi zao za utii kwa kusema,

«قَدْ بَايَعْتُكَ عَلَى ذَلِكَ»

“Nimepokea ahadi yako ya utii juu ya hayo.”¹

Hayo ni maneno ya Al-Bukhari. Imamu Ahmad amenukuu kuwa Umaymah bint Ruqayyah رضي الله عنها amesema, “Nilikwenda kwa Mtume ﷺ nikifuatana na baadhi wanawake ili kumpa ahadi ya utii na akachukua ahadi zetu kama ilivyoelezwa katika Qur’an, kuwa tusimshirikishe Allah تعالى, n.k; kama katika Aya hiyo. Akasema,

«فِيمَا اسْتَطَعْتُنَّ وَأَطَقْتُنَّ»

“Kadiri ya unavyoweza kustahamili kutekeleza.”

Tukasema, ‘Kwa hakika, Allah تعالى na Mjumbe Wake wana huruma kwetu zaidi kuliko sisi tulivyo katika nafsi zetu.’ Tukasema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah, hutashikana nasi mikono?’ Amesema,

«إِنِّي لَا أَصَافِحُ النِّسَاءَ، إِنَّمَا قَوْلِي لِمَرْأَةٍ وَاحِدَةٍ كَقَوْلِي لِمِائَةِ امْرَأَةٍ»

“Hakika mimi sishiki mikono ya wanawake, kwani kauli yangu kwa mwanamke mmoja ni kama kauli yangu kwa wanawake mia.”²

Hadith hii ina isnadi sahihi ya usimulizi; At-Tirmidhi, An-Nasa’i na Ibn Majah waliikusanya.³ Al-Bukhari pia amenukuu kuwa Umm ‘Atiyah رضي الله عنها alisema, “Mtume ﷺ alichukua ahadi zetu za utii na kutusomea Aya,

«أَنْ لَا يُشْرِكَنَّ بِاللَّهِ شَيْئًا»

“...kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote...”

¹ Fat’h Al-Bari 8:504.

² Ahmad 6:367.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 5:220 na An-Nasai 7:149, An-Nasai katika Al-Kubra 6:488 na Ibn Majah 2:959.

na akatukataza kuomboleza maiti. Baada ya hapo, (mwanamke) alinyoosha mkono na kusema, 'Lakini mwanamke fulani alishirikiana nami katika kuomboleza (kifo cha jamaa yangu)), hivyo lazima nimlipe.' Mtume ﷺ hakumkatalia hilo, hivyo alikwenda huko na kurejea kwa Mtume ﷺ na akapokea ahadi yake ya utii."¹

Muslim pia aliikusanya Hadithi hii.² Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'Ubadah bin as-Samit رضي الله عنه, "Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ, aliposema,

«تَبَايَعُونِي عَلَى أَنْ لَا تُشْرِكُوا بِاللَّهِ شَيْئًا، وَلَا تَسْرِقُوا، وَلَا تَزْنُوا، وَلَا تَقْتُلُوا
أَوْلَادَكُمْ»

"Nipeni ahadi kuwa hamtamshirikisha Allah, wala kuiba, wala kuzini, wala kuwaua watoto wenu."

Akasoma Aya inayoanzia;

إِذَا جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ

"Watakapokujia wanawake Waumini..."

Na alichukua ahadi ya utii kutoka kwa wanawake. Akaongeza,

«فَمَنْ وَفَى بِكُمْ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ، وَمَنْ أَصَابَ مِنْ ذَلِكَ شَيْئًا فَعَرُوبَ بِهِ فَهُوَ كَفَّارَةٌ
لَهُ، وَمَنْ أَصَابَ مِنْ ذَلِكَ شَيْئًا فَسْتَرَهُ اللَّهُ عَلَيْهِ فَهُوَ إِلَى اللَّهِ، إِنْ شَاءَ غَفَرَ لَهُ، وَإِنْ
شَاءَ عَذَّبَهُ»

"Atakaetimiza ahadi hii ya utii miongoni mwenu, atapata malipo kutoka kwa Allah. Atakayekiuka chochote katika ahadi hiyo ataadhibiwa (duniani), adhabu itakuwa kwa ajili ya kuwafutia dhambi. Mwenye kukiuka chochote katika ahadi hiyo na Allah akamsitiri, basi ni juu ya Allah Kumuadhibu au Kumsamehe Akitaka."³ Sahihi Mbili zimenukuu Hadithi hii.⁴

¹ Fat'h Al-Bari 8:506.

² Muslim 2:646.

³ Ahmad 5:314.

⁴ Fat'h Al-Bari 8:506 na Muslim 3:1333.

Kauli ya Allah تعالى،

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعَنَّكَ

“Ewe Nabii! Watakapo kujia wanawake Waumini wanakuahidi...”

Inamaanisha, ‘kama mwanamke yeyote atakujia ili kukupa ahadi ya utii na akakubali masharti hayo, basi pokea ahadi ya utii kutoka kwake,’

عَلَىٰ أَنْ لَا يُشْرِكَنَّ بِاللَّهِ شَيْئًا وَلَا يَسْرِقَنَّ

“...kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba...”

Inamaanisha, mali ya watu wengine. Katika hali ambayo mume hatimizi wajibu wake wa kumtunza mkewe, basi mke huyo anaruhusiwa kutumia sehemu ya mali ya mumewe kwa wema, inayofaa kumpa mwanamke huyo matunzo. Hii huwa hivyo bila ya kujali kama Mume anajua kuhusu matendo ya mkewe au hapana, kutokana na ushahidi wa Hadithi ambapo Hind bint ‘Utbah رضي الله عنها alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Abu Sufyan ni mbahili! Hanipi matumizi ya kimaisha kwa ajili ya familia yetu na mimi mwenyewe. Je, ninaruhusiwa kuchukua kisiri mali yake bila ya yeye kujua.” Mtume ﷺ akamuambia,

«خُذِي مِنْ مَالِهِ بِالْمَعْرُوفِ، مَا يَكْفِيكَ وَيَكْفِي بَيْنِكَ»

“Chukua kiasi katika mali yake kinachokutosha na kutosha watoto wako.”¹

Hadithi hii imenukuliwa katika Sahihi Mbili. Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا يَزِينَنَّ

“...wala hawatazini...”

Ni sawa na Kauli Yake،

وَلَا تَقْرُبُوا الزَّيْنَىٰ إِنَّهُ كَانَ فَجِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

“Wala msikaribie uzinzi. Hakika huo ni uchafu na njia mbaya.” (17:32)

¹ Fath Al-Bari 13:183 ma Muslim 3:1338.

Hadith iliyokusanywa kutoka kwa Samurah inataja kuwa wazunifu wana adhabu iumizayo katika moto wa Jahanamu.¹

Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'A'ishah رضي الله عنها amesema, "Fatimah bint `Utbah رضي الله عنها alikuja kumpa ahadi ya utii Mtume ﷺ, ambaye alipokea ahadi ya utii kutoka kwake,

أَنْ لَا يُشْرِكَنَّ بِاللَّهِ شَيْئًا وَلَا يَسْرِقَنَّ وَلَا يَزْنِينَ

“...kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini...”

Fatimah رضي الله عنها kwa aibu aliweka mkono wake kichwani kwake. Mtume ﷺ akapendezwa na kitendo chake hicho." A'ishah رضي الله عنها akasema, "Ewe mwanamke! Pokea ahadi ya utii, kwa sababu wallahi, sote sisi tunampa ahadi ya utii juu ya hayo hayo." Akasema, 'Ndiyo.' Na akatoa ahadi ya utii juu ya mambo hayo yaliyotajwa katika Aya."² Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا يَقْتُلَنَّ أَوْلَادَهُنَّ

“...hawatawauwa watoto wao...”

Inajumuisha kuua watoto baada ya kuzaliwa. Watu wa *Jahiliyyah* walikuwa wakiwaua watoto wao kwa sababu waliogopa umaskini. Aya inajumuisha suala la kuua kijusi, kama baadhi ya wanawake wajinga wanavyofanya kwa sababu mbalimbali. Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا يَأْتِينَ بِيْهْتِنٍ يَفْتَرِينَهُ بَيْنَ أَيْدِيْهِنَّ وَأَرْجُلِهِنَّ

“...hawataleta uzushi wanaouzua tu wenyewe baina ya mikono yao na miguu yao.”

Ibn ' Abbas رضي الله عنهما amesema, "Inamaanisha kuwa hawanasibishi waume wao isipokuwa watoto wao wa halali." Muqatil amesema sawa na hivyo.³ Kauli ya Allah تعالى,

¹ Ahmad 5:9.

² Ahmad 6:151.

³ At-Tabari 23:340.

وَلَا يَعْصِيَنَّكَ فِي مَعْرُوفٍ¹

“...wala hawatakuasi katika jambo jema...”

Maana yake: ‘Kuwa watakutii utakapowaamuru kufanya wema na kuwakataza ovu.’ Al-Bukhari amenukuu kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا يَعْصِيَنَّكَ فِي مَعْرُوفٍ²

“...wala hawatakuasi katika jambo jema...”

“Hili lilikuwa sharti Aliloweka Allah تعالى juu ya wanawake.”¹ Maymun bin Mihran amesema, “Allah تعالى Hakuamrisha kumtii Mtume Wake kwa ajili ya jingine isipokuwa *Ma`ruf*, na *Ma`ruf* yenyewe ni utii.”² Ibn Zayd amesema, “Allah تعالى Aliamrisha kumtii Mjumbe Wake, mbora wa Viumbe Wake, na hilo ni *Ma`ruf*.”³

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Umm ‘Atiyah Al-Ansariyah رضي الله عنها amesema, “Miongoni mwa masharti yaliyokuwepo katika ahadi yetu ya utii kwa Mtume ﷺ ilikuwa kutokuomboleza. Mwanamke mmoja akasema, ‘Familia fulani ilinifariji kwa kumuomboleza maiti wangu, basi kwanza nitawalipa.’ Akaenda kuwalipa kwa hilo, akaja kuweka ahadi yake ya utii. Yeye tu, na Umm Sulaym bint Milhan رضي الله عنها, mama wa Anas bin Malik, walifanya hivyo.”⁴ Al-Bukhari alikusanya Hadithi hii kutoka kwa njia ya Hafsa bint Sirin رضي الله عنها kutoka kwa Umm ‘Atiyah Nusaybah Al-Ansariyah رضي الله عنها, Allah تعالى Awe radhi kwake.⁵

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Usaid bin Abi Usaid Al-Barrad amesema kuwa mwanamke mmoja aliyeweka ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ alisema, “Miongoni mwa masharti yaliyokuwemo katika ahadi ya utii kwa Mtume ﷺ tuliyopewa, ni kuwa tusiasi kitendo chochote cha *Ma`ruf* (wema) kama alivyoamuru. Tusikwaruze nyuso zetu, kung’oa nywele zetu (kwa huzuni), kurarua nguo zetu wala kuomboleza, kwa kulalama wakati wa msiba.”

¹ *Fat’h Al-Bari* 8:506.

² Al-Qurtubi 18:73.

³ At-Tabari 23:345.

⁴ At-Tabari 23:346.

⁵ Al-Bukhari 4892.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ قَدْ يَئِسُوا مِنَ الْآخِرَةِ كَمَا يَئِسَ
 الْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَابِ الْقُبُورِ ﴿١٣﴾

13. Enyi mlioamini! Msiwafanye rafiki zenu watu ambao Mwenyezi Mungu Amewakasirikia. Hao wamekwisha kata tamaa ya Akhera, kama makafiri walivyowakatia tamaa watu wa makaburini.

Kama mwanzoni mwa surah, Allah تعالى Anakataza kuwafanya makafiri kama marafiki wa kuwahifadhi, mwishoni mwa surah, Anasema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ

“Enyi mlioamini! Msiwafanye rafiki zenu watu ambao Mwenyezi Mungu Amewakasirikia.”

Inamaanisha Wayahudi, Wakristo na makafiri wengine ambao Allah تعالى Amewakasirikia na wamelaaniwa. Wanaopaswa kukataliwa na kufukuzwa na Allah تعالى. (Allah تعالى Anasema hapa), ‘mnawezaje kuwa washirika wao, marafiki na wenza, baada ya Allah تعالى kuamua kuwa wanapaswa kukata tamaa ya kupata jema au furaha yoyote huko Akhera.’

Kauli ya Allah تعالى,

كَمَا يَئِسَ الْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَابِ الْقُبُورِ

“...kama makafiri walivyowakatia tamaa watu wa makaburini.”

Hii inaweza kuwa na maana mbili. Mosi, makafiri wanakata tamaa ya kuonana na ndugu zao waliozikwa makaburini, kwasababu hawaamini Kiama au kufufuliwa. Kwa hiyo, hawana matumaini kuwa watakutana nao tena, kwa mujibu wa itikadi yao. Pili, kama makafiri waliozikwa makaburini hawana matumaini ya kupata jema lolote (yaani, baada ya kuona adhabu na kujua kuwa Ufufuo ni kweli). Al-A'mash amesimulia kutoka kwa Abu Ad-Dhuha kutoka kwa Masruq kuwa Ibn Mas'ud عنهما رضي الله عنهمamesema,

كَمَا يَئِسَ الْكُفَّارُ مِنْ أَصْحَابِ الْقُبُورِ

“...kama makafiri walivyowakatia tamaa watu wa makaburini.”

“Kama kafiri anakata tamaa wakati anapofariki na anatambua na kujua jaza yake (mbaya).” Hii ni kauli ya Mujahid, ‘Ikrimah, Muqatil, Ibn Zayd, Al-Kalbi na Mansur,¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى amechagua maelezo haya.²

Huu ni mwisho wa *Tafsiriya Surat Al-Mumtahanah*, kila sfa njema Anastahiki Allah تعالى.



¹ At-Tabari 23:348.

² At-Tabari 23:348.

Tafsiri ya Suratu As-Saff

Sura ya 61

Iliteremshwa Madinah

Fadhila za *Suratu As-Saff*

Imamu Ahmad amenukuu kuwa ‘Abdullah bin Salam رضي الله عنه amesema, “Tuliuliza, `Ni nani kati yetu aende kwa Mtume ﷺ na kumuuliza kuhusu amali Anazozipenda zaidi Allah تعالي.’ Hakuna miongoni mwetu aliyejitolea. Mtume ﷺ alimtuma mtu kuja kutuita na akatusomea Surah hii, *Suratu As-Saff*, yote.”¹



¹ Ahmad 5:452.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الصَّفِّ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ
 الْحَكِيمُ ﴿١﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا
 تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا لَا
 تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الَّذِينَ يُقِيمُونَ فِي
 سَبِيلِهِ صَفًّا كَانَهُم بِئِنَّ مَرْضُوصٍ ﴿٤﴾ وَإِذْ قَالَ
 مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يَنْقُورِ لِمَ تُوذُونِي وَقَدْ تَعْلَمُونَ أَنِّي
 رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ ۗ فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاغَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا
 يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٥﴾ وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ
 يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ
 مِنَ التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدُ
 فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُبِينٌ ﴿٦﴾

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي
 الْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١﴾
 يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ
 مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقْتًا
 عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا لَا
 تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ
 الَّذِينَ يُقِيمُونَ فِي سَبِيلِهِ
 صَفًّا كَانَهُم بِئِنَّ مَرْضُوصٍ ﴿٤﴾

1. Vinamtakasa Mwenyezi Mungu viliomo katika mbingu na katika ardhi. Na Yeye ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.

2. Enyi mlioamini! Kwa nini mnasema msiyoyatenda?

3. Yanachukiza vikubwa mno kwa Mwenyezi

Mungu kuwa mnasema msiyoyatenda.

4. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wanaopigana katika Njia Yake kwa safu kama jengo liliokamatana.

Karipio kwa Wanaosema Wasiyoyatenda

Tumeshaeleza katika sehemu nyingi maana ya Kauli ya Allah تعالى،

سَبِّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٠١﴾

“Vinamtakasa Mwenyezi Mungu viliomo katika mbingu na katika ardhi. Na Yeye ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Kwa hiyo, hatuna haja ya kurudia maana yake hapa.¹ Kauli ya Allah تعالى،

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا لِمَ تَقُوْلُوْنَ مَا لَا تَفْعَلُوْنَ ﴿١٠٢﴾

“Enyi mlioamini! Kwa nini mnasema msiyoyatenda?”

Inawakanusha wanaokataa kutimiza ahadi zao. Ayah hii tukufu inaunga mkono mtazamo wa wanazuoni wengi wa *Salaf*, kuwa ni lazima kutimiza ahadi, bila ya kujali kama ahadi hiyo itagharimu hali na mali. Kadhalika wametoa ushahidi kupitia Sunna, kwa mujibu wa Hadithi iliyoandikwa katika Sahihi Mbili ambayo Mtume ﷺ amesema,

«آيَةُ الْمُتَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا أُؤْتِمِنَ خَانَ»

*“Alama za mnafiki ni tatu: anapoahidi, huvunja ahadi yake, anapozungumza, hudanganya; na anapoaminiwa, husaliti.”*²

Na katika Hadithi nyingine katika Sahih,

«أَرْبَعٌ مَنْ كُنَّ فِيهِ كَانَ مُنَافِقًا خَالِصًا، وَمَنْ كَانَ فِيهِ وَاحِدَةٌ مِنْهُنَّ كَانَتْ فِيهِ حَضَلَةٌ
مِنْ بَغَايٍ حَتَّى يَدْعَهَا»

*“Kuna sifa nne ambazo mtu akiwa nazo, basi huyo ni mnafiki, na kama ana mojawapo, anakuwa na sifa moja ya unafiki, mpaka atakapoiacha.”*³

¹ Angalia juzu ya tisa, *Tafsir ya Surat Al-Hadid* (57:1).

² *Fath Al-Bari* 1:111 na *Muslim* 1:78.

³ *Fath Al-Bari* 1:111.

Kwa hivyo, ametaja kuwa kuvunja ahadi ni katika sifa hizo nne. Tumetaja maana ya Hadithi hizi mbili mwanzoni mwa maelezo ya Sahih Al-Bukhari, na Allah تعالی Ndiye Anayestahiki Sifa na Shukrani. Kwa hiyo Allah تعالی Amedokeza maana hiyo, Alipoendeleza maonyo Yake kwa Kusema,

كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٦١﴾

“Yanachukiza vikubwa mno kwa Mwenyezi Mungu kuwa mnasema msiyoyatenda.”

Imamu Ahmad na Abu Dawud amenukuu kuwa ‘Abdullah bin ‘Amir bin Rabi` ah رضي الله عنه amesema, “Mtume ﷺ alitujia nilipokuwa bado kijana, na nikatoka nje kucheza. Mama yangu akaniambia, ‘Ewe ‘Abdullah! Njoo, ninataka kukupa kitu.’ Mtume ﷺ akaniambia,

«وَمَا أَرَدْتُ أَنْ تُعْطِيَهُ؟»

“Unataka kumpa nini?”

Akasema, ‘Tende.’ Akasema,

«أَمَّا إِنَّكَ لَوَ لَمْ تَفْعَلِي كُتِبَتْ عَلَيْكَ كَذِبَةٌ»

“Kama hutampa (hizo tende), utaandikiwa katika daftari lako kuwa umeongopa.”¹

Muqatil bin Hayyan amesema, “Waumini walisema, ‘Kama tungejua amali Anazozipenda zaidi Allah تعالی, tungezifanya.’ Allah تعالی Akawaeleza amali zinazopendeza zaidi Kwake, kwa Kusema,

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الَّذِينَ يُقْتَلُونَ فِي سَبِيلِهِ صَفًّا

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wanaopigana katika Njia Yake kwa safu...”

Allah تعالی Amesema Anachokipenda, na wakajaribiwa katika Siku ya Uhud. Hata hivyo, walirudi nyuma na kukimbia, huku wakimuacha Mtume ﷺ nyuma yao. Kwa ajili hiyo, Allah تعالی Alishusha Aya hii:

¹ Ahmad 3:447 na Abu Dawud 5:265.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا لِمَ تَقُوْلُوْنَ مَا لَا تَفْعَلُوْنَ ﴿٦١﴾

“Enyi mlioamini! Kwa nini mnasema msiyoyatenda?”

Allah تعالى Anasema hapa, ‘Ninayempenda zaidi kati yenu, ni mtu anayepigana kwa ajili yangu.’”² Wengine wamesema kuwa ilishuka kuhusu kadhia ya kupigana vita, mmoja wao aliposema kuwa alipigana na kustahamili vita, ilhali hakufanya hivyo. Qatadah na Adh-Dhahhak wamesema kuwa Ayah hii iliteremka ili kuwaonya baadhi ya watu waliokuwa wakisema kuwa waliua, walipigana, walichoma (mikuki n.k), na walifanya kadha wa kadha vitani, ilhali hawakufanya hivyo. Sa’id bin Jubayr amesema kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الَّذِيْنَ يُقْتَلُوْنَ فِيْ سَبِيْلِهِۦ صَفًا

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wanaopigana katika Njia Yake kwa safu...”

“Kabla ya Mtume ﷺ kuanza kupigana vita na adui, alikuwa akipanga safu za majeshi; katika Surah hii, Allah تعالى Anawafundisha waumini kufanya vivyo.”² Pia amesema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

كَانَهُمْ بَنِيْنَ مَّرْصُوْصٍ

“...kama jengo liliokamatana.”

Inamaanisha sehemu zake zimeungana imara; katika safu kwa ajili ya vita. Muqatil bin Hayyan amesema, “Zimeungana imara.” Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما ametoa rai juu ya maana ya Aya,

كَانَهُمْ بَنِيْنَ مَّرْصُوْصٍ

“...kama jengo liliokamatana.”

Kwa kusema, “Wao ni kama jengo imara lisilotingishika, kwasababu sehemu zake zimekamatana.”³

¹ Ad-Dur Al-Manthur 8:265.

² Al-Qurtubi 18:81.

³ Ad-Dur Al-Manthur 8:147.

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ يَنْقُورِ لِمَ تُؤْذُونَنِي وَقَدْ تَعْلَمُونَ أَنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ ۗ
 فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاغَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٦١﴾ وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ
 مَرْيَمَ يَبْنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا
 بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدٌ ۗ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٦٢﴾

5. Na Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kwa nini mnaniudhi, nanyi mnajua kuwa hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu niliyetumwa kwenu? Walipopotoka, Mwenyezi Mungu Aliziachia nyoyo zao zipotoke. Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wapotovu.

6. Na Isa bin Mariamu aliposema: Enyi Wana wa Israeli! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninayethibitisha yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakaye kuja baada yangu; jina lake ni Ahmad! Lakini alipowaletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi uliodhaahiri!

Musa عليه السلام Anawasihi Watu wake Wasimuudhi, na Allah تعالى Kuziachia Nyoyo Zao Zipotee

Allah تعالى Anaeleza kuwa mja Wake, Mtume Musa عليه السلام, mwana wa 'Imran, ambaye Allah تعالى Alizungumza naye moja kwa moja, aliwaambia watu wake,

لِمَ تُؤْذُونَنِي وَقَدْ تَعْلَمُونَ أَنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ ۗ

“Kwa nini mnaniudhi, nanyi mnajua kuwa hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu niliyetumwa kwenu?”

Maana yake: ‘Kwa nini mnaniudhi huku mnajua ukweli kuhusu Ujumbe niliotumwa kwenu.’

Hili linamfariji Mtume ﷺ kwa aliyofanyiwa na makafiri kwa watu wake na wengine. Inamtaka awe na subira. Ndipo siku moja akasema,

«رَحْمَةُ اللَّهِ عَلَىٰ مُوسَىٰ لَقَدْ أُودِيَ بِأَكْثَرِ مِن هَذَا فَصَبَرَ»

“Allah Amrehemu Musa: aliudhiwa zaidi ya hivi, na alisubiri.”¹

Kwa hiyo waumini wamekatazwa kumhuzunisha au kumuudhi Mtume ﷺ kwa namna yoyote. kama Allah تعالى Alivyosema,

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ ءَادَوْا مُوسَىٰ فَبَرَأَهُ اللَّهُ مِمَّا قَالُوا ؕ وَكَانَ عِنْدَ اللَّهِ

وَجِيمًا ﴿٣٣﴾

“Enyi mlioamini! Msiwe kama wale waliomtaabisha Musa, lakini Mwenyezi Mungu Akamtakasa na waliyoyasema, naye alikuwa mwenye hishima mbele ya Mwenyezi Mungu.” (33:69)

Na Kauli Yake:

فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاعَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ ؕ

“Walipopotoka, Mwenyezi Mungu Aliziachia nyoyo zao zipotoke.”

Inamaanisha Wayahudi walipoacha kufuata uongofu, ilhali waliujua, Allah تعالى Alizigeuza nyoyo zao zisifuata uongofu. Badala yake, Allah تعالى Aliwawekea mashaka, wasiwasi na kushindwa nyoyoni mwao, kama Alivyosema,

وَنُقَلِّبُ أَفْعَادَهُمْ وَأَبْصَرَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ ؕ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَنَدَّرَهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

“Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyo kuwa hawakuamini mara ya kwanza, Tunawaacha katika maasi yao wakitangatanga.” (6:110)

Na Kauli Yake:

وَمَنْ يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا

تَوَلَّىٰ وَنُصَلِّهِمْ جَهَنَّمَ ۖ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿١٢٥﴾

¹ Fat’h Al-Bari 7:652.

“Na anayempinga Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu, na akafuata njia isiyokuwa ya Waumini, Tutamuelekeza alikoelekea, na Tutamuingiza katika Jahannamu. Na hayo ni marejeo maovu.” (4:115),

Na, Sawa na hivyo Allah تعالى Amesema;

وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

“Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wapotovu.” (9:24)

Bishara Alizotoa ‘Isa عليه السلام Kuhusu Mtume Wetu na kuwa Jina Lake ni Ahmad ﷺ.

Allah تعالى Amesema;

وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَبْنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ
التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدُ^ط

“Na Isa bin Mariamu aliposema: Enyi Wana wa Israili! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninayethibitisha yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakayekuja baada yangu; jina lake ni Ahmad!”

‘Isa عليه السلام amesema, “Taurati ilifikisha Habari njema za kuja kwangu, na kuja kwangu kunathibitisha ukweli wa Taurati. Na mimi ninafikisha Habari njema za Mtume atakayekuja baada yangu. Yeye ni Mtume asiyejua kusoma, wa Makka, Mwarabu, Ahmad.”

‘Isa عليه السلام, ni Mtume wa mwisho kwa Bani Israil. Aliishi pamoja na Bani Israil kwa muda mchache, huku akifikisha habari njema za ujio wa Muhammad ﷺ, ambaye pia anaitwa Ahmad, Mtume wa Mwisho.

Baada ya Muhammad, hakutakuwa na utume au Mitume. Inayabainisha hayo Hadithi aliyokusanya Al-Bukhari katika Sahih yake kutoka kwa Jubayr bin Mut’im رضي الله عنه, ambaye alisema, “Nilimsikia Mtume ﷺ (akisema),

«إِنَّ لِي أَسْمَاءَ: أَنَا مُحَمَّدٌ، وَأَنَا أَحْمَدُ، وَأَنَا الْمَاجِي الَّذِي يَمْحُو اللَّهُ بِهِ الْكُفْرَ،
وَأَنَا الْحَاشِرُ الَّذِي يُحْشِرُ النَّاسَ عَلَى قَدَمَيَّ، وَأَنَا الْعَاقِبُ»

*"Hakika mimi nina majina. Mimi ni Muhammad na Ahmad. Mimi ni Al-Mahi ambaye kupitia kwangu Allah Ataufuta ukafiri. Mimi ni Al-Hashir, ambaye watu watafufuliwa juu ya nyayo zangu. Mimi pia ni Al-Aqib, yaani, hakutakuwa na Mtume baada yangu."*¹

Pia Muslim aliihusanya Hadithi hii kutoka kwa Az-Zuhri kutoka kwa Jubayr.²

Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Khalid bin Ma'dan amesema kuwa baadhi ya Masahaba wa Mtume ﷺ walisema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Tueleze kuhusu nafsi yako." Akasema,

«دَعْوَةُ أَبِي إِبْرَاهِيمَ، وَبُشْرَى عَيْسَى، وَرَأَتْ أُمِّي حِينَ حَمَلْتِ بِي كَأَنَّهُ خَرَجَ مِنْهَا
نُورٌ أَضَاءَتْ لَهُ قُصُورُ بَصْرَى مِنْ أَرْضِ الشَّامِ»

*"Mimi ni dua ya baba yangu Ibrahim na habari njema aliyofikisha 'Isa. Mama yangu aliposhika mimba yangu, aliota ndoto kana kwamba alitokwa na nuru ikiangaza majumba ya Busra katika ardhi ya Ash-Sham."*³

Hadithi hii ina isnadi nzuri ya masimulizi inayoungwa mkono na masimulizi mengine.

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Al-'Irbadh bin Sariyah رضي الله عنه amesema, "Mtume ﷺ amesema,

«إِنِّي عِنْدَ اللَّهِ لَخَاتِمُ النَّبِيِّينَ، وَإِنَّ آدَمَ لَمُنْجِدٌ فِي طَيْبَتِهِ، وَسَأَنْبِئُكُمْ بِأَوَّلِ ذَلِكَ:
دَعْوَةُ أَبِي إِبْرَاهِيمَ، وَبِشْرَاةُ عَيْسَى بِي، وَرُؤْيَا أُمِّي الَّتِي رَأَتْ، وَكَذَلِكَ أُمَّهَاتُ
النَّبِيِّينَ بَرَّيْنِ»

¹ Fat'h Al-Bari 8:509.

² Muslm 4:1828.

³ Ibn Hisham 1:145.

"Mimi kwa Allah ni Mtume wa Mwisho, na wakati huo hata Adam yungali kutokana na udongo wake. Nitakuambieni mwanzo wa hili, "Ni Dua ya baba yangu Ibrahim, habari njema aliyofikisha 'Isa kuhusu mimi, na ndoto aliyoiota mama yangu. Vile vile Mama wa Manabii wote waliota ndoto kama hiyo."¹

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Abu Umamah رضي الله عنه amesema, "Nilisema, 'Ewe Mtume! Ipi ilikuwa habari njema ya kwanza ya kuja kwako?' Akasema,

«دَعْوَةُ أَبِي إِبْرَاهِيمَ، وَبُشْرَى عِيسَى، وَرَأَتْ أُمِّي أَنَّهُ يَخْرُجُ مِنْهَا نُورٌ أَضَاءَتْ لَهُ
فُضُورُ الشَّامِ»

"(Matokeo ya) dua ya Baba yangu Ibrahim na habari njema aliyofikisha 'Isa. Mama yangu aliona nuru ndotoni mwake ikitokea kwake ikiangazia katika maeneo ya Ash-Sham."²

Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ aliwatuma watu themanini, akiwemo 'Abdullah bin Mas'ud, Ja'far bin Abi Talib, 'Abdullah bin 'Urfutah, 'Uthman bin Madh'un, Abu Musa, na wengine رضي الله عنهم, kwenda kwa Mfalme An-Najashi. Makuraishi wakamtuma 'Amr bin al-'As na 'Umarah bin al-Walid wakiwa na zawadi za kumpa Mfalme An-Najashi. 'Amr na 'Umarah, walikuja kwa Mfalme An-Najashi, wakasujudu mbele yake na kusimama katika upande wake wa kulia na kushoto. 'Amr na 'Umarah wakasema, "Baadhi ya watoto na binamu zetu wamehamia katika ardhi yenu; wametuacha sisi na dini yetu." Mfalme An-Najashi akasema, "Wako wapi?." Wakajibu, "Wapo katika ardhi yako, agiza waitwe." Mfalme An-Najashi akawaita Waislamu. Ja'far رضي الله عنه akawaambia Waislamu, "Nitakuwa msemaji wenu leo." Waislamu wakamfuata Ja'far رضي الله عنه na walipoingia kwa Mfalme hokusujudu baada ya kumsalimia. Wakamuambia Ja'far رضي الله عنه, "Kwa nini humsujudii Mfalme?" Ja'far akasema, "Sisi huwa tunamsujudia Allah تعالى." Wakasema, "Kwa nini?" Akajibu, "Allah تعالى Amemtuma Mjumbe kwetu, anayetuamrisha kuwa tusimsujudie yeyote isipokuwa Allah تعالى. Pia ametuamrisha kusali na kutoa sadaka." 'Amr bin al-

¹ Ahmad 4:127.

² Ahmad 5:262. Kuna udhaifu katika baadhi ya masimulizi haya. Maulamaa wengi wana rai kuwa zinaungana mkono zenyewe kwa zenyewe, kadhalika mwandishi ana rai sawa na hiyo.

'As akasema, "Wanavuruga itikadi yenu kuhusu 'Isa, mwana wa Maryam." Mfalme akauliza, "Mnasemaje kuhusu 'Isa na mama yake, Maryam?"¹ Ja' far akasema, "Sisi husema kauli ya Allah تعالی tu, kuwa yeye ni neno la Allah تعالی, roho Aliyoumba Allah تعالی na Akamteremshia bikira ambaye hakupata kuguswa na mtu wala kuzaa watoto hapo kabla." An-Najashi akainua bua na kusema, "Enyi Wahabeshi na watawa! Wallah! Wanachokisema kuhusu 'Isa hakizidi tunachokisema sisi kuhusu yeye, hakuna hata cha kutofautiana na bua hili. Mnakaribishwa kwetu, na salamu kwa aliyekutumeni. Ninashuhudia kuwa huyo ni Mtume ﷺ tunayesoma habari zake katika Injili. Yeye ni Mtume ambaye 'Isa, mwana wa Maryam, alimbashiria kuja kwake. Mtaishi popote mnapotaka. Wallahi! Kama nisingekabidhiwa majukumu ya ufalme, ningemuendea, ili nimtukuze kwa kumbebea viatu na maji yake ya kuchukulia udhu."

Mfalme akaamrisha zawadi za washirikina zirejeshwe. 'Abdullah bin Mas'ud akarejea na baadaye alishiriki katika vita vya Badr. Akasema kuwa Mtume ﷺ alipopata habari za kufariki kwa An-Najashi, alimuomba Allah تعالی Amsamehe.²

Kauli ya Allah تعالی,

فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ

"Lakini alipowaitea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi ulio dhaahiri."

Inarejea kwa Ahmad, aliyekuwa amebashiriwa, kwa mujibu wa Vitabu vya vizazi vilivyotangulia, kwa mujibu wa Ibn Jurayj رحمه الله تعالی na Ibn Jarir رحمه الله تعالی. Mtume ﷺ alipotokeza akiwa na dalili za wazi, makafiri walisema,

هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ

"Huu ni uchawi ulio dhaahiri!"

* * *

¹Maana yake: Allah تعالی alisema "Kuwa" na akafanyika.

²Ahmad 1:461.

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُوَ يُدْعَى إِلَى
 الْإِسْلَامِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٦١﴾ يُرِيدُونَ
 لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَاللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِ وَلَوْ كَرِهَ
 الْكَافِرُونَ ﴿٦٢﴾ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَى وَدِينِ
 الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٦٣﴾
 يَتَأَيَّمُوا عَلَى الدِّينِ ءَامَنُوا هَلْ أَذُكَّرْ عَلَى نَجْرَتِهِ تُنْجِبُكُمْ مِنْ
 عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٦٤﴾ تَوَمَّنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي
 سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ ۗ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ
 تَعْمَلُونَ ﴿٦٥﴾ يَغْفِرُ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلْكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي
 مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَمَسْكِنٍ طَيِّبَةٍ فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ ۗ ذَٰلِكَ
 الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٦﴾ وَأُخْرَىٰ تُحِبُّونَهَا ۗ نَصْرٌ مِنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ
 قَرِيبٌ ۗ وَبَشِيرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٧﴾ يَتَأَيَّمُوا عَلَى الدِّينِ ءَامَنُوا كُونُوا
 أَنْصَارَ اللَّهِ كَمَا قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ لِلْحَوَارِيِّينَ مَنْ
 أَنْصَارِي إِلَى اللَّهِ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ فَقَامَتِ
 طَائِفَةٌ مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَكَفَرَتِ طَائِفَةٌ ۗ فَأَيَّدْنَا الَّذِينَ
 ءَامَنُوا عَلَىٰ عَدُوِّهِمْ فَأَصْبَحُوا ظَاهِرِينَ ﴿٦٨﴾

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ
 الْكَذِبَ وَهُوَ يُدْعَى إِلَى الْإِسْلَامِ ۗ
 وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٦١﴾
 يُرِيدُونَ لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ
 وَاللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ
 ﴿٦٢﴾ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ
 بِالْهُدَى وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى
 الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٦٣﴾

7. Na ni nani mwenye kudhulumu zaidi kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, naye anaitwa kwenye Uislamu? Na Mwenyezi Mungu Hawa-ongoi watu madhaalimu.

8. Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu Atakamilisha nuru Yake ijapokuwa makafiri watachukia.

9. Yeye Ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa uwongofu na Dini ya haki ili ipate kuzishinda dini zote, ijapokuwa washirikina watachukia.

Kutajwa kwa Watu Madhalimu Zaidi Kuliko Wote, na Bishara ya Utimilifu wa Nuru ya Uislamu na Kuzishinda Dini Zote

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُوَ يُدْعَى إِلَى الْإِسْلَامِ

“Na ni nani mwenye kudhulumu zaidi kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, naye anaitwa kwenye Uislamu?”

Inamaanisha, hakuna dhalimu zaidi kuliko anayedanganya kuhusu Allah تعالى na anamuekea washindani na washirika, hata anapoitwa katika Tawhid na kumuabudu kwa unyoofu na Ikhlas. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema,

وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

“Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu madhaalimu.”

Kauli ya Allah تعالى،

يُرِيدُونَ لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ

“Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao.”

Kwa kuashiria kuwa makafiri watajaribu kuuvuruga ukweli kwa uongo. Majaribio yao ni kama kutaka kuzima jua kwa mdomo, haiwezekani. Huo ndio mfano wa jitihada zao za kujaribu kuuzima ukweli. Kwa hivyo Kauli ya Allah تعالى،

وَاللَّهُ مِتُّمُ نُورِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٦١﴾ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ

لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٦٢﴾

“Na Mwenyezi Mungu Atakamilisha Nuru Yake ijapokuwa makafiri wata chukia.” “Yeye Ndiye Aliyemtuma Mjumbe Wake kwa uongofu na Dini ya ukweli ili Kuupa ushindi juu ya dini (zingine) zote ingawa washirikina wanachukia (hilo).”

Tumeleza maana ya Aya hiyo, katika *Tafsir ya Surah Bara'ah*.¹ Kila Sifa Njema Anastahiki Allah تعالى.

¹ Ambayo imeelezwa kwa kifupi katika juzu ya tisa, *Tafsir ya Surat At-Tawbah* (932).

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذَلُّكُمْ عَلَىٰ تَجْرِئَةِ تُجَاجِلِكُمْ مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿١٠﴾ تَوَمِّنُونَ بِاللَّهِ
 وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ ؕ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْمَلُونَ
 ﴿١١﴾ يَغْفِرَ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلْكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرَىٰ مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَمَسْكِنٍ طَيِّبَةٍ فِي
 جَنَّاتٍ عَدْنٍ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٢﴾ وَأُخْرَىٰ تُحِبُّونَهَا ۖ نَصْرٌ مِّنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ ۖ وَبَشِيرٌ
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٣﴾

10. Enyi mliaoamini! Nikuonesheni biashara itakayokuoieni na adhabu iumizayo?

11. Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na piganeni Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu, ikiwa nyinyi mnajua.

12. Atakusameheni dhambi zenu, na Atakutieni katika Mabustani yapitiwayo na mito kati yake, na makazi mazuri katika Bustani za milele. Huko ndio kufuzu kukubwa.

13. Na kinginecho mkipendacho, nacho ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi ulio karibu! Na wapeni habari njema Waumini!

Biashara Inayomuokoa Mtu na Adhabu lumizayo

Tumetaja Hadithi ya 'Abdullah bin Salam رضي الله عنه ambamo Masahaba walitaka kumuuliza Mtume ﷺ kuhusu amali njema kwa Allah تعالى, ili wazifanye. Allah تعالى Akateremsha Surah hii, ikiwemo Aya hii,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذَلُّكُمْ عَلَىٰ تَجْرِئَةِ تُجَاجِلِكُمْ مِّنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿١٠﴾

“Enyi mliaoamini! Nikuonesheni biashara itakayokuoieni na adhabu iliyo chungu?”

Allah تعالى Akaeleza biashara hiyo kubwa kuwa kamwe haitafeli, biashara hiyo itampa mtu anachokitaka na kumuondolea asichokipenda. Allah تعالى Amesema,

تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٧﴾

“Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na piganeni Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu, ikiwa nyinyi mnajua.”

Hii ni bora zaidi kuliko biashara ya kidunia katika kujitahidi kuihangaikia hiyo peke yake. Allah تعالى Amesema,

يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ

“Atakusameheni dhambi zenu.”

Inamaanisha, ‘kama mtatimiza Nilichokuamrisheni na Kukuongozeni, basi Nitasamehe dhambi zenu na Kukuingizeni katika bustani za Peponi. Humo, mtakuwa na makazi bora na sehemu za juu.’

Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

وَيُدْخِلْكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَمَسْكِنٍ طَيِّبَةٍ فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٨﴾

“...na Atakutieni katika Mabustani yapitiwayo na mito kati yake, na maskani nzuri nzuri katika Bustani za milele. Huko ndio kufuzu kukubwa.”

Kauli ya Allah تعالى,

وَأُخْرَىٰ تُحِبُّونَهَا ۖ

“Na kinginecho mkipendacho.”

Inamaanisha, ‘Nitakupeni neema nyingi zaidi mnazozipenda,’

نَصْرٌ مِّنَ اللَّهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ ۚ

“...ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi wa karibu...”

Inamaanisha, ikiwa mtapigana katika Njia ya Allah تعالى na kuisaidia Dini Yake, Atakupeni ushindi. Allah تعالى Amesema,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن نَّصُرُوا اللَّهَ يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ ﴿٧﴾

“Enyi mlioamini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu Naye Atakunusuruni na Ataithibitisha miguu yenu.” (47:7),

Na Akasema,

وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَن يَنْصُرُهُ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾

“Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu Humsaidia yule anayemsaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu Mtukufu.” (22:40)

Kauli ya Allah تعالى,

وَفَتَحَ قَرِيبٌ

“...na ushindi ulio karibu!”

Maana yake: Itakuja hivi karibuni, na hii ni neema iliyozidishwa inayopatikana duniani na inaendelea. Kuwa na furaha Akhera ni kwa ajili ya wenye kumtii Allah تعالى na Mjumbe Wake na kumsaidia Allah تعالى na Dini Yake.

Allah تعالى Amesema;

وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ

“Na wabashirieni Waumini!”

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا أَنْصَارَ اللَّهِ كَمَا قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ لِلْحَوَارِيِّينَ مَن أَنْصَارِي إِلَى اللَّهِ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ فَأَمَّتْ طَائِفَةٌ مِّنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَكَفَرَت طَائِفَةٌ فَأَيَّدْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا عَلَىٰ عَدُوِّهِمْ فَأَصْبَحُوا ظَاهِرِينَ ﴿٤١﴾

14. Enyi mlioamini! Kuweni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu, kama alivyosema Isa bin Mariamu kuwaambia wanafunzi wake: Nani wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu? Wakasema wanafunzi: Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu! Basi taifa moja la Wana

wa Israeli liliamini, na taifa jingine lilikufuru. Basi Tukawaunga mkono walioamini dhidi ya maadui zao, wakawa wenye kushinda.

Waislamu Mara zote ndio Wenye Kunusuru Dini

Allah تعالى Anawaamrisha waumini wawe ni wenye kumsaidia Allah تعالى katika nyakati zote, kwa maneno na vitendo vyao vyote, kwa kujitolea nafsi na mali zao.

Allah تعالى Anawaamrisha waitikie wito Wake na wa Mjumbe Wake, kama wanafunzi walivyomuambia Nabii 'Isa عليه السلام pale waliposema,

مَنْ أَنْصَارِي إِلَى اللَّهِ ط

"Nani wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu?"

Inamaanisha, 'nani watakaonisaidia katika kufikisha Ujumbe wa Allah تعالى.'

قَالَ الْخَوَارِثُونَ

"Hawariyyun wakasema.."

Wafuasi wa 'Isa عليه السلام,

نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ ط

"Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu!"

Inamaanisha, 'tutakusaidia kuhusu Ujumbe uliotumwa na tutakusaidia kuufikisha.' Ambapo, 'Isa عليه السلام aliwatuma wanafunzi kwenda sehemu mbalimbali za Ash-Sham ili kuwalingania Wagiriki na Waisrael waingie katika Uislamu. Kadhalika, katika siku za Hajj, Mtume ﷺ alikuwa akisema,

«مَنْ رَجُلٌ يُؤْمِنِي حَتَّىٰ أَبْلَغَ رِسَالَةَ رَبِّي؟ فَإِنَّ قُرَيْشًا قَدْ مَنَعُونِي أَنْ أَبْلَغَ رِسَالَةَ رَبِّي»

"Nani atakayenisaidia katika kufikisha Ujumbe wa Mola Wangu Mlezi. Kwa hakika, Makuraishi wamenizuia kufikisha Ujumbe wa Mola Wangu Mlezi."¹

¹ Ahmad 3:323, Al-Hakim 2:624 na Al-Bayhaqi 8:146.

Allah تعالی Aliwainua Aws na Khazraj ili kumsaidia Mtume ﷺ. Walikuwa watu wa Madinah ambao walimpa ahadi ya utii na wakamsaidia, Na walimpa sharti la kumsaidia kila mtu mweusi na mwekundu kama anghamia kwao. Alipohamia kwao pamoja na Masahaba wake, walitimiza yale waliyomwahidi Allah تعالی. Hayo ndiyo yaliyomfanya Allah na Mjumbe Wake kuwaita wao, *Al-Ansar*, yaani Wasaidizi. Jina hilo likawa mashuhuri kwao. Allah تعالی Awe radhi kwao na wao wawe radhi Kwake, pia.

Kundi Moja la Wana wa Israel Lilimuamini 'Isa عليه السلام na Jingine Lilimpinga

Kauli ya Allah تعالی,

فَقَامَتَ طَائِفَةٌ مِّنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَكَفَرَتَ طَائِفَةٌ

“Basi taifa moja la Wana wa Israeli liliamini, na taifa jingine lilikufuru.”

Nabii 'Isa عليه السلام alipofikisha Ujumbe wa Mola Wake Mlezi kwa watu wake na wanafunzi kumsaidia, kundi la Bani Israel liliamini. Walipokea uongofu walioletewa na 'Isa عليه السلام, ilhali kundi jingine, lilipotoka. Kundi hili lilikataa alichowaletea 'Isa عليه السلام, na kukataa utume na wakazua uongo mbaya kabisa kuhusu yeye na mama yake. Wao ni Wayahudi, Allah تعالی Awalaani mpaka Siku ya Hukumu. Kundi jingine lilizidisha kumkweza 'Isa عليه السلام, mpaka likampandisha daraja na utukufu zaidi ya utume aliopeva na Allah تعالی.

Waligawanyika katika madhehebu na makundi madogo madogo, baadhi yao walisema kuwa 'Isa alikuwa mwana wa Allah, huku wengine wakisema kuwa alikuwa mmoja katika utatu, na ndio sababu humuomba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu! Baadhi yao walisema kuwa 'Isa alikuwa Allah, kama tulivyotaja katika *Tafsir ya Surat An-Nisa*.¹

¹ Angala juzu ya tatu, *Tafsir ya Surat An-Nisa* (4:171).

Allah تعالیٰ Huwapa Ushindi Kundi la Waumini

Kauli ya Allah تعالیٰ,

فَأَيَّدْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا عَلٰى عَدُوِّهِمْ

“Basi Tukawaunga mkono walio amini dhidi ya maadui zao...”

Maana yake: ‘Tuliwapa ushindi juu ya kundi la Wakristo lililowakataa,’

فَأَصْبَحُوا ظَاهِرِينَ

“...wakawa wenye kushinda.”

‘Juu ya kundi la kikafiri, Tulipomtuma Muhammad ﷺ.

Imamu Abu Ja`far bin Jarir At -Tabari رحمه الله تعالیٰ amesimulia kuwa Ibn ‘Abbas عليه السلام amesema, “Allah تعالیٰ Alipoamua kumuinua ‘Isa عليه السلام mbinguni, ‘Isa عليه السلام aliwaendea Masahaba wake huku matone ya maji yakidondoka kutoka kichwani kwake. Wakati huo, kulikuwa na watu kumi na wawili katika Nyumba. ‘Isa عليه السلام akawaambia, ‘Baadhi yenu mtanikana mara kumi na mbili baada ya kuniamini.’ Akauliza, ‘Nani kati yenu anayejitolea kushabihiana na mimi na apate kuuliwa badala yangu? Mtu huyo atakuwa pamoja nami katika mahali pangu (Peponi).’ Mmojawapo kati ya waliokuwa wadogo kiumri waliokuwepo alijitolea lakini ‘Isa عليه السلام alimuamuru aketi chini. ‘Isa عليه السلام alikariri kauli yake hiyo na kijana huyo akasimama tena na kujitolea, na ‘Isa akamwambia tena akae chini. ‘Isa عليه السلام alikariri maneno hayo hayo na kijana huyo huku akijitolea. Mara hii, ‘Isa عليه السلام alimuambia, ‘Basi utakuwa wewe.’ Muonekano wa sura ya ‘Isa ukawekwa kwa kijana huyo, huku ‘Isa عليه السلام, aliinuliwa kwenda mbinguni kupitia mwanya katika paa la Nyumba hiyo. Wayahudi wakaja kumtafuta ‘Isa عليه السلام na wakamkamata yule aliyeonekana kama yeye, wakamuua kwa kumsulubu msalabani. Baadhi yao walimkufuru ‘Isa mara kumi na mbili, baada ya kuwa tayari walishamuamini. Wakagawanyika katika makundi matatu. Kundi moja, Al-Ya`qubiyah, walisema, ‘Allah تعالیٰ Alikuwa pamoja nasi kwa kadiri alivyotaka akapanda mbinguni.’

Kundi jingine, An-Nasturiyyah walisema, ‘Mwana wa Allah alikuwa pamoja nasi kadiri Allah تعالیٰ Alivyotaka Akamuinua mbinguni.’ Kundi la tatu likasema, ‘Mja na Mtume wa Allah alikuwa pamoja nasi kwa kadiri Allah تعالیٰ Alivyotaka

halafu Allah تعالى akamuinua Kwake.' Kundi hili lilikuwa la Waislamu. Makundi mawili yale ya kikafiri, yaliungana dhidi ya kundi la Waislamu na kuliangamiza. Uislamu uliendelea kufichikana mpaka Allah تعالى Alipomtuma Muhammad,

فَأَمَّنْتَ طَائِفَةٌ مِّنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَكَفَرْتَ طَائِفَةٌ

“Basi taifa moja la Wana wa Israeli liliamini, na taifa jingine lilikufuru.”

Aya hii inalihusu kundi miongoni mwa Bani Israel lililokufuru na kundi lililoamini, katika wakati wa 'Isa عليه السلام,

فَأَيَّدْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا عَلَىٰ عَدُوِّهِمْ فَأَصْبَحُوا ظَاهِرِينَ

“Basi Tukawaunga mkono walioamini dhidi ya maadui zao, wakawa wenye kushinda.”

Kwa ushindi aliopata Muhammad ﷺ juu ya dini ya makafiri, ulioishinda dini yao.¹

Hayo ndiyo maneno yaliyo katika kitabu chake kwa ajili ya Tafsiri ya Ayah hii tukufu. Sawa na hivyo, An-Nasa'i aliikusanya kauli ya Ibn 'Abbas رضي الله عنهما katika Sunan yake.²

Kwa hiyo, umma wa Muhammad ﷺ mara zote utaenea juu ya ukweli mpaka amri ya Allah تعالى (Saa ya Mwisho) isimame, huku wakiwa katika njia hii. Kundi la mwisho litapigana dhidi ya Ad-Dajjal likiwa pamoja na 'Isa عليه السلام, kwa mujibu wa Hadithi zilizo katika vitabu sahihi.³

Huu ni mwisho wa *Tafsiru ya Surat As-Saff*. Kila sifa njema na shukrani Anastahiki Allah تعالى.



¹ At-Tabari 23:366

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:489. Toleo hili la habari ya upaaji huchukulika kuwa ni katika visa vya *Israiliyyat* ambavyo Muislamu hapaswi kuamini wala kukanusha.

³ *Fat'h Al-Bari* 13:306, Muslim 3:1524 na Abu Dawud 3:11

Tafsiri ya Suratul Jumu'ah Sura ya 62 Iliteremshwa Madinah

Fadhila za *Suratu Al-Jumu'ah*

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na Abu Hurayrah رضي الله عنه wamesimulia kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisoma *Suratu Al-Jumu'ah* na *Surat Al-Munafiqin* katika Sala ya Ijumaa. Muslim aliikusanya Hadithi hii katika *Sahih* yake.¹



¹Muslim 2:597, 599.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْجُمُعَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ۝ هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ لَافِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ۝ وَآخَرِينَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوا بِهِمْ ۝ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ۝ ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ ۝ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ۝

يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ۝ هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ لَافِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ۝ وَآخَرِينَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوا بِهِمْ ۝ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ۝ ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ ۝ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ۝

1. Viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi vinamtakasa Mwenyezi Mungu, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.
2. Yeye Ndiye Aliyempeleka Mtume kwenye watu wasiojua kusoma, awesomee Aya Zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapokuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu uliodhaahiri.
3. Na kwa wengine ambao bado hawajaungana nao. Na Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.
4. Hiyo ni Fadhila ya Mwenyezi Mungu Anayompa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kubwa.

Kila Kitu Kinamsifu na Kinamtukuza Allah تعالى.

Allah تعالى Anaeleza kuwa kila kitu mbinguni na duniani kinamtukuza, wakiwemo kila aina ya wanyama na viumbe hai. Allah تعالى Amesema katika Ayah nyingine,

وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ

“Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa Sifa Zake.” (17:44)

Kauli ya Allah تعالى,

الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ

“Mfalme, Mtakatifu.” Inamaanisha kuwa Yeye ni Mmiliki na Mfalme wa mbingu na dunia Ambaye Anayadhibiti mambo yao kikamilifu. Yeye ni Mtukufu, Ameepukana na kila upungufu, Sifa Zake ni kamilifu,

الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ

“Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.” Ambaye maelezo yake yameshajadiliwa katika sehemu nyingi.

Fadhila za Allah تعالى kwa Kumtuma Muhammad ﷺ

Allah تعالى Amesema,

هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِّنْهُمْ

“Yeye Ndiye Aliyempeleka Mtume kwenye watu wasiojua kusoma.”

Neno ‘wasiojua kusoma’ hapa linakusudia Waarabu. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَقُلْ لِلَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْأُمِّيِّينَ ءَأَسْلَمْتُمْ ؕ فَإِنِ أَسْلَمُوا فَقَدِ اهْتَدَوْا ؕ وَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاغُ ؕ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿٦٢﴾

“Na waambie waliopewa Kitabu na wasio na kisomo: Je! Mmesilimu? Wakisilimu basi wameongoka. Na wakikengeuka basi juu yako ni kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja Wake.” (3:20)

Kutajwa wasiojua kusoma haimanishi kuwa Muhammad ﷺ ndiye pekee aliyetumwa kwao, kwasababu baraka walizobarikiwa Waarabu ni kubwa zaidi kuliko watu wa mataifa mengine. Katika Aya nyingine, Kauli ya Allah تعالیٰ،

وَإِنَّهُ لَذِكْرٌ لَّكَ وَلِقَوْمِكَ

**“Na hakika haya ni ukumbusho kwako na kwa kaumu yako.”
(43:44).**

Kwa hakika, Qur'an ni ukumbusho hata kwa wasio Waarabu waizingatie. Allah تعالیٰ Amesema,

وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ

“Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe.” (26:214)

Aya hizi hazipingani na Kauli za Allah تعالیٰ،

قُلْ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliyetumwa na Mwenyezi Mungu.” (7:158), na,

لَأَنْذِرْكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

“...ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia.” (6:19)

Na katika Kauli Yake kuhusu Qur'an،

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَأَلْنَاوْهُ مَوْعِدُهُ

“...na anaye mkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao.” (11:17)

Kuna Aya nyingine inayoonesha kuwa Ujumbe wake ni kwa wote. Mtume ﷺ, alitumwa kwa watu wote, wanadamu na majini. Tulishataja maana yake hapo mwanzoni katika Surat Al-An'am kwa kuleta Aya na Hadithi kadhaa. Kila Sifa njema na Shukrani Anastahiki Allah تعالیٰ. Ayah hii inathibitisha kuwa Allah تعالیٰ kwa hakika Ameipokea dua ya rafiki yake, Ibrahim عليه السلام alipomuomba awapelekee Mtume watu wa Makkah kutoka miongoni mwao wenyewe. Atakayewasomea Maneno ya Allah تعالیٰ, kuwatakasa na kuwafundisha kitabu na Hikmah. Kwa hivyo, Allah تعالیٰ kila Sifa Njema na Shukrani Kwake - Alimtuma pindi Mitume walipositishwa kupelekwa na njia kuzuiwa. Kwa hakika ulikuwa

wakati ambapo ilikuwepo na haja kubwa ya kufanyika hayo. Hususani kwa kuwa Allah تعالى Aliwachukia watu wa dunia, Waarabu na wasio-Waarabu, isipokuwa wachache waliopewa Kitabu, walioendelea kuwa na imani ya kweli. Allah تعالى Alimtuma kwao 'Isa bin Maryam عليه السلام. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema,

هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ
وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٦٢﴾

“Yeye Ndiye Aliyempeleka Mtume kwenye watu wasiojua kusoma, awesomee Aya Zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri.”

Hapo zamani, Waarabu walishika Dini ya Ibrahim عليه السلام. Baadaye wakabadilika, wakaivuruga na kuichafua, kwa kuchagua ushirikina badala ya *Tawhid* na mashaka badala ya uhakika. Wakazusha dini ambayo Allah تعالى Hakuiweka, kama watu wa Kitabu walivyofanya pindi walipobadili na kuchafua Vitabu vyao Vitukufu. Allah تعالى Alimtuma Muhammad ﷺ, kwa sheria tukufu, Dini kamilifu ya kuwafaa wanadamu wote na majini. Ndani yake, kuna uongofu na maelezo ya haja zao zote za duniani na Akhera. Inawaweka karibu na Peponi na radhi za Allah تعالى na kuwaepusha na moto na ghadhabu za Allah تعالى. Ndani mwake, kuna ufafanuzi wa Hukumu katika masuala yote makubwa na madogo ya dini katika misingi na tanzu. Kwa Muhammad ﷺ Allah تعالى Amemkusanyia sifa zote nzuri za Mitume wa kabla yake, na Amempa ambacho hakuwapa vizazi vya mwanzo na vya mwisho vya wanadamu. Rehema na amani za Allah تعالى zimfikie Muhammad ﷺ mpaka Siku ya Kiama.

Muhammad ﷺ ni Mtume kwa Waarabu na Wasio-Waarabu

Kauli ya Allah تعالى,

وَأَخْرَجْنَا مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوا بِهِمْ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٣﴾

“Na kwa wengine ambao bado hawajaungana nao. Na Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Imamu Abu 'Abdullah Al-Bukhari رحمه الله تعالى, amenukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, “Tulikuwa tumekaa pamoja na Mtume ﷺ, ilipomshukia *Suratu Al-Jumu'ah*;

وَأَخْرَيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوا بِهِمْ^٤

“Na kwa wengine ambao bado hawajaungana nao.”

Wakasema, ‘Kina nani hao, Ewe Mjumbe wa Allah’ Mtume ﷺ hakujibu, mpaka swali likakariwa mara tatu. Wakati huo, Salman Al-Farisi رضي الله عنه alikuwa pamoja nasi. Mtume ﷺ akaweka mkono wake juu ya Salman رضي الله عنه, kwa kusema,

«لَوْ كَانَ الْإِيمَانُ عِنْدَ الثَّرَيَّا لَنَأَلَّهُ رِجَالٌ - أَوْ رَجُلٌ - مِنْ هَؤُلَاءِ»

“Kama imani ingekuwa juu ya Ath-Thurayya, basi baadhi ya watu au mtu kutoka kwa watu hao angeipata.”¹

Muslim, At-Tirmidhi, An-Nasai, Ibn Abi Hatim na Ibn Jarir waliikusanya Hadithi hii.² Hadithi hii inaashiria kuwa Surat Al-Jumu'ah ilishuka Al-Madinah na kuwa Ujumbe wa Mtume ﷺ ni kwa wote. Mtume ﷺ ameeleza Kauli ya Allah تعالى,

وَأَخْرَيْنَ مِنْهُمْ

“Na kwa wengine...” Kwa kutaja Uajemi. Ndio sababu Mtume ﷺ alituma salamu kwenda kwa wafalme wa Uajemi na Roma, na wengine, kuwalingania juu ya Allah تعالى na kufuata ujumbe aliotumwa kwao. Ndio sababu Mujahid na wengine kadhaa wamesema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

وَأَخْرَيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوا بِهِمْ^٤

“Na kwa wengine ambao bado hawajaungana nao.”

Yaani kwa wasio -Waarabu wote wenye kuamini ukweli wa Mtume ﷺ.³ Kauli ya Allah تعالى,

وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Na Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Anasema kuwa Yeye ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima katika sheria na kudura Anayopanga. Kauli ya Allah تعالى,

¹ Fat'h Al-Bari 8:510.

² Muslim 4:1972, Tuhat Al-Ahwadhi 9:209, 10:433, An-Nasai katika Al-Kubra 5:75, 6:490, na At-Tabari 23:375.

³ At-Tabari 23:374.

ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٦٢﴾

“Hiyo ni Fadhila ya Mwenyezi Mungu Anayompa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kubwa.

Inakusudia Utume Aliompa Muhammad ﷺ na sifa nyingi nzuri Alizoupendelea Ummah huu, kwa Kuwapelekea wao Muhammad ﷺ.

* * *

“Sema: Enyi mlio Mayahudi! Ikiwa nyinyi mnadai kuwa ni vipenzi vya Mwenyezi Mungu pasipo kuwa watu wengine, basi yatamanini mauti, ikiwa mnasema kweli.”

Inamaanisha, kama mnadai kuwa mko katika uongofu sahihi na kuwa Muhammad ﷺ na Masahaba wake رضي الله عنهم wamepotea, basi muombeni Allah تعالى Awafishe kundi lililopotoka kati ya mawili, ikiwa nyinyi ni wa kweli katika madai yenu. Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا يَتَمَنَّوْنَهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيهِمْ^٤

“Wala hawatayatamani kabisa, kwa sababu ya iliyokwisha yatanguliza mikono yao.”

Maana yake: Kwasababu ya ukafiri, dhuluma na madhambi waliyofanya.

وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ

“Na Mwenyezi Mungu Anawajua waliodhulumu.”

Tumeshaitaja changamoto hii ya kuapizana kwa Wayahudi katika Surat Al-Baqarah, ambapo Allah تعالى Amesema،

قُلْ إِنْ كَانَتْ لَكُمْ الدَّارُ الْآخِرَةُ عِنْدَ اللَّهِ خَالِصَةً مِّنْ دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوْا الْمَوْتَ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٤﴾ وَلَنْ يَتَمَنَّوَهُ أَبَدًا بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيهِمْ^٥ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٤٥﴾
وَلَتَجِدَنَّهُمْ أَحْرَصَ النَّاسِ عَلَى حَيَاتِهِمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا^٦ يُوَدُّ أَحَدُهُمْ لَوْ يُعَمَّرَ أَلْفَ سَنَةٍ وَمَا هُوَ بِمُزَحَّزِحٍ مِنْهُ مِنَ الْعَذَابِ أَنْ يُعَمَّرَ^٧ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿٤٦﴾

“Sema: Ikiwa nyumba ya Akhera iliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni yenu tu bila ya watu wengine, basi tamanini mauti kama nyinyi mnasema kweli. Wala hawatayatamani kamwe kwa sababu ya yale yaliyotangulizwa na mikono yao; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwajua vyema wanaodhulumu. Na hakika utawaona ni wenye kuwashinda watu wote kwa pupa ya kuishi, na kuliko washirikina. Kila mmoja wao anatamani lau angelipewa umri wa miaka elfu. Wala hayo ya kuzidishiwa umri hayamuondoshei adhabu; na Mwenyezi Mungu Anayaona wanayo yatenda.” (2:94-96)

Tulishaeleza maana hizo katika Aya hiyo, kuwa changamoto ya kuapizana na kulaaniana ilihusu Wayahudi kumuomba Allah تعالى Aliangamize kundi potofu, yaani wao au wapinzani wao. Pia tumetaja changamoto kama hiyo ya kuapizana na kulaaniana dhidi ya Wakristo katika *Suratu Al-Imran*,

فَمَنْ حَاجَّكَ فِيهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَكُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَكُمْ وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَلْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكٰذِبِينَ ﴿٦١﴾

“Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooi tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.” (3:61)

Na dhidi ya washirikina, katika *Suratu Maryam*,

قُلْ مَنْ كَانَ فِي الضَّلٰلَةِ فَلْيَمْدُدْ لَهُ الرَّحْمٰنُ مَدًّا

“Sema: Walio katika upotofu basi Arrahmani Mwingi wa Rahema Atawazidishia muda...” (19:75)

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema, “Abu Jahl, Allah تعالى Amlaani, alisema, ‘Kama nitamuona Muhammad ﷺ akisali katika Ka`bah, nitapanda shingoni kwake.’ Mtume ﷺ aliposikia hayo, alisema,

«لَوْ فَعَلَ لِأَخَذْتَهُ الْمَلَائِكَةُ عِيَانًا وَلَوْ أَنَّ الْيَهُودَ تَمَتُّوْا الْمَوْتَ لَمَاتُوا وَرَأَوْا مَقَاعِدَهُمْ مِنَ النَّارِ، وَلَوْ خَرَجَ الَّذِينَ يُيَاهِلُونَ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ لَرَجَعُوا لَا يَجِدُونَ أَهْلًا وَلَا مَالًا»

“Kama angefanya hivyo, malaika angemnyakua hadharani. Kama Wayahudi wangetamani mauti, wangekufa na wangeona makazi yao katika Moto wa Jahanamu. Kama wangekubali kutoka ambao walitaka kulaaniana na Mjumbe wa Allah ﷻ, wasingezikuta familia na mali zao baada ya kurejea (nyumbani kwao).”¹

Al-Bukhari, At -Tirmidhi na An-Nasa’i wameinukuu.² Kauli Yake;

¹ Ahmad 1:248. Angalia *Surah Aal ‘Imran* (3:61) katika juzu ya pili kwa maana ya *Mubahalaha*.

² *Fat’h Al-Bari* 8:590, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:277, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:518, 308

قُلْ إِنَّ أَلَمَّوَتَ الَّذِي تَفْرُوَت مِنَّهُ فَإِنَّهُ مُلْتَقِيكُمْ ۗ ثُمَّ تَرْدُونَ إِلَىٰ عَلِيمِ الْغَيْبِ
وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥٨﴾

“Sema: Hayo mauti mnayoyakimbia, bila ya shaka yatakukuteni. Kisha mtarudishwa kwa Mwenye Kuyajua yaliyofichikana na yanayoonekana. Hapo Atakuambieni mliyokuwa mkiyatenda.”

Ni sawa na Kauli Yake katika Surat An-Nisa’:

أَيْنَمَا تَكُونُوا يُدْرِكُكُمُ أَلَمَّوَتٌ وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشِيدَةٍ

“Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu.” (4:78)

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِن يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ
ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٥٩﴾ فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانْتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا
مِن فَضْلِ اللَّهِ وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٦٠﴾

9. Enyi mlio amini! Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua.

10. Na itakapokwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa.

Al-Jumu'ah, na Amri na Fadhila za Siku ya Ijumaa

Siku ya Ijumaa imeitwa *Al-Jumu'ah* kwa sababu imetokana na neno *Al-Jam'*, kilugha, ni mkusanyiko. Waislamu hukusanyika kila wiki, katika siku ya Ijumaa katika sehemu za ibada. Ilikuwa siku ya Ijumaa pindi Allah تعالی Alipomaliza Kuumba, siku ya sita, Allah تعالی Aliumba mbingu na ardhi. Katika siku ya Ijumaa, Allah تعالی Alimuumba Adam عليه السلام, na Kumueka Peponi, na katika siku hiyo, alitolewa Peponi. Siku ya Ijumaa itasimama Saa ya Mwisho. Kuna saa katika siku ya Ijumaa, ambapo muumini akiomba jambo kwa Allah تعالی hupewa alichokiomba. Hayo yamethibiti katika Hadithi nyingi sahihi. Zamani,

siku ya Ijumaa ilikuwa ikiitwa, 'Arubah. Ni kweli kuwa umma zilizopita zilijulishwa kuhusu siku ya Ijumaa, lakini zikapotoka. Wayahudi walichagua Jumamosi kuwa siku yao tukufu, lakini Adam عليه السلام hakuumbwa katika siku ya Jumamosi. Wakristo walichagua Jumapili, ambayo ni siku ulipoanza Uumbaji. Allah تعالى Aliuchagulia Umma huu siku ya Ijumaa, kwa sababu ni siku Uumbaji ulipomalizika. Al-Bukhari na Muslim wamenukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«نَحْنُ الْآخِرُونَ السَّابِقُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، بَيَدِ أُنْثَاهُمْ أَوْتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِنَا، ثُمَّ إِنَّ هَذَا يَوْمَهُمُ الَّذِي فَرَضَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ فَاخْتَلَفُوا فِيهِ فَهَدَانَا اللَّهُ لَهُ، فَالْتَأَسُّ لَنَا فِيهِ نَبْعٌ، الْيَهُودُ غَدًا وَالنَّصَارَى بَعْدَ غَدٍ»

"Sisi ni wa mwisho, wa mwanzo Siku ya Kiama, ingawa umma uliotangulia ulipewa Vitabu kabla yetu. Na hii (siku ya Ijumaa) ilikuwa yao na walifaradhishiwa, lakini walitofautiana. Hivyo, Allah Akatuongoza kwa ajili yake, kwa hiyo na watu wote wanakuwa nyuma yetu: Wayahudi kesho na Wakristo kesho kutwa."¹

Hayo ni maneno ya Al-Bukhari. Katika masimulizi mengine ya Muslim;

«أَضَلَّ اللَّهُ عَنِ الْجُمُعَةِ مَنْ كَانَ قَبْلَنَا، فَكَانَ لِلْيَهُودِ يَوْمَ السَّبْتِ، وَكَانَ لِلنَّصَارَى يَوْمَ الْأَحَدِ، فَجَاءَ اللَّهُ بِنَا فَهَدَانَا اللَّهُ لِيَوْمِ الْجُمُعَةِ، فَجَعَلَ الْجُمُعَةَ وَالسَّبْتَ وَالْأَحَدَ، وَكَذَلِكَ هُمْ تَبِعَ لَنَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ نَحْنُ الْآخِرُونَ مِنْ أَهْلِ الدُّنْيَا، وَالْأَوْلُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ الْمُنْفِضِيُّ بَيْنَهُمْ قَبْلَ الْخَلَائِقِ»

"Allah Aliwapoteza wa kabla yetu kwenye Ijumaa. Kwa Wayahudi imekuwa siku ya Jumamosi, na kwa Wakristo imekuwa siku ya Jumapili. Allah Akatuleta sisi na Kutuongoza katika siku ya Ijumaa. Akazifanya; Siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili, na katika mpangilio huo watakuja nyuma yetu katika Siku ya Kiama. Sisi ni wa mwisho katika watu wa dunia na wa kwanza kati ya viumbe kuhukumiwa katika Siku ya Kiama."²

¹ Fath Al-Bari 11:526 na Muslim 2:586.

² Muslim 2:586.

Umuhimu wa Kumtaja Allah تعالى katika Siku ya Ijumaa, kwa Kuhudhuria Khutbah na Sala

Allah تعالى Amewaamuru waumini kukusanyika ili kumuabudu katika siku ya Ijumaa,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ

“Enyi mlioamini! Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: lendeo na kuelekea. Maana ya Sa'iy (kuharakisha) hapa hakumaanishi kutembea haraka. Inamaanisha umuhimu wake tu. 'Umar bin al-Khattab na Ibn Mas'ud - رضي الله عنه - waliisoma;

(فَانضُوا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ)

“nendeni kwenye dhikri ya Allah”¹

Ama kuhusu kutembea upesi katika kuiendea Sala, kwa hakika kumekatazwa, kwa kuwa imenukuliwa katika Sahihi Mbili kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا سَمِعْتُمُ الْإِقَامَةَ فَامْشُوا إِلَى الصَّلَاةِ وَعَلَيْكُمْ السَّكِينَةُ وَالْوَقَارُ وَلَا تُسْرِعُوا، فَمَا أَدْرَأَكُمُ فَصَلُّوا وَمَا فَاتَكُمُ فَأْتِمُوا»

*“Mnaposikia iqamah, iendeeni Sala kwa utulivu na heshima na msiharakisha. Na msali kwa mnachokikuta na mkamilishe mlichokikosa.”*²

Haya ni maneno yaliyoandikwa katika Al-Bukhari. Abu Qatadah amesema, “Tulikuwa katika Sala nyuma ya Mtume ﷺ, akasikia vurumai. Mwishoni mwa Sala, Mtume ﷺ akasema;

«مَا شَأْنُكُمْ»

“Mna nini?”

¹ At-Tabari 23:381.

² Fat'h Al-Bari 2:138 na Muslim 1:420.

Wakasema, 'Tuliharakisha kuja katika Sala.' Mtume ﷺ akasema,

«فَلَا تَفْعَلُوا، إِذَا أَنْتُمْ الصَّلَاةَ فَاْمَشُوا وَعَلَيْكُمْ السَّكِينَةُ فَمَا أَدْرَكْتُمْ فَصَلُّوا وَمَا فَاتَكُمْ فَأَتِمُّوا»

*"Msifanye hivyo. Mnapokuja kusali tembeeni, muwe watulivu. Salini sehemu iliyosalia ya Sala na mkamilishe sehemu mliyoikosa."*¹

Sahihi Mbili zimeikusanya Hadithi hii. Al-Hasan ametoa rai, "Wallah! Kuharakishia Sala hakufanywi kwa miguu. Kwa hakika walikatazwa kuendea Swala bila ya utulivu na heshima. Bali ni kuhusu nyoyo, nia, na unyenyekevu." Qatadah amesema,

فَأَسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ

"...nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu,"

Inamaanisha kuwa mharakisha kuiendea Sala kwa moyo na matendo, na mtembee kuiendea."²

Imependekezwa kwa wenye kuiendea Sala ya Ijumaa kufanya *Ghusl* (kuoga) kabla ya kwenda. Imekusanywa katika Sahihi Mbili kuwa 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا جَاءَ أَحَدُكُمُ الْجُمُعَةَ فَلْيَغْتَسِلْ»

*"Mmoja wenu anapokuja Ijumaa, basi aoge."*³

Sahihi Mbili zimenukuu kuwa Abu Sa'id رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«غُسْلُ يَوْمِ الْجُمُعَةِ وَاجِبٌ عَلَىٰ كُلِّ مُخْتَلِمٍ»

*"Josho la Siku ya Jumu'ah ni Wajib kwa kila mwenye kubaleghe (Muhtalim)."*⁴

¹ *Fat'h Al-Bari* 2:137 na *Muslim* 1:422.

² *At-Tabari* 23:381.

³ *Fat'h Al-Bari* 2:415 na *Muslim* 2:579.

⁴ *Fat'h Al-Bari* 2:415 na *Muslim* 2:580. *Muhtalim* ni mwanamume aliyefikia umri wa baleghe.

Abu Hurayrah رضي الله عنه amesimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

«حَقُّ اللَّهِ عَلَى كُلِّ مُسْلِمٍ أَنْ يَغْتَسِلَ فِي كُلِّ سَبْعَةِ أَيَّامٍ، يَغْسِلُ رَأْسَهُ وَجَسَدَهُ»

“Ni haki ya Allah juu ya kila Muislamu kuoga kila siku saba, kwa kuosha kichwa chake na mwili.”

Muslim aliikusanya Hadithi hii.¹ Jabir رضي الله عنه amesimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

«عَلَى كُلِّ رَجُلٍ مُسْلِمٍ فِي كُلِّ سَبْعَةِ أَيَّامٍ غُسْلُ يَوْمٍ وَهُوَ يَوْمُ الْجُمُعَةِ»

“Katika kila siku saba, kila Muislam anatakiwa kuoga angalau siku moja, nayo ni siku ya Ijumaa.”

Ahmad, An-Nasa'i na Ibn Hibban aliikusanya Hadithi hii.²

Fadhila za Jumu'ah

Imamu Ahmad amenukuu kuwa 'Aws bin 'Aws Ath-Thaqaf رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«مَنْ غَسَّلَ وَاعْتَسَلَ يَوْمَ الْجُمُعَةِ وَبَكَرَ وَابْتَكَّرَ وَمَشَى وَلَمْ يَرْكَبْ، وَدَنَا مِنَ الْإِمَامِ وَاسْتَمَعَ وَلَمْ يَلْغُ، كَانَ لَهُ بِكُلِّ خُطْوَةٍ أَجْرُ سَنَةِ صِيَامِهَا وَقِيَامِهَا»

“Mwenye kuosha (Kichwa chake) na kuoga vizuri katika Siku ya Ijumuaa, na akaenda mapema, na kuwahi hotuba ya mwanzo, akatembea kwa miguu, sio kwa kipando, na akawa karibu na Imamu na akasikiliza bila ya kuzungumza, atapata malipo ya mwaka mzima ya swaumu na kusimama katika Sala na kwa kila hatua anayotembea.”³

Hadithi hii ina isnadi nyingi za usimulizi, wakusanyaji wa Sunan Nne waliikusanya, na At –Tirmidhi aliipa daraja la Hasan.⁴

¹ Muslim 2:582.

² Ahmad 3:304, An-Nasai 3:93, na Ibn Hibban 2:262.

³ Ahmad 4:9.

⁴ Abu Dawud 1:246. 247, Tuhfat Al-Ahwadhi 3:3, An-Nasai 3:95,97, na Ibn Majah 1:246.

Sahihi Mbili pia zimenukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ اغْتَسَلَ يَوْمَ الْجُمُعَةِ غُسْلَ الْجَنَابَةِ ثُمَّ رَاحَ فِي السَّاعَةِ الْأُولَى فَكَأَنَّمَا قَرَّبَ بَدَنَةً، وَمَنْ رَاحَ فِي السَّاعَةِ الثَّانِيَةِ فَكَأَنَّمَا قَرَّبَ بَقَرَةً، وَمَنْ رَاحَ فِي السَّاعَةِ الثَّلَاثَةِ فَكَأَنَّمَا قَرَّبَ كَبْشًا أَقْرَنَ، وَمَنْ رَاحَ فِي السَّاعَةِ الرَّابِعَةِ فَكَأَنَّمَا قَرَّبَ دَجَاجَةً، وَمَنْ رَاحَ فِي السَّاعَةِ الْخَامِسَةِ فَكَأَنَّمَا قَرَّبَ بَيْضَةً، فَإِذَا خَرَجَ الْإِمَامُ حَضَرَتِ الْمَلَائِكَةُ يَسْتَمِعُونَ الذُّكْرَ»

"Mwenye kuoga katika siku ya Ijumaa uogaji wa janaba, akaenda kusali katika saa ya kwanza, ni kama ametoa sadaka ya ngamia. Mwenye kwenda katika saa ya pili, ni kama aliyetoa sadaka ya ng'ombe. Mwenye kwenda katika saa ya tatu, basi ni kama aliyetoa sadaka ya kondoo dume. Mwenye kwenda katika saa ya nne, atakuwa sawa na aliyetoa sadaka ya kuku. Mwenye kwenda katika saa ya tano, ni kama aliyetoa sadaka ya yai. Imamu akishakuja, malaika wanahudhuria kusikiliza dhikri ya Allah."¹

Imependekezwa kuwa mtu ajitwaharishe mwili, aoge, avae nguo nzuri, ajitie manukato na kutumia Siwak (mswaki) kwa ajili ya Jumu'ah. Tulishataja kuwa Abu Sa'id رضي الله عنه amesimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

«غُسْلُ يَوْمِ الْجُمُعَةِ وَاجِبٌ عَلَى كُلِّ مُحْتَلِمٍ وَالسَّوَاكُ وَأَنْ يَمَسَّ مِنْ طَيِّبٍ أَهْلِيهِ»

"Kuoga katika Siku ya Jumu'ah ni Wajib kwa kila aliye balebale na pia kutumia mswaki na kujitia manukato ya nyumbani kwake."²

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Abu Ayyub Al-Ansari رضي الله عنه amesema kuwa alimsikia Mtume ﷺ (akisema),

«مَنْ اغْتَسَلَ يَوْمَ الْجُمُعَةِ وَمَسَّ مِنْ طَيِّبٍ أَهْلِيهِ إِنْ كَانَ عِنْدَهُ وَلَيْسَ مِنْ أَحْسَنِ ثِيَابِهِ ثُمَّ خَرَجَ حَتَّى يَأْتِيَ الْمَسْجِدَ فَيَرْكَعَ إِنْ بَدَأَ لَهُ وَلَمْ يُؤَدِّ أَحَدًا، ثُمَّ أَنْصَتَ إِذَا خَرَجَ إِمَامُهُ حَتَّى يُصَلِّيَ كَمَا نَتَّ كَفَّارَةً لِمَا بَيْنَهَا وَبَيْنَ الْجُمُعَةِ الْأُخْرَى»

¹ Fat'h Al-Bari 2:425 na Muslim 2:582.

² Fat'h Al-Bari 2:423.

"Mwenye kuoga siku ya Ijumaa na kutumia manukato, ikiwa anayo, akavaa nguo zake nzuri zaidi, akaenda Masjid na kusali Sala ya sunna, akitaka, asimsumbue yeyote, na akamsikiliza Imamu anapohutubu na mpaka anaanza Sala. Yote hayo yatakuwa kafara ya baina ya Ijumaa hiyo na inayofuatia."¹

Abu Dawud na Ibn Majah wamenukuu katika *Sunan* zao kuwa 'Abdullah bin Salam رضي الله عنه amesema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema, huku akiwa juu ya Minbar:

«مَا عَلَى أَحَدِكُمْ لَوْ اشْتَرَى ثَوْبَيْنِ لِيَوْمِ الْجُمُعَةِ سِوَى ثَوْبَيْنِ مِهْنَتِهِ»

"Kuna ubaya gani kama mmoja wenu amenunua nguo mbili kwa ajili ya Siku ya Jumu'ah, zisizokuwa anazovaa kila siku."²

'A'ishah رضي الله عنها amesema kuwa Mtume ﷺ aliwahutubia watu siku ya Ijumaa, alipowaona watu waliovaa nguo za *Nimar*,³ Mtume ﷺ alisema,

«مَا عَلَى أَحَدِكُمْ إِنْ وَجَدَ سَعَةً أَنْ يَتَّخِذَ ثَوْبَيْنِ لِيَوْمِ الْجُمُعَةِ سِوَى ثَوْبَيْنِ مِهْنَتِهِ»

"Mmoja wenu anapokuwa na mali, awe na nguo mbili kwa ajili ya Ijumaa, zisizokuwa nguo mbili alizozoea kuvaa kila siku."

Ibn Majah aliikusanya Hadithi hii.⁴

Maana ya Wito katika Ayah ni Adhana Inayotangulia Khutbah

Kauli ya Allah تعالى،

إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ

"Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa,"

Inamaanisha adhana inayosomwa ni ya pili ambayo, katika wakati wa Mtume ﷺ, pindi alipotoka nje ya nyumba yake na kukaa juu ya Minbar. Adhana ilikuwa ikisomwa mbele ya Mtume ﷺ karibu na mlango wa Masjid. Ama kuhusu

¹ Ahmad 5:420.

² Ahmad 1:650 na Ibn Majah 1:348.

³ Namna ya joho ambalo Waarabu huvaa.

⁴ Ibn Majah 1:349.

Adhana ya kwanza aliyoongeza Amiri wa waumini, 'Uthman bin Affan رضي الله عنه ilikuwa hivyo, kwa sababu Waislamu waliongezeka idadi katika zama zake. Al-Bukhari amenukuu kuwa As-Sa'ib bin Yazid amesema, "Katika wakati wa uhai wa Mtume ﷺ, Abubakr na 'Umar رضي الله عنهما, adhana ya sala ya Ijumaa ilikuwa ikisomwa huku Imamu akiwa amekaa katika mimbari. Lakini wakati wa 'Uthman رضي الله عنه pindi Waislamu walipoongezeka idadi, wito wa ziada ulisomwa katika Az-Zawra', yaani *adhana* ilikuwa ikisomwa katika nyumba iliyokuwa ikiitwa Az-Zawra.'"¹

Az-Zawra' ilikuwa nyumba ndefu zaidi huko Al-Madinah karibu na Masjid.

Kukatazwa Kununua na Kuuza Baada ya Wito wa Ijumaa, na Himizo la Kutafuta Riziki Baada yake

Kauli ya Allah تعالى،

وَذُرُوا الْبَيْعَ

"...na wacheni biashara."

Maana yake: Kuharakisha kumtaja Allah تعالى na kuacha biashara, pindi wito wa Swala ya Ijumaa unapofanyika. Kwa hiyo, wanazuoni wa Kiislamu wanaafikiana, 'Waislamu wamekatakazwa kufanya miamala ya kibiashara baada ya Adhana ya pili.' Kauli ya Allah تعالى،

ذَالِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ

"Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua."

Maana yake: 'Kuacha kwenu kununua na kuuza, na badala yake, kuzingatia jambo la kumtaja Allah تعالى na Sala ni bora zaidi kwenu duniani na Akhera, kama lakini mnajua.' Kauli ya Allah تعالى،

فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ

"Na itakapo kwisha Sala."

Maana yake: Sala ya Ijumaa inapokamilika.

¹ Fat'h Al-Bari 2:457.

فَاتْتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا مِنْ فَضْلِ اللَّهِ

“...tawanyikeni katika nchi mtafute Fadhila za Mwenyezi Mungu.”

Baada ya Allah تعالی Kuwakataza Waislamu kufanya kazi baada ya kusikia adhana na Kuwaamrisha Kukusanyika kwa ajili ya Sala ya Ijumaa, Aliwaruhusu kutawanyika ardhini na kutafuta neema baada ya kumalizika Sala. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی amenukuu kuwa Sala ya Ijumaa ilipomalizika, 'Irak bin Malik alikuwa akisimama katika mlango wa Masjid na kuomba dua kwa kusema, “Ewe Allah تعالی! Nimeitikia na kufuata Wito Wako, na kusali Sala Uliyoanimrisha na kutawanyika kama Ulivyoni amrisha. Kwa hivyo, nipe Fadhila Zako na Wewe ni Mbora zaidi katika wenye kutoa riziki.”¹

Kauli ya Allah تعالی,

وَأَذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ

“...na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa.”

Inamaanisha ilhali mkiwa mnanunua na kuuza, kutoa na kuchukua, kumkumbuka sana Allah تعالی na msiiachilie dunia ikushughulisheni dhidi ya manufaa yenu ya Akhera.

Kuna Hadithi inayoeleza,

«مَنْ دَخَلَ سُوقًا مِنَ الْأَسْوَاقِ فَقَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، كَتَبَ اللَّهُ لَهُ أَلْفَ حَسَنَةٍ وَمَعَهَا عَنَّةُ أَلْفِ أَلْفِ سَيِّئَةٍ»

“Mwenye kuingia sokoni na kusema, “La ilaha illallah, Peke Yake, na hana mshirika, Utukufu ni Wake na Sifa Njema zote ni Zake, Yeye ni Muweza wa kila kitu.” Allah Atamuandikia mema maelfu kwa maelfu na kumfutia maovu maelfu kwa maelfu.”²

¹ Al-Qurtubi 18:108.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:386. Wanazuoni wengi huiona Hadithi hii kuwa si sahihi. Al-Hakim, Ash-Shawkani, Ibn Taymiyah na Al-Albani ni miongoni mwenye kuichukulia kuwa inakubalika.

Mujahid amesema, "Mja (wa Allah) hatakuwa katika wenye kumtaja Allah تعالى mara kwa mara, isipokuwa mpaka atakapofanya hivyo huku akiwa katika kusimama, kukaa na kulala."

وَإِذَا رَأَوْا تِجْرَةً أَوْ هَمَّوْا أَنْفَضُوا إِلَيْهَا وَتَرَكُوكَ قَائِمًا قُلْ مَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ مِنَ اللَّهِو وَمِنَ
التِّجْرَةِ وَاللَّهُ خَيْرُ الرَّازِقِينَ ﴿١١﴾

11. Na wanapoiona biashara au pumbao wanayakimbilia hayo na wakakuacha umesimama. Sema: Yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko pumbao na biashara. Na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa watoa riziki.

Kukatazwa Kuondoka Masjid Wakati Imamu Anahutubu

Inakosoa kilichotokea wakati wa hotuba ya Ijumaa moja, msafara ulipowasili Al-Madinah na watu wakakimbilia biashara.

Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذَا رَأَوْا تِجْرَةً أَوْ هَمَّوْا أَنْفَضُوا إِلَيْهَا وَتَرَكُوكَ قَائِمًا

"Na wanapoiona biashara au pumbao wanayakimbilia hayo na wakakuacha umesimama."

Inamaanisha, juu ya *Minbar*, kutoa Khutbah. *Tabi'n* wengi wanafuata kauli hiyo, kama vile Abu Al-'Aliyah, Al-Hasan, Zayd bin Aslam na Qatadah.¹

Muqatil bin Hayyan wamesema kuwa msafara huo ulikuwa wa Dihyah bin Khalifah kabla hajasilimu, na alikuwa na ngoma. Kwa hivyo, waliukimbilia msafara huo na kumuacha Mtume ﷺ akiwa amesimama juu ya *Minbar*. Watu wachache tu walibakia, kwa mujibu wa Hadithi sahihi kuwa Imamu Ahmad amenukuu kuwa Jabir رضي الله عنه amesema, "Siku moja, msafara ulifika Al-Madinah huku Mtume ﷺ akitoa Khutbah. Watu wakaondoka, na watu kumi na wawili tu ndio waliobakia pamoja na Mtume ﷺ."

¹ At-Tabari 23:387.

Kisha Allah تعالى Aliteremsha Aya hii,

وَإِذَا رَأَوْا تِجْرَةً أَوْ هَمَّوْا أَنْفَضُوا إِلَيْهَا

“Na wanapoiona biashara au pumbao wanayakimbilia hayo...”¹

Sahihi Mbili pia zimenukuu Hadithi hii.²

Kauli ya Allah تعالى,

وَتَرَكُوكَ قَائِمًا

“...na wakakuacha umesimama.”

Inathibitisha kuwa Imamu anapaswa kutoa hutuba ya Ijumaa akiwa amesimama. Katika Sahih yake, Imamu Muslim amenukuu kuwa Jabir bin Samurah رضي الله عنه amesema, “(Wakati wa *Jumu'ah*.) Mtume ﷺ alitoa hotuba mbili, na alikuwa akikaa katikati yao. Mtume ﷺ alikuwa akisoma Qur'an na kuwakumbusha watu (kuhusu Allah تعالى).”³ Kauli ya Allah تعالى,

قُلْ مَا عِنْدَ اللَّهِ

“Sema: Yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Malipo yaliyoko kwa Allah تعالى.

خَيْرٌ مِّنَ اللَّهِ وَوَمِنَ الشَّجَرَةِ وَاللَّهُ خَيْرُ الرَّزَاقِينَ

“Ni bora kuliko pumbao na biashara. Na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa watoa riziki.”

Inamaanisha kwa ajili ya wenye kumtumaini na kutafuta riziki Zake wanaporuhusiwa kufanya hivyo.

Huu ni mwisho wa *Tafsiri ya Surat Al-Jumu'ah*. Kila sifa njema na shukrani Anastahiki Allah تعالى na kutoka Kwake hupatikana mafanikio na kuepukana na makosa.



¹ Ahmad 3:313.

² *Fat'h Al-Bari* 8:511 na Muslim 2:590.

³ Muslim 2:589 katika Akhera.

Tafsiri ya Suratul Munafiqun

Sura ya 63

Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمُنَافِقُونَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِذَا جَاءَكَ الْمُنَافِقُونَ قَالُوا نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ لَرَسُولُهُ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَكَاذِبُونَ ﴿١﴾
 أَخَذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢﴾
 ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ ءَامَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا فَطُبِعَ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٣﴾ * وَإِذَا رَأَيْتَهُمْ تُعْجِبُكَ أَجْسَامُهُمْ ۗ وَإِنْ يَقُولُوا تَسْمَعُ لِقَوْلِهِمْ ۗ كَأَنَّهُمْ خُشْبٌ مُّسْنَدَةٌ ۗ يَحْسَبُونَ كُلَّ صَيْحَةٍ عَلَيْهِمْ ۗ هُمُ الْعَدُوُّ فَاحْذَرْهُمْ ۗ قَتَلَهُمُ اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ هُمُ الْكَاذِبُونَ ﴿٤﴾

إِذَا جَاءَكَ الْمُنَافِقُونَ قَالُوا نَشْهَدُ
 إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ
 لَرَسُولُهُ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ
 لَكَاذِبُونَ ﴿١﴾ أَخَذُوا أَيْمَانَهُمْ
 جُنَّةً فَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ إِنَّهُمْ
 سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢﴾ ذَلِكَ
 بِأَنَّهُمْ ءَامَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا فَطُبِعَ عَلَى
 قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٣﴾ * وَإِذَا
 رَأَيْتَهُمْ تُعْجِبُكَ أَجْسَامُهُمْ ۗ وَإِنْ
 يَقُولُوا تَسْمَعُ لِقَوْلِهِمْ ۗ كَأَنَّهُمْ
 خُشْبٌ مُّسْنَدَةٌ ۗ يَحْسَبُونَ كُلَّ صَيْحَةٍ عَلَيْهِمْ ۗ

هُمُ الْعَدُوُّ فَاحْذَرْهُمْ ۗ قَتَلَهُمُ اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ هُمُ الْكَاذِبُونَ ﴿٤﴾

1. Wanapokujia wanafiki husema: Tunashuhudia ya kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anajua kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Anashuhudia ya kuwa hakika wanaafiki ni waongo.

2. Wamevifanya viapo vyao ni kinga, na wao wakajizua kuifuata Njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika ni mabaya kabisa waliyokuwa wakiyafanya.

3. Hayo ni kwa sababu ya kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo umepigwa muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawafahamu lolote.

4. Na unapowaona, miili yao inakupendeza, na wakisema, unasiliza usemi wao. Lakini wao ni kama magogo yaliyo egemezwa. Wao hudhania kila ukelele unaopigwa ni kwa ajili yao. Hao ni maadui; tahadhari nao. Mwenyezi Mungu Awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki?

Hali ya Wanafiki na Tabia Zao

Allah تعالى Anaeleza kuwa wanafiki walijifanya kuwa ni Waislamu walipomuendea Mtume ﷺ. Kiukweli, hawakuwa Waislamu, bali kinyume chake. Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

إِذَا جَاءَكَ الْمُنَافِقُونَ قَالُوا نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ

“Wanapokujia wanaafiki husema: Tunashuhudia ya kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: ‘Wanafiki wanapokujia kwako, wanatamka Kauli yake na kujidai kuiamini.’ Allah تعالى Anafahamisha kuwa hakuna ukweli wa Kauli yao, na ndio sababu Akasema,

وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ لَرَسُولُهُ

“Na Mwenyezi Mungu Anajua kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.”

Akasema,

وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَكَاذِبُونَ

“...na Mwenyezi Mungu Anashuhudia ya kuwa hakika wanafiki ni waongo.”

Maana yake: Katika walioyaeleza japokuwa kwa nje yanakubaliana na hali halisi. lakini hawakuamini kuswihi kile wanachokieleza wala ukweli wake, na ndio sababu Allah تعالی Akatangaza uongo wa itikadi yao. Kauli ya Allah تعالی,

أَتَّخِذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

“Wamevifanya viapo vyao ni kinga, na wao wakajizua kuifuata Njia ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Wanafiki wanajikinga dhidi ya Waislamu wanapoapa kiapo cha uongo cha dhambi ilhali si wakweli. Baadhi ya Waislamu walidanganyika kwa kuwa hawakuujua uongo wao, wakawadhania kuwa wao ni Waislamu. Baadhi ya Waislamu waliwaamini walichokisema na hata kuwaiga tabia zao za nje. Hata hivyo, kiundani, wanafiki walitaka kuuangamiza Uislamu na Waislamu, na ndio sababu kuwaamini kungewadhuru sana watu.

Kwa ajili hiyo, Allah تعالی Akasema,

فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“...wakajizua kuifuata Njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika ni mabaya kabisa waliyokuwa wakiyafanya.”¹

Kauli ya Allah تعالی,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ ءَامَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا فَطُبِعَ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ

“Hayo ni kwa sababu ya kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo umepigwa muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawafahamu lolote.”

Inamaanisha, Amewahukumu kuwa ni wanafiki kwasababu wameritadi kutoka katika imani kwenda kwenye ukafiri na kuuacha uongofu kwa ajili ya upotovu. Kwa hiyo, Allah تعالی Alipiga muhuri nyoyo zao na kwa ajili hiyo, hawataweza kuufahamu uongofu, wala jema lolote kuzifikia nyoyo zao. Kiukweli, nyoyo zao hazitafahamu, wala hazitapata uongofu. Kauli ya Allah تعالی,

¹ At-Tabari 23:394.

وَإِذَا رَأَيْتَهُمْ تُعْجِبُكَ أَجْسَامُهُمْ ۖ وَإِنْ يَقُولُوا تَسْمَعُ لِقَوْلِهِمْ ۗ

“Na unapowaona, miili yao inakupendeza, na wakisema, unasikiliza usemi wao.”

Maana yake: Wanafiki wana muonekano mzuri wa juujuu na wana ufasaha. Mtu akiwasikia wakizungumza, atawasikiliza maneno yao fasaha, ingawa wanafiki kiukweli ni dhaifu, hafifu, wamejaa hofu, kutishika na woga. Kauli ya Allah تعالى،

تَحْسَبُونَ كُلَّ صَيْحَةٍ عَلَيْهِمْ ۗ

“Wao hudhania kila ukelele unaopigwa ni kwa ajili yao.”

Inamaanisha kila linapotokea tukio au jambo la kutisha, hudhania kuwa linaelekea kwao. Hii ni dalili ya woga wao, kama alivyosema Allah تعالى kuhusu wao،

أَشِحَّةً عَلَيْكُمْ ۗ فَإِذَا جَاءَ الْخَوْفُ رَأَيْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ تَدُورُ أَعْيُنُهُمْ كَالَّذِي يُغْشَىٰ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۗ فَإِذَا ذَهَبَ الْخَوْفُ سَلَقُوكُمْ بِأَلْسِنَةٍ حِدَادٍ أَشِحَّةً عَلَى الْخَيْرِ ۗ أُولَٰئِكَ لَا يُؤْمِنُوا فَأَحْبَبَ اللَّهُ أَنْ يَمْلَأَهُمْ ۗ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٦٣﴾

“Wana choyo juu yenu. Ikifika khofu utawaona wanakutazama na macho yao yanazunguka, kama yule ambaye aliyezimia kwa kukaribia mauti. Na khofu ikiondoka wanakuudhini kwa ndimi kali, nao ni mabakhili kwa kila la kheri. Hao hawakuamini, basi Mwenyezi Mungu Amevibat’ilisha vitendo vyao. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.”

Wao ni maumbo yasiyo na kitu, na kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema،

هُرُّ الْعَدُوِّ فَاحْذَرُهُمْ ۗ قَتَلَهُمُ اللَّهُ ۗ أَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ

“Hao ni maadui; tahadhari nao. Mwenyezi Mungu Awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki?”

Inamaanisha jinsi walivyopotoshwa, mbali na uongofu. Imamu Ahmad amemnukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema،

«إِنَّ لِلْمُنَافِقِينَ عَلَامَاتٍ يُعْرَفُونَ بِهَا: تَحِيَّتُهُمْ لَعَنَهُ وَطَعَامُهُمْ نُهْبَةٌ وَغَنِيمَتُهُمْ غُلُولٌ لَا يَقْرَبُونَ الْمَسَاجِدَ إِلَّا مَهْجَرًا، وَلَا يَأْتُونَ الصَّلَاةَ إِلَّا دُبْرًا، مُسْتَكْبِرِينَ لَا يَأْتُونَ وَلَا يُؤْتُونَ، خُسْبٌ بِاللَّيْلِ صُحْبٌ بِالنَّهَارِ - وَفِي رِوَايَةٍ - سُحْبٌ بِالنَّهَارِ»

“Hakika wanafiki wana alama ambazo hujulikana kwazo. Salamu zao ni laana, chakula chao ni cha wizi na ngawira wanazokusanya ni za wizi. Hukwepa Masjid na hawaji katika Swala isipokuwa mwishoni. Wao ni wajeuri; si rahisi sana kwao kuchanganyika na watu, wala si rahisi kwa watu kuchanganyika nao. Wao ni kama vipande vya mbao wakati wa usiku na wana kelele wakati wa mchana.”¹

* * *

¹Ahmad 2:293. Pia imeandikwa na Al-Bazzar. Ndani yake kuna msimuliaji ambaye wanazuoni wengi humchukulia kuwa hakubaliki, yuko peke yake katika masimulizi haya, na ndiye pekee anayesimulia kutoka kwa mtu anayesema kuwa alimsikia. Kwa sababu hizo, Ibn Hibban aliyaweka masimulizi haya katika *Al-Majruhin*, huku akisema kuwa hairuhusiwi kumtumia huyo kwa uthibitisho.

Wanafiki Hawapendi Mtume ﷺ Awaombe Msamaha Kwa Allah تعالی

Kauli ya Allah تعالی

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُولُ اللَّهِ لَوَّأَ رُءُوسَهُمْ
 وَرَأَيْتَهُمْ يَصُدُّونَ وَهُمْ مُسْتَكْبِرُونَ ﴿٥﴾ سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ
 أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ لَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ
 لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٦﴾ هُمُ الَّذِينَ يَقُولُونَ لَا
 تُنْفِقُوا عَلَيَّ مِنْ عِنْدِ رَسُولِ اللَّهِ حَتَّىٰ يَنْفَضُوا ۗ وَاللَّهُ
 خَزَائِنُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَفْقَهُونَ
 ﴿٧﴾ يَقُولُونَ لِنِ رَجَعْنَا إِلَى الْمَدِينَةِ لِيُخْرِجَنَا الْأَعْرُ
 مِنْهَا الْأَذَلَّ ۗ وَاللَّهُ الْعَزِيزُ الرَّسُولِ ۗ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَكِنَّ
 الْمُنَافِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨﴾ يَتَأَيَّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا
 تُلْهِكُمْ أَمْوَالِكُمْ وَلَا أَوْلَادِكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ يَفْعَلْ
 ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٩﴾ وَأَنْفِقُوا مِنْ مَا
 رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ
 لَوْلَا أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَقَ ۗ وَأَكُن مِّنَ
 الصَّالِحِينَ ﴿١٠﴾ وَلَنْ يُؤَخَّرَ اللَّهُ نَفْسًا إِذَا جَاءَ أَجَلُهَا ۗ وَاللَّهُ
 خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١١﴾

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُولُ اللَّهِ لَوَّأَ رُءُوسَهُمْ وَرَأَيْتَهُمْ يَصُدُّونَ وَهُمْ مُسْتَكْبِرُونَ ﴿٥﴾ سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ لَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٦﴾ هُمُ الَّذِينَ يَقُولُونَ لَا تُنْفِقُوا عَلَيَّ مِنْ عِنْدِ رَسُولِ اللَّهِ حَتَّىٰ يَنْفَضُوا ۗ وَاللَّهُ خَزَائِنُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٧﴾ يَقُولُونَ لِنِ رَجَعْنَا إِلَى الْمَدِينَةِ لِيُخْرِجَنَا الْأَعْرُ مِنْهَا الْأَذَلَّ ۗ وَاللَّهُ الْعَزِيزُ الرَّسُولِ ۗ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨﴾

5. Na wanapoambiwa: Njooi ili Mtume wa Mwenyezi Mungu Akuombeeni maghira, huvigeza vichwa vyao, na unawaona wanageuka nao wamejaa kiburi.

6. Sawa sawa kwao, ukiwatakia maghfira au hukuwatakia maghfira, Mwenyezi Mungu Hatawaghufiria. Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wapotovu.

7. Hao ndio wanaosema: Msitoe mali kwa ajili ya walioko kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ili waondokelee mbali! Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye khazina za mbingu na ardhi, lakini wanafiki hawafahamu.

8. Wanasema: Tukirejea Madina mwenye utukufu zaidi bila ya shaka atamfukuza aliye mnyonge. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Utukufu - Yeye, na Mtume Wake, na Waumini. Lakini wanafiki hawajui.

Allah تعالى Anaeleza kuhusu wanafiki, Allah تعالى Awalaani,

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُولُ اللَّهِ لَوَّأَ رُءُوسَهُمْ

“Na wanapoambiwa: Njooi ili Mtume wa Mwenyezi Mungu Akuombeeni maghfira, huvigeuza vichwa vyao.”

Inamaanisha, wanageuka na kuacha wito kwa ujeuri na kwa kudharau walichoitiwa.

Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

وَرَأَيْتُهُمْ يَصُدُّونَ وَهُمْ مُسْتَكْبِرُونَ

“...na unawaona wanageuka nao wamejaa kiburi.”

Allah تعالى Amewaadhibu kwa sababu ya tabia hiyo, kwa kusema,

سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ لَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ

الْفٰسِقِينَ ﴿٦٣﴾

“Sawa sawa kwao, ukiwatakia maghfira au hukuwatakia maghfira, Mwenyezi Mungu Hatawaghufiria. Hakika Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu wapotovu.”

Sawa na Kauli ya Allah ﷻ katika *Surat Bara'ah*, na maelezo yake yaliyofuatia huko,¹ na hapa tutaleta baadhi ya Hadithi zinazoeleza hilo.

Salaf wengi wanataja kuwa Aya yote hiyo ilishuka kumhusu 'Abdullah bin Ubay bin Salul, kama tutakavyoeleza hivi punde, Allah ﷻ Akipenda na tunamtumaini na kumtegemea Yeye.

Katika kitabu chake, *As-Sirah*, Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى amesema, "Baada ya kuisha vita vya Uhud, Mtume ﷺ alirejea Al-Madinah. 'Abdullah bin Ubay bin Salul – kama Ibn Shihab alivyonisimulia – alikuwa akisimama katika kila siku ya Ijumaa, bila ya kupingwa na yeyote kwa sababu alikuwa kiongozi wa watu wake, Mtume ﷺ alikuwa akikaa juu ya *Minbar*, kabla kidogo ya kuwahutubia watu Jumu`ah. 'Abdullah bin Ubay alikuwa akisema, `Enyi watu! Huyu ni Mtume wa Allah kwenu. Allah ﷻ Ametutukuza kwa kumtuma na Ametupa nguvu kupitia kwake. Msaidieni, muheshimuni na mumsikilize na kumtii.' Halafu alikuwa akiketi chini. Kwa hivyo baada ya vita vya Uhud, hata baada ya kufanya aliyoyafanya, alirejea Al-Madinah pamoja na theluthi ya Jeshi, alisimama na kukariri maneno yale yale. Lakini Waislamu walimshika nguo zake na kumuambia, 'Kaa chini, ewe adui wa Allah! Wewe hustahiki kusimama baada ya yale uliyoyafanya.' 'Abdullah alitoka nje ya Masjid kwa kukatisha safu za watu huku akisema, 'Wallahi!, utadhani nimesema jambo baya ilhali nilitaka kumsaidia.' Baadhi ya watu katika Al-Ansar walikutana naye katika mlango wa Masjid na kumuuliza yaliyotokea. Akasema, 'Nilisimama tu na kumsaidia lakini baadhi ya watu, Masahaba wake رضي الله عنهم, walinirukia, wakanivuta na kunionya, kana kwamba nilisema jambo baya; nilitaka tu kumsaidia.' Wakamuambia, `Ole wako! Rudi ili Mtume akuombe msamaha kwa Allah ﷻ.' Akasema, 'Wallahi!, Sina haja ya yeye kumwomba Allah ﷻ Anisamehe.'"²

Qatadah na As-Suddi wamesema, "Aya hii ilishuka kumhusu 'Abdullah bin Ubay. Mdogo wake alimuendea Mtume ﷺ na kumfikishia maneno mabaya aliyoyasema Abdullah. Mtume ﷺ alimuita 'Abdullah, aliapa kwa Allah ﷻ kuwa hakusema chochote. *Ansar* walimuendea kijana huyo na kumuonya. Hata hivyo, Allah ﷻ Aliteremsha mlichosikia kuhusu suala la 'Abdullah na adui

¹ Angalia juzu ya nne, *Tafsir ya Surat At-Tawbah* (9:80).

² Ibn Hisham 3:111.

wa Allah akaambiwa, `Nenda kwa Mtume ﷺ, 'lakini aligeuza kichwa chake, na kusema kuwa hatafanya hivyo."¹

Yunusu bin Bukair amesema kutoka kwa Muhammad bin Ishaq amesema kuwa Muhammad bin Yahya bin Hibban, 'Abdullah bin Abi Bakr na 'Asim bin 'Umar bin Qatadah walimsimulia kisa cha Bani Al-Mustaliq. Wakasema kuwa Mtume ﷺ alipokuwa katika sehemu hiyo, Jahjah bin Sa'id Al-Ghifari, mfanyakazi wa 'Umar, na Sinan bin Wabr walipigania chanzo cha maji. Sinan akaita, "Enyi *Ansar*", ilhali Al-Jahjah aliita, "Enyi *Muhajirin!*"

Zayd bin Arqam na watu kadhaa katika Ansar walikuwa wamekaa pamoja na 'Abdullah bin Ubay bin Salul wakati huo. 'Abdullah aliposikia yaliyotokea, akasema, "Wanatusumbua katika ardhi yetu. Wallahi! Mfano wetu na Makuraishi hawa wapumbavu, ni mfano wa, 'Mliseni mbwa wenu mpaka apate nguvu, na atakuumeni.' Wallahi! Tutakaporejea Madinah, mwenye nguvu atamfukuza mnyonge kutoka huko." Akawaambia watu wake waliokuwa wamekaa pamoja naye, kwa kuwaambia, "Mmefanya nini? Mmewaacha wakae katika ardhi yenu na kugawana nao mali zenu. Wallahi! Kama mtawaacha wataondoka kwenda kwingine badala ya kwenu." Zayd bin Arqam alisikia maneno haya na akamfikishia Mtume ﷺ. Zayd alikuwa bado kijana mdogo. 'Umar bin al-Khattab رضي الله عنه alikuwa pamoja na Mtume ﷺ na alisema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Muamuru 'Abbad bin Bishr amkate kichwa chake shingoni mwake." Mtume ﷺ akamjibu,

«فَكَيْفَ إِذَا تَحَدَّثَ النَّاسُ يَا عُمَرُ أَنْ مُحَمَّدًا يُنْتَلِ أَصْحَابَهُ، لَا، وَلَكِنْ نَادَى يَا عُمَرُ
الرَّحِيلَ»

"Itakuwaje watu wakihadithiana kuwa Muhammad anawaua Masahaba wake, Ewe 'Umar, Hapana. Hata hivyo, waamrishe watu waanze safari (ya kurudi Madinah)."

'Abdullah bin Ubay bin Salul alipoambiwa kuwa kauli yake imemfikia Mtume ﷺ, alimwendea na kukana alichosema. Aliapa kwa Allah تعالى kuwa hakusema maneno aliyofikisha Zayd bin Arqam. 'Abdullah bin Ubay alikuwa kiongozi wa

¹ At-Tabari 23:399.

watu wake na wakasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Huenda kijana hakisikia vyema yaliyosemwa.” Mtume ﷺ alianza safari katika muda wa kawaida na kukutana na Usayd bin al-Hudhayr, ambaye alimsalimia kwa kukiri utume wake. Usayd رضي الله عنه akasema, “Wallah! Unakaribia kuanza safari katika wakati usio wa kawaida.” Mtume ﷺ akamuambia,

«أَمَا بَلَغَكَ مَا قَالَ صَاحِبِكَ ابْنُ أَبِي؟ زَعَمَ أَنَّهُ إِذَا قَدِمَ الْمَدِينَةَ سَيُخْرِجُ الْأَعْرَضَ مِنْهَا
الْأَذَلَّ،

“Kwani maneno ya rafiki yako, Ibn Ubay hayajakufikia alipodai kuwa atakaporejea Madinah, mwenye nguvu atamfukuza mnyonge.”

Usayd رضي الله عنه akasema, “Kwa hakika, wewe ndio mwenye nguvu, Ewe Mjumbe wa Allah, na yeye ni mwenye fedheha.” Usayd رضي الله عنه akasema, “Mfanyie subira, Ewe Mjumbe wa Allah! Wallah! Allah تعالى Alipokuleta wewe kwetu, tulikaribia kukusanya lulu (za taji) ili tumchague awe mfalme wetu. Anadhani kuwa umemuondolea ufalme.” Mtume ﷺ alisafiri pamoja na watu mpaka usiku ukaingia, kisha sehemu ya usiku huo mpaka mwanzoni mwa mchana ulifuatia akapiga kambi pamoja na watu. Alitaka kuwashughulisha ili wasizungumzie kilichotokea. Baada tu ya watu kushuka chini, walikwenda kulala na *Suratu Al-Munafiqin* ikashuka.¹

Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bayhaqi رحمه الله تعالى amemnukuu Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنه kuwa amesema, “Tulikuwa katika vita pamoja na Mtume ﷺ na mtu mmoja katika Muhajirin alimpiga teke mtu mmoja katika Ansari. Ansari huyo akaita, ‘Enyi *Ansar!* Na yule mtu katika Muhajir naye aliita, ‘Enyi *Muhajirin!*’ Mtume ﷺ alisikia na kusema,

«مَا بَالُ دَعْوَى الْجَاهِلِيَّةِ؟ دَعْوَاهَا فَإِنَّهَا مُنْتَبَهَةٌ

“Wito gani huu wa Jahiliyyah! Uacheni kwani huo ni uvundo.”

‘Abdullah bin Ubay alisikia na kusema, ‘Kwani wao (Muhajirin) wamefanya hivyo, Wallahi! Tutakaporejea Madina, mtukufu zaidi atamfukuza mnyonge.” Ansar kwa wakati huo, walikuwa wengi kuliko Muhajirin wakati Mtume ﷺ alipokuja Madinah, lakini baadaye *Muhajirin* waliongezeka idadi. Kauli yake

¹ Ibn Hisham 2:290-292.

ilipomfikia Mtume ﷺ, 'Umar رضي الله عنه alisimama na kusema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Niruhusu nikate kichwa cha mnafiki huyu! ' Mtume ﷺ akamuambia:

«ذَعْدُ، لَا يَتَحَدَّثُ النَّاسُ أَنْ مُحَمَّدًا يَقْتُلُ أَصْحَابَهُ»

*"Muache, watu wasije kusema kuwa Muhammad anaua Masahaba wake."*¹

Imamu Ahmad,² Al-Bukhari na Muslim³ wameikusanya Hadithi hii. 'Ikrimah na Ibn Zayd na wengine wamesema kuwa Mtume ﷺ na Masahaba wake waliporejea Madina, 'Abdullah, mwana wa 'Abdullah bin Ubay bin Salul, alibakia katika lango la Madina huku ameshikilia panga. Watu walipita karibu yake walipokuwa wakirejea Madinah, halafu baba yake akaja. 'Abdullah, mwana wa 'Abdullah, akamuambia baba yake, "Bakia hapo hapo ulipo." Na baba yake akamuuliza sababu, mwanaye akamjibu, "Wallahi! Hutapita hapa isipokuwa mpaka Mtume ﷺ akuruhusu kufanya hivyo, kwani yeye ni Mtukufu zaidi ilhali wewe umefedheheka." Mtume ﷺ alipofika, na alikuwa katika safu za mwisho, 'Abdullah bin Ubay alimlalamikia kuhusu mwanaye akasema, "Wallahi, Ewe Mjumbe wa Allah! hataingia isipokuwa mpaka useme wewe." Mtume ﷺ akamruhusu 'Abdullah bin Ubay na mwanaye akasema, "Sasa ingia, kwani Mtume ﷺ amekuruhusu."⁴

Katika Musnad wake, Abu Bakr 'Abdullah bin az-Zubayr Al-Humaydi رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Abu Harun Al-Madani kuwa 'Abdullah, mwana wa 'Abdullah bin Ubay bin Salul, alimuambia baba yake, "Hutaingia Madinah mpaka useme, 'Mtume ﷺ ni Mtukufu na mimi ni dhalili." Mtume ﷺ alipofika, 'Abdullah, mwana wa 'Abdullah bin Ubay bin Salul alimuambia, "Ewe Mjumbe wa Allah! Niliambiwa kuwa umeamua kuwa baba yangu auliwe. Ninaapa kwa Aliyekutuma pamoja na Ukweli, sikumuangalia usoni mwake kwa sababu ya kumheshimu. Lakini ukitaka, nitakuletea kichwa chake, kwa sababu sitapenda kumuona atakayemuua baba yangu."⁵

¹ Dalail An-Nubuwwah 4:53.

³ Ahmad 3:392.

³ Al-Bukhari na. 4907, Muslim na. 2584.

⁴ At-Tabari 23:403, 405.

⁵ Musnad Al-Humaydi 2:520.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُمْ ءَمْوَالُكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ ؕ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ
فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٥﴾ وَأَنْفِقُوا مِنْ مَّا رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ أَحَدَكُمُ
الْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَا أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُن مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٦﴾
وَلَنْ يُؤَخِّرَ اللَّهُ نَفْسًا إِذَا جَاءَ أَجَلُهَا ؕ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٧﴾

9. Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio waliopata khasara.

10. Na toeni katika Tulichokupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola Wangu Mlezi! Hunicheleweshi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?

11. Wala Mwenyezi Mungu Hataiakhirisha nafsi yoyote inapofika ajali yake; na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda.

Msisitizo wa Kuacha Kuipa Dunia Kipaumbele na Kutoa Sadaka Kabla ya Mauti

Allah تعالیٰ Anawaamuru waumini Kumtaja mara kwa mara na Anakataza kushughulika zaidi na mali na watoto. Allah تعالیٰ Anawaambia kuwa wenye kuishughulikia sana dunia, anasa zake na kuacha kumtii na kumtaja Allah تعالیٰ ambalo ndio lengo la kuumbwa kwao, watakuwa wenye hasara. Watapata hasara yao wenyewe na familia zao katika Siku ya Kiama.

Allah تعالیٰ Anahimiza waumini kutoa mali katika njia Yake,

وَأَنْفِقُوا مِنْ مَّا رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَا أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ
أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُن مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٦﴾

“Na toeni katika Tulichokupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola Wangu Mlezi! Hunicheleweshi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?”

Kwa hakika, kila mtu mwenye kuangukia katika kushindwa kwake atajuta wakati wa kifo chake na ataomba muda zaidi, japo kidogo, ili afanye vyema na kupata alichokikosa. Hapana, bali kilichotokea kimeshatokea, na kijacho, kwa hakika kitakuja. Kila mmoja atahesabiwa makosa yake.

Ama kuhusu makafiri, watakuwa kama Alivyosema Allah تعالى،

وَأَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ فَيَقُولُ الَّذِينَ ظَلَمُوا رَبَّنَا أَخِّرْنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ نَجْتِ
دَعْوَتَكَ وَتَتَّبِعِ الرَّسُولَ ۗ أَوْلَمْ تَكُونُوا أَقْسَمْتُمْ مِّن قَبْلُ مَا لَكُم مِّن زَوَالٍ ﴿٤٤﴾

“Na waonye watu siku itapowajia adhabu, na waliodhulumu waseme: Ewe Mola Wetu Mlezi! Tuakhirishe muda kidogo tuitikie wito wako na tuwafuate Mitume. Kwani nyinyi si mliapa zamani kwamba hamtaondokewa?” (14:44), na,

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُونِ ﴿٩٩﴾ لَعَلِّي أَعْمَلُ صَالِحًا فِيمَا تَرَكْتُ
كَلَّا ۗ إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَائِلُهَا ۗ وَمِن وَرَائِهِم بَرْزَخٌ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٠٠﴾

“Mpaka yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: Mola Wangu Mlezi! Nirudishe. Ili nitende mema sasa badala ya yale niliyo yaacha. Wapi! Hii ni kauli aisemayo yeye tu. Na nyuma yao kipo kizuizi mpaka siku watapofufuliwa.” (23:99-100)

Kisha Allah تعالى Akasema;

وَلَن يُؤَخِّرَ اللَّهُ نَفْسًا إِذَا جَاءَ أَجْلُهَا ۗ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ

“Wala Mwenyezi Mungu Hataichelewesha nafsi yoyote inapofika ajali yake; na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda.”

Inamaanisha, wakati wa mauti unapowadia, hakuna atakayepewa muda. Kwa hakika, Yeye Anayajua yote waliyoyafanya hapo kabla. Kauli ya Allah تعالى،

وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ

“...na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda.”

Huu ni mwisho wa *Tafsiri ya Suratu Al-Munafiqun*. Kila Sifa Njema na Shukrani ni za Allah تعالى, na mafanikio yote na usahihi ni Wake yeye.

Huu ni mwisho wa Juzuu ya Tisa, Juzuu ya Kumi itanzia katika *Tafsiri ya Suratu At-Taghabun*.

